JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO AWAMU YA PILI

"SEKTA YA KILIMO KWA MAENDELEO YA VIWANDA"

Novemba, 2017

PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO AWAMU YA PILI

Novemba, 2017

# DIBAJI

Maendeleo katika sekta ya kilimo ni muhimu hasa katika kukuza uchumi wa Taifa na kuleta msukumo kwenye ukuaji wa sekta ya viwanda. Ukuaji wa sekta ya kilimo una umuhimu mkubwa katika kuzalisha chakula cha kutosha ili kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula na lishe kwa wananchi wakati wote. Sekta ya kilimo inachangia takribani asilimia 29.1 ya pato la Taifa, asilimia 65.5 ya ajira, asilimia 65 ya malighafi inayotumika katika sekta ya viwanda na asilimia 30 ya pato la bidhaa zinazouzwa nje ya nchi.

Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(Agricultural Sector Development Programme Phase Two-ASDP II)* imeandaliwa ili kuweka msukumo kwenye maendeleo ya uchumi wa nchi kwa kuzingatia vipaumbele vya maendeleo na Dira ya Taifa ya mwaka 2025 *(Tanzania Development Vision 2025-TDV 2025);* Mpango wa Taswira ya Muda Mrefu wa Taifa wa mwaka 2012-2025 *(Long Term Perspective Plan-LTPP 2012-2025);* Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Pili (*Five Year Development Plan Phase Two-FYDP II 2016-2021*); Mpango wa Taifa wa Uwekezaji kwenye Kilimo na Usalama wa Chakula *(Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan-TAFSIP)*; Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Strategy -ASDS)* na Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ni ya miaka kumi (10) kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2027/28. Programu hii itatekelezwa kwa awamu mbili za miaka mitano kwa kila awamu kuanzia mwaka 2017/18.

Malengo makuu ya Programu ya *ASDP II* ni kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo (kilimo, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija, kukifanya kilimo kiwe cha kibiashara zaidi na kuongeza pato la wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha yao, usalama wa chakula na lishe. Programu hii ina maeneo makuu manne (4) ya kipaumbele ambayo ni :- (i) Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Maji na Ardhi; lengo likiwa ni kuongeza wigo wa upatikanaji wa maji na matumizi bora ya ardhi kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi; (ii) Kuongeza Tija na Faida kwa lengo la kuongeza uzalishaji wenye tija hasa kwenye mazao ya kipaumbele; (iii)Kuongeza Thamani ya Mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuleta ushindani kwenye soko na sekta binafsi na kuhakikisha uanzishwaji wa vyama vya wakulima; (iv) Kuweka Mazingira Wezeshi ya Kuendeleza Sekta ya kilimo na kuwezesha uratibu, ufuatiliaji na kufanya tathmini ya sekta ikiwa ni pamoja na kuimarisha taasisi na kuweka mazingira wezeshi ya uratibu.

Mafanikio yanayotarajiwa kutokana na utekelezaji wa ASDP II ni pamoja na :- (i) Kuhakikisha na kuongeza uzalishaji wa chakula na bidhaa mbalimbali ili kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania; kuhakikisha Taifa lina akiba ya chakula cha kutosha na kujitosheleza kwa malighafi kwa ajili ya sekta ya viwanda, (ii) Kupunguza ongezeko la maradhi yanayosababishwa na lishe duni hasa maeneo ya vijijini pamoja na kuzuia uwezakano wa kupata majanga (maafa) ya asili; (iii) Kuongezeka kwa shughuli za kibiashara zinazohusisha sekta ya kilimo zitakazochangia kuongeza kipato kwa takriban asilimia 97.5 ya kaya zinazotegemea kilimo hususan maeneo ya vijijini; (iv) Kulinda rasilimali za nchi na kujenga uwezo wa Watanzania wa kulinda rasilimali zao na pia kuhakikisha wanatumia ardhi na maji vizuri ili waweze kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; (v) Kuimarisha uwezo wa taasisi wa kutafuta rasilimali fedha ili kuendeleza sekta ya kilimo; (vi) Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa majanga au maafa kwa kubuni na kugundua vifaa muhimu na vya kisasa vya usimamizi wa majanga hatarishi; (vii) Kupunguza kukosekana kwa usawa wa kijinsia; (viii) Kupunguza ajira za watoto katika sekta ya kilimo na kukuza kazi zenye staha na (ix) Kupunguza uharibifu wa mazingira utokanao na kilimo na hivyo kuzingatia kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi (*Climate Smart Agriculture*).

Ni kwa muktadha huo hapo juu, napenda kuwasilisha kwa wadau wote Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini *(ASDP II)* kwa ajili ya utekelezaji. Ni matumaini yangu kwamba Programu hii itatekelezwa kwa ushirikiano wa wadau wote ikiwa ni pamoja na sekta ya umma, sekta binafsi, washirika wa maendeleo, taasisi za kifedha na tasisi zisizokuwa za kiserikali.

Nitoe wito kwa wadau wote katika sekta ya kilimo kushirikiana kwa pamoja ili kuhakikisha mageuzi ya kilimo yanafanikiwa kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wa viwanda na nchi kwa ujumla. Ni muhimu pia kuhakikisha kwamba juhudi hizi za pamoja na mikakati tuliyojiwekea iwe shirikishi na kuungwa mkono na kila mmoja wetu.

Natanguliza shukrani zangu kwa kushiriki na ushirikiano wenu.

**Mhe. Dkt. Charles Tizeba (MB),**
**WAZIRI WA KILIMO**

# YALIYOMO

**DIBAJI** ..... iii
**MUHTASARI** ..... 1
**I. UTANGULIZI** ..... 8
A. Viashiria vya Uchumi na mchango wa Sekta ya Kilimo kwenye Uchumi ..... 8
B. Sekta ya Kilimo ..... 9
C. Sera ..... 12
**II. PROGRAMU, MIRADI NA MATUMIZI** ..... 15
A. Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza (ASDP-1) ..... 15
B. Miradi Mbalimbali katika Sekta ya Kilimo ..... 16
C. Mapitio katika Sekta ya Kilimo na Matumizi ya Fedha za Umma ..... 18
**III. UANDAAJI WA PROGRAMU YA ASDP II NA MISINGI YAKE** ..... 23
A. Tulichojifunza Kutokana na Utekelezaji wa ASDP-1 ..... 23
B. Changamoto kwenye Mifumo na Vichocheo vya Sekta ya Kilimo ..... 25
C. Uandaaji wa Programu ya ASDP II ..... 28
D. Misingi Mikuu ya Uundaji wa Programu ya ASDP II ..... 30
E. Wigo, Mtazamo na Awamu za Programu ya ASDP II ..... 32
F. Uandaaji wa Vipaumbele na Dira ..... 36
G. Misingi na Mbinu za Uandaaji wa Programu ya ASDP II ..... 37
H. Nadharia ya Mageuzi ..... 40
**IV. MALENGO NA MAELEZO YA PROGRAMU YA ASDP II** ..... 41
A. Lengo la Programu ..... 42
B. Maeneo ya Kipaumbele ya Uwekezaji ..... 46
C. Eneo Kuu la 1: Usimamizi na Matumizi Endelevu ya Maji na Ardhi ..... 48
D. Eneo Kuu la 2: Kuongeza Tija na Faida ..... 60
E. Eneo Kuu la 3: Biashara na Uongezaji Thamani kwenye Mazao ..... 87
F. Eneo Kuu la 4: Kuimarisha viwezeshi vya sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini ..... 108
**V. GHARAMA, UGHARAMIAJI NA USIMAMIZI WA FEDHA ZA PROGRAMU** ..... 135
A. Gharama za Programu kwa Ujumla ..... 135
B. Mpango wa Ugharamiaji ..... 142
C. Utaratibu wa Ugharamiaji wa Programu ..... 143
**VI. MUUNDO WA TAASISI NA MGAWANYO WA MAJUKUMU KWA AJILI YA UTEKELEZAJI** ..... 146
A. Utekelezaji wa ASDP II katika Ngazi ya Taifa ..... 146
B. Ngazi ya Mkoa ..... 146
C. Ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ..... 147
D. Uratibu wa Programu ..... 147
E. Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa na Ufuatiliaji ..... 149
F. Masuala ya usalama, usimamizi wa kijamii na Mazingira ..... 150
**VII. FAIDA NA UCHAMBUZI WA KIUCHUMI NA FEDHA ZA PROGRAMU** ..... 152
A. Muhtasari kuhusiana na Faida ..... 152
B. Uchambuzi wa Kiuchumi na Fedha ..... 154
C. Faida za Kiuchumi ..... 157
D. Gharama za Uendeshaji ..... 158
E. Uchambuzi wa kiuchumi na matokeo ya mradi katika mazingira ya uwekezaji ..... 158

F. Uendelevu wa Programu ..... 159
**VIII. UTEKELEZAJI NA MATOKEO YA PROGRAMU YA ASDP II NA ATHARI ZAKE ... 160**
A. Upimaji wa Utekelezaji na Wadau ..... 160
B. Athari ..... 161

**KIAMBATISHO NA. I: Mpangilio wa Utekelezaji wa ASDP II ..... 163**

**KIAMBATISHO NA. II: Mfumo wa ufuatiliaji Matokeo ya ASDP II ..... 177**

**KIAMBATISHO NA. III: Mfumo wa Uratibu wa ASDP II ..... 214**

**KIAMBATISHO NA. IV: Mahitaji ya Bajeti ya Programu na Miradi ..... 224**

**KIAMBATISHO NA. V: Takwimu, Ufuatiliaji na Tathmini ..... 235**

**KIAMBATISHO NA. VI: Uchambuzi wa Kiuchumi na Fedha ..... 251**

**KIAMBATISHO NA. VII: Uchambuzi wa vihatirishi na mikakati / hatua za kukabiliana navyo ..... 260**

**KIAMBATISHO NA. VIII: Ramani na Vielelezo muhimu ..... 262**

**KIAMBATISHO NA. IX: Vigezo vya Kuchagua Wilaya za Kipaumbele ..... 269**

**KIAMBATISHO NA. X: Mabadiliko ya Tabianchi na utekelezaji wa mpango wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (ACRP) ..... 271**

**KIAMBATISHO NA. XI: Mikakati Mbadala ya kuhamasisha Uwekezaji katika Pembejeo za Kilimo ... 275**

**KIAMBATISHO NA. XII: Uongozi katika ASDP II, Uratibu na Mawasiliano Kuanzia Ngazi ya Kijiji hadi Taifa ..... 277**

**KIAMBATISHO NA. XIII: Kanuni za uwekezaji katika Kilimo ..... 283**

**KIAMBATISHO NA. XIV: Nyaraka muhimu za rejea ..... 283**

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Matumizi ya kawaida Wizara za Kilimo; Mifugo na Uvuvi (TSh milioni) ..... 20
Jedwali Na. 2: Matumizi ya kawaida kwenye kilimo na uwiano wa mchango wa Kilimo kwenye pato la Taifa ..... 20
Jedwali Na. 3: Matumizi kwa ajili ya teknolojia- Wizara ya Kilimo (TSh milioni) ..... 21
Jedwali Na. 4: Viwango vya ukusanyaji mapato na utekelezaji wa bajeti ..... 22
Jadweli Na. 5: Vikwazo vikuu na vichochezi vya kimaudhui ..... 26
Jedwali Na. 6: Uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula (2005–2010) ..... 33
Jedwali Na. 7: Mazao ya kipaumbele katika kanda za kiikolojia za kilimo na awamu za bidhaa muhimu kwa mkoa ..... 34
Jedwali Na. 8: Bidhaa za kipaumbele katika mnyororo wa thamani kikanda ..... 35
Jedwali Na. 9: Maeneo ya kimkakati ya ASDS na utambuzi wa maeneo ya kipaumbele ..... 37
Jedwali Na. 10: Uainishaji wa kaya za vijijini zinazojihusisha na shughuli za Kilimo ..... 44
Jedwali Na. 11: Maeneo Makuu na Malengo ya Kimkakati ya ASDP II ..... 46

Jedwali Na. 12: Kanda za Kiikolojia za Kilimo na wilaya zitakazoshiriki katika ASDP II ..... 47
Jedwali Na. 13: Eneo Kuu 1: Malengo Mahsusi na Matokeo ya ASDS..... 48
Jedwali Na. 14: Shughuli za kipaumbele katika Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa ajili ya maendeleo ya mazao na mifugo……..…….....50
Jedwali Na. 15: Muhtasari wa skimu za umwagiliaji za kipaumbele kwenye BRN na zile zilizobaki za ASDP-1 (2015/2020) ..... 54
Jedwali Na. 16: Shughuli za kipaumbele kwa ajili ya kuboresha usimamizi bora wa maji kwa ajili kilimo kinachotegemea mvua .....55
Jedwali Na. 17: Shughuli za kipaumbele za upatikanaji wa rasilimali maji kwa ajili ya mifugo/uvuvi..... 56
Jedwali Na. 18: Uwekezaji katika ASDP II na maeneo ya kuyashughulikia kwa ajili ya kuboresha ustahimilivu wa mifumo ya kilimo ..... 59
Jedwali Na.19: Bajeti ya maendeleo ya miaka mitano/ makadirio ya uwekezaji katika eneo kuu la 1 katika bei ya mwaka 2016 (TSh milioni)... .....59
Jedwali Na. 20: Eneo Kuu la 2: Malengo Mahsusi na Matokeo ..... 61
Jedwali Na. 21: Malengo kwa ajili ya shughuli za kipaumbele za kuongeza tija ya uzalishaji katika mifugo na uvuvi (Miaka 10) ..... .62
Jedwali Na. 22: Shughuli za kipaumbele za huduma za ugani kwa ajili ya mifugo..... 69
Jedwali Na. 23: Shughuli za kipaumbele za huduma za ugani kwa ajili ya uvuvi ..... 70
Jedwali Na. 24: Shughuli za kipaumbele maeneo na uwekezaji kwa ajili ya mafunzo ya mifugo na uvuvi .....71
Jedwali Na. 25: Shughuli za kipaumbele kwa ajili ya upatikanaji wa pembejeo za Mifugo/Uvuvi ..... 75
Jedwali Na. 26: Vituo vya Utafiti wa Mazao na Mifugo katika Kanda za Ikolojia za Kilimo ..... 77
Jedwali Na. 27: Vipaumbele vya uwekezaji na maeneo ya utekelezaji kwa ajili ya Utafiti wa Mifugo na Uvuvi ……....……..…..78
Jedwali Na. 28: Mapendekezo ya shughuli za Usalama wa Chakula na Lishe.....84
Jedwali Na. 29: Bajeti ya Maendeleo/Makadirio ya uwekezaji kwa ajili ya Eneo Kuu la 2 …….....86
Jedwali Na. 30: Eneo Kuu la 3: Malengo na Matokeo maalum yanayohusiana na ASDS .....89
Jedwali Na. 31: Malengo ya minyororo ya thamani ya bidhaa za kipaumbele na mikakati kufikia matokeo yanayotarajiwa……..….....90
Jedwali Na. 32: Muhtasari wa shughuli na maeneo ya utekelezaji katika kukuza masoko katika ngazi ya Kitaifa na Mkoa……..…....…....95
Jedwali Na. 33:Shughuli za kipaumbele za udhibiti na usimamizi wa ubora wa Mifugo na Uvuvi…….. ..... 96
Jedwali Na. 34: Shughuli za kipaumbele za kuongeza thamani na usindikaji kwenye mnyororo wa thamani wa biashara…….....98
Jedwali Na. 35: Shughuli za kipaumbele za kuelekea kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna…….....…….....99
Jedwali Na. 36: Maeneo ya kimkakati ya utekelezaji yaliyopendekezwa kwa ajili ya Kuongeza Thamani na Usindikaji wa Mazao….....100
Jedwali Na. 37: Maeneo ya kimkakati ya utekelezaji kwa ajili ya yaliopendekezwa ya kuongeza

Thamani na Usindikaji Mazao (Mifugo/Uvuvi)……..…….....101
Jedwali Na. 38: Maeneo ya utekelezaji na shughuli kwa ajili ya kuboresha uwekezaji vijijini/kilimo (rasimu).....105
Jedwali Na. 39: Bajeti ya Maendeleo/ Makadirio ya uwekezaji kwa ajili ya Eneo Kuu la 3 (TSh milioni)..... .107
Jedwali Na. 40: Eneo Kuu la 4:Malengo mahususi na matokeo yanayohusiana na ASDS.. ..... 108
Jedwali Na. 41: Maeneo muhimu ya sera na shughuli zinazohusiana na ukuaji wa Sekta ya Kilimo (Wizara). .....110
Jedwali Na. 42: Vyama vya wakulima kwa vikundi .....112
Jedwali Na. 43: Maeneo ya utekelezaji kwa ajili kuwawezesha wakulima na kuimarisha vyama vyao .....114
Jedwali Na. 44: Maeneo ya kipaumbele ya ASDP II yaliyopendekezwa katika shughuli na uendeshaji wa ushirika. .....116
Jedwali Na. 45: Vyombo vya uratibu mifumo na wajumbe wa ASDP II katika ngazi ya Taifa, (Muhtasari).....118
Jedwali Na. 46: Vyombo vya uratibu mifumo na wajumbe wa ASDP II katika ngazi ya OR-TAMISEMI, (Muhtasari) .....119
Jedwali Na. 47: Mapendekezo ya hatua za kukuza TEHAMA na usimazi wa mawasiliano na utunzaji wa taarifa..... 128
Jedwali Na. 48: Shughuli na maeneo ya utekelezaji ili kuboresha uwekezaji vijijini/kilimo..... ..132
Jedwali Na. 49: Bajeti ya maendeleo ya makadirio ya uwekezaji kwa miaka mitano kwenye Eneo Kuu la 4 (TSh milioni ) …….....…....134
Jedwali Na. 50: Mahitaji ya bajeti ya ASDP II kwa kila eneo kuu kwa miaka mitano ya kwanza. ..... 135
Jedwali Na. 51: Bajeti ya maendeleo ya ASDP II kwa ujumla..... 136
Jedwali Na. 52: Kiwango cha michango ya bajeti ya maendeleo kinachotarajiwa kuchangiwa kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha. ..... 142
Jedwali Na. 53: Mpango wa fedha wa ASDP II (Muhtasari wa gharama zote). ..... 143
Jedwali Na. 54:Muhtasari wa vyombo vya uratibu wajumbe na mtiririko wa vikao vya ASDP II katika ngazi ya Taifa……...……..146
Jedwali Na. 55: Muhtasari wa vyombo vya uratibu wajumbe na mtirirko wa vikao vya ASDP II katika Ngazi ya OR-TAMISEMI, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa .....148
Jedwali Na. 56: Faida ghafi katika hali ya sasa, ya baadaye na baadaye ya kuwepo na kutokuwepo kwa nradi..... 155
Jedwali Na. 57: Faida ghafi ya mifugo katika hali ya sasa, ya baadaye na baadaye ya kuwepo na kutokuwepo kwa Mradi……. .....156
Jedwali Na. 58: Faida halisi ya shamba katika hali ya sasa, ya baadaye na baadaye ya kuwepo na kutokuwepo kwa mradi. ..... 157
Jedwali Na. 59: Uchambuzi wa Kiuchumi . ..... 159
Jedwali Na. 60: Mzunguko wa Ufuatiliaji katika ngazi za utekelezaji wa ASDP II..... 236
Jedwali Na. 61: Mzunguko wa Ufuatiliaji katika ngazi za utekelezaji wa ASDP II..... 236

Jedwali Na. 62: Majukumu ya ufuatiliaji katika ngazi ya halmashauri ..... 239
Jedwali Na. 63: Tafiti na sensa muhimu kwa ajili ya takwimu za kilimo ..... 241
Jedwali Na. 64: Matokeo na Viashiria vya ASDP-1 ..... 249
Jedwali Na. A1: Muhtasari wa uratibu wa ASDP II, utaratibu, wajumbe na kazi ..... 220
Jedwali Na. A2: Tija ya mazao katika hali ya sasa, baadaye kukiwa na mradi na bila ya mradi ..... 251
Jedwali Na. A3: Faida ya ghafi ya mazao katika hali ya sasa, baadaye kukiwa na mradi na bila mradi 252
Jedwali Na. A4: Mpangilio wa mazao na wingi wa mimea ..... 253
Jedwali Na. A5: Faida ya jumla katika hali ya sasa, baadaye kukiwa na mradi na bila ya mradi ..... 254
Jedwali Na. A6: Mapato halisi katika hali ya sasa, baadaye bila ya na kuwepo kwa mradi ..... 254
Jedwali Na. A7: Mapato ya jumla kwa upande wa mifugo katika hali ya sasa, baadaye kukiwa na mradi na bila mradi ..... 255
Jedwali Na. A8: Faida ya jumla kwa mifugo sasa, baadaye kukiwa na mradi na bila mradi ..... 256
Jedwali Na. A9: Fedha na gharama za uwekezaji kiuchumi ..... 257
Jedwali Na. A10: Uchambuzi wa kina na uwezekano wa kiuchumi ..... 258
Jedwali Na. A11: Kanda za Ikolojia za Kilimo (AEZ), bidhaa na wilaya za kipaumbele (kwa majaribio) ..... 263
Jedwali Na. A12: Uzalishaji wa Kilimo —mazao ya kilimo ..... 265
Jedwali Na. A13: Uzalishaji wa Kilimo —mazao ya biashara (katika vipimo vya tani) ..... 265
Jedwali Na. A14: Maeneo ya kipaumbele ya utekelezaji wa uwekezaji: ACRP (Iliyopigiwa mstari ni maeneo muhimu ya kipaumbele) ..... 273
Jedwali Na. A15: Vipengele vya kushughulikia na Mipango Mkakati ..... 274

# Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1: Kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa Kwa sekta (Asilimia, kwa kurejea bei za mwaka 2007) ..... 8
Kielelezo Na. 2: Mchango wa Sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa (%), kwa bei kurejea za mwaka 2001 ..... 9
Kielelezo Na. 3: Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi (kwa bei za sasa—TSh.bilioni) ..... 10
Kielelezo Na. 4: Asilimia ya Pato la Taifa kutokana na shughuli za kiuchumi kwa Asilimia (Katika asilimia ya Pato la Taifa kwa ujumla kwa bei za sasa katika TSh) ..... 10
Kielelezo Na. 5: Mazao makuu yanayozalishwa Tanzania (1961–2013, kwa tani ) ..... 11
Kielelezo Na. 6: Mabadiliko ya wastani wa tija ya mazao makuu Tanzania (1961–2013, kg/ha) ..... 11
Kielelezo Na.7: Mfumo wa sera kwa ajili ya kuleta mageuzi katika sekta ya……..... 13
Kielelezo Na. 8. Matumizi ya Kawaida kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ngazi ya Taifa ..... 19
Kielelezo Na. 9. Matumizi ya kawaida kwenye sekta ya Kilimo kwa kuwianisha na jumla ya matuimizi yote ya bajeti ya kawaida ..... 21
Kielelezo Na.10. Matumizi ya bajeti kwenye maendeleo ya miradi ya Kilimo fedha za ndani na nje ..... 23
Kielelezo Na.11: Mazingira ya Tanzania kwa ajili ya kuendeleza Kilimo (2015–2024) ..... 28

Kielelezo Na 12: Mfumo wa uandaaji wa ASDP-II. ..... 29
Kielelezo Na 13: Mfumo wa utoaji fedha kwa ajili ya ASDP-II ..... 29
Kielelezo Na 14: Nadharia ya Mageuzi ..... 40
Kielelezo Na 15: Muundo wa mnyororo wa matokeo ya ASDP-II ..... 41
Kielelezo Na 16: Lengo, Mikakati na Matokeo ya ASDP-II ..... 41
Kielelezo Na 17: Lengo la ASDP II na maeneo makuu ya utekelezaji..... 42
Kielelezo Na 18: Maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji ya ASDP II..... 43
Kielelezo Na 19: Maeneo makuu na vipaumbele vya ASDP II ..... 45
Kielelezo Na 20: Mbinu ya mnyororo wa thamani kwenye ASDP II..... 88
Kielelezo Na 21: Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa ASDP na utendaji wa sekta ..... …122
Kielelezo Na 22: Mfumo wa utoaji fedha kwa ajili ya ASDP II..... …144
Kielelezo Na 23: Mfumo wa uratibu wa ASDP II…. ..... …214
Kielelezo Na A24: Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa ASDP II na utendaji wa sekta na miradi .. 237
Kielelezo Na A25: Mfumo wa kukusanya takwimu za Kilimo ..... …238
Kielelezo Na A26: Mchango wa washirika wa maendeleo kwa kuzingatia eneo na mnyororo wa thamani katika sekta ndogo ya Mazao ..... 247
Kielelezo Na A27: Mchango wa washirika wa maendeleo kwa kuzingatia eneo na mnyororo wa thamani kwenye sekta ndogo ya Mifugo na Uvuvi ..... 248
Kielelezo Na A28: Kanda za Ikolojia za Kilimo ..... 262
Kielelezo Na A29: Kanda na Vituo vya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Kanda za Kati, Mashariki, Ziwa, Kaskazini, Kusini, Nyanda za Juu Kusini na Magharibi)..... 266
Kielelezo Na A30: Kanda za Ikolojia za Kilimo Tanzania ..... 266
Kielelezo Na A31: Kanda za kujikimu Tanzania ..... 267
Kielelezo Na A32: Ramani – Wilaya ambazo hazina uhakika wa usalama wa chakula (2006-13)..... 267
Kielelezo Na A33: Ramani– Mtawanyiko wa Ng'ombe Tanzania kwa 2008 ..... 268
Kielelezo Na A34: Ramani-Wilaya za kipaumbele zinazolengwa katika ASDP II ..... 270

# Orodha ya Masanduku

Sanduku Na. 1: Kanuni muhimu za kuandaa ASDPII ..... 30
Sanduku Na. 2:Masuala ya msingi kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi—usimamizi husishi wa rutuba ya udongo..... 51
Sanduku Na. 3: Ajenda kwa ajili ya kuendeleza Kilimo endelevu cha shadidi na stahimilivu ..... 58
Sanduku Na. 4: Kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa ufanisi ..... 64
Sanduku Na. 5: Taasisi mafunzo ya ufundi ..... 68
Sanduku Na. 6: Masuala muhimu ya sera na maboresho ya kitaasisi ..... 110
Sanduku Na. 7: Miradi iliyo nje ya bajeti ya Serikali..... 120

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| **AASS** | Annual Agricultural Sample Survey |
| **AEZ** | Agro-Ecological Zone |
| **AfDB** | African Development Bank |
| **AR4D** | Agricultural Research for Development |
| **ARDS** | Agricultural Routine Data System |
| **ASA** | Agricultural Seed Agency |
| **ASDP** | Agricultural Sector Development Programme |
| **ASDS** | Agricultural Sector Development Strategy |
| **ASLMs** | Agriculture Sector Lead Ministries |
| **ASR** | Agriculture Sector Review |
| **ASSP** | Agricultural Statistics Strategic Plan |
| **ATI** | Agricultural Training Institute |
| **BRN** | Big Results Now |
| **CAADP** | Comprehensive Africa Agriculture Development Programme |
| **CKM** | Communication and Knowledge Management |
| **CVC** | Commodity Value Chain |
| **DADG** | District Agriculture Development Grant |
| **DADP** | District Agricultural Development Plan |
| **DAICO** | District Agricultural, Irrigation and Cooperative Officer |
| **DCP** | District Commodity Value Chain Platform |
| **DED** | District Executive Director |
| **DLFO** | District Livestock and Fisheries Officer |
| **EAAPP** | East Africa Agricultural Productivity Project |
| **FAO** | Food and Agriculture Organization of the United Nations |
| **FFS** | Farmers Field School |
| **FTC** | Farmer Training Centre |
| **ICT** | Information and Communication Technologies |
| **IFAD** | International Fund for Agricultural Development |
| **IPM** | Integrated Pest Management |
| **JICA** | Japan International Cooperation Agency |
| **JSR** | Joint Sector Review |
| **LGAs** | Local Government Authorities |
| **LITA** | Livestock Training Agency |
| **LITI** | Livestock Training Institute |
| **M&E** | Monitoring and Evaluation |
| **MAFC** | Ministry of Agriculture Food Security and Cooperatives |
| **MIVARF** | Marketing Infrastructure Value Addition and Rural Finance |

| | |
|---|---|
| **MLFD** | Ministry of Livestock and Fisheries Development |
| **NAIVS** | National Agricultural Input Voucher Scheme |
| **NASSM** | National Agricultural Sector Stakeholders Meeting |
| **NCU** | National Coordination Unit |
| **NEPAD** | New Partnership for Africa's Development |
| **NSCA** | National Sample Census of Agriculture and Livestock |
| **PER** | Public Expenditure Review |
| **PMO-RALG** | Prime Minister's Office- Regional Administration and Local Government |
| **PO-RALG** | President's Office - Regional Administration and Local Government |
| **PPP** | Public Private Partnership |
| **PSP** | Private Service Providers |
| **RAS** | Regional Administrative Secretariat |
| **SACCOS** | Savings and Credit Cooperative Society |
| **SADC** | Southern Africa Development Community |
| **SAGCOT** | Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania |
| **SWAp** | Sector Wide Approach |
| **TAFSIP** | Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan |
| **TALIRI** | Tanzania Livestock Research Institute |
| **TARI** | Tanzania Agricultural Research Institute |
| **TCD** | Technical Committee of Directors |
| **TOSCI** | Tanzania Official Seed Certification Institute |
| **TTPU** | Technology Transfer and Partnership Units |
| **USAID** | United States Agency for International Development |
| **VAEO** | Village Agricultural Extension Officer |
| **WAEO** | Ward Agricultural Extension Officer |
| **WARC** | Ward Agricultural Resource Centre |

# MUHTASARI

Serikali imekamilisha na kuzindua utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *( Agricultural Sector Development Progamme Phase Two-ASDP II)*. Programu itatekelezwa kwa muda wa miaka kumi kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2027/2028. Utekelezaji wa ASDP II utafanyika katika awamu mbili za miaka mitano (5) kwa kila. Awamu ya kwanza ya utekelezaji imeanza mwaka 2017/2018 na itafikia mwisho wa utekelezaji mwaka 2022/2023, wakati awamu ya pili itaanza kutekelezwa mwaka 2023/2024 na kufikia mwisho mwaka 2027/2028. ASDP II ni mwendelezo wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza *(Agricultural Sector Development Programme Phase One -ASDP I)* iliyotekelezwa kuanzia mwaka 2006/2007 hadi 2013/2014. Hivyo maandalizi na ukamilishaji wa ASDP II umezingatia uzoefu uliotokana na utekelezaji wa ASDP I.

ASDP II inalenga kuleta mageuzi kwenye sekta ya kilimo ambayo inajumuisha shughuli za kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi. Programu itaongeza tija, kukifanya kilimo kiwe cha kibiashara na kuongeza kipato cha wakulima wadogo na wa kati ili ya kuboresha maisha yao, kuongeza uhakika wa usalama wa chakula na lishe na pia kuchangia kwenye pato la Taifa. Mkakati wa ASDP II ni kuwabadilisha wakulima wadogo na wa kati kutoka kwenye kilimo cha kujikimu kwenda kwenye kilimo cha kibiashara. Mabadiliko hayo yalifanyika hatua kwa hatua kwa kuimarisha na kuwezesha mifumo itakayochochea maendeleo ya sekta, kutatua changamoto na kutumia fursa zilizopo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji endelevu na wenye tija kwa kuzingatia mahitaji ya soko na biashara yenye ushindani kwenye mnyororo wa thamani.

Maandalizi ya programu yameshirikisha wadau katika ngazi mbalimbali. Hivyo, programu hii ni matokeo ya maoni, ushauri, utafiti, fursa na matakwa ya wadau wote katika sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, wavuvi, sekta binafsi, washirika wa maendeleo, vyama vya wakulima na mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta ya umma. Yaliyomo kwenye andiko la programu hii ni pamoja na (i) utangulizi (ii) programu, miradi na matumizi ya fedha za umma (iii) mchakato wa kuandaa ASDP II na misingi yake (iv) malengo ya ASDP (v) gharama na ugharamiaji wa programu na usimamizi wa fedha (vi) taasisi na mgawanyo wa majukumu (vii) faida na uchambuzi wa kiuchumi na fedha na (viii) utekelezaji wa ASDP II na athari zake. Yafuatayo kwa muhtasari ni maeneo muhimu ya programu.

## A. VIASHIRIA VYA KIUCHUMI NA MCHANGO WA SEKTA YA KILIMO KWENYE UCHUMI.

1. Viashiria vya kiuchumi vya Tanzania vinaonesha ukuaji mkubwa wa pato la Taifa kabla na wakati wa utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza (ASDP I) iliyoanza mwaka 2006. Katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, ukuaji wa uchumi umeendelea kukua kwa kasi zaidi na kufikia wastani wa ukuaji wa asilimia 6% hadi 7% kwa mwaka. Kiwango cha ukuaji wa pato la Taifa kilikuwa 7% mwaka 2016[1]. Hata hivyo, wastani wa ukuaji wa sekta ya kilimo kwa mwaka 2016, ulikuwa chini ya ukuaji wa pato la Taifa. Kiwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo katika kipindi cha 2006-2014 kilikuwa ni asilimia 3.9 kwa mwaka, na kilipungua hadi asilimia 2.9 mwaka 2015 na kisha kikaongezeka hadi asilimia 3.0 mwaka 2016[2].

2. Sekta ya kilimo inatoa mchango mkubwa kwenye ukuaji na maendeleo ya uchumi wa nchi. Sehemu kubwa ya uzalishaji inachangiwa na wakulima wadogo ambao wanalima zaidi ya asilimia 90 ya eneo lote linalolimwa nchini. Sekta ya kilimo inatoa ajira kwa Watanzania wapatao asilimia 65.5 na kuchangia kipato cha wakulima, wafugaji na wavuvi kwa asilimia 70%. Sekta ya kilimo pia inachangia asilimia 29 ya pato la Taifa, asilimia 30 ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi na asilimia 65 ya malighafi za viwandani (URT, 2014). Katika mwaka wa fedha 2016/17, sekta ya kilimo ilichangia asilimia 29.1 ya pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 23 ya mwaka 2014 (FYDP 2015/2016) na kuchangia pia asilimia 65.5 ya ajira (NBS, 2017). Sekta ya kilimo iliongeza hali ya usalama wa chakula na lishe ambapo utoshelevu wa chakula uliongezeka hadi asilimia 125 mwaka 2016/2017 kutoka asilimia 123 mwaka 2014/2015.

1 *http://www.worldbank.org/en/country/tanzania/overview, Agosti 2017*
2 *Benki kuu. Taarifa ya mapitio ya hali ya uchumi ya robo mwaka, Mei 2017*

## B. MAFANIKIO YA ASDP I

3. Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza (ASDP I) ilizinduliwa mwaka 2006 ili kutoa mwongozo mpana wa sekta kuchangia malengo ya kupunguza umaskini hasa vijijini kutoka asilimia 27 hadi asilimia 14 na kuongeza ukuaji wa sekta ya kilimo hadi asilimia 10 kufikia mwaka 2010. Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa ASDP I ni pamoja na kutumika kwa mbinu shirikishi ya uibuaji, upangaji na utekelezaji wa miradi kuanzia ngazi ya chini ambapo asilimia 75 ya bajeti ilipelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, asilimia 20 ilitumika Kitaifa na asilimia 5 ilitumika katika ngazi ya Mikoa. Mafanikio mengine ni pamoja na kujenga uwezo wa wataalamu na wa kimuundo katika ngazi ya Halmashauri, Mkoa na Taifa. Pia kuimarika kwa huduma bora za utafiti ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya tafiti ziliofanywa kwa ajili ya mazao na mifugo.

4. Utekelezaji wa ASDP I ulichangia kuongezeka kwa matumizi ya pembejeo za kilimo ikiwemo uzalishaji na matumizi ya baadhi ya mbegu bora, kuongezeka kwa matumizi ya mbolea, zana za kilimo kama vile matrekta makubwa na madogo, wanyamakazi na hivyo kuongezeka kwa eneo la kilimo kwa asilimia 148. Wakati wa utekelezaji wa ASDP I kilimo cha umwagiliaji nchini kiliimarishwa. Kwa kukarabati, kuboresha na kujenga miundombinu ya umwagiliaji na hivyo kuongezeka kwa eneo la umwagiliaji kutoka hekta 264,338 mwaka 2005/2006 hadi hekta 461,326 mwaka 2014.

5. Kuendelezwa kwa miundombinu ya masoko na mifumo ya masoko kwa ajili ya kuongeza thamani ya bidhaa ikiwemo ukarabati wa maghala na kujenga masoko ya mazao na mifugo na kuendeleza mifumo ya masoko ya malipo ya bidhaa kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani. Aidha, kiwango cha utoshelevu wa chakula kiliongezeka kutoka asilimia 103 mwaka 2009/2010 hadi asilimia 123 mwaka 2015/2016.

6. Mfumuko wa bei utokanao na bei ya vyakula ulipungua kutoka asilimia 7.01 mwaka 2006 hadi asilimia 5.56 mwaka 2010 na asilimia 5.6 mwaka 2015. Aidha, kufika Oktoba 2016 mfumuko wa bei ulipungua na kufika asilimia 4.5. Aidha, kiasi na thamani ya mauzo ya mazao nje ya nchi kiliongezeka hususan kwa mazao ya biashara yale ya asili ambayo ni kahawa, pamba, mkonge, chai, tumbaku na korosho.

## C. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI WA ASDP I

7. Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa ASDP I ni pamoja na udhaifu katika udhibiti, usimamizi na uratibu ukiwemo uratibu kati ya wizara na wizara na kati ya wizara na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kukosekana kwa usimamizi na uratibu madhubuti kulisababisha ukosefu wa mgawanyo mzuri wa majukumu, mifumo duni ya uwajibikaji na hivyo uratibu duni wadau wa sekta. Hali hiyo ilisababisha mtawanyiko wa rasilimali fedha ambao haukuwa na matokeo makubwa na kukiwa ni ugumu wa kupima matokeo ya ASDP I.

8. Changamoto nyingine ni kutokuwepo kwa mazingira rafiki na wezeshi ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na sera na kanuni. Kadhalika, tatizo la upatikanaji wa takwimu za uhakika na mifumo dhaifu ya takwimu iliongeza tatizo kwenye ufuatiliaji na tathmini ya sekta. Programu hiyo pia ilikuwa na changamoto na uwezo mdogo wa kiufundi na kifedha hususan katika miradi ya umwagiliaji. Pamoja na uwezo mdogo wa kupanga, kusimamia na kutekeleza miradi katika ngazi ya Halmashauri. Mazingira hayo yalichangia kucheleweshwa kwa malipo na matumizi ya fedha zilizopangwa mwaka hadi mwaka.

## D. MAFUNZO NA UZOEFU WA UTEKELEZAJI WA ASDP I

9. Uwekezaji wa umma katika sekta ya kilimo ni tofauti na sekta nyingine kwa sababu hauna matokeo ya moja kwa moja bila kuishirikisha sekta binafsi. Hivyo, ni muhimu kwa sekta ya umma kuweka mazingira wezeshi na kuiwezesha sekta binafsi (wafanyabiashara) ili kufikia malengo. Mafunzo na uzoefu uliopatikana kupitia utekelezaji wa ASDP I yatasaidia katika utekelezaji wa ASDP II. Baadhi ya masuala ya msingi ya kuzingatia ni (i) Mtazamo mpana wa utekelezaji wa pamoja uliofanywa na sekta ya kilimo unawezekana na ni muhimu sana katika uendelezaji wa sekta ya kilimo; (ii) Ni muhimu kuimarisha vyama vya ushirika (iii) Ni muhimu kuwa na mpango madhubuti na wa kipaumbele kwenye maeneo yenye fursa kubwa, ambayo ni pamoja na uzalishaji kuimarisha viwango vya juu vya minyororo

ya thamani (iv) Kuzingatia udhibiti, usimamizi, uratibu na ufuatiliaji wa mpango (v) Kuweka mazingira wezeshi ili kuisadia sekta ya kilimo (vi) Uwekezaji zaidi unahitajika katika sekta ya kilimo (serikali, sekta binafsi na washirika wa maendeleo). Hivyo, ni muhimu kuunganisha nguvu na kuratibu shughuli za sekta ya kilimo na serikali inapaswa kuwezesha na kuboresha ushiriki wa sekta binafsi, washirika wa maendeleo na ushiriki wa wadau wengine katika sekta ya kilimo.

## E. MAGEUZI KATIKA SEKTA YA KILIMO KUPITIA ASDP II

10. **Dhamira ya Programu**. ASDP II inalenga kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo kwa kutekeleza shughuli mbalimbali kwa kuzingatia vipaumbele ili kupunguza umaskini, kuongeza usalama wa chakula na lishe na ukuaji wa pato la Taifa. Pamoja kukabiliana na vikwazo na changamoto za utendaji wa sekta pia ASDP II itaongeza kasi ya ukuaji wa mchango wa sekta katika pato la Taifa, kuboresha ukuaji wa kipato cha wakulima wadogo na kuhakikisha usalama wa chakula ifikapo mwaka 2025. Utekelezaji wa Programu utazingatia mikakati yote ya kitaifa *(Tanzania Development Vision -TDV 2025)*, Mpango wa Taswira ya Muda Mrefu (LTPP 2012-2025) Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili (FYDP II 2016-2021), Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDS ) na Ilani ya uchaguzi ya CCM ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2015.

11. Minyororo ya thamani ya kipaumbele kwa kufuata Kanda za Kiikolojia za Kilimo (AEZ): ASDP II itatekelezwa katika mikoa yote kurahisisha utoaji wa huduma za msingi za umma kwa kujenga uwezo, kutoa huduma za ushauri kulingana na mahitaji, nk. Hata hivyo, kiwango cha uwekezaji kitazingatia bidhaa katika mnyororo wa thamani, Kanda za Kiikolojia za Kilimo na mbinu za utekelezaji zitategemeana na mazao ya kipaumbele yaliyochaguliwa kwenye kanda husika ya kiikolojia. Vigezo vya uchaguaji wa mazao ni pamoja na mchango wa zao katika kuhakikisha usalama wa chakula na lishe; bidhaa au zao linalolimwa au kuchakatwa na idadi kubwa ya wakulima, wafugaji na wavuvi hasa wadogo, upatikanaji wa teknolojia ya kuongeza uzalishaji na tija ya mazao; mchango wa zao katika upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda; (ajenda ya viwanda) na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na pia zao lizingatie soko la ndani na uwezo wa kuuzwa nje ya nchi.

12. Mazao ya kipaumbele katika utekelezaji wa ASDP II kwa miaka mitano ya mwanzo yalihusisha mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Mazao hayo ni mpunga, mahindi, muhogo, viazi, ndizi, kahawa, pamba, mazao ya mbegu za mafuta (alizeti, michikichi, ufuta, nazi), korosho, chai, sukari na mazao ya bustani. Mazao ya mifugo na uvuvi ni: maziwa, nyama ya ng'ombe, mbuzi, kuku, samaki, na mwani. Pamoja na kwamba mikoa imepangwa katika makundi ya Kanda za Kiikolojia za Kilimo, uchaguaji wa mazao utategemea na upatikanaji wa miundombinu husika.

13. Mazingira wezeshi: ASDP II itaweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuvutia uwekezaji, sekta binafsi ikiwa ni pamoja na wakulima kuwekeza kwenye kilimo. Mazingira wezeshi yatalinda na kuongeza upatikanaji wa ardhi kwa wakulima wadogo, kukuza mifumo bora ya soko na kutumia faida linganishi katika baadhi ya bidhaa zitakazowezesha uboreshaji wa maisha ya Watanzania.

14. Programu pia inalenga katika kuongeza ufanisi wa ugawaji na utumiaji wa rasilimali ili kuleta matokeo yenye tija.

15. ASDP II inasisitiza kuwepo kwa uongozi madhubuti na unaohusisha miundo ya uongozi imara ili kuhakikisha ufanisi wa uratibu, utawala, uwajibikaji na usimamizi.

## F. LENGO, MKAKATI NA MATOKEO YA ASDP II

16. Lengo: Kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo (mazao, mifugo na uvuvi) ili kuongeza tija, kufanya kilimo kiwe cha kibiashara na kuongeza kipato kwa wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha yao na kuongeza usalama wa chakula na lishe.

17. Mkakati: Kubadili wakulima wadogo kutoka kwenye kilimo cha kujikimu na kuwa wakulima endelevu wa kibiashara kwa kuamsha vichocheo vitakavyo wawezesha kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kipaumbele kwa kufuata mnyororo wa thamani.

18. Matokeo: ongezeko la upatikanaji wa uhakika wa masoko, kuongeza thamani, kipato cha wakulima, usalama wa chakula na lishe na Pato la Taifa.

## G. MANENO MAKUU YA ASDP II NA MAENEO YA UWEKEZAJI NA MIRADI/MIUNDO

19. Utekelezaji wa ASDP II unahusisha maeneo makuu manne ya kipaumbele yenye maeneo 23 ya kipaumbele ya uwekezaji. Maeneo hayo makuu pamoja na maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji yameainishwa kama ifuatavyo;

    **Eneo Kuu 1:** Usimamizi na Matumizi Endelevu ya Maji na Ardhi. Lengo la kipaumbele hiki ni matumizi endelevu ya maji na ardhi kwa ajili ya mazao, mifugo na uvuvi. Maeneo ya uwekezaji chini ya kipaumbele hiki ni (i) Mpango wa matumizi bora ya ardhi na usimamizi wa maji (ii) Kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji (iii) Usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji (iv) Uendelezaji wa vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo na uvuvi na (v) Kukuza na kuendeleza teknolojia za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi *(Climate Smart Agriculture -CSA).*

    **Eneo Kuu 2:** Kuongoza Tija na Faida. Lengo ni kuongeza kiwango cha uzalishaji chenye tija ambapo mkulima atatumia eneo dogo na kupata mavuno mengi zaidi na kwa kutumia gharama ndogo pia kufuata soko na kuimarisha mnyororo wa thamani wa bidhaa husika. Maeneo ya uwekezaji wa kipaumbele ni (i) Kuimarisha huduma za ugani, huduma za mafunzo (mazao, mifugo na uvuvi) (ii) Uboreshaji wa upatikanaji wa pembejeo kwa ajili ya mazao, mifugo na uvuvi na huduma za afya ya mimea na mifugo (iii) Utafiti na maendeleo (iv) Kuimarisha na kuongeza matumizi ya zana bora (mazao, mifugo na uvuvi) na (v) Uboreshaji wa Usalama wa chakula na lishe.

    **Eneo Kuu 3:** Biashara na Uongezaji Thamani kwenye mazao. Lengo ni kuboresha na kupanua masoko ya mazao, mifugo na uvuvi na kuongeza thamani ya mazao kwa kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi na vyama vya wakulima. Maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji ni (i) Kuendeleza upatikanaji wa masoko kwa bidhaa zote zilizopewa kipaumbele (ii) Kuendeleza upatikanaji wa masoko kwa ajili ya kilimo, uvuvi na bidhaa za mifugo na (iii) Kuendeleza usindikaji na kuongeza thamani ya mazao.

    **Eneo Kuu 4:** Mazingira Wezeshi, Uratibu na Ufuatiliaji na Tathmini: Lengo ni kuweka mazingira wezeshi na kuimarisha taasisi, mifumo na uratibu. Maeneo ya uwekezaji ni (i) Kupitia sera na miongozo inayohusiana na kilimo, mifugo na uvuvi na kuboresha mazingira ya biashara kwenye sekta ya kilimo; (ii) Kuimarisha uwezo wa wazalishaji hasa wakulima wadogo na wasindikaji ili wazalishe na kusindika kwa kupitia vyama au ushirika wa wakulima; (iii) Kuimarisha ushiriki wa jinsia zote kwenye shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi (iv) Kuboresha na kuimarisha uratibu wa sekta (v) Kuboresha uwezo na mifumo ya ukusanyaji na usimamizi wa takwimu za kilimo (vi) Uwezo wa usimamizi na uboreshaji wa Mfumo (vii) Kuimarisha mifumo ya tathmini na ufuatiliaji wa Sekta ya Kilimo (viii) Kujenga uwezo katika ngazi zote (ix) Uboreshaji wa teknolojia ya habari na mawasaliano (TEHAMA) kwa ajili ya Kilimo; na (x) Kutoa huduma za kifedha.

20. Hata hivyo, ili kurahisisha utekelezaji wa Programu, kila eneo la uwekezaji limeandaliwa miradi mbalimbali ya uwekezaji ambapo jumla ya miradi 56 imeandaliwa kwa ajili ya utekelezaji. Katika ngazi ya Halmashauri, miradi ya uwekezaji ya ASDP II itatekelezwa kama sehemu ya Mpango wa Maendeleo ya Wilaya. Miradi iliyopendekezwa itaandaliwa na kuwezeshwa katika ngazi zote na pia kuandaliwa viashiria vya utekelezaji.

## H. MPANGO, MTIRIRIKO NA MPANGILIO WA UTEKELEZAJI WA ASDP II

21. Ili kuwa na utekelezaji wenye mtiririko mzuri, miradi ya ASDP II imepangwa kwa kufuata umuhimu na muda wa utekelezaji. Hii ni pamoja na mpango wa utekelezaji, umuhimu, mchakato na muda wa utekelezaji wa miradi ambao utaleta matokeo na kutatua changamoto kwa kutumia fursa zilizopo ili kuleta mageuzi chanya kwenye sekta ya kilimo. Kwa kuzingatia changamoto za sasa ambazo zinawakabili wakulima wadogo na wawekezaji, ni muhimu kuweka mazingira rafiki ya kuiwezesha sekta na vipaumbele vyake kutekelezeka. Kwa hiyo, msisitizo wa utekelezaji utaanza na **eneo kuu la 4** ambalo linawezesha utekelezaji wa vipengele na vipaumbele vingine ili kurahisisha uwekezaji wa sekta binafsi na umma kuwa rafiki. Eneo kuu linalofuata ni la 3 (Biashara na Kuongeza thamani), ambalo ni

kichocheo cha kuongeza uzalishaji, tija na kilimo chenye faida chini ya eneo kuu la 2. Utekelezaji wa maeneo hayo utahitaji matumizi endelevu ya maji na ardhi chini ya eneo kuu la 1. Hata hivyo, mtiririko wa utekelezaji uliopendekezwa ili kuchochea utekelezaji wa programu utategemeana na upatikanaji wa rasilimali. Kimsingi miradi yote inaweza kutekelezwa kwa wakati mmoja iwapo fedha zinapatikana. Iwapo kutakuwa na ugumu wa upatikanaji wa fedha, eneo kuu la 1 la kipaumbele lianze kutekelezwa na kufuatiwa na maeneo mengine yaliyopendekezwa. .

## I. MFUMO WA KITAASISI CHINI YA ASDP II

22. Wakati wa utekelezaji wa ASDP I kulikuwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na udhaifu wa udhibiti, taasisi na usimamizi wa programu na fedha. Changamoto hizi zilichangiwa na usimamizi duni na mifumo dhaifu ya uwajibikaji kwenye miradi katika ngazi zote. Pia, kulikuwa na ushirikiano hafifu ndani ya wizara za kisekta na ukosefu wa fedha kwenye maeneo[3] muhimu mathalani umwagiliaji.

23. ASDP II imeweka mifumo imara ya taasisi, utaratibu wa udhibiti na usimamizi bora wa miradi kuanzia ngazi ya Kitaifa hadi Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii ni pamoja na: ushiriki wa Serikali katika uratibu wa wadau wote na pia ushirikiano wa wadau kwa ajili ya ufanisi wa sekta; majukumu kwa kila mdau; uwajibikaji na utekelezaji wa programu kwa kuzingatia vipaumbele na matokeo; kuwezesha usimamizi sahihi wa fedha na mifumo ya ukaguzi katika programu na miradi. Uongozi wote wa Programu utakuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kitengo cha Taifa cha uratibu wa ASDP II kitatekeleza shughuli za kila siku za programu na kusimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Wizara ya Kilimo. Wizara za Kisekta zitakuwa na vitengo vya uratibu wa ASDP II ndani ya Wizara zao na wadau muhimu wataendelea kutoa ushauri wa kitaalamu.

24. Mikutano ya ASDP II katika ngazi ya Taifa itajumuisha Mkutano wa Taifa wa Wadau wa Sekta ya Kilimo *(National Agricultural Sector Stakeholders Meeting-NASSM)* ambao utatanguliwa na Mkutano wa Mawaziri wa Wizara za kisekta. Pia kutakuwa na Mkutano wa Makatibu Wakuu wa Wizara za Sekta ya Kilimo, Kamati ya Usimamizi na Maamuzi ya Sekta ya kilimo *(Agricultural Sector Committee -ASC),* Kamati ya Ushauri wa Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Consultative Group-ASCG),* Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi *(Technical Committe of Directors)* na mikutano ya Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II ambacho kitaongozwa na Mratibu mkuu wa Programu.

25. Mkutano Mkuu wa Wadau wote katika Sekta ya Kilimo (NASSM) utakuwa chini ya uenyekiti wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na washiriki wake watakuwa ni pamoja na Mawaziri kutoka Wizara zote za Sekta ya Kilimo, Makatibu Wakuu kutoka Wizara za Sekta ya Kilimo, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Sera na Mipango kutoka katika Wizara za Sekta ya kilimo, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Idara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Wilaya; taasisi za utafiti; maafisa wa mafunzo ya ugani; wawakilishi kutoka mashirika ya wabia wa maendeleo na sekta binafsi na wakuu wa bodi za mazao, mifugo na uvuvi. Ajenda ya mkutano huu wa kila mwaka ni kujadili maendeleo ya sekta ya kilimo, vipaumbele, miongozo na sera kwenye sekta ya kilimo na kutoa ushauri, mwongozo na maelekezo ya utekelezaji wa ASDP II.

26. Kamati ya Usimamizi na Maamuzi ya sekta ya kilimo (ASC) itakuwa chini ya Uenyekiti wa Waziri wa nchi Ofisi ya Waziri Mkuu. Wajumbe katika mkutano huu ni pamoja na Makatibu Wakuu kutoka Wizara za Sekta ya Kilimo, Wakurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara za Sekta ya kilimo, Washirika wa Maendeleo na Mashirika yasiyo ya kiserikali. Ajenda itajumuisha mapitio na kupitisha mipango ya ASDP II, bajeti, ripoti za tathmini na ufuatiliaji n.k

27. Mkutano wa Kamati ya Ushauri wa Sekta ya Kilimo (ASCG) utaongozwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu. Wajumbe watakuwa ni: Makatibu Wakuu kutoka Wizara za Sekta ya Kilimo, Wakurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara za Sekta ya kilimo, Wawakilishi wa Wahisani wa maendeleo na mashirika yasiyo ya Kiserikali. Ajenda itajumuisha masuala ya sera, mapitio na kupitisha mipango ya ASDP II, bajeti, taarifa za tathmini na ufuatiliaji n.k.

3 *Ripoti ya orodha ya miradi ya uwekezaji katika kilimo nchini (TAN-AIM, 2015/2016)*

28. Mkutano wa Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi utaongozwa Mkurugenzi wa Uratibu wa Shughuli za Serikali-Ofisi ya Waziri Mkuu. Wajumbe wa mkutano huu ni: Wakurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara za Sekta ya Kilimo. Ajenda ya mkutano huu itajumuisha mapitio na mipango ya bajeti na kuandaa hadidu za rejea za vikao mbalimbali, kuandaa taarifa za tathmini na ufuatiliaji n.k.

29. Mkutano wa Viongozi wa Maneno Makuu ya ASDP II utaongozwa na Mkurugenzi wa utaratibu wa sekta OR-TAMISEMI. Wanachama watakuwa ni wenyeviti wa vikundi kazi vya kitaalamu (TWG) na ajenda itakua ni kupitia mipango ya maeneo makuu, kupitia na kuchambua taarifa.

30. Vikundi Kazi vya Kitaalam (TWGs) vya makundi mbalimbali vitasimamiwa na wakuu wa TWG na wajumbe watakuwa ni wataalam kutoka kwenye idara za wizara za kisekta na ajenda itajumuisha maandalizi na uhakiki wa mipango ya bajeti ya ASDP II na kuwasilisha ripoti mbalimbali za utekelezaji wa ASDP II.

31. Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II kitatumika pia kama Sekretarieti ya ASDP II, inayoongozwa na Mratibu Mkuu wa Programu wa Taifa. Wajumbe ni pamoja na wataalam walioteuliwa na wizara za kisekta kufanya kazi kwenye timu ya uratibu ya ASDP II na sekta binafsi. Ajenda ya kikao ni kutekeleza shughuli za kila siku za ASDP na kuandaa vikao mbalimbali vya Programu .

32. Kwa utekelezaji wa ufanisi, uratibu na uongozi kutakuwa na kitengo cha uratibu katika ngazi ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo itasimamia uratibu na usimamamizi wa shughuli zote za ASDP II kuanzia ngazi ya kijiji.

## J. TATHMINI NA UFUATILIAJI WA ASDP II

33. Kutakuwa na ufuatiliaji na tathmini ya ndani na nje ya ASDP II. Katika ngazi ya kata, Serikali itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji ambapo Afisa Mtendaji wa Kata atakuwa na jukumu la kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Afisa Mtendaji wa Kijiji. Mfumo wa usimamizi na ufuatiliji wa ASDP II utawekwa katika ngazi zote ( Taifa, OR-TAMISEMI, Mikoa na Wilaya). Kitengo cha Taifa cha uratibu kitaratibu mapitio ya mwaka na tathmini. Aidha, katika ngazi ya Taifa na OR-TAMISEMI kutakuwa na Kikundi Kazi cha Ufuatiliaji na Tathmini mzunguko wa ufuatiliaji na tathmini iliowekwa ili kufikia matokeo yanayotarajiwa.

## K. GHARAMA , UGHARAMIAJI NA USIMAMIAJI WA ASDP II

34. Makadirio ya gharama za utekelezaji wa ASDP II kwa miaka mitano ni kiasi cha Shilingi za Kitanzania trilioni13.819 (Dola za Marekani bilioni 5.979). Na wastani wa makadirio ya gharama za utekelezaji kwa mwaka ni kati ya Shilingi za Kitanzania trilioni 2.284 (Dola za Marekani milioni 988) hadi shilingi trilioni 3.238 (Dola za Marekani milioni 1,400). Kati ya fedha hizo, kiasi cha asilimia 25 kitatumika katika ngazi ya Wizara za Kisekta na asilimia 75 zitatumika katika kutekeleza shughuli za ASDP II ngazi ya Halmashauri.

35. Mgawanyo wa rasilimali fedha kwa kila eneo kuu la programu ni kama ifuatavyo **Eneo kuu la 1:** Matumizi Endelevu ya Maji na Ardhi shilingi trilioni 2,024 (Dola za Marekani milioni 941) zimetengwa kwa ajili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Eneo kuu la. 1 litachukua asilimia15 ya gharama zote za utekelezaji wa Programu. Gharama za **Eneo kuu la. 2:** Kuongeza Uzalishaji na Tija zinakadiriwa kutumika shilingi za Kitanzania trilioni 8.081 (Dola za Marekani milioni 3.758) au asilimia 58 ya jumla ya gharama za Programu. **Eneo Kuu la. 3:** Biashara na Uongezaji Thamani kwenye mazao (ikiwa ni pamoja na uwekezaji wa kuendeleza mnyororo wa thamani) inakadiriwa kugharimu shilingi trilioni1,483 (Dola za Marekani milioni 1.663) au asilimia 26 ya jumla ya gharama zote za Programu. Kadhalika, gharama za **Eneo kuu la.4:** Mazingira Wezeshi, Uratibu, Ufuatiliji na Tathmini inakadiriwa kuchukua kiasi cha shilingi bilioni 137 (Dola za Marekani milioni 67) au asilimia 1 ya gharama za Programu hii.

36. Vyanzo vikuu vya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ASDP II, ni pamoja na: Serikali, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ikiwa ni pamoja na sekta binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali na wakulima. Msingi ya kuandaa mpango wa mahitaji ya fedha za programu imezingatia kiasi ambacho

kitatolewa na wachangiaji kwa kila eneo kuu na dogo na utekelezaji. Kwa upande wa uchangiaji wa fedha za Programu, Serikali inapendelea kutumia utaratibu wa Mfuko wa Pamoja (*basket fund*). Hata hivyo, baadhi ya wadau wanapendelea kufadhili miradi ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kutumia mfumo wa moja kwa moja *(stand-alone project)* bila ya kupitisha fedha kwenye mfuko wa pamoja. Ni muhimu kuwepo kwa mawasiliano bayana, uwazi na uratibu wakati wa upangaji wa pamoja wa mipango na bajeti na utekelezaji wa Programu.

## L. MUHTASARI WA MANUFAA YA PROGRAMU

37. Mageuzi ya kilimo na kasi ya kukua kwa maendeleo hasa vijijini yatatoa mchango mkubwa kwenye ukuaji wa uchumi wa nchi. Manufaa makuu ya Programu ni pamoja na: (i) Kuongezeka kwa tija na uzalishaji endelevu wa bidhaa za chakula na zisizo za chakula ili kuboresha mapato kwa wakulima, kuongeza uhakika wa upatikanaji wa chakula katika ngazi ya kaya na kitaifa, na kutoa malighafi kwa ajili ya viwanda vya kilimo; (ii) Kupunguza kiwango cha lishe duni na utapiamlo katika jamii za vijijini na ulinzi kutokana na athari za majanga ya asili; (iii) Kuongezeka kwa Kilimo cha kibiashara na kipato kinachotokana na shughuli za mashambani na zisizo za mashambani hususani wakulima wadogo (ambao ni asilimia 97.5 ya kaya za vijijini); (iv) Kulinda na kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa muda mrefu wa rasilimali za Tanzania kupitia njia endelevu za usimamizi wa ardhi na maji na hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na (v) Kuimarika kwa uwezo wa kitaasisi wa kuhamasisha na kusimamia rasilimali kwa maendeleo ya sekta ya kilimo. Programu hii itachangia katika malengo ya maendeleo ya kitaifa kama yalivyoainishwa katika Dira ya Taifa 2025.

38. Faida nyingine zinazotazamiwa ni pamoja na (i) Kupungua kwa upotevu wa mazao wakati na baada ya kuvuna (ii) Kuongezeka kwa mapato ya nje (iii) Kuongeza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali za kilimo (iv) Kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wakulima wadogo na wajasiriamali wa vijijini; (v) Kupungua kwa gharama za uzalishaji katika shughuli za kilimo na kuongeza ufanisi katika mnyororo wa thamani kabla na baada ya mavuno; (vi) Kuongezeka kwa ushiriki wa wakulima katika vyama vya ushirika (vii) Kuboresha upatikanaji wa masoko kupitia uendelezaji wa miundombinu; (viii) Kuongezeka kwa ajira za vijijini; (ix) Kuongezeka kwa tija ya uzalishaji kutokana na kilimo cha umwagiliaji; (x) Kulinda uoto wa asili na viumbe hai (*biodiversity*); na (xi) Kuimarishwa kwa mfumo wa usimamizi wa majanga kwa kuongeza zana na matumizi yake; (xii) Kuongeza hali ya usawa wa kijinsia; (xiii) Kupunguzwa kwa ajira za watoto katika sekta ya kilimo kwa kuzingatia miongozo ya Shirika la Kazi Duniani (ILO)[4]; na (xiv) Kupungua kwa mchango wa Kilimo katika uharibifu wa mazingira kutokana na matumizi ya teknolojia zinazostahimili mabadailiko ya tabianchi[5].

4 *Maazimio ya kongamano la kimataifa kuhusu haki za wafanyakazi wa mashambani "Geneva,15-18 Septemba 2003"*

5 *(Lipper et al.2014)*

# I. UTANGULIZI[6]

## A. Viashiria vya kiuchumi na Sekta ya Kilimo[7]

1. Viashiria vya uchumi wa Tanzania vinabainisha ukuaji mkubwa wa Pato la ndani la Taifa kabla na wakati wa utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza (ASDP-1) ulioanza mwaka 2006. Kati ya mwaka 2006 na 2014 kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa ilikuwa kati ya asilimia 6.0 na asilimia 8.1 kwa kutumia bei za mwaka 2007. Pamoja na viwango vya ukuaji wa Pato la Taifa wa sekta ya kilimo, ulikuwa chini ya ukuaji wa Pato la Taifa isipokuwa mwaka 2008 ambapo ukuaji ulifikia asilimia 6.5 (tazama kielelezo Na.1)[8]. Kwa wastani, sekta za huduma na viwanda zilionesha kiwango kikubwa cha ukuaji kuliko sekta ya Kilimo. Kiwango cha ukuaji wa sekta ya Kilimo katika kipindi cha mwaka 2006-2014 kilikuwa ni wastani wa asilimia 3.9 kwa mwaka, na sekta za huduma na viwanda ilikuwa ni sawa na wastani wa asilimia 8 na wastani wa asilimia 7.8 mtawalia. Mchango wa sekta ya Kilimo kwenye Pato la Taifa ulipungua kutoka asilimia 27.7 mwaka 2006 hadi asilimia 23.2 mwaka 2012, wakati mchango wa sekta za huduma na viwanda uliongezeka kutoka asilimia 20 hadi asilimia 22, na kutoka asilimia 46 hadi asilimia 49 kwa kipindi hicho[9].

**Kielelezo Na.1: Kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa kwa sekta (%, kwa bei za mwaka 2007)**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania. Marejeo ya kiuchumi ya kila mwaka, Mei 2015

2. Kutokana na kushuka kwa mchango wa sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa na ukuaji wa wa Uchumi, ni dhahiri kuwa ukuaji huo hauwanufaishi walio wengi katika sekta ya Kilimo ambao ni wengi. Hali hiyo imechangia wale wanaotegemea sekta ya kilimo kuendesha maisha yao kushindwa kujinasua kutoka katika lindi la umaskini. Kwa mfano, kwa takwimu za idadi ya watu vijijini walikadiriwa ilikuwa ni asilimia 80 ya idadi ya watu wote nchini na kiwango cha umaskini vijijini kilikuwa asilimia 40. Mwaka 2007, baada ya miaka 15, idadi ya watu vijijini ilikuwa asilimia 74 ya idadi ya watu wote nchini na kiwango cha umasikini ulikadiriwa kuwa asilimia 37.8. Ni dhahiri kwamba idadi ya watu na kiwango cha umaskini vijijini nchini Tanzania hakijabadilika kwa kiwango kikubwa. Sekta ambazo zinachangia katika ukuaji wa uchumi, kama vile ujenzi, fedha, madini, huduma[10], na mawasiliano ya simu hazikutoa fursa za ajira katika maeneo ya vijijini na hazijaleta manufaa ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja kwa watu wa vijijini. Aidha, ukuaji mkubwa wa uchumi kwa zaidi ya muongo mmoja ulipita haukuhusisha kupungua kwa umaskini kwa kiasi kikubwa kutokana na sekta ya kilimo kukua kwa kiasi

6 *Utangulizi sura ya I na II) imetoholewa kutoka msaada wa FAO-TCIA kwenye ASDP I-BF June 2013.*

7 *Taarifa ya hali ya uchumi ya Tanzania: Benki ya Dunia, Oktoba 2012.*

8 *Angalia pia http://data.worldbank.org/indicator/NY.GDP.MKTP.KD.ZG/countries.*

9 *Kulingana na Benki ya Dunia (http://data.worldbank.org/indicator/NV.AGR.TOTL.ZS/countries) asilimia ya thamani ya mauzo ya kilimo,katika pato la Taifa linakadiriwa kuwa 28.1%, 27.7%, 28.7% na 28.4% kwa mwaka 2010, 2011, 2012 na 2013 kadhalika kwa hali hii kilimo kinawiana na ISIC katika mgawanyo wa 1–5 na kwa kujumuisha misitu, uwindaji na uvuvi, pamoja na mazao ya kilimo na mifugo.*

10 *Kujumuisha na utalii.*

kidogo ukilinganisha na sekta nyingine. Hivyo, ukuaji wa sekta ya Kilimo haujachochea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa Pato la Taifa kama ilivyokuwa katika miaka ya 1970 na 1980 ambapo ukuaji wa sekta hiyo ulichangia asilimia 50 ya Pato la Taifa ni wazi kwamba ukuaji wa sekta ya Kilimo haukuchangia kupungua kwa umaskini nchini Tanzania[11].

3. Kwa mujibu wa taarifa za uchumi kwa mwaka 2012 za Tanzania zilionesha[12]ukuaji wa kasi na utenganifu wa uchumi umezalisha gawio kwa Tanzania katika miaka ya hivi karibuni na kuchangia kuongezeka kwa pato la kila Mtanzania hadi asilimia 70 katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Hata hivyo, manufaa hayo hayajawanufaisha walio wengi. Ili kupambana na umaskini ulioko vijijini ni muhimu kuwepo kwa mifumo ya kiuchumi ambayo inawaunganisha wakulima, wafugaji na wavuvi na masoko. Uchumi wa aina hiyo huhamasisha wakulima, wafugaji na wavuvi kuzalisha mazao yenye kuongeza kipato zaidi mazao ambayo si ya asilia na kuwezesha kupunguza idadi ya watu kukimbilia mijini. Hiyo itawezesha ukuaji na usawa wa maendeleo ya kiuchumi nchini. Aidha, badala ya kufanya marekebisho madogo ya kisera katika kupambana na umaskini vijijini yanahitajika mabadiliko makubwa ya kisera ambayo yatahusisha: (i) Kilimo-biashara; (ii) Upanuzi wa shughuli za sekta ya kilimo kwa kuzalisha bidhaa mbalimbali; na (iii) Uendelezaji wa miji. Changamoto ya watunga sera nchini ni kuchochea nguvu za mabadiliko endelevu katika hayo mambo matatu.

## B. Sekta ya Kilimo

4. Mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa ambao unajumuisha shughuli za mazao, mifugo, misitu na uwindaji, na uvuvi katika miaka ya hivi karibuni ulifikia asilimia 18, 5, 3 na 1.4, mtawalia. Tanzania ina jumla ya hekta (ha) milioni 7.1 za ardhi ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji, kati ya hizo hekta milioni 2.3 zina fursa ya kiwango cha juu cha kuendelezwa na hekta milioni 4.8 zina fursa ya kiwango cha kati cha kuendelezwa kwa kutumia mito, maziwa, sehemu oevu na maeneo ya miamba ya maji. Hadi kufikia mwaka 2015, kati ya hekta milioni 2.3 zenye fursa ya kiwango cha juu ni hekta 461,326 sawa na asilimia 20 ambazo miundombinu yake ilikuwa imeendelezwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji (MAFC, 2015). Inakadiriwa kuwa asilimia 55 ya ardhi inaweza kutumika kwa ajili ya shughuli za kilimo, na zaidi ya asilimia 51 kwa ajili ya malisho ya mifugo. Hata hivyo, ni asilimia 6 tu ya ardhi ya kilimo imetumika. Tabia ya kulima na kufuga kwa kuhama hama husababisha uharibifu wa mazingira ikiwemo misitu na ardhi. Tanzania ni moja ya nchi chache za Afrika ambazo bado zina rasilimali nyingi ya wanyamapori na maeneo yaliyohifadhiwa ambayo ni takribani asilimia 25 ya eneo la ardhi yote.

**Kielelezo Na.2. Mchango wa sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa (%), kwa bei za mwaka 2001**




11 *Mapitio ya sera ya chakula na kilimo Tanzania. Ripoti ya MAFAP, 2013, FAO, Rome, Italy*
12 *Taarifa ya Benki ya Dunia :http://www-wds.worldbank.org/*

Ukuaji wa Sekta ya kilimo kwa kiasi kikubwa unakwamishwa na tija ndogo katika matumizi ya ardhi na nguvukazi. Japokuwa hali hiyo husababishwa na mambo mengi, sababu kuu za msingi ni pamoja na: (i) Mbinu duni za uzalishaji; (ii) Ukosefu wa masoko, miundombinu duni ya masoko na uongezaji mdogo wa thamani katika ngazi ya mkulima; (iii) Miundombinu duni ikiwa ni pamoja na barabara za vijijini, mawasiliano na nishati ya umeme ; na (iv) Uhaba wa fedha kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya kilimo. Aidha, matumizi ya pembejeo bora kwa ajili ya kuongeza tija ni kidogo ikilinagnishwa na nchi nyingine. Kwa mfano, wakulima wa Tanzania hutumia kati ya kilo 8-10 za mbolea kwa hekta, ikilinganishwa na wastani wa kilo 16 kwa hekta kwa nchi za Jumuiya ya Nchi Zinazoendelea Kusini mwa Afrika (SADC), nchi ya Malawi inatumia wastani wa kilo 27 kwa hekta na nchi ya China kilo 279 kwa hekta kwa wastani. Pamoja na kiwango hicho cha chini cha matumizi ya mbolea, pia soko la Tanzania limeshindwa kutumia kiasi kilichokuwepo cha mbolea kutoka kwa wafanyabiashara ambapo kulikuwa na ziada ya kati ya asilimia 15 na 30 katika misimu ya 2007/2008 na 2009/2010. Mahitaji ya mbegu bora kwa mwaka ni takriban tani 120,000 wakati upatikanaji wake ni tani 30,000 tu sawa na asilimia 25 ya mahitaji yote. Kati ya tani 30,000 asilimia 75 ni za mahindi. Pamoja na upatikanaji na matumizi kidogo ya pembejeo bora, kumekuwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya pembejeo kuanzia mwaka 2007/2008 baada ya Serikali kuanza kutoa ruzuku ya pembejeo kwa mfumo wa Vocha (NAIVS). Hii iliimaanisha kuwa mfumo huo umeongeza matumizi ya pembejeo kwa wakulima.

**Kielelezo Na.3: Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi (kwa bei ya sasa—TSh bilioni)**[13]




**Kielelezo Na.4:Asilimia ya Pato la Taifa kutokana na shuguli za kiuchumi (katika% ya Pato la Taifa—kwa bei ya sasa)**




5. **Sekta ndogo ya mazao.** Taarifa za uzalishaji wa mazao makuu aina zote katika kipindi cha miaka 50 iliyopita kama zinavyotolewa na Shirika la Chakula Duniani (FAOSTAT) zinaonesha kuwa mabadiliko yalianza kutokea mwaka 2000 ambapo: (i) Uzalishaji wa nafaka (mahindi, mchele, mtama na uwele) uliongezeka na kuzidi kiasi cha muhogo unaozalishwa kwa mwaka; (ii) Ongezeko kubwa la uzalishaji lilitokea hasa katika mahindi, ndizi, sukari na mazao mengine ya mizizi na kiasi kidogo kwa mazao ya

13 *Imenukuliwa kwenye taarifa ta mapato Tanzania bara (mwaka 2007). Ofisi ya taifa ya takwimu, Wizara ya Fedha, Novemba 2014.*

mbegu za mafuta (Kielelezo No.5). Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita, tija ya uzalishaji ya mazao makuu ya chakula iliongezeka maradufu na kufikia takriban tani 1.5 ya mahindi na tani 2.0 ya mpunga kwa hekta. Uzalishaji wa mazao ya jamii ya mikunde na mbegu za mafuta pia uliongezeka, japokuwa uliendelea kuwa chini ya wastani wa tani 1.0 kwa hekta kwa msimu kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 6.

**Kielelezo Na.5: Mazao makuu yanayozalishwa Tanzania (1961–2013, kwa tani)**




**Kielelezo Na.6: Mabadiliko ya tija ya mazao makuu kwa tija nchini Tanzania (1961–2013, kg/ha)**




6. **Sekta ndogo ya Mifugo.** Sekta hii inajumuisha takriban ng'ombe milioni 21.3, mbuzi milioni 15.2, na kondoo milioni 6.4. Mifugo mingine ni pamoja na Nguruwe milioni 1.9, kuku wa kienyeji milioni 35.1 na kuku wa kisasa milioni 23. Tanzania ni nchi ya tatu kwa idadi kubwa ya ng'ombe Afrika baada ya Ethiopia na Sudan. Takriban asilimia 90 ya idadi ya mifugo ni ya asili ambayo inauwezo mdogo wa kuzalisha maziwa na nyama. Sekta ndogo ya Mifugo inakua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 4.2 ikilinganishwa na asilimia 3.6 ya sekta nzima. Idadi ya ng'ombe iliongezeka kwa wastani wa asilimia 1.4 na ufugaji wa kuku ulifikia kiwango cha ukuaji cha asilimia 9.6 hadi kufikia kuku milioni 58.

7. **Uchakataji wa nyama.** Serikali imehamasisha sekta binafsi kuwekeza katika machinjio ya kisasa katika mikoa ya Rukwa, Dodoma, Arusha, Morogoro na Pwani. Aidha, serikali imeuza baadhi ya hisa zake katika kampuni zinazomilikiwa na Serikali kama vile Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) na

machinjio ya Dodoma. Japokuwa katika kipindi cha 2001 hadi 2009 idadi ya viwanda vya kusindika maziwa imeongezeka kutoka 22 hadi 39, bado kuna fursa kubwa ya kuongeza viwanda vya kusindika maziwa hadi kufikia lita bilioni 1.5 kwa mwaka, kwani kwa sasa maziwa yanayosindikwa ni asilimia 20 tu ya maziwa yanayokusanywa. Hali kadhalika kampuni binafsi zimeanza tena kusindika maziwa katika viwanda vilivyopo Musoma, Arusha, Tanga, Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Mbeya na Njombe. Kufuatia uboreshaji wa mazingira ya kufanya biashara, idadi ya viwanda vya kusindika ngozi imeongezeka kutoka viwanda 3 hadi 6 kati ya mwaka 2001- 2009, vyenye uwezo wa kusindika asilimia 52 ya ngozi zinazozalishwa sawa na futi za mraba milioni 48.2 zenye thamani ya Shilingi bilioni 12.8 (mwaka 2009).

8. **Uvuvi.** Tanzania ina rasilimali ya uvuvi katika maji chumvi (baharini) na maji baridi (maziwa, mito na mabwawa). Maji ya bahari ni eneo la kilomita za mraba 64,0000 na ukanda wa pwani una kilometa 1,424. Ukanda Maalum wa Kiuchumi (EEZ) unafikia ukubwa wa kilomita za mraba zipatazo 223,000 hivyo kuipa nchi eneo la ziada la bahari lenye rasilimali za uvuvi. Eneo la uvuvi katika maji baridi ya maziwa makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa) una kilomita za mraba 62,000. Aidha, kuna maziwa madogo ya asili, maziwa yaliyochimbwa na binadamu, mifumo ya mito na maeneo mengi oevu ambayo yana rasilimali za samaki. Licha ya uwepo wa fursa hizo kubwa za uvuvi, rasilimali nyingi zikiwemo zile za EEZ hazijatumika. Sekta ya uvuvi inaendeshwa zaidi na wavuvi wadogo na wafugaji wa samaki ambao kwa kawaida wanatumia teknolojia duni. Hivyo, sekta ndogo ya uvuvi ni eneo ambalo kama likitumika vizuri litaweza kuimarisha uchumi kwa kiasi kikubwa. Ukuaji wa sekta ndogo ya uvuvi umekuwa ukibadilika kila mwaka. Kwa mfano mwaka 2014 ukuaji ulikuwa asilimia 2.0 na mwaka 2013 ulikuwa asilimia 5.5. Kwa muda mrefu mchango wa sekta ndogo ya uvuvi katika Pato la Taifa umekuwa hauongezeki au kuwa na mabadiliko kidogo ya asilimia 0.1. Mwaka 2010 mchango wa shughuli za uvuvi ulikuwa asilimia 1.5 kabla ya kupungua hadi asilimia 1.4 mwaka 2011 na 2012; mwaka 2013 na 2014 ulipungua zaidi kufikia asilimia 1.3.

9. **Uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Usindikaji.** Sekta hii ndogo ina uwezo wa kuzalisha ajira, kuongeza tija katika uzalishaji, kuhawilisha teknolojia, kuongeza ushindani, kupunguza uingizaji wa bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi kutoka nje ya nchi, kuongeza mauzo ya bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi nje ya nchi, na kuchangia maendeleo endelevu ya kiuchumi ya Taifa. Ingawa kuna ongezeko la uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ya nchi, uwekezaji katika sekta ya kilimo umebaki kuwa mdogo kwa kiasi cha asilimia 2 hadi asilimia 3 ya uwekezaji wote unaotoka nje (Dola milioni 31.4 mwaka 2011). Ukuaji wa haraka wa miji na kuongezeka kwa kipato ni sababu za kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa zilizosindikwa. Hata hivyo, uendelezaji mdogo wa viwanda vya kusindika bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi umeshindwa kutoa mchango wa kutosha kuwezesha kupunguza uingizaji wa bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi kutoka nje kwa ajili ya masoko ya chakula mijini. Kushindwa kukidhi mahitaji na upatikanaji wa bidhaa za vyakula vilivyo sindikwa ulisababisha kuongezeka mara tatu kwa gharama za uagizaji wa chakula kati ya mwaka 2006 na 2013 sawa na Dola za Kimarekani milioni 963.9. Duniani kote ukuaji wa uchumi unatokana na maendeleo ya sekta ya kilimo kwa kusindika mazao ya msingi, hivyo kusababisha kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta za viwanda na huduma.

## C. Mazingira ya Kisera

10. Tanzania imekuwa na sera za muda mrefu na wa kati hususan katika sekta ya Kilimo. Mifumo ya sera ya muda mrefu inatoa kipaumbele kwa sekta ya kilimo na hivyo kuchangia katika maboresho ya sera mbalimbali zikiwemo za sekta ndogo. Masuala yanayohusiana na usimamizi wa maliasili yanashughulikiwa kama inavyotakiwa ili kufikia malengo ya muda mrefu ya kijamii na kiuchumi. Sera muhimu ambazo zinashughulikia sekta ya kilimo zinaelezewa kwa muhtasari katika sehemu zinazofuata.

11. **Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025.** Hii ni dira ya muda mrefu iliyowekwa na Serikali ya Tanzania ili kuleta maendeleo. Dira inaelekeza kuwa ifikapo mwaka 2025, Tanzania itakuwa na maendeleo makubwa, yanayolenga watu, amani, jamii imara iliyoungana na yenye kiwango bora cha maisha na kiwango kikubwa cha maendeleo ya watu *"Uchumi uliobadilika kutoka tija ndogo ya uchumi wa kilimo kwenda uchumi wa kati, unaoongozwa na mbinu za kisasa za uzalishaji katika shughuli za kilimo ambazo zimeunganishwa kwa ufanisi na kuzingatia shughuli za viwanda na huduma katika*

*maeneo ya vijijini na mijini. Msingi ulio imara wa uchumi wa uzalishaji, ushindani utawekwa"*. Sekta ya kilimo inatambulika kuwa eneo muhimu ambapo hatua za kimkakati zitatekelezwa ili kuchangia katika kujenga msingi imara na madhubuti wa uchumi kwa ajili ya uzalishaji, ushindani na uchumi imara[14].

**Kielelezo Na. 7. Mfumo wa Sera kwa ajili ya kuleta mageuzi katika ya Sekta ya Kilimo**




12. **Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania Awamu ya Kwanza na ya Pili** Mkakati huu unajulikana kama MKUKUTA I na II ni mojawapo ya mikakati ya Kitaifa inayolenga kulifikisha Taifa kwenye Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs). Vipengele muhimu katika kuandaa MKUKUTA I na II vilikuwa ni umiliki wa Kitaifa na mashauriano na wadau kwa lengo la kukuza na kuimarisha ushirikiano kati ya sekta na wadau. Mkakati unahitaji utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya bajeti ya Serikali ili ifungamane na malengo ya Kitaifa na kuwa na mahusiano ya moja kwa moja ya kufanya mapitio ya matumizi ya bajeti hiyo. Mfumo wa Pamoja wa ushirikiano wa maendeleo umeandaliwa na washirika wa maendeleo ili kuongeza kasi na ufanisi wa misaada, usawa na ufanisi ili kufikia malengo[15] ya MKUKUTA. Maeneo ya kimkakati ya MKUKUTA II ni Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato, ukilenga usawa na kuongezeka kwa uzalishaji wa ajira, msingi wa maendeleo endelevu, usalama wa chakula na huduma za kisasa na za kuaminika za upatikanaji wa nishati na miundombinu ya kutosha kwa ajili ya shughuli za uzalishaji. Sekta ya Kilimo imetambulika kama moja ya maeneo muhimu ya kukuza uchumi na njia ya kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025.

13. **Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDS).** Mkakati huu umezingatia mabadiliko katika mazingira ya kiuchumi na sera yalivyo sasa. ASDS imeweka mwelekeo mpya wa maendeleo ya sekta, imejumuisha malengo ya Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Kilimo Afrika (CAADP) na imeakisi maono na kanuni nyingi zilizotajwa katika Mpango wa Tanzania wa Uwekezaji katika Kilimo na Usalama wa Chakula (TAFSIP). Aidha, inasisitiza haja ya kuendelea kuwa na utekelezaji mpana katika sekta wa kupanga, kuratibu na kuunganisha rasilimali (sekta ya umma na sekta binafsi) zinazohitajika

14 *Serikali ya Tanzania. 1999a. Dira ya Taifa 2025. Dar es Salaam.*

15 *Serikali ya Tanzania. 2010b. Mkakati wa Taifa wa Kukuza na Kupunguza umaskini II (NSGRP II) Dar es Salaam, Wizara ya Fedha na Uchumi*

ili kuharakisha utekelezaji wa mipango iliyopo na kuingiza mipango mipya inayohusu vipaumbele vya maendeleo ya kitaifa, kikanda na kisekta. Kwa kiasi kikubwa na kwa kuendana na TAFSIP, ASDS inafafanua mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa sekta na kutambua maeneo ya kimkakati ya uwekezaji wa sekta ya umma na sekta binafsi ili kufikia malengo na matokeo yanayotarajiwa. ASDS pia inaelezea kwa kina sera, mikakati na maeneo ya kipaumbele kuimarishwa katika kufikia maendeleo ya kilimo na vijijini, na kuchangia malengo ya Dira ya Taifa 2025, pamoja na ukuaji wa uchumi na malengo ya kupunguza umaskini katika mikakati ya MKUKUTA. Vipengele muhimu vilivyotambuliwa na ASDS ni pamoja na: (i) umuhumu wa sayansi na teknolojia (utafiti, ugani, matumizi ya mbolea kwa wakulima wadogo); (ii) vipaumbele vingine kama vile umwagiliaji, fedha, uendeshaji wa kibiashara, uendelezaji wa kilimo na upatikanaji wa masoko; na pia (iii) kuunganisha mipango mingine ya kisekta kama vile Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT).

14. **Kilimo Kwanza (KK)**. Mdororo wa kiuchumi wa dunia na kupanda kwa bei za vyakula katika mwaka 2008/2009 uliamsha upya ari ya viongozi katika sekta ya kilimo chini za Umoja wa Afrika na jumuiya ya kimataifa. Serikali imefanikisha mipango ya kushirikisha sekta binafsi na kuimarisha kilimo katika shughuli zote za sekta, kusisitiza umuhimu wa Kilimo Kwanza, ambayo ina maana ya (kilimo kipewe kipaumbele). Kimataifa, nchi imepokea msaada wa kundi la G8 ili kuhamasisha mitaji na tekinolojia kutoka sekta binafsi za nje kwa ajili ya kuinua sekta ya kilimo. Mipango mingi iliandaliwa ili kuongeza upatikanaji wa teknolojia (kama vile, mbegu bora na mbolea), kuendeleza masoko na kuongeza mauzo nje ya nchi. Serikali, washirika wa maendeleo na sekta binafsi walikubali kufuata mfumo wa kongani ili kuongeza rasilimali watu na fedha ili kufikia malengo na kupata matokeo katika muda mfupi iwezekanavyo. SAGCOT ni miongoni mwa mipango ya kwanza chini ya mfumo huu ambapo ushirikiano kati ya Serikali, wakulima wadogo na wakulima wakubwa wa kibiashara/ wasindikaji unasisitizwa. Maendeleo haya yameongeza msaada wa ziada kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ili iratibiwe kupitia mfumo wa ASDP.

15. **Mpango wa Tanzania wa Uwekezaji katika Kilimo na Usalama wa Chakula (TAFSIP).** TAFSIP ni matokeo ya maridhiano ya nchi za Afika katika kuendeleza kilimo kupitia CAADP[16] ili kuchangia katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025. Ni mpango wa miaka 10 wa maendeleo ya kilimo ambao umebainisha maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji katika sekta ya umma na binafsi katika kuendeleza sekta ya kilimo, maendeleo vijijini, usalama wa chakula na lishe. Ni mfumo unaoweka vipaumbele, mipango, uratibu, uwajibikaji, na uwekezaji ambao utaongoza mwelekeo wa maendeleo ya sekta ya kilimo nchini katika miaka kumi ijayo. Ili kufikia malengo ya CAADP, mpango wa uwekezaji una maeneo makuu saba ambayo kila moja lina lengo lake la kimkakati na programu za uwekezaji mkubwa. Maeneno hayo ni (i) Kuendeleza Kilimo cha umwagiliaji, Usimamizi endelevu wa matumizi ya Maji na Ardhi; (ii) Tija ya kilimo na maendeleo ya kibiashara vijijini; (iii) Kuimarisha Miundombinu ya vijijini, Upatikanaji wa masoko na biashara; (iv) Kuendeleza sekta binafsi; (v) Usalama wa chakula na lishe; (vi) Usimamizi wa Majanga, Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na mbinu za Kuyapunguza na (vii) Kuboresha Sera na Uimarishaji wa Taasisi.

16. Malengo ya CAADP ni pamoja na (i) kufikia wastani wa ukuaji wa sekta wa asilimia 6 kwa mwaka na Serikali kutenga asilimia 10 ya bajeti kwa ajili ya maendeleo ya Sekta ya kilimo (ii) kuwepo na Usalama wa chakula na lishe (iii) kuendeleza na kuimarisha masoko kikanda na kimaeneo (iv) kuwaunganisha wakulima, wafugaji na wavuvi katika mfumo wa masoko (v) kufikia mgawanyo sawa na wenye tija wa rasilimali. Malengo hayo, yamepewa msukumo zaidi katika Tamko la Malabo (2014) ambalo linazitaka nchi za Afrika: (i) kutenga angalau asilimia 10 ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya kilimo na kuhakikisha ufanisi wake katika matumizi; (ii) kufanya mageuzi katika kilimo na kuhakikisha ukuaji jumuishi kwa kuongeza maradufu tija ya uzalishaji katika kilimo, kuimarisha minyororo ya thamani katika bidhaa za kilimo na kuongeza ufanyaji wa biashara na huduma mara tatu zaidi miongoni mwa nchi za Afrika; na (iii) kuimarisha na kujenga uwezo kwa ajili ya kuleta mageuzi kupitia mipango, sera na taasisi, uongozi, uratibu, ushirikiano, taarifa na takwimu. Nchi za Afrika kupitia CAADP, zimekubaliana kwa kauli moja kutoa msaada wa kiufundi na kifedha kwa ajili ya mageuzi ya sekta ya kilimo na kuendeleza sekta binafsi ya kilimo, pamoja na kushughulikia masuala ya biashara. CAADP inatilia mkazo katika:

16 *Mpango wa ushirikiano wa Maendeleo wa Umoja wa Afrika (NEPAD), Azimio la Mkutano wa Wakuu wa Afrikala Maputo, Mozambique mwaka 2003.*

(i) kubadilisha mitazamo na fikra ili kuendeleza kilimo cha kibiashara; (ii) kuhamasisha uandaaji wa sera ambazo zinasisitizia uongezaji wa tija katika kilimo; (iii) kupanua wigo wa masoko katika ngazi ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa; na (iv) kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji binafsi ili kusaidia kukuza sekta ya kilimo. Tofauti na Azimio la Maputo, Azimio la Malabo limeweka viashiria vya matokeo ya utekelezaji yatakayofikiwa ili kuwa na ukuaji wa pamoja na uendelevu, kuweka tena ahadi mpya zinazohusu upangaji wa mipango na uwajibikaji ambayo itafanyiwa mapitio mara mbili kwa mwaka yanayohusisha ufuatiliaji na utoaji wa taarifa ya maendeleo ya utekelezaji.

# II. PROGRAMU, MIRADI NA MATUMIZI

## A. Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza (ASDP 1)

17. **Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza (ASDP I)** ni mojawapo ya njia muhimu ambayo serikali imetumia katika kufikia malengo ya Dira ya maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 na kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDS). Programu ilikuwa na malengo yafuatayo: (i) kuwezesha wakulima kupata na kutumia utaalamu wa kilimo, teknolojia, mfumo wa masoko na miundombinu ambayo yatachangia katika kuongezeka kwa tija, faida na mapato yatokanayo na kilimo; na (ii) kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi kwa kuboresha mazingira ya sera. Malengo haya yatafikiwa kwa: (i) kuboresha uwezo wa wakulima, ikiwa ni pamoja na makundi yasiyo na uhakika wa chakula na yenye mahitaji maalumu, kwa kuainisha mahitaji ya huduma za kilimo na kujenga ushirikiano na watoa huduma; (ii) kuboresha na kuimarisha uwezo wa sekta ya umma na binafsi wa kutoa huduma za kilimo ili kukidhi matakwa na kutoa ushauri sahihi, huduma na teknolojia; (iii) kuongeza ubora na kiwango cha uwekezaji wa umma katika miundombinu kwa kupanga mipango kiuweledi na kufanya tathmini ya kutosha; na (iv) kuimarisha taasisi za masoko, pamoja na sera na mifumo ya udhibiti na uwezo wa uratibu katika ngazi ya Taifa. Matokeo haya yatapatikana kwa kupitia ngazi za Serikali za Mitaa na Taifa, kama inavyoelezwa katika aya zinazofuata.

18. ASDP I ilizinduliwa mwaka 2006 ili kuwezesha uwekezaji mpana katika sekta na kuchangia malengo ya kupunguza umasikini vijijini kutoka asilimia 27 hadi asilimia 14 ifikapo mwaka 2010, na kuongeza ukuaji wa kilimo hadi asilimia 10 kwa mwaka ifikapo mwaka 2010. ASDP ilitekelezwa katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo kiasi cha asilimia 75 ya fedha za maendeleo za Mfuko wa Pamoja zilipangwa kusaidia utekelezaji wa shughuli katika mamlaka hizo kupitia utaratibu wa kutoa ruzuku kulingana na utendaji. Fedha kupitia Mfuko wa Pamoja zilionesha ufanisi katika matumizi ya misaada ya kifedha ikilinganishwa na fedha kupitia kwenye miradi ya moja kwa moja. ASDP pia ililenga katika kutoa huduma kwa upana zaidi na kuboresha mazingira ya udhibiti na usimamizi imara wa rasilimali kwa walengwa. ASDP iliandaliwa na kutekelezwa kwa miaka 15 ambapo awamu ya kwanza ya miaka 7 ilitekelezwa mwaka 2006/2007 hadi 2012/2013.

19. Licha ya kuwepo kwa ucheleweshaji wa kuchangia fedha kupitia Mfuko wa Pamoja mwanzoni mwa Programu, utekelezaji wa ASDP uliendelea kuimarika na kufanikiwa kuanzisha dhana ya uwekezaji mpana wa kisekta katika kilimo. Dhana ya utekelezaji wa ASDP kwa sasa inaeleweka kutoka ngazi ya Taifa hadi kijiji. ASDP 1 imewezesha kuundwa kwa mfumo wa uendeshaji ambao umehuisha na kuimarisha uandaaji wa mipango, usimamizi wa fedha, mifumo ya ufuatiliaji na utoaji taarifa, ambayo yote imeonesha kuwa bora. imewezesha kujenga uwezo wa rasilimali watu na vifaa, hasa katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA); uwezo ambao utasaidia utekelezaji wa shughuli za ASDP II, na kuweka mazingira ambayo mipango mipya itaweza kutumia na kuchangia kufikia malengo ya sekta.

20. ASDP-1 pia ilikabiliwa na changamoto katika utekelezaji. Kwa upande wa bajeti, kulikuwa na mtawanyo wa rasilimali fedha kutekeleza miradi midogo midogo ambayo ilikuwa ni vigumu kutathmini mafanikio yake na kuandaa taarifa za utekelezaji. Aidha, kulikuwa na changamoto zinazohusiana na uwezo mdogo wa kiufundi hasa kwenye Halmashauri katika kupanga, kuweka vipaumbele na kutekeleza. Kuwepo kwa bakaa ya fedha mwaka hadi mwaka (mfano asilimia 30 zilizotolewa kwa ajili ya umwagiliaji) imethibitisha kuwa uwezo wa kupanga, kusimamia na kupata matokeo ulikuwa ni changamoto. Makubaliano ya Washirika wa Maendeleo kama ilivyotarajiwa wakati wa kuanza utekelezaji wa ASDP yalififia na kusababisha kuanzishwa kwa miradi ambayo fedha zake hazikuwekwa kwenye Mfuko wa

Pamoja. Kwa kuzingatia Azimio la Paris na Ajenda ya Accra kuhusu makubaliano ya kutoa misaada ya maendeleo kwa ufanisi, sekta ya kilimo ilikabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa usimamizi imara. Changamoto nyingine ni pamoja na ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika shughuli za Programu, usaidizi mdogo kwa vikundi vya wakulima hususan katika masoko na usindikaji, miradi ya umwagiliaji isiyokamilika na hivyo kupunguza manufaa endelevu yaliyokusudiwa.

21. **Mradi wa Uwekezaji wa Sekta ya Kilimo katika Wilaya-DASIP.** Ulitekelezwa kuanzia mwaka 2006 hadi 2013 sambamba na ASDP-1 katika wilaya 28 za mikoa ya Kagera, Kigoma, Mwanza, Mara na Shinyanga kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 83 ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na ulipangwa kunufaisha watu 570,000. Mradi ulilenga kuongeza tija na mapato ya kaya za vijijini kwa: (i) kuwajengea uwezo wakulima; (ii) kupanga mipango ya jamii ya uwekezaji katika sekta ya kilimo, hasa miundombinu na (ii) huduma za kifedha vijijini na masoko.

## B. Miradi mbalimbali katika Sekta ya Kilimo

22. Mbali na ASDP-1, miradi mikubwa iliyoendelea katika sekta ya kilimo, ni pamoja na: *AFSP* (Mradi wa Kuongeza Usalama wa Chakula) wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 245, uliotekelezwa mwaka 2009-2013 na Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia. Lengo lilikuwa ni kuchangia uzalishaji na tija kwa mazao ya chakula katika maeneo yaliyolengwa kwa kuboresha upatikanaji wa pembejeo muhimu za kilimo cha mahindi na mpunga (idadi ya wanufaika ni kaya milioni 1.75). Mradi wa AFSP ulikuwa na sehemu kuu tatu: (i) Kuboresha upatikanaji wa mbegu bora na mbolea za mahindi na mpunga, kwa kuimarisha Mfumo wa Taifa wa Vocha za Pembejeo za Kilimo (NAIVS); (ii) Kuimarisha mifumo ya usambazaji wa pembejeo za kilimo, kwa kuimarisha mitandao ya mawakala wa pembejeo na mfumo wa mbegu wa kitaifa; na (iii) Usimamizi wa mradi na ufuatiliaji natathmini. Aidha, AFSP ilitoa fedha kugharamia: (i) ASDP-1 (Dola za Marekani milioni 30), zilizolenga uhamasishaji wa uzalishaji katika kilimo endelevu, ikiwa ni pamoja na miradi ya umwagiliaji na usimamizi wa rasilimali maji, usimamizi jumuishi wa rutuba ya udongo kwa kuimarisha utafiti na uwezo wa ushauri wa usimamizi wa virutubisho vya udongo na kilimo hifadhi; na (ii) Kwa Awamu ya Pili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (AF-TASAF-2, Dola za Marekani milioni 30), ili kuimarisha usalama wa chakula vijijini kwa watu wasio na uhakika wa chakula na watu wenye mahitaji maalum.

23. **MIVARF:** Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Masoko, Uongezaji wa Thamani na Huduma za Kifedha Vijijini unaogharamiwa kwa pamoja na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa jumla ya Dola za Marekani milioni 170 Chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu Progamu inatekelezwa katika mikoa 26 ya Tanzania (21 Bara na 5 Zanzibar) katika jumla ya wilaya 141. Programu hiyo inatarajiwa kunufaisha moja kwa moja karibu kaya 500,000 za vijijini. Lengo la MIVARF ni kuimarisha kipato na usalama wa chakula kwa walengwa kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma za kifedha na masoko. Programu inalenga katika kuimarisha miundombinu na mifumo ya masoko, na sekta ya fedha vijijini. Kipekee programu inalenga: (i) kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha na teknolojia vijijini kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji, huduma na rasilimali; na (ii) kuongeza upatikanaji endelevu wa masoko ya pembejeo na mazao pamoja na fursa za biashara vijijini.

24. **MUVI:** Programu ya Kusaidia Biashara Ndogo na za Kati Vijijini ilitekelezwa kwa Jumla ya Dola za Kimarekani milioni 25, unatekelezwa kupitia Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji ili kusaidia kuongeza fursa za ajira katika mikoa 6 ya Iringa, Manyara, Mwanza, Pwani, Ruvuma na Tanga. Programu hiyo inasaidia wajasiriamali vijijini kupata ujuzi, maarifa na upatikanaji wa masoko ili kuongeza uzalishaji, faida na mapato yatokanayo na shughuli zisizokuwa za kilimo. Programu hiyo ina malengo matatu: (i) kuboresha uelewa wa wajasiriamali vijijini kuhusu fursa za masoko na namna fursa hizo zinavyoweza kutumika katika kuendeleza na kutekeleza mkakati wa mawasiliano na mafunzo ya ujasiriamali kuboresha biashara zao; (ii) kuboresha uratibu na ushirikiano wa minyororo ya thamani, kwa kuundwa na kuimarisha uhusiano wa minyororo ya thamani iliyochaguliwa; na (iii) kuimarisha taasisi za sekta za umma na binafsi kutoa msaada wenye ufanisi na tija kwa wajasiriamali walioko vijijini.

25. **SAGCOT:** (Huu ni Mpango maalum wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania): Lengo la mpango huu ni kupanua uwekezaji wa kilimo cha kibiashara utakaoleta ukuaji wa kipato kwa wakulima wadogo na kuzalisha ajira katika minyororo ya thamani katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania. Jukumu lake ni kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi na ushirikiano kwa kuchochea kiasi kikubwa cha uwekezaji wa sekta binafsi inayowajibika, inayolenga kukuza kilimo kwa kasi na kwa uendelevu, ili kuwa na manufaa makubwa katika usalama wa chakula, kupunguza umaskini na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. SAGCOT inahamasisha 'kongani' ya kilimo chenye faida na huduma za biashara ambazo zinawanufaisha wakulima wadogo na jamii kwa ujumla. SAGCOT inalenga katika uongezaji wa thamani, kuendeleza miundombinu, kuongeza tija na uzalishaji katika kilimo na mashirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi kulingana na mikakati na vipaumbele vya ASDS na KK.[17]

26. **Azma ya Matokeo makubwa sasa** (*Big Results Now)* Kutokana na kasi ndogo ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 Serikali ilianzisha azimio hili linalojulikana kama "Matokeo Makubwa Sasa". Mpango huu ulianza kwa kushirikisha sekta sita, ambazo ni Kilimo, Elimu, Ukusanyaji mapato, Nishati, Usafirishaji na Maji. Timu ya Watalaam ambayo ilikuwa katika maabara iliandaa mipango[18] ya utekelezaji ya vipaumbele kwa miaka miwili ijayo. Lengo la BRN katika Kilimo ni kushughulikia vikwazo na changamoto ili kuongeza kasi ya kukua kwa pato la Taifa litokanalo na kilimo, kuboresha mapato ya wakulima wadogo na kuhakikisha usalama wa chakula ifikapo mwaka 2015. Lengo lingetimia kwa kutumia mfumo wa kuunganisha wakulima wadogo kupitia mazao ya nafaka na mazao yenye uwezo mkubwa wa kuchangia katika kupunguza uagizaji wa chakula kutoka nje, kuongeza kipato cha wakulima na usalama wa chakula. Maeneo makuu matatu ya kipaumbele ni: (i) kujenga mfumo wa wakulima wadogo kuuza mahindi kwa pamoja kupitia maghala 275 katika wilaya 8; (ii) kukarabati na kuendesha skimu 78 za umwagiliaji mpunga kitaalamu na kibiashara katika wilaya 10; (iii) kuanzisha mashamba makubwa 25 ya kilimo cha kibiashara cha miwa na mpunga katika eneo la SAGCOT. Lengo katika mipango hiyo mitatu ilikua ni kuwa na ongezeko la sukari[19] tani 150,000, mchele tani 290,000 na mahindi tani 100,000 ifikapo juni 2016. BRN imetoa msukumo mpya na utashi wa kisiasa, uongozi na uratibu baina ya wizara mbalimbali, Ugharamiaji wa shughuli zilizopendekezwa na jinsi ya utekelezaji, uliratibiwa na Ofisi ya Rais chini ya kitengo maalum cha *Presidential Delivery Bureau (PDB*) na Idara ya Kilimo (*Agricultural Delivery Division -ADD*)

27. Ili kuhakikisha ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ya kilimo kupitia BRN unaimarika, Serikali ilianza kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na uwekezaji. Miongoni mwa maeneo yaliyoshughulikiwa ni mazingira ya uwekezaji hasa kwa makampuni ndogo na za kati ambazo ni muhimu kuweza kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025. Pia mwanzoni mwaka 2014 ilifanyika Maabara ya Mazingira ya Biashara iliyohusisha, maeneo sita (6) muhimu ambayo ni: (i) upatikanaji wa ardhi na uhakika wa umiliki; (ii) usimamizi wa mikataba, sheria na kanuni; (iii) kupambana na rushwa; (iv) sheria za kazi na ujuzi; (v) kuoanisha kanuni na taasisi; na (vi) kodi, wingi wa tozo, ada na ushuru.

28. EAAPP. (Mpango wa Tija ya Kilimo Afrika Mashariki) : Mpango ulilenga kusaidia vituo vya umahiri vya kikanda (RCoE) kuchangia kwenye kuongeza tija na ukuaji katika kilimo kwa kuimarisha na kukuza ushirikiano wa kikanda katika kuendeleza teknolojia, mafunzo na kusambaza programu nne za mazao ya kipaumbele (ngano-Ethiopia; mpunga-Tanzania; muhogo-Uganda; na maziwa-Kenya). EAAPP imedhamiria kuongeza utaalamu wa kikanda katika utafiti wa kilimo kwa ajili ya maendeleo (AR4D) na kuwezesha kuhawilisha teknolojia za kilimo, habari na ujuzi ndani na katika mipaka ya kitaifa. Sehemu kuu za programu ni: (i) kuimarisha uwezo wa taasisi za RCoE; (ii) kuzalisha teknolojia na kuzisambaza kwa wingi, kutoa mafunzo, kulenga vipaumbele vya kikanda na kutumia mikakati shirikishi; (iii) kuboresha upatikanaji wa mbegu bora ikiwa ni pamoja na kuimarisha mazingira mazuri ya kubadilishana mbegu na biashara kikanda; na (iv) uratibu wa mpango na usimamizi katika viwango

*17 ASDP na SAGCOT ziko nyanda za juu kusini na kongani na zinalenga wakulima wadogo, kuendeleza kilimo cha biashara kwa kuunganisha wakulima na wajasiriamali ili kuimarisha ushindani wa soko la ndani na kimataifa. ASDP II itajenga uwezo wa wakulima wadogo ili waendelee kuongeza faida kutokana na msaada toka SAGCOT, kama vile kilimo cha mkataba na kuendeleza wakulima nje ya skimu na huduma ya mfuko wa ruzuku ya kuchochea uwekezaji wa SAGCOT*

*18 Hii na zaidi ya mpango halisi kama ilivyoelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya kilimo.*

*19 Kwa mkopo wa IFAD (Dola milioni 40) pamoja na AfDB (Dola milioni 30)*

vya kitaifa na kikanda. Kwa shughuli za uratibu za kikanda, kila nchi inayohusika inachangia asilimia 2.7 ya gharama za mpango kwa ASARECA[20], kwa ajili ya uratibu wa shughuli za kikanda.

29. **FTF** (*Feed the Future*): Serikali ya Marekani kupitia shirika la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) imetoa Dola milioni 70 kwa ajili ya kugharamia mpango wa FTF Tanzania. Asilimia 80 ya fedha hizo zimewekezwa kwenye eneo la SAGCOT na zilizobaki zinalenga mikoa ya Manyara na Dodoma na Zanzibar. Mkakati wa FTF unaendana na TAFSIP, na ni sehemu ya mpango mkakati wa USAID katika kufikia ukuaji wa uchumi endelevu kupitia kilimo na kuboresha hali ya lishe kwa Watanzania wote. Uwekezaji unadhamiria kuboresha fursa za kiuchumi na mapato kupitia uwekezaji unaongozwa na sekta binafsi kwa ubia pamoja na wanawake na vijana. Matokeo tarajiwa ni kuongeza tija katika uzalishaji (mahindi na mpunga), kupata masoko kwa wazalishaji wa mboga na matunda na kuongezeka kwa idadi ya watoto wanaopata chakula chenye lishe bora. Mpango unalenga kufikia wakulima wadogo 100,000 (ambao ni karibu asilimia 2 ya wakulima wote wadogo). Aidha, FTF inasaidia serikali ya Tanzania: (i) Kufanya maamuzi ya sera kutokana na utafiti na takwimu, ikiwa ni pamoja na kuthibitisha matokeo ya kufuta marufuku ya kuuza mahindi nje, kuchunguza fidia ya ardhi na mipango ya kukodisha na kutekeleza mfumo wa usajili wa dhamana; na (ii) Kujenga uwezo wa rasilimali watu na kuimarisha uwezo wa utafiti shirikishi katika vyuo vikuu na taasisi za kitaifa. FTF pia inahamasisha na kuimarisha uvumbuzi wa ndani, ikiwa ni pamoja na kuongeza virutubisho muhimu vya chakula, kuboresha upatikanaji wa vyakula vya lishe na kuongeza wigo wa virutubisho vya aina mbalimbali kwenye mnyororo wa thamani.

30 **Ugharamiaji wa ASDP-1:** Katika miaka 10 iliyopita, ASDS imetekelezwa kupita ASDP kwa ufadhili wa serikali (kuu na serikali za mitaa), Benki ya Dunia, AfDB, IFAD, Serikali ya Japan na Ireland, na Umoja wa Ulaya. ASDS na ASDP imesisitiza njia ya sekta nzima na mfuko wa pamoja kama aina iliyopendekezwa ya mchango kutoka kwa washirika wa maendeleo ili kukuza usawa wa hatua za sekta, kinyume na kuenea kwa miradi ya jadi. Kiujumla, inaonekana kuwa katika kipindi cha utekelezaji wa ASDP-1, mchango wa washirika wa maendeleo kwenye sekta ya kilimo taratibu uliongezeka kuelekea ugharamiaji unaolenga kurejea miradi ya "asili" kwa miradi/programu zilizotekelezwa kwa bajeti mbalmbali za sekta lakini pia kuongezeka kwa misaada iliyo nje ya bajeti. Ingawa si mara zote kutambuliwa, miradi kadhaa iliyosimama peke yake ilijengwa juu ya mifumo iliyoendelezwa na kuimarishwa na ASDP-1, hasa ngazi ya Mamlaka za Halmashauri (LGA) kuhamasishwa kwa pande zote kunapendekezwa lakini kutopatiwa fedha za kutosha za uwezo wa msingi (Huduma za Ugani na Ruzuku ya Kujenga Uwezo) imeshusha kiwango ambacho kingefikiwa. Washirika wa Maendeleo pia walitoa ahadi za kusadia uwekezaji katika mpango wa BRN au mipango maalumu, yenye kuelekeza uwekezaji katika eneo la SAGCOT. ASDP II ipo wazi kufadhiliwa kupitia mifumo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Pamoja.

## C. Mapitio Katika Sekta ya Kilimo na Matumizi ya fedha za Umma (ASR-PER)

31. Kuna tofauti kati ya vyanzo vya taarifa zinazohusiana na uwekezaji wa sekta ya umma katika kilimo. Kwa mfano, Sekretariati ya ASDP hutumia bajeti na matumizi yaliyofanywa na wizara za sekta (ASLMs). Mfumo huu unaacha uwekezaji uliyofanywa na idara na taasisi zinazojishughulisha kilimo hivyo kuwa na taarifa zinazoonesha kiwango kidogo cha uwekezaji wa umma. Kwa upande mwingine Wizara ya Fedha ina tafsiri pana ya sekta ya kilimo kuliko inayotolewa katika ASDP. Chanzo cha uhakika kuhusu matumizi ya umma katika kilimo ni mfululizo wa taarifa za mapitio za kila mwaka za matumizi ya fedha za umma ya kilimo tangu mwaka 2006, ikiwa ni pamoja na taarifa ya mapitio ya hivi karibuni ya Matumizi ya Sekta ya Kilimo (ASR-PER) mwaka 2014 iliyotoka Machi 2015[21]. Malengo makuu ya ASR-PER ni: (i) Kutoa uchambuzi wa kina kuhusu masuala ya sera zinazohusu sekta, na (ii) kuweka takwimu muhimu na viashiria vya maendeleo ya sekta, mipango ya Serikali na matumizi ya fedha za umma.

---

*20 ASARECA ni taasisi inayolenga kuimarisha mpango wa pamoja wa kuendeleza utafiti, ugani, mafunzo na elimu ili kuleta ukuaji wa kiuchumi, kukabiliana na umaskini, kutokomeza njaa na kuimarisha matumizi endelevu ya rasilimali kwa nchi 11 zinazoshiriki. ASARECA inalenga kuendeleza maarifa ya kisayansi, sera na teknolojia kama chombo cha kutimiza malengo ya NEPAD, CAADP na MDGs.*

*21 Mapitio ya sekta na matumizi ya fedha za umma 2014, MAFC, Machi 2015.*

32. ASR-PER inakusanya takwimu za matumizi ya umma kwa kutumia uainishaji wa kawaida wa Serikali ambao unajumuisha mazao, mifugo, uvuvi na uzalishaji wa misitu. Takwimu zinajumuisha fedha kutoka vyanzo vya bajeti za ndani pamoja na michango ya wafadhili (misaada kwa serikali) na mikopo rasmi. Matumizi kwenye miradi ya umwagiliaji pia yanajumuishwa, japokuwa misaada kwa ajili ya usindikaji na masoko ya bidhaa za kilimo haikujumuishwa. Takwimu zinazokusanywa katika mapitio ya mwaka ya ASR-PER zinatumika kufuatilia matumizi halisi ikilinganishwa na kiwango kilichopangwa katika Azimio la Maputo la 2003 na kusisitizwa katika Azimio la Malabo la 2014 ambapo Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika waliahidi kutenga asilimia 10 ya matumizi yote ya umma kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo. Dhamira hii kimsingi inalenga kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo kufikia lengo la asilimia 6 kwa mwaka ili kupunguza umaskini na kuongeza usalama wa chakula.

33. Matumizi ya umma katika kilimo yanaonekana katika bajeti kuu ya Serikali hasa kama matumizi ya kawaida na maendeleo ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika (MAFC) na Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi (MLFD). Vilevile, huduma kwa wakulima zinatolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na zinafadhiliwa kwa njia ya ruzuku kutoka bajeti kuu. Sekta ya kilimo pia inapata msaada wa maendeleo, Hata hivyo ni sehemu tu ya bajeti inaonekana katika makadirio ya bajeti na taarifa za kifedha.

34. **Matumizi ya kawaida kupitia** Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Mipango ya maendeleo ya kilimo katika wilaya yameongezeka katika miaka ya hivi karibuni. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa inatokana na kuongezeka kwa ruzuku ya pembejeo (2009–2012) na ruzuku inayopatiwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Matumizi ya NFRA, ruzuku ya pembejeo na fedha zinazopelekwa kwenye taasisi za serikali katika sekta ya Kilimo zinazojisimamia zenyewe ni kama inavyonekana katika **Kielelezo Na.8.**

35. Katika mwaka 2013/14, jumla ya matumizi ya kawaida kupitia Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi yalikadiriwa kuwa Shilingi bilioni 306.6 pamoja na matumizi maalum (ambayo ni ruzuku kwa NFRA, ruzuku ya pembejeo na fedha zilizopelekwa kwenye taasisi nyingine za wizara) hivyo kuchukua shilingi bilioni 238.1 sawa na asilimia 78 ya bajeti yote ya Wizara ya Kilimo. Kwa upande mwingine, matumizi ya kawaida (gharama za watumishi na uendeshaji) zilifikia Shilingi bilioni 68.5 billioni (asilimia 22 ya bajeti yote ya Wizara ya Kilimo). Pamoja na kwamba ruzuku ya NFRA na ruzuku ya pembejeo imeongezeka kuanzia mwaka 2011/12, matumizi ya watumishi na gharama za uendeshaji kwa ujumla wake hazijabadilika. Kiuhalisia, matumizi ya kawaida katika ngazi ya wizara yamepungua (**Jedwali Na.1**).

**Kielelezo Na. 8. Matumizi ya kwaida kwa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na uvuvi-ngazi ya Taifa**




Chanzo: ASR-PER, Machi 2015 (kwa kuzingatia makadirio ya bajeti ya miaka mbalimbali).

**Jedwali Na. 1:Matumizi ya Kawaida katika Wizara za Kilimo na Mifugo/Uvuvi (TSh.milioni)**

| | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Halisi | Halisi | Halisi | Halisi | Kadirio | Kadirio |
| **Matumizi ya Kawaida** | | | | | | |
| **Gharama za Watumishi** | | | | | | |
| Wizara ya Kilimo | 16,953 | 18,490 | 21,659 | 25,167 | 26,328 | 27,169 |
| Wizara ya Mifugo na Uvuvi | 11,467 | 15,669 | 17,238 | 16,721 | 18,429 | 18,429 |
| **Malipo ya Uendeshaji** | | | | | | |
| Wizara ya Kilimo | 11,673 | 9,781 | 7,174 | 16,368 | 14,516 | 14,916 |
| Wizara ya Mifugo na Uvuvi | 15,373 | 12,501 | 10,371 | 8,836 | 9,207 | 7,533 |
| **Jumla ya matumizi ya kawaida** | **55,465** | **56,441** | **56,442** | **67,091** | **68,479** | **68,047** |
| **Matumizi maalum[22]** | | | | | | |
| Ruzuku za pembejeo-Kilimo | 54,963 | 56,902 | 39,893 | 47,858 | 97,014 | 96,900 |
| Ruzuku za pembejeo-Mifugo | 332 | 149 | 26 | 127 | 106 | 37 |
| Matumizi-NFRA | 54,657 | 74,383 | 28,134 | 42,423 | 110,400 | 111,254 |
| Mengineyo | 50,761 | 22,436 | 24,269 | 32,432 | 30,596 | 35,401 |
| **Jumla ya Matumizi maalum** | **160,714** | **153,870** | **92,323** | **122,839** | **238,115** | **243,592** |
| **Jumla ya matumizi ya Wizara za Kilimo na Mifugo/Uvuvi** | **216,179** | **210,311** | **148,765** | **189,930** | **306,594** | **311,639** |

Chanzo: ASR-PER, Machi 2015 (kwa kuzingatia makadirio ya bajeti ya miaka mbalimbali).

36. Kwa upande wa matumizi ya Serikali za Mitaa, **Jedwali Na. 2** linaonesha kiasi cha matumizi ya wilaya ni zaidi ya asilimia 60 ya matumizi yote. Hata hivyo, ikilinganishwa na pato litokanalo na sekta ya kilimo, matumizi ya kila siku matumizi ya kawaida katika ngazi ya Taifa pamoja na ngazi ya wilaya na matumizi ya maendeleo ni sawa na asilimia 1.2 hadi 1.7 ya pato la kilimo. Zaidi ya hayo, mchango wa kilimo kwenye pato la Taifa umeendelea kupungua wakati matumizi yanaongezeka. Aidha, Huduma za kitaalamu na ugani zinachangia kwa sehemu kubwa kwenye matumizi ya wilaya.

**Jedwali Na. 2: Matumizi ya Kawaida kwenye kilimo na uwiano wa mchango wa Kilimo kwenye Pato la Taifa**

| | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Halisi | Halisi | Halisi | Halisi | Kadirio | Kadirio |
| Matumizi ya Kawaida-Wizarani | 55,465 | 56,441 | 56,442 | 67,091 | 68,479 | 68,047 |
| Matumizi ya kawaida-Wilayani | | 37,098 | 48,365 | 58,652 | | |
| Maendeleo ya wilaya | | 69,631 | 56,227 | 34,909 | | |
| **Jumla (TSh milioni)** | | **163,170** | **161,034** | **160,652** | | |
| Pato la Taifa la kilimo (TSh bilioni) | | 9,429 | 11,675 | 13,780 | | |
| Matumizi ya kawaida ya mara kwa mara kama asilimia ya Pato la Taifa la kilimo | | 1.7% | 1.4% | 1.2% | | |

Chanzo: ASR-PER, 2015 (Makadirio ya bajeti kwa serikali kuu na TAMISEMI-Matumizi ya wilaya).

37. Kuongezeka kwa bajeti kwa ajili ya shughuli za kiteknolojia ni muhimu sana na ni muhimu ikazingatiwa

22 *'Matumizi maalumu' ni pamoja na ununuzi katika hifadhi ya Taifa ya chakula ( NFRA), Ruzuku ya pembejeo na ruzuku kwa taasisi zingine za Serikali za ndani na kimataifa*

na Wizara zote ikiwa ni pamoja na Wizara ya Kilimo. Pia ni muhimu kuzingatia bajeti na matumizi ya shughuli za utafiti, uzalishaji mimea, zana za kilimo na huduma za umwagiliaji ambapo kwa sasa ni kati ya asilimia 40 na 50 ukiondoa ruzuku inayokwenda Hifadhi ya Taifa ya Chakula na ruzuku za pembejeo. Hata hivyo, matumizi ya kuongezeka kwa teknolojia kwenye kilimo yanakadiriwa kuwa asilimia 0.3 tu ya matumizi yote, kiwango ambacho ni cha chini sana.

**Jedwali Na. 3: Matumizi kwa ajili ya Teknolojia katika Wizara ya Kilimo (TSh milioni )**

| | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | halisi | halisi | halisi | Halisi | Iliyokubaliwa | iliyokubaliwa |
| Wafanyakazi-Kilimo | 16,953 | 18,490 | 21,659 | 25,167 | 26,328 | 27,169 |
| Malipo ya uendeshaji bila ruzuku za pembejeo-Kilimo | 11,673 | 9,781 | 7,174 | 16,368 | 14,516 | 14,916 |
| Wizara ya Kilimo-Uhamisho bila NFRA | 45,606 | 19,033 | 19,454 | 17,388 | 19,988 | 28,332 |
| Jumla ya fedha bila yaruzuku za kilimo na NFRA-Kilimo | 74,231 | 47,303 | 48,288 | 58,922 | 60,831 | 70,417 |
| Matumizi kwenye teknolojia za kilimo | 17,076 | 18,263 | 22,400 | 28,641 | 29,073 | 27,953 |
| Asilimia kwenye Teknolojia bila ruzuku za kilimo na NFRA | 23.0% | 38.6% | 46.4% | 48.6% | 47.8% | 39.7% |

Chanzo: ASR-PER, March 2015 (kwa msingi wa makadirio ya bajeti kwa miaka mingi).

38. Hakuna tathmini ya kutosha ya makadirio ya matumizi ya shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi yakilinganishwa na uwiano wa jumla wa matumizi yote ya Serikali isipokuwa takwimu kuhusiana na matumizi ya kawaida iliyofanywa na ASR-PER. Pia, kutokana na ukosefu wa takwimu za kutosha za matumizi ya shughuli za kilimo zinazofanywa na washirika wa maendeleo, haikuwa rahisi kufanya makisio ya uwiano na kutoa takwimu halisi. Hata hivyo, matokeo ya uchambuzi yaliyofanywa na ASR-PER yanaonesha kwamba matumizi ya kawaida ya shughuli za kilimo ni takribani asilimia 2 ya bajeti ya Serikali. Kama matumizi ya Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) na ruzuku ya pembejeo yatajumuishwa, matumizi ya kawaida ya shughuli za kilimo yanakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 3 hadi 3.7 (bila ya madeni) kati ya mwaka 2010/2011 na 2013/2014 (Kielelezo Na 9). Kuongezeka kwa bajeti ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2013/2014 ilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) na ruzuku ya pembejeo.

**Kielelezo Na. 9. Matumizi ya kawaida kwenye Sekta ya kilimo kwa kuwianisha na jumla ya matumizi yote ya bajeti ya kawaida**




Chanzo: ASR-PER, March 2015

39. Kwa ujumla bajeti ya Serikali kwa ajili ya shughuli za sekta ya kilimo bado ni ndogo (chini ya kiwango cha asilimia 10 zilizotajwa kwenye Azimio la Maputo la mwaka 2003) hata kama itajumuishwa na fedha zinazohudumia Hifadhi ya Taifa ya Chakula na ruzuku ya pembejeo.Tanzania ni moja ya nchi ambazo zimetia saini makubaliano ya CAADP, hivyo inao wajibu wa kuongeza uwekezaji kwenye sekta ya kilimo ili kufikia lengo la ukuaji wa sekta hiyo wa asilimia 6 kwa mwaka. Kufuatia makubaliano

hayo, nchi ina wajibu wa kutenga angalau asilimia 10 ya bajeti yote ya Serikali kwa mwaka kwa ajili ya maendeleo ya shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi. Ili kufikia malengo hayo ya ongezeko kubwa la uwekezaji katika maendeleo endelevu ya sekta ya kilimo, ASDP II inatarajiwa kutoa mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya sekta ya kilimo.

40. Ukusanyaji wa mapato na utekelezaji wa bajeti. Katika mwaka 2012/2013, mapato halisi yaliyokusanywa yalifikia asilimia 92 ya makadirio, wakati matumizi ya kawaida yalifikia asilimia 95 ya makadirio. Katika mwaka 2013/2014, kiwango cha ukusanyaji wa mapato na matumizi kilikua chini ya utekelezaji wa bajeti kwa kiwango cha asilimia 88 na asilimia 87 kwa mfuatano huo isipokuwa kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2013/2014. Kwa ujumla, kiwango kidogo cha utekelezaji wa bajeti katika Wizara ya Kilimo kilitokana na matumizi ya kawaida ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula na ruzuku ya pembejeo.

**Jedwali Na. 4: Viwango vya ukusanyaji wa mapato na utekelezaji wa bajeti**

| | Jumla | Wizara ya Kilimo | Wizara ya Mifugo na Uvuvi |
|---|---|---|---|
| **2012/13** | | | |
| Mapato | 92% | | |
| Matumizi | 95% | | |
| **Wizara ya Kilimo**<br>Matumizi ya kawaida | | 84% | 80% |
| Matumizi ya Maendeleo: Ndani | | 41% | 48% |
| Nje | | 97% | 80% |
| **2013/14** | | | |
| Mapato ya ndani | 88% | | |
| Matumizi ya kawaida | 87% | | |
| **Wizara ya Kilimo na Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi:** | | | |
| Matumizi ya kawaida | | 71% | 90% |
| Maendeleo | | 82% | 40% |

Chanzo: ASR-PER, March 2015 (ripoti ya robo ya nne kwa bajeti ya 2013 na 2014).

41. **Fedha za Maendeleo.** Kwa upande wa fedha za maendeleo, taarifa ya *ASR-PER* ya Machi 2015 ilibainisha kutokamilika kwa taarifa zinazohusiana na matumizi ya fedha za maendeleo katika sekta ya kilimo. Kuna vyanzo vikuu viwili ambavyo takwimu hizi zinaweza kupatikana: (i) Nyaraka za bajeti ya Serikali (ii) jukwaa la usimamizi wa misaada (*aid management platform*) ambalo washirika wa maendeleo hutoa taarifa husika.

42. Kwa ujumla, kiasi cha misaada ya kimaendeleo katika bajeti ya Serikali bado ni kidogo, na wadau wa maendeleo huchangia zaidi kwa njia ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, hakuna takwimu zinazoonesha matumizi ya fedha za misaada nje ya bajeti (*off-budget*), na pia, takwimu za matumizi ya mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) hazipo. Pamoja na kwamba orodha ya miradi ya kilimo na wafadhili wake imeelezwa katika kitabu cha bajeti, orodha hiyo haina takwimu za kutosha na haijaonyesha matumizi ya kila mwaka. Kulingana na takwimu zilizopo, matumizi ya bajeti ya maendeleo kutoka kwa wafadhili au washirika wa maendeleo ni kiasi cha shilingi bilioni 183 (Kielelezo Na. 10). Fedha hizo zilitumika kwenye ASDP I na pia AFSP. Katika miaka miwili ya 2013/2014 na 2014/2015, matumizi ya bajeti kwa wafadhili katika sekta ya kilimo yalipungua hasa baada ya AFSP kufikia mwisho wa muda wake mwaka 2013/2014. Kwa mfano mwaka 2014/2015 kiasi cha makadirio ya matumizi ya fedha za maendeleo kwa ajili ya sekta ya kilimo ilikuwa ni shilingi za Kitanzania bilioni 97 kwa ajili ya shughuli za maendeleo za sekta ya kilimo. Kwa upande wa matumizi ya fedha za ndani za maendeleo (*local development fund*) za maendeleo katika sekta ya kilimo, Kielelezo Na. 10 kinaonesha kuwa ni shilingi bilioni 16 tu zilitumika katika mwaka 2011/2012, Matumizi hayo yaliongezeka kwa kiasi kikubwa

mwaka 2013/2014 na kufikia shilingi bilioni 72 mwaka 2014/2015. Kiasi kidogo cha matumizi ya fedha za maendeleo za ndani kinatoa picha halisi ya hali ya fedha katika kuhudumia sekta ya kilimo katika ngazi ya Taifa au wizara na pia Serikali za Mitaa.

**Kielelezo Na 10. Matumizi ya bajeti kwenye maendeleo ya miradi ya kilimo Fedha za Ndani na Nje**




Chanzo:ASR-PER, Machi 2015 (Makadirio ya bajeti, 2013/2014 na 2014/2015)

# III. UANDAAJI WA PROGRAMU YA ASDP II NA MISINGI YAKE

## A. Tulichojifunza kutokana na utekelezaji wa ASDP-1

43. Tofauti na sekta nyingine, matokeo ya uwekezaji unaofanywa na serikali katika sekta ya kilimo yanaweza yasionekane moja kwa moja kama ilivyotarajiwa isipokuwa kwa kushirikisha na kuwezesha baadhi ya sekta kama vile sekta binafsi (wakulima na wadau wengine). Uzoefu uliopatikana wakati wa utekelezaji wa ASDP-1 (programu na miradi mingine inayohusiana), uzoefu huo utatumika na kusaidia utekelezaji wa ASDP II[23]; masuala hayo ni: (i) Umuhimu wa ushirikishaji wa wadau mbalimbali katika kupanga, kutekeleza, na kukusanya rasilimali kwa pamoja kwa ajili ya utekelezaji wa ASDP II kwa kutumia mfumo wa SWAp[24]. (ii) Kuwepo na kuimarishwa kwa mipango yenye matokeo kuanzia ngazi ya chini hadi ya kitaifa ikiwa ni pamoja na kupanga, kutekeleza, tathmini na ufuatiliaji ili kufikia kukua kwa uzalishaji endelevu, kupitia matumizi ya teknolojia katika mnyororo wa thamani ambao unaleta ushindani na upatikanaji wa masoko; (iii) Kupanga na kutenga fedha za kutekeleza vipaumbele vyenye kuleta mabadiliko chanya kwenye maeneo yenye matokeo makubwa, pia kuimarisha hatua lengwa

23 *Imenukuliwa toka taarifa ya tathmini ya ASDP-1 (Juni 2012) na tathmini nyingine zilizofanyika za miradi ndani na nje ya bajeti. .*

24 *Tathmini ya IFAD kwa Tanzania ( Dec 2014 Unedited Final Version, p. 71).*

za mnyororo wa thamani, kama vile masoko na kusaidia upatikanaji wa miundombinu ya kuongeza thamani. (iv) Kuwezesha vyama vya wakulima, Wavuvi na Wafugaji kushiriki kwenye masoko na kuongeza thamani; (v) Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji endelevu na kuimarisha mfumo wa usimamizi na mipango imara utakaosaidia maendeleo ya miundombinu imara na usimamizi wa rasilimali maji, usimamizi wa kitaalamu na taasisi ,upatikanaji wa huduma na pembejeo; (vi) Kuratibu na kusimamia mipango na fedha na kushirikiana na sekta binafsi, (vii) Mpango wa tathmini na ufuatiliaji unapaswa kuwa na takwimu zilizofanyiwa utafiti kitaifa na mfumo wa takwimu za kilimo yaani ARDS. Mfumo huo unapaswa kuwezeshwa ili kutoa taarifa sahihi kwa muda sahihi kwa ajili ya kupima mafanikio ya ASDP II (viii) Kuboresha upatikanaji wa mbegu bora na mbolea kwa wakati ili kuongeza kiwango cha uzalishaji na kuimarisha uzalishaji endelevu.

44. Vipengele muhimu vya kuzingatia vilivyotokana na uzoefu wa utekelezaji wa ASDP-1 ni kama ifuatavyo:[25]

a) *Mfumo wa utekelezaji wa pamoja :* Mfumo huu ni muhimu kuendelezwa kwa sababu ya uwepo wa uwajibikaji wa kutosha kwa wadau ikiwemo Serikali, wafadhili na sekta binafsi katika ngazi zote. Mfumo huo pia umeonesha kwamba mafanikio ya utekelezaji wa Programu yanahitaji uongozi bora katika ngazi zote zinazosimamia sekta ya kilimo.

b) *Ugumu wa kupima matokeo kutokana na mgawanyo finyu wa rasilimali katika kila eneo la mradi.*

Wakati ASDP I inazinduliwa, utekelezaji wake ulijumuisha wilaya zote za Tanzania Bara. Hata hivyo, kulitokea changamoto ya upimaji matokeo kutokana na mgawanyo finyu wa rasilimali fedha katika kila eneo la utekelezaji wa mradi bila kuwepo kwa vipaumbele mahsusi. Utekelezaji wa ASDP II unahusisha na kusisitiza vipaumbele.

c) Mafanikio ya ugatuzi wa madaraka katika sekta ya kilimo. Kujumuishwa kwa misaada ya fedha katika Mipango shirikishi ya Maendeleo ya Kilimo katika ngazi ya wilaya na maamuzi ya utekelezaji wa pamoja umeleta mafanikio katika sekta ya kilimo na nyingine. Aidha, ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Wizara za kisekta (ASLMs) umesaidia kurahisisha uratibu na usimamizi wa sekta ya kilimo.

d) Kuongezeka *mahitaji ya uzalishaji sambamba na kuongeza thamani, masoko na kuongeza kipato cha mkulima;* ASDP-1 iliweka mkazo zaidi katika teknolojia ya uzalishaji, usambazaji na usindikaji. Aidha, taarifa inaonesha kuwa wakulima wengi wana ujuzi kuhusu mbinu bora za uzalishaji, isipokuwa kwa mazao mapya na mbinu mpya ambazo zinaibuka mara kwa mara. Changamoto iliyopo ni jinsi wakulima watakavyoongeza kipato chao, kuongeza thamani na kuzalisha kwa tija kwa kufuata mahitaji ya soko. Uzalishaji na usambazaji wa teknolojia lazima uzingatie mahitaji ya wakulima na kutatua matatizo yanayowagusa ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa masoko.

e) *Maendeleo hafifu na uimarishaji wa Vyama vya Msingi na Ushirika:* Kujenga na kuimarisha vyama vya ushirika, au kuwawezesha wakulima ni jambo linatotakiwa kufanyika katika miradi na mipango mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ASDP II. Hata hivyo, kuna ukuaji mdogo katika eneo hilo, hivyo kuleta changamoto katika maendeleo ya ushirika huduma za ugani, uzalishaji mdogo wenye tija na upatikanaji wa masoko.

f) *Ukosefu wa uwazi kuhusu jinsi sekta ya umma inavyoweza kushirikiana na sekta binafsi katika kuendeleza sekta ya kilimo;* maendeleo ya mnyororo wa thamani yanahitaji ushirikiano baina ya sekta binafsi na washirika wa maendeleo kuanzia hatua ya kupanga mipango. Ushirikiano na uratibu madhubuti kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ni muhimu katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ASDP II. Kwa sasa, kuna ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika kufanya biashara za kilimo na watoa huduma binafsi. Hali hii ni lazima irekebishwe wakati wa utekelezaji wa ASDP II kwa kushirikisha kikamilifu sekta binafsi na taarifa nyingine kama vile SAGCOT au vyama na taasisi zisizo za kiserikali n.k.[26]

---

25 *Imetoholewa kutoka kwenye taarifa ya tathmini ya ASDP Juni 2011 na Taarifa ya Kukamilika kwa Utekelezaji wa ASDPI Jan 2014.*

26 *Imetoholewa kutoka kwenye taarifa ya tathmini na uchambuzi ya IFAD-COSOP (Dec 2014).*

g) *Kutokamilika kwa miradi ya umwagiliaji na matengenezo duni kunazuia mapato endelevu kwa wakulima;* miradi mingi ya umwagiliaji haikukamilika kutokana na mipango na usimamizi hafifu wa maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji, uhaba wa rasilimali na upatikanaji mdogo wa huduma za kitaalamu na teknolojia za uzalishaji. Umwagiliaji ilikuwa ni sehemu muhimu katika uwekezaji wa ASDP-1 ambapo hekta 112,500 ziliboreshwa na kuendelezwa kutoka mwaka 2006-2012 (wastani wa hekta 18,920 kwa mwaka). Hata hivyo, miradi ya umwagiliaji ilikumbana na matatizo kabla, wakati na baada ya ujenzi na uendeshaji. Ili kuondoa matatizo yaliyojitokeza ikiwemo usimamizi, upatikanaji wa maji na ukarabati wa miundombinu, ni muhimu utekelezaji wa ASDP II ukazingatia uchambuzi yakinifu, ili kubaini miundombinu ya umwagiliaji yenye gharama nafuu, eneo la kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji na taasisi za kusimamia umwagiliaji. Miradi mingi ya umwagiliaji iliboreshwa lakini haikuendelea kukarabatiwa, pamoja na usimamizi hafifu hivyo kusababisha kuchakaa mapema.

h) *Tathmini na ufuatiliaji jumuishi na changamoto za utekelezaji.* Mfumo wa Tathmimi na Ufuatiliaji wa ASDP I ulitegemea takwimu zilizotokana na tafiti za Taifa ambazo hazikutoa taarifa muhimu za mafanikio ya programu kwa wakati. Pia ukusanyaji wa takwimu kwa mwaka haukuweza kufanyika kama ilivyokuwa imepangwa hadi mwaka 2008/2009. Kutokana na hali hiyo, taarifa za tathmini zilitegemea taarifa kutoka Halmashauri ambazo hazikukamilika na zenye makosa. Kutokana na changamoto hizo orodha ya viashiria vya kupima programu na uboreshaji wake vilikuwa vikifanyiwa marekebisho mara kwa mara ili kuonesha matokeo ya malengo ya programu. Mambo muhimu ya kujifunza kutokana na uzoefu huo wa ufuatiliaji na tathmini wa ASDP I ambayo yatasaidia utekelezaji wa ASDP II ni: (i) Kuhakikisha kwamba ukusanyaji wa takwimu katika sekta ya kilimo kitaifa na ARDS una rasilimali za kutosha na kwamba takwimu ni lazima zifanyiwe uchambuzi wa kina na matokeo yake yatolewe mapema na kwa wakati; (ii) Ni muhimu kuwezesha kifedha ukusanyaji wa takwimu kila mwaka ili kutoa tathmini ya utekelezaji wa kila mwaka; na (iii) Ni muhimu kutumia taarifa ya ufuatiliaji na tathmini kama chombo cha kufuatilia utekelezaji wa programu ili kupima faida kama vile uzalishaji na matumizi ya teknolojia.

45. Kwa ujumla, utekelezaji wa ASDP-1 kwa kutumia utaratibu wa SWAp umeonekana kuleta ufanisi na matokeo endelevu. ASDP-1 iliweka mfumo imara kwa kujenga miundombinu na huduma za ugani kwa wakulima wadogo kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikihusisha miradi mingine iliyotekelezwa. Kutokuwepo kwa mikakati imara iliyolenga masoko ya kilimo na maendeleo ya mazao kwa kufuata mnyororo wa thamani kulikwamisha ufanisi wa programu. Katika miaka ya hivi karibuni, wabia wa maendeleo na mashirika yasiyo ya kiserikali yameunga mkono mikakati mingi ya maendeleo ya kilimo ikiwa ni pamoja na mnyororo wa thamani japo kumekuwepo na kukosekana kwa uratibu thabiti. ASDP I ilikuwa na msisitizo finyu wa kutafuta na kuendeleza masoko ya kilimo na mnyororo wa thamani kutokana na kutokuwepo kwa mipango sahihi. Ufanisi wa ASDP II utahusisha matokeo shirikishi ya mpango na muunganiko wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ikiwa ni pamoja na mfumo wa takwimu za sekta ya kilimo. Uwekezaji zaidi unahitajika kwenye sekta ya kilimo ili kukuza uwezo wa kitaasisi, mbinu za kuwafikia wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani pamoja na kuwekeza katika sera nzuri ili kuleta matokeo endelevu katika Sekta ya Kilimo.

## B. Changamoto kwenye Mifumo ya Kilimo na Vichocheo vya Utatuzi

46. Muhtasari wa changamoto tarajiwa na vikwazo katika utekelezaji wa ASDP II ni kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 5: Vikwazo vikuu na vichochezi vya mada**

| Eneo | Vikwazo vikuu | Vichocheo |
|---|---|---|
| Wawezeshaji | • Utekelezaji hafifu wa sera zilizopo<br>• Uratibu usiokidhi kupitia taasisi na mahusiano dhaifu katika Mikoa na ngazi ya Halmashauri.<br>• Upungufu wa takwimu na mifumo ya takwimu kwa ajili ya kutoa maamuzi na kubadilishana taarifa<br>• Miundombinu duni ya uzalishaji wa mimea na mifugo, nishati, maji, upatikanaji wa soko)<br>• Upungufu wa mifumo ya umilikishaji ardhi, mipango na utekelezaji<br>• Uhusiano dhaifu kati ya sekta ya umma na sekta binafsi | • Serikali kumiliki, kuboresha, kutekeleza kwa ufanisi,kufuatilia na kutathmini sera zinazofaa |
| Tija | • Mifumo hafifu ya utafiti katika sekta ya kilimo na uwezeshaji kifedha mdogo (upungufu wa wataalamu, kuchelewa kujibu mahitaji ya wakulima)<br>• Udhaifu wa kubadilisha ubunifu wa bidhaa ambazo hutumiwa na wakulima (mbayo ni mifumo ya kawaida zaidi na si ya kilimo na tovuti maalum);<br>• Muunganiko, mbinu na uunganishaji dhaifu wa ubunifu kati ya utafiti na ugani na wadau / watendaji<br>• Upungufu wa genetiki bora (mifugo na uvuvi)<br>• Kutokuwepo kwa jitihada za kutosha za utafiti wa mazao, mifugo na uvuvi<br>• Kukosekana kwa udhibiti wa kutosha wa magonjwa na wadudu<br>• Upungufu wa vifaa vya huduma za ugani (usafiri, vifaa na huduma za mifugo, vifaa vya ugani)<br>• Upungufu wa uwezo wa uchunguzi (vifaa na wataalamu)<br>• Kiwango cha juu cha vifo vya ndama kutokana na magonjwa ya kupe na jamii ya kupe | • Kuimarisha mifumo ya kilimo:<br>• Utafiti na ugani, na viunganisho vyao;<br>• Mbegu, mbolea, vizazi vya wanyama na vifaranga vya samaki<br>• Mifumo mingine ya pembejeo ikiwa ni pamoja na utumiaji wa mashine<br>• Huduma za afya ya wanyama na mimea<br>• Maabara za uchunguzi (mifugo, nk) |
| Upatikanaji wa Tija | • Upungufu wa mbegu na mifumo bora kwa ajili ya mifugo, mazao na uvuvi<br>• Upungufu wa wagani na mifumo ya uwezeshaji ugani<br>• Matumizi madogo ya pembejeo (mbolea, mbegu, mitambo, lishe ya chakula, chanjo, vifaranga samaki) nk.<br>• Uchache wa majukwaa na mijadala vijijini (ya vyama vya wakulima, biashara ndogo na za kati) kuruhusu wakulima kushirikiana na serikali na sekta binafsi<br>• Upungufu wa mashine za kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa chanjo ya mifugo<br>• Upungufu wa maendeleo ya matumizi na ufuatiliaji wa chanjo<br>• Ukosefu wa upimaji na ufuatiliaji ubora wa dawa za kudhibiti kupe na dawa nyingine za wadudu kwa ajili ya kudhibiti magonjwa na wadudu. | • Kuimarisha uzalishaji wa chanjo ya mifugo kitaifa<br>• Kuimarisha uwezo katika upimaji na ufuatiliaji wa dawa za kudhibiti kupe na dawa nyingine |
| Uongezaji Thamani | • Upotevu mkubwa wa mazao baada ya mavuno (kati ya asilimia 25 hadi 35) unaochangiwa na upungufu wa wataalamu wa kilimo, vifaa, hifadhi na upatikanaji wa masoko<br>• Upungufu wa taarifa za masoko na utafiti<br>• Uzalishaji mdogo wa maziwa, nyama na mayai<br>• Ubora mdogo wa wanyama na bidhaa za wanyama ambao hauwezi kushindana au kupata masoko mazuri<br>• Utekelezaji duni na udhaifu wa viwango vya ubora na usalama wa chakula.<br>• Kukosekana kwa miundo bora ya vyama vya ushirika vya wakulima ili kuhakikisha bei ya ushindani na mahitaji ya kuaminika<br>• Uduni wa sekta binafsi, mfumo mgumu wa kanuni na uwepo wa soko dhaifu<br>• Upatikanaji mdogo wa mikopo na bima | • Kukuza utumiaji wa pembejeo kwa ajili matokeo na masoko ya mikopo<br>• Kukuza utendaji mzuri wa vyama vya wakulima na vyama vya ushirika<br>• Kuimarisha mazingira mazuri ya ushiriki wa sekta binafsi ikiwa ni pamoja na kukuza ushirikiano wa serikali na sekta binafsi (PPP) |
| Masuala mtambuka: Jinsia, uimarishaji wa utawala bora, uwezo wa taasisi katika ngazi mbalimbali (BMGF 2014). | | |

47 **Muhtasari wa vikwazo vikuu vya kisekta**[27]

i. Mazingira duni ya sera na kutofautiana kwa utekelezaji wa sera kufikia malengo endelevu ya ukuaji wa kilimo;
ii. Ukuaji mdogo na kiwango kidogo cha tija , ikiwa ni pamoja na upatikanaji mdogo na endelevu wa pembejeo ( mbolea na mbegu, kuboresha aina za mifugo (uhimilishaji), vifaranga vya samaki, chanjo na dawa za mifugo);
iii. Uwezo duni wa uzalishaji wa mifugo ya asili na usambazaji mdogo wa mifugo bora,
iv. Uwezo duni wa kutoa huduma bora za kilimo na kisheria kwa mazao, mifugo na uvuvi.
v. Kutokuwepo kwa vipaumbele kwa ajili ya uwekezaji wa umma na sekta binafsi katika miundombinu (kwa mfano, umwagiliaji, barabara za vijijini, miundombinu ya kuhifadhi, nishati vijijini, miundombinu ya soko);
vi. Vizuizi katika ufanisi na ushindani wa masoko na usindikaji wa bidhaa za kilimo pamoja na maendeleo madogo ya mnyororo wa thamani;
vii. Upatikanaji mdogo wa mikopo kutoka taasisi za fedha;
viii. Uwezo mdogo wa matumizi bora ya ardhi na umiliki halali kwa ajili ya watumiaji wa ardhi;
ix. Uwezo dhaifu wa kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa;
x. Uwezo dhaifu wa taasisi na rasilimali watu pamoja na uratibu mdogo miongoni mwa wadau katika ngazi ya taifa na Halmashauri, pamoja na mfumo dhaifu wa takwimu za kilimo.

48 Mfumo Mkakati na Vichocheo vya Kukuza Kilimo Jumuishi na Kupunguza Umaskini: Ili kufikia lengo la ASDS, ASDP-2 itatekelezwa kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana kupitia utekelezaji wa ASDP-1. Vifuatavyo ni vichocheo vya kutekeleza mpango mkakati wa kukuza kilimo na kupunguza umaskini vijijini[28].

- *Sera na Sheria.* Kukuza ufanisi kwa kuboresha sera za kilimo ili kuleta mageuzi yatakayowezesha tija na kuchochea shughuli mbalimbali kwenye mnyororo wa thamani. Utaratibu huu utahakikisha upatikanaji na matumizi ya mbegu bora, mbolea, viuatilifu, na dawa ya mifugo, chanjo, uhimilishaji, vifaranga vya samaki kuzingatia viwango vya usafi kwa lengo la kuhakikisha ushindani wa masoko ya nje, sera na kanuni za masoko, kuimarisha maendeleo ya mnyororo wa thamani, motisha endelevu kwa watendaji mbalimbali, sambamba na faida ya ulinganishi ya soko la Tanzania. Katika mfumo wa udhibiti (sheria, mifumo ya taasisi na rasilimali watu), serikali pia inafanya kazi za: (i) Kuendeleza mazingira mazuri ya kisheria kwa kuimarisha vyama vya ushirika vya wakulima na jamii; (ii) Matumizi bora ya ardhi kwa kilimo, (iii) Kukuza matumizi ya zana za kilimo, (iv) Uwezeshaji wa mikataba ya kilimo kwa ajili ya masoko; (v) Mfuko wa udhibiti bei; na (vi) Mageuzi ya Sheria za mazao.

- *Uzalishaji/tija na Biashara.* Kuongeza uzalishaji endelevu wa mazao, mifugo / samaki na kuuza bidhaa nje kutaboresha lishe na usalama wa chakula katika kaya, pamoja na kuuza ziada. Kuongeza ushindani na faida kwa wakulima kutawezeshwa na: (i) Teknolojia endelevu za uzalishaji (ikiwemo hali ya hewa nzuri), zitakazowezeshwa kwa njia ya uhusiano wa utafiti na ugani, (ii) Ufanisi wa mifumo ya ugani kwa kutumia TEHAMA; (iii) Ukuaji na ujumuishaji wa majukumu ya sekta binafsi; (iv) Upatikanaji endelevu wa mikopo vijijini na (v) Vyama bora vya ushirika vya wakulima vyenye nguvu ambavyo pia vitasaidia upanuzi wa masoko na maendeleo ya mnyororo wa thamani.

- *Ujumuishaji wa Sekta Binafsi.* Kuchochea maendeleo ya upanuzi na ujumuishaji wa sekta binafsi utakaowezeshwa na: (i) Ufanisi wa ushirikiano wa sekta ya umma na sekta binafsi na (ii) kuongeza miundombinu ya vijijini (hasa umwagiliaji mdogo, vifaa vinavyotumika baada ya mavuno, miundombinu ya mifugo, maghala na barabara za vijijini). Hii itachangia pia kuongeza fursa mbalimbali za ajira katika kilimo.

---

27 *Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili unajumuisha, utangulizi na muhtasari kwa ajili ya sekta ya kilimo ambayo inaeleza kwa muhtsari hali halisi ya sekta ya kilimo. Uchambuzi unaonesha taswira inayofanana kisekta. Mfumo uliosasashwa wa kaya utakuwa muhimu katika kuendeleza mikakati na uchukuaji wa hatua mbalimbali*
*Ili kufikia ukuaji jumuishi wa Kilimo na kupunguza umaskini vijijini, uchambuzi mahsusi unatakiwa ufanyike ili kuweka malengo yanayotekelezeka katka kaya, ikolojia za Kilimo kwa kuzingatia mnyororo wa thamani . Uchambuzi unatoa taswira ya sekta inayofanana, :*

28 *Ili kufikia ukuaji wa kilimo ma kupungua kwa umaskini, vijijini, uchambuzi wa kina unahitajika ili kuboresha kaya za kilimo na maeneo yaliyotambuliwa kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa.*

- *Uwezo wa taasisi na Uratibu.* Kuimarisha maendeleo ya kitaasisi na ufanisi, ni pamoja na: (i) Maendeleo ya uwezo wa wahusika wakuu kwenye kuzingatia matokeo katika ngazi ya kitaifa na Halmashauri; (ii) Ufanisi, uwazi na uwajibikaji wa ugatuzi wa huduma muhimu za kilimo na utekelezaji;(iii) Ufanisi na uwepo wa matokeo halisi katika mpango, bajeti na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini katika ngazi mbalimbali kwa kushirikisha wadau wote, (iv) Kuimarisha huduma za lishe na usalama wa chakula; na (v) Kuimarisha mchakato na mbinu za uratibu ndani ya wizara za Sekta ya Kilimo, mashirika /wizara nyingine za sekta, washirika wa maendeleo, serikali za mitaa / taasisi, sekta binafsi na wadau wengine muhimu (ikiwa ni pamoja na wakulima na taasisi kwenye mnyororo wa thamani)

## C. Uandaaji wa Programu ya ASDP II

49 Utekelezaji wa ASDP-1 uliwezekana kutokana na kufanyika kwa mapitio kwa pamoja yaliyotoa taarifa za mafanikio na changamoto kwenye sekta ya kilimo. Mapitio ya kila mwaka ya ufanisi wa sekta yalijumuisha Wizara za kisekta pamoja na washirika wa maendeleo, wafanyabiashara, Halmashauri na wawakilishi wa wakulima katika ngazi za mitaa na kitaifa. Mapitio hayo yalisaidia kuondolewa kwa vikwazo vya utekelezaji na kufanya marekebisho katika mipango mbalimbali. Taarifa kutoka kwenye mamlaka za usimamizi na kwa wahusika wa utekelezaji wa programu zilikusanywa na Sekretarieti ya ASDP na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Juhudi zimefanywa ili kuingiza mambo ya kujifunza kutoka ASDP I kwa ajili ya ASDP II na kushughulikia changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa ASDP I ili kuepuka vikwazo kama ilivyoanishwa na tathmini ya ASDP I iliyofanyika mwaka 2011 na taarifa ya mwaka 2014.

**Kielelezo Na 11: Mazingira ya Tanzania kwa ajili ya Kuendeleza Kilimo (2015–2024)**




50 Katika kipindi cha miaka iliyopita, mashauriano ya kina yalifanyika kati ya Serikali, wawakilishi wa sekta binafsi, sekta ya umma, wafadhili na Serikali za Mitaa, ili kufahamu kilichofanyika na ambacho hakikufanyika wakati wa utekelezaji. Kwa ujumla, ASDP-II inahusisha kazi zote zinazohusiana na Sekta ya Kilimo zinazowezeshwa na fedha kutoka Serikalini, washirika wa maendeleo na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa kuzingatia ASDS na vipengele husika vya mfumo wa TAFSIP.

51 **Mfumo wa Mfuko wa Pamoja wa fedha ulionesha changamoto wakati wa ASDP-1** na hivyo kusababisha baadhi ya misaada ya washirika wa maendeleo kuelekezwa kwenye miradi mahsusi. Japokuwa mfumo wa ugharamiaji wa pamoja unapendwa kutumiwa na Serikali, mchango wa Serikali si wa kuridhisha. Washirika wa maendeleo wanaweka sehemu kubwa ya fedha zao kwa kutumia

utaratibu wa miradi ndani na nje ya bajeti. Utaratibu wa kuelekeza fedha kwenye miradi mahsusi umeonekana kutokuwa na tija kutokana na kukosekana kwa utekelezaji jumuishi pamoja na mfumo imara wa tathmini na ufuatiliaji.

52 ASDP II ni Programu inayozingatia matokeo makubwa ya kuendeleza Sekta ya Kilimo. Pamoja na ASDP II kutekeleza ASDS, pia inajielekeza pia kwenye kuboresha mazingira na sera katika kilimo na kutilia mkazo kwenye programu za maendeleo za kisekta (mazao, mifugo, uvuvi, masoko, usalama wa chakula na lishe) pamoja na kuboresha sekta binafsi. Vielelezo Na. 12 na 13 vinaonesha muundo wa programu na mfumo wa upatikanaji wa fedha kwa: i) Kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi, ii) Uratibu endelevu kati ya Serikali na sekta binafsi, hasa kwa kuzingatia mfano wa SAGGOT, iii) Kuongeza uwajibikaji kwenye sekta (kupanga bajeti, pamoja na ufuatiliaji na tathmini) kwa ajili ya kuongeza uwajibikaji na utendaji katika ngazi ya kitaifa na Serikali za Mitaa.

**Kielelezo Na. 12: Mfumo wa Uandaaji wa ASDP II.**




**Kielelezo Na. 13: Mfumo wa utoaji wa fedha kwa ajili ya ASDP II**



53 Jukumu muhimu la Wizara za Kisekta za Kilimo (ASLMs), wakiongozwa na Wizara ya Kilimo ni kuratibu na kuoanisha vipaumbele vya uwekezaji kwa kushirikisha wadau mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya sekta. Pia kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya wakulima ili watoke kwenye umaskini wa kipato, ikiwa ni pamoja na kuchochea sekta binafsi iweze kuwekeza zaidi na kushirikiana na Serikali kwa kutumia mfumo wa mahusiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)[29].

## D. Misingi Mikuu ya Uandaaji wa Programu ya ASDP II

54 Sambamba na sifa muhimu za ASDS, kanuni zifuatazo zinasisitiza uandaaji wa ASDP II.

**Sanduku Na. 1: Kanuni muhimu za kuandaa ASDP II**

**Kanuni muhimu za kuandaa ASDP II**

- **Kipaumbele cha kibiashara kinachozingatia mifumo ya uzalishaji endelevu wa wakulima wadogo** -kwa kufuata mahitaji ya soko ;
- **Kipaumbele kinachozingatia minyororo ya thamani ya mazao katika Kanda za Kiikolojia za Kilimo (AEZ)** – kwa kuzingatia uwekezaji katika mazao yenye matokeo makubwa katika tija, faida, kuboresha hali ya maisha ya mkulima, biashara na viwanda.
- **Kuchochea ushiriki wa wadau wote,** ikiwa ni pamoja na ushiriki wa wakulima na sekta binafsi katika ngazi zote kwa kuongeza ushirika na umiliki. Hii itahusisha kuongezeka kwa udhibiti wa rasilimali za umma na wadau wote kwenye mnyororo wa thamani wa mazao katika ngazi zote kwa ajili ya kuboresha ufanisi na uhusiano.
- **Uwezeshaji wa wakulima na wadau** katika mnyororo wa thamani kwa kuimarisha uwezo wa wakulima na kuimarisha ushirika.
- **Utoaji wa huduma kwa wadau wengi:** ASDP ilenge kuwavutia watoa huduma wengi kwa pamoja ili kuongeza unafuu wa gharama na ushindani wa utoaji huduma.
- **Ugawaji wa rasilimali kutokana na matokeo.** Ugawaji wa rasilimali kwa Halmashauri utakuwa wa uwazi na usawa kwa kuendelea kutumia mfumo wa kugawa ruzuku. Uhamasishwaji wa Halmashauri kutumia fedha zao kwa ufanisi utaendelezwa kupitia tathmini ya kila mwaka. Hata hivyo, Halmashauri zitalazimika kufuzu vigezo vya kiutendaji vilivyowekwa ili kupata usaidizi wa fedha za msingi za kuimarisha uwezo wa ndani wa kiutendaji na uwezo katika uwekezaji.
- **Kuwezesha uimarishaji wa uwekezaji binafsi na ushirikiano wa umma na binafsi (PPPs)** chini ya mfumo wa mnyororo wa thamani wa mazao wa MSIPs: kutafuta michango kulingana na utendaji na maeneo ya vipaumbele yaliyokubaliwa.
- **Ushirikiano wa wadau kwa kufuata mifumo ya Serikali:** mifumo iliyopo ( Bajeti ya Serikali MTEF, DADPs, na utoaji ruzuku) itatumiwa ili kuongeza ufanisi na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa wadau kwa kufuata vipaumbele..

55 Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) ambayo itatekelezwa kwa miaka 10 (2017 / 2018-2027 / 2028) imejikita katika kutatua changamoto na mapungufu ya ASDP-1. Lengo la ASDP II ni kushughulikia vikwazo vikuu na changamoto zinazokwamisha sekta ya kilimo ili kuongeza mchango wa kilimo katika Pato la Taifa, kuboresha ukuaji wa kipato cha wakulima wadogo na kuhakikisha usalama wa chakula ifikapo mwaka 2025. Programu imeandaliwa kwa kuzingatia uwekezaji wenye mafanikio chini ya ASDP-1, sambamba na mifumo ya sera ya muda mrefu na ya kati, ASDS (2001), TAFSIP (2011), ASDS (2015) na mafunzo yaliyopatikana kutoka kwenye utekelezaji wa

29 *Dhana ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi katika shughuli za uzalishaji na huduma za kijamii inahitaji kuwepo na utaratibu ambao sekta binafsi itakuwa inajenga, inakarabati na kuendesha shughuli zote kulingana na makubaliano maalum. Serikali itaweka mazingira wezeshi. (PPP, 2009).*

.

ASDP-1. Misingi ifuatayo ilizingatiwa katika uandaaji wa ASDP II.

56 **Muundo wa ASDP II unalenga kuimarisha biashara kwa wakulima wadogo** kwa mtazamo wa kusaidia wakulima kutoka kwenye kilimo cha kujikimu kwenda kwenye kilimo cha kibiashara na kuendesha kilimo-biashara. Hii inatokana na ukweli kuwa usalama wa chakula ni muhimu kwa ajili ya kupunguza umaskini, lakini si suluhisho kamili. Ili kupunguza umaskini kipato kwa kaya lazima kiongezeke kutoka katika viwango vya chini vya sasa. Wakulima wadogo wanatakiwa kuzalisha kwa ajili ya soko na pia wapaswa wakulima wasaidiwe kuunganishwa kwenye mnyororo wa wafanyabiashara wa mazao na wasambazaji wa pembejeo. Lengo kuu ni kuunganisha sekta ya kilimo na viwanda ili kuongeza ufanisi na kupanua mahitaji ya chakula kwa ajili ya walaji wa mijini. Sambamba na kuweka mkazo kwa wafanyabiashara wadogo, uhusishaji mkubwa wa ushiriki wa sekta binafsi hamasishwa, katika uzalishaji wa kilimo kwa ajili ya biashara na katika masoko, usindikaji na mnyororo wa usambazaji wa pembejeo za kilimo. Uwekezaji katika barabara za vijijini / miundombinu, usindikaji hasa katika kusaga nafaka na ufungashaji na matumizi endelevu ya maliasili vitawekewa mkazo katika kupanua masoko, hasa kwa mazao ya kipaumbele.

57 **Kuzingatia matokeo.** Mambo muhimu ya kujumuisha katika utekelezaji wa ASDP II kutokana na uzoefu wa ASDP Ini pamoja na, kuwekeza rasilimali kwa wingi kwenye mnyoyoro wa thamani wa mazao ya kipaumbele katika Kanda za Kilimo za Kiikolojia na wilaya zilizochaguliwa ili kuleta matokeo makubwa na kuyasambaza katika maeneo mengine, wakati wakulima wadogo[30] wakizalisha kwa kulenga soko. Ili kupata matokeo makubwa inapendekezwa utekelezaji wa programu ufanyike kwa awamu ili kuimarisha utekelezaji wa mnyororo wa thamani katika idadi ndogo ya wilaya. Wilaya ambazo hazitafikiwa katika awamu ya kwanza, zitafikiwa katika awamu inayofuata na hivyo utekelezaji wa programu utafikia mikoa na wilaya zote baada ya muda.

58 **Kuongeza tija kwa ajili ya usalama endelevu wa chakula na lishe, kipato cha mkulima na ukuaji wa uchumi.** ASDP II itatatua changamoto katika maeneo yenye upungufu wa chakula kwa kuongeza uzalishaji wa ziada wa chakula na ubora wa mazao, mifugo na uvuvi katika wilaya ambazo zina fursa za kuzalisha ziada. Maeneo yenye upungufu wa chakula yatafaidika kutokana na ziada ya chakula kinachozalishwa kwenye wilaya zenye fursa ya kuzalisha ziada kwa kuhamasisha sera ya masoko na sekta binafsi. Lengo la programu ni kuhakikisha utoshelevu wa chakula, na kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi ambapo Tanzania itapata faida linganifu katika masoko ya kikanda na kimataifa. Kipaumbele cha uwekezaji ni kupanua kilimo cha umwagiliaji, kuendeleza malisho, udhibiti wa magonjwa ya mifugo, kuendeleza uvuvi, uzalishaji kwa kutumia zana za kilimo, utafiti na maendeleo, upatikanaji wa teknolojia za kisasa za kilimo na pembejeo sahihi.

59 **Kuongeza usimamizi wa rasilimali kwa wanufaika.** ASDP-1 ilisisitiza umuhimu wa kupaza sauti ya wazalishaji (wakulima/wafugaji) katika kupanga na kutekeleza mipango katika ngazi ya Halmashauri na katika kuongeza maamuzi yao na kudhibiti usimamizi, kubuni na kuongezeka uwekezaji kulingana na mahitaji yao. Japo kuwa yapo mafanikio yaliyopatikana katika utaratibu huo, bado unahitajika mkazo zaidi katika utekelezaji wa ASDP II. Utaratibu huo utazingatiwa katika kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini mipango na mifumo ya fedha. ASDP II inahimiza vikundi vya wakulima, vyama vya ushirika na wajasiriamali kudhibiti mgao wa rasilimali kwa kuzingatia taratibu za uwazi.

60 **Utoaji huduma kwa wigo mpana:** kutokana na uzoefu wa nchi za jirani, ASDP I ilitilia mkazo wa kuimarisha mfumo wa vyama na vikundi vya wakulima na watoa huduma ikiwa ni pamoja na ushirika kwa ajili ya kutoa na kupokea huduma na ushauri. Kwa kutumia uzoefu wa ASDP I ni muhimu kuendelea kukuza sekta binafsi, ushirika na vyama vya wakulima (FO, CSO, NGOs). ASDP II inalenga kutoa wigo mpana wa watoa huduma kwa kuunganisha huduma ya kilimo-biashara na sekta binafsi pamoja na mikataba kwa wakulima na watoa huduma ya kilimo-biashara na ushauri.

61 **Huduma endelevu kwa mazao mbalimbali (Mseto)**. ASDS inasisitiza kuwepo kwa vyanzo mbalimbali na endelevu vya kuongeza uzalishaji wa mazao, mifugo na uvuvi vinavyoongeza mapato, kupunguza vihatarishi na mabadiliko ya bei. Kupitia ASDP II, kutakuwa na mazao mbalimbali yatakayoendelezwa kwa kufuata mnyororo wa thamani utakaosaidia kuongeza thamani ya mazao ya vipaumbele. Ni muhimu kuimarisha mifumo ya uzalishaji katika ufugaji kwa kutumia mabaki ya mazao, udongo endelevu na usimamizi wa mifumo ya maji na matumizi bora ya mifumo ya umwagiliaji. Taratibu na uratibu

30 *Kutoa msaada kwa watu wenye mahitaji maalum ni muhimu na uzingatiwe wakati wa utoaji wa msaada .*

utazingatiwa ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa soko la uhakika. Ni muhimu pia kupanua kilimo cha umwagiliaji na kufungua fursa kwa kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali kama vile kilimo cha mboga na matunda. Aidha, programu inalenga kutatua changamoto za magonjwa ya mazao na mifugo, kuboresha upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo, uboreshaji na upatikanaji wa ardhi ya malisho ya mifugo, kuongeza upatikanaji wa hisa, kibiashara katika sekta ya mifugo na ufugaji wa samaki na uvuvi endelevu. Hivyo, ASDP II itahamasisha utumiaji wa maliasili, ikiwa ni pamoja na maji, kwa ufanisi zaidi na kusaidia upatikanaji wa masoko ya mazao ndani na nje ya nchi.

62 **Usalama wa Chakula na Lishe.** Ingawa ASDP II itatekelezwa kwa kufuata vipaumbele, usalama wa chakula na lishe ni eneo muhimu litakalozingatiwa. Hali ya lishe kwa jamii bado ni eneo linalohitaji msukumo zaidi hasa katika maeneo ya vijijini. Hii ni kwasababu kwa muda wa muongo mmoja uliopita eneo la lishe bora limeonekana kuwa lenye changamoto. Katika kuoanisha mipango mbalimbali, ASDP II itachangia kuwepo kwa lishe bora vijijini hasa kwa: (i) Kuimarisha tafiti za kilimo zitakazotatua tatizo la lishe na usalama wa chakula, kwa mfano, mazao yenye ubora kwa ajili ya viini lishe kama protini ikiwa ni pamoja na mahindi, mchele, nyama na maziwa ya mifugo na samaki (ii) Kusaidia kutoa huduma na ugani shirikishi na ushauri kwa mfano, Mashamba Darasa pamoja na elimu kwa mkulima na upatikanaji wa habari katika vituo vya rasilimali ngazi ya kata na vijiji na matumizi makubwa ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa usambazaji wa taarifa; (iii) Kupanua upatikanaji wa mbegu za aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mbegu za mazao, mifugo, samaki na kuimarisha mitandao ya usambazaji wa mazao kwa kutumia kanuni zinazofaa; na (iv) Usindikaji wa chakula chenye lishe bora. Hii ni pamoja na kuboresha uwezo wa taasisi zinazotoa huduma kwa ajili ya lishe bora na ukuaji endelevu.

63 **Kuhusisha Wanawake na Vijana.** Inafahamika kuwa wanawake na vijana ni eneo mtambuka ambalo linahitajika kushughulikiwa katika ngazi zote. ASDP II itachangia kwa kufanya kazi za uchambuzi wa kijamii/uchumi na jinsia/vijana[31]. Mkakati utahakikisha jinsia zote na vijana wanahusishwa kikamilifu katika uandaaji na utekelezaji wa shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi. Mfumo endelevu kwa ajili ya kufanikisha hilo upo katika mkakati wa jinsia na vijana na katika mkakati wa uendeshaji mipango ya shughuli za kila wilaya, au vitengo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji na kufafanua mifumo wa utekelezaji. Utofautishaji wa makundi kwa mali, ulemavu, umri na sifa nyingine za kiuchumi na kijamii unahitajika kuhakikisha kwamba makundi mengi zaidi ya watu wasiojiweza yanafaidika na mpango huo. Kulingana na uchambuzi na maudhui jumuishi ya shughuli za jinsia na vijana, ASDP II kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itahakikisha inatoa msaada wa kutosha kwa makundi lengwa.

64 **Kuzingatia Mabadiliko ya Tabianchi.** ASDP II itatekelezwa kwa kuzingatia mwenendo na mabadiliko ya Tabianchi, ikiwa ni pamoja na kutumia miongozo mbalimbali inayoelekeza mbinu za kufuata ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwenye sekta ya kilimo. Kukithiri kwa jotoridi na upungufu au ongezeko la mvua linahitaji tafiti na kuimarisha teknolojia kwa ajili ya manufaa ya wakulima, wafugaji na wavuvi. Uwezo wa wakulima, wavuvi na wafugaji kuendana na mabadiliko ya hali ya hewa kutaimarisha na kuhakikisha athari katika mifumo na shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi zinadhibitiwa. Orodha ya machaguo ya njia za kupunguza athari za mabadiliko ya hali ya hewa, ikiwa ni pamoja na kilimo cha uhifadhi wa mazingira[32] itazingatiwa na kujaribiwa na kusambazwa kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. ASDP II itazingatia mipango ya kujenga uwezo kwa ajili ya majaribio (*FFSs*), maafisa ugani na wataalamu wa kada mbalimbali wa masuala yanayohusiana na maendeleo ya hali ya hewa, na kuandaa vipindi maalum kwa ajili ya kuhabarisha wakulima, wafugaji na wavuvi mara kwa mara.

## E. Wigo, Mtazamo na Awamu za Programu ya ASDP II

65 Wigo na mtazamo wa Programu ya ASDP-1 ulijumuisha utekelezaji kwa nchi nzima na ulihusisha maeneo madogo madogo takriban kwenye sekta zote za kilimo na mifugo kwa kutegemea vipaumbele na maamuzi ya uwekezaji ya Halmashauri. **Utekelezaji wa ASDP II utajumuisha wilaya zote katika**

31 *Kutofautisha makundi kulingana na uwezo, mahitaji, umri na masula mengine ya kijamii yatahitajika ili kutambua mahitaji tofauti ya makundi hayo kwa ajili ya kuwapa msaada unaostahili. .*

32 *Angalia pia 'Save and grow'. FAO 2012 .*

**suala la utoaji wa huduma za kilimo, mifugo na uvuvi kwa umma** ambalo ni msaada wa msingi kwa ajili ya kujenga uwezo, mahitaji yatokanayo na huduma za ushauri, nk. **Hata hivyo wigo wa uwekezaji utalenga mazao ya kipaumbele yaliyochaguliwa katika Kanda za Kilimo za Kiikolojia.** Lengo ni kuongeza uwekezaji katika sekta ya kilimo, na kuongeza usalama wa chakula na lishe badala ya kuagiza chakula nje ya nchi. Hivyo, Sababu kuu za uwekezaji kwa kuzingatia mazao ya kipaumbele na maeneo ya kiikolojia ni: (i) Kuongeza tija endelevu na ushindani wa uzalishaji kwa kufuata mnyororo wa thamani wa bidhaa za kipaumbele, (ii) Kuongeza thamani ya mazao na masoko ya ndani na nje ya nchi, na usambazaji wa kuaminika wa malighafi kwa viwanda vya ndani; (iii) Kuruhusu matokeo makubwa ya uwekezaji kwenye miundombinu, (iv) Kumalizia/ kukamilisha uwekezaji na miradi iliyokuwa chini ya ASDP-1 (hasa kilimo cha umwagiliaji, ongezeko la thamani na miundombinu ya masoko); (v) Kuimarisha na kuboresha upatikanaji wa pembejeo za kilimo na huduma za kifedha kwa gharama za chini na kuimarisha mnyororo wa usambazaji wa pembejeo, kadri ushindani unavyoongezeka; na (vi) Kukuza uwekezaji mkubwa wa sekta binafsi hasa katika mnyororo wa mazao ya kipaumbele.

66 Kuimarisha Uwezo wa Taasisi. Programu imelenga: (i) Kuwezesha na kuimarisha ushirika wa wakulima wadogo, kufanya kilimo kiwe cha kibiashara; (ii) Kusaidia kilimo-biashara kuunganishwa na mifumo ya uzalishaji kwa ajili ya masoko na kuendeleza mnyororo wa thamani, (iii) Kuimarisha huduma za umma na binafsi kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya teknolojia bora na kilimo-biashara, (iv) Kuwezesha maendeleo ya masoko (sera na miundombinu) na miundombinu ya uzalishaji mali; na (v) Kujenga uwezo wa kitaasisi katika ngazi mbalimbali, kwa ajili ya watendaji wa Serikali na mashirika yasiyo ya serikali.

67 Uchaguaji wa mazao na bidhaa za kipaumbele. Kwa kutumia vigezo[33] vya usalama wa chakula na lishe mapato ya zao kutokana na mauzo ya nje na mchango katika uzalishaji wa kilimo, bidhaa chache zilionekana ni muhimu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Kwa upande wa mchango wa nishati katika ulaji wa chakula kwa Watanzania, mahindi, mihogo, mchele na kunde huchangia takriban asilimia 53 ya nishati. Katika eneo la Kilimo-biashara, tumbaku (asilimia 17.6), pamba (asilimia 14.5) na kahawa (asilimia 14.1) huchangia takriban asilimia 46 ya thamani ya mauzo nje. Ngano (asilimia 31.4) na mawese (asilimia 27.3) inajumuisha sehemu kuu ya jumla ya thamani ya chakula cha kuagizwa kwa wingi kutoka nje kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na. 6: Bidhaa za kilimo, uzalishaji, biashara na lishe (2005 - 2010)**

| Bidhaa | Mchango katika thamani ya uzalishaji | Mchango katika thamani ya kuuza nje | Mchango katika thamani ya kuagiza, | Mchango katika lishe* |
|---|---|---|---|---|
| Karanga | 1.2 | 6.7 | 0.0 | 0.2 |
| Kahawa | 0.8 | 14.1 | 0.0 | 0.0 |
| Maziwa ya ng'ombe | 7.3 | 0.0 | 0.6 | 2.6 |
| **Mahindi** | **6.5** | **0.8** | 2.9 | **24.3** |
| Mazao ya jamii ya mikunde | 10.6 | 7.5 | 0.7 | 8.5 |
| Mchele | 5.2 | n.d. | n.d. | 9.1 |
| Pamba | 2.9 | 14.5 | 0.1 | n.a. |
| Sukari | 1.2 | 1.6 | 8.6 | 4.0 |
| Ngano | 0.2 | 1.4 | 31.4 | 5.9 |
| **Muhogo** | 8.2 | **0.0** | **0.0** | **10.5** |
| Mifugo | 12.0 | 0.1 | d 0.6 | 1.6 |
| Mtama/uwele | 2.4 | 0.1 | 0.2 | 3.8 |
| Chai | 0.5 | 6.3 | 0.0 | 0.0 |
| Ndizi | ***12.7*** | 0.0 | 0.0 | ***4.0*** |

33 *Kulingana na tafiti ya hivi karibuni ya FAO (MAFAP/SPAAA, 2013).*

| Bidhaa | Mchango katika thamani ya uzalishaji | Mchango katika thamani ya kuuza nje | Mchango katika thamani ya kuagiza, | Mchango katika lishe* |
|---|---|---|---|---|
| Mawese | 0.0 | 1.6 | ***27.3*** | 3.3 |
| Tumbaku | 1.3 | 17.6 | 1.1 | n.a. |

Chanzo: MAFAP (2013). Mapitio ya chakula ya sera za kilimo Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. MAFAP Taarifa ya nchi, FAO, Rome, Italy, p 62.

68 Pamoja na vigezo vya hapo juu, kwa kutumia vigezo vya uwezekano wa biashara, upatikanaji wa teknolojia kwa ajili ya kuboresha tija na faida, na uwezekano wa kuongeza na kupunguza orodha ya bidhaa za kipaumbele imepungua.

**Jedwali Na. 7: Mazao ya kipaumbele katika Kanda za Ikolojia ya kilimo na awamu za bidhaa muhimu kwa eneo**

| ***Kanda za kiikolojia za kilimo (kanda za zamani)***[34] | **Bidhaa za kipaumble** | | | **Lishe**[b] | **Masoko** | **Uwiano wa wafadhili** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Mazao** | **Mifugo na samaki** | **Mazao ya biashara** | | | |
| **Kati** Nusu jagwa-(*Unimodal*)-(Dodoma, Singida, Shinyanga, Tabora) | Alizeti/ mahindi / mtama/uwele, mchele, viazi, kilimo cha maua[35] mazao ya bustani | nyama, hides/ ngozi, maziwa, mbuzi | pamba, tumbaku | **Mbaya zaidi** | Wastani | Wastani |
| **Ziwa** (*Unimodal/ bimodal*) – (Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Geita, Simiyu) | mchele, maindi, muhogo,ndizi, viazi, mtama/ uwele,kilimo cha mazao ya bustani | kuku, samaki | katani, kahawa, miwa | **Sawa** | Nzuri | Wastani wa chini |
| **Nyanda za juu Kaskazini** (*Bimodal*) – (Arusha, Kilimanjaro, Manyara) | Mahindi,mchele, jamii ya mikunde, viazi,kilimo cha mazao ya bustani, ndizi | nyama, ngozi, maziwa, mbuzi, | kahawa, ngano | **Mbaya zaidi** | Nzuri | Wastani |
| **Pwani ya mashariki-** (*Unimodal/ bimodal*)- Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Mtwara, Lindi | Muhogo, mchele, mahindi, viazi, mbegu za mafuta[36], kilimo cha mazao ya bustani | kuku, samaki | karanga,miwa, seaweed, katani | Mbaya | Wastani | Wastani wa Juu |
| **Nyanda za unyevu***(mafuriko, swamp)***-** Morogoro (Kilombero, Wami), Pwani (Rufiji), Mbeya (Usangu) | Mchele | nyama, ngozi, maziwa, mbuzi, | Miwa | Mbaya | Nzuri | Wastani wa Juu |
| **Nyanda za Juu Kusini Magharibi** (*Bimodal*) Rukwa, Kigoma, Kagera (Karagwe, Misenyi, Ngara) | Mahindi, kilimo cha bustani, ndizi, mimea, viazi, mchele | kuku, samaki | kahawa,ngano, miwa | Sawa | **Mbaya** | **Wastani wa Chini** |
| **Nyanda za Juu Kusini** *(Bimodal)* Mbeya, Iringa, Njombe, Morogoro | Mahindi, Mchele, viazi, kilimo cha mazao ya bustani | maziwa, nyama, samaki, | kahawa, katani,kokoa ,chai | **Mbaya zaidi** | Nzuri | Wastani wa juu |
| **Miinuko *(Unimodal)*** Tabora,magharibi Rukwa/ Katavi, Mbeya, Ruvuma kusini, Morogoro, Mwanza kusini, Simiyu, Geita | | kuku, mbuzi, ngozi | | | | |

34 *Kuzingatia eneo la kijiografia*
35 *Mazao ya bustani ni pamoja na Mbogamboga, matunda n.k*
36 *Mazao ya mbegu za mafuta yanajumuisha: alizeti, ufuta, mawese, nazi, karanga n.k*

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kusini**<br>*Nusu jagwa* Lindi, Mtwara pwani | Mihogo, mchele | | karanga, uwono | **Mbaya zaidi** | **Mbaya** | **chini** |

a. Mazao ya bustani kuendeleza lishe kwa kaya na masoko, kupanua eneo la umwagiliaji,
b. Lishe, masoko na ufadhili: Matokeo ya jumla (BMGF, 2014)
c. Jumla ya kaya kwa kuzingatia wingi wa watu takwimu za mwaka 2012 karibu 70% za kaya ziko vijijini na wastaniwa kaya ni watu 5.

**Jedwali Na. 8: Bidhaa za Kipaumbele katika Mnyororo wa Thamani Kikanda**

| Ikolojia ya kilimo kikanda | Mkoa | Walegwa HHs | Bidhaa zenye kipaumbele | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Mazao | Mifugo na samaki | Mazao ya biashaa |
| Kati | | 715,000 (8%) | Mahindi<br>Tumbaku<br>Mtama na Uwele | Nyama ya ng'ombe:<br>Nyama: mbuzi<br>Kuku | Mazao ya mafuta (Alizeti na mawese)<br>Kilimo cha mboga na matunda |
| Pwani | | 2,300,000 (25%) | Mchele<br>Mahindi<br>Muhogo<br>Maharage | Maziwa<br>Nyama<br>Samaki<br>Mwani | Karanga,<br>Miwa<br>Mazao ya mafuta (Ufuta na Nazi)<br>Mboga na matunda |
| Ziwa | | 2,100,000 (23%) | Mahindi<br>Mahindi<br>Viazi | Nyama:<br>Nyama-Mbuzi<br>Samaki | Pamba<br>Kahawa<br>Miwa<br>Mboga na matunda. Na ndizi |
| Nyanda ya kaskazini | | 1,035,000 (11%) | Mahindi<br>Kunde & Maharage<br>Ndizi | Maziwa,<br>Nyama ya ngombe: | Kahawa<br>Mbogamboga na Matunda |
| Kusini | | 570,000 (6%) | Muhogo<br>Mazao ya Mafuta<br>Mahindi | Nyama ya Mbuzi:<br>Kuku<br>Samaki | Karanga |
| Nyanda za kusini | | 2,395,000 (26%) | Mahindi<br>Viazi (mviringo na,vitamu)<br>Mchele | Nyama ya ng'ombe<br>Kuku<br>Maziwa<br>Samaki | Chai/kahawa<br>Mboga na matunda<br>Miwa |

69 **Utekelezaji wa ASDP II na uwekezaji kwenye ikolojia za Kilimo.** Mbinu ya utekelezaji wa ASDP II itakuwa ni "kila kanda iwe na zao/bidhaa moja ya kipaumbele"[37]. Mikoa itapangwa kwa makundi ili usambazaji wa huduma na mapendekezo ya teknolojia yaweze kuelekezwa kwenye mifumo ya uzalishaji na kaya sahihi za vijijini[38]. Utoaji wa huduma za umma utafikia wilaya zote na utaungwa mkono na miradi mingine ambayo inafadhiliwa na mashirika ya kimataifa, wafadhili na mashirika yasiyo ya kiserikali. Uratibu wa wilaya ulioanzishwa na ASDP I kupitia DADP utaboreshwa ikiwa ni pamoja na sekta binafsi.

70 **Vigezo vya kuchagua Ikolojia.** Uchaguzi wa Ikolojia na kongani utazingatia vigezo vitano kwa kuanzia na kiwango cha uzalishaji wa zao kwa kanda. Pia uchaguzi utazingatia uzalishaji mkubwa wa zao la kipaumbele kwa kufuata mnyororo wa thamani. Vilevile, uchaguzi utaangalia mahitaji muhimu ya soko kwa ajili ya malighafi na bidhaa zinazosindikwa katika mkoa na kanda. Vigezo vingine ni pamoja na uwezo uliopo wa usindikaji ndani ya kanda. Mifumo au mchango endelevu wa uzalishaji wa ndani, usalama wa chakula katika kaya na uzalishaji wenye tija kwa ajili ya kipato na ongezeko la thamani pamoja na maendeleo ya biashara- kilimo, masoko ili kuongeza mauzo ya nje ya bidhaa za kilimo.

71 **Vigezo vya kuchagua mnyororo wa thamani wa bidhaa.** ASDP II itazingatia mnyororo wa thamani wa bidhaa au mazao ya vipaumbele. Uteuzi wa mnyororo wa thamani utazingatia mchango wa zao au bidhaa husika kwenye usalama wa chakula na lishe na kuwasaidia wakulima wadogo. Pia utazingatia gharama nafuu na ukamilishaji wa miradi inayoendelea kwanza, ajenda ya maendeleo ya viwanda katika Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na soko la ndani pamoja na soko la nje.

## F. Uandaaji wa Vipaumbele na Dira

72 Kuwepo kwa vipaumbele ni muhimu ili kutumia fursa na kuongeza msukumo wa uwekezaji katika maeneo yenye kuleta tija. ASDP II inalenga kuwekeza kwenye mazao ya kipaumbele. Maeneo ya uzalishaji yataanzishwa kwa ajili ya mazao ya kimkakati kwa kila kanda ya kilimo. Jedwali Na. 7 na 8 yanaonesha uwezo wa kanda za mazao ya kipaumbele katika wilaya na mkoa. Uchaguzi wa zao au bidhaa utapitiwa kila mara na wadau wote wa mnyororo wa thamani katika Halmashauri na pia wakati wa mapitio ya mpango. Kuwepo kwa ikolojia za kilimo kutaongeza utoaji wa huduma muhimu za kiuchumi na kupata mahitaji ya pamoja ikiwa ni pamoja na miundombinu na pia kupunguza gharama. Kwa kila wilaya kutakuwepo na mikutano au majukwaa ya wadau ambayo yatajadili na kuamua bidhaa au zao la kipaumbele litakalotekelezwa kwa kufuata mnyororo wa thamani (mfano, wazalishaji, wafanyabiashara, wasindikaji na watoa huduma) katika wilaya husika. Mazao au bidhaa za kipaumbele za ASDP II ni kama vile mahindi, mchele, mtama na uwele, muhogo, mazao ya bustani, mazao ya mbegu za mafuta (alizeti, mawese, nazi, ufuta), pamba, kahawa, miwa, korosho, chai, viazi, maharage/kunde, ndizi, samaki, maziwa, nyama, mbuzi na kondoo, kuku na mwani. Mazao au bidhaa hizi zimechaguliwa kutokana na umuhimu na mchango wake kwenye usalama wa chakula, mbadala wa kuagizwa nje ya nchi na kwa ajili ya mauzo katika masoko ya ndani na nje.

73 Wakati wa ASDP I ilitumika mbinu ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo *(O&OD)* na kuibua miradi mbalimbali kuanzia ngazi ya kijiji. Kwa kutumia mbinu hiyo ya *O&OD* kwa kufuata mnyororo wa thamani, ASDP II itasaidia upatikanaji na utumiaji wa teknolojia zilizoboreshwa kama vile mbegu bora, mbolea, utumiaji wa matone na mashine za maji kwa ajili ya uzalishaji wa mazao, mifugo na uvuvi na pia kuwepo kwa miundombinu na huduma za biashara na masoko ya kilimo na kuongeza thamani. Ni muhimu kuihusisha sekta binafsi, ikiwa ni pamoja na kampuni na vyama vya ushirika ili kuimarisha upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima, usindikaji wa mazao na huduma za masoko. Kusaidia wakulima kutumia pembejeo bora kwa ufanisi na kuhamasisha utafiti na huduma za ushauri kwa gharama nafuu ni jambo la msingi pia. Kwa kufanya hayo kutachochoea tija na pato endelevu kwa mkulima. Kutakuwepo na upatikanaji mpana wa aina mbalimbali za mbegu bora na mbinu za kuongeza rutuba kwenye udongo kwa ajili ya kilimo endelevu. ASDP II italenga kudhibiti majanga, ikiwa ni

37 *Angalia zaidi Kiambatisho Na. 1 kwa ajili ya uendeshaji wa kongani*

38 *Angalia pia kaya za vijijini*

pamoja na yale yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi kusambaza teknolojia sahihi kwa ajili ya uzalishaji na kuongeza tija pia kuvutia wajasilimali vijana kwenye sekta ya kilimo

74 **Mbinu na zao la kipaumbele.** ASDP II itawekeza kwa kufuata maeneo ya kipaumbele kwa kuzingatia mnyororo wa thamani wa zao na bidhaa kwa kuzingatia mazao ya kipaumbele katika kila ikolojia. Kutokana na ufinyu wa rasilimali, siyo kila zao litaingia kwenye mpango wa ASDP II. Kutokana na uzoefu uliopatikana, maeneo na mazao ambayo hayataingia kwenye mpango yataongezwa kuanzia kipindi cha kati cha utekelezaji kwa kujumuisha wilaya tatu hadi sita katika maeneo ya kiikolojia kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa ikiwemo (i) Utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa kufuata mnyororo wa thamani kwa mazao au bidhaa zilizopo kwenye ASDP II; (ii) Kiwango cha uzalishaji na tija kwa kila zao linalotokana na mifugo,uvuvi na kilimo; (iii) Miundombinu (mf. barabara, reli, umeme[39] n.k) na masoko; (iv) Matokeo ya tathmini ya kila mchango wa zao na uwekezaji wake katika ngazi ya wilaya; (v) Historia ya nyuma ya mchango na ushiriki wa wilaya kwenye mipango mbalimbali ya maendeleo; (vi) Ushiriki wa sekta binafsi katika wilaya husika zinazosaidia mnyororo wa thamani wa bidhaa; na (vii) Kuzingatia mipango na miradi mingine inayoendelea katika wilaya husika (miradi kama vile *FTF, MIVARF, MUVI, TAFSIP*) ili kuepuka mrundikano wa miradi katika eneo moja yenye lengo moja.

## G. Misingi na Mbinu za uandaaji wa Programu ya ASDP II

75 **Mkakati wa ASDS** na uzoefu uliopatikana wakati wa utekelezaji wa awamu ya kwanza ya ASDP vimesaidia katika uandaaji wa ASDP II. Mapendekezo saba ya Maeneo yenye Matokeo ya Kimkakati ya ASDS yaliyomo ndani ya ASDP II yamewekwa kwenye makundi manne kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 9.

**Jedwali Na. 9: Maeneo ya kimkakati ya ASDS na utambuzi wa maeneo ya kipaumbele.**

| ASDS. Maeneo ya matokeo ya kimkakati | ASDP II. Maeneo ya mpango wa kipaumbele |
|---|---|
| 1.**Kukuza usimamizi wa matumizi endelevu ya maji na ardhi** kwa ajili ya mazao, mifugo na uvuvi pamoja na mifumo yenye kustahimili mabadiliko ya hali ya hewani kukuza umwagiliaji). | **P1: usimamizi wa matumizi endelevu ya maji na ardhi** kwa ajili ya mazao, mifugo na uvuvi pamoja na mifumo yenye kustahimili mabadiliko ya hali ya hewa. |
| 2. **Kuboresha tija na Faida kwenye sekta ya Kilimo** (mazao, mifugo na uvuvi),<br>kwa njia ya utafiti, ugani, upatikanaji wa pembejeo, na utumiaji wa zana za kilimo. | **P2. Kuboresha tija na faida kwenye sekta ya kilimo** (mazao, mifugo na uvuvi), usalama wa chakula na lishe bora |
| 3. **Kuimarisha na Kukuza ushindani wa minyororo ya thamani** (kuwezeshwa kwa vyama vya wakulima, kukuza kilimo-biashara na ongezeko la thamani, upatikanaji wa masoko na kuboresha miundombinu vijijini) | **P3. Biashara na uongezaji Thamani kwenye mazao** (upatikanaji wa masoko, kuongeza thamani, biashara na maendeleo ya sekta binafsi) |
| 4.**Kuimarisha Taasisi, viwezeshi na muundo wa uratibu imara** (mfumo wa sera, udhibiti na taasisi uliohamasishwa, uwezo wa kitaasisi, usimamizi wa maarifa na TEHAMA ulioimarishwa, usalama wa chakula na lishe, uratibu wa sekta umeboreshwa, ufuatiliaji na tathmini takwimu za kilimo ulioimarishwa) | **P4. Kuimarisha viwezeshi vya sekta**<br>(ikiwa ni pamoja na sera, usimamizi na mawasiliano na maarifa, TEHAMA, uratibu,ufuatiliaji na tathmini)<br>Kukuza na kuimarisha ushirikishwaji wa jinsia katika sekta ya kilimo. |

76 Malengo ya Mkakati wa ASDS yanafafanuliwa kama ifuatavyo: (1) Kukuza usimamizi endelevu wa

39 *Matumizi ya umeme vijijini ni kidogo kwani kaya zinazotumia umeme kwa ajili ya kuwashia taa na kupikia ni 20.7% na 1.7% (Sensa ya Watu na Makazi 2012).*

.

maji na ardhi (kwa ajili ya mazao, mifugo na uvuvi) na kukuza kilimo bora kinachohimili mabadiliko ya tabianchi; (2) Kuboresha tija na faida ya kilimo kwa kutilia mkazo utafiti bora, ugani, upatikanaji wa pembejeo na utumiaji wa zana; (3) Kuimarisha na kukuza ushindani wa maendeleo ya mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo (mazao, mifugo, uvuvi), kwa kuzingatia ushirika wa wakulima, kuboresha ongezeko la thamani na kuongeza upatikanaji wa masoko, fedha na miundombinu vijijini; na (4) Kuimarisha utendaji wa kitaasisi, viwezeshi (sera na mfumo wa udhibiti) na uratibu madhubuti wa taasisi za sekta za umma na binafsi katika sekta ya kilimo kwa ngazi za kitaifa na za mitaa.

77 Matokeo yote ya ASDS yaliyotarajiwa, yameandaliwa upya pamoja na maeneo manne ya mpango yaliyopendekezwa na kuboreshwa zaidi kwa kupitia timu na warsha ya majadiliano. Maeneo mtambuka ya sekta pia yamejumuishwa, kama vile: (i) Usawa wa kijinsia pamoja na uwiano sawa wa ushiriki wa wanaume na wanawake katika maendeleo ya kilimo; (ii) Ajira binafsi kwa vijana wa vijijini; (iii) Kupunguza maambukizi ya VVU/UKIMWI na athari zake, (iv) Utawala bora na uwajibikaji.

78 Uwekezaji wa umma/maeneo katika maeneo wezeshi yaliyopendekezwa yametambuliwa. Maeneo hayo ni (i) Utafiti; (ii) Mafunzo ya ugani, huduma za habari na usimamizi wa maarifa; (ii) Vyama vya wakulima / wadau; (iii) Upatikanaji wa pembejeo; (iv) Miundombinu ya vijijini; (v) Upatikanaji wa fedha za vijijini; (vi) Mfumo wa sera na udhibiti; na (vii) Uratibu, ufuatiliaji na tathmini. Kwa kutumia mfumo wa wadau wa umma na wadau wasio wa kiserikali walitambua kipaumbele uwekezaji/hatua za msaada (kikundi cha shughuli) kuwezesha kufikia matokeo yaliyotarajiwa kwa njia zilizopendekezwa, katika kila ngazi ya kitaifa na Halmashauri (ikiwa ni pamoja na ngazi ya mkoa kukidhi mahitaji ya uratibu).

79 Kwa kuzingatia majadiliano ya kina na wadau muhimu wa sekta ya umma na binafsi, ASDP II imejengwa kwenye vipaumbele vinne: (P1) Usimamizi wa matumizi endelevu ya maji na ardhi (mazao, mifugo na uvuvi); (P2) Kuimarisha tija na faida; (P3) Biashara na uongezji wa thamani kwenye mazao (kujenga minyororo ya thamani yenye ushindani); na (P4) Kuimarisha viwezeshi na uratibu wa sekta (ngazi za kitaifa, kikanda na halmashauri). Mabadiliko makubwa ya uwekezaji yalikuwa ni kuongeza vipengele kwa ajili ya kuimarisha sera, usalama wa chakula na lishe, uimarishaji wa uwezo, uratibu na ufuatiliaji na tathmini.

80 Hatua za kipaumbele zilijadiliwa kwa kina, na bajeti zinazohusiana zilikadiriwa na kulinganishwa na uwekezaji wa sasa wa bajeti ya maendeleo, hasa katika ngazi ya kitaifa na makadirio ya uwekezaji wa DADP ngazi ya Halmashauri yamezingatiwa. Ingawa sehemu kubwa ya mapendekezo ya uwekezaji yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ASDP II imebainisha maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji kama kichocheo muhimu cha ukuaji wa sekta ya kilimo na kupunguza umaskini vijijini. Vichocheo muhimu kwa utekelezaji wa ASDP II (na mabadiliko ya kipaumbele dhidi ya ASDP-1) yanafupishwa kama ifuatavyo:

a. **Uongozi bora na mabadiliko ya kifikra** katika ngazi zote kutasaidia ukamilishaji wa mpango.

b. Uratibu wa sekta nzima (upangaji wa sekta nzima unaozingatia matokeo, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini) ikiwa ni pamoja na mipango yote ya "bidhaa za umma" na miradi katika sekta ya kilimo ngazi ya taifa na Halmashauri (i) katika ngazi ya kitaifa, ufanisi wa uratibu ndani ya ASLM na katika mifumo ya kiserikali pamoja na mipango na miradi ya msaada wa sekta na utazingatiwa (ii) katika ngazi ya halmashauri, kwa njia ya mifumo shirikishi ya upangaji / utekelezaji, kujenga uwezo na uwekezaji makini;

c. **Dhamira ya uwekezaji katika Halmashauri inayolenga minyororo ya thamani** ya bidhaa za kipaumbele na usawa bora kati ya sekta ndogo kulingana na faida zao za kulinganisha katika kila Kanda ya Kilimo ya Kiikolojia na kuzingatia uungwaji mkono wa makundi katika wilaya, kwa kiwango cha juu na cha chini (vigezo vya kipaumbele) na kufafanuliwa kwa awamu. ASDP II itaongeza uwekezaji hatua kwa hatua katika ngazi ya Halmashauri. Hiyo itategemea kanuni za: (i) Kudumisha mipango shirikishi / mifumo ya utekelezaji na kuimarisha uwezo kwa wafanyakazi; (ii) Kutekeleza uwekezaji wa umwagiliaji (chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji katika ngazi ya wilaya) tayari umejulikana kwa kiasi kikubwa kwa miaka mitano ijayo chini ya ASDP II na kukamilisha palipoachwa na ASDP-1;

(iii) Kuimarisha uwekezaji katika upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo cha mifugo na uvuvi[40]; na (iv) Kutekeleza uwekezaji wa DADP uliozingatia kwa karibu mnyororo wa kipaumbele wa thamani katika makundi yaliyochaguliwa na kusambazwa kwa ajili ya mifugo.

d. Kwa upande wa mifugo, kuimarisha ufugaji wa ng'ombe wa nyama/ng'ombe wa maziwa kunahitaji matumizi zaidi ya mifugo bora inayostahimili mifumo muhimu iliyopo ikiwa ni pamoja na kilimo cha uchungaji au ufugaji. Uzalishaji mkubwa utategemea pia na mambo mengine kama kudhibiti magonjwa, ambayo yanahitaji kuimarisha uwezo wa kugundua magonjwa (huduma za uchunguzi wa maabara ya mifugo) na upatikanaji wa chanjo.

e. Eneo muhimu la uwekezaji linalotambuliwa kama kichocheo kikubwa cha sekta na unufaikaji na ukuaji mkubwa wa msaada wa bajeti, ni pamoja na: (i) Umwagiliaji unabakia kuwa kipaumbele kama vile ilivyoelezwa katika ASDP II; (ii) Uhusiano wa utafiti na huduma za ugani, ikiwa ni pamoja na utafiti unaofaa wa kanda/wilaya (iii) Upatikanaji wa ujuzi wa kiufundi (teknolojia bora) kwa wakulima, kupanua mitandao ya sekta binafsi ya usambazaji wa pembejeo (mbegu/mbegu bora za mifugo/ vifaranga vya samaki, mbolea, vyakula, madawa ya mifugo na chanjo, nk); (iv) Upatikanaji mkubwa wa huduma za ushindani wa utumiaji zana kwa ajili ya uzalishaji na usindikaji baada ya mavuno/kuongeza thamani; (v) Kupungua kwa upotevu wa mazao na mifugo baada ya mavuno (vifo vya ndama); (vi) Kutoa huduma maalum za sekta za biashara za kilimo kwa ngazi ya kikanda na (vii) Uwezo wa kutambua wadudu/ vimelea na upatikanaji wa chanjo bora.

f. Matumizi ya teknolojia ya kisasa ya habari na mawasiliano kwa ufanisi wa uratibu, ukusanyaji wa takwimu, usindikaji, usambazaji, wadau kupata mtiririko wa habari za mahitaji na usambazaji (yaani, kiufundi, masoko, ufuatiliaji na tathmini).

g. Uwezeshaji wa wakulima na uimarishwaji wa mashirika ya wakulima ili kuimarisha ushiriki na umiliki wa maendeleo ya vijijini, kuelekea kwenye uboreshaji wa hali ya maisha, ikiwa ni pamoja na kuimarisha vyama vya uchumi vyama vya ushirika, kuimarisha habari za ndani na huduma za kiufundi kwa wanachama wao.

h. Kuimarisha mifumo endelevu ya uzalishaji na matumizi ya maliasili kwa kukuza kilimo cha uhifadhi wa mazingira, usimamizi wa maji na rutuba ya udongo (mifumo ya afya ya udongo), udhibiti wa wadudu, mifugo, kutunza mifugo kulingana na uwezo wa ardhi, nk.

i. **Matumizi ya tathmini ya matokeo na athari ngazi ya sekta** kwa kutumia huduma za kitaifa za takwimu za kilimo kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa ajili ya utekelezaji wa Sensa ya Taifa ya Kilimo na Mifugo (inayofanywa kila baada ya miaka 10) na sensa ya kilimo ya kila mwaka (AASS) na kuhakikisha uchambuzi wa taarifa kwa wakati;

j. **Usaidizi wa kuimarisha sera na kanuni ili** kuwezesha uoanishaji na ushiriki mkubwa wa sekta binafsi na msaada endelevu wa kuimarisha sera za kupeleka madaraka kwa wananchi na uwezo wa ngazi ya halmashauri na umilikaji wa sera hizo ili zieleweke na kuweza kupata msaada wa wadau.

k. **Kuhuisha njia za utoaji fedha na usimamizi** wa kuunganisha kwenye bajeti na mpango mbalimbali nje na ndani ya bajeti. Shughuli za msingi katika programu kama vile uratibu (mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini), kuimarisha uwezo katika ngazi ya kitaifa na za mitaa itahitaji kufadhiliwa kupitia mfuko wa pamoja (michango ya serikali na mashirika ya maendeleo ) na /au michango ya hiari (mfano, asilimia 5) itachangiwa kutoka kwenye programu (ndani na nje ya bajeti) na kila mradi katika sekta hiyo.

l. **Miundo, mifumo, michakato na taratibu za utawala, uwajibikaji na usimamizi.** Kuna ulazima wa kuwa na majukumu yanayoeleweka na mamlaka katika ngazi zote, na mifumo ya uwajibikaji.

40 *Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo (2011) imeanisha maeneo ya kipaumbele yafuatayo: (i) Miundombinu ya mifugo; (ii) Undelezaji wa nyanda za malisho na maji kwa ajili ya mifugo; (iii) Uzalishaji wa mbegu za malisho; (iv) Utafiti wa mifugo, mafunzo na huduma za ugani; (v) Kuboresha mifugo na kuku ; (vi) Udhibiti wa magonjwa na kuanzisha ukanda huru kwa magonjwa ya mifugo; (vii) Upatikanaji na utumiaji wa pembejeo (viii) Mazingira wezeshi kwa ajili ya uwekezaji wa sekta binafsi; na (ix) Takwimu na taarifa za masoko ya mifugo*

## H. Nadharia ya Mageuzi.

81 **Kutatua changamoto za ASDP 1.** Programu ina maeneo manne makuu na miradi kadhaa ya kutekelezwa kwa miaka mitano. Lengo hilo litafikiwa kwa kuweka vipaumbele, makundi (tabaka) na mpangilio wa shughuli na miradi. Njia iliyochaguliwa na Serikali ni kutekeleza miradi kwa kutoa matokeo na kuleta mabadiliko chanya. Serikali itaweka mazingira wezeshi yanayohitajika kwa kutekeleza sehemu ya nne ikifuatiwa na ya tatu, ya pili na ya kwanza. Mpangilio huo utatekelezwa kama ifuatavyo-

i. Kutatua changamoto nyingi za ASDP I,
ii. Kujenga mazingira wezeshi kwa ajili ya vipengele vingine kufanya kazi hasa ajenda ya viwanda na ongezeko la thamani (mahitaji na usambazaji) na
iii. Kufungamanisha vipengele na miradi kulingana na vipaumbele.

Hata hivyo, kipaumbele hiki hakitaathiri utekelezaji wa mipango mingine. Hii ina maana kuwa mipango inaweza kutekelezwa kwa mpangilio au kwa pamoja. **Kielelezo Na. 14** kinaonesha vipaumbele na nadharia ya mabadiliko.

**Kielelezo 14: Nadharia ya Mageuzi**




Pia Programu itazingatia uwekezaji wa ndani unaolenga minyororo ya thamani ya bidhaa za kipaumbele kulingana na faida ya ulinganishi kwenye kila eneo la ikolojia kwa kuzingatia kongani (kongani ya wilaya[41]).

82 **Mpango, mpangilio na Ratiba ya utekelezaji wa ASDP II.** Ili kutekeleza ASDP II, maeneo makuu ya Programu na miradi yamepangwa kwa mpangilio na ratiba ambayo itajenga na kuleta mabadiliko pamoja na matokeo makubwa. Utekelezaji wa programu, mpangilio, upangaji ratiba utahusisha umuhimu wa maeneo makuu na miradi ambayo itatatua changamoto za sekta, itatumia fursa na kuleta mabadiliko chanya. Pia, kuna haja ya kutekeleza miradi ambayo itajenga mazingira wezeshi ("kuzibua

41 *Wilaya zenya bidhaa zinazofanana katika kanda ya kiikolojia ya Kilimo zitandaa mnyororo wa thamani wa bidhaa unaofanana*

bomba ili kuruhusu maji yatiririke"). Utekelezaji utaanza na eneo kuu la 4 ambalo litajenga mazingira wezeshi kwa ajili ya sekta binafsi na umma ikiwa ni pamoja na wakulima wadogo. Maelezo ya kina ya mipango, mpangilio na ratiba ya utekelezaji yanapatikana kwenye **Kiambatisho Na. I.**

## IV: MALENGO NA MAELEZO YA PROGRAMU YA ASDP II

83 Awamu ya Pili ya Programu ya ASDP (2017/2018- 2027/2028) imeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Taswira ya Muda Mrefu (LTPP)[42], Mpango wa Maendeleowa Taifa wa Miaka Mitano, MKUKUTA, Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDS) na Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka (2015-2020). Awamu hii ya Programu pia imezingatia yaliyotokana au kujifunza katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya ASDP na ASDS, kupanua na kuimarisha wigo wa utekelezaji na uendeshaji kwa kuzingatia uratibu na mfuatano maalum wa vichocheo vya ukuaji wa sekta na mabadiliko kuelekea katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini vijijini. Kwa kuzingatia mafunzo yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa awamu ya kwanza na kuunganisha na malengo ya kitaifa na kimataifa, muundo wa jumla wa mnyororo wa matokeo umeelezwa katika **Kielelezo Na. 15.**[43]

**Kielelezo Na. 15: Muundo wa Mnyororo wa Matokeo ya ASDP II**




**Kielelezo 16: Lengo, Mkakati na Matokeo ya ASDP II**

**Lengo:** *Kuleta mageuzi kwenye sekta ya kilimo (kilimo, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija, kufanya kilimo kiwe cha kibiashara zaidi na kuongeza pato la wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha yao, usalama wa chakula na lishe.*

**Mkakati:** Kufanya mageuzi kwa wakulima wadogo kutoka kilimo cha kujikimu kwenda kilimo endelevu cha kibiashara kwa kuendeleza na kuamsha vichocheo vya sekta na kuwezesha wakulima wadogo kuongeza tija katika mazao ya kipaumbele (kilimo, mifugo, uvuvi) katika mfumo endelevu wa uzalishaji na kuunganishwa na masoko endelevu kwa ushindani wa kibiashara na uendelezaji wa mnyororo wa thamani wa zao.

**Matokeo:** Kuongezeka kwa uzalishaji na tija, kuwepo kwa masoko, kuongezeka kwa thamani ya mazao, usalama wa chakula na lishe na kuongezeka kwa kipato cha mkulima na pato la Taifa.

42 *Mpango wa Muda Mrefu wa Maendeleo ya Taifa umeanisha maeneo yatakayotekelezwa kwa vipindi vya miaka mitano mitano (2011/2012–2025/2026). Miaka mitano ya kwanza ililenga katika kuondoa vikwazo vya kukua kwa uchumi; miaka mitano ya pili inalenga katika kujenga uchumi wa viwanda na miaka mitano ya mwisho inalenga kuongeza biashara ya bidhaa za viwandani nje ya nchi.*

43 *Imetoholewa kutoka ASDS*

## A. Lengo la Programu

84 **Lengo la ASDS.** Kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, Lengo kuu la Sekta ni "kuchangia katika ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini vijijini na kuboresha usalama wa chakula na lishe nchini Tanzania". Malengo na Mikakati muhimu ya ASDS ni: (i) Kuandaa mazingira wezeshi ya kisera na kitaasisi kwa ajili ya kuimarisha ushindani wa kisasa katika sekta ya kilimo, ikichochewa na ujumuishi na uimairishaji wa ushiriki wa sekta binafsi; (ii) Kufikia ongezeko endelevu katika uzalishaji, tija, faida na ushindani katika uendelezaji wa mnyororo wa thamani kwenye sekta ya kilimo unaochagizwa na wakulima wadogo; na (iii) Kuimarisha utendaji na uratibu wa taasisi husika za umma na sekta binafsi kwenye sekta ya kilimo katika ngazi za Taifa na Wilaya, inayowezeshwa na kuimarika kwa ustahimilivu.

85 ASDS inalenga kufikia shabaha zifuatazo ifikapo 2024/2025; (i) ukuaji jumuishi na endelevu wa sekta ya kilimo kwa 6% kwa mwaka, (ii) kupunguza umaskini vijijini kutoka asilimia 33.3 mwaka 2011/2012 hadi 24 mwaka 2025, na (iii) kuimarisha usalama wa chakula na lishe kutoka asilimia 11.3 katika mwaka 2011/2012 hadi 5 ifikapo mwaka 2025.

86 **Malengo ya Maendeleo ya ASDP II**[44]. Lengo la ASDP II ni: kuleta mageuzi ya sekta ya kilimo (mazao, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija, kufanya kilimo kiwe cha kibiashara na kuongeza pato la wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha yao, uhakika wa usalama wa chakula na lishe, Kielelezo Na.17 hapa chini kinaonesha jengo la ASDP II na lengo kuu kama 'paa' la jengo, 'kuta zinawakilisha maeneo makuu1, 2,3,4 katika msingi wa ujenzi.

**Kielelezo Na. 17: Lengo la ASDP II na Maeneo Makuu ya utekelezaji**




44 *ASDP II ni programu ya miaka 10 itakayotekelezwa kuanzia mwaka 2017/2018 hadi mwaka 2027/2028*

**Kielelezo Na. 18: Maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji wa ASDP II**

| Eneo Kuu 1: Usimamizi endelevu wa matumizi ya Maji na Ardhi | Eneo Kuu 2: Uongezaji wa Uzalishaji na Faida katika sekta ya Kilimo | Eneo Kuu 3: Biashara na Uongezaji Thamani kwenye Mazao |
|---|---|---|
| 1. Mpango wa matumizi ya ardhi na usimamizi wa vyanzo/ machanuo ya maji<br>2. Kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji<br>3. Usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji<br>4. Kuendeleza vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo na uvuvi<br>5. Kuhamasisha teknolojia za kilimo hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi | 1. Kuimarisha huduma za Ugani wa Kilimo na mafunzo na uhamasishaji wa teknolojia za kilimo (mazao, mifugo na uvuvi)<br>2. Uboreshaji wa Upatikanaji wa pembejeo za mazao, mifugo na uvuvi pamoja na huduma za afya katika mazao, mifugo na uvuvi<br>3. Kuimarisha Utafiti na maendeleo ya mazao, mifugo na uvuvi<br>4. Kuimarisha na kuhamasisha matumizi ya zana za kilimo (mazao, mifugo na uvuvi)<br>5. Kuimarisha Usalama wa chakula na lishe | 1. Kuendeleza upatikanaji wa soko kwa bidhaa zote za kipaumbele<br>2. Kukuza upatikanaji wa soko kwa ajili uvuvi na bidhaa za mifugo.<br>3. Kuendeleza usindikaji na kuongeza bidhaa zitokanazo na mazao, mifugo na uvuvi |
| **Eneo Kuu 4: Kuimarisha Mazingira wezeshi ya Sekta, Uratibu na Ufuatiliaji na Tathimini** | | |
| 1. Kuboresha Sera na Mfumo wa Usimamizi na Mazingira ya Biashara<br>2. Kuimarisha miundo na uwezo wa kitaaluma kwa vikundi na vyama vya ushirika vilivyopo na vipya vya wazalishaji, wafanyabiashara na wasindikaji wadogo<br>3. Kuhamasisha na kuimarisha ushirikishwaji wa wanawake na vijana katika sekta ya kilimo<br>4. Kuboresha na kuimarisha uratibu wa wima (kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI kwenda RSs na Halmashauri za Mitaa) na uratibu kati ya ASLMs | 5. Kuboresha uwezo na usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji na utunzaji wa takwimu za sekta ya kilimo<br>6. Kuboresha uwezo na mifumo ya usimamizi<br>7. Kuweka mifumo imara ya ufuatiliaji na tathmini katika sekta ya kilimo<br>8. Kuboresha uwezo wa kitaasisi katika ngazi zote<br>9. Kuboresha TEHAMA kwa ajili ya huduma na mifumo ya taarifa za sekta ya kilimo<br>10. Kutoa huduma za mikopo midogo katika sekta ya kilimo | |

87 Mkakati ni kubadilisha wakulima wadogo kutoka katika kilimo cha kujikimu na kwenda kwenye kilimo endelevu cha kibiashara kwa kuimarisha na kuamsha vichocheo vya sekta na kusaidia wakulima wadogo kuongeza uzalishaji wa mazao ya kipaumbele ndani ya mifumo endelevu ya uzalishaji na uunganishwaji katika masoko kwa ajili ya kuimarisha ushindani na uendelezaji wa mnyororo wa thamani.

88 Malengo ya Maendeleo kwenye sekta ya kilimo yatapimwa kwa viashiria vya awali vifuatavyo[45]:

(i) Ukuaji wa sekta ya kilimo (mazao, mifugo na uvuvi)

(ii) Tofauti ya wastani wa uzalishaji wa mazao yaliyolengwa (mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi) kwa mwaka

(iii) Tofauti ya kipato kinachotokana na mazao, mifugo/uvuvi kwa wanufaika (wanaume/ wanawake/ vijana)

(iv) Wastani wa bei ya mlaji anayopata mkulima kutokana na wastani wa bei ya shambani (halisi) katika mazao ya kipaumbele.

(v) Tofauti katika ujazo na thamani ya mapato yote ya mauzo katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kipaumbele

(vi) Tofauti katika kiasi cha chakula (na lishe) kwa kaya zisizo salama katika maeneo yaliyohifadhiwa (wastani wa alama za mlo kamili kwa kaya) ikilinganishwa na maeneo mengine

(vii) Idadi ya wanufaika (au asilimia ya makundi ya kijamii na jinsia)

(viii) Kuongezeka kwa kiasi cha mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi

(ix) Kuongezeka kwa pato la mkulima (kwa kaya za vijijini)

45 *Hivyo ni baadhi ya viashiria: Mfumo wa matokeo umeoneshwa kwa kina katika Kiambatisho Na. II (Mfumo wa matokeo na tathmini). Viashiria hivyo vitawekwa katika makundi kijinsia pale itakapowezekana.*

89 **Lengo la Programu:** Programu imejikita katika uwekezaji wa umma unaokabiliana na changamoto za uzalishaji na kuimarisha vichocheo vya kipaumbele ili kuongeza tija endelevu katika uzalishaji na faida kwa wakulima kwa kuzingatia mnyororo wa thamani wa mazao ya kipaumbele katika makundi ya wilaya zilizochaguliwa na kuimarisha uwezo wa kitaasisi katika sekta za umma na sekta binafsi (majukwaa) hususan katika ngazi ya wilaya. Programu itajikita katika mazao makuu ya kipaumbele yenye tija katika uzalishaji kulingana na maeneo yaliochaguliwa na itaendelezwa katika mazao mengine kulingana na makundi ya wilaya na ikolojia ya kanda za kilimo, kwa kuzingatia kipaumbele cha mnyororo wa thamani wa mazao, kama ilivyoainishwa katika sehemu ya III (E na F). Programu itazingatia kuongeza mapato na faida ya mifumo ya uzalishaji, ikilenga kusaidia kuimarisha mnyororo wa thamani wa mazao ya kipaumbele, kwa kutilia mkazo ujenzi wa ushirikiano wa kibiashara kati ya wakulima wadogo, masoko na biashara kilimo. Hii itahusisha utekelezaji utakaosaidia kuleta mageuzi kwa wakulima wadogo ili wazalishe kwa kulenga masoko (kibiashara ) kwa kuongeza uzalishaji na tija endelevu. Itahusisha pia ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuongeza thamani ya mazao katika ngazi za chini kwa kuboresha ufanisi katika masoko ili kuongeza ukuaji wa kipato kwa kujumlisha matokeo ya hatua mbalimbali kama vile kuhifadhi katika maghala na usindikaji katika kilimo. Maeneo muhimu ya uwekezaji katika ngazi ya Kitaifa na Halmashauri ni pamoja na miundombinu, huduma za ugani, uwezeshwaji wa mkulima[46] na wadau wengine na taasisi zao, uimarishaji wa uwezo, mageuzi ya sera na kisheria na kuimarisha taasisi zinazotekeleza program kutokana na kuimarika kwa uratibu na kuunganishwa kwa ufuatiliaji na tathmini ya sekta ya kilimo katika ngazi mbalimbali.

**Wanufaikaji** ni pamoja na wakulima wadogo wa mazao, mifugo na wavuvi, vyama vyao na mashirika yao pamoja na wadau wa kilimo biashara (kuongeza thamani na soko) ambao hutengeneza ubia katika minyororo ya thamani ya mazao ya kipaumbele kwa kuzingatia ushiriki wa wanawake na vijana katika mnyororo wa thamani wa zao la kupaumbele. Wakulima wadogo wenye uwezo wa kuongeza uzalishaji na mauzo ya mazao yao watasaidiwa katika upatikanaji wa teknolojia, kujengewa uwezo kupitia vyama vya ushirika ili wazalishe kulingana na mahitaji ya soko na kuunganishwa na wadau mbalimbali wa kilimo biashara. Idadi ya wanufaika wa moja kwa moja watakua katika makundi, na taasisi za wadau zitaimarishwa na kuwa msaada endelevu wa misingi muhimu ya vichocheo vya sekta.

**Jedwali Na. 10: Uainishaji wa kaya za vijijini zinazojihusisha na shughuli za kilimo**

| Ukubwa wa Eneo (ha) | Mazao tu | | Mifugo | | Mazao na Mifugo | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya kaya | % | Idadi ya kaya | % | Idadi ya kaya | % | Idadi ya kaya | % |
| A. 0.01–0.50 | 484,585 | *14* | 47,773 | *80* | 181,083 | *8* | 713,441 | *13* |
| B1. 0.51–1.25<br>B2. 1.26–2.50 | 1,045,293<br>1,191,939 | *31*<br>*35* | 4,198<br>2,352 | *7*<br>*4* | 481,164<br>720,494 | *22*<br>*32* | 1,530,656<br>1,914,786 | *27*<br>*34* |
| C. 2.51–5.00<br>D. Zaidi ya 5.00 | 493,775<br>206,481 | *14*<br>*6* | 2,059<br>3,463 | *3*<br>*6* | 482,001<br>359,670 | *22*<br>*16* | 977,833<br>569,614 | *17*<br>*10* |
| **JUMLA** | **3,422,072** | ***100*** | **59,845** | ***100*** | **2,224,411** | ***100*** | ***5,706,329*** | ***100*** |

Chanzo: Sensa ya Kilimo Tanzania 2007/2008

90 Programu itahusisha wazalishaji wanaozalisha kulingana na mahitaji ya soko lililo tayari (kundi C na D, katika Jedwali Na. 10), na kusaidia kujenga uwezo wa uzalishaji na upatikanaji wa soko katika kundi B, lenye theluthi mbili ya jamii ya wakulima. Kundi A linawakilisha sehemu ya wakulima wadogo, hasa wakulima wanaozalisha kwa ajili ya kujikimu, ambao wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa ardhi na wafanyakazi wa mashambani. Kama wanunuzi wakubwa wa chakula, kundi hili lina uwezo mdogo wa uzalishaji kwa ajili ya soko (isipokuwa kwa kilimo cha mboga na matunda) na linahitaji kuungwa mkono na programu nyingine za maendeleo ya kijamii (kama vile, TASAF) na pia kwa njia ya kujenga uwezo wa kitaalam, hususan kwa vijana, kwa kuwaweka katika makundi mengine ya kiuchumi ya vijijini na Mjini.

46 *Wakulima ni pamoja na wakulima wa mazao,wafugaji na wavuvi .*

91 Mtizamo, vihatarishi juu ya athari mbalimbali na sifa za uwekezaji kwa wakulima wadogo wa kibiashara (zaidi ya eneo la hekta 1.0 lililopandwa) unakaribia theluthi mbili ya kaya za wakulima vijijini ni tofauti na wale walio na eneo dogo. Kimsingi, wao huuza angalau theluthi moja ya mazao wanayozalisha na kutafuta fursa za kuongeza kipato kutokana na mashamba yao kwani wao tayari wanalenga kupata faida, kwa kuchukua tahadhari. Zaidi ya hayo, matumizi yao ya nguvu kazi katika upatikanaji wa huduma na bidhaa huongeza ajira vijijini kipato na usalama wa chakula kwa familia zisizokuwa na mashamba vijijini.

92 Maeneo Makuu ya Programu. Programu ina maeneo makuu manne yanayotegemeana (tazama Kielelezo Na.19): (i) Usimamizi wa Matumizi Endelevu ya Maji na Ardhi, ikiwa ni pamoja na kuwezesha ustahimilivu wa kilimo hifadhi na endelevu; (ii) Kuongeza tija na faida ya kilimo kwa kuzalisha, kukuza /kutumia teknolojia endelevu, usalama endelevu wa chakula na lishe; (iii) Biashara na Uongezaji Thamani kwenye mazao ili kujenga minyororo ya thamani ya bidhaa yenye ushindani; na (iv) Kuimarisha Mazingira Wezeshi, Uratibu na Ufuatiliaji na Tathmini katika sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na mifumo ya sera, uwezo wa taasisi na uratibu, pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya sekta nzima.

**Kielelezo Na. 19: Maeneo Makuu na vipaumbele vya ASDP II**



## B. Maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji (muhtasari)

93 Ili kuongeza tija ya mazao, mifugo na uvuvi kwa wakulima uwekezaji ni kipaumbele cha kwanza katika kuongeza fursa za kibiashara ndani ya mfumo wa matumizi endelevu ya maliasili. Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za utafiti na maendeleo, huduma za ugani, umwagiliaji, maji kwa ajili ya mifugo, maeneo ya malisho, zana na kuboresha upatikanaji wa pembejeo za mazao/mifugo / uvuvi kutachochea juhudi za kuongeza tija katika sekta. Uwekezaji katika kujenga uwezo wa taasisi na miundombinu vijijini (barabara, umeme, vifaa) utahitajika ili kuongeza upatikanaji wa masoko na kuhakikisha huduma bora kwa ajili ya mabadiliko ya sekta. ASDP II pia inajumuisha maeneo mahsusi ya utekelezaji ili kuboresha hali ya usalama wa chakula na lishe katika kaya vijijini na kuboresha ustahimilivu wa mifumo ya hali ya maisha ya vijijini ili kupunguza madhara ya majanga ya asili, ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

94 Katika kuchochea ukuaji wa sekta ya kilimo ili kufikia kiwango kinachotarajiwa cha **asimilia 6** kwa mwaka, uwekezaji wa Sekta ya umma na binafsi unahitajika. Matokeo bora katika suala la ukuaji wa uchumi, usalama wa chakula na kupunguza umaskini yanaweza kupatikana iwapo kutakuwa na uwiano sawa wa uwezeshwaji kwa sekta ndogo zote za kibiashara na wakulima wadogo, zinazolenga bidhaa kuu ambazo zinazalishwa na kutumika kwa kiasi kikubwa na wakazi, pamoja na juhudi za kusaidia wakulima wadogo kuelekea katika safu ya wakulima wa kilimo kidogo cha kibiashara. Shughuli za uwekezaji kwenye ASDP II zimewekwa kwenye makundi katika maeneo husika ya programu pamoja na maeneo makuu na madogo. Taswira ya maeneo ya uwekezaji ya kipaumbele ya kimkakati iko katika **Jedwali Na. 11**

**Jedwali Na. 11: Maeneo Makuu na malengo ya kimkakati ya ASDP II**

| Maeneo makuu ya Programu | Uwekezaji wa kimkakati wa kipaumbele |
|---|---|
| **Eneo Kuu 1:** Usimamizi wa Matumizi Endelevu ya Maji na Ardhi | Usimamizi wa matumizi endelevu ya maji na ardhi na ongezeko la ustahimilivu (umwagiliaji, mabwawa na visima, mipango ya matumizi ya ardhi, udongo rutuba usimamizi, malisho maendeleo, madimbwi / mabwawa) |
| **Eneo Kuu 2:** Kuimarisha Tija na Faida katika kilimo | Kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa tija kwa ajili ya masoko ya kilimo-biashara ya bidhaa za kipaumbele (minyororo ya thamani ya mazao, mifugo na uvuvi) |
| **Eneo kuu 3:** Biashara na Kuongeza Thamani (kujenga mnyororo wa thamani wenye ushindani) | Kupanua upatikanaji wa kuongeza thamani na mifumo ya masoko ya ushindani vijijini kwa wakulima kwa ajili ya minyororo ya thamani ya bidhaa, inayoendeshwa kwa kujumuisha, kuimarisha na kuendeleza sekta binafsi na mashirika ya wakulima wenye ufanisi. |
| **Eneo Kuu 4:** Kuimrisha Mazingira Wezeshi ya Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini | Mfumo wa sera na usimamizi<br>Kuimarisha uwezo wa taasisi na usimamizi wa maarifa.<br>Usalama wa chakula na lishe (ikiwa ni pamoja na kutoa tahadhari mapema na njia salama<br>Uratibu (kuwezesha kupanga na utekelezaji katika ngazi zote)<br>Ufuatiliaji na tathmini (ikiwa ni pamoja na takwimu za kilimo) |

95 Utekelezaji na uwekezaji kwenye vipaumbele katika kanda za kilimo za kiikolojia na kongani za kiwilaya. Programu italenga: (i) Kurejesha msingi wa fedha za kujenga uwezo na huduma za ugani katika sekta ya kilimo, kuandaa uwezo wa wafanyakazi na taasisi ili kuendeleza uwekezaji wa sekta; na (ii) Uwekezaji wa hatua kwa hatua kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa za kipaumbele katika kanda za kilimo za kiikolojia. Aidha, Programu italenga katika uwekezaji ambao utakabiliana na vikwazo na kuongeza kutambuliwa kwa viwezeshi katika kukuza tija endelevu na ukuaji wa faida kwa wakulima. Programu italenga katika mnyororo wa thamani wa bidhaa zenye fursa kubwa katika kanda za kilimo za kiikolojia. Kanda za kilimo za kiikolojia[47]na wilaya zitakazoshiriki katika utekelezaji wa ASDP II zinaonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 12:**

47 *Bidhaa za kipaumbele kwa kila Kanda ya Ikolojia za Kilimo ni kama inavyoonekana kwenye Majedwali Na. 7, 8 na 21*

**Jedwali Na. 12: kanda za kilimo za kiikolojia (AEZ) na wilaya zitakazoshiriki katika ASDP II**

| | Kanda Za Kiikolojia - AEZ | Mkoa | Wilaya |
|---|---|---|---|
| 1 | Nyanda kame (aina moja 400-900 mm ) | Mara (E) | Musoma (M), Musoma (V), Serengeti, Bunda, Tarime, Rorya |
| | | Dodoma (E) | Masai Steppe, Tarangire, Mkomazi, Pangani na Dodoma Mashariki |
| | | Simiyu | Bariadi, Maswa, Meatu, Itilima, Busega |
| | | Manyara (E) | Kiteto, Simanjiro |
| 2 | Pwani ya mashariki | Lindi | Lindi (V), Lindi (M), Liwale, Ruangwa, Kilwa, Nachingwea. |
| | | Mtwara | Mtwara (M), Mtwara (V), Masasi, Nanyumbu, Tandahimba, Newala |
| | | Tanga | Handeni, Kilindi, Korogwe (V), Lushoto, Muheza, Mkinga, Pangani, Tanga, Korogwe |
| | | Pwani | Kibaha (M), Kibaha (V), Bagamoyo, Mafia, Mkuranga, Kisarawe, Rufiji |
| | | Dar-es-Sal. | Ilala, Kinondoni, Temeke |
| 3 | Nyanda za juu Kaskazini (aina mbili) | Arusha (S) | Arusha (V), Meru, Arusha (M), Karatu, Monduli, Longido, Ngorongoro |
| | | Kilimanjaro (N) | Moshi (V)., Hai, Siha, Moshi (M), Mwanga, Rombo, Same |
| | | Manyara (E) | Babati (M), Babati (V) , Hanang, Mbulu |
| 4 | Miinuko (wa aina moja) | W: Tabora, Rukwa/Katavi | Tabora (M), Igunga, Nzega, Sikonge, Tabora (Uyui, Urambo<br>Mpanda (V), Mpanda(M ), Mlele |
| | | Mbeya (N) | Chunya (N) |
| | | Ruvuma + Morogoro (S) | Songea (M), Songea (V), Namtumbo, Mbinga, Tunduru, Ulanga (Mo) |
| | | Mwanza | Mwanza (J), Magu, Geita, Ukerewe, Missungwi, Sengerema, Kwimba |
| | | Geita | Geita (V), Chato, Bukombe, Nyang'wale, Mbogwe |
| 5 | Ukanda wa kati ni nusu jangwa (wa aina moja) | Dodoma (W) | Kondoa, Dodoma MC, Mpwapwa, Kongwa, Bahi, Chamwino |
| | | Singida | Singida (V), Singida (M), Manyoni, Iramba, Ikungi, Mkalama |
| | | Shinyanga | Shinyanga (M) Shinyanga (V), Kishapu, Kahama |
| | | Morogoro | Morogoro (M), Morogoro (V), Mvomero |
| 6 | Nyanda za juu kusini | S-Mbeya | Mbeya (M), Mbeya (V), Mbarali, Kyela, Rungwe, Mbozi, Ileje, Chunya (S) |
| | | S-Iringa | Iringa (V), Kilolo (V), Iringa (S), Mufindi, |
| | | Njombe | Makete, Ludewa, Njombe (M), Njombe (V), Makambako, |
| | | Morogoro NW | Kilombero, Kilosa |
| 7 | Nyanda za juu kusini magharibi | Rukwa | Sumbawanga (V), Sumbawanga (M), Nkasi, Mpanda (V), Mpanda (M) |
| 8 | Nyanda za juu magharibi | Kigoma | Kasulu, Kibondo, Kigoma (V), Kigoma (M) |
| | | Kagera | Biharamulo, Bukoba (V), Misenyi, Bukoba (M), Karagwe, Muleba, Ngara |

Chanzo: ASDP II BF (2013) - ARD; Tanzania CSA Program (2015) na de Pawn, 1984

## C. Eneo Kuu 1: Usimamizi wa Matumizi Endelevu ya Maji na Ardhi (mazao, mifugo na uvuvi)

96 Malengo ya kimkakati, matokeo na viashiria husika vya eneo kuu la usimamizi wa matumizi endelevu ya maji na ardhi yanafafanuliwa kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 13: Eneo kuu 1: malengo mahsusi na matokeo ya ASDS**

| Lengo mahsusi | Matokeo | Viashiria vya matokeo |
|---|---|---|
| ***Eneo Kuu 1. Usimamizi wa matumizi endelevu ya maji na ardhi (Mfano kwa ajili ya umwagiliaji, maji kwa ajili ya mifugo, ardhi yenye mazao, malisho, madimbwi / mabwawa, na rutuba ya udongo)*** | Kupanua matumizi endelevu ya maji na ardhi<br>Usimamizi bora wa rasilimali kwa ajili ya mazao, mifugo, na uvuvi | - Ongezeko (asilimia) la miradi yenye matumizi endelevu ya umwagiliaji<br>- Ongezeko (asilimia) la wafugaji wanaofikia vyanzo vya kudumu vya maji (ya asili au mwanadamu)<br>- Ongezeko (asilimia) la miundombinu ya kisasa ya umwagiliaji na usimamizi wa kitaalam<br>- Ranchi bora zenye malisho na maji endelevu kwa ajili ya mifugo<br>- kuongezeka eneo (ha) la ufugaji wa samaki<br>- Kuongezeka kwa idadi ya wakulima wa kilimo cha mazao ya bahari<br>- Ongezeko (asilimia) la wadau kuendeleza teknolojia ya hifadhi ya mazingira inayohimili mabadliko ya tabianchi |
| | 1.1 Mpango bora wa Matumizi endelevu ya Ardhi na usimamizi wa Mifereji ya Maji na udongo | - Ongezeko (asilimia) ya wilaya zenye mipango ya matumizi bora ya ardhi<br>- Ongezeko (asilimia) ya vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi<br>- Ongezeko (asilimia) ya mabwawa yenye mipango shirikishi ya usimamizi<br>- Kuongezeka kwa eneo lenye uzalishaji bora katika sekta ya kilimo<br>- Ongezeko (asilimia) la wingi wa maji kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo |
| | 1.2. Matumizi na usimamizi jumuishi wa maji kwa ajili ya maendeleo ya Mazao / Umwagiliaji na Mifugo / Uvuvi | - Kuongezeka kwa eneo la kilimo cha umwagiliaji<br>- Kuongezeka kwa misimu ya kilimo cha mazao yanayolimwa kwenye skimu za umwagiliaji<br>- Kuongezeka kwa vituo vya kudumu vya maji kwa ajili ya mifugo<br>- kuongezeka eneo (ha) la ufugaji wa samaki<br>- Kuongezeka kwa idadi ya wakulima wa kilimo cha mazao ya baharini |
| | 1.3.Ustahimilivu ulioimarikakwenye mabadiliko/utofauti wa hali ya hewa na majanga ya asili | - Ongezeko la asilimia ya wakulima wa (mazao, mifugo na uvuvi) kukubali teknolojia na desturi ya kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi<br>- Ongezeko la idadi ya halmashauri zenye kilimo kinachostahimili mabadiliko tabianchi kwenye DADPs yao<br>- Kuongezeka kwa idadi ya ASLMs zenye kilimo kinachostahimili mabadiliko tabianchi kwenye mipango yao<br>- Upungufu wa asilimia ya kaya zenye hatari ya mafuriko au ukame |

97 Eneo Kuu 1 limegawanyika katika maeneo madogo matatu (3):

**ENEO KUU 1. USIMAMIZI NA MATUMIZI ENDELEVU YA MAJI NA ARDHI**

Eneo dogo 1.1: Mpango bora wa matumizi ya ardhi na usimamizi endelevu wa vyanzo vya maji na uhifadhi wa udongo

Eneo dogo 1.2: Matumizi na usimamizi shirikishi wa maji kwa ajili ya maendeleo ya kilimo, mifugo na uvuvi

Eneo dogo 1.3: Kuendeleza teknolojia za kilimo zenye ustahimilivu wa majanga ya asili na mabadiliko ya tabianchi

### Eneo dogo 1.1: Mpango wa matumizi bora ya ardhi na usimamizi endelevu wa vyanzo vya maji na uhifadhi wa udongo

98 **Kuongezeka kwa idadi ya watu na mifugo kunatishia matumizi endelevu ya ardhi.** Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na ongezeko la eneo linalolimwa mazao pamoja na migogoro kati ya wakulima na wafugaji kunako athiri maendeleo ya sekta. Uhamasishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi na usimamizi madhubuti ni muhimu kwa ajili ya uendelevu wa sekta. Eneo hili la kimkakati linahitaji mbinu mbalimbali za wadau kwa ajili ya matumizi endelevu ya ardhi katika mazao, mifugo (malisho na ranchi) na uvuvi kwa: (i) Kuandaa mipango ya matumizi ya bora ya ardhi ya nchi nzima (ngazi ya taifa na kijiji) kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Ardhi, Nyumba na Makazi, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Kituo cha Uwekezaji Tanzania; (ii) Usimamizi endelevu wa malisho na nyanda za malisho ili kuzuia au kupunguza uharibifu wa ardhi na kuenea kwa jangwa pamoja na mbinu ya kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi; (iii) Kuimarika kwa usimamizi bora wa rutuba ya udongo kwa kutumia mbinu bora za kulima ardhi na matumizi endelevu ya mbolea; na (iv) Ufugaji bora wa samaki kwa kujumuisha ufugaji wa samaki nchi kavu.

99 Pamoja na kwamba bado kuna maeneo ya ardhi ya kilimo ambayo hayatumiwi kwa ajili ya uzalishaji wa mazao na mifugo au uzalishaji wa samaki, ziada kubwa ya uzalishaji kutoka katika sekta ndogo ya wakulima wadogo inatarajiwa kutoka katika uboreshaji wa tija. Zaidi ya hayo, katika sekta kubwa ya kibiashara, uwekezaji ili kuongeza matumizi ya rasilimali za ardhi utakua ni chanzo cha ukuaji. Upanuzi wa eneo unahitaji kuendana na hatua za kulinda haki za kimila za ardhi.

100 ASDP II inatarajiwa kuongoza jitihada za kuhifadhi na kutumia maliasili za Tanzania katika namna endelevu ya uzalishaji kwa kutumia mfumo endelevu wa usimamizi wa ardhi na maji. Hatua za kuimarisha sera na mfumo wa kisheria kwa ajili ya matumizi ya ardhi na maji pia zitahusisha ujenzi wa uwezo wa kitaasisi na kiufundi kama maeneo ya kipaumbele. Vilevile, ni muhimu kuzuia uharibifu wa ardhi ya kilimo na ranchi katika maeneo yenye mvua za kutosha ambayo yanachukua sehemu kubwa ya nchi. Kupungua kwa rutuba ya udongo kunatishia kilimo uendelevu. Hivyo kuna haja ya kukarabati maeneo yaliyoharibika ili kuzuia kuzorota zaidi kupitia usimamizi bora wa afya ya udongo, kuanzishwa kwa hatua za kuhifadhi udongo, upandaji miti, kilimo sahihi cha uhifadhi wa mazingira na mbinu endelevu ya usimamizi wa malisho.

### Matumizi ya Ardhi na Maji

101 Upangaji wa matumizi bora ya ardhi ni mpangilio na utaratibu endelevu unaofanyika ili kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya maendeleo endelevu ya rasilimali za ardhi ambayo yatakidhi mahitaji ya watu. Upangaji unatathmini muonekano wa kimazingira, hali ya kijamii na kiuchumi, mfumo wa taasisi na uwezo wa kisheria na vikwazo vinavyohusu matumizi endelevu ya rasilimali za ardhi na kuwawezesha watu kufanya maamuzi kuhusu jinsi ya kugawa rasilimali hizo.

102 Kuongezeka kwa uhaba wa ardhi kunahitaji mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali, yote yakilenga kuongeza matumizi ya rasilimali ardhi kwa uangalifu ili kuepuka uharibifu na migogoro ya matumizi ya ardhi pamoja na matatizo mengine yatokanayo na ardhi kama vile njaa na vita. Mipango ya matumizi ya ardhi inaweza kutumika kusaidia maendeleo endelevu katika maeneo lengwa (maendeleo ya taifa) au mahsusi ili kuhakikisha kulindwa kwa huduma za mfumo wa kutegemeana pia mipango ya kiikolojia inaweza kutumika kulinda viumbe hai na thamani kubwa ya uhifadhi wa mazingira ikiwemo usimamizi wa maliasili, usimamizi wa mbuga za taifa, na usimamizi wa kanda ya kati ya mbuga za wanyama na matumizi mengine. Inaweza pia kupunguza au kuendana na mabadiliko ya tabianchi, kuzuia au kujiandaa kukabiliana na maafa, kuhakikisha usalama wa chakula, kuendeleza maeneo yaliyokuwa na migogoro zamani au kupunguza migogoro ya ardhi na kuboresha usimamizi wa ardhi. Pia itachangia kushughulikia masuala ya umiliki wa ardhi, kuepuka unyang'anyaji wa ardhi na kupunguza madhara yake.

103 Katika kukabiliana na vikwazo na changamoto za sasa za maendeleo, lengo la programu hii ni kuboresha

mipango ya matumizi bora ya ardhi na upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya shughuli husika za wakazi, ikiwa ni pamoja na ardhi kwa ya ajili kilimo na malisho na upatikanaji wa maji. Upangaji wa matumizi ya ardhi ni suala mtambuka la kisekta kati ya mazao ya kilimo na mifugo na matumizi mengine inayoruhusu kujumuisha ushirikishwaji katika mipango ya maendeleo ya halmashauri. Mbali na uwezeshaji wa ngazi ya Taifa kuendana na sera na msaada wa kiufundi, utekelezaji wa shughuli za upangaji wa matumizi bora ya ardhi kwa kiasi kikubwa utajumuishwa kwenye utekelezaji wa uwekezaji ngazi ya Halmashauri chini ya shughuli za Utafiti wa kilimo kwa ajili ya Maendeleo (AR4D) na Mipango ya Wilaya ya Kuendeleza Kilimo (DADPs). Kipaumbele cha Uwekezaji /miradi ya kitaifa na halmashauri imeoneshwa katika **Jedwali Na.14**.

**Jedwali Na. 14: Shughuli za kipaumbele katika mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa ajili ya maendeleo ya mazao na mifugo**

| *Maeneo ya uwekezaji/utekelezaji* | *shughuli za kipaumbele* |
|---|---|
| **Mpango wa matumizi bora ya ardhi na usimamizi wa maeneo oevu** | - Mpango shirikishi wa kupanga matumizi bora ya ardhi na usimamizi wa maeneo oevu<br>- Kutengeneza na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo<br>- Kujenga uwezo wa usimamizi wa matumizi bora ya ardhi<br>- Usimamizi wa maji yanayotiririka ndani na nje ya shamba (pamoja na utumiaji wa dhana za kilimo zilizokubalika)<br>- Uhifadhi wa ardhi isiyo na uwezo mkubwa wa kuzalisha ulinzi wa maeneo (upandaji miti, matuta, nk) -Utafiti kwa maendeleo na kutambua matumizi sahihi ya ardhi ya jumuiya |
| **Usimamizi wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo** | - Kutambua na kuweka mipaka ya ardhi ya kilimo ili kuongeza usalama na kuhamasisha uwekezaji katika kilimo<br>- Kuanzisha na kutekeleza mipango endelevu ya usimamizi wa ardhi ya kilimo<br>- Kuhamasisha matumizi ya teknolojia zinazofaa kwa usimamizi wa ardhi na maji kwa ajili ya kuboresha mbinu za kilimo |
| **Kuendeleza ranchi na malisho** | - Kuandaa na kutekeleza mipango endelevu ya usimamizi wa nyanda za malisho<br>- Kuboresha malisho (mbegu/hei, mashamba ya majaribio)<br>- Kuimarisha mfumo wa tahadhari kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wakati na mikakati ya kupunguza.<br>- Kusaidia uhifadhi wa mazingira katika jamii ya wafugaji |
| **Maendeleo ya maeneo ya malisho na uhifadhi wa mbolea** | - Kuhamasisha uzalishaji na kuboresha malisho na miti ya malisho<br>- Hifadhi ya chakula cha mifugo (Hei/Sileji) |
| **Wadudu na magonjwa waenezayo** | |
| ***Ufuatiliaji wa mikakati ya uwekezaji*** | - Tathmini ya matokeo na ufanisi wa wa uwekezaji katika umwagiliaji na maji ya mvua . |

[A]usimamizi wa miradi kuwa sehemu ya mfumo wa usimamizi na ufuatiaji (eneo dogo 4.5)

## Usimamizi endelevu wa udongo na kuendeleza kilimo hifadhi[48]

104 Kupungua kwa rutuba ya udongo kunakotokana na ulimaji wa kuendelea (bila kupumzisha) na kiwango cha chini cha matumizi ya mbolea kwa ajili ya kurejesha rutuba ya udongo inaaminika kuwa ni sababu muhimu inayochangia mavuno kidogo ya mazao. Kuzorota kwa maeneo ya malisho hutishia maisha ya jamii za wafugaji, hivyo usimamizi bora wa ranchi za malisho, ikiwa ni pamoja na kufanya maandalizi ya kukabiliana na ukame, na pia aina mbadala ya kuongeza kipato na kupunguza shinikizo la malisho muhimu. Mipango ya kusaidia Sekta inapaswa ilenge kuongeza tija na uzalishaji huku ikiweka uwiano kati ya maeneo yenye uwekezaji wa tija wa hali ya juu na maeneo yasiyo na uwekezaji ili kupambana

48 *Angalia pia 'Save and grow': http://www.fao.org/ag/save-and-grow/index_en.html*

na hali ya umaskini vijijini. Ili kuongeza viwango vya tija endelevu, kuna haja ya kukuza teknolojia sahihi, ikiwa ni pamoja na uhifadhi wa maji na udongo, usimamizi jumuishi wa rutuba ya udongo, kilimo cha misitu, mbinu za kilimo cha kuhifadhi mazingira na maarifa mengine ya asilia. Zaidi ya hayo, uchaguzi kati ya kuongeza tija ya uzalishaji na usimamizi wa rasilimali yatapunguzwa ndani ya kilimo endelevu cha mifumo ya kilimo iliyopitishwa.

105 **Usimamizi jumuishi wa afya ya udongo.** Mavuno bora hupatikana wakati virutubisho kutoka katika mchanganyiko wa mbolea za viwandani na vyanzo vya mbolea za zitokanazo na viumbe hai, kama vile naitrojeni ya mazao/miti na viumbe (mboji, uozo). Usimamizi jumuishi wa rutuba ya udongo unahakikisha kwamba virutubisho vinafikia mmea pindi vinapohitajika na havichafui maliasili na kuokoa fedha za wakulima. Sera za kukuza afya ya udongo lazima zihamasishe uhifadhi wa kilimo na mifumo ya mchanganyiko wa mazao - mifugo na ya kilimo cha msitu ambayo itaongeza rutuba ya udongo na kuhimiza usimamizi maalum na sahihi wa virutubisho. Udongo wenye wingi wa viumbe hai na mimea ni msingi wa kuongezeka kwa tija ya uzalishaji mazao.

### Sanduku Na. 2: Masuala ya msingi kwa ajili y matumizi bora ya ardhi-Usimamizi husishi wa rutuba ya udongo

**Kuhamasisha usimamizi jumuishi wa rasilimali :**

- Kutunza udongo kwa ajili ya viumbe hai na shughuli zinazohusiana na viumbe na kibaiolojia ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa unyevu na kuongeza rutuba kwenye udongo kupitia matumizi ya mbolea, mboji, matandazo na usimamizi bora wa mabaki ya mazao
- Usimamizi jumuishi wa rutuba ya mmea wenye gharama nafuu. Usimamizi bora wa mazao na mbegu zilizo bora za aina mbalimbali, uboreshaji wa mazao unanza mwanzo wa mvua, udhibiti jumuishi wa magugu na wadudu
- Usimamizi bora wa maji ya mvua, na kupunguza mmonyonyoko wa udongo ili kuboresha hali ya unyevu wa udongo.
- Uboreshaji wa udongo na uwezo wa kupitisha maji, kwa kuhifadhi udongo kwa kutumia mazao ya miti ya mizizi.
- Kuboresha ardhi iliyoharibiwa kwa uharibufu wa mazingira na madawa na mmonyonyoko wa udongo.
- Kuwepo kwa mifumo ya uzalishaji wa mazao kwa kutumia umwagiliaji, pia kuboresha ufanisi wa matumizi ya maji: kuboresha usambazaji wa maji ili kupunguza upotevu wa maji, kutandaza majani ili kupunguza upotevu wa maji, na kupunguza vihatarishi vya chumvi kwa kufuata mbinu sahihi za umwagiliaji.
- Kuwepo kwa mifumo ya uzalishaji wa mifugo, ushirikiano bora wa uzalishaji wa mazao na mifugo katika mifumo yote ya kilimo na mfumo wa kulima na kufuga kwa pamoja
- Kupitishwa kwa njia binafsi za kujifunza - mbinu shirikishi za jumuiya za maendeleo na teknolojia
- Uboreshaji bora wa ardhi ambao huwapa wakulima manufaa ya kiuchumi, kijamii na mazingira.

Chanzo: Mpango Mkakati wa Uwekezaji kwa ajili ya Matumizi Endelevu ya Ardhi Afrika Kusini mwa Jangwa (FAO, 2007)

106 **Kuendeleza Kilimo Hifadhi.** Kilimo hifadhi ni dhana ya utunzaji rasilimali kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ambayo inajitahidi kufikia faida inayokubalika pamoja na viwango vya juu na endelevu ya uzalishaji sanjari na kuhifadhi mazingira (FAO, 2007). Kilimo hifadhi hutegemea kanuni tatu muhimu: (i) Kutumia kiwango kidogo cha zana kutifua ardhi (kiwango cha chini cha ulimaji); (ii) Kujenga na kudumisha uasilia wa udongo; na (iii) Kufanya mzunguko wa mazao ya aina zaidi ya mbili. Shughuli kuu zinazopendekezwa zimejikita katika: (i) Kujenga ufahamu kwa kusambaza taarifa kuhusu usimamizi jumuishi wa rutuba ya udongo na kilimo hifadhi; (ii) Kujenga uwezo wa

maafisa wa ugani na wakulima kuhusu kilimo hifadhi; na (iii) Kurekebisha sera na kanuni za kilimo hifadhi, ikiwa ni pamoja na pembejeo za kilimo (kuwekwe viwango vya zana za kilimo hifadhi). Mbali na hilo, mwitikio wa sera na msaada wa kiufundi, pamoja na shughuli zinazosaidia kilimo hifadhi zitajumishwa katika uwekezaji ngazi ya halmashauri na kutekelezwa chini ya DADPs. Vifaa mbalimbali vya shughuli za ugani vitatumika kutoa mafunzo kwa wakulima na kukuza ukulima bora ulio endelevu ili kuongeza uzalishaji wa mazao makuu kwa kuboresha afya ya udongo na usimamizi jumuishi wa rutuba ya udongo. ASDP II pia itawezesha wakulima kupata pembejeo zinazohitajika ( eneo dogo 2.3), zana za kazi kwa ajili ya uzalishaji na baada ya mavuno (eneo dogo 2.4) na huduma zinazohusiana na fedha.

**Eneo dogo 1.2 matumizi na usimamizi shirikishi wa maji kwa ajili ya maendeleo ya kilimo, mifugo na uvuvi.**

107 **Ufanisi na ujumuishi katika matumizi ya maji kwa ajili ya umwagiliaji, mifugo na uvuvi.** Maeneo tarajiwa ya kimkakati na ubunifu ni: (i) Uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza tija kwa kulenga maeneo ya kipaumbele yenye faida kubwa; (ii) Kuimarisha umoja wa umwagiliaji kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi bora wa miundombinu na rasilimali, (iii) Kuimarisha huduma na usimamizi katika halmashauri na umoja wa umwagiliaji, (iv) Kutekeleza uratibu wa mpango wa rasilimali maji na usimamizi katika maeneo ya vyanzo vya maji; (v) Kuongeza ufanisi wa matumizi ya maji, (vi) Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji; (vii) Kutunga na kusimamia sheria na kanuni ambazo zitalinda maeneo yenye uwezekano wa umwagiliaji na maendeleo umwagiliaji; (viii) Kuendeleza jitihada za kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali za maji na matumizi kwa njia ya kuongeza uangalizi wa Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMF) na kuimarisha uwezo wa usimamizi jumuishi wa rasilimali maji.

108 **Uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za maji ni kipaumbele kikubwa.** Hili litatimizwa kupitia mipango ya usimamizi wa maeneo oevu, uvunaji wa maji, na kuboresha mifumo ya umwagiliaji na mifereji kwa wakulima wadogo na wakubwa ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya maji na kuhakikisha uwekezaji endelevu. Uwekezaji huu mkubwa utahusisha miundombinu ya umwagiliaji, vifaa na huduma za usimamizi jumuishi wa maji. Uwekezaji unalenga kuboresha mifumo ya umwagiliaji wa asili, ukarabati wa mifumo iliyoharibika na kuongeza eneo la umwagiliaji katika maeneo yanayotambuliwa. Kuongezeka kwa ufanisi wa mifumo ya umwagiliaji kupitia mifumo imara ya usimamizi wa kitaalamu kutaboresha mapato ya wakulima na uwekezaji endelevu. Mbali na umwagiliaji wa mazao, uwekezaji mahsusi utawezesha upatikanaji wa vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo na uvuvi.

109 **Kuongeza ushindani wa matumizi endelevu ya rasilimali.** Pamoja na mabadiliko ya tabianchi, mahitaji ya maji kwa sekta mbalimbali (kilimo, nishati, matumizi ya binadamu, maeneo oevu na hifadhi ya wamyama pori, nk) yanazidi kuwa na ushindani. Hakuna uhakika wa mgao endelevu wa maji katika sekta ya kilimo, ambayo inatumia maji kwa wingi. Sera zitasaidia kuondoa ruzuku potofu zinazosababisha wakulima kupoteza maji. Kimataifa, usimamizi wa rasilimali za maji unahitaj kuboreshwa kwa ufanisi wa matumizi ya maji kupitia viwango vya uchukuaji endelevu, matengenezo ya miundombinu, mipango ya matumizi bora ya ardhi na kufuatilia athari za mazingira. Uboreshaji endelevu unahitaji teknolojia nzuri na sahihi kwa ajili ya umwagiliaji na shughuli za kilimo zinazotumia mbinu za kutegemeana ili kuhifadhi maji, kuvuna maji ya mvua na kuongezea maji kwa kumwagilia mazao yanayotegemea mvua. Licha ya tija kubwa, umwagiliaji upo kwenye shinikizo kubwa la kupunguza madhara yake katika mazingira: umwagiliaji sahihi wa kitaalamu ambao hutoa matumizi yenye kuaminika na rahisi ya maji na kutumia tena maji taka yatakuwa ni jukwaa kubwa kwa ajili ya uboreshaji endelevu. Kuongezeka kwa tija ya mazao yanayotegemea mvua kutategemea matumizi ya mbegu bora, mazao yanayostahimili ukame na usimamizi wa mbinu zinazohifadhi/okoa maji.

**Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji Mazao.**

110 Lengo la kilimo cha umwagiliaji ni kuboresha uzalishaji wa mazao na kuwa na faida endelevu ya kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima wadogo na wakubwa ili kuongeza tija katika maeneo ya umwagiliaji yaliyongezeka kwa kutumia maji kidogo yanayopatikana muda wote. Hii itasaidia katika: (i) Kuendeleza mipango ya umwagiliaji na usimamizi wa kitaalamu; na (ii) Kuendeleza miundombinu ya maji kwa ajili ya umwagiaji, mifugo na uvuvi, ikiwa ni pamoja na ukarabati na upanuzi wa

miundombinu iliyokuwa chini ya ASDP-1. Wakati wa ASDP-I eneo la umwagiliaji liliongezeka kwa hekta 100,000. Katika ngazi za chini, mahitaji ya umwagiliaji yalibainishwa na kuingizwa kwenye mpango wa kilimo wa Halmashauri kama sehemu ya Mpango wa Kilimo wa Wilaya. Katika ngazi ya kitaifa, miradi ya umwagiliaji mikubwa na iliyokuwa inaingiliana kati ya wilaya zaidi ya moja, miundombinu yake ilifadhiliwa kwa kutumia Mfuko wa Maendeleo wa Umwagiliaji wa Taifa.

111 Ingawa wastani wa gharama ya kuendeleza kila hekta ya umwagiliaji inaonekana kuwa chini au sawa na gharama katika ukanda wa Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ipo fursa ya kupunguza gharama za kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji na kuongeza ufanisi katika matumizi ya maji. Tathmini[49] ya matokeo ya ASDP-1 inaonesha kuwa kupunguza gharama ni suala ambalo linahitaji kutafutiwa ufumbuzi chini ya ASDP II. Hivyo, mkakati madhubuti kwa utakaosaidia usanifu na kukamilika kwa miundombinu ya umwagiliaji, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika matumizi ya maji inabidi ubaniwe. Uwiano wa mazao katika skimu za umwagiliaji ipo chini, ikizingatiwa kuwa ni asilimia 25 tu ya eneo linalomwagiliwa wakati wa kipindi cha mvua na pia eneo hupata maji kutokana na kumwagiliwa katika kipindi cha kiangazi. Michango ya ada ya maji kwa wadau wa umwagiliaji na matengenezo ya miundombinu pia ilikuwa kidogo.

**112 Kuimarisha huduma za kitaalam kwa ajili ya maendeleo ya umwagiliaji.** Katika ngazi ya kitaifa, kazi hii itaimarisha uwezo wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na ofisi za kanda za umwagiliaji au mikoa katika: (i) Kupanga mikakati na kuweka vipaumbele kwa ajili ya maendeleo endelevu ya umwagiliaji, ikiwa ni pamoja na tathmini na usimamizi wa rasilimali maji na mazingira; (ii) Kutoa msaada wa kiufundi na kuboresha mipango na usanifu wa miundombinu katika uwekezaji endelevu wa umwagiliaji; na (iii) Ufuatiliaji wa utendaji na manufaa ya uwekezaji wa umwagiliaji uliopo, ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa takwimu za mara kwa mara na usimamizi katika masuala muhimu ya maendeleo ya umwagiliaji.

**113 Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika ASDP II,** katika kazi na huduma za umwagiliaji kwa: (i) Kujenga uwezo wa ujenzi na ukarabati wa wakandarasi wa ndani/kampuni za uhandisi katika kazi/utoaji wa huduma kwa ajili ya maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji kwenye kanda na (ii) Kuingia mikataba na makampuni binafsi ya uhandisi kwa ajili ya huduma za usimamizi, kuanzia mwaka wa kwanza wa ASDP II. Mifumo ya taarifa kwa miradi ya umwagiliaji itaboreshwa na mfumo wa usimamizi wa takwimu utaanzishwa ili kuruhusu uwekaji wa kina wa vipaumbele, mipango na bajeti ya uwekezaji. Mpango wa Maendeleo ya Rasilimali watu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji utahuishwa pamoja na kuweka vipaumbele ili kuimarisha utendaji katika ngazi zote za utendaji kwa kuajiri wataalamu wanaohitajika.

**114 Kuimarisha umoja wa wamwagiliaji kwa ajili ya usimamizi bora wa kitaalam wa umwagiliaji** ili uwe na tija endelevu. Shughuli hii itaimarisha uwezo wa umoja wa umwagiliaji [50]kwa ajili ya maendeleo ya ufanisi na usimamizi wa miradi ya umwagiliaji ndani ya mfumo wa Sera ya Umwagiliaji ya mwaka 2010 na Mwongozo Kabambe wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji. Kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, pamoja na uongozi wa vyama vya umwagiliaji, ASDP II: (i) Itafanya mapitio ya katiba za Umoja wa Wamwagiliaji zilizopo na sheria ndogo ili kuainisha mapungufu na kufanya maboresho muhimu yatakayoendana na muundo uliopitishwa wa Sheria Ndogo ya Umoja wa Wamwagiliaji, kwa miradi ya kilimo cha umwagiliaji, Uendeshaji na Matengenezo chini ya DADPs na Sheria ya Umwagiliaji ya mwaka (2013); (ii) Kubainisha tofauti ya maarifa na ujuzi wa umoja wa wamwagiliaji (IOs), mahitaji ya mafunzo, kuandaa mpango wa mafunzo na kusaidia katika utoaji wa mafunzo yanayotakiwa, kwa kutumia rasilimali watu na watoa huduma wanaohitajika; (iii) Kutoa mafunzo kwa umoja wa wamwagiliaji na wadau wengine kuhusu Sheria ya Umwagiliaji ya mwaka 2013 na Kanuni zake, na (iv) Kuandaa mwongozo wa usimamizi wa umoja wa wamwagiliaji kwa ajili ya utekelezaji wa sheria na kanuni zilizopo na uendeshaji sahihi waskimu.

115 ASDP II itaboresha uendeshaji wa miradi iliyopo kupitia wataalamu na watoa[51] huduma binafsi za umwagiliaji ili kuimarisha uwezo wa umoja wa wamwagiliaji na kuwapatia msaada wa kiufundi kwa: (i) kuboresha ufanisi katika maendeleo ya miradi / kuboresha shughuli za uendeshaji, pia kuhusisha

*49 Angalia tathmini ya matokeo ya Uwekezaji wa Kilimo cha umwagiliaji katika taarifa ya ASDP Aprili 2013.*

*50 Ushiriki wa wakulima katika umoja wa Wamwagiliaji ni wa kisheria kwa ajili ya uendelevu wa miundombinu na Kilimo cha umwagiliaji. Uimarishaji na uwezeshwaji wa vyama vya wakulima umeelezwa katika eneo kuu la 3*

*51 Masuala ya masoko yanajadiliwa katika sehemu ya mnyororo wa thamani na kilimo-biashara.*

kilimo cha mseto wa mazao; (ii) Matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya umwagiliaji; (iii) Kuongeza ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za maji, ikiwa ni pamoja na mbinu za kutunza maji, (iv) Kuimarisha upatikanaji wa teknolojia (Kilimo Shadidi cha Mpunga), n.k, taarifa na huduma ya ushauri, na (v) Kuimarisha uhusiano na mawakala wa pembejeo, watoa huduma za matumizi ya matrekta na zana, wasindikaji, masoko ya bidhaa na taasisi za kifedha. Katika kipindi cha 2015-2020, utekelezaji utalenga: (i) Skimu 78 za umwagiliaji wa mpunga zenye jumla ya hekta 56,000 , zitakazonufaisha wakulima wadogo wapatao 70,000 katika ukanda wa kilimo wa nyanda za juu kusini wa kilimo; na (ii) Kukamilisha utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ambayo ilianza kutekelezwa wakati wa ASDP-1. Kwa miaka iliyobaki (2021-2025) mpango utaangalia uboreshwaji wa mbinu hii ya kukarabati na kuendeleza zaidi skimu za umwagiliaji zitakazopewa kipaumbele.

116 **Kuendeleza [52]miundombinu ya umwagiliaji.** Miundombinu ya umwagiliaji iliyojengwa wakati wa ASDP-1 na BRN itakuwa ni kipaumbele cha kwanza, na itatafutiwa fedha kwa ajili ya shughuli ya upanuzi wa kilimo cha umwagiliaji kwa njia ya ujenzi mpya wa miradi midogo na ya kati au upanuzi wa miradi ya umwagiliaji iliyokuwepo. Umiliki wa mfumo mzima wa kitaalamu wa umwagiliaji utajumuisha wanakikundi/umoja wa wamwagiliaji. Ni muhimu umoja wa wamwagiliaji uwe na mfumo mzuri wa kuendesha na kuendeleza skimu za umwagiliaji. Uwezeshaji utahusisha maeneo matatu ya uwekezaji kama muhtasari unavyoonesha katika **Jedwali Na.15**

**Jedwali Na. 15: Muhtasari wa Skimu za Umwagiliaji za kipaumbele kwenye BRN na zile zilizobaki za ASDP-1(2015/2020)**

| Mradi wa umwagiliaji | Jumla ya idadi ya miradi ya umwagiliaji | Jumla ya idadi ya miradi ambayo haijakamilika ya ASDP-I | Idadi ya miradi ambayo haijakamilika au mpya | | Jumla miradi mipya | Jumla ya eneo (ha) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | JICA | Jumla BRN | | |
| **Jumla** | **367** | **280** | **120** | **78** | **87** | **162,122** |
| **(i) mchakato wa utekelezaji unafanywa na JICA na USAID** | | | | | | |
| Zilizotengwa na JICA | 120 | 77 | 107 | 13 | 43 | 51,964 |
| Ruzuku ya *Global Accelerated Food Security Programme(GAFSP)* | 4 | 3 | | 4 | | 10,000 |
| Ruzuku ya USAID | 5 | 0 | 0 | 2 | 5 | 18,600 |
| **(i) Kukamilisha, Ukarabati na uendelezaji wa skimu 63 za BRN (Benki ya Dunia)** | | | | | | |
| **Sehemu ya BRN** | 59 | 21 | (13) | 63 | 39 | 25,879 |
| **(i) Kukamilisha, ukarabati na uendelezaji miradi 179 ya ASDP-1** | | | | | | |
| **ASDP-1 vipaumbele** | 179 | 179 | 0 | 0 | 0 | 52,243 |
| **Jumla ya eneo** (ha) | | | | 59,558 /l | | |

52 *Imetoholewa kutoka katika tarrifa ya uwekezaji wa umwagiliaji chini ya ASDP IBF na BRN (FAO-TCIA 2013).*

**117 Utekelezaji.** Miongozo miwili ya kuendeleza skimu za umwagiliaji iliyopo[53], itaboreshwa kwa kushughulikia mapungufu yaliyoonekana wakati wa utekelezaji wa ASDP-1. Utaratibu uliokubaliwa na kuelezwa katika "Mwongozo Kabambe wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji" utatumika. Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Umwagiliaji (NIDF) utagharamia miradi mikubwa na iliyo na mahitaji mengi ambayo iko katika wilaya kadhaa. Mkakati kwa ajili ya maendeleo ya umwagiliaji utatekelezwa chini ya ASDP II na kuchangia pia muundo wa udhibiti endelevu wa matumizi ya ardhi na maji.

### Kuboresha usimamizi wa maji katika maeneo yanayolimwa kwa kutegemea mvua

**118 Wakulima wengi wanajihusisha na kilimo cha kutegemea mvua.** Utabiri wa mvua za msimu na kuboresha usimamizi wa maji katika mfumo wa kilimo cha uvumilivu kutawapunguzia hasara wakulima katika uzalishaji. Aidha, utafanyika uhamasishaji wa kupanda mazao ya aina mbalimbali yanayoendana na matumizi ya unyevu mdogo kwenye udongo, kufuata mbinu zinazoongeza uhifadhi wa maji na unyevu katika udongo, kuzingatia kilimo cha mzunguko kwa kutumia mazao ya mizizi inayopenya kina kirefu chini ya ardhi na kupunguza uvukizi kwa kuweka matandazo. Ili kuboresha tija ya kilimo kinachotegemea mvua kwa kiasi kikubwa uzingatiaji wa kanuni zote za uzalishaji wa mazao ni muhimu. Hii ni pamoja na kuvuna maji yanayotiririka, kupunguza utifuaji wa udongo, kuweka matandazo na usimamizi wa matumizi ya bayonuai ambayo ni muhimu katika kuongeza upatikanaji wa unyevu kwenye udongo.

**119** Usimamizi wa maji yanayotiririka shambani unaweza kufikiwa kwa mbinu mbalimbali. Kwa mfano, matumizi ya majaruba katika eneo lililolimwa umeonesha mafanikio katika kipindi cha mpito cha hali ya hewa na kuongeza upatikanaji wa unyevu katika udongo kila baada ya mvua kunyesha. Mfano mwingine ni kukusanya maji yanayotiririka kutoka kwenye miinuko au hifadhi ambayo inaweza kusimamiwa na mkulima na kumwezesha kupata maji ya kuongezea kwenye kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo, hatua hizo mbili huwa na athari kwa watumiaji wengine hivyo kuhitaji usimamizi wa ujumla wa bonde la mto. Kuna haja ya kuimarisha huduma za ugani kwa wakulima wanaotegemea kilimo cha mvua, ikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi wa kina wa mwenendo wa mvua na upungufu wa unyevu katika udongo ili kuimarisha uzalishaji uliopo wakati huu wa athari za mabadiliko ya tabianchi. Kuendeleza manufaa ya kimazingira na uhifadhi wa unyevu kwenye udongo kutanufaisha mifumo inayotegemeana na itategemea pia kiwango cha matumizi ya zana shambani (tazama eneo dogo 2.4), ambayo hutumia fursa za kunyesha kwa mvua.

**120 Sera na vipaumbele vya uwekezaji.** Mchango halisi wa uwekezaji katika uzalishaji wa kilimo cha kutegemea mvua na umwagiliaji katika ngazi ya Taifa unatakiwa kufanyiwa tathmini katika mifumo mbalimbali ya uzalishaji katika kanda za ikolojia za kilimo zilizolengwa. Ikiwa uzalishaji wa kutegemea mvua za msimu utaimarishwa kwa kuhamasisha uhifadhi wa unyevu wa udongo, kilimo cha kutegemea mvua kinaweza kutumika kama nguzo ya kuhamasisha kuhifadhi unyevu wa udongo, na itabidi jitihada hizo kutambuliwa vizuri. Faida halisi za kiwango cha chini cha uwekezaji katika uzalishaji wa mazao endelevu kwa kutegemea mvua na kiwango cha juu cha uwekezaji katika uzalishaji kwa kutumia umwagiliaji zinatakiwa kufanyiwa tathmini yakinifu ya kitaalamu, kijamii na kiuchumi dhidi ya malengo ya maendeleo. Maeneo muhimu ya uwekezaji yanapendekezwa katika **Jedwali Na. 16.**

### Jedwali Na. 16: Shughuli za kipaumbele kwa ajili ya usimamizi bora wa maji kwa ajili ya kilimo kinachotegemea mvua

| Maeneo ya uwekezaji | Shughuli ze kipaumbele |
|---|---|
| **Huduma za ugani na utafiti** | - Kuboresha ulimaji wa mazao tofauti tofauti ili kuboresha udongo na usimamizi wa maji<br>- Kuhamasisha kilimo hifadhi |

53 *Mwongozo wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji (chini ya DADPs – 01/2010) na "Mwongozo wa Kuendesha Mfuko wa Umwagiliaji wa Wilaya na Mfuko wa Umwagiliaji wa Taifa " (chini ya ASDP—uliorekebishwa 04/2011. Kama ilivyokuwa katika ASDP-1, jamii itachangia 20% ya gharama za kuendeleza Kilimo cha umwagiliaji na angalau asilimia 5 faida kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo .*

| Maeneo ya uwekezaji | Shughuli ze kipaumbele |
|---|---|
| Hatua za utekelezaji shambani | - Usimamizi wa ndani na nje ya shamba (ikiwa ni pamoja na msaada matumizi ya zana za kilimo )<br>- Kuhamasisha kuzuia mmomonyoko wa udongo na kuongeza kiwango cha rutuba ya viumbe hai |
| Mandhari | - Usimamizi wa ndani na nje ya shamba (ikiwa ni pamoja vyanzo vya juu) |
| Sera na mikakati ya uwekezaji | - Tathmini ya athari na ufanisi katika uwekezaji wa kilimo cha umwagiliaji na cha mvua ya kutosha |

### Rasilimali za maji kwa ajili ya mifugo na uvuvi

121 Zaidi ya asilimia 70 ya idadi ya mifugo inapatikana katika maeneo kame ya kanda ya Kaskazini, Kati na Magharibi mwa Tanzania. Huduma ya usambazaji wa maji katika maeneo ya wafugaji na wakulima wanaolima na kufuga unahusisha usimamizi wa: (i) Maji ya chemchem, visima vifupi na (ii) Maji ya mito na mabwawa na vyanzo vya maji kutokana na kuvuna maji ya mvua. Chini ya ASDP-1 karibia mabwawa 1,060 na visima 40 vilijengwa kati ya mwaka 2001 na 2010 katika ngazi za halmashauri na kuboresha upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo na kupunguza kuhamahama kwa wafugaji na mifugo yao wakati wa kutafuta maji.

122 Lengo ni kuongeza zaidi upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo na samaki kwa kuendeleza na kudumisha vyanzo vya maji vya kuaminika. Vipaumbele vya uwekezaji vimeoneshwa katika **Jedwali Na. 17**

### Jedwali Na. 17: Shughuli za kipaumbele za upatikanaji wa rasilimali maji kwa ajili ya ufugaji / uvuvi

| Maeneo ya uwekezaji | Shughuli za vipaumbele |
|---|---|
| Kuendeleza na kudumisha vyanzo vya maji ya kuaminika kwa ajili ya mifugo | - Kujenga na kudumisha mabwawa, visima, nk (Upangaji shirikishi, utekelezaji na usimamizi pamoja na wadau wa mifugo).<br>- Uboreshaji wa malisho (mbegu/uzalishaji wa nyasi, uzalishaji unaotegemea umwagiliaji na mashamba ya mfano). |
| Kuendeleza ufugaji wa samaki na chanzo kingine cha vyakula vya bahari | - Kuwezesha ujenzi wa mabwawa ya samaki<br>- Mabwawa ya samaki katika maziwa<br>- Kuendeleza uzalishaji wa bidhaa nyingine za baharini |
| Kuwezesha uendelezaji wa kilimo cha mwani katika bahari | - Kuwezesha uendelezaji wa kilimo cha mwani katika bahari |
| Kuendeleza kilimo cha mwani | - Kuwezesha uhamasishaji miongoni mwa wavuvi juu ya mifumo ya ekolojia ya bahari<br>- Kuwezesha uendeshaji wa utafiti katika sekta ya uvuvi<br>- Kufanyika kwa doria kwenye pembe za bahari<br>- Kuboresha kiwango cha ubora wa uvuvi na mazao ya uvuvi |

*Angalizo la Bajeti: Ujenzi wa mabwawa 10 kila moja kwa gharama ya shilingi bilioni 1*

### Eneo dogo 1.3: Kuendeleza teknolojia za kilimo zenye ustahimilivu wa majanga ya asili na mabadiliko ya tabianchi

123 **Tofauti ya hali ya hewa/mabadiliko ya hali ya hewa** yanatoa changamoto mpya kwa wakulima na wafugaji wa Kitanzania. Ingawa hakuna uhakika wa kiwango cha mabadiliko yanayotokea katika ikolojia za kanda za kilimo hapa nchini, kuna dalili za kuongezeka kujirudia kwa matukio ya hali hewa. Hali hii inahitaji kiwango cha kutosha cha maandalizi ili kusimamia athari na kukabiliana na

matokeo yake kwenye kaya zenye mazingira magumu, ikiwa ni pamoja na kupoteza mali. Juhudi za kukabiliana na athari za majanga na mabadiliko ya hali ya hewa huwa zinakabiliwa na changamoto[54] nyingi ikiwa ni pamoja na: (i) Uwezo mdogo wa kuzalisha na kusambaza taarifa mapema kuhusu majanga; (ii) Mwitikio mdogo katika kukabiliana na hali ya dharura ikiwa ni pamoja na uhaba wa zana, (iii) Uhaba wa taarifa za hali ya hewa, (iv) Ukosefu wa mpangilio mzuri wa kukabiliana na maafa kwa kulenga vyanzo vikuu vya majanga katika nchi (v) Ushirikiano mdogo wa taasisi wa kutoa taarifa za tahadhari ya maafa na majanga (vi) Upatikanaji mdogo wa fedha za kukabiliana na maafa.

124 **Mwelekeo wa Mabadiliko ya Tabianchi** ni muhimu kuwekewa msukumo zaidi ili kusaidia katika suala la usimamizi wa maliasili na mazingira. Kutokana na kiwango kikubwa cha shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi, mabadiliko ya hali ya hewa yanaweza kuathiri shughuli hizo kwa njia mbalimbali, hususan katika kipindi cha utekelezaji wa ASDP II. Kilimo cha Tanzania kwa kiwango kikubwa kinategemea mvua wakati upatikanaji wa mvua ya kutosha umeanza kupungua kutokana na uhalibifu wa mazingira hivyo kuleta athari ya kuwepo kwa jangwa na ukame. Kuna haja ya kuimarisha maendeleo ya mifumo imara zaidi ya masuala ya mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya shughuli za kilimo zilizopo.

125 **Kuhamasisha matumizi ya teknolojia zinazohimili mabadiliko ya tabianchi**[55], ni mbinu shirikishi inayosaidia uendelezaji wa sekta ya kilimo kwa kulinda mazingira kwa njia ya: (i) Kujenga mfumo wa kilimo chenye kuhimili mabadiliko ya tabianchi; na (ii) Kupunguza uzalishaji wa gesi joto kutokana na kilimo (ikiwa ni pamoja na mazao, mifugo na uvuvi). Katika kukabiliana na tishio linaloendelea kukua la mabadiliko ya tabianchi, wizara za kisekta zina wajibu wa kuchukua hatua za kukabiliana na kuendana na mabadiliko ya tabianchi. Hatua zinazo hitaji kuchukuliwa ni pamoja na: (i) Kufanya utafiti na kubadilishana taarifa na taasisi nyingine za utafiti (kikanda na kimataifa); (ii) Kuboresha ufanisi wa matumizi ya maji katika shughuli za kilimo; (iii) Kukuza usimamizi jumuishi wa ardhi na udongo; (iv) Kuwezesha utekelezaji wa sera ya mazingira kwa wakulima na wafugaji; na (v) Kujenga uelewa, mifumo ya kisera, mikakati na mipango, kuimarisha taasisi kwa kuongeza fedha kwa ajili ya masuala ya kulinda mazingira.

126 Kutunza na kulinda[56] mazingira kwa kuimarisha na kuweka mbinu endelevu za uzalishaji wa kilimo ambacho kitatunza na kuimarisha maliasili. Kuongezeka kwa mahitaji ya chakula bado ni changamoto inayosababishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuwepo kwa ushindani wa matumizi ya ardhi yenye rutuba, maji na nishati. Mtazamo mpya ni "uimarishaji wa uzalishaji endelevu wa mazao", ambayo yatazalishwa katika eneo moja litakalotunza rasilimali, kupunguza athari kwenye mazingira na kuimarisha rasilimali muhimu za asili na uendeshaji wa huduma za mazingira. Kanuni muhimu ni: (i) mifumo ya kilimo inayotunza rasilimali na kutoa tija kubwa, kijamii na kiuchumi na faida ya mazingira kwa ajili ya kuhamasisha uzalishaji wa mazao na mifugo; (ii) upatikanaji wa aina bora za mimea/mbegu, maeneo ya wanyama kuzaliana na vifaranga vya samaki (ii) matumizi ya njia bora za kilimo ikiwa ni pamoja na usimamizi wa afya ya udongo na rutuba ya udongo, usimamizi wa maji ya mvua, usimamizi wa maji yanayotumika kwa kilimo cha umwagiliaji na ulinzi wa afya bora ya mimea na wanyama. Ili kuhamasisha wakulima wadogo kutumia uzalishaji wa mazao endelevu, sera / kanuni na taasisi zinahitaji kuhamasisha wakulima wadogo kutumia rasilimali za asili kwa mipango endelevu (yaani huduma za mazingira), kujenga uwezo katika utafiti na teknolojia na kupunguza gharama za upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya uwekezaji.

54 *Ushuhuda kutoka : Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi Afrika . CTA 2014.*

55 *Imetoholewa kutoka ASDS (Septemba 2015) na Programu ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Tanzania ,inayoratibiwa na Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Makamu wa Rais (2015–2025).*

56 *Angalia pia SAVE and GROW: http://www.fao.org/ag/save-and-Grow/.*

**Sanduku Na. 3: Ajenda kwa ajili ya kuendeleza kilimo endelevu na stahimilivu.**

Ajenda ya uendelezaji wa kilimo endelevu inahitaji kutatua changamoto za mahitaji ya soko la bidhaa za mazao, mifugo na samaki kutokana na ongezeko la idadi ya watu duniani (na mijini), matumizi duni ya rasilimali za asili, uhaba wa nishati na mabadiliko ya hali ya hewa. Ili kuendeleza kilimo endelevu ajenda itahusisha;

- **Kwanza,** kuongeza ustahimilivu na kukuza uendelezaji wa mazingira, wakati wa kuongeza uzalishaji, ni muhimu kushughulikia kwa pamoja maagizo ya kuzalisha zaidi, kwa ufanisi zaidi, na kuhifadhi au kutunza msingi wa rasilimali za asili kwa ajli ya vizazi vijavyo vya vijijini katika ajenda mpya ya kuendeleza vijiji na kupunguza umasikini.
- **Pili,** Huwekeza kwa wakulima ujuzi na mtaji pamoja na utafiti wa kisayansi ili kushughulikia matatizo maalum kwenye mazingira, kwa lengo la kuendeleza mwitikio ambao umeenea katika ukanda wa kilimo wa kiikolojia. Hakuna ajenda ya kuimarisha mpango endelevu, lakini pia njia ya utaratibu ni mabadiliko ya mazingira, na kuunganisha maarifa ya wakulima na kisayansi ni sehemu ya ajenda ya mabadiliko.
- **Tatu,** kujenga ustahimilivu (mfano mabadiliko ya hali ya hewa) katika mifumo ya kilimo, na hivyo kuimarisha uwezo wa wakulima wadogo wa kukabiliana na athari. Uimarishaji wa kilimo endelevu unapaswa kuchukuliwa kama mbinu ya kuongeza wigo wa kuchagua wakulima wanawake na wanaume kwa njia bora ili kukamata soko wakati wa kupunguza hasara, au kuimarisha uwezo wao wa kusimamia.
- **Nne,** kuhamasisha sera na kuungwa mkono na vyama vya kisiasa, ikiwa ni pamoja na motisha ya kutosha na hatua za kukabiliana na athari kwa kuimarisha kilimo endelevu kinachoendana na mazingira . Hii inahitaji, hasa, ustawi wa ardhi vizuri ili kuhamasisha uwekezaji wa muda mrefu, bei rafiki na kusimamia matumizi ya maliasili na pembejeo za kilimo, na msaada wa kuendeleza fursa za masoko

Chanzo: Imetoholewa kutoka Mpango wa Tanzania wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (ACRP), 2014–2019

Wakulima wanahitaji elimu bora, kulingana na mahitaji yao, mbinu mpya za kujifunza kwa wakulima na kuunganisha vyanzo vya taarifa na rasilimali. Mazingira mazuri ya kuendeleza uwezo wa kuimarisha kilimo endelevu unahitaji kujenga muungano, kushirikiana majukumu na kujenga ushirikiano kati ya Serikali, asasi za kiraia, sekta binafsi na wakulima wote na vyama vyao.

127 Mbali na uwezeshaji katika ngazi ya taifa, kukabiliana na sera na msaada wa kiufundi, utekelezaji wa shughuli za mabadiliko ya tabianchi utaingizwa katika shughuli zote za ASDP II, ikiwa ni pamoja na utafiti, uzalishaji endelevu wa mazao, ufugaji na uvuvi na usimamizi wa mazao baada ya kuvuna kwa kuongeza ustawi na ushirikiano. Uwekezaji maalum utaunganishwa katika uwekezaji wa ngazi za Serikali za Mitaa na kutekelezwa kupitia DADPs. Sehemu kuu za hatua za ASDP II zimeelezwa katika Jedwali Na. 18.

**Jedwali Na. 18: Uwekezaji katika ASDP I1 na Maeneo ya Kuyashughulikia kwa ajili ya kuboresha ustahimilivu wa mifumo ya kilimo**

| Maeneo ya uwekezaji | Shughuli za kipaumbele |
|---|---|
| **Usimamizi wa sera** | - Athari kuhusu makundi ya wanyonge, kutambua fursa za kukabiliana na hali ikiwa ni pamoja na mikakati inayotokana na sera za mabadiliko ya hali ya hewa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki<br>- Kuimarisha utoaji wa taarifa za tahadhari mapema na maandalizi<br>- Kuongeza hatua ya usimamizi wa tahadhari, ikiwa ni pamoja na bima kwa ajili ya maafa. |
| **Mazao** | - Utafiti na upanuzi wa mazao mapya / mazao aina mbalimbali na mifumo ya kilimo endelevu inayofaa kwenye eneo lenye joto kali / kame (kuingizwa)<br>- Kuendeleza kilimo cha hifadhi, ikiwa ni pamoja na matumizi ya zana za kilimo<br>- utabiri wa hali ya hewa wa muda mfupi na muda mrefu kwa mwitikio wa Kilimo |
| **Mifugo/ uvuvi** | - Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi na uwezo wa kiufundi na mifumo ya kutoa taarifa za tahadhari ya mapema kwa kutoa taarifa kwa wakati na mwitikio<br>- Kuendeleza mikakati ya kushughulikia mabadiliko ya hali ya hewa kwa ajili ya kuelekea uzalishaji endelevu wa mifugo na uvuvi.<br>- Kuwaunga mkono wafugaji na vyama vyao katika kutekeleza hatua za kukabiliana<br>na changamoto zinazoikumba mifugo na Uvuvi |

**128 Uwekezaji katika ngazi ya Taifa na Halmashauri Eneo kuu la 1:**

**Jedwali Na. 19: bajeti ya maendeleo ya mpango wa miaka mitano/makadirio ya uwekezaji katika Eneo kuu 1 kwa bei za mwaka 2016 Tanzania**

**ENEO KUU LA 1: USIMAMIZI ENDELEVU WA MATUMIZI YA MAJI NA ARDHI – GHARAMA YA MSINGI IMEKADIRIWA KATIKA BEI ZA MWAKA 2016 (Shilingi Milioni)**

| Eneo dogo | Mwaka wa 1 | Mwaka wa pili | Mwaka wa tatu | Mwaka wa nne | Mwaka wa tano | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.1.1. Usimamizi Jumuishi wa Matumizi ya Ardhi kwa ajili ya utatuzi wa migogoro, uzalishaji endelevu wa kilimo na maendeleo ya viwand. | 29,759 | 31,014 | 34,532 | 0 | 0 | 95,305 |
| 1.1.1.2 Kuimarisha uzalishaji katika malisho na uhifadhi kwa tija endelevu ya mifugo. | 14,132 | 14,517 | 13,715 | 13,501 | 16,284 | 72,149 |
| 1.1.1.3 Kuimarisha upatikanaji wa ardhi ya kilimo kwa ajili ya uwezeshaji wa vijana. | 4,464 | 4,150 | 5,753 | 4,534 | 6,321 | 25,222 |
| 1.1.1. 4 Kuboresha uratibu na usimamizi wa maji na ufuatiliaji mifumo ya maji na usimamizi endelevu wa rasilimali. | - | 1,366 | 928 | 839 | 916 | 4,049 |
| 1.2.1.1 Ukarabati na maendeleo ya miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji na tija. | 16,370 | 184,589 | 172,338 | 175,278 | 189,619 | 738,194 |
| 1.2.1.2 Kuendeleza mifumo midogo ya umwagiliaji kwa ajili ya uzalishaji bora wa mazao yenye tija. | 5,873 | 50,129 | 57,162 | 59,915 | 65,430 | 238,509 |

| ENEO KUU LA 1: USIMAMIZI ENDELEVU WA MATUMIZI YA MAJI NA ARDHI – GHARAMA YA MSINGI IMEKADIRIWA KATIKA BEI ZA MWAKA 2016 (Shilingi Milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Eneo dogo** | **Mwaka wa 1** | **Mwaka wa pili** | **Mwaka wa tatu** | **Mwaka wa nne** | **Mwaka wa tano** | **Jumla** |
| 1.2.2.1 Uimarishaji wa miradi ya umwagiliaji katika usimamizi na utendaji. | 1,823 | 1,652 | 2,250 | 1,787 | 2,592 | 10,104 |
| 1.2.3.1 Kuendeleza miundombinu ya maji kwa ajili ya tija ya mifugo. | 2,856 | 66,582 | 77,456 | 76,103 | 85,464 | 308,461 |
| 1.2.3.2 Kukuza ujenzi wa vituo vya kisasa vya maji jumuishi kwa mazao, mifugo na uvuvi. | 42,069 | 79,875 | 111,447 | 158,157 | 88,773 | 480,321 |
| 1.3.1.1 Kukuza na kuendeleza kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na teknolojia ya kilimo cha kutunza mazingira. | 1,905 | 13,984 | 8,745 | 6,345 | 10,445 | 41,424 |
| 1.3.1.2 Kukuza njia ya mfumo wa ikolojia kwa ajili usimamizi wa uvuvi na Kilimo. | 1,090 | 1,045 | 1,730 | 795 | 1,329 | 5,989 |
| 1.3.1.3 Kuimarisha mfumo wa utoaji wa taarifa za tahadhari. | 1,960 | 1,052 | 1,009 | 396 | 501 | 4,918 |
| **JUMLA YA ENEO 1** | **122,301** | **449,955** | **487,065** | **497,648** | **467,674** | **2,024,643** |

## D. Eneo kuu 2: Kuongeza Tija na Faida

129 Malengo mkakati, matokeo na viashiria vinavyohusiana na “kuongezeka kwa tija na faida” katika sekta ya kilimo imelezewa katika **Jedwali Na.20.**

**Jedwali Na. 20: Eneo kuu 2: Kuhusiana na malengo mahsusi na matokeo ya ASDS**

| *Lengo mahsusi* | *Matokeo* | *Viashiria vya matokeo* |
|---|---|---|
| ***LM 2. Kuongeza kiwango cha uzalishaji wa tija katika Kilimo-biashara kwa ajili ya masoko ya bidhaa za vipaumbele*** | ***Kuongezeka kwa uzalishaji katika kilimo*** | - Mayai kwa kuku kwa siku, uzito kwa/ ng'ombe katika soko, kilo kwa samaki) kwa minyororo ya thamani ya bidhaa za kipaumbele<br>- Mabadiliko ya asilimia katika ufanisi wa kazi (Shilingi za Kitanzania kwa mkulima kwa msimu)<br>- Mabadiliko ya (asilimia) katika utapiamlo (kudumaa na chini ya uzito sahihi ) |
| | ***Kuongezeka kwa faida katika kilimo*** | - Mabadiliko ya faida ghafi (ha) Shilingi kwa ng'ombe wa maziwa , Shilingi kwa mfugo, nk kwa minyororo ya thamani ya bidhaa za vipaumbele<br>- Mabadiliko ya faida/ faida halisi (Shilingi kwa bidhaa au mradi) ya bidhaa ya kipaumbele<br>- Mapato halisi kwa mkulima, mfugaji au mvuvi |
| | 2.1. Kuboreka kwa upatikana-ji wa pembejeo za kilimo na huduma za afya | - Wakulima wanaopata na kutumia pembejeo bora<br>- Kiwango cha kuota kwa mbegu<br>- Uzalishaji wa mazao<br>- Upatikanaji wa ruzuku<br>- Faida kutokana na ruzuku<br>- Mabadiliko ya asilimia ya wakulima wanaotumia mbolea<br>- Mabadiliko ya asilimia ya wakulima wanaotumia mbegu bora<br>- Mabadiliko ya asilimia ya wafugaji wanaopata huduma za uhimilishaji |
| | 2.2. Kuboresha upatikanaji wa pembejeo za kilimo / na huduma za afya | - upatikanaji na utumiaji wa pembejeo – kiwango cha kuota mbegu<br>- Uzalishaji wa mazao<br>- Upatikanaji wa ruzuku<br>- Faida kutokana na ruzuku<br>- Mabadiliko ya asilimia ya wakulima wanaotumia mbolea<br>- Mabadiliko ya asilimia ya wakulima wanaotumia mbegu bora<br>- Mabadiliko ya asilimia ya wafugaji kupata huduma za uhimilishaji |
| | 2.3. Kuboreka kwa utafiti kwa ajili ya maendeleo ya kilimo | - Majaribio ya teknolojia mpya zilizotolewa na kusambazwa na vituo vya utafiti (kwa mfano aina mpya)<br>- Uwezo wa vituo vya utafiti wa kuzalisha teknolojia zenye ubora wa juu<br>- Mgao wa bajeti ya kawaida na ya maendeleo na kutolewa kwa fedha |
| | 2.4 Kuboreka kwa upatikana-ji wa huduma za zana | - Uwezo wa utumiaji wa huduma za zana<br>- Kaya kupata huduma mbalimbali za kutumia zana katika bidhaa za kipaumbele katika minyororo ya thamani<br>- Asilimia ya mabadiliko ya kaya zinazopata huduma ya usindikaji wa bidhaa za kipaumbele katika minyororo thamani<br>- Upotevu wa mazao ya kipaumbele katika mnyororo wa thamani baada ya mavuno |
| | 2.5 Kuboreka kwa usalama wa chakula na lishe | - Kaya za vijijini zinazoishi juu au chini ya mstari wa umaskini wa chakula<br>- Kujitosheleza kwa chakula kitaifa<br>- Matukio ya Utapiamlo (sugu au ya muda) Tanzania<br>- Upungufu wa virutubisho kwenye lishe kwa watoto na wanawake wajawazito<br>- Kaya zinazopata chakula chenye lishe na cha aina mbalimbali<br>- Kaya zinazolima kwa mifumo mbalimbali ya kuboresha mlo na kupunguza hatari ya uhaba wa chakula<br>- Kaya zinazopata protini ya mifugo na samaki<br>- Wilaya zinazopata chakula cha msaada kutoka NFRA<br>- Kiasi cha chakula kilichohifadhiwa na NFRA<br>- Kaya zinazopokea msaada wa dharura wa chakula |

**ENEO KUU 2: KUONGEZA TIJA NA FAIDA**

**Eneo dogo 2.1: Mafunzo ya ugani na huduma za mawasiliano**
**Eneo dogo 2.2: Upatikanaji wa pembejeo za kilimo na huduma za afya ya mimea na mifugo**
**Eneo dogo 2.3: Utafiti kwa maendeleo ya kilimo (AR4D)**
**Eneo dogo 2.4: Upatikanaji wa huduma na Matumizi ya Zana bora za kilimo**
**Eneo dogo 2.5: Usalama wa chakula na lishe.**

130 Mkakati unalenga kuongeza na kuendeleza uzalishaji wa tija katika bidhaa za kipaumbele (mazao, mifugo na uvuvi) kwa kulenga wakulima wadogo wa kibiashara, katika kuhakikisha kuna usalama wa chakula wa kaya na pia kilimo cha biashara. Kuna haja ya kuongeza kasi ya matumizi ya teknolojia zinazoongeza mavuno na kupunguza upotevu wa mazao shambani kabla na baada ya kuvuna, ikihusisha matumizi ya mbegu bora na mbolea, kupitia kuboreka kwa upatikanaji wa mikopo, huduma

za afya ya mifugo na huduma za zana bora. Eneo kuu la 2 limegawanyika katika maeneo madogo matano. Kipaumbele cha Serikali ya Tanzania kwa sekta ya kilimo na viwanda vya kilimo ni kufikia ongezeko la uzalishaji endelevu wa asilimia 6 ya kiwango cha ukuaji[57]. **Lengo mahususi la eneo hili ni kuwezesha kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa tija katika kilimo cha kibiashara kwa bidhaa za vipaumbele** katika minyororo ya thamani ya mazao, mifugo na uvuvi. Kuongeza tija ya bidhaa za kilimo ni muhimu kwa ajili ya usalama wa chakula na kilimo cha kibiashara katika kaya, wakati upanuzi wa eneo unapaswa kufanywa chini ya mifumo bora ya uzalishaji. Lengo na matokeo yaliyopendekezwa yatafikiwa kwa kupitia mwingiliano wa maeneo madogo matano: (i) Huduma za ugani na ushauri, mafunzo na habari; (ii) Upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa ajili ya mazao, mifugo na uvuvi; (iii) Utafiti kwa maendeleo; (iv) Upatikanaji wa huduma za zana za uzalishaji na uzuiaji wa upotevu wa mazao baada ya kuvuna; na (v) Usalama wa chakula na lishe.

131 Kwa kuzingatia wakulima wadogo wa kibiashara, mkakati katika eneo hili ni kuongeza utoaji na utumiaji wa teknolojia zinazohitajika, kuimarisha uzalishaji wenye tija wa bidhaa za kipaumbele katika mnyororo wa thamani ndani ya mfumo wa uzalishaji endelevu kwa ajili ya mazao, mifugo na uvuvi. Hii itafanikiwa kupitia: (i) Upatikanaji mpana wa teknolojia zinazoendana na mahitaji ya kibiashara ya wadau wa mnyororo wa thamani wa bidhaa; (ii) Kumwezesha mkulima kufikia ujuzi wa kiufundi na chaguzi za matumizi; (iii) Kuongezeka kwa upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima kupitia mawakala wa pembejeo (yaani, mbegu , vipando na safu za mifugo, mbolea, vyakula vya mifugo na madawa ya kilimo ); na (iv) Msaada wa huduma nyingine za teknolojia kama vile zana, huduma za afya ya mimea, mifugo, nk. Huduma za ushauri na mafunzo zitajumuisha masuala ya chakula na lishe, ikiwemo kukuza aina mbalimbali za mazao yanayosaidia kuongeza lishe bora, ufahamu kuhusu masuala mtambuka kama vile jinsia; vijana, mazingira na usimamizi endelevu wa mali asili, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, na kuzuia athari na udhibiti kama inavyotakiwa.

132 Mifumo imara ya uzalishaji endelevu itahusisha usimamizi wa rasilimali za asili (ardhi na maji), kilimo hifadhi, mbinu jumuishi za kurutubisha udongo, udhibiti wa wadudu , magonjwa, na udhibiti wa upotevu wa mazao baada ya kuvuna. Mbinu hizi zitaandaliwa vizuri kwa kuimarisha huduma za kikanda na za kitaifa za utafiti kwa maendeleo, mahitaji ya huduma za ugani na njia za usambazaji binafsi wa pembejeo (mbegu bora, koosafu/vifaranga vya samaki, mbolea, madawa ya kilimo, dawa za mifugo, chanjo, n.k). Msaada pia utatolewa kwa ajili ya: Usimamizi endelevu wa rasilimali za ardhi na maji; Matumizi ya zana za kilimo kwa ajili ya uzalishaji na kuongeza thamani; Vifaa vya uzalishaji, usindikaji na masoko na huduma za maabara kwa ajili ya uchunguzi sahihi, kudhibiti na kuzuia wadudu na magonjwa.

133 Uendelezaji wa mifugo utatoa mchango mkubwa katika ukuaji wa sekta kupitia matumizi bora ya rasilimali na mazao ya chakula, biashara, kuongeza uwezo wa usindikaji na kuboresha ufanisi wa masoko. Hatua maalum pia zitachukuliwa ili kuboresha usimamizi wa uvuvi na ufugaji wa kwenye maji ikiwa ni pamoja na miundombinu (bandari ya kisasa ya uvuvi) na hatua za usafi.

**Jedwali Na. 21: Malengo kwa ajili ya shughuli za kipaumbele kwa ajili ya kuongeza tija ya uzalishaji katika mifugo na uvuvi (miaka 10)**

| Sekta ndogo | Malengo mahususi / matokeo |
|---|---|
| Sekta ndogo ya Mifugo na Uvuvi | - Upatikanaji na matumizi ya pembejeo/ na zana<br>- Kuimarisha utafiti, huduma za ugani na shughuli za mafunzo (miundombinu)<br>- Kuwa na vyanzo mbalimbali vipya vya mapato |
| Uzalishaji wa nyama | - Maji na malisho ya mifugo na uvuvi (miundombinu) -Eneo kuu la 1;<br>- Kuboresha uzalishaji wa tija wa nyama kwa ajili ya uzalishaji wa kibiashara wa nyama bora inayokidhi viwango vya masoko ya ndani na nje |
| Uzalishaji wa maziwa | - Kuongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya masoko ya ndani na nje (kuongeza mapato) |

57 *Kuza Pato la Sekta kutoka Shilingi bilioni 9,600 (Dola za Marekani 6.4 bilioni) mwaka 2010/2011 hadi kufikia Shilingi bilioni 30,600 (Dola za Marekani bilioni 20.4) mwaka 2030/2031. Pato la Taifa miongoni mwa wanaoishi vijijini litaongezeka kutoka Dola za Marekani 180 hadi Dola za Marekani 360 katika kipindi hicho*

| Sekta ndogo | Malengo mahususi / matokeo |
|---|---|
| Uzalishaji wa mayai. | - Kukidhi mahitaji ya ndani na kuongeza mapato ya wafugaji wa kuku |
| Ngozi na uzalishaji wa bidhaa nyingine | - Kuongeza ubora, ukusanyaji na usindikaji wa ngozi kwa ajili ya masoko ya ndani na nje.<br>- Matumizi kwa ajili ya chakula, vyakula vya mifugo, madawa na nishati. |
| Wanyamakazi | - Kuongezeka mapato kwa wakulima kwa ajili ya shughuli za Kilimo na uzalishaji mdogo |
| Kukuza upatikanaji wa masoko ya wanyama na bidhaa za wanyama | - Kuendeleza ushirika na vyama vingine vya wakulima<br>- Kuboresha huduma za ukaguzi wa mifugo (kuboresha kuzuia na kudhibiti)<br>- Kuanzishwa ukanda huru wa magonjwa na kuimarisha taarifana ufuatiliaji juu ya magonjwa<br>- Kuimarisha huduma za maabara kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa |
| Uzalishaji wa kilimo cha samaki kwenye maji na uvuvi kwenye vyanzo vya asili | - Kukuza ufugaji wa samaki na huduma za uzalishaji katikakwenye maji na huduma na upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi<br>- Kuongezeka kwa tija katika uzalishaji wa ukuzaji viumbe kwenye maji kuongeza kwa mapato ya wakulima wa samaki katika wanaokuza viumbe kwenye maji<br>- Kuhuisha kanuni za uvuvi na kusimamia kwasharia na naendelevu na uzalishaji wa samaki |

Chanzo: Kutoka Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo. Desemba 2011.

**Eneo dogo 2.1: Mafunzo ya ugani huduma za mawasiliano**

134 **Uzalishaji wenye tija kwa wakulima wadogo wa mazao , mifugo na bidhaa za uvuvi ni kidogo** kutokana na matumizi duni ya teknolojia za kilimo bora, ushirikiano mdogo kati ya utafiti na huduma za ugani ( umma na binafsi), upatikanaji mdogo wa pembejeo za kilimo kukosekana kwa masoko ya uhakika na fursa za kuongeza thamani. Sheria na kanuni zinazokinzana na huduma ndogo za ukaguzi wa mazao pia zinazuia upatikanaji wa masoko ya kanda na kimataifa, wakati uwezo wa usimamizi na ufuatiliaji husababisha matumizi yasiyo endelevu (ardhi na maji) na matumizi ya madawa.

135 Kwa ujumla ASDP-1 ilikuwa muhimu katika kuweka mfumo wa utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima wadogo kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, ingawa ufikiaji wake na ubora wa huduma ulizingatia zaidi uzalishaji wa mazao, bila kuweka mkazo kuhusu mifugo na uvuvi na uhifadhi wa mazao baada ya kuvuna na masoko. ASDPI ilichangia kutoa ajira na mafunzo rasmi na ongezeko la kiujumla la mifumo ya huduma za ugani wa sekta ya umma,[58] huku ikizingatia zaidi teknolojia za uzalishaji. Mfumo wa sasa wa huduma za ugani kwa mazao na mifugo unategemea sana sekta ya umma. Jitihada za hivi karibuni za kuanzisha utaratibu wa PPP, mashamba darasa na vituo vya rasilimali za kata (WARC) unaonesha mwelekeo mzuri wa huduma za usaidizi zaidi kwa wakulima. Hatua nyingine za kupima na kuongeza kasi ya ubunifu wa utoaji wa huduma za kiufundi kwa gharama nafuu zinazotolewa na kusimamiwa kwa ushirikiano wa karibu na vyama vya wakulima inapaswa kuchukuliwa.

136 Huduma za ugani na mafunzo zinachangia kwa kiasi kikubwa kama kuwaunganisha wakulima na teknolojia mpya, taarifa na ujuzi ambao ni muhimu katika kuimarisha uzalishaji wa kilimo endelevu kama inavyooneshwa kwenye Sanduku Na. 4. Ili kukidhi mahitaji ya wakulima na umiliki katika kuongeza uzalishaji endelevu wa kilimo, kuna haja ya: (i) Kuimarisha uhusiano wa utafiti; (ii) Kutumia njia mpya katika ushiriki wa utoaji wa huduma za ugani, (iii) Kutumia TEHAMA, kama simu za mkononi na mtandao, ikiwa ni pamoja na kupatiwa mafunzo kutoka ngazi ya juu (iv) Kuhamasisha matumizi ya kanuni bora za kilimo (kilimo hifadhi , njia bora za kilimo, Mbinu Jumuishi za Udhibiti wa Wadudu na Magonjwa -*IPM,* nk); (v) Kuwezesha wakulima kupata pembejeo bora (mbegu/ vichembe hai, mbolea, vyakula vya mifugo, chanjo. (vi) Kuimarisha udhibiti wa wadudu na mfumo wa utoaji wa taarifa za tahadhari; (vii) Kuunganisha taasisi za sekta binafsi na umma zinazohusisha wadau wa mnyororo wa thamani wa bidhaa wa vijijini (ikiwa ni pamoja na vyama vya wakulima na (viii) Kuimarisha uwezo wa maabara wa kuchunguza na kubaini magonjwa na vimelea na wasambazaji wa magonjwa mapya na yanayotokea tena.

58 *Idadi ya maafisa wa Kijiji/Kata walikuwepo mwezi juni 2013 walikuwa 7,974 (hutuba ya bajeti ya wizara ya 2014/2015)*

### Sanduku Na. 4: Kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa ufanisi

***Je mbinu za sasa za utoaji huduma za ugani bado zinakidhi mahitaji ya wakulima?***

Serikali imelenga kufanya mageuzi ya utoaji wa huduma za ugani zinazozingatia ubora wa bidhaa/ mazao kwa kushirikiana na sekta binafsi na. Kupitia majukumu ya kisheria ya Serikali, mifumo ya mageuzi ya taasisi kuanzia Taasisi ya Utafiti ya Kilimo,vituo vya mafunzo ya kilimo ngazi ya kata, mashamba darasa na kadhalika. ASDP II itakuwa na mfumo kabambe wa uratibu wa miradi na programu zote katika sekta ya kilimo.

**Mapendekezo ya kuimarisha utoaji wa huduma za ugani**

**(i)** **Aina ya Mkulima/mteja.** Hii ni pamoja na kuzingatia jinsia, rasilimali, aina ya biashara, Kanda za Ikolojia za Kilimo, hali ya hewa, fursa za soko, mtaji wa jamii na upatikanaji wa mikopo, nk.

**(ii)** **Ujumuishi katika utoaji wa huduma za ugani** zinazojumuisha sekta ya umma, na mashirika binafsi (ikiwa ni pamoja na mahusiano na usambazaji wa pembejeo). Kuendeleza mchakato wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ugani na kutumia njia mbalimbali za mawasiliano kuimarisha utoaji wa huduma za sekta binafsi;

**(iii)** **Kuimarisha ushirikiano wa mafunzo na ugani** ili kushughulikia masuala halisi ya wakulima ya uendeshaji na timu za Wawezeshaji wa Wilaya (DFTs), mipango ya pamoja na msaada wa kifedha. Kuunganisha taasisi za mafunzo chini ya mwamvuli mmoja (Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, ATIs, LITAs, Shirika la Elimu na Mafunzo ya Uvuvi) na kuimarisha uwezo na ufanisi wao.

**(iv)** **Kuongeza idadi ya wagani (ili kila kijiji kipate afisa ugani wanahitajika zaidi ya 9,139** uhaba wa maafisa ugani kwa kila kijiji kunaathiri uundaji wa timu ya wataalamu katika ngazi ya kata. Hivyo, ipo haja ya kuendelea kuimarisha upatikanaji wa ujuzi na mafunzo kwa vitendo kwa watalaamu wa ugani kulingana na mnyororo wa thamani wa mazao.

**(v)** **Mbinu shirikishi / mifano na mbinu zilizotumiwa katika utoaji wa huduma za ugani,** (mfumo/ bidhaa, gharama nzuri): (i) Mbinu mbalimbali / mifano zitumiwe ikiwa ni pamoja na VBA na RIPAT; (ii) Miongozo / miongozo ya huduma za ugani; (iii) Kutumia TEHAMA; na (iv) Kuwezesha wakulima kuunda vyombo vya kujitegemea / usaidizi (kwa mfano, Vyama vya Kuweka na Kukopa, Vikundi vya Wakulima (Kujifunza), Vyama vya Ushirika wa Masoko ya Kilimo (AMCOS), nk

**(vi)** **Mipangilio ya taasisi katika utoaji wa huduma za ugani:** Chama cha kitaaluma cha maafisa ugani, mafunzo rejea, tathmini ya utendaji wa kawaida; kuimarisha timu za ugani za wilaya na utafiti na vyama vya wakulima, kutekeleza / kuwezesha WARCs kufanya kazi (TEHAMA) na kutumia sera / mkakati wa PPP ili kuboresha ufanisi kwa utoaji wa ugani (miongozo?)

**(vii)** **Ugharamiaji wa huduma za ugani :** mambo ya msingi ya kuzingatia kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa huduma za ugani ni pamoja na kuongeza bajeti kwa ajili ya huduma za ugani (Ruzuku ya huduma za ugani, Ruzuku ya kujenga uwezo ), kuwapa motisha wataalamu, kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi na kubadilisha utamaduni wa utendaji kazi

**Matarajio ya baadaye:** Mabadiliko ya huduma ya ugani ni muhimu kwa kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo kwa (i) Kuhakikisha huduma bora kwa kushirikisha wahusika muhimu; (ii) kutambua tofauti za wakulima ikiwa ni pamoja na jinsia; (iii) Kutafakari marekebisho ya taasisi ya utafiti / mafunzo); (iv) Kupata taarifa zinazohusu TEHAMA; (v) Kusaidia na kuwezesha kituo cha kilimo cha kata Maafisa ugani wa kijiji kufuatilia vituo vya kata vya rasilimali za kilimo na (vi) Kuratibu misaada yote ya ugani katika mitaa na mikutano ya kila mwaka ya kupanga na tathmini; na (vii) Kujenga uwezo wa kitaalamu wa wafanyakazi wa ugani.

137 Lengo ni kuendeleza mfumo wa usambazaji wa teknolojia kwa ajili ya matumizi ya wakulima ambao utasaidia kuongezeka kwa uzalishaji endelevu, tija na faida kwa wakulima kwa mazao muhimu kulingana na mahitaji ya soko. Kwa kuendeleza urefu uliopatikana kutoka ASDP-1, eneo hili litatoa msaada wa kuimarisha utoaji wa taarifa za masoko zinazoendana na mahitaji na huduma za taarifa kwa wakulima wadogo, kuweka mifumo iliyofanikiwa kama shamba darasa, mkulima kwa mkulima na utumiaji wa teknolojia mpya ya mawasiliano zikiwemo simu ya mkononi, mitandao ya kijamii na vyombo vingine vya habari na pia kuongezeka kwa umiliki wa watoa huduma katika mnyororo wa thamani wa bidhaa hasa maafisa ugani. Umakini mkubwa utatumika wa kuhimiza kuzingatia masuala mtambuka kama wanawake na vijana kujihusisha na kilimo, lishe, na utawala bora na usimamizi wa kitaalamu kwa wakulima na vyama vya mnyororo wa thamani wa bidhaa ukihusisha vyama vya ushirika.

138 Katika ngazi ya Taifa, eneo hili linatilia mkazo katika kufanya maboresho ya sera na taasisi kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati ya kilimo kusaidia utekelezaji katika ngazi ya chini, vyombo vya habari (programu za runinga na redio katika ngazi ya Taifa, magazeti, maonesho ya kilimo, kushirikiana na mashirika ya kimataifa n.k) na kusaidia teknolojia ya mawasiliano. ASDP II itasaidia kutoa mafunzo na huduma za kiufundi kama usimamizi wa matumizi bora ya ardhi, vifaa vya uzalishaji wa wanyama na mimea, utumiaji wa zana za kilimo na pia kusaidia usimamizi wa sera na sheria.

139 Katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, eneo hili dogo litasaidia kuongeza ufanisi na ubora wa huduma za ugani ambapo wakulima watapata teknolojia mpya ili kuongeza uzalishaji wa tija wa mazao na mifugo ya kipaumbele, kuboresha mnyororo wa thamani na kuhamasisha mageuzi ya mfumo wa kilimo ili kuwezesha usimamizi wa madhara yatokanayo na usalama wa chakula na lishe. Eneo hili dogo litasaidia utekelezaji wa mikakati ifuatayo:

*i.* *Kuelekeza huduma za kiufundi katika Kilimo cha kibiashara* kwa kulenga katika mnyororo wa thamani wa bidhaa za kipaumbele kwa kuwezeshwa na majukwa ya wilaya. Huduma za kiufundi za kilimo za umma zitafanywa na watoa ushauri wa biashara ili kuunda timu jumuishi za mnyororo wa thamani wa bidhaa katika ngazi za wilaya na kata. Huduma za usaidizi zitatoa mafunzo maalum na kufundisha timu za wawezeshaji wa wilaya na kata za kilimo ili kuruhusu kuhusika kwao katika kuendeleza kilimo-biashara na kuimarisha ushirikiano wa kilimo-biashara. Ili kuimarisha uwezeshaji wa wakulima na vyama vya wakulima (angalia eneo dogo la 3.1), shamba darasa na ugani wa wakulima kwa wakulima utaimarishwa kwa mafunzo, kuwahamasisha na kusaidia wakulima kutoa huduma za kitaalamu kwa vyama vya ushirika na wakulima wa vijijini. Njia hii itasaidia kuhamasisha utoaji wa huduma bora kulingana na mahitaji ya soko na huduma za utafiti kwa maendeleo.

*ii.* *Kufanya majaribio ya teknolojia za kilimo na kuzisambaza* ili kuruhusu uchaguzi mpana wa wakulima kwa kuimarisha uhusiano wa utafiti-ugani-wakulima kupitia mfumo wa utafiti wa washiriki na muonekano wa usimamizi wa ugani ulioendelezwa wakati wa ASDP-1. Hii itajumuisha: (a) Kusaidia maafisa ugani wa wilaya kuunganisha Tafiti za kilimo kwa ajili ya maendeleo na timu za kitaalamu za wilaya; (b) Kutekeleza kwa majaribio utafiti wa mnyororo wa thamani wa bidhaa za wilaya (kata mbili/wilaya/mwaka) za bidhaa za kipaumbele; na (c) Kusambaza/kueneza teknolojia zilizofanyiwa majaribio (kata mbili/wilaya/mwaka) na mashamba ya mfano (vijiji viwili kwa mwaka) yanayolenga mnyororo wa thamani wa bidhaa za kipaumbele, ili kuhakikisha kuwa wakulima wanakuwa na ufahamu mkubwa na wanapata teknolojia zilizoboreshwa/pembejeo na teknolojia za kudhibiti upotevu wa mazao baada ya kuvuna.

*iii.* *Kuboresha upatikanaji wa taarifa za kiufundi na kiuchumi* kwa wadau wa vijijini kwa kuimarisha upatikanaji wa taarifa za masoko kupitia matumizi ya teknolojia mpya, ikiwa ni pamoja na mawasiliano ya jadi na teknolojia mpya za mawasiliano ya TEHAMA (k.m., mtandao na simu za mkononi). Kuanzishwa kwa miundombinu ya mawasiliano yenye ufanisi na msaada wa kiufundi (angalia eneo dogo la 2.1), shughuli zinalenga kuwawezesha wakulima na wadau wa mnyororo wa thamani wa bidhaa kupata taarifa muhimu za kiufundi na kiuchumi kwa ajili ya kuendeleza biashara zao za kilimo. Ili kufikia azma hiyo, wataalamu wa kiufundi wa wilaya, vikundi vya ugani vya vijiji na wakulima viongozi watapatiwa vifaa na kuunganishwa na dawati la msaada wa kitaalam katika ngazi zote kwa ajili ya kubadilishana taarifa kwa kutumia mitandao na simu za mkononi. Hata hivyo, upatikanaji wa taarifa kwa ajili ya wakulima utaendelezwa kwa njia za vipeperushi/maelezo ya kitaalamu, programu za redio na makundi ya majadiliano ya wasikilizaji na uanzishwaji wa kituo cha rasilimali za kilimo katika kata katika maeneo ambayo vituo hivyo havijaanzishwa.

*iv.* *Kuboresha / kuimarisha uwezo wa taasisi za mafunzo ya kilimo* (ATI) na taasisi za mafunzo ya mifugo (LITIs) ili kuwezesha kazi zao za: (i) Kutoa elimu na uzalishaji wa maafisa ugani (ngazi ya astashahada na shahada); (ii) Kutoa mafunzo ya huduma na uboreshaji kwa maafisa wa ugani waliopo ikiwa ni pamoja na kuwaendeleza kutoka ngazi ya stashahada hadi shahada na (iii)

Mchango kwa watoa huduma za kitaalam kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na wakulima (kazi ya ngazi ya mitaa).

v. *Kuimarisha huduma za afya za mimea na mifugo, ikiwa ni pamoja na udhibiti wa ubora wa pembejeo na mavuno.*

140 Katika ngazi ya kitaifa / kanda, eneo dogo la ugani litasaidia huduma za ugani wa kilimo katika ngazi za kitaifa na sekretarieti za mikoa kwa kuweka mikakati na kutoa huduma za kitaalam katika wilaya. Hii itahusisha kuimarisha uwezo kwa ajili ya huduma za ubunifu unaolenga masoko ya bidhaa katika mnyororo wa thamani na huduma za ushauri kwa mifumo kwa ajili ya kilimo endelevu; kuandaa miongozo na taarifa maalumu na vifaa vya mafunzo; kuimarisha msaada wa mbinu na miongozo kwa ajili ya kutoa huduma za ugani na kuwezesha vyuo vya kilimo na mifugo ili viweze kutoa mafunzo bora. Katika ngazi ya mitaa, huduma za kiufundi zitafadhiliwa kupitia maeneo husika. Maafisa ugani wa wilaya, kata na vijiji ambao watasaidiwa na watoa huduma binafsi za kilimo, (APS), watakuwa na majukumu muhimu ya kufanya majaribio na kueneza teknolojia / mifumo iliyofanikiwa ndani na nje ya wilaya.

### Ugani wa Mazao, Mafunzo na Uhamsishaji

141 Idara ya huduma za ugani wa mazao chini ya wizara ina majukumu ya: (i) Kushauri juu ya uandaaji wa mikakati na sera; (ii) Kuboresha mbinu za utoaji wa huduma za ugani kwa ajili ya matumizi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa; (iii) Kuweka viwango vya utoaji huduma na kufuatilia utekelezaji wake; (iv) Kutoa miongozo ya kiutaalamu kuhusu kilimo bora na endelevu kwa ajili ya Sekretarieti ya Mkoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa; (v) Kusambaza machapisho ya kiufundi kwa ajili ya kutoa huduma za ugani kwa matumizi ya Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; (vi) Kuwezesha unganisho la huduma za ugani- utafiti na wakulima; (vii) Kuratibu na kuwezesha watoa huduma za ugani wa sekta binafsi; (viii) Kuwezesha mafunzo na kujenga uwezo wa wagani; (ix) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya mawasiliano kutoa huduma za ugani; na (x) Kufuatilia na kutathmini utoaji wa huduma za ugani.

142 ASDP-1 ilihamasisha ubunifu katika utoaji wa huduma za ugani, ikiwa ni pamoja na matumizi ya njia ya shamba darasa ili kuongeza usambazaji wa teknolojia na matumizi miongoni mwa wakulima wadogo. Njia ya shamba darasa imetambuliwa kuwa yenye ufanisi na watoa huduma za ugani wa umma na binafsi/watoa huduma za ugani katika mashirika yasiyo ya kiserikali, ingawa kuieneza kwake itahitaji kuhuishwa kwa sekta za umma na binafsi zinazotoa huduma za ugani na ushirikiano wa makundi yote katika mnyororo wa thamani kutoa msukumo kwa wanawake na vijana. Njia ya shamba darasa itatumika sawa na njia nyingine kama ziara za mafunzo za kubadilishana uzoefu kati ya mkulima na mkulima, huduma za kiufundi na masoko ndani ya vyama vya wakulima n.k, vilevile kuanzishwa kwa huduma za utoaji wa taarifa za kiufundi na za kiuchumi ambazo zimetoholewa kwa ajili ya mahitaji ya watumiaji mbalimbali (mkulima, maafisa ugani, wataalamu wa wilaya, wataalamu wa ngazi ya wizara, nk).

143 **Katika ngazi ya Taifa,** maeneo muhimu yanayopendekezwa kwa ajili ya utoaji wa huduma za ugani katika kilimo ni:

i. Kuimarisha rasilimali watu na vitendea kazi kwa ajili ya utoaji wa huduma za kitaifa za ugani, hususan kwa ajili ya uvumbuzi wa mbinu na wa kitaasisi na usaidizi wa kiwango cha juu.

ii. Kuchangia katika uoanishaji wa mbinu za shamba darasa kwenye minyororo ya thamani na uzingatiaji wa wanawake na vijana, ili kuwasaidia wakulima waliohitimu shamba darasa kuanzisha mashamba darasa kwa ajili ya wakulima wengine, kuhamasisha kujifunza na ziara za kubadilishana uzoefu kati ya wakulima na wagani.

iii. Kuharakisha mageuzi ya utoaji wa huduma za ugani kwa kuandaa mkakati wa kuendeleza huduma za ugani kuboresha mahusiano ya utafiti na ugani , uoanishaji wa uwezeshwaji wa huduma za ugani za sekta ya umma na binafsi, kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika usambazaji wa teknolojia na taarifa za masoko kwenye minyororo ya thamani ya bidhaa;

*Ikiwa kama ni sehemu ya kutekeleza Sera ya Taifa ya Kilimo (2013), Wizara imejiandaa kuendeleza Mkakati wa Ugani wa Taifa na mfumo wa kisheria kwa huduma za ugani ambao utafafanua: (i) Uhusiano wa wadau muhimu katika utoaji na uwezeshaji wa kifedha katika huduma za ugani.(ii.) majukumu ya wagani na wateja wanaotakiwa kuhudumiwa. (iii) Kuratibu wadau wa utoaji wa huduma za ugani ; na (iv) Kuanzisha jukwaa la majadiliano la wadau muhimu waliopo katika huduma za ugani.*

iv. Kukarabati miundombinu na kuongeza vifaa katika vituo vinne vya mafunzo ya wakulima na kitengo cha elimu ya wakulima *(FEU)* ili kusambaza teknolojia za kisasa.

v. Uimarishaji wa ufuatiliaji katika ngazi ya halmashauri na kujenga uwezo wa huduma za ugani katika Sekretarieti za Mkoa, wilaya na kata ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma zinazotolewa na sekta za umma na binafsi na ukaguzi wa shughuli za shamba (ikiwa ni pamoja na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano).

144 Katika ngazi ya Halmashauri vipaumbele vya uwekezaji ni kama ifuatavyo:

i. Kuimarisha rasilimali watu na vitendea kazi kwa ajili ya utoaji wa huduma za ugani katika ngazi ya kata ikiwemo mafunzo ya ujuzi wa kitaalamu, mafunzo rejea, vitendea kazi na usafiri.

ii. Kuboresha mazingira ya kuishi na kazi katika ngazi za kata na vijiji;

iii. Kujenga na kuimarisha timu za ugani katika kata.

iv. Kutoa vifaa na kuwezesha utendaji kazi wa vituo vya kata vya rasilimali za kilimo, ikiwa ni pamoja na kuanzisha mashamba ya majaribio ya teknolojia.

v. Kushirikiana na vitengo vya ushirikiano vya utafiti na ugani kikanda (TTPU) na kuimarisha utafiti wa shambani na mitandao ya majaribio ya aina mbalimbali za njia endelevu za usimamizi wa kilimo katika minyororo ya thamani ya bidhaa za kipaumbele.

vi. Kupanua maarifa ya kiufundi na kiuchumi ili kusaidia uwezeshaji wa wakulima katika kuendeleza mnyororo wa thamani kuanzia uzalishaji hadi masoko.

vii. Kuendeleza mfumo bora wa kuwajibika kwa mahitaji/ maswali ya kitaalamu ya wakulima kwa kuendeleza mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika ngazi za halmashauri kwa kuongeza huduma za ugani na ushauri .

145 **Mafunzo.** Wizara ya Kilimo ina Taasisi za Mafunzo ya Kilimo (ATIs) 14 kwa ajili ya sekta ndogo ya mazao. Miundombinu mingi inahitaji ukarabati ili kuchochea ufanisi wa utoaji mafunzo na mazingira mazuri kwa wafanyakazi. Taasisi hizi pia zina ukosefu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Hii huathiri sana mafunzo kwa vitendo na ujuzi unaopatikana hauendani na mahitaji ya sasa ya soko la ajira. Mitaala inayotumika katika taasisi hizi inahitaji kupitiwa upya. Uwezo wa rasilimali watu wa Idara ya Mafunzo wakufunzi 195, maafisa kilimo 94 na wafanyakazi wasaidizi 119 unahitajika kuongezwa kwa kuwa na programu maalum za kozi ndefu na fupi za kuwaendeleza.

146 Lengo ni kuimarisha uwezo wa mafunzo kwa wataalamu wa kilimo (kiwango cha astashahada na shahada, na mafunzo kazini) na ufikiaji wa taasisi za umma na kampuni binafsi zenye wataalamu bora wa kilimo, ambao mafunzo yao yanatambuliwa na Baraza la Taifa la Elimu na Ufundi (NACTE). Mizunguko ya mafunzo pia itaruhusu uwezeshaji wa vijana katika kujiajiri na kuanzisha viwanda vidogo katika Kilimo-biashara. Maeneo ya kipaumbele ya uwezeshwaji ni pamoja na: (i) Kukarabati mazingira ya kuishi pamoja na kujifunzia ya taasisi 14 za mafunzo ya kilimo; (ii) Utoaji wa vifaa vya kujifunzia, misaada,maktaba, vifaa vya usafiri na samani; (iii) Kuendeleza mashamba ya mafunzo kwa vitendo/ maeneo ya majaribio kwa wanafunzi/ wakulima katika taasisi za mafunzo ya kilimo (iv) Kujenga uwezo wa wakufunzi (195), maafisa kilimo 94 na wafanyakazi wasaidizi (119) katika makao makuu ya wizara na vyuo vya mafunzo ya kilimo katika kozi fupi na ndefu (v) Kuimarisha mitaala ya kufundishia programu za ngazi ya stashada na astashahada kwa wakulima kuhusu masuala ya masoko, tathmini na ufuatiliaji, uandaaji mipango na bajeti ya uwekezaji wa kibiashara na kusaidia vyama vya wakulima.

### Sanduku Na. 5: Taasisi za mafunzo ya ufundi

ATI / LITI inaunda ngazi ya kati ya kiufundi kati ya ASLM na Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambazo hutoa mafunzo kwa vitendo na maarifa kwa wataalamu wa kilimo ambao wanaweza kuajiriwa katika sekta ya umma na binafsi. ATI / LITI pia hufanya mafunzo ya muda mfupi kwa viongozi wa wakulima. Wanafunzi takribani 1,600 na 2,700 wanafunzi wanahitimu kila mwaka kutoka vyuo vya mafunzo ya kilimo. ASDP II inahitaji kuimarisha vyuo vinane (8) ili kuimarisha huduma za ugani. Hii itafanyika ili kufikia:

(i) Wataalam wenye ujuzi wa ugani wa kilimo na mafundi (stashahada na astashahada). Pengo la Maafisa ugani wa mazao ni 6,244 (15,802 ni jumla ya mahitaji), wakati wa makao makuu pengo ni 142 + 372 kwa kada zingine (takribani wanafunzi 2,700 wanahitimu kila mwaka kutoka ATI). Pengo la Maafisa ugani wa mifugo ni takriban 10,000 (mahitaji ya jumla ni 16,000).

(ii) Mafunzo kwa maafisa ugani walioko katika ajira.

(iii) Mafunzo ya wataalam walioko katika ajira na ya wakulima hutolewa na ATI na LITI hasa kwa wakulima na kuimarisha usimamizi wa vyama vya wakulima, uongozi na huduma za kiufundi na kiuchumi kwa wanachama wao.

Kwa hivyo, taasisi hizi zinahitaji maboresho makubwa katika zana na vifaa vya mafunzo ya vitendo katika uzalishaji na uuzaji, vinavyotokana na mahitaji ya wakulima wa kanda. Taasisi hizi huendeshwa kwa kutumia bajeti ya serikali mipango / miradi, bodi za mnyororo wa thamani wa bidhaa, wajasiriamali binafsi na wanafunzi.

147 **"Kitengo" cha Kuendeleza Mazao.** Kuboresha uzalishaji, tija na masoko kwa sekta ndogo za mazao kwa kuhamasisha njia bora za kilimo na ujuzi wa ujasiliamali kama vile 'kilimo cha kibiashara' kwa wakulima wadogo, hasa katika maeneo ya uzalishaji mazao. Mikakati ya kuboresha uzalishaji, tija na masoko kwa sekta ndogo ya mazao itajumuisha yafuatayo: (i) Biashara ya uzalishaji wa mazao ya nayostahimili ukame (hususani muhogo); (ii) Kuendeleza programu/ mipango na kuanzisha mikakati na miundombinu ya kilimo cha matunda na mbogamboga; (iii) Mafunzo ya wataalamu wa kilimo cha matunda na mbogamboga na wakulima wakubwa katika njia bora za kilimo na kuendeleza mnyororo wa thamani; (iv) Kuendeleza mkakati na kutekeleza mpango wa kukuza kilimo hai ili kuongeza mahitaji ya bidhaa hizo; (v) Kuunda mkakati wa maendeleo ya mbegu za mafuta na mpango wa utekelezaji; na (vi) Kuboresha na kudumisha bustani za mazao katika maeneo muhimu matano ili kuanzisha vyanzo vya kuaminika vya uzalishaji wa miche. Kitengo cha kukuza mazao pia hutoa huduma za kitaalamu kwa bodi tisa za mazao (chai, kahawa, pamba, katani, pareto, tumbaku, sukari, korosho, nafaka na mazao mchanganyiko). Msaada huu ni pamoja na,: (i) Mapitio na maboresho ya mikakati yao ya maendeleo; (ii) Ufuatiliaji wa kitaalamu kwa watendaji muhimu wa mnyororo wa thamani na wakulima wakubwa na (iii) Kukuza kilimo cha mkataba

148 Uwekezaji wa kipaumbele uliopendekezwa ni pamoja na: (i) Utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya mazao katika bodi tisa za mazao; na (ii) Shughuli nyingine zinazohusiana na masoko ya muhogo, uendeshaji wa mkakati wa maendeleo ya kilimo cha bustani, mafunzo na vifaa vya kazi vya halmashauri na wafanyakazi wa wizara, utekelezaji wa kazi za udhibiti na ufuatiliaji. Kuweka mkakati wa kazi husika za bodi za mazao, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji utakuwa wa umuhimu kwenye kuongeza ufanisi wa misaada.

### Mafunzo na Huduma za Ugani wa Mifugo na Uvuvi

149 Huduma za ugani wa mifugo na uvuvi zinahusika na usambazaji wa ujuzi na maarifa kwa wakulima na kupeana taarifa za kitalamu na kiuchumi na uzoefu miongoni mwa wadau wa mnyororo wa thamani, kuongeza uzalishaji, tija na mapato kwa wazalishaji. Huduma za ugani kwa sasa hutolewa na watoa huduma wa umma na kuna ongezeko kidogo la ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma kupitia njia mbalimbali, hasa kwa huduma za afya ya mifugo. Hivi sasa, huduma za ugani za mifugo ni pamoja na wagani wa mifugo 4,172 katika wilaya, ngazi za kata na vijiji (upungufu wa wagani unakadiriwa kuwa ni 16,000).

150 Chini ya mfumo wa ugani, Mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo (LITS) ni muhimu kwa

ajili ya biashara ya kimataifa ya uuzaji wa mifugo na kuhakikisha usalama wa chakula na afya kwa walaji. Usafirishaji nje wa mifugo na bidhaa za mifugo unakabiliwa na changamoto ya ueneaji wa magonjwa ya mifugo na masoko ya bidhaa za mifugo katika nchi zinazoagiza kutoka nje. Maeneo ya kipaumbele kwa uwekezaji kwa ajili ya mifugo na uvuvi na huduma za msaada wa kitaalamu ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 22:**

**Jedwali Na. 22: Shughuli za kipaumbele za huduma za ugani kwa ajili mifugo**

| **Maeneo ya uwekezaji / shughuli za kipaumbele** |
|---|
| **Ngazi ya Taifa na Kanda:** |
| • Kuanzisha mashamba ya mafunzo kwa vitendo na mashamba ya majaribio kwa ajili ya wanafunzi na wakulima<br>• Kuratibu watoa huduma za ugani za mifugo na kufanya ufuatiliaji wa kiufundi.<br>• Kuwawezesha maafisa ugani wa mifugo 594 kutoka Serikali za Mitaa zote na makao makuu kupata mafunzo katika ngazi ya Shahada ya Uzamili (MSc)<br>• Kukarabati miundombinu ya mifugo na kujenga na viwanja vitatu vya maonesho ya kilimo katika kanda 7 |
| • Kuanzisha na kuweka vifaa katika studio saba (7) za kurekodi programu za TV na redio katika ngazi ya Taifa<br>• Kuanzisha mfuko wa fedha wa dhamana kwa ajili ya vifaa vya kutambua mifugo |
| • Kuusambaza Mfumo wa Kitaifa wa Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo (TANLITS), pamoja na kuimarisha dawati la huduma kwa mteja TANLITS kwa kuweka mtandao wa kuaminika na kuunganishwa katika tovuti<br>• Kutekeleza mafunzo ya muda mfupi na ya muda mrefu ya mameneja /watendaji wa TANLITS,TEHAMA na wataalamu wengine juu ya usimamizi wa kanzidata, programu ya kompyuta, uhandisi wa kompyuta na usimamizi wa mfumo.<br>• Kuandaa na kusambaza machapisho ya vifaa vya uhamasishaji wa umma kuhusu TANLIT ikiwa ni pamoja na kutumia machapisho, magazeti, vipindi vya redio na kufanya mikutano ya uhamasishaji na warsha ili kulenga wadau katika mikoa 25 |
| **Katika ngazi ya halmashauri** |
| • Kutambua mapungufu ya elimu kwa umma / binafsi kwa watoa huduma za ugani za mifugo katika Halmashauri zote, kukuza huduma za kibinafsi za kiufundi (ufugaji, huduma za afya, nk). |
| • Kutoa vifaa vya ugani yakiwemo, magari 147 na pikipiki 4000 katika Serikali za Mitaa 147, mafunzo ya wakulima 294,000 na teknolojia bora za uzalishaji wa mifugo kwa Halmashauri zote.<br>• Kuanzisha vituo 147 vya maendeleo ya rasilimali za mifugo katika Halmashauri zote<br>• Kuendeleza matumizi ya TEHAMA katika kutoa taarifa na ushauri kwa wafugaji |
| • Kuwezesha mamlaka za Serikali za Mitaa 147 kuhamasisha uanzishaji na kuimarisha vikundi vya wakulima, mashirika, na vyama vya ushirika |
| • Kuwajengea uwezo wafugaji 30,700 juu ya ujuzi na usimamizi na ujasiriamali.<br>• Kutoa mafunzo kuhusu ufuatiliaji wa utambulisho wa mifugo kwa maafisa utambuzi na ufuatiliaji wa Hal mashauri 165 na maafisa mifugo 25 ngazi ya mkoa na kuwezesha waendeshaji wa TANLITS katika halmashauri 147 za serikali ya mitaa katika shughuli za TANLITS na mtandao wa mawasiliano.<br>• Msaada wa vifaa vya ufungaji na mpango wa TANLITS kwa kutoa vibali vya machinjio na kuuza nyama nje. |

**Jedwali Na. 23: Shughuli za Kipaumbele za huduma za ugani wa uvuvi**

| Maeneo ya uwekezaji |
|---|
| **Kitaifa / kikanda**<br>1. Kuboresha ushirikiano kati ya watoa huduma wa ugani.<br>2. Kuongezea utaalamu kwa maafisa ugani wa uvuvi na wavuvi / wafugaji wa samaki.<br>3. Kuimarisha uzalishaji bora wa chakula cha samaki na vifaranga vya samaki.<br>4. Ukarabati wa miundombinu iliyopo.<br>5. Kujenga uwezo kwenye matumizi ya teknolojia mpya na kuwezesha matumizi ya vifaa.<br>6. Ujenzi wa viwanda vya kusindika Dagaa kutoka maji baridi na chumvi.<br>7. Kuimarisha huduma ya kuhifadhi (kugandisha barafu na chumba cha baridi) katika Ziwa Tanganyika. |

| Maeneo ya uwekezaji |
|---|
| **Ngazi ya halmashauri** |
| 1. Kuunga mkono sekta binafsi katika ushiriki wa utoaji wa huduma za ugani wa uvuvi / ukuzaji viumbe kwenye maji.<br>2. Kuanzisha na kuimarisha vyama vya wavuvi na wafugaji wa samaki (maji na mtumiaji ardhi).<br>3. Kuendeleza na kuimarisha miundombinu-rasilimali katika vituo vya huduma za ugani za uvuvi na wa ukuzaji wa viumbe kwenye maji.<br>4. Kuimarisha utoaji wa huduma za kiufundi kwa ajili ya wavuvi / wafugaji wa viumbe kwenye maji samaki. |

151 **Mafunzo. Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (*Livestock Training Agency-LITA*)** ni kati ya wakala watatu chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Wakala wa Utendaji Kifungu Namba 30 ya 1997 na marekebisho yake Septemba 2011. LITA iliundwa kutokana na kuunganisha Taasisi sita za Mafunzo ya Mifugo (*Livestock Training Institutes-LITIs*) ambazo zilikuwa ni Tengeru, Mpwapwa, Morogoro, Madaba, Buhuri na Temeke. Mwaka 2013 na 2014 vituo vya Mabuki na Kikulula vilianzishwa. Jukumu kubwa la LITA ni kutekeleza malengo ya maendeleo ya mifugo kama ilivyoelezwa katika Sera ya Taifa ya Mifugo (2006) na mipango ya kimkakati ya wizara. Shughuli kuu ya LITA ni kutoa mafunzo ya ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa kozi ya Afya ya Mifugo na Uzalishaji katika NTA ngazi ya 4 - 6 na pia inatoa mafunzo mbalimbali maalumu kwa wateja / wakulima. Kozi fupi ni pamoja na; Uzalishaji wa ndege (Kuku), Ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, Usindikaji wa maziwa, Ufugaji wa ng'ombe wa nyama, Uzalishaji wa malisho, utunzaji na ujasiriamali wa ngozi na kwato . LITA inatoa mafunzo kwa kulenga Elimu na Mafunzo ya Ustadi (CBET) ili kuhakikisha uzalishaji wa wahitimu wenye uwezo ambao wanaweza kuajiriwa na Serikali, Sekta binafsi au kujiajiri na hivyo kuchangia maendeleo ya sekta ya mifugo na uchumi wa taifa. Msingi wa huduma bora za ugani ni kuimarisha miundombinu, vifaa vya kufundishia na kuboresha mtaala.

152 Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi *(Fisheries Education and Training Agency- FETA)* ulianzishwa kwa kuunganisha Kituo cha Maendeleo ya Uvuvi cha Mbegani na Taasisi ya Uvuvi wa Maji Baridi Nyegezi. Jukumu kuu la Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi ni kuisaidia Wizara katika: (i) Utoaji wa elimu ya uvuvi na mafunzo kuhusu ukuzaji viumbe kwenye maji, usimamizi na teknolojia za uvuvi ; na (ii) Kufanya utafiti na kushauri katika kukuza maendeleo endelevu ya sekta zinazoendana na uvuvi. Mpango huu utahamasisha upatikanaji wa huduma za umma na binafsi kwa wafugaji wa viumbe kwenye maji, wavuvi wadogo na kampuni za kibiashara na wadau wengine, ambao ni watoaji wakubwa wa elimu na mafunzo bora ya uvuvi na, kuboresha huduma za ugani, kuendeleza teknolojia ya uvuvi na kukuza ufugaji wa viumbe kwenye maji kupitia maonesho na ushauri wa vitendo.

153 Kwa pamoja LITA na Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi wanatekeleza kazi za taasisi za mafunzo ya mifugo na uvuvi (LITIs na FTIs) pamoja na kazi nyingine zinazoonyeshwa kwenye muundo wa nyaraka zao, ikiwa ni pamoja na: (i) Mafunzo, utafiti na ushauri kwa maeneo ya kusimamia na kuratibu mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi, utafiti wa vitendo na huduma maalum za ushauri; (ii)

Huduma za kusaidia uzalishaji wa mifugo, bidhaa za mifugo na mazao mengine ya kilimo; na (iii) Huduma za msaada wa kibiashara kwa wakala katika maeneo kama vile utawala, usimamizi wa rasilimali watu na fedha, uuzaji wa huduma za wakala na bidhaa na usimamizi wa mali ili kukidhi mahitaji ya wateja.

**Jedwali Na. 24: Shughuli za kipaumbele na maeneo ya uwekezaji katika mafunzo ya mifugo na uvuvi**

| A) MIFUGO: kufundisha wataalam kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya mifugo |
|---|
| a. Kujenga uwezo wa wafanyakazi, mapitio ya mitaala na mipango ya mafunzo na LITA kupatiwa vifaa kwa ajili ya kutoa mafunzo ya mifugo.<br>b. Kutoa mafunzo kwa wafugaji 100,000 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu teknolojia za kuboresha mifugo.<br>c. Miundombinu ya mifugo: kwa mfumo wa fadhili, jenga na karabati vituo vya mafunzo 8 vya LITA<br>d. Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa wizara: kuwezesha wafanyakazi wa DRTE na LITA kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ziara za mafunzo na warsha za mafunzo kwa mwaka |

| B) UVUVI:Kufundisha wataalam kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya uvuvi |
|---|
| 1. Kujenga uwezo wa taasisi za mafunzo<br>2. Kuimarisha utoaji wa taarifa na vifaa vya mafunzo<br>3. Kufadhili matengenezo ya miundombinu ya taasisi za mafunzo<br>4. Kuimarisha miongozo ya mafunzo<br>5. Kufadhili mpango wa Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi kuhusu uchambuzi wa mnyororo wa thamani, utambuzi wa mapungufu ya teknolojia, uwezekano wa kuongeza thamani na kukabiliana na vikwazo vya masoko katika mnyororo wa thamani wa dagaa<br>6. Ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za mafunzo<br>7. Kuendeleza miamba bandia kwa ajili ya marejesho endelevu ya samaki waliomalizika na kuimarishwa kwa kilimo cha mwani katika eneo la pwani, Tanzania |

### Eneo dogo 2.2: Upatikanaji wa pembejeo za kilimo na huduma za afya ya mimea na mifugo

154 Jitihada za Serikali kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo za Kilimo *(National Agricultural Input Voucher Scheme - NAIVS)* kwa ajili ya kuongeza upatikanaji na matumizi ya mbegu bora na mbolea zinazotolewa na mtandao mkubwa wa mawakala zimeimarisha matumizi ya mbegu bora na mbolea kwa wakulima wadogo suala hili linahitaji ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na: (i) Ruzuku za pembejeo ; (ii) Kubuni mfuko wa mkopo wa pembejeo za kilimo unaotumika kwa mahitaji ya wakulima wadogo; (iii) Kuwezesha wafanyabiashara binafsi wa kilimo kuimarisha mtandao wao wa biashara ili kuongeza upatikanaji wa pembejeo bora; (iv) Huduma bora ya ugani na mafunzo ili kuongeza kasi ya matumizi ya teknolojia mpya; (v) Huimarisha usimamizi wa rutuba ya udongo, hususan katika matumizi ya mbolea zisizo na kemikali pamoja na shughuli za mifugo; na (vi) Kuimarisha mifumo ya kitaifa ya mbegu inayoshirikisha vituo vya utafiti , Wakala wa Mbegu za Kilimo, Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania *(Tanzania Official Seed Certification Institute- TOSCI)*, wazalishaji na wasambazaji binafsi wa mbegu za kilimo.

155 Uzoefu wa utoaji wa ruzuku katika kuongeza tija kwenye mazao unaweza kutumika katika teknolojia za mifugo ikiwa ni pamoja na: (i) Kuongezeka kwa upatikanaji wa Uhimilishaji (kwa ajili ya kuboresha nasaba za mifugo ya asili; (ii) Kuboresha afya ya mifugo kupitia njia za kudhibiti na kukomesha magonjwa na wadudu (k.m., chanjo, majosho, dawa za mifugo); na (iii) Usambazaji wa mbegu za malisho kwa ajili ya kuboresha ranchi, kuzuia mmomonyoko wa ardhi, nk. Kwa ajili ya kuendeleza ufugaji wa samaki na upatikanaji wa vifaranga vya samaki, ruzuku kwa vifaranga vya samaki vilivyothibitishwa na chakula inaweza kuzingatiwa kupitia ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) katika uzalishaji wa vifaranga vya samaki na vyakula.

156 **Lengo ni kuongeza upatikanaji na ufanisi katika matumizi ya pembejeo za kilimo** (yaani, mbegu, miche, na mbegu bora za mifugo, vifaranga vya samaki , mbolea, chakula cha mifugo na dawa za kilimo) kwa kuongeza idadi ya wakulima wadogo, ambayo itasaidia kuongezeka kwa uzalishaji na tija ya bidhaa za kipaumbele kwa ajili ya mazao, mifugo na uvuvi. Kadri wakulima wanavyoongeza matumizi ya teknolojia kwa ajili ya kuongeza ufanisi, kipato na ustahimilivu, ndivyo uhakikishwaji wa uwepo na upatikanaji wa pembejeo muhimu unavyohitajika. Kwa hiyo usaidizi wa sekta ya umma utawezesha na kudhibiti upatikanaji mkubwa wa pembejeo bora za kilimo (mbegu, aina ya mifugo, nk) kwa mkulima zitakazouzwa na kusambazwa kupitia ushindani wa sekta binafsi.

157 Msaada maalum utazingatia minyororo ya thamani ya mazao ya kipaumbele katika makundi ya wilaya yaliyochaguliwa, na utajumuisha maeneo ya utekelezaji yafuatayo:

*i.* *Kusaidia upatikanaji wa mbegu bora za mazao* kwa kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi (ikiwa ni pamoja na vikundi vya wakulima) katika minyororo ya usambazaji wa mbegu. Msaada huu unalenga katika uzalishaji mkubwa na usambazaji wa mbegu kwa mazao ya kipaumbele ili kuhakikisha upatikanaji wa kiasi cha kutosha cha mbegu bora kwa watumiaji. Shughuli kuu zitakazogharimiwa ni pamoja na: (a) Kusaidia wazalishaji na wasambazaji wa mbegu na kutoa msaada wa kitaalamu kwenye sekta binafsi za mbegu, (b) Kuunga mkono Chama cha Wafanyabiashara wa Mbegu Tanzania (TASTA) na mfumo wa taarifa za soko la mbegu (mahitaji ya mbegu na utoaji wa aina na bei); (c) Kuimarisha uwezo wa majukumu ya TOSCI (d) Kuwezesha kitengo cha mbegu wizarani kwa ajili ya ufuatiliaji wa mkakati wa maendeleo ya mbegu wa sekta na kuandaa mipango na tathmini ya mwaka ya mbegu katika sekta inayohusisha wadau wote; (e) Wakala wa Mbegu za Kilimo kuzalisha mbegu za msingi kwa ajili ya uzalishaji wa aina tofauti; na (f) Kusaidia wakulima/ taasisi binafsi kuzalisha mbegu kwa wingi, ikiwa ni pamoja na vikundi vya wakulima wa Mbegu za Daraja la Kuazimiwa.

*ii.* *Kuboreshwa kwa upatikanaji wa pembejeo bora za mazao* (mbegu, mbolea, madawa ya kilimo na zana) kwa kuimarisha mifumo ya usambazaji wa pembejeo kitaifa na kiwilaya inayotekelezwa na mtandao wa mawakala wa pembejeo za kilimo. Shughuli zitajumuisha: (a) Kuimarisha uwezo wa kiufundi, kuwalinda kibiashara mawakala wapatao 1,000 katika maeneo yaliyopangwa; (b) Majaribio ya kutumia teknolojia za kisasa kwa wasambazaji wa mbegu na wagani katika ngazi ya halmashauri (wasambazaji 5-10 kwa wilaya iliyochaguliwa); (c) Kuimarisha uwezo wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA); (d) Kuchochea ushirikiano (kilimo cha mkataba, nk) kati ya vikundi vya wakulima na wafanyabiashara wa kilimo katika mnyororo wa thamani wa mazao yaliyochaguliwa kwa ajili ya uzalishaji na mfumo wa masoko endelevu (mifumo ya stakabadhi); na (e) Kuhamasisha matumizi ya kilimo hifadhi na kuhusisha usambazaji wa pakiti za mbegu na pembejeo nyingine kwa uzalishaji bora, pamoja na mazao yenye lishe bora kama vile mikunde na mazao ya matunda, mbogamboga na maua.

*iii.* *Uzalishaji wa mbegu bora za malisho* ili kuongeza tija na uzalishaji wa vyakula bora vya mifugo kwa lengo la kukabiliana na ongezeko la idadi ya mifugo na matokeo husika kiuchumi na kimazingira. Uwekezaji kwa mifugo illiyoboreshwa unahitaji kwenda sambamba na uwekezaji wa kuendeleza malisho katika kanda za kilimo husika ili kuongeza tija na kuchangia mapato ya wafugaji. Kuingiza mikakati ya kuendeleza malisho katika mfumo wa kilimo na teknolojia ya uzalishaji wa hei itachangia katika kuongeza upatikanaji wa malisho ya kutosha na ya ziada kwa mwaka mzima.

*iv.* *Uzalishaji wa madume ya ng'ombe na mbegu bora za ng'ombe kwa ajili ya kuboresha mifugo ya asili.* Lengo la kupandisha kwa vikundi vya wakulima vya utafiti vilivyochaguliwa ni kuboresha uwezo wa utoaji wa maziwa kwa ng'ombe wa asili kwa kutumia mbegu za kisasa na asili, huku wakizingatia kiwango cha juu cha kukabiliana na rasilimali asili na chakula cha mifugo na mazingira kwa ujumla. Ili kukabiliana na mahitaji ya wafugaji, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, Mpwapwa iligawa madume aina ya Mpwapwa yaliyoboreshwa 640 na ng'ombe 780 kati ya mwaka 2006 na 2015, ambayo baadhi yalitumika kupandisha ng'ombe wa aina tofauti. Mahitaji ya sasa ni: (a) Kuzalisha ng'ombe bora ambayo majike yatakuwa na uwezo wa kutoa lita 2,800 za maziwa kwa mwaka katika maeneo yenye mvua za wastani nchini Tanzania; (b) Kuongeza uzalishaji wa mitamba bora na madume ili kukidhi mahitaji ya wafugaji wa ng'ombe bora aina ya Mpwapwa na mchanganyiko wake (c) Kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za ng'ombe kwa njia ya Uhimilishaji kutoka katika vituo vinavyozalisha mbegu.

v. *Uzalishaji wa vifaranga vya samaki kwa ukuzaji wa viumbe kwenye maji.* Ufugaji wa samaki na viumbe vingine katika maji baridi na maji bahari unakuwa na mchango muhimu wa chakula duniani na usalama wa lishe, lakini pia kwa kuboresha maisha na ajira vijijini . Kutokana na kupungua kwa upatikanaji wa samaki na kwa kuongezeka kwa idadi ya watu, ustawi wa kiuchumi na wa mazingira endelevu ya nchi kavu na baharini, ukuzaji wa viumbe unahitaji kuendelezwa nchini Tanzania. Hii ina maanisha kuongezeka kwa upatikanaji wa pembejeo za ukuzaji viumbe kwenye maji (mbegu, vyakula, mbolea zisizo na kemikali), na kuhamasisha teknolojia sahihi za ukuzaji viumbe kwenye maji, kuimarisha huduma za ugani na mafunzo. Shughuli za utekelezaji za kipaumbele ni pamoja na: (a) Maangulio ya mayai ya Sato, Mwatiko, Kambare na Kaa; (b) Chakula na kuendeleza uzalishaji wa aina ya samaki waliochaguliwa; (c) Uendelezaji wa ufugaji wa Kamba kwa makundi ya wafugaji wadogo wa Pwani; (d) Kufuga samaki kwa njia ya vizimba katika maeneo yaliyochaguliwa ya umwagiliaji; (e) Kuhamasisha maendeleo ya ufugaji wa aina za asili; na (f) Kuhamasisha uongezaji wa thamani wa zao la mwani.

**158 Ruzuku ya pembejeo.** Mpango wa Taifa wa Utoaji wa Ruzuku za Pembejeo (NAIVS/AFSP 2008-2014) ulitekeleza ruzuku ambayo ilichangia kuongezeka kwa uzalishaji wa ziada wa tani milioni 2.5 za nafaka, kupitia ongezeko la zao la mahindi (kilogramu 433 kwa ekari) na mpunga (kilogramu 263 kwa ekari). Mbali na changamoto nyingi, kiwango cha mwisho cha kiuchumi (ERR) cha NAIVS kilikadiriwa kuwa asilimia 53.5. Tathmini ilibaini kuwa karibu theluthi mbili ya walengwa milioni 2.5 waliendelea kununua mbegu bora wakati theluthi moja iliendelea kununua mbolea kwa bei za soko, baada ya kipindi cha utekelezaji kukamilika. Zaidi ya hayo, pamoja na kuongezeka kwa ufahamu wa matumizi ya pembejeo za kilimo, NAIVS pia iliimarisha mifumo ya uzalishaji wa mbegu na uhusiano baina ya wakulima na mawakala kwa kuwapa mafunzo kuhusu matumizi ya pembejeo.

159 Hata hivyo, kwa kuzingatia gharama kubwa za uwekezaji, Serikali ilijaribu kuandaa mpango wa kufuatilia utoaji wa mikopo ya ruzuku kwa wakulima wadogo kwa kulipa benki tofauti kati ya kiasi cha riba ya kibiashara ya asilimia 18 na riba ya programu ya asilimia 4. Aidha, Serikali imekubali kulipa benki za kibiashara asilimia 50 ya thamani ya mkopo kama dhamana dhidi ya mkopo. Wakulima walitarajiwa kutoa asilimia 20 ya gharama za pembejeo (dhidi ya asilimia 50 katika NAIVS), na kuacha benki kubeba asilimia 30 iliyobaki ya gharama. Wakulima wanatarajiwa pia kukubaliana na kuuza mazao yao kupitia wafanyabiashara waliothibitishwa au ghala, na kuruhusu mabenki kulipwa kwanza. Masuala kadhaa, ikiwa ni pamoja na riba ndogo ya benki na kuchelewa kwa ufadhili wa Serikali katika utekelezaji wa mpango huo ulipunguza kasi ya kuanzishwa na kusambaa kwenye maeneo mengine .

### Pembejeo za mazao (mbegu, mbolea na madawa ya kilimo)

**160 Mbegu.** Mahitaji ya soko la mbegu bora katika nchi yanakadiriwa kuwa tani 60,000 kwa mwaka, wakati upatikanaji wa mbegu bora kwa sasa (hasa mahindi na mpunga) ni tani 35,352. Aidha, inakadiriwa kuwa ni asilimia 25 tu ya wakulima wanatumia mbegu bora, vilevile upatikanaji na uwepo wa mbegu bora, na ufahamu juu ya aina bora / matumizi ya teknolojia zinazofaa katika hali ya mazingira ya kilimo chao bado ni mdogo.

**161 Mbolea na madawa za kilimo.** Ingawa matumizi ya mbolea yaliongezeka na mitandao ya usambazaji binafsi kuanzishwa kupitia mfumo wa vocha, kiwango cha matumizi ya mbolea bado ni kidogo, hasa kwa mbolea ya msingi. Utunzaji wa rutuba ya udongo unahitaji kuunganishwa kwenye utafiti kama huduma za ugani kwa matumizi bora zaidi ya mbolea wakati wa kuongeza rutuba na afya ya udongo. Aidha, matumizi ya dawa za mimea (dawa za kuua magugu na wadudu, nk) hayatoshelezi na hivyo mafunzo kwa wasambazaji wa pembejeo na wakulima na ushauri wa kitaalamu unahitajika ili kuwezesha matumizi mazuri, endelevu na matumizi salama ya dawa za wadudu zilizopendekezwa.

**162 Kuimarisha upatikanaji na matumizi bora ya mbegu na mbolea kwa wakulima wadogo.** Malengo ya utekelezaji ya wakulima yatafanikiwa kwa: (i) Kuimarisha ufahamu wa wakulima juu ya mbegu bora na mbolea (vipeperushi, redio / runinga, mafunzo, majaribio, nk); (ii) Kuongeza uzalishaji wa mbegu za daraja la kuazimiwa, hasa kwa aina ambazo hazizalishwi na sekta binafsi, kutoa mafunzo, kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za msingi na zana ndogo za kilimo; (iii) Kuimarisha mtandao wa mawakala wa pembejeo; (iv) Kuimarisha Wakala wa Mbegu za Kilimo na kuimarisha biashara ya mbegu binafsi na wakulima na uzalishaji wa mbegu bora (kushirikiana na vituo vya utafiti vya kilimo); (v) Kusaidia kamati ya mbegu ya kitaifa na kamati zinazopitisha aina mbalimbali za mbegu;

(vi) Kuwezesha chama cha wafanyabiashara wa mbegu na kubadilishana taarifa katika sekta hiyo; na (vii) Kuimarisha huduma za udhibiti na uhakika wa ubora wa pembejeo za kilimo.

163 **Kuzingatia ufanisi wa kiuchumi kwa lengo la ruzuku, Serikali ya Tanzania itasimamia mzunguko wa ruzuku ya pembejeo,** lakini malengo na taratibu bado hazijafafanuliwa. Ingawa vocha za kielektroniki hurahisisha utekelezaji (ikiwa ni pamoja na kupunguza viwango vya ruzuku kwa muda), kufuatilia na uendeshaji. Aidha, mbinu kama hiyo inaweza kutumika kwa pembejeo nyingine kama vile dawa za kilimo zikiwemo dawa za mifugo (kwa mfano, dawa za kuogeshea mifugo) na pia huduma kama vile matumizi ya zana bora za kilimo (maandalizi ya shamba, miche, upururaji, nk) kusaidia upatikanaji wa mahitaji ya wakulima na maendeleo ya biashara kwa watoa huduma binafsi. Ingawa Mamlaka ya Serikali za Mitaa zitafaidika na ruzuku, kuna haja ya kutoa msaada wa kiufundi kutoka ngazi ya mkoa na ngazi ya kitaifa : (i) Kuandaa mfumo imara wa ruzuku na uliohuishwa; (ii) Kuratibu utekelezaji kati ya wafanyakazi wa umma na binafsi katika ngazi zote, ikiwa ni pamoja na kuweka uhusiano kwenye mnyororo wa thamani wa mazao; (iii) Kutoa ushauri wa kitaalamu na kusaidia wakati wa utekelezaji; (iv) Kuimarisha utafiti wa kilimo na huduma za ushauri ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya pembejeo kwa wakulima kupitia usimamizi jumuishi; na (v) Kutekeleza mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji wa mfumo wa ruzuku.

164 **Kuimarisha huduma za udhibiti wa pembejeo za Kilimo** ili kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora na mbolea. Udhibiti wa ubora wa mbegu unafanywa na TOSCI wakati udhibiti wa ubora wa mbolea unafanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA). Katika makubaliano ya matokeo, TOSCI inahitaji kuungwa mkono zaidi na: (i) Chama cha Kimataifa cha Upimaji wa Mbegu ili kuhakikisha kwamba mbegu zinazozalishwa na kuthibitishwa nchini zinakidhi viwango vya kimataifa, (ii) Kuanzishwa kwa vituo vipya huko Mtwara (Kusini) na Tabora (Kati) mwaka 2019; (iii) Kutoa mafunzo kwa wachunguzi wa mbegu katika ngazi ya wilaya (iv) Kuwezesha vifaa vya ofisi na maabara, Msaada wa TFRA utajumuisha: (i) Kuwezesha majengo ya ofisi ya Wizara ya Kilimo ili kutoa huduma zake kwa ufanisi; (ii) Kuimarisha maabara ya kupima mbolea na udongo katika Taasisi ya Utafiti ya Mlingano; (iii) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa TFRA na wakaguzi wa mbolea katika ngazi ya wilaya; na (iv) Kutoa mafunzo na kuajiri wakaguzi.

165 Mfumo wa udhibiti unahitaji kuimarishwa ili kudhibiti ubora na uhifadhi bora wa bidhaa na mabaki yake. Shughuli za uhifadhi zinatakiwa pia kuhusisha ofisi ya msajili wa dawa za wadudu na Huduma za Afya ya Mimea (*PHS*) ambayo ndiyo inawajibika kutekeleza Sheria ya Udhibiti wa mimea inayohusika na usimamizi wa dawa za wadudu. Aidha, kama sehemu ya kuhakikisha ufahamu wa wadau juu ya sheria zilizopo, inatarajiwa kuwa mafunzo kwa watekelezaji wa sheria kwenda sambamba na kuwajengea uelewa wadau na ufuatiliaji wa sheria.

166 **Huduma za Afya ya mimea** ina lengo la kupunguza kiwango cha upotevu wa mazao kabla na baada ya kuvuna hasa kutokana na milipuko ya wadudu kama vile nzige wekundu na kwelea kwelea. Udhibiti na utafiti hufanywa na Serikali na mashirika ya kimataifa kwa pamoja. Majukumu ya Huduma za Afya ya mimea ni pamoja na udhibiti wa milipuko ya wadudu, kuhamasisha Udhibiti Jumuishi wa Wadudu (IPM) na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa mimea ili kudhibiti uingizaji wa mimea kutoka nje / usafirishaji nje ya nchi, karantini ya mimea na huduma za uhakiki wa ubora wa mimea, kanuni za usajili na usimamizi wa madawa ya wadudu. Uwezo uliopo wa huduma za udhibiti nchini Tanzania una mapungufu kadhaa ikiwemo ya miundombinu na rasilimali watu ambao unatakiwa kushughulikiwa ili kufuata viwango vya mazao.

167 Lengo maalum la shughuli za Huduma za Afya ya Mimea zilizopendekezwa ni pamoja na: (i) Kudhibiti wadudu na magonjwa ili kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya kuvuna; (ii) Kuandaa mikakati na mbinu za udhibiti wa wadudu ambazo zitachochea uzalishaji wa mazao na hifadhi ya mazingira; (iii) Kuimarisha taratibu za udhibiti ambazo zitazuia kuingia na kuenea kwa wadudu ili kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa masoko endelevu ya ndani na nje; (iv) Kuboresha na kuimarisha teknolojia za kuhifadhi dawa za wadudu kwa ajili ya kulinda afya ya binadamu na mazingira; (v) Kutoa michango ya kitaalam kwa lengo la kuhuisha sheria za ubora wa mimea za kanda (Jumuiya ya Afrika Mashariki) na miundo ya kanuni na matumizi yake (v) Kuwajengea uwezo watumishi wa huduma za afya ya mimea (PHS) ujuzi mpya ili kuwawezesha kutoa huduma kwa ufanisi.

168 Maeneo ya utekelezaji kwa ajili ya kufanikisha malengo haya ni: (i) Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa huduma za afya ya mimea (*PHS*); (ii) kuimarisha uwezo wa huduma za kusimamia karantini na ukaguzi ; (iii) Kuimarisha utaratibu za kuorodhesha wadudu na kusimamia takwimu za ufuatiliaji; (iv) Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa dawa za wadudu ikihusisha mabaki ; (v) Kuendeleza na kutumia teknolojia za udhibiti jumuishi wa wadudu (*IPM)*; (vi) kufanya mageuzi ya taasisi ili kuhuisha muundo wa taasisi kisheria (vii) Kuimarisha utoaji wa taarifa za tahadhari mapema, udhibiti na ufuatiliaji wa milipuko ya wadudu; (viii) Kuimarisha udhibiti wa sumu kuvu katika nafaka za chakula na malisho; na (ix) Kuimarisha utoaji wa taarifa za tahadhari mapema na udhibiti wa wadudu wavamizi.

### Pembejeo za mifugo na uvuvi

169 Kiujumla maeneo ya utekelezaji ya vipaumbele kwa kuboresha upatikanaji na matumizi ya pembejeo bora kwa ajili ya uzalishaji wa mifugo na samaki, ikijumuisha mbegu za mifugo/vifaranga vya samaki, pembejeo za uzalishaji na afya/madawa ya mifugo vimeooneshwa katika **Jedwali Na. 25.**

**Jedwali Na. 25: Shughuli za kipaumbele kwa ajili ya upatikanaji wa pembejeo za mifugo / uvuvi**

| Maeneo ya uwekezaji | Shughuli za kipaumbele |
|---|---|
| **CHAKULA CHA MIFUGO/SAMAKI** | |
| **Vyakula vya mifugo na virutubisho kwa ajili ya kuongeza tija** | - Kuhamasisha uzalishaji wa vyakula bora vya mifugo, usindikaji na masoko<br>- Udhibiti wa ubora wa chakula cha mifugo (huduma za maabara).<br>- Kuhamasisha matumizi ya mabaki ya bidhaa za kilimo na viwanda kama chakula cha mifugo.<br>- Upatikanaji wa huduma bora za afya ya mifugo, madawa ya mifugo na vifaa<br>- Kuboresha usalama wa walaji wa bidhaa za mifugo.<br>- Kudhibiti sumu kuvu katika chakula cha mifugo na cha samaki. |
| **Ubora / wingi wa chakula na mbegu za samaki kwa ajili ya kuongeza tija** | - Kuwezesha sekta binafsi kuzalisha vifaranga vya samaki kwa wingi na ubora<br>- Kuboresha miongozo ya uzalishaji chakula cha samaki na ujenzi wa maatamio ya samaki |
| **SHUGHULI ZA KUDHIBITI MAGONJWA YA MIFUGO / SAMAKI NA AFYA YA MIFUGO YA UMMA** | |
| **Udhibiti wa magonjwa ya mifugo yasio na mipaka (kwa ajili ya kuwa na viwanda endelevu).** | - Kuwezesha uthibitishaji wa afya ya mifugo.<br>- Kuimarisha vituo vya kukagua usafi wa mifugo.<br>- Kuimarisha uwezo wa ufuatiliaji magonjwa ya mifugo yasiyo na mipaka (TAD)<br>- Kuimarisha uwezo wa maabara wa kutambua magonjwa.<br>- Kueleweshа umma na kufanya kampeni za chanjo ya magonjwa ya mifugo yasiyo na mipaka ya kipaumbele.<br>- Uwezo wa kutambua taadhari ya mapema na kukabiliana. |
| **Magonjwa ya vimelea na vekta** | - Kuimarisha udhibiti wa magonjwa ya vimelea na kupe (ruzuku kwa ajili ya dawa za kudhibiti kupe).<br>- Kuimarisha chanjo ya kudhibiti ndigana kali.<br>- Ruzuku ya dawa ya kudhibiti kupe kwa ajili ya eneo zima la udhibiti jumuishi wa wadudu.<br>- Udhibiti wa mbung'o na malale.<br>- Kuimarisha uwezo wa maabara kugundua vekta na vimelea. |
| **Afya za Mifugo ya umma** | - Kuimarisha udhibiti wa magonjwa yanayoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama ili kulinda afya ya binadamu.<br>- Kuongeza uelewa kwa umma juu ya magonjwa yatokanayo na wanyama.<br>- Kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa yanayotokana na vyakula. |
| **Bidhaa za samaki wanaofugwa** | - Kutekeleza ufuatiliaji wa magonjwa ya samaki na viumbe vingine kwenye maji.<br>- Ufuatiliaji wa samaki wanaofugwa na magonjwa mengine ya viumbe vingine kwenye maji.<br>- Mafunzo juu ya utunzaji wa bidhaa za viumbe wa wanaokuzwa kwenye maji na uchambuzi wa hatari ya kuingiza chakula cha samaki kutoka nje ya nchi.<br>- Mafunzo juu ya kuweka mfumo wa usalama wa mazingira katika mashamba ya mwani na samaki. |
| **SHUGHULI ZA KUDHIBITI MAGONJWA YA MIFUGO / SAMAKI NA AFYA YA MIFUGO YA UMMA** | |
| **Udhibiti wa ubora wa samaki na ulinzi katika uvuvi** | - Kuimarisha maabara ya udhibiti wa ubora ya Nyegezi<br>- Kuimarisha vituo vya ulinzi katika uvuvi<br>- Kujenga uwezo, ikiwa ni pamoja na kutambua na kukabiliana na tahadhari za mapema |

170 **Kuimarisha upatikanaji wa dawa za kuogeshea, dawa za mifugo na chanjo** ili kuhakikisha uzuiaji na ustahimilivu wa magonjwa. Serikali ilianzisha kituo cha uzalishaji wa chanjo kilichopo Kibaha Pwani mwaka 2012. Kituo hiki kwa sasa kinazalisha aina mbili za chanjo: (i) Chanjo ya kudhibiti ugonjwa wa mdondo (takriban dozi milioni 4 kwa mwezi au asilimia 50 ya mahitaji) ; na (ii) Chanjo ya kudhibiti kimeta na chambavu (dozi 10,000 kila mwezi). Uzalishaji kwa sasa ni mdogo kutokana na ukosefu wa vifaa na wafanyakazi wenye ujuzi. Uzalishaji wa chanjo utaboreshwa kwa : (i) Kutoa vifaa maalum kwa ajili ya uzalishaji wa chanjo; (ii) Mafunzo maalum kwa wafanyakazi; (iii) Kujenga na kuimarisha kitengo cha udhibiti wa ubora; na (iv) Kuendeleza miundombinu ya utafiti na uzalishaji wa chanjo. Chanjo za mifugo kwa ujumla zinajulikana kama bidhaa za umma na matumizi yake yataimarishwa vizuri chini ya programu za ruzuku.

171 **Kuimarisha huduma za matibabu ya mifugo kwa:** (i) Kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi ( punguzo la kodi na ruzuku) ili kusaidia jitihada za Serikali katika utoaji wa huduma za uzalishaji wa mifugo na tiba kwenye ngazi ya Halmashauri kwa kuongeza idadi ya majosho ya ng'ombe, vituo vya uhimilishaji *(AI)*, vifaa vya chanjo na utotoleshaji wa vifaranga vya kuku na (ii) Kuhamasisha uanzishwaji wa vituo katika jamii vya kutumia vifaa vya kutotoleshea kuku kwa pamoja, majosho, madume ya ng'ombe ya kisasa, vifaa vya uhimilishaji na chanjo.

172 **Maendeleo endelevu ya uvuvi** yatazingatia mfumo wa kutegemeana wa viumbe hai na mazingira itakayohusisha: (i) Kuendeleza ujuzi kwa ajili ya maendeleo endelevu ya uvuvi; (ii) uhamasishaji na kujenga uelewa miongoni mwa wavuvi; (iii) mapitio ya mpango wa usimamizi wa uvuvi wa baharini; (iv) uendeshaji wa utendaji wa vituo *(MCS)* kwa ajili ya utoaji wa leseni na usajili wa vyombo vya uvuvi; (v) kuongeza thamani ya samaki na bidhaa zake na (vi) usajili na uwezeshaji wa vitengo vyote vya usimamzi wa fukwe, vyama vya wavuvi, nk.

### Eneo dogo 2.3: Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo (AR4D)

173 **Lengo maalum la eneo hili dogo ni kuboresha mifumo ya utoaji wa teknolojia kuendana na mahitaji ya wakulima na soko, ambayo itasaidia kuongezeka kwa tija na uzalishaji wa bidhaa za kipaumbele**. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana ni: (i) Kuboresha mifumo ya utoaji wa teknolojia kuendana na mahitaji ya wakulima na soko ambayo yatasaidia kuongezeka kwa tija na uzalishajii wa bidhaa za kipaumbele; (ii) Kutoa msaada kwenye mfumo wa usambazaji wa teknolojia kupitia uimarishaji wa mahusiano ya huduma za utafiti na ugani; (iii) Kujenga uwezo wa taasisi za utafiti kujitegemea katika suala la raslimali watu, fedha na mazingira (miundombinu, vifaa); (iv) Kuimarisha ushiriki katika utambulisho, utekelezaji na tathmini ya utafiti unaohusisha wigo wa wadau; na (v) kuimarisha ushirikiano wa taasisi za utafiti za kikanda na kimataifa ikiwa ni pamoja na Kundi la Ushauri wa Utafiti wa Kilimo Kimataifa na sekta binafsi.

174 Kuzingatia misingi ya mbinu shirikishi zilizoanzishwa chini ya ASDP-1, uwekezaji kwenye tafiti za kilimo kwa ajili ya maendeleo utajumuisha ajenda zinazotokana na mahitaji ya kiutafiti/ shughuli zinazolenga kipaumbele cha mnyororo wa thamani wa bidhaa za mazao, mifugo na samaki katika kila Kanda za Kilimo za Kiikolojia. Zaidi ya jukumu la ushauri kwa PPP kwa ajili ya utafiti unaofaa na msaada wa kitaalamu, eneo hili dogo litasaidia shughuli za utafiti unaofaa na mahitaji ya kipaumbele ya teknolojia katika mnyororo wa thamani wa bidhaa kwa ajili ya matokeo ya tija, ndani ya mifumo ya uzalishaji endelevu kulingana na:

*i.* *Uboreshaji wa teknolojia kwa ajili ya mteja na mahitaji ili kuongeza uchaguzi wa teknolojia kwa watumiaji,* na kutilia mkazo aina na uchaguzi wa mazao na mifugo, uboreshaji na uendelezaji wa uzalishaji na usambazaji wa mbegu, utunzaji endelevu wa maliasili (udongo na maji), kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi, udhibiti jumuishi wa wadudu, udhibiti jumuishi wa magonjwa na uhifadhi baada ya kuvuna, ikiwa ni pamoja na mahitaji ya mteja ya kuongeza thamani, masuala ya lishe na kupunguza upotevu baada ya kuvuna. Mifuko ya fedha za Utafiti wa Kilimo na Maendeleo kikanda, iliyoanzishwa kipindi cha ASDP-1, itatumika kutoa misaada ya kifedha kwa miradi ya kilimo kwa kuzingatia mnyororo wa thamani wa mazao ya kipaumbele. Mfuko huu wa ushindani upo wazi kwa watafiti wa umma na binafsi kufanya utafiti wa mteja, kulingana na vipaumbele vya utafiti wa kanda.

ii. *Ushirikiano na mitandao imara kwa ajili ya utafiti wa mnyororo wa thamani wa mazao ya kipaumbele* katika ngazi za kitaifa, kikanda na za kimataifa kwenye chanzo cha teknolojia zinazotumika . Hii itafanikiwa kwa kuimarisha mitandao na Kundi la Ushauri wa Utafiti wa Kilimo Kimataifa na taasisi nyingine za utafiti za kimataifa, kikanda za umma na binafsi kwenye chanzo cha teknolojia zinazotumika katika mahitaji ya mifumo ya ndani na mabadiliko ya kidunia. Aidha, uratibu na kuunda mtandao wa utafiti wa kilimo kwa ajili ya maendeleo katika ngazi ya taifa kwenye mnyororo wa thamani wa mazao yaliyolengwa na maeneo mtambuka (chakula na lishe, utunzaji jumuishi wa maliasili, mabadiliko ya tabianchi, masuala ya kijinsia, nk) utaimarishwa. Hii itatumika kubadilishana taarifa mara kwa mara na jukwaa la utafiti wa mnyororo wa thamani wa mazao ya kipaumbele katika ngazi ya kanda na taifa ikiwemo kuandaa mipango ya utafiti ya mwaka, mapitio ya programu na kufanya tathmini na wadau kwa pamoja.

iii. Kuboresha upatikanaji wa teknolojia bora kwa watumiaji kwa kuimarisha uhusiano kati ya utafiti na ugani na usimamizi wa taarifa za kiuchumi na kiufundi pamoja na usimamizi wa habari na mawasiliano. Hii itafanikiwa kupitia kitengo cha ushirikiano na usambazaji wa teknolojia (TTPU) na usimamizi bora wa taarifa za kilimo na mawasiliano ya teknolojia zilizopo. Timu za TTPU (wataalam wa mazao/mifugo na habari) zitawezeshwa kufanya kazi kama kiungo imara kati ya timu za utafiti za kikanda na Jukwaa la wadau wa mnyororo wa thamani wa zao katika Wilaya (DCP) na maafisa utafiti wa mazao, mifugo na samaki. Uwezo wa utoaji huduma kwa timu za TTPU katika kila Kanda ya Kilimo ya Kiikolojia utaimarishwa kwa kuongeza uwezo wa wafanyakazi na kiufundi kushughulikia maarifa na uhusiano kati ya mtandao wa utafiti wa Kanda ya Kilimo ya Kiikolojia na timu ya uwezeshaji ya kilimo ya Wilaya kwa ajili ya mazao na mifugo, pamoja na jukwaa la wadau wavumbuzi kwa ajili ya mnyororo wa thamani wa mazao ya kipaumbele. Orodha ya teknolojia ya kanda itaboreshwa na kusambazwa wakati mpango wa utafiti wa shamba pamoja na majaribio yatatolewa kwa mnyororo wa thamani wa mazao yaliyolengwa katika makundi ya wilaya yaliyochaguliwa. Uwezo wa kiuchumi wa jamii utaunganishwa katika timu za kitaalam ili kuzalisha ujuzi zaidi juu ya tabia za kiuchumi za kijamii katika mifumo ya kilimo, chaguzi za sera ndogo ndogo, ufanisi wa soko na matokeo yanayotokana na matumizi makubwa ya teknolojia bora kwa wakulima.

**Jedwali Na. 26: Vituo vya utafiti wa mazao na mifugo katika Kanda za Ikolojia za kilimo**

| Kanda za Kilimo ya Kiikolojia (AEZ) | Utafiti wa Mazao | Utafiti wa Mifugo/uvuvi | |
|---|---|---|---|
| | | TALIRI | TAFIRI |
| Kame | Selian na HORTI Tengeru | Mpwapwa, Mabuki na Kongwa | Mwanza na Kigoma |
| Nusu jagwa (Kaskazini na kusini) | Makutupora, Hombolo, Ilonga, Dakawa | Mpwapwa Kongwa, Naliendele | |
| Mashariki na pwani na *alluvial plains* | Mlingano, Mikocheni, Kibaha, Naliendele, Uyole, Katrin Dakawa | Tanga + TVLA DSM (Kibaha na Temeke) | TAFIRI–DSM |
| Miinuko | Uyole, Ukiriguru, Tumbi | (b) Mabuki na Uyole | Mwanza na Mara |
| Nyanda ya kaskazini (bi) | Selian & HORTI Tengeru | West Kilimanjaro | Mwanza and Mara |
| Nyanda ya kusini | Uyole na Kifyulilo | (c) Uyole | Mbeya na Kigoma; |
| Nyanda ya magharibi na kusini magharibi | Maruku na Tumbi | (d) Mabuki | Kigoma |

Ajenda ya Taifa ya Utafiti wa Maendeleo ya Mifugo (2015), Ajenda ya Taifa ya Utafiti wa Maendeleo ya Uvuvi (2015).

iv. *Ufanisi wa usimamizi wa taarifa za kilimo na mawasiliano ya teknolojia zinazopatikana utakuzwa,* kwa kutumia Teknolojia za kisasa za mawasiliano na habari katika ngazi ya kitaifa na halmashauri. Utafiti wa kilimo kwa maendeleo utachangia kwa: (a) kuanzisha jukwaa la kitaifa la ushirikiano wa uvumbuzi kati ya utafiti na ugani wa kilimo, (b) kuingiza taarifa mpya kwenye kanzidata ya teknolojia ya habari, (c) kuendana na taarifa zilizopo za kiufundi kwa mahitaji ya jamii (wakulima, wajasiriamali, taasisi za mafunzo ya kilimo, taasisi zisizo za kiserikali na wengine); na (d)

kuwezesha watumiaji kupata huduma kupitia TEHAMA (mtandao na simu za mikononi) kwa ajili ya kubadilishana taarifa na michakato ya kujifunza. Hii itahitaji uwekezaji katika miundombinu bora ya mawasiliano na rasilimali watu kwa ajili ya kuendeleza ubunifu wa teknolojia ya kuendana na njia za usambazaji.

v. *Kuimarisha taasisi za utafiti (utafiti wa kilimo kwa maendeleo) zilizochaguliwa kuelekea utafiti endelevu* na kuwezesha uendelezaji wa mnyororo wa thamani wa mazao ya kipaumbele kwa: (a) Kuchangia uimarishaji wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI); Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania (TVLA), Taasisi ya Utafiti Mifugo Tanzania (TALIRI) na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), (b) Kuimarisha rasilimali watu kwa ajili ya utafiti na wataalam wa mazao, mifugo na uvuvi, kwa kuzingatia mapungufu ya uwezo na mahitaji ya mnyororo wa thamani wa mazao yatakayobainishwa kupitia tathmini ya mahitaji ya mafunzo (c) Kuimarisha miundombinu ya kipaumbele ya utafiti na vifaa vya maabara ya kanda zilizochaguliwa ARI, TVLA, TALIRI, LITA,, Elimu ya Uvuvi na Wakala wa Mafunzo (FETA) na TAFIRI; (d) Kuimarisha ushirikiano kati ya sekta za umma na binafsi kwa mbinu endelevu za uwezeshaji kwa ajili ya utafiti wa kilimo kupitia ZARDEF; na (e) Kuimarisha mahusiano bora kati ya TTPUs na timu za uwezeshaji za wilaya za mazao, mifugo na uvuvi.

175 **Ufanisi wa upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini** wa utafiti wa kilimo kwa maendeleo ni kigezo muhimu cha ubora wa utafiti. Ushirikishaji wa wadau katika kupanga mipango, pia kuwepo kwa ufuatiliaji na tathmini ni muhimu kwa ajili ya ubora wa tafiti zinazofanyika. Kwa hiyo, ASDP II itafuatilia na kutathmini mipango na mikakati na kiwango cha utekelezaji na ufanisi wa matokeo ya tafiti katika ngazi mbalimbali na kupata mrejesho wa matumizi na matokeo ya tafiti hizo.

176 **Utafiti wa Mifugo na Uvuvi.** Idara ya Uratibu wa Utafiti, Mafunzo na ugani (DRTE) inaratibu utafiti wa mifugo na uvuvi unaotekelezwa kwa mujibu wa mamlaka ya TALIRI, TAFIRI na taasisi nyingine za utafiti kama vile TVLA, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Serikali za Mitaa, bodi za maziwa na nyama, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), Mashirika ya kijamii (*CBOs*) na wadau wengine muhimu wanaofanya tafiti. Uratibu pia umeongezwa hadi kwenye shughuli za ushirikiano za utafiti wa mifugo na uvuvi katika taasisi na mashirika ya kimataifa ya utafiti. Vipaumbele vya utafiti wa mifugo na uvuvi katika Kanda za Kilimo za Kiikolojia vimeainishwa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 27.

**Jedwali Na. 27: Vipaumbele vya Uwekezaji na Maeneo ya Utekelezaji katika Utafiti wa Mifugo na Uvuvi**

| Maeneo ya utekelezaji | Maeneo/shughuli kipaumbele |
|---|---|
| **Ng'ombe wa maziwa** | - Uboreshaji wa teknolojia za uzalishaji wa maziwa wenye tija<br>- Uchaguzi wa mbegu bora, matumizi yake na utunzaji bora wa mifugo ya asili<br>- Uchunguzi wa magonjwa na kuzuia na udhibiti wa ugonjwa / wadudu na vimelea |
| **Ng'ombe wa nyama** | - Kuboresha uzalishaji wa nyama wenye tija /uteuzi, utunzaji wa chembe hai za asili (*germplasm*)<br>- Uchunguzi wa magonjwa na kuzuia na udhibiti wa magonjwa na wadudu na vimelea |
| **Kondoo na mbuzi** | - Kuboresha uzalishaji wenye tija wa kondoo na mbuzi / uchaguzi wa mbegu bora, uhifadhi wa rasilimali na mbegu za asili |
| **Nguruwe** | - Magonjwa na chakula |
| **Kuku (nyama /mayai)** | - Kuzuia na kudhibiti magonjwa na upimaji wa ubora wa malisho. |
| **Malisho** | - Utafiti juu ya malisho na uzalishaji wa lishe |
| **Magonjwa ya mifugo** | - Utafiti juu ya kuzuia magonjwa na kudhibiti / ubora wa chanjo ya magonjwa ya wanyama<br>- Utafiti juu ya wadudu,na vimelea vya ugonjwa; kudhibiti pembejeo za mifugo / mazao<br>- Kutengeneza vifaa vya uchunguzi na vifaa vingine vya kibaiolojia / maabara |

| Maeneo ya utekelezaji | Maeneo/shughuli kipaumbele |
|---|---|
| **Uvuvi** | - Utafiti juu ya idadi ya samaki na tathmini ya vyanzo vya uvuvi, na Sensa ya wavuvi na vyombo vya wavuvi<br>- Athari za shughuli za kibinadamu kwa vyanzo vya maji, ikiwa ni pamoja na uvuvi haramu<br>- Utafiti juu ya kupunguza upotevu baada ya mavuno katika dagaa<br>- Kuboresha teknolojia ya utunzaji, uhifadhi, usindikaji na usambazaji wa samaki na vifaa<br>- Athari za teknolojia mbalimbali za usindikaji kwenye thamani lishe ya samaki<br>- teknolojia ya zana za uvuvi, mbinu na ufundi<br>- Utafiti juu ya kuongeza samaki katika vyanzo vya maji yenye kina kifupi<br>- Mchakato wa masoko na kujifunza juu ya hali ya ulaji wa samaki ndani ya nchi<br>- Mahusiano kati ya Utafiti na ugani |
| **Ukuzaji wa viumbe kwenye maji** | - Uzalishaji wa chakula bora cha samaki na; uhakikia wa ubora wa samaki, aina bora ya samaki wa kufugwa<br>- Kuzalisha samaki, vinasaba, na teknolojia ya viini tete, teknolojia ya vitotoleshi na uhakiki wa ubora<br>- Kuandaa mfumo wa ukuzaji samaki kwenye maji<br>- Mahusiano kati ya Utafiti na ugani |

[a]mambo makuu katika uwekezaji ni ukarabati na uimarishaji wa miundombinu na vifaa vya utafiti (madimbwi, vyumba baridi, vyanzo vya maji, uzalishaji chanjo, vifaa vya usindikaji, nk), kujenga uwezo, na manunuzi ya madume ya ng'ombe, mbuzi dume na jike, kuku na vifaranga vya samaki.

### Eneo dogo 2.4: Upatikanaji wa huduma na matumizi ya zana bora za kilimo

177 Kiwango cha chini cha utumiaji wa zana za kilimo ni kikwazo kikubwa katika kuongeza uzalishaji na tija hasa kwa wakulima wadogo. Juhudi za serikali za kukuza matumizi ya zana za kilimo , ni pamoja na: (i) Kutoa msamaha wa kodi kwa uagizaji wa zana za kilimo na vipuri, (ii) Kutoa ruzuku kwenye mfuko wa pembejeo (AGITF) na dirisha la kilimo katika mabenki kwa mfano Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) na benki ya kilimo ili kupanua wigo wa mikopo kwa ajili ya ununuzi wa matrekta na mashine; (iii) Vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) vinavyofanya vizuri vinatoa mikopo kwa wanachama wake kwa ajili ya kununua zana za kilimo. Katika mfumo huu, ASDP II inapendekeza mambo yafuatayo yafanyike: (i) Kushirikiana na sekta binafsi kuhamasisha matumizi ya zana za kilimo kupitia maonesho ya teknolojia za kisasa (matrekta makubwa na madogo na zana za kuvunia n.k) na zana rahisi za kilimo kama vile zana za kupalilia na za kupanda mbegu, n.k.; (ii) Kuwezesha utoaji wa huduma za kifedha kwa ajili ya zana za kilimo; (iii) Kusaidia taasisi za elimu kuandaa wahandisi mahiri kulingana na mahitaji ya sekta; na (iv) Kuweka mazingira ya kibiashara mazuri kwa ajili ya kuagiza zana za kilimo na vipuri.

178 Utumiaji wa zana za kilimo ni muhimu katika kukabiliana na tatizo la nguvukazi na uzalishaji mdogo (uzalishaji na baada ya kuvuna) na wakulima wadogo kushindwa kufanya shughuli za kilimo kwa muda sahihi ( kupanda, kupalilia ). Kuongezeka na kukua kwa maeneo ya mazao kunahitaji utumiaji wa zana bora za kilimo ili kuruhusu shguhuli za kilimo kufanyika kwa muda muafaka na kupunguza ugumu wa kazi wakati wa uzalishaji na baada ya kuvuna. Ni muhimu utumiaji wa mashine ukubalike na uwe endelevu, wakati wakulima wakiendelea na utaratibu wa kupata uelewa wa kiufundi na ukubwa wa shughuli za kilimo kutokana na uwekezaji ulioanzishwa wakati wa ASDP-1, uwekezaji zaidi katika zana za kilimo utawezeshwa, ikiwa ni pamoja na vyama vya wakulima na uanzishaji na uimarishaji wa watoa huduma binafsi wanaomiliki zana za kilimo (huduma ya kibiashara) ili kuwa uendelevu. Aidha, ni muhimu kuwawezesha wakulima wadogo kutumia teknolojia zinazopunguza harubu kama vile kulima kwa kutokukwatua ardhi.

179 Hatua ya awali kuhusu utumiaji wa zana za kilimo utalenga katika kujiimarisha kifedha na kiuchumi na kuandaa taratibu /kanuni za kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha kujitokeza kwa sekta binafsi kutoa huduma za matrekta na zana bora. Mpango huo pia utahakikisha kuna sheria ambayo itawezesha kukodisha na kutumia mali zisizo za kudumu kama dhamana kiasi kwamba sekta binafsi itakuwa chombo cha kuwawezesha kuwekeza katika zana za kilimo.

**180 Lengo la ASDP II ni kuwezesha upatikanaji wa huduma na matumizi bora ya zana za kilimo ili kuongeza faida, tija endelevu ya uzalishaji na kuongeza thamani na kipato cha mkulima.**

**Kuwezesha watoa huduma binafsi wa zana za kilimo** ( uzalishaji, uvunaji, usindikaji na usafirishaji) utawezesha wazalishaji wadogo kuongeza tija, kutumia mbinu endelevu za utunzaji wa ardhi, lakini pia kuwavutia wajasiriamali vijana kushiriki katika shughuli za sekta ya kilimo. Upatikanaji wa huduma binafsi za zana za kilimo kwa wakulima wadogo kutaimarishwa na kuboresha mkakati wa Taifa wa uendelezaji wa zana za kilimo, ikiwa ni pamoja na mfumo wa kusimamia kwa ajili ya mpangilio wa huduma binafsi endelevu na wenye faida. Ni muhimu kuwashirikisha wadau na makampuni mbalimbali yanayotoa huduma za matrekta /vifaa, benki za biashara na watoa huduma wa zana za kilimo.

181 **Pamoja nakuwepo kwa sera na mfumo wa kitaasisi wa kupunguza matumizi ya nguvu kazi na kuhamasisha teknolojia (tazama eneo dogo 4.1),** ASDP II itahamasisha njia bora za utunzaji wa mashamba na mazingira ili kupunguza gharama na utumiaji wa pembejeo na gharama, kuhifadhi udongo, mazingira na kuzalisha mazao bora, mifugo, samaki bora na mazao mengine ya mashambani. Shughuli kuu ni pamoja na:

a. *Kuongeza mahitaji ya huduma za zana za* kilimo katika shughuli za uzalishaji na baada ya kuvuna mazao kwa kufanya maonesho, kampeni za uhamasishaji na kutoa ruzuku ili kuongeza uelewa wa wakulima kwa ajili ya uzalishaji endelevu wa kilimo na ukuaji wa tija.

b. *Kuboresha upatikanaji wa aina mbalimbali za zana za kisasa kwa vikundi vya wakulima au vyama vya ushirika* ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa matrekta makubwa na madogo na zana za kukokotwa na wanyamakazi kwa ajili ya uzalishaji, uhifadhi baada ya mavuno na usafirishaji.

c. *Kuwezesha usambazaji wa huduma binafsi za zana za kisasa* kwa ajili ya kuongeza tija na uzalishaji kupitia uimarishaji wa mikataba yenye mafanikio, uzingatiaji wa suala la biashara/mfumo wa biashara unaojirudia na mpya (kukodisha, mikataba kati ya waagizaji kutoka nje ya nchi, taasisi za kifedha na watoa huduma za zana za kisasa n.k.). Usambazaji ambao unahimiza kilimo cha utumiaji wa zana za kisasa kupitia mipangilio ya kukodisha na misaada mingine ya kifedha kwa kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi kwenye uvumbuzi wa teknolojia.

d. *Uendelezaji wa upatikanaji wa taarifa na kufanya tathmini na kuongeza vifaa / mashine* kwa ajili ya utoaji wa huduma za zana za kilimo endelevu, uendeshaji na matengenezo ya vituo vya rasilimali na mafunzo.

182 Mkakati huu utaanzishwa katika mwaka wa kwanza wa Programu na kutekelezwa kuanzia mwaka wa pili na kuendelea kwa kupitia yafuatayo: (i) Kuchochea utoaji wa huduma binafsi za upatikanaji wa mafunzo ya kitaalamu na taarifa ya kiufundi kwa wadau katika mnyororo wa utumiaji wa mashine kwa ajili ya uendeshaji endelevu wa zana za kisasa za kilimo na vituo vya mafunzo ya kilimo; na (ii) Kuongeza mahitaji ya huduma za mbinu za kilimo kwa kutoa ruzuku ili kuwawezesha wakulima wadogo kununua zana hizo kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo (zana za kukokotwa na wanyamakazi/ matrekta ya magurudumu mawili) na upatikanaji wa huduma binafsi za zana za kilimo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji na baada ya kuvuna.

183 Maendeleo ya rasilimali watu na kuanzisha kituo cha kumbukumbu za zana za kilimo yanaweza kutekelezwa kwa njia ya mtandao wa Taasisi za Mafunzo ya Kilimo (ATI) au vituo maalum vya mtandao na ATI zilizochaguliwa ili kutoa mafunzo ya utumiaji wa zana za kisasa za kilimo kwa wataalamu mbalimbali. Hii itasaidia kuondoa matatizo ya uwezo mdogo wakutumia zana, uharibifu wa mashine, marekebisho madogo ya mashine na ukosefu wa vipuri ambayo huchangia kwa wajasiriamali kutokufanikiwa kwenye biashara zao. Ili kuendeleza biashara, lazima kuruhusu waagizaji wa matrekta kutoka nje ya nchi kuanzisha vitengo vya uuzaji na matengenezo. Pia, wawekezaji wa huduma za zana za kisasa wanapaswa kuhimizwa kujiimarisha na kuwa na zana bora za uhifadhi wa kilimo na vifaa kwa ajili ya utunzaji endelevu wa udongo (angalia pia eneo dogo 1.1).

*Matumizi endelevu ya zana bora za kilimo ni pamoja na kuongeza matumizi ya teknolojia zinazopunguza nguvukazi, ikiwa ni pamoja na zana sahihi za uzalishaji ( kilimo hifadhi katika e/d 1.3), kuongeza thamani (angalia e/d 3.3) katika usindikaji wa mazao ya kilimo) na shughuli zingine za utunzaji wa shamba. Hii inalenga utunzaji endelevu wa udongo katika mfumo wa kilimo hifadhi ( angalia pia "Save and grow", FAO 2012)*

### Eneo dogo 2.5: Usalama wa chakula na lishe

184 **Usalama wa chakula na lishe usipozingatiwa katika uzalishaji unaweza kusababisha athari katika afya ya binadamu hasa maeneo ya vijijini.** Uhaba wa chakula unaweza kusababishwa na uzalishaji duni au majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi. Utafiti uliofanyika mwaka 2012 kuhusu usalama wa chakula na upatikanaji wake ulibaini kwamba, mwaka 2010-2011 takribani kaya 730,000 sawa na asilimia nane (8) zilikuwa hazina chakula cha kutosha, kati ya hizo takribani kaya 150,000 (asilimia 2 ya kaya zote) zilichukuliwa kama kaya zenye ukosefu wa chakula uliopitiliza. Aidha, mikoa ya kaskazini na kanda ya kati ya Tanzania iliathirika na kiwango cha ukosefu wa usalama wa chakula katika baadhi ya maeneo kwa asilimia 45. Uzalishaji wa chakula hutegemea sana mvua ya kutosha ambayo pia ni rahisi kukabiliwa na mabadiliko ya hali ya hewa, hasa katika maeneo ambayo hupata mvua kiasi hivyo kusababisha mikoa hiyo kukabiliwa na uhaba wa chakula katika maeneo yao. Hivyo, ni muhimu kutulia mkazo kuzalisha kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji na kuzalisha mazao ya mseto yanayostahimili ukame kwa ajili ya upatikanaji na usambazaji wa chakula.

**Utapiamlo** ni miongoni mwa kikwazo kikubwa katika afya ya binadamu na maendeleo ya kiuchumi: Katika mwaka 2010 (DHS, 2010), utafiti ulibaini kuwepo kwa utapiamlo uliokithiri wa asilimia 42 uliosababisha watoto chini ya umri wa miaka 5 na wanawake wanaonyonyesha watoto wa umri huo kudumaa kutokana na tatizo la utapiamlo. Tanzania ina kiwango kikubwa cha utapiamlo, hasa kwa watoto wanaoishi vijijini katika kaya maskini ukilinganisha na watoto waishio mijini. Hii inatokana na na matumizi duni ya chakula; uelewa mdogo juu ya lishe, maandalizi ya chakula na tabia ya ulaji wa chakula kwa watoto, na majukumu mengi waliyonayo wazazi.

185 **Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula** (NFRA) awali wakala ulianzishwa kwa ajili ya kuhifadhi chakula. Wakala kwa sasa hutumika kuhakikisha bei ya chakula inapopanda, mazao yaliyohifadhiwa na Wakala huingizwa sokoni ili kudhibiti mfumuko wa bei za chakula ili walaji wamudu kununua. Katika mwaka 2014 NFRA ilinunua mahindi kiasi cha tani 300,000 kwa bei ya juu ya soko kutoka kwa wakulima. Kwa upande wa uhifadhi ni muhimu kuondoa mvurugano katika sekta kwa kuepuka kukodisha baadhi ya maghala ya kuhifadhia mazao kutoka sekta binafsi na hivyo kupunguza uwezo wa Sekta binafsi kushindana kutokana na bei ya mazao inavyobadilika.

186 **Masuala ya sera** Ili kuondokana na madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na kupanda kwa bei za chakula na ukosefu wa usalama wa chakula kwa makundi maalum yanayoathirika zaidi ni muhimu kupewa kipaumbele kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi. Serikali ya Tanzania inachukua hatua za kuboresha upatikanaji wa chakula, ikiwa ni pamoja na: (i) Kuimarisha na kuboresha mifumo ya kutoa taarifa za tahadhari mapema kuhusu uzalishaji wa mazao, uliopo kwenye mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za kilimo; (ii) Kuimarisha mfumo wa kuhifadhi chakula na usambazaji wa NFRA ikiwemo uboreshaji wa maghala ya kuhifadhia mazao na ushirikishwaji wa sekta binafsi, (iii) Kusimamia uagizaji wa chakula unaozingatia mahitaji na usambazaji wa chakula; (iv) Kuanzisha na kuendeleza uhusiano mzuri baina ya nchi wanachama katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi Zinazoendelea Kusini mwa Afrika -SADC kwa ajili ya kufuatilia hali ya usalama wa chakula ya kikanda, ikiwa ni pamoja na matumizi ya chakula kulingana na dharura itakayojitokeza katika maeneo hayo.

187 **Jinsi ya kukabiliana na Majanga.** Baadhi ya majanga yanayotokea hapa nchini ni pamoja na ukame, mvua kubwa inayosababisha mafuriko, magonjwa ya wadudu wanao hama hama, magonjwa ya mazao na mifugo, ukataji miti hovyo na uharibifu wa udongo. Uzalishaji wa mazao na ufugaji huathiriwa moja kwa moja na majanga hayo hasa kwa wakulima wadogo kunako sababisha ukosefu wa chakula na hatimaye kuwafanya kuwa maskini wa kupindukia. Athari ya mabadiliko ya tabianchi yanatarajiwa kuongezeka katika nyakati zijazo hivyo hatua stahiki na za haraka zinahitajika kupewa kipaumbele ili kuongeza ustahimilivu katika kilimo (tazama hatua ya kuzuia katika eneo dogo 1.3). Ili kukabiliana na majanga yanayoweza kujitokeza, hatua zinazohitajika kuchukuliwa ni pamoja na: (i) Kuimarisha mfumo wa kutoa taarifa za tahadhari mapema kuhusu hali ya uzalishaji pamoja na mfumo wa kufuatilia na kutambua mapema wadudu na magonjwa yanayojitokeza; (ii) Kuratibu mfumo wa ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za hali ya hewa nchini (iii) Kutumia taarifa za hali ya hewa kwa ufanisi na kujiandaa kukabiliana na majanga; (iv) Kuimarisha ushirikiano wa Taasisi mbalimbali

kuhusu magonjwa yanayoweza kujitokeza ambayo yana sababishwa na wadudu kwa ajili ya kugundua mapema ili kukabiliana nayo; na (v) Kuratibu shughuli/njia mbadala zinazohifadhi mazingira katika sekta ya kilimo na kuhakikisha zinazingatia mahitaji ya kaya maskini na kutafutiwa ufumbuzi.

188 **Lishe.** Utapiamlo mara nyingi hurithishwa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine: utapiamlo kwa wajawazito huathiri vibaya matokeo ya mafanikio ya elimu na kupunguza tija katika utu uzima. Madhara ya utapiamlo yanaongezeka kwa kunywa maji yasiyo salama , hali duni ya usafi, na ukosefu wa taarifa na elimu juu ya lishe bora na usafi wa mazingira. Kufikia usalama wa lishe kunahitajika ushiriki wa sekta mbalimbali, ikiwa ni pamoja na: (i) Kukuza ufahamu miongoni mwa kaya za vijijini, hasa kulenga utapiamlo wa mtoto na wazazi, lishe bora na usafi wa mazingira; (ii) Kutumia zaidi maafisa lishe katika ngazi ya Halmashauri ambao wanaweza kuwa sehemu ya huduma na mafunzo ya ugani katika nyanja ya lishe chini ya wawezeshaji katika ngazi ya Halmashauri; (iii) Kuimarisha na kusambaza urutubishaji wa chakula; (iv) Kutoa mipango ya usalama wa kijamii kwa watu wenye ulemavu ambao huhitaji ulinzi madhubuti dhidi ya majanga (chakula / fedha kwa ajili ya kazi); na (v) Kuimarisha ushirikiano na wizara zinazohusika kwenye mipango ya kutoa chakula mashuleni kwenye maeneo ya vijijini inapohitajika.

189 **Usalama wa chakula na lishe umejumuishwa kwenye sera, mikakati na miradi mbalimbali.** Katika harakati za uhamasishaji wa masuala ya lishe, kuna chombo cha juu cha maamuzi kinachohusika na masuala ya lishe nchini Tanzania kinachoitwa Kamati ya Usimamizi wa Masuala ya Lishe. Chombo hiki kinajumuisha pamoja Makatibu Wakuu kutoka kwenye sekta tisa, washirika wa maendeleo, mashirika ya Umoja wa Mataifa, asasi za kiraia, vyuo vikuu na wafanyabiashara. Kikosi kazi hicho kinajumuisha sekta mbalimbali na husimamiwa na Mkurugenzi kutoka Kitengo cha Taifa cha Chakula na Lishe (TFNC). Wadau /washiriki wote wana husika kikamilifu katika jitihada za kuhamasisha masuala ya lishe na kushiriki katika mpango huo.

190 **Lengo la eneo hili dogo ni kuhakikisha kuwa masuala ya usalama endelevu wa chakula na lishe nchini Tanzania yanahusisha wadau wote katika utekelezaji wa mikakati iliyolengwa ili kuhakikisha usalama wa chakula na lishe katika ngazi zote.** Mkazo utawekwa ili kuhakikisha kuwa chakula kinakuwepo wakati wote kinapatikana na kinatumika kwa matumizi sahihi ya chakula ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa chakula, utunzaji, biashara / masoko na mikakati sahihi / hatua dhidi ya madhara ya majanga yatakayojitokeza. Maeneo ya kimkakati yamegawanyika katika sehemu nne (4) za utekelezaji: (i) Ufuatiliaji wa mazao / mifugo na utoaji wa taarifa za tahadhari ya mapema ili kuongeza usalama wa chakula, (ii) Kuwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya chakula ya kimkakati, (iii) Usimamizi wa mazao baada ya kuvuna kwa ajili ya kupunguza upotevu wa chakula, na (iv) Uchangiaji katika masuala ya kuboresha lishe.

191 **Ufuatiliaji na utoaji wa tahadhari ya mapema kwa mazao na mifugo.** Kuanzia mwaka 1992/1993,Wizara ya Kilimo iliandaa mwongozo wa kufanya tathmini ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kutumia dodoso. Hii iliboreshwa na baadaye mwongozo huu ulitumika katika kukusanya taarifa ambazo zilitumika katika mfumo wa upatikanaji wa taarifa/takwimu.Taarifa hizi zilizopo katika kutoka Ofisi za Taifa za Takwimu (NBS) zinatumika kushughulikia changamoto za makadirio ya wilaya kupitia mfumo wa utoaji wa taarifa. Mfumo huu hapo awali ulitumiwa na serikali katika kutoa taarifa za kukisia hali ya usalama wa chakula na ripoti za hali ya hewa ikiwemo mvua, kupitia Takwimu za Kilimo (AGSTATS). Hata hivyo, mifumo hiyo imekuwa muhimu katika kutoa takwimu za msingi kwa ajili ya usimamizi wa chakula na sekta ya kilimo kwa jumla.

192 **Mfumo wa Uchambuzi wa Uhakika wa Chakula na Lishe (MUCHALI) una jukumu la :** (i) Kukabiliana na athari za upungufu wa uzalishaji wa chakula kwa mwaka na usalama wa chakula na lishe miongoni mwa wakazi katika ngazi ya halmashauri waliotambuliwa na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zinazohusika na usalama wa chakula na lishe; (ii) Kutambua hali ya upatikanaji wa usalama wa chakula na idadi ya watu wasiojiweza/ wenye mahitaji maalum kutokana na tatizo la upatikanaji wa chakula katika mwaka husika na kutathmini ukubwa wa tatizo, na (iii) kutambua na kupendekeza hatua stahiki kwa watu wenye mahitaji maalum katika jamii. Mbinu itakayotumika itahusisha usalama wa chakula na lishe *(LFSN)* inayotumia uainishaji jumuishi wa usalama wa chakula ili kufanya uchambuzi na kutoa taarifa. Mbinu ya *LFSN* inahusisha viashiria vya msingi jumuishi katika uzalishaji wa mazao, mifugo na uvuvi, upatikanaji na bei,lishe, upatikanaji wa maji, mali na mikakati,

na pia vipimo vya hali ya hewa hususan mvua na mifumo mingine ya maisha. Aidha, kiwango cha utapiamlo ndani ya nchi na kimataifa hutambulika. Kwa ujumla, taarifa ya kila mwaka hutolewa kwa wakati muafaka kwa watoa maamuzi. Wakati mwingine changamoto za kupata uhakika/ sahihi wa taarifa hizo zinaendelea kushughulikiwa na kuwekewa msisitizo. Hivyo, kujenga uwezo, mfumo wa kukusanya takwimu za mvua, dodoso 1 (FSQ1) linalotumika kukusanya taarifa zinazohusu usalama wa chakula, mikutano ya ushirikiano na uzoefu, na upatikanaji wa fedha kwa wakati ni masuala muhimu kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji.

193 **Jinsi ya kukabiliana na majanga na ustahimilivu.** Kaya za vijijini zitaendelea kupewa msaada maalum ili kuwa na uhakika wa chakula na kuwalinda dhidi ya majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi, hasa ukame. Ni mategemeo kuwa ASDP II itaendelea kupunguza idadi ya kaya maskini kuendelea kupatiwa misaada ya chakula na kutafutiwa njia mbadala ya kuweza kuishi. Njia mbadala ya kujikinga/kukabiliana na majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi zitaendelea kuboreshwa ili kupunguza vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano na wanawake wajawazito. Fedha za kutosha zitatengwa kwa ajili ya kupunguza majanga na jinsi ya kujikinga na majanga hayo (rejea eneo dogo 1.3). Mipango ya ziada ya kimkakati itakayoainisha njia mbadala za kukabiliana na majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi na jinsi ya kulinda rasilimali za kaya zitaendelea kutekelezwa na kusaidia uwekezaji katika uzalishaji kupitia hatua mbalimbali za ujenzi wa miundombinu ya vijijini, upatikanaji wa masoko, kuboresha kilimo kiwe chenye tija, uelewa/elimu, huduma za afya na huduma nyingine.

194 **Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula na mkakati wa kuhifadhi chakula.** Uwezo wa *NFRA* wa kuhifadhi chakula (kwa bajeti ya matumizi ya kawaida ya serikali) utazingatia yafuatayo: (i) Kiwango cha kuhifadhi (ii) uwazi na taratibu za kupokea na kutoa kiasi cha mzigo uliohifadhiwa, kiasi cha mzigo, mzunguko wa mzigo uliohifadhiwa, na taratibu za kifedha zinazoonesha jinsi mzigo ulivyohifadhiwa; na (iii) sheria na taratibu ya jinsi ilivyoshughulikia suala la upandaji wa bei ya chakula uliojitokeza. Zaidi ya hayo, kiwango cha juu cha stahimilivu wa mifumo ya uzalishaji, uwazi wa masoko ya mazao ya chakula na kuingia mikataba na sekta binafsi inapaswa kuruhusiwa hatua kwa hatua. Uhusiano kati ya *NFRA* na Kitengo cha kutoa Tahadhari ya Mapema ya Mazao (uboreshaji wa mfumo jumuishi) na usahihi wa taarifa/takwimu ikiwa ni pamoja na kiasi kilichohifadhiwa na sekta binafsi na mkulima unahitajika kuimarishwa kwa kubadilishana taarifa/habari.

195 **Kuanzisha mfumo wa tahadhari ya mapema kwa ajili ya mifugo na uvuvi.** Tahadhari ya mapema dhidi ya majanga ya tabianchi ni muhimu kwa kuiwezesha serikali kuchukua hatua muafaka, ili kupunguza/kujikinga na athari kubwa zinazoweza kujitokeza, hususan kwa wafugaji na wavuvi wadogo. Hii inajumuisha utekelezaji wa majukumu ya kipaumbele kama vile: (i) Kujenga uelewa kwa kuweka mikakati ya kupunguza madhara miongoni mwa wafugaji na jinsi ya kujikinga, (ii) Kufundisha na kukusanya taarifa kwenye Halmashauri, (iii) Kuainisha rasilimali fedha zilizopo, kutenga maeneo maalum ya ufugaji na upangaji wa kanda na maeneo salama ya mifugo, na ununuzi wa zana na vifaa, (iv) Kutoa mafunzo kwa watumishi wapya/wanaojiunga, kozi fupi kwa ajili ya watumishi waliopo makao makuu na ngazi za halmashauri (tahadhari ya mapema ya mifugo kwa jamii); (v) Kuongeza vifaa kwa ajili ya ufanisi, uchambuzi wa takwimu na kutoa taarifa;na (vi) Kuwepo na mfumo wa ufuatiliaji wa malisho, maji na rasilimali za chakula cha mifugo wenye ufanisi na gharama nafuu.

196 **Usalama wa chakula cha mifugo na ustahimilivu dhidi ya majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi** (angalia pia eneo dogo 1.3) utaboreshwa kwa (i) Kujenga mabwawa 10, visima 20 na malambo 20; (ii) Kufanya ukarabati wa mabwawa 4, visima 20 na malambo 50; (iii) Jinsi ya uhifadhi na matumizi bora ya malisho; na (v) Kuandaa mipango ya usimamizi wa eneo la malisho katika maeneo tajwa ya malisho kwenye Serikali za Mitaa.

197 **Usimamizi baada ya kuvuna kwa ajili ya kupunguza upotevu wa chakula.** Mifumo ya usimamizi baada ya mavuno inalenga kufikia usambazaji usalama wa chakula na lishe kwa ufanisi na ufasaha katika kushughulikia masuala muhimu kati ya uzalishaji na matumizi ya bidhaa za kilimo. Upotevu mkubwa wa mazao baada ya kuvuna unabaki kuwa ni eneo muhimu linalohitaji kutafutiwa ufumbuzi, kama ambavyo tafiti mbalimbali zilivyoonesha kuwa wakulima hupoteza hadi asilimia 40 ya nafaka zinazozalishwa, hata hivyo upotevu wa mazao unatofautiana kulingana na aina ya mazao na kanda

ya kilimo kijiografia. Masuala makuu yanayosababisha ni uharibifu wa kimaumbo na athari za fangasi, wadudu na panya na mchwa wakati wa usafirishaji, uhifadhi na hasa kwenye bidhaa zenye kuharibika haraka ziposindikwa (tazama eneo dogo 3.2). Hivyo ni muhimu kuboresha na kubainisha maeneo yanayotekelezwa kati ya idara zilizopo kwenye Wizara zinazohusika na masuala ya usalama wa chakula, hasa kwa shughuli zinazohusiana na miundombinu ya kuhifadhi, usimamizi, kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna, kuongeza thamani na usindikaji wa bidhaa za kilimo.

198 **Mchango jumuishi katika uboreshaji wa lishe Mkakati wa lishe kitaifa,** ulikamilishwa na *TNFC* ambao umebainisha uwepo wa kiwango kikubwa cha utapiamlo nchini. Mkakati wa lishe kitaifa unatambua kuwa ongezeko la uzalishaji wa chakula si lazima kutafsiri kuwa ni matokeo ya uboreshwaji wa usalama wa chakula na lishe, kaya lazima pia zipatiwe taarifa na elimu kuhusu mbinu bora za lishe na usafi wa mazingira. Tofauti na kupewa msaada wa dharura wa chakula, hatua za ziada kama vile uzalishaji wa usalama na ulinzi wa mali katika kaya utatekelezwa kutokana na uwekezaji katika miradi inayozalisha chakula na matumizi ya chakula chenye kuzingatia uwepo wa madini muhimu kwa kuboresha viwango vya matumizi ya chakula. Mbinu za uchanganyaji wa vyakula mbalimbali na mabadiliko ya tabia ya ulaji wa vyakula zitaingizwa katika mipango yote ya sekta za maendeleo vijijini, itakayojumuisha utoaji wa elimu ya afya. Mbali na kuzalisha chakula cha zaidi na bora, kaya maskini zinazoishi vijijini, zinapaswa kuelewa jinsi ya kutumia chakula walichonacho kwa kuzingatia hali ya mazingira yaliyopo katika maeneo wanayoishi.

199 **Muungano bora wa milo/vyakula mchanganyiko na mabadiliko ya kitabia ya lishe katika programu ya sekta ya kilimo.** Kaya za vijijini zanapaswa kuelewa umuhimu wa chakula katika ustawi wa jamii na kuwa na elimu ya kutumia chakula walichonacho kwa njia nzuri iwezekanavyo. Katika muktadha huu, kuna mvutano kati ya sera zinazohimiza kilimo cha biashara (mara nyingi hushirikisha ongezeko maalum) hivyo ni muhimu kudumisha mifumo ya kilimo cha mseto na lishe. Aina nyingine ya Sera zinazohusu usalama wa chakula na lishe ni pamoja na usalama wa chakula na viini lishe vilivyopo kwenye chakula: viwango vya sasa vina haja ya kuboreshwa ikiwa ni pamoja na mikrobiolojia, viwango vya kemikali vilivyomo kwenye vyakula, upangaji wa viwango vya ufungashaji, uhifadhi salama na usafirishaji. Usalama wa chakula na viwango vipya vya viini lishe vilivyoko kwenye mafuta ya kula, ngano na unga wa mahindi (na vyakula vingine vya mifugo). Hii pia ni muhimu katika kufikia masoko ya nje na itaongeza ushindani katika soko la ndani. Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo kwa ajili ya usalama wa chakula na lishe ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 28.**

**Jedwali Na. 28: Mapendekezo ya maeneo ya utekelezaji kwa ajili ya usalama wa chakula na lishe**

| Hatua/ eneo | Mapendekezo ya shughuli za uwekezaji |
|---|---|
| **1. Mfumo wa kutoa tahadhari mapema kwa ajili ya usalama wa chakula** | |
| Kuimarisha uwezo wa taasisi wa kazi za kutabiri uzalishaji wa mazao na mifugo na kuboreshwa mazingira ya kazi | i. Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wapya, kozi maalum kwa ajili ya watumishi wanaendelea<br>ii. Kununua vifaa vitakavyoongeza ufanisi katika eneo la kazi, uchambuzi wa takwimu na kujenga uwezo wa uchambuzi kwa watumishi |
| Ukusanyaji wa takwimu za mvua na ufuatiliaji wa mazao | i. Ukaguzi na tathmini kuelekea kuimarisha vituo vya mvua kutimiza mfumo ya tahadhari ya mapemaii. Kukarabati vituo muhimu vya mvua (600) katika nchi nzima. |
| Dodoso la usalama wa chakula kwa utabiri wa mazao na usahihi wa takwimu na uaminifu. | i. Kuboresha na kuweka mfumo wa ukusanyaji taarifa nchini kufuatia kwa kushirikiana na *NBS*<br>i. Kuunganisha mfumo wa *ASS*, *ARDS* na kitengo cha kutoa taarifa ya tahadhari ya mapema<br>ii. NMS kutoa taarifa sahihi ili kuwezesha upatikanaji wa makadirio katika ngazi ya wilaya (kwa sasa makisio ni ya mkoa)<br>i. Kukabiliana na kuimarisha *MUCHALI* kwa wakati mwafaka |
| Kutumia usahihi wa taarifa kwa ajili kufanya maamuzi ya kisera | i. Kuimarisha ushirikiano wa sasa kati ya NBS na Wizara ya Kilimo (ushirikiano katika tafiti za muda mfupi)<br>ii. Kufanya mikutano ya kiufundi na wafanyakazi ngazi ya wilaya na mkoa,<br>iii. Kuimarisha uwezo wa Serikali za Mitaa |

| Hatua/ eneo | Mapendekezo ya shughuli za uwekezaji |
|---|---|
| **1. Mfumo wa kutoa tahadhari mapema kwa ajili ya usalama wa chakula** | |
| Uchukuaji wa tahadhari na hatua za kukabiliana nazo kwa ajili ya Mifugo/uvuvi | i. Mafunzo kwa wilaya na wachunguzi wa jamii kwa ajili ya ukusanyaji wa takwimu, kuwapatia vitendea kazi ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa takwimu, usindikaji na kutoa taarifa kwa wakati muafaka<br>ii. Kuandaa ramani ya rasilimali (kuanza na mfumo wa ufuatiliaji wa malisho, rasilimali za maji na mifugo) uteuzi na kuweka mazingira ya maeneo ya usalama wa mifugo na kuwa na tovuti, na ununuzi wa vifaa na viwezeshi<br>iii. Kutoa uelewa kwa wakulima na wafugaji juu ya mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi<br>iv. Ulishaji salama wa mifugo na ustahimilivu dhidi ya majanga kwa kujenga/ ukarabati wa mabwawa na visima<br>v. Kuimarisha huduma za ukaguzi wa mifugo<br>vi. Mafunzo kwa wafugaji na wakulima kuhusu uhifadhi<br>vii. Mipango ya usimamizi maeneo ya malisho ya mifugo ambayo yamepimwa katika halmashauri 40. |
| **2. Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula** | |
| Usimamizi wa hifadhi ya chakula | i. Kuhifadhi na kusimamia kiwango cha chini / kiwango sahihi cha chakula cha hifadhi ya taifa<br>ii. Kushirikisha sekta binafsi katika usimamizi wa hifadhi ya chakula<br>iii. Kuimarisha mifumo ya usalama wa chakula katika jamii kwa ajili ya chakula, ikiwa inafaa |
| **3. Kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna (angalia pia 3.2 kuongeza thamani na usindikaji)** | |
| Kiwango kikubwa cha upotevu wa mazao baada ya kuvuna kutokana na mifumo mibovu ya usaidizi/ na uwezo mdogo wa teknolojia na utunzaji | i. Kuendelea kutoa miongozo ya udhibiti sahihi wa upotevu wa mazao baada ya kuvuna na uhifadhi wa mazao yaliochaguliwa<br>ii. Kukuza na kusambaza teknolojia ambayo itakuza ubora wa utunzaji na uhifadhi wa chakula katika ngazi zote<br>iii. Kuboresha na kuongeza thamani na kujenga miundombinu ya kuhifadhi na masoko kwa ajili ya kupunguza upotevu na ubora wa chakula (tazama eneo dogo 3.2) |
| **4. Uboreshaji wa lishe** | |
| Kupunguza utapiamlo Tanzania na kuboresha usalama, upatikanaj na matumizi ya chakula na lishe (Mikoa mitano yenye upungufu wa chakula) | i. Kutoa elimu kuhusu usalama wa chakula na lishe katika ngazi zote katika sekta ya kilimo (kuingizwa katika ugani)<br>ii. Kuimarisha mfumo wa taarifa za usalama wa chakula na lishe, ubora/ umuhimu wa takwimu na ramani kwa ajili ya kutoa tahadhari kwa wakati<br>iii. Kuhamasisha mbinu mbalimbali kwa ajili ya usalama endelevu wa chakula katika kaya<br>iv. Kutekeleza mbinu mbadala zitakazosaidia kulinda afya ya kaya kwa kutumia viini lishe vitakavyoboresha matumizi ya chakula .<br>v. Kuhamasisha matumizi ya viini lishe na matumizi ya teknolojia bora ya kuchanganya viini lishe hivyo kwenye unga ili kuongeza ubora wa chakula kwa ajili ya watoto na akina mama wajawazito<br>vi. Kuhamasisha teknolojia ya gharama nafuu ili kupunguza mzigo wa kazi za wanawake kwa ajili ya maandalizi ya chakula na kuhudumia watoto<br>vii. Kuboresha usalama wa chakula ili kujikinga na sumukuvu itokanayo na mazao ambayo hayakukauka vizuri<br>viii. Kuwawezesha watumishi wa Serikali za Mitaa kuhusu mfumo wa uchambuzi wa chakula na lishe |

**200 Muhtasari wa uwekezaji kwa eneo kuu la 2:**

**Eneo Kuu la 2:**

**KUONGEZEKA KWA TIJA NA FAIDA ( Viwango vimekadiliwa kwa thamani ya mwaka 2016)**

**Jedwali Na. 29: Bajeti ya maendeleo makadirio ya uwekezaji kwa ajili ya Eneo kuu la 2 (TSh milioni)**

| Gharama za bidhaa | mwaka 1 | mwaka 2 | mwaka 3 | Mwaka 4 | mwaka 5 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **2.1.1.1** Kukuza na uimarishaji wa huduma za ugani katika kilimo (bidhaa zote) | 1,311,913 | 772,652 | 849,529 | 838,081 | 921,148 | 4,693,323 |
| **2.1.12** Kukuza na kuimarisha mafunzo ya kilimo (bidhaa zote) | 4,373 | 9,720 | 9,349 | 8,506 | 9,222 | 41,170 |
| **2.2.1.1** Kuboresha upatikanaji na uwepo wa pembejeo bora za kilimo kwa bei nafuu ili kuongeza tija na faida (bidhaa zote) | 149,389 | 136,695 | 150,284 | 164,670 | 181,057 | 782,095 |
| **2.2.1.2** Kuboresha upatikanaji na uwepo wa pembejeo bora za ufugaji wa ndege wafugwao | 4,176 | 2,652 | 2,800 | 2,962 | 3,141 | 15,731 |
| **2.2.1.3** Kununua meli ya uvuvi kwa ajili ya kuongeza uzalishaji | 1,664 | 93,408 | 768 | 1,099 | 987 | 97,926 |
| **2.2.1.4** Kuimarisha na kuanzisha maeneo ya bandari ili kuboresha tija ya uvuvi | 1,146 | 4,533 | 5,008 | 4,246 | 4,639 | 19,572 |
| **2.2.1.5** Kuendeleza bandari za uvuvi wa baharini kwa ajili ya kuongezea faida | 4,115 | 5,176 | 7,350 | 4,460 | 2,090 | 23,191 |
| **2.2.1.6** Kuboresha wavuvi wadogo ili kuongeza uzalishaji na tija ya Samaki | 55,090 | 50,853 | 48,517 | 6,658 | 4,388 | 165,506 |
| **2.2.1.7** Uimarishaji wa vitengo vya usimamizi wa fukwe za bahari kwa ajili ya usimamizi endelevu, ulinzi na uhifadhi wa rasilimali ya uvuvi | 2,537 | 2,134 | 2,199 | 2,147 | 2,319 | 11,336 |
| **2.2.1.8** Uboreshaji wa huduma za afya ya mimea | 13,322 | 11,191 | 7,608 | 1,389 | 478 | 33,988 |
| **2.2.1.9** Uzalishaji wa chanjo na madawa | 44,570 | 36,191 | 39,700 | 3,705 | 4,380 | 128,546 |
| **2.2.1.10a** Uboreshaji wa huduma za afya ya mifugo | 262,550 | 295,128 | 332,216 | 371,559 | 420,078 | 1,681,531 |
| **2.2.1.10b** Uboreshaji wa huduma za afya ya viumbe wa majini | 1,518 | 1,238 | 1,241 | 1,340 | 1,395 | 6,732 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **2.3.1.1** Uimarishaji wa uwezo wa utafiti wa kilimo kwa maendeleo ya teknolojia, mahusiano ya viwanda na usambazaji wa matokeo ( kila sekta ndogo) | 7,559 | 29,197 | 29,504 | 8,708 | 9,516 | 84,484 |
| **2.3.2.1** Usambazaji wa teknolojia jumuishi ili kuongeza uzalishaji na tija (bidhaa zote) | 12,409 | 16,384 | 11,616 | 11,110 | 11,371 | 62,890 |
| **2.3.2.2** Kukuza na kuimarisha vizazi vya mifugo kwa njia za teknolojia ya kisasa ya uzalishaji | 4,833 | 3,895 | 2,683 | 2,738 | 3,011 | 17,160 |
| **2.4.1.1** Kuimarisha na kukuza mbinu za kisasa za kilimo kwa ajili ya kuboresha mnyororo wa thamani | 9,250 | 5,753 | 5,699 | 5,707 | 5,717 | 32,126 |
| **2.5.1.1** Kuboresha uwepo, upatikanaji na matumizi bora ya vyanzo vya chakula vyenye virutubisho muhimu (bidhaa zote) | 14,153 | 11,722 | 12,960 | 14,297 | 10,394 | 63,526 |
| **2.5.1.2** Kuongeza uzalishaji na kukuza mtama na ulezi kwa ajili ya chakula na matumizi ya viwandani | 20,538 | 22,167 | 23,955 | 25,921 | 28,084 | 120,665 |
| **JUMLA YA ENEO KUU LA 2** | **1,925,105** | **1,510,689** | **1,542,986** | **1,479,303** | **1,623,415** | **8,081,498** |

## E. Eneo Kuu la 3: Biashara na Uongezaji Thamani kwenye Mazao (kuimarisha ushindani katika minyororo ya thamani ya bidhaa)

201 Wakati wa utekelezaji wa ASDP-1, kulikuwa na kasi ndogo katika kusaidia upatikanaji wa masoko na uongezaji wa thamani kutokana na vikwazo mbalimbali ambavyo ni pamoja na: (i) Kilimo kubaki na sifa ya mazao na mifugo ambayo tija yake ni ndogo na kutozalishwa kibiashara (ii) Ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika kilimo-biashara, (iii) Sera zisizoruhusu minyororo ya thamani kutoa faida kikamilifu kupitia ushirikiano wa kikanda; na (iv) Uratibu usioridhisha katika mnyororo wa thamani. Kadhalika, katika ngazi ya utekelezaji, masuala zaidi yalitambuliwa kama vile: (i) Dosari za kubuni na kutekeleza (ii) Upungufu wa uchambuzi wa masuala ya mnyororo wa thamani katika ngazi za Mitaa, Wilaya, Mikoa na Taifa; (iii) Uwezo dhaifu wa utekelezaji katika sekta ya umma na binafsi, na (iv) Uzoefu mdogo wa kupata masoko na taarifa za masoko.

202 Uanishaji wa uzalishaji kibiashara unatarajiwa kuleta mabadiliko ya msingi katika muundo na kazi za sekta ya kilimo ya Tanzania ikiwa ni pamoja na: (i) kuongezeka kwa kiasi cha ubora wa mazao ya kilimo yatakayoingia katika soko la ndani na nje, (ii) kuongezeka kwa shughuli nyingine kwa wazalishaji wadogo (na kipato) zitokanazo na kuongeza thamani ya mazao na mifugo (shughuli zisizo za asili ); (iii) kuongezeka kwa upatikanaji wa malighafi za viwanda, (iv) kuboresha upatikanaji wa pembejeo na huduma za kifedha kwa mkulima; (v) kuwepo kwa mashirika imara ya wakulima; na (vi) kuboresha miundombinu na mawasiliano. Kiwango cha juu cha shughuli za biashara pia kinatarajiwa kupanua fursa za biashara vijijini zisizo za kilimo-biashara na ajira za mashambani na zisizo za mashambani, ambazo zinajumuisha vijana.

**203 Mbinu ya Uendelezaji mnyororo wa thamani wa bidhaa.** Uendelezaji wa mnyororo wa thamani unahusisha hatua mbalimbali kuanzia pembejeo, uzalishaji, usindikaji na mifumo ya masoko / usambazaji wa bidhaa muhimu, ikiwa ni pamoja na kuongeza thamani. Mbinu za uongezaji wa thamani ni kama zinavyoonekana katika Kielelezo Na.20 ambacho, kinaelezea masuala yanayopaswa kukabiliwa katika kila hatua kuelekea katika myororo wa thamani wenye sifa ya kibiashara, kitaalamu na utendaji kwa ujumla. Kuna mwelekeo sahihi wa wakulima wadogo na kuboresha majukumu yao na mahusiano ndani ya mnyororo wa thamani unaowahusu. Umakini hasa utawekwa katika kuendeleza uwezo wa kitaasisi wa mashirika ya wakulima wadogo kukubaliana, kujadiliana na kusimamia mpangilio mpya wa kimasoko na sekta binafsi kwa ajili ya uhusiano wenye manufaa na ushirikiano kibiashara kwa pande zote mbili.

**Kielelezo Na.20: Mbinu ya Uendelezaji Mnyororo wa Thamani kwenye ASDP II**




204 Kuelekea kujenga mnyororo wa thamani wa ushindani, ASDP II itasaidia wakulima wadogo kulima na kuzalisha kwa kuzingatia upatikanaji wa soko na ubora wa mazao ili kilimo kiwe cha kibiashara na ushindani. ASDP II itasaidia kuwaunganisha wakulima na wasambazaji wa pembejeo kwa kuzingatia mahitaji yao. Ni muhimu sekta binafsi kuongoza maendeleo ya kilimo-biashara. Pia ASDP II itachochea ushiriki wa sekta binafsi kwa kuandaa mazingira bora ya uwekezaji, kuimarika kwa uwezo wa biashara na utoaji wa huduma ndani ya sekta za umma na binafsi (PPP).

205 Sehemu hii inalenga upatikanaji wa mfumo wa masoko wenye ushindani kwa ajili ya ongezeko la thamani kwa bidhaa za kipaumbele utakaotokana na mchango wa sekta binafsi iliyoimarika na vyama vya wazalishaji vyenye nguvu. Malengo mkakati, matokeo na viashiria vinavyohusiana ni kama inavyoonyeshwa katika **Jedwali Na. 30.**

**Jedwali Na. 30: ASDP II Eneo Kuu 3: Mahusiano na Matokeo ya ASDS**

| Lengo | Matokeo | Viashiria vya matokeo |
|---|---|---|
| Eneo dogo 3. ***Kuboresha na kupanua masoko na kuongeza thamani kupitia sekta binafsi iliyoimarika na vyama vya wazalishaji vyenye nguvu*** | ***Mnyororo wa thamani wenye ushindani*** | - Kiasi na na thamani ya mauzo ya nje - Uwekezaji wa moja kwa moja na mtiririko wa mtaji binafsi katika sekta ya kilimo<br>- Fursa za ajira kutokana na uwekezaji mpya na upanuzi wa kilimo-biashara<br>- Kiasi na thamani ya uingizaji wa bidhaa za chakula<br>- Bei ya kuuzia mazao shambani na ya kiwandani<br>- Kiwango cha ushiriki katika soko kwa ngazi zote - Ukubalifu wa bidhaa kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa<br>- Miundombinu yenye viwango katika mnyororo wa thamani<br>- Ushiriki wa makundi yenye mahitaji maalum (wanawake, vijana, na wafugaji) katika mnyororo wa thamani<br>- Ushiriki wa makundi yenye mahitaji maalum (wanawake, vijana, na wafugaji) katika biashara<br>- Ushiriki wa makundi yenye mahitaji maalum (wanawake, vijana, na wafugaji) katika kufanya maamuzi katika mnyororo wa thamani<br>- Manufaa yatakayopatikana kwa makundi yenye mahitaji maalum wanawake,vijana,na wafugaji) kutokana na utekelezaji wa shughuli za ASDP II katika mnyororo wa thamani |
| | Eneo dogo 3.1 Upatikanaji miundombinu vijijini (masoko / malipo) kuboresha | - % ya mabadiliko ya uwekezaji katika miundombinu ya masoko<br>- % mkulima / Vikundi vya wakulima / Wafanyabiashara wanaotumia miundombinu ya masoko iliyoboreshwa katika maeneo ya vijijini |
| | Eneo dogo 3.2 Uendelezaji wa kilimo-biashara kuongeza thamani na usindikaji | - % ya mabadiliko ya ongezeko la thamani ya mazao na bidhaa<br>- % ya mabadiliko ya upotevu wa mazao baada ya kuvuna |

Maboresho ya sera, kanuni na ya kitaasisi yanahitajika ili kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa mikakati yote ya kilimo kwa ufanisi.

Uendelezaji wa Kilimo Biashara- Uongezaji wa thamani na Usindikaji

206 Eneo Kuu la 3 limegawanyika katika maeneo madogo mawili.

**Eneo kuu 3: Biashara na Uongezaji Thamani kwenye Mazao (Kuendeleza ushindani wa mnyororo wa thamani wa bidhaa)**
Eneo dogo 3.1: Masoko
Eneo dogo 3.2: Uendelezaji wa Kilimo-biashara: Uongezaji wa thamani na Usindikaji

207 Kushirikisha wakulima wadogo na kukuza ushirikiano wa wadau wa kimkakati wanaohusika kwenye bidhaa za kipaumbele katika mnyororo wa thamani kuanzia kwa wazalishaji, wasindikaji na walaji. Hii itasaidia kuhamasisha wakulima wadogo kuzalisha kibiashara na hivyo kuongeza ubora wa bidhaa utakaoleta ushindani katika masoko ya ndani, kikanda na Kimataifa. Lengo la kipengele hiki ni kuongeza ufanisi kwa wakulima na vikundi vyao, ili kutumia fursa ya kupata pembejeo na kufikia masoko kwa wakati na uongezaji wa thamani wa mazao ya kilimo (ikiwamo usindikaji) kwenye vipaumbele katika mnyororo wa thamani, na kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta binafsi ili waweze kuwekeza. Kuwepo kwa Sera madhubuti (tazama Eneo dogo 4.1), Hii itawezekana kwa kupitia uwezeshaji wa Sekta ya umma, Vikundi vya wadau vilivyo imara (wakulima, wasindikaji, walaji, nk), upatikanaji wa taarifa na ushauri sahihi, kuimarisha uhusiano na ushirikiano kwa uwekezaji kwenye mnyororo wa thamani uliolengwa na upatikanaji wa miundombinu muhimu.

208 Kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa zilizokusudiwa kutafanikiwa kwa kuwepo yafuatayo: (i) Matumizi bora ya teknolojia, ikiwemo matumizi ya pembejeo na zana za kilimo (ii) Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ili kuweza kulima mara mbili kwa mwaka, hasa kwa ajili ya mazao ya mpunga na mazao ya bustani (iii) Kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna na kuongeza thamani, na (iv) Kuendeleza na kuhamasisha matumizi ya fursa za masoko kwa kuvijengea uwezo vikundi vya wakulima, kuwaunganisha na wadau wengine walioko kwenye mnyororo wa thamani na upatikanaji wa miundombinu katika jamii husika.

**209 Vipaumbele.** Kutakuwa na miradi inayoleta tija ambayo italenga kutatua changamoto zinazowakabili wakulima. Programu hii italenga hasa kwenye mnyororo wa thamani wa mazao na bidhaa ambazo ni muhimu katika mfumo wa uzalishaji wenye matokeo yatayopimika kwa wingi na ubora katika ukuaji; umuhimu wa kiikolojia katika mfumo wa kilimo (rejea pia ASDP-1 hasa vipaumbele vya wilayani) na mahitaji ya soko. Hivyo, hivi vitakuwa ni vigezo muhimu vya kuzingatia wakati wa uchaguzi wa zao au bidhaa husika. Mfano SAGCOT imejikita kwenye bidhaa za kipaumbele ambazo ni, mahindi, mpunga, chai na miwa katika maeneo ya Nyanda za Juu Kusini. Kama Programu ya kitaifa ya Sekta ya Kilimo, ASDP II itaanza kwa kuzingatia vipaumbele vya mnyororo wa thamani utakaohusisha mazao, mifugo na Uvuvi katika kila ikolojia ya kilimo-AEZ, na utekelezaji wa shughuli za kilimo zitazingatia wilaya chache zenye fursa ya uzalishaji zinazofanana kitabia/ikolojia ambazo zitachanguliwa/zitabainishwa kupitia majukwaa ya kikanda ya wadau katika eneo husika. Kwa kuzingatia uchambuzi wa matarajio ya ukuaji katika minyororo wa thamani utakaozingatia vipaumbele katika ikolojia za kilimo (AEZs), mikakati maalum ya kufikia ukuaji huo endelevu ni kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na. 31: Malengo ya minyororo ya thamani ya bidhaa za kipaumbele na mikakati ya kufikia matokeo yanayotarajiwa**

| *Matokeo* | *Vipaumbele vya kiikolojia* | *Mikakati ya kufanikisha matokeo tuliyo tarajia* |
|---|---|---|
| **MAHINDI:** Tanzania ni muuzaji mkubwa wa mahindi katika ukanda wa Afrika Mashariki. Kulingana na mwenendo wa hivi karibuni, Tanzania inategemea kuuza nje ya nchi zaidi ya tani 500,000 za mahindi kila mwaka, katika nchi za jirani hasa (Kenya) | Nyanda za juu kusini<br><br>Magharibi na kusini -magharibi<br><br>Nyanda za juu kaskazini | i. Kutoa motisha kwa wazalishaji ili kuongeza matumizi ya teknolojia za kisasa (mbegu na mbolea)<br>ii. Kuhamasisha uhifadhi wa mazao katika maghala ili kutoa motisha na kuimarisha soko na hivyo kuongeza bei ya mkulima hadi kufikia asilimia 50<br>iii. Kuelimisha wazalishaji kuwa mapato mazuri yatawezesha wakulima kuwekeza kwenye uzalishaji (kutumia pembejeo)<br>iv. Kuhamasisha kilimo cha uhifadhi wa ardhi kwa ajili ya uzalishaji endelevu<br>v. Kuhamasisha kilimo cha mzunguko wa mazao ya mahindi na jamii ya mikunde kwa ajili ya kuongeza rutuba kwenye udongo na vyakula vya mifugo<br>vi. Kuanzisha vyama vya ushirika ili kuwa na nguvu ya kiuchumi ya pamoja |
| **MCHELE:** Tanzania inajitosheleza kwa uzalishaji wa mchele (na kuanza kuuza nje mchele ( ni moja ya nchi yenye uwezo wa kuuza nje mara kwa mara) | Mashariki<br><br>Maeneo yote ya umwagiliaji | i. Kuongeza tija katika uzalishaji– kuongeza ufanisi katika matumizi ya teknolojia bora<br>ii. Kuwa na maeneo ya pamoja yatakayoleta ufanisi katika usimamizi wa kilimo cha umwagiliaji<br>iii. Kukarabati miundombinu ya umwagiliaji<br>iv. Kuhifadhi mazao ghalani na kuongeza thamani ili kuunganishwa na soko<br>v. Kuzalisha mbogamboga wakati umwagiliaji<br>vi. Kuimarisha usimamizi wa skimu za umwagiliaji mpunga zilizopo |

| *Matokeo* | *Vipaumbele vya kiikolojia* | *Mikakati ya kufanikisha matokeo tuliyo tarajia* |
|---|---|---|
| **MAZAO YA MAFUTA:** Tanzania bado haijitoshelezi kwa mafuta ya kula (kuna upungufu wa zaidi ya asilimia 50 hivyo uagizaji wa mafuta ya kula ya kutoka nje) | Kanda ya Kati Jangwa (N) (alizeti) ikiwa ni pamoja na michikichi Kigoma | i. Kutoa motisha kwa ajili ya kuzalisha kwa tija kutokana na matumizi ya mbegu bora na usimamizi wa udongo na maji<br>ii. Kubadilisha kilimo cha mzunguko kwa kutumia mazao ya jamii ya mikunde<br>iii. Kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kuongeza thamani vya kati vya vyama vya wakulima wadogo na Sekta binafsi |
| | Nusu jangwa (S) (ufuta) | i. Kuongeza uzalishaji wenye tija (aina mbalimbali za mbegu, usimamizi wa urubishaji udongo)<br>ii. Kutoa motisha kwa Vikundi vya wakulima kwa uhifadhi wa pamoja, upangaji wa madaraja kulingana na aina ya mbegu)<br>iii. kuboresha uuzaji / mauzo ya nje ya mazao yao (bei kuongezeka hadi asilimia 50) |
| **MAZIWA:** Tanzania inaagiza asilimia 25% ya bidhaa za maziwa | - Kanda ya Ziwa<br>- Kanda ya Pwani<br>- Kanda ya Kati<br>- Maeneo ya Mijini | i. Kuboresha koo safu za mifugo kwa ajili ya maziwa, kuboresha vyakula vya mifugo na usimamizi wa afya ya mifugo<br>ii. Kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi /Vyama vya wazalishaji maziwa / vyama vya ushirika; vikundi ya masoko<br>iii. Kuwepo kwa Vituo vya ukusanyaji maziwa, na udhibiti wa ubora<br>iv. kuboresha vyakula vya mifugo (soya / mahindi, nk)) |
| **NYAMA:** kukidhi mahitaji ya ndani na kuuza nje ya nchi (Mashariki ya Kati) | Kanda ya kati na nusu jangwa na nyanda za juu kusini | i. Kuboresha koo safu ya mifugo kwa ajili ya nyama<br>ii. Kuanzisha na kuimarisha vyama vya wadau wa sekta ya nyama katika mnyororo wa thamani<br>iii. Kuanzisha na kuimarisha mfumo wa unenepeshaji wa mifugo kwa ajili ya kupata nyama bora<br>iv. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za taarifa za masoko |
| Kilimo cha mazao ya bustani (matunda na mboga). Uzalishaji kwa ajili ya matumizi ya ndani na kuuza nje ya nchi | Maeneo yote ya mjini na Nyanda za Juu | i. Kusimamia uzalishaji wa kutumia kitalu nyumba<br>ii. Kilimo cha umwagiliaji wakati ambao siyo wa msimu<br>iii. Kuanzisha vikundi vya uzalishaji na uuzaji wa mazao ya kilimo |
| Mazao ya biashara ya asilia (korosho, kahawa, katani nk) Kuongeza wingi na ubora kwa ajili ya kuuuza nje ya nchi | | i. Kuongeza tija ya uzalishaji na ubora wa bidhaa<br>ii. Kulenga masoko maalum kwenye masoko ya kimataifa<br>iii. Kuongeza thamani mazao (korosho, kahawa, chai, nk)<br>iv. Kupanua wigo wa bidhaa kwa kutengeneza bidhaa nyingine |
| Bidhaa za mbuzi na kuku. Kuchangia kuboresha lishe na mapato | kanda zote | i. Upatikanaji wa koo safu<br>ii. Kuboresha ujuzi wa usimamizi, kuhuisha mfumo wa kilimo<br>iii. Kuimarisha afya za mifugo (ikiwa ni pamoja na chanjo)<br>iv. Mikakati ya vyakula vya mifugo kutokana na mabaki ya mazao mashambani<br>v. Kuzalisha kibiashara wa nyama ya kuku na mbuzi na bidhaa zake |

| *Matokeo* | *Vipaumbele vya kiikolojia* | *Mikakati ya kufanikisha matokeo tuliyo tarajia* |
|---|---|---|
| **SAMAKI:** Wazalishaji wakubwa wa samaki na kuuza nje ukanda wa Pwani wa bahari ya Hindi. Kuhakikisha kuwa, shughuli za uvuvi ni endelevu na katika kuboresha maisha ya wavuvi na na kuchangia Pato la Taifa | Maziwa makuu, (Victoria, Tanganyika, Nyasa na Rukwa). Pia, mito na Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi | i. Kutumia mfumo wa kiikolojia katika kuongeza usimamizi wa uvuvi<br>ii. Uanzishwaji wa usajili wa vitengo vya usimamizi wa fukwe<br>iii. Kuongezea thamani bidhaa za uvuvi<br>iv. Kupunguza upotevu wa samaki hadi asilimia sifuri<br>v. Kuhamasisha ufugaji wa samaki katika mabwawa na matundu kwenye maziwa/bahari<br>vi. Kuwezesha sekta binafsi kuzalisha kwa wingi na ubora vifaranga vya samaki na chakula cha samaki<br>vii. Kuwezesha vyuo vya kufundishia ufugaji wa samaki kutoa mafunzo kwa vitendo |

Chanzo: Imekusanywa na FAO ujumbe wa ASDP-BF, 2013

210 **Kujenga uwezo na uwekezaji.** Kujenga uwezo wa kitaasisi, kuhamasisha vikundi vya wadau katika mnyororo wa thamani na kutoa elimu ya kilimo-biashara vitabaki kuwa msingi muhimu kwa ajili ya kuendeleza mnyororo wa thamani (angalia pia eneo dogo 4.1). Huduma za msaada za kutoa elimu ya Kilimo-biashara itahusisha uingiaji wa mkataba na watoa huduma binafsi ambao watatoa mafunzo maalum ya kusaidia walengwa kuandaa mipango ya uwekezaji, kuimarisha uwezo wa usimamizi na kuboresha upatikanaji wa fedha. Shughuli hizo zitatekelezwa hatua kwa hatua kwa majaribio katika kila ikolojia ya Kilimo au kwa makundi (i) Kuenezwa katika wilaya zinazoonesha uhitaji ; na (ii) Kuenezwa kwa kutumia mnyororo wa thamani za sehemu husika kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa nyingine. Kamati za Mkoa zitakuwa zikifanya maamuzi kuhusu umuhimu kwa kuzingatia fursa na uwezo uliopo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa wa mnyororo wa thamani ambao unaunganishwa na vipaumbele vya uwekezaji.

211 Kuendeleza miradi na programu zinazoendelea kutekelezwa, ASDP II kwa kuzingatia uzoefu wa kongani katika mnyororo wa thamani wa bidhaa itaendelea kueneza kongani hizo katika ikolojia zote za kilimo. Mnyororo wa bidhaa za kipaumbele za mazao, mifugo na uvuvi utakuwa unaimarishwa hatua kwa hatua, kulingana na wadau walivyochagua. Ili kufikia ukuaji mpana kwa ajili ya kupunguza umaskini vijijini. Mnyororo ya thamani wa bidhaa utaunganishwa na vipaumbele vilivyoko kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya kwa kuzingatia vipaumbele vya kikanda na kitaifa ili kuchochea na kuzingatia uwekezaji na upunguzaji wa gharama na kuongeza uwezo wa kuzalisha zaidi.

212 **Ufadhili katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa.** ASDP II itazingatia utoaji wa ruzuku za ushindani kama mfuko wa fedha za ziada kwa ajili ya uwekezaji katika mnyororo wa thamani wa bidhaa wenye faida na kujenga ushirikiano katika kuendeleza kilimo-biashara.

213 **Kuimarisha mfumo wa uratibu katika ngazi za Mamlaka za Serikali ya Mitaa.** Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya huduma za ugani za mazao na mifugo kwa kuzingatia vipaumbele, eneo husika na kujenga uwezo wa kupanga, kutekeleza na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za mnyororo wa thamani wa bidhaa. Hii ni pamoja na kuzisaidia Halmashauri kuwa na mnyororo wa thamani wa bidhaa za kipaumbele, kwa kushirikisha wadau wa Sekta za Umma na Binafsi.

214 Msaada jumuishi wa kuhusisha uvumbuzi na kujenga uwezo kwa ajili ya uzalishaji, kuongeza thamani na masoko utashawishi matokeo yanayohitajika katika vipaumbele vya minyororo ya thamani ili kuleta mabadiliko endelevu katika mifumo ya uzalishaji. Kwa ujumla, eneo hili kuu la 'Biashara na uongezaji Thamani kwenye mazao' litasaidia kujenga minyororo ya thamani ya ushindani kupitia shughuli zilizopo katika maeneo manne madogo: (i) Kuwezesha na kuimarisha vikundi vya wakulima; (ii) Kuongeza thamani na usindikaji; (iii) Kufikia masoko; na (iv) Upatikanaji wa mikopo katika meneo ya vijijini.

### Eneo dogo 3.1: Masoko

215 Kuwepo kwa Sera ya Masoko ya Kilimo *(AMP, 2008)* kulisaidia kuongeza ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, kama vile *MVIWATA, MUVI* na *RLDC* ili kuwawezesha wazalishaji na kuongeza uhakika wa upatikanaji wa masoko. Kumekuwepo na programu kadhaa / miradi katika miaka ya hivi karibuni ambayo ilisaidia kuendeleza sekta ya kilimo katika kuboresha masoko: Moja ya programu hizo ni ile iliyohusu miundombinu ya masoko, kuongeza thamani na upatikanaji wa mikopo Vijijini (MIVARF). Mipango mingine katika kusaidia maendeleo ya masoko ni pamoja na PADEP, DASIP, na baadhi ya miradi mingine ambayo inatekelezwa na mashirika yasiyo ya kiserikali.

**216** **Biashara ya Ndani, Kikanda na Kimataifa.** Serikali ya Tanzania itaendelea kukuza biashara ya ndani, kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuia ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC)* na kimataifa kwa ajili ya mazao ya kilimo na chakula. Hatua zinazohitajika ni pamoja na kukuza na kuimarisha: (i) biashara ya ndani na nje kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TANTRADE)*; (ii) kuhamasisha kampeni ya kutumia bidhaa zilizotengenezwa Tanzania kwa kutumia **Kauli mbiu** isemayo **"Nunua bidhaa zilizotengenezwa Tanzania Jenga Tanzania"** (iii) kuboresha mauzo ya nje kwa mazao ya biashara asilia ikiwa ni pamoja na tumbaku, kahawa, pareto, mkonge, chai, korosho, pamba na usindikaji wake; na (v) kuongeza mauzo ya nje ya samaki na mazao ya bustani, lakini pia kuwa na mkakati wa mauzo ya mahindi na mchele kwa nchi jirani na mashirika mbalimbali. Katika hilo, Serikali inapendekeza kupanua kanda maalum za usindikaji katika mikoa ya kipaumbele na kuimarisha mfumo uliopo sasa wa mashauriano ya mara kwa mara na Sekta binafsi na mashirika kuhusu taratibu zinazotakiwa kufuatwa ili kuleta matokeo chanya katika biashara na kupata faida.

**217** **Upatikanaji wa masoko.** Wizara za Sekta ya Kilimo zitaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza sera, sheria, kanuni na kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara za ndani, kikanda na kimataifa, ikiwa ni pamoja na: (i) kuanzisha na kusaidia utekelezaji wa soko la bidhaa kwa bidhaa zitakazopendekezwa; (ii) kuongeza uelewa kwa wadau juu ya viwango vya ubora katika masoko na kusimamia utekelezaji wa upangaji wa madaraja na itifaki kwa bidhaa mbalimbali; (ii) kuendelea kufanya mapitio ya sheria zilizopo na usimamizi wa mfumo wa masoko ya kilimo, (iv) kuboresha mfumo na taarifa za masoko na matumizi yake kwa kwa ajili ya kufanya maamuzi kibiashara; (v) kuimarisha mifumo ya utekelezaji wa usimamizi wa usalama wa chakula kwa kuzingatia ufuatiliaji-matumizi ya simbomilia na uhifadhi uliosahihi , na (vi) kuboresha utekelezaji wa kanuni na taratibu sahihi za kufanya biashara ili kupunguza vikwazo vya ushuru.

**218** **Uendelezaji wa Miundombinu ya vijijini na masoko** (barabara, masoko, maghala ya watu binafsi na ya umma, umeme, mawasiliano, nk) ni kipaumbele cha juu kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa pembejeo na masoko ya mazao ili kuvutia wawekezaji katika shughuli zinazohusiana na kilimo kama vile usindikaji, lakini pia kwa wakulima kupata bei nzuri, kufikia masoko kwa wakati, kuongeza kipato kwa mkulima na fursa za ajira vijijini. Kuboresha miundombinu ya usafiri, usambazaji wa taarifa za masoko na kuondoa vikwazo vya biashara ya mpakani kunaweza pia kuchangia ukuaji wa uchumi.

**219** **Sekta binafsi inatarajiwa kuongoza katika usindikaji na masoko ya mazao ya kilimo** ili waweze kukidhi mahitaji ya walaji kwa wingi, ubora na usalama. Kama masoko ya ndani na kikanda yanaendelea kupanuka kutakuwa na umuhimu wa kuzingatia masuala ya ubora na usalama wa chakula, hivyo kinachotakiwa ni uboreshwaji wa kanuni na huduma za utoaji vyeti vya umahiri . Serikali ya Tanzania (tazama ASDS), kupitia Wizara za Sekta ya Kilimo, zitafanyakazi kwa karibu na sekta binafsi na washirika wa maendeleo ili kuendeleza jitihada zake za: (i) Kuboresha na kuzifanyia ukarabati barabara za vijijini, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uwekezaji binafsi, (ii) Kuongeza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani[59] kwa kuwawezesha mafunzo kwa wakulima, kuongeza ujenzi wa maghala ya kuhifadhi mazao katika ngazi zote katika Mamlaka za Serikali za Mikoa na Mitaa; (iii) Kuongeza uwepo wa vifaa vya kuhifadhia baridi hasa kwa bidhaa za maziwa, nyama na bidhaa za

59 *Kuanzia mwaka 2007 mfumo wa stakabadhi ghalani (WRS) umefanya kazi nzuri katika uboreshaji wa masoko ya kilimo (pamba, kahawa, korosho, mahindi , mchele, alizeti na ufuta. Mfumo wa soko la bidhaa unaoandaliwa chini ya uratibu wa Mamlaka ya Soko la Mitaji.*

samaki; (iv) Kushirikiana kwa karibu na Wakala wa Umeme Vijijini ili maeneo ya vijijini yawe na umeme; na (v) Kujenga na kuendeleza miundombinu ya masoko katika maeneo ya kijijini, kata na wilaya, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa masoko ya mipakani[60] ili kuhamasisha biashara za mipakani na nchi jirani.

220 **Lengo ni kuendeleza na kuongeza upatikanaji wa masoko yenye faida ndani na nje ya kwa ajili ya bidhaa za kipaumbele katika minyororo ya thamani.** Hii itakuwa na mafanikio kwa kuanzisha utaratibu endelevu wa masoko (tazama COWABAMA katika Eneo dogo 3.2) kwenye kijiji /mkulima na kusaidia: (i) kuanzisha na kuhamasisha matumizi ya mfumo wa taarifa za masoko; (ii) kuimarisha na kuendeleza matumizi ya mfumo wa stakabadhi za ghala, na (iii) kuanzisha na kufanya majaribio soko la bidhaa, ikiwa ni pamoja na kujenga maghala ya kimkakati yanapohitajika, kwa kuanzia na mazao makuu ya biashara yakiwemo korosho, kahawa, ufuta, nk.

221 **Upatikanaji wa masoko kwa ajili ya nyama, maziwa na samaki.** Miundombinu ya mifugo ni pamoja na minada iliyo eneo inapopita mifugo, kukusanyikia na kusubiria mifugo wakati wa kuuzwa na majosho kwa ajili ya kuua kupe. Masoko ya msingi na makuu yatakuwa na uzio, mizani na vifaa vingine. Jumla ya masoko ya msingi ya mifugo 300 husimamiwa na Serikali za Mitaa kwa ajili ya masoko ya ndani na ya usambazaji katika masoko ya makuu na ya mwisho yaliyoko Themi (Arusha), Weruweru (Moshi), Korogwe (Tanga), Lumecha (Songea) na Pugu (Dar -es-Salaam), ambayo nayo husambaza katika masoko ya mjini na nje na katika masoko 10 ya mpakani.

222 **Huduma za Taarifa za Masoko (MIS).** Upatikanaji wa taarifa za kilimo-biashara ni muhimu wakati wa kufanya maamuzi. Taarifa za masoko uhusisha maeneo, bei, wingi na ubora wa bidhaa inayouzwa au kununuliwa katika maeneo maalum. Hali ilivyo sasa, upatikanaji wa taarifa, hazipatikana na hazikusanywi kwa wakati na taasisi mbalimbali na usambazaji wake ni hafifu. Ni muhimu kuwepo na uuimarishwa kwa mfumo imara zaidi wa ukusanyaji wa takwimu za masoko na kuwezeshwa katika uwekezaji baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi- *PPP* kwa kutumia *TEHAMA* (mtandao, simu ya mkononi, ujumbe wa maandishi) kwa ajili ya kutoa taarifa muhimu za masoko. Hali hii itawezesha upatikanaji wa masoko na kuboresha mahusiano baina ya wazalishaji, wanunuzi na wadau wengine katika mnyororo wa bidhaa .

223 **Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala (WRS) katika kuunganisha masoko.** Jitihada na mafanikio ya kuboresha masoko kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za ghala kwa wabia wa maendeleo na taasisi za fedha kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika, kuruhusu uuzaji wa kutumia soko la uhakika (ikiwa ni pamoja na kuuza kwa wanunuzi kwa kutumia mkataba kutumia minada, soko maalum), kuboresha bei ya mkulima kwa lengo la kupata bei nzuri ya pembejeo na mauzo ya mazao, kupungua hasara na kuwa na mzunguko wa fedha wa kuaminika. Utekelezaji wa vipaumbele vya ASDP II katika awamu ya kwanza ni kuimarisha upatikanaji wa maghala na miundombinu ya masoko katika ngazi ya kijiji (tazama eneo dogo 3.2 COWABAMA) , kwa kuwa Mfumo wa Stakabadhi ghalani huhitaji maghala ya kuhifadhi yenye uwezo wa kuhifadhi tani angalau 5,000 ili kukabiliana na gharama shughuli za usimamizi, dhamana ya kitaalamu, matengenezo ya miundombinu, bima, leseni, nk, kama Sheria Na. 10 ya Mfumo wa Stakabadhi ghalani ya mwaka 2010 inavyoelekeza. Mfumo wa Stakabadhi ghalani utafanyika kwa majaribio katika maeneo 10 muhimu (uwezo wa wastani wa tani 300 kila moja) ili kuruhusu kazi ya kukusanya mazao[61]. Aidha, hatua kwa hatua za mahitaji ya soko yatasababisha kuingia makubaliano ya kimkataba kati ya vyama vya ushirika, watoa huduma za umma na binafsi, benki za vijijini, wakala wa pembejeo, na wakulima wakubwa au wakusanyaji wa mazao ambao wana uhusiano na viwanda vya kilimo, soko la bidhaa, wauzaji wa jumla na wauzaji wa bidhaa nje ya nchi. Ili kuwezesha kuendeleza mahusiano haya, ASDP II itasaidia katika kubadilishana taarifa, ushauri katika mnyororo wa thamani na kutoa utaalamu wa kiufundi na kiuchumi.

224 **Uanzishwaji wa soko la bidhaa.** Hatua ya awali ya kuanzisha soko hili ni kuwa na wataalam wenye

60 *Kukamilika kwa ujenzi wa soko la kimataifa Kibaigwa (mahindi, mtama na nyama), Segera (mazao ya bustani – Mkoani Tanga) na Makambako (kwa ajili ya biashara zote- mkoani Njombe). Masoko ya mpakani yanategemewa kusaidia wakulima kwa kuimarisha bei kutokana na wadau wote kutumia sehemu moja*

61 *Angalia pia shughuli za majaribio zinazopendekezwa kwa ajili ya soko la bidhaa katika Jedwali Na.32*

maarifa kuhusu masoko, kutambua fursa zilizopo, nafasi yake, mahitaji, vyanzo vya taarifa na wadau muhimu, hasa makampuni binafsi. Hii itasaidia kuanzishwa kwa kozi ya mafunzo maalam ya masoko. Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji itaendeleza kusimamia mfumo wa ukusanyaji taarifa za masoko za ikiwa ni pamoja na: (i) vyanzo vya taarifa katika mikoa; (ii) kuhuisha mara kwa mara orodha ya makampuni, wafanyabiashara, makampuni yanayohusika na usafirishaji, upatikanaji wa vyanzo vya vifaa vya kukusanyia taarifa za masoko; na (iii) kanuni, viwango na takwimu za biashara. Kuendeleza kusisitiza matumizi ya maghala kwa ajili ya soko ya bidhaa lililoanzishwa kwa kuanza kutumika kwa baadhi ya mazao ikiwemo korosho na kahawa. Mazao mengine kama vile mahindi na mengine yatatumika baada ya soko hilo kuonesha ufanisi. Kwa kupitia mwongozo maalumu kutoka Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji, uwezo wa kitaalam utaendelezwa, ikiwa ni pamoja na kujifunza na kupata uzoefu kutoka katika nchi jirani (Ethiopia, Malawi, Afrika Kusini, Uganda, nk). ASDP II itasaidia kubadilishana ushauri katika mnyororo wa thamani na kutoa utaalam maalum wa kiufundi kwa ajili ya kuendeleza bidhaa za kipaumbele kupitia *PPP*.

**Jedwali Na. 32: Muhtasari wa shughuli na maeneo ya utekelezaji katika kukuza masoko katika ngazi ya kitaifa / mkoa**

| Maeneo ya utekelezaji | Shughuli |
|---|---|
| **Utafiti wa soko** (gharama, ushindani kwa bidhaa za kipaumbele katika mnyororo wa thamani | - Fursa za uwekezaji wa masoko ya ndani na nje<br>- Kutathmini gharama za masoko katika makundi kwenye mnyororo wa thamani |
| **Taarifa za soko** | - Kuwezesha kufikia masoko kwa bidhaa za Tanzania<br>- Kuhakikisha ubora wa bidhaa na upatikanaji wake |
| Kuendeleza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi ghalani (WRS) | - Kuwezesha ujenzi na ukarabati wa maghala na usimamizi (tani angalau 5,000);<br>- Kuainisha maghala yatakayotumika katika mfumo wa Stakabadhi ghalani (mahitaji na fursa za WRS);<br>- Kujenga uelewa na uwezo kwa watumiaji wa mfumo na kuwaunganisha wadau (Vikundi vya wakulima, Taasisi za fedha na wanunuzi) katika ngazi mbalimbali;<br>- Kuwezesha utekelezaji wa majaribio wa Mfumo wa Stakabadhi ghalani. |
| Soko la Bidhaa Tanzania (Majaribio) | - Kujenga uelewa kuhusu soko la bidha kwa sekta za umma na sekta binafsi<br>- Kujenga uelewa na uwezo wa wadau wakuu<br>- Kuimarisha uwezo wa 'Bodi ya Usimamizi wa Leseni za ghala' kuwezesha ufanisi wa Soko la bidhaa<br>- Kuboresha mfumo wa kisheria na kutafsiri upya jukumu la bodi za Masoko ya mazao<br>- Kuzingatia mageuzi ya sheria za mazao ambayo itapelekea kutungwa kwa sheria za mazao (marekebisho) No., 20/2009<br>- Kuendeleza mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya soko la bidhaa<br>- Kuandaa mpango wa Biashara kwa ajili ya kupata fedha za kuendesha soko la bidhaa<br>- Kuandaa miongozo na kuongeza uwezo wa wadau wanaohusika<br>- Kuwezesha utekelezaji wa soko la bidhaa<br>- Kuanzisha na kuendeleza matumizi ya taarifa za soko la bidhaa |
| Kuboresha mfumo wa taarifa za masoko | - Kuongeza upatikanaji wa taarifa za masoko kwa kulingana na mahitaji ya kipaumbele cha minyororo ya thamani ya bidhaa<br>- Kuimarisha mfumo wa taarifa za masoko (MIS) uliyopo ili kuziba mapungufu (matumizi ya TEHAMA ili kufanya iwe na ufanisi)<br>- Kukuza ufanisi wa usambaaji wa taarifa za masoko na uwezo wa mtumiaji |

| Maeneo ya utekelezaji | Shughuli |
|---|---|
| Kuhamasisha uuzaji wa mazao ya kilimo katika masoko ya ndani /kikanda na kimataifa | - Kushiriki katika maonyesho mbalimbali ndani na nje ya nchi<br>- Kuhamasisha matumizi ya bidhaa zilizotengenezwa na viwanda vya ndani<br>- Kuboresha na kufikia viwango, ubora na usambazaji wa bidhaa<br>- Kuhamasisha matumizi ya miundombinu ya masoko ikiwa ni pamoja na barabara za vijijini, maghala, masoko ya kimkakati, mipakani vituo vya pamoja vya masoko mipakani, minada, machinjio, vituo vya ukusanyaji wa maziwa<br>- Kuimarisha majukumu ya bodi za mazao (angalia pia eneo dogo 2.2)<br>- Ufuatiliaji na usalama wa bidhaa za kilimo |
| Kuhamasisha bidhaa za samaki | - Kushiriki katika maonyesho mbalimbali ndani na nje ya nchi<br>- Ufuatiliaji na usalama wa bidhaa za samaki na ufugaji wa samaki;<br>- Kujenga uelewa na ushirikiano kati ya sekta za umma na Sekta binafsi |

Chanzo: Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji

225 **Udhibiti wa ubora wa mifugo na uvuvi na uhakika wa usalama wa bidhaa za mifugo na uvuvi.** Maeneo ya kipaumbele ya utekelezaji na mapendekezo ya uwekezaji katika ngazi ya kitaifa / kanda ni pamoja na (**Jedwali Na. 34**).

**Jedwali Na. 33: Shughuli za kipaumbele za udhibiti wa ubora wa mifugo na uvuvi**

| Eneo la utekelezaji | Hatua za kipaumbele |
|---|---|
| Masoko ya mifugo na bidhaa | - Kuwapa wazalishaji elimu na ujuzi juu ya ubora wa bidhaa<br>- Kuimarisha uwezo wa bodi ya udhibiti wa mifugo (bodi ya maziwa, nyama, ngozi, na vyakula vya mifugo)<br>- Kuimarisha na kuoanisha sheria / kanuni ya bidhaa bora za mifugo<br>- Kuimarisha uhusiano kati ya wafugaji na wanunuzi<br>- Kuimarisha bodi ya udhibiti (TSh milioni 500 kwa mwaka) |
| Miundombinu ya masoko ya mifugo | - Uwekezaji katika miundombinu muhimu ya masoko ya mifugo<br>- Kuhamasisha na kusimamia matumizi ya viwango vya sekta kwa ajili ya usalama na ubora |
| Taarifa ya masoko kuhusu mifugo | - Kuimarisha mfumo wa taarifa za masoko ya mifugo (ukusanyaji wa takwimu, usindikaji / uchambuzi na usambazaji kwa kutumia TEHAMA kwa kuwashirikisha wadau wa sekta za umma na binafsi |
| Kuwezesha masoko ya pembejeo bora za mifugo na bidhaa zake ili kukuza uzalishaji na kulinda afya ya wanyama / walaji | - Kujenga uelewa kwa umma juu ya chanjo za mifugo za zinazotengenezwa hapa nchini (chanjo za Newcastle, Antrax blackquarter),<br>- Kuimarisha uwezo wa maabara<br>- Kuhamasisha maabara za Sekta binafsi kwa ajili ya udhibiti ubora<br>- Kusaidia ufuatiliaji wa ubora wa pembejeo za mifugo na chakula kwa wanyama zenye uasilia wa zilipotengenezwa |
| Masoko ya bidhaa za samaki | - Kuboresha viwango na ubora wa samaki na bidhaa zake |
| Uvuvi, masoko na miundombinu | - Uwekezaji katika miundombinu ya masoko na vifaa vya uvuvi<br>- Kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa viwango vya sekta kwa ajili ya usalama na ubora |
| Taarifa za masoko ya samaki na mazao ya baharini (ufugaji samaki) | - Kuboresha na kuimarisha mifumo ya taarifa za masoko ya samaki na bidhaa zake kwa kuzingatia (ukusanyaji wa takwimu, usindikaji na usambazaji kwa kutumia TEHAMA) kwa kushirikisha wadau wa sekta ya umma na Sekta binafsi<br>- Kufanya uchambuzi wa mnyororo wa thamani wa mwani na samaki |
| Ufuatiliaji, kuweka alama na ustawi wa wanyama | - Tasisi za mifugo kuongeza utendaji na ubora<br>- Kukuza uungwaji mkono wa ustawi wa wanyama |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo

**226 Katika ngazi ya Halmashauri,** uwekezaji mkubwa na ukuzaji wa masoko na mnyororo wa thamani wa bidhaa ni vipaumbele katika mipango ya maendeleo ya kilimo ya wilaya. Maeneo muhimu ya kuwekeza ni pamoja na: (i) uboreshaji wa miundombinu ya barabara / usafirishaji; (ii) ukarabati / ujenzi wa masoko ya halmashauri, ikiwa ni pamoja na vifaa vya kuhifadhi-baridi, machinjio, vifaa kwa ajili ya ufugaji wa samaki; na (iii) ushauri wa kitaalam na wa kiufundi wa kilimo-biashara na kujenga uwezo utakaokidhi ubora wa mazao,mifugo na uvuvi. Ufuatiliaji wa uwekezaji katika maeneo ya kipaumbele utafanyika kwa kushirikiana na Jukwaa la Wilaya ambalo linahusisha wadau wa mnyororo wa thamani wa bidhaa katika eneo husika.

### Eneo Dogo 3.2: Uendelezaji wa Kilimo-biashara: Uongezaji wa thamani na usindikaji

227 Uongezaji wa thamani na usindikaji wa mazao ni vitu muhimu kwenye kuchochea kilimo-biashara, mapato na kuongeza ajira katika maeneo ya vijijini, lakini pia matumizi ya mabaki ya usindikaji wa mazao hutumika kwa ajili ya chakula cha mifugo. Ingawa kuna uhusiano mkubwa kwa kutoa fursa za soko kulingana na mahitaji ya bidhaa zilizosindikwa, kiwango cha miundombinu na vifaa vya usindikaji wa mazao bado kipo chini na kinachangia kuwepo kwa uharibifu na upotevu mkubwa wa mazao baada ya mavuno.

**228 Maendeleo ya kilimo-biashara na sekta binafsi.** Kilimo-biashara kina lenga kuleta ushindani kwa kuishirikisha sekta binafsi ili kuchochea maendeleo ya sekta ya kilimo kwa njia ya kuongeza uwekezaji binafsi na huduma katika sekta. Hii itakuwa na mafanikio na pia (i) Hupunguza upotevu wa mavuno na kuongeza thamani, (ii) Kuboresha ufungashaji, utunzaji, uhifadhi katika vifaa vya baridi na usafirishaji wa mazao ya kilimo; (iii) Kuongeza teknolojia kwa ajili ya kutunza mazingira, kwa kuzingatia sheria na kanuni husika; na (iv) Kuongeza ufanyaji wa biashara na mazingira wezeshi ya uwekezaji kwenye eneo la usindikaji.

229 Mikakati ya utekelezaji wa ASDP II ni pamoja na: (i) Kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza, hasa kwa kufuata mfano ulioonyesha mafanikio wakati wa utekelezaji wa SAGCOT, (ii) Kuendelea kuboresha mazingira wezeshi ya kufanya biashara kwa kuwa kuna sera za biashara, taratibu / kanuni za kuuza na kuagiza mazao kutoka nje ya nchi, kuwekeza, kodi, na masuala mengine yanayohusiana na taasisi nyingine, kama vile *TIC*, (iii) Kuanzisha na kuimarisha jukwaa la mazungumzo kati ya wadau wakuu wa Sekta ya umma na Sekta binafsi, kujadili juu ya uboreshaji wa mazingira ya biashara; na (iv) Kupanua huduma za mikopo ya kilimo kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali kama vile *TIB*- kuwa na dirisha la kilimo na Mfuko wa pembejeo za kilimo- *AGTIF*, Benki ya maendeleo ya kilimo -*TADB*, lakini pia uwepo wa Benki za biashara kwa ajili ya kuvutia uwekezaji wa kati na wa muda mrefu katika sekta.

**230 Lengo la hiki kipengele kidogo ni kuwawezesha wakulima wadogo, vikundi vya wakulima na wadau wengine kwenye mnyororo wa thamani ili waweze kuwekeza kwenye mnyororo wa thamani ambao una faida hasa katika eneo la kuongeza thamani kwenye mazao ya kilimo yaliyobainishwa ikiwa ni pamoja usindikaji wa bidhaa za kilimo, ili kuongeza kipato.** Walengwa katika uwekezaji kwenye mnyororo wa thamani katika ngazi ya halmashauri ni wadau wote katika sekta ya kilimo ambao watawezeshwa kitaalamu ikiwa ni pamoja na: (i) kupewa ushauri wa kilimo-biashara na kujengewa uwezo (ii) kupatiwa utaratibu wa uwezeshaji wa mikopo kwa wakulima kwa maendeleo ya kilimo-biashara kwa njia ya ushindani na (iii) kutambua na kuendeleza fursa za biashara. Uelewa kuhusu elimu ya ujasiriamali na kuongeza thamani kwenye bidhaa za kilimo kunawezesha wakulima waishio vijijini kujiajiri wenyewe, hasa vijana na wanawake. Usindikaji wa mazao ni lazima ufanyike ikiwa ni pamoja na kuzingatia taratibu za kuweka mazingira bora ya kazi na usalama kazini, kuzingatia usawa wa jinsia na ajira kwa vijana, kuzuia ajira kwa watoto.

**Jedwali Na. 34: Shughuli za kipaumbele za Kuongeza thamani na usindikaji kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa za kilimo.**

| Maeneo ya uwekezaji | Shughuli kipaumbele |
|---|---|
| Maeneo muhimu yanayowezesha kuendeleza uzalishaji wa kibiashara | - Kuimarisha Taasisi:<br>- Kuzingatia mnyororo wa thamani wa Wilaya / mkoa ambao umezingatia umuhimu wa kilimo-biashara<br>- Kuhakikisha utoaji wa huduma ya kilimo-biashara kwa sekta binafsi katika ngazi ya Mkoa inatolewa |
| Usimamizi wa mifumo ya baada ya mavuno | - Kuimarisha teknolojia za uhifadhi wa mazao ngazi ya kijiji na usimamizi wa kitaalamu unazingatiwa |
| Uwekezaji unaozingatia Kilimo-biashara (usindikaji, kuongeza thamani) kwenye bidhaa za kipaumbele kwa kufuata mnyororo wa thamani | - kuandaa mipango wa biashara inayozingatia kilimo-biashara ikiwa ni pamoja na msaada kwa<br>- Kuboresha miundombinu ya uongezaji wa thamani–usindikaji inayohitajika katika suala la upatikanaji wa huduma kama vile umeme, maji, nk<br>- Kutoa fedha katika eneo la uwekezaji wa ndani kwa kutumia ushindani |

231 Udhaifu uliojitokeza kwenye taasisi ambazo hazikuwa na uwezo na uelewa wa kilimo-biashara, umeathiri uendelezaji wa mnyororo wa thamani wa mazao na bidhaa kupitia miradi mbalimbali iliyobuniwa na kutekelezwa katika ngazi za Halmashauri. Hivyo jitihada zitakazohitajika katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya ni kuboresha uratibu wenye ufanisi wa shughuli zote zinazohusika katika mnyororo wa thamani ambao utakuwa unafanana kwa kila ngazi ya Mkoa. Kwa hiyo, timu ya uwezeshaji ya Mkoa ambayo inaundwa kwa kushirikisha Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni lazima iwe yenye kutoa matokeo chanya ya kuzalisha kibiashara kwa kuijengea uwezo timu ya wawezeshaji ngazi ya Wilaya na wataalamu wanaohusika katika sekta ya kilimo.

232 **Majukwaa ya mnyororo wa thamani wa bidhaa ngazi ya Wilaya.** Ili kuboresha uratibu miongoni mwa wadau katika ngazi ya Halmashauri, uwepo wa majukwaa ya wadau wanaohusika katika bidhaa za kipaumbele kufuata mnyororo wa thamani ni muhimu sana kwa kuwa litasaidia kuendeleza na kuhakikisha utekelezaji wa mikakati ya kuongeza uzalishaji wenye tija, uongezaji wa thamani bidhaa za kilimo na upatikanaji wa masoko unafikiwa. Majukwaa haya yataendeleza mahusiano yenye kuleta tija miongoni mwa wadau wa mnyororo wa thamani wenye lengo la kuongeza uzalishaji, ubora wa mazao, kuongeza thamani na biashara ya bidhaa zilizochaguliwa. Majukwaa haya yatakuwa muhimu katika kuanzisha namna bora ya kuwaunganisha wadau kutoka sekta ya umma na Sekta binafsi na kuleta mabadiliko ya kibiashara kwa walengwa walioko kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa zilizobainishwa. Majukwaa haya ndio yatakayoongoza katika kuweka mikakati na mahusiano mazuri ya kibiashara yatakayojenga uelewa mzuri wa mahitaji ya wazalishaji, wasindikaji, wasafirishaji, wenye maghala, wafanyabiashara na masoko. Majukwaa haya pia yatashiriki kwenye ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo ya sekta ngazi ya wilaya.

233 **Timu ya wawezeshaji ngazi ya ya Mkoa. Uelewa wa kilimo biashara katika ngazi ya wilaya bado hauridhishi,** Ni jukumu la timu ya wawezeshaji ngazi ya Mkoa kutoa huduma za masuala ya kitaalamu katika ngazi ya Halmashauri na itasaidia watendaji na vikundi au ushirika kuendeleza mnyororo wa thamani ili mkulima aweze kupata faida kutokana na shughuli za uzalishaji, kuongeza thamani na masoko ya bidhaa za mazao ya kipaumbele. Timu hii ni chombo muhimu kwa ajili ya kushirikisha wadau mbalimbali kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa na mazao katika ngazi ya halmashauri. Katika maeneo ambayo hayana watoa huduma, au watoa huduma ambao hawana uwezo, ASDP II itasaidia kuhamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa watoa huduma hizo kwa kutoa elimu na kujenga uwezo kwa watoa huduma zinazohitajika katika eneo husika. Huduma hizi zitatolewa kwa kuingia mikataba na walengwa walioko kwenye mkoa (au makundi yaliyoko kwenye wilaya) ambayo yatatumika kujenga uwezo na utoaji wa huduma za kilimo-biashara kwa vikundi vya wakulima na wadau wengine walioko kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa zilizobainishwa.

234 **Mfumo wa uhifadhi wa mazao baada ya kuvuna una** lengo la kuhakikisha kuwepo kwa uhakika na ufanisi katika usambazaji wa chakula unaozingatia maeneo muhimu kati ya uzalishaji na matumizi ya chakula. Upotevu wa chakula baada ya mavuno umeendelea kuwa jambo linalohitaji kupewa umuhimu.

Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa wakulima hupoteza hadi asilimia 40 ya nafaka zinazozalishwa, ingawa upotevu huo hutofautiana kwa kiasi kikubwa kulingana na aina ya zao na eneo au ukanda wa kijiografia. Suala muhimu ni kuhakikisha mazao yaliyovunwa hayaathiriwi dhidi ya hali ya hewa (maji, joto na vumbi) na mabadiliko ya kibaolojia ya mazao (sumu kuvu, ukungu, wadudu na wanyama waharibifu). Pia kupunguza uharibifu wakati wa usafirishaji na uhifadhi. Kwa mantiki hiyo, ipo haja ya kupitia na kuboresha majukumu yanayotekelezwa na Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara hasa katika kuhuisha shughuli zinazohusiana na miundombinu ya kuhifadhi, kusimamia na kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna na kuongeza thamani na usindikaji wa mazao ya kilimo.

**Jedwali Na. 35 Hatua za kipaumbele za kuelekea kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno**

| Upunguzaji hasara za mazao baada ya mavuno | |
|---|---|
| **Maeneo ya utekelezaji** | **Hatua/ shughuli zilizo pendekezwa** |
| **Upotevu mkubwa wa mazao baada ya mavuno** kutokana na mifumo/ teknolojia duni na uwezo mdogo wa uhifadhi | i. Kundaa na kusambaza miongozo ya jinsi ya kuhifadhi mazao kabla na baada ya mavuno kwenye mazao yaliyochaguliwa (kipaumbele muhimu kuzingatiwa ni uwepo wa sumu kuvu kwenye nafaka)<br>ii. Kuandaa miongozo sahihi ya utunzaji wa vyama, maziwa na ngozi baada ya kusindikwa<br>iii. Kuhamasisha na kusambaza teknolojia ambazo zinazohamasisha utunzaji na usalama wa chakula unaohusisha bidhaa za mifugo kama vile nyama, maziwa na ngozi)<br>iv. Usimamizi wa hifadhi wa kitaalamu (angalia COWABAMA)<br>v. Kuimarisha miundombinu bora ya masoko eneo dogo 3.3) |
| **Bidhaa au mazao yanayoharibika kwa muda mfupi** (kilimo cha mazao ya bustani) bidhaa za mifugo na uvuvi (maziwa, nyama, samaki nk) | i. Kuimarisha miundombinu ya masoko ikiwemo vifaa vya kuhifadhi baridi<br>ii. Ushirikishwaji wa sekta binafsi zinazohusika katika kuleta mageuzi& upatikanaji wa masoko<br>iii. Kutoa uelewa kuhusu ubora wa bidhaa na jinsi ya kufikia ubora huo |
| Kuhuisha Sera Sheria na kanuni zilizopo kwenye Taasisi za Sekta ya Umma | Kuhuisha maeneo yanayohusu miundombinu na usimamizi wa uhifadhi, kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno na kuongeza thamani zinazohusisha Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |

235 **Uhifadhi ya mazao ngazi ya kijiji kupitia mfumo wa uwekezaji wa Ghala *(COWABAMA)*.** Lengo la uwekezaji huu, ni kuendeleza na kuhamasisha wakulima wadogo kuyafikia masoko na kupata faida baada ya kuhifadhi bidhaa zilizobainishwa kwenye maghala. Hii itasaidia kuwaunganisha na wanunuzi wakubwa walioko ndani na nje ya nchi. Kwa kuanzia Mradi utaanza na ujenzi wa maghala 275 yatakayohifadhi mahindi katika maeneo yanayosimamiwa na SAGCOT na maghala 78 kwa ajili ya kuhifadhi mpunga katika skimu za umwagiliaji. Maghala yatakayojengwa yatakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani nyingi zaidi na kunufaisha takriban kaya 165,000. Baadaye, mpango huu unatarajia kuenea katika wilaya nyingine ambazo zina uwezo wa mkubwa wa kuzalisha mahindi na kuongeza bidhaa nyingine zenye fursa za kibiashara, kama vile alizeti maziwa na kilimo cha bustani.

236 Mpango huu (COWABAMA) utaendelea kukarabati maghala yaliyopo vijijini na kuongeza ujenzi wa maghala mapya. Kwa ujumla, mradi huu utahusisha: (i) Kuimarisha vifaa vya uhifadhi na miundombinu ya masoko (kuunganisha barabara za mashambani) katika ngazi ya kijiji; (ii) Kuhamasisha uhifadhi wa mazao kwa pamoja, (iii) Kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara hasa katika maeneo ya kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ubora wa bidhaa, (iv) Kusaidia upatikanaji wa njia zinazoongeza uzalishaji ili kuhakikisha usambazaji wa bidhaa kwa ajili ya matumizi sahihi ya maghala, na (v) Kuunganisha maghala yaliyohifadhi bidhaa na mfumo wa stakabadhi ghalani, soko la bidhaa na huduma za kuongeza thamani. Kwa miaka minne na kuendelea, mradi huu itaendelea kusambazwa katika wilaya nyingine na bidhaa za kipaumbele (mazao na mifugo) zilizoko kwenye kanda za kilimo za kiikolojia. Kwa kutumia mafanikio yaliyopatikana, programu itaendelea kusambazwa zaidi hadi kwenye kanda nyingine za kilimo za kiikolojia ambazo zitahusisha bidhaa za kipaumbele kama vile alizeti na maziwa/nyama, ili kupunguza umaskini katika maeneo ya wilaya kwa kila ikolojia ambayo itatumika kama eneo la kupata uzoefu.

237 Uwekezaji unaohusu kilimo-biashara (usindikaji, kuongezaji wa thamani ) kwa kufuata mnyororo wa thamani wa bidhaa za kipaumbele. Mbali na ushauri na kujenga uelewa, ASDP II itahamasisha uwekezaji katika ngazi ya Taifa na ngazi ya Serikali za Mkoa na mitaa utakaohusisha uhitaji unaohitajika katika kilimo biashara, kuimarisha miundombinu ya uhifadhi kibiashara na kuhamasisha Sekta binafsi kuwekeza katika maendeleo ya kilimo- biashara.

238 Sekta za umma zitahusika katika kuwezesha utoaji wa huduma za kiufundi kwa ajili ya utekelezaji katika ngazi ya Serikali za mitaa. Mapendekezo ya maeneo ya kipaumbele ya utekelezaji yanayolenga usindikaji wa bidhaa ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.36.**

**Jedwali Na. 36: Maeneo ya kimkakati ya utekelezaji yaliyopendekezwa kwa ajili ya kuongeza thamani na usindikaji wa mazao**

| Maeneo ya utekelezaji | Shughuli za kimkakati |
|---|---|
| Kuainisha wajasiriamali | - Kuanisha wajasiriamali, vyama vya wajasiriamali, na shughuli wanazofanya katika minyororo ya thamani ya bidhaa iliyolengwa |
| Mafunzo kwa Wajasiriamali | - Kupanga mafunzo ya wajasiriamali katika mpango wa biashara wa usindikaji wa mazao, hasa kuongeza thamani ya bidhaa zilizopo kwenye mnyororo wa thaamni ndani ya kila Kanda ya Kilimo ya Kiikolojia. |
| Ufungashaji na utambulisho | - Kubainisha mahitaji/kujenga uelewa wa wajasiriamali kwenye mpango wa biashara kwa kufuata vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mnyororo wa thamani<br>- Kujenga uelewa kwa wajasiriamali na vikundi vya wajasiriamali<br>- Kuhamasisha umiliki wa bidhaa na ubora<br>- Kuunganisha wasindikaji na wazalishaji wa vifungashio (kutembelea maeneo yenye uzoefu, mafunzo kwa vitendo, kujifunza kulingana na mahitaji, nk) |
| Viwanda vya kisasa vya kusindika mazao kwa ajili ya minyororo ya thamani ya bidhaa iliyochaguliwa | - Kutambua mahitaji ya kipaumbele katika mnyororo wa thamani wa bidhaa<br>- Uhamasishaji, utafiti, uchunguzi, kujenga uwezo na kutoa huduma za kiufundi za kilimo-biashara<br>- Kuwezesha utumiaji wa zana za kisasa kwa kuendeleza teknolojia na mpango wa fedha (msaada na kanuni ngazi ya taifa) |
| Kuhamasisha utumiaji wa zana za kisasa zinazopunguza upotevu wa bidhaa baada ya kuvuna | - Tathmini ya matumizi na ubora wa zana za kisasa<br>- Kuhamasisha zana bora zinazopunguza upotevu wa bidhaa<br>- Kuwa na sampuli za mfano kwa ajili ya utunzaji wa bidhaa baada ya mavuno katika minyororo ya thmani ya bidhaa |
| Kuboresha ubora wa bidhaa na ufuatiliaji | - Kujenga uwezo/uelewa wa ufuatiliaji wa bidhaa<br>- Kuwa na maabara zilizokubalika na kupewa cheti cha ubora kimataifa kwa ajili ya kudhibiti ubora wa bidhaa |
| Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Ujasiriamali (NEDF) | - Kuhamasisha matumizi ya Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Ujasiriamali |
| Kuanzishwa kwa wajasiriamali kwenye kanda maalumu za uuzaji wa bidhaa za kilimo nje ya nchi | - Kuainisha na kutambua maeneo kwa ajili ya kuanzisha kanda maalum ya uuzaji wa bidhaa za kilimo nje ya nchi<br>- Kuhamasisha sekta binafsi kuendeleza kanda maalum ya kuuza bdhaa za kilimo nje ya nchi<br>- Kufuatilia utekelezaji wa maendeleo ya kanda maalum ya kuuza bidhaa za kilimo nje ya nchi (EPZ) |
| Kuanzisha na kuendeleza kongano za viwanda vya kukamua alizeti | - Kuainisha na kutambua maeneo kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya kukamua alizeti<br>- Kuhamasisha wadau kuanzisha kongani za viwanda vya kukamua mafuta ya alizeti<br>- Kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa kongani za viwanda vya kukamua alizeti |

Chanzo: Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, 2015

239 Maeneo ya kipaumbele yaliyotambuliwa kwa ajili ya usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao na mifugo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 37**

**Jedwali Na. 37: Maeneo ya kimkakati ya utekelezaji yaliyopendekezwa kwa ajili ya kuongeza thamani na usindikaji wa mazao (mifugo / uvuvi).**

| Maeneo ya utekelezaji | Shughuli za mkakati |
|---|---|
| **Usindikaji maziwa** | - Kuendeleza miundombinu na vifaa vya ukusanyaji na usindikaji wa maziwa (takribani shilingi milioni kila moja)<br>- Kuzingatia ubora (mafunzo kuhusu ubora na usalama wa bidhaa za maziwa) |
| **Usindikaji nyama** | - Kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora kwa kuwekeza katika usindikaji nyama, vifaa vya machinjio, mafunzo katika usindikaji.<br>- Kujenga machinjio 5 katika maeneo muhimu ya masoko ya mifugo (takribani TSh bilioni 3 kila moja) |
| **Usindikaji wa ngozi** | - Kuhamasisha uzalishaji na ubora wa ngozi, ukusanyaji na usindikaji |
| **Bidhaa nyingine za mifugo** | - Kuhamasisha uzalishaji, usindikaji na utunzaji wa bidhaa nyingine za mifugo |
| **Usindikaji wa Dagaa Kutoka kwenye maji baridi** | - Kuhamasisha ubora wakati wa uchakataji na kuongeza thamani<br>- Mafunzo juu ya bidhaa salama na bora<br>- Kuboresha ukusanyaji wa 'dagaa' na mbinu sahihi za uvuaji dagaa (Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa na Rukwa) |
| Uhamasishaji wa kuongeza thamani, usindikaji, utunzaji wa bidhaa nyingine za samaki | - Kuboresha mbinu sahihi za uvuvi salama; kupunguza upotevu wa samaki baada ya kuvua |
| **Bidhaa zingine za uvuvi** | - Uongezaji wa thamani wa zao la mwani |
| **Kanuni za mifugo na uvuvi** | - Kuwezesha bidhaa za mifugo na ubora wa bidhaa nyingine za mifugo<br>- Utoaji wa leseni na usajili wa vyombo vya uvuvi |

240 **Katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kuwezesha uwekezaji wa kilimo biashara** katika ngazi ya Halmashauri kwa kufuata mnyororo wa thamani wa bidhaa za kipaumbele (CVC) utahamasishwa kwa kufanya yafuatayo: (i) Kuboresha miundombinu inayohitajika kama vile umeme na maji nk.; (ii) Kuimarisha kilimo-biashara ikiwa ni pamoja na kusaidia uandaaji wa mipango ya kibiashara na kusaidia uwekezaji kwa kutumia ruzuku ya ushindani. Miundombinu hiyo itawezesha wajasiliamali kuwekeza katika usindikaji wa mazao ya kilimo na uongezaji wa thamani.

241 **Uwekezaji wa umma katika kilimo-biashara.** Kama ilivyokuwa wakati wa utekelezaji wa ASDP-1, ugharamiaji katika shughuli za uwekezaji ulifanyika kwa kutumia dirisha la ruzuku ya uwekezaji (DADG) katika kuwezesha uendelezaji wa miradi bora ya uwekezaji ya kipaumbele iliyosimamiwa na sekta ya umma kwa kuendeleza miundombinu iliyolengwa (barabara, masoko n.k) na miundombinu ya upatikanaji wa (maji, umeme n.k.) ili kuwezesha uendelezaji wa minyororo ya thamani ya mazao katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uchaguzi wa mradi na utekelezaji utazingatia utaratibu uliotumika wakati wa ASDP-1 ambapo mchango wa wanufaika na Mamlaka za Serikali za Mitaa utakuwa unaongezeka taratibu kulingana na ongezeko la mapato yatokanayo na minyororo ya thamani ya mazao ya kipumbele yaliyochaguliwa.

### Eneo Dogo 3.4: Kuongeza Upatikanaji wa Fedha Vijijini

242 **Usuli:** Kutotosheleza kwa huduma za kifedha zinazotolewa kwa wakulima wadogo wa kibiashara ni kikwazo kikubwa kwa ukuaji wa kilimo na inakuwa kizuizi cha kuongezeka kiwango cha uwekezaji na kasi ya ukuaji wa kilimo cha kibiashara. Benki za kibiashara zinasita kutoa mikopo kwa sekta ya kilimo na zinashindwa kufika katika maeneo ya vijijini. Kuna taasisi chache zinazotoa huduma za kifedha zinazolenga wakulima, lakini pia zina uwezo mdogo wa kuzifikia kaya nyingi za vijijini kutokana na uhaba wa wafanyakazi wenye ujuzi, mtandao wa matawi machache na huduma za fedha. Wajasiriamali wadogo na wa kati wanaojihusisha na uongezaji wa thamani pia hukutana na kikwazo cha upatikanaji wa rasilimali fedha.

243 Kwa sasa, hatua zilizoasisiwa na Serikali za kuhamasisha kuwepo kwa taratibu za upatikanaji wa huduma za kifedha kwa ajili ya kilimo zinahusisha yafuatayo (i) Mfumo jumuishi wa kifedha wa kitaifa

(Kamati ya Uendeshaji iko chini ya uenyekiti wa Benki Kuu ya Tanzania na ina wajumbe kutoka Wizara ya Kilimo, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (*CMSA*), Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (*TIRA,*) Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), Mfuko wa Udhamini wa Sekta ya Fedha (*FSDT*), Chama cha Taasisi za Kutoa Huduma Ndogo Ndogo za Fedha (*TAMFI*) na Waendeshaji wa Makampuni ya Simu za Mikononi; (ii) Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOs*), hukopesha akiba na fedha ilizokopa kutoka katika benki za biashara kwa Wakulima wadogo walio Wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo, lakini pia taratibu kama hizo hufanyika kupitia Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACAS*) na Benki za Jamii Vijijini (*VICOBA*) na Vyama vingine vya aina hizo; (iii) Mfumo wa Stakabadhi za ghalani kwa ajili ya wakulima wadogo kufikia huduma za kifedha kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao za kilimo (hususan kwa mazao asilia ya biashara); (iv) Benki ya Taifa ya Ushirika ambayo inalenga kutoa huduma za kifedha kwa vyama vya ushirika (Vyama Vikuu vya Ushirika); (v) Dirisha la utoaji mikopo lilopo katika Benki ya Rasilimali Tanzania; (vi) Benki ya Ushirika Kilimanjaro na Benki ya Ushirika ya Wakulima Kagera; (vii) Kutoa mikopo kwa vijana ili kushiriki katika shughuli za kuongeza kipato ikiwa ni pamoja na kilimo (Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo); (viii) Mamlaka za Serikali ya Mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato kutoka vyanzo vyake vya ndani na kuzielekeza katika kukopesha vijana na wanawake katika eneo lao la Utawala;(ix) Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo *(AGITF*) ambao uko chini ya Wizara ya Kilimo; (x) Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kutoa mikopo kwa watu binafsi na vyama vya ushirika (Wakulima scheme); (xii) Mfumo wa Taifa wa Vocha za Pembejeo za Kilimo (*NAIVS*) na programu nyingine zitakazofuatia; na (xiii) Programu ya Kuboresha Miundombinu ya Masoko kuongeza Thamani na Huduma za Fedha Vijijini (*MIVARF*) [62] kutoa ruzuku kwa Vikundi vya Umwagiliaji au Vyama vya Ushirika vya Masoko ya Mpunga kwa ajili ya ununuzi wa mashine za ukubwa wa kati za kukoboa mpunga. Serikali imeanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa ajili ya kutoa mikopo ya uwekezaji katika sekta, wakati Mfuko Kichocheo (angalia mfano wa *SACGOT*) na Mpango wa Dhamana ya Mikopo ni baadhi ya hatua mbalimbali zilizoasisiwa kuelekea Biashara husishi za vijijini.

**244** Idadi ya benki za biashara inaongezeka (Takriban benki 50 mwaka 2014) na baadhi ya benki hizo zimepanua wigo wa huduma zao hadi katika sekta ya kilimo na usindikaji wa mazao ya kilimo. Utoaji wa huduma za kifedha (mazao na mifugo) kutoka benki za biashara kwa maana ya mkopo kwa jumla katika sekta umekuwa ukiongeza taratibu na kufikia kiwango sawa na asilimia 10 ya mikopo yote inayotolewa (Takriban Shilingi Trilioni 1). Mfuko wa Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (*Private Agriculture Sector Support -PASS*) ambayo ilianzishwa mwaka 2000 kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*) kupitia Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini (*CRDB*) imekuwa ikitoa msada wa kuandaa mipango biashara na udhamini. Taasisi zilizo rasmi na zisizo rasmi za utoaji huduma ndogo za fedha (MFIs), utoaji wa huduma za kifedha kwa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) pia zinasaidia uchumi wa kilimo wa wakulima wadogo katika maeneo ya vijijini. Hatua zilizoasisiwa za kuwepo mfumo jumuishi wa huduma za kifedha wa Kitaifa kupitia Wizara ya Fedha na Mipango zinakusudia kuwa na mpango wa utekelezaji unaolenga asilimia 50 ya watu wazima kupata huduma rasmi za kifedha ifikapo 2016.

**245** Kwa ujumla jitihada mbalimbali zinazoasisiwa na umma, zinazohusiana na miradi na taasisi za kifedha zipo katika ngazi ya Taifa na ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuhamasisha ufikiwaji wa huduma za kifedha za sekta ya Umma, lakini hakuna mkakati ulio wazi (na mpango wa kueleweka na kabambe wa utekelezaji ) unaohamasisha uwepo wa mifumo ya utoaji huduma za kifedha Vijijini ili kuongeza uwekezaji wa wadau katika sekta ya kilimo kupitia ubia endelevu wa kati ya sekta za Umma na Binafsi. Kuboresha huduma za kifedha katika sekta ni suala muhimu la sera ili kuwezesha uwekezaji wa sekta binafsi.

**246** **Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDS),** Kwa kuzingatia Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo hatua zinazotarajiwa kuchukuliwa ni pamoja na: (i) Kuhamasisha huduma za benki za kijamii zilizopo na kuanzisha nyingine mpya katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; (ii) Kubuni vifurushi vya mikopo ya kilimo vinavyowafaa wakulima wadogo; (iii) Kutoa msaada wa kuanzisha taasisi imara za kifedha ngazi za chini kama vile Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo

62 *Kwa ajili ya huduma za kifedha vijijini MIRVAF inalenga kuboresha vyama visivyo rasmi katika ngazi ya chini , SACCOS taasisi zingine ndogo za kifedha, na wajasiriamali wadogo na wa kati vijijini.*

(*SACCOS*) na Benki za Jamii Vijijini (*VICOBA*) ikiwa ni chanzo cha awali cha kutoa huduma za kifedha kwa wakulima wadogo wa kibiashara; (iv) Kuhuisha Sera ya Taifa ya huduma ndogo za fedha kwa kushirikiana na Wizara zingine ili zizingatie mabadiliko ya sasa ya kiteknolojia kama vile matumizi ya huduma za kibenki kwa kutumia simu za mikononi, mifuko ya malipo ya uzeeni na Bima, ambayo ni muhimu kwa kaya za vijijini zinazoingia katika kilimo cha kibiashara; (v) Kuimarisha majukumu ya usimamizi/udhibiti ya Idara ya Ushirika katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji wa Taasisi za Huduma ndogo za kifedha; (vi) Kuharakisha juhudi za kupanua huduma za kifedha katika kilimo kupitia dirisha la kilimo lililopo Benki ya Uwekezaji Tanzania (*TIB*), Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (*AGITF*), kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa ajili ya uwekezaji wa muda mrefu na wakati kwenye uzalishaji na usindikaji katika kilimo; na (vii) Kuhamasisha utoaji wa mikopo kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo kutoka mabenki ya biashara.

247 Maeneo ya kipaumbele ya kufanyia kazi kwa ajili ya kupanua huduma za kifedha vijijini kwa ajili ya wazalishaji wadogo na wajasiriamali/wasafirishaji nje ya nchi (Wajasiriamali wadogo na wa Kati / wenye viwanda vidogo na vya kati, ni pamoja na :

i. **Kuandaa mkakati kabambe wa huduma za kifedha wa vijijini pamoja na** mpango wa utekelezaji kwa ajili ya kuhamasiha uwekezaji wa kibiashara na faida katika uendelezaji wa minyororo ya thamani ya mazao ya kilimo kwa wadau wote wanaoshiriki.

ii. **Kuimarisha Vyama vya Ushirika na vyama vingine vya kiuchumi pamoja na** Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa (*SACCOS*)/ Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACAS*) vinavyohusiana na hivyo (udhibiti wa kijamii kama dhamana) kwa ajili ya kutoa huduma endelevu za kifedha (ndogo) (na zinazomilikiwa na wadau) katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

iii. **Kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha katika sekta ya kilimo** za muda mfupi hadi za muda wa kati kupitia utaratibu wa ubia kati ya Umma na Sekta Binafsi, kwa kushirikisha wengine, Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Mabenki Binafsi yanayowekeza katika sekta za maeneo ya vijijini , n.k.

iv. **Kuwezesha wakulima katika uwekezaji wa kilimo** kwa kufanya yafuatayo kati ya mengine: (a) Kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa stakabadhi ghalani ili kuepuka suala la dhamana; (b) Kuimarisha kilimo cha mkataba (makubaliano ya kimkataba kati ya vyama vya wazalishaji, wafanyabiashara za kilimo, wasafirishaji nje ya nchi benki/na watoa huduma za kifedha; (c) kuandaa mfumo wa sera wa kisheria kwa ajili mikataba ya 'kukodisha', huhusan kwa ajili ya kuhamasisha utoaji wa huduma binafsi za matumizi ya zana za kilimo (makubaliano ya kimkataba kati ya waagizaji wa zana, mabenki ya uwekezaji pamoja na watoa huduma binafsi wa zana za kilimo).

**248 Mkakati Kabambe wa Huduma za kifedha Vijijini na Mpango wa Utekelezaji.** Kuna fungamano dogo miongoni mwa hatua kadha zilizoasisiwa na sekta ya umma na binafsi katika kuhamasisha kuwepo kwa utaratibu wa kutoa huduma za kifedha vijijini, hivyo kusababisha kuwepo kwa haja ya kuandaa, kuimarisha na kutekeleza mkakati unaohusisha wadau mbalimbali ili kukuza uwekezaji katika kilimo. Mikakati kwa ajili ya kuboresha viungo vya huduma za kifedha vijijini inaweza kujumuisha yafuatayo (i) Kuhamasisha na kuimarisha udhibiti wa sekta yenyewe kupitia mitandao ya Asasi za Vyama vya Ushirika vya SACCOS za Vijijini; (ii) Kuwezesha uunganishwaji wa Asasi za Wakulima (vyama) na Vyama vya Ushirika vya huduma za kifedha, taasisi za mikopo midogo na/au benki za biashara; (iii) Kuongeza uwezo wa wazalishaji, wafanyabiashara, vyama vya wasindikaji, vyama na vyama vya ushirika kujadiliana kwa kuwapatia taarifa bora za hali ya masoko, ukusanyaji wa pamoja wa mazao na kutumia fursa za huduma za kifedha; (iv) Kuimarisha Sekta ya Umma katika majukumu yake ya kudhibiti sekta ya fedha.

**249 Huduma za kifedha ngazi za chini**[63], kwa lengo ni kuzijengea uwezo taasisi zisizo rasmi za huduma za kifedha na SACCOS kwa kuziimarisha ili ziwe vyombo endelevu vinavyojitosheleza, kuzisaidia Taasisi za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (*MFIs*) zilizochaguliwa ili ziweze kupanua wigo wa ufikiaji wa Jamii za Vijijini na kusaidia benki ya kijamii yaliyochaguliwa kama mbadala wa watoa huduma za kifedha Vijijini. Kipengele kidogo husika pia kinalenga kusaidia maendeleo ya ushirika Tanzania kuimarisha utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika. Maeneo

63 *Angalia pia MIRVAF na tulichojifunza (IFAD).*

ya utekelezaji ni pamoja na kuimarisha utendaji wa kifedha na undeshaji wa vyama visivyo rasmi ngazi ya chini, *SACCOS* na Taasisi zingine za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (*MFIs*) (vyama visivyo rasmi kugeuzwa kuwa Taasisi za utoaji huduma ndogo za fedha katika misingi uendelevu), lakini pia kuimarisha uhusiano wa kiutekelezaji kati ya taasisi za utoaji huduma ndogo za fedha na taasisi rasmi za kifedha/mikopo.

**250** **Mfumo wa Stakabadhi Ghalani (WRS)**[64] kutumia mazao yaliyoko ghalani kama dhamana ya kuweza kupata mkopo unaowezekana kutoka Taasisi za kifedha zinazoshiriki.Taasisi za kifedha uweka vigezo kwa waendesha ghala wanaostahili kupata mikopo kwa kuzingatia orodha ya vigezo vya kupima na rejea ambavyo ni pamoja na: (i) Utawala na muundo wa uanachama ; (ii) Kuwepo kwa sheria ndogo ndogo, nyaraka za maelekezo na dondoo za mikutano ; (iii) Tamko la kifedha ambalo ndani yake hujumuisha tamko la mapato, matumizi, faida/hasara katika biashara (na mizania ya mali na madeni (iv) Mali; (v) Historia ya mikopo; na (vi) Makubaliano ya kimkataba na wanunuzi wa mazao. ASDP II itasadia taasisi za kifedha zinazoshiriki katika usimamizi wa dhamana ya mazao yaliyohifadhiwa ghalani, kufanya uchambuzi wa mnyororo wa thamani, usimamizi wa vihatarishi katika kilimo; na utafiti na ufuatiliaji wa masoko ili kupunguza athari zitokanazo na kudiriki kufanya shughuli hizo. Kwa ajili ya kuimarisha ufikiwaji wa taasisi za huduma za kifedha vijijini katika kupata takwimu za fursa za kutoa huduma za kifedha, uchambuzi wa kina wa kifedha utafanyika kwa ajili ya kufahamu mapato halisi kama asilimia ya mapato ghafi uwezo wa kutumia rasilimali ili kupata faida, na uwezo wa kurejesha mkopo n.k, kwa wadau wote katika minyororo ya thamani wanaopata msaada na kuandaa nyaraka za maelekezo/kiada na miongozo ya mafunzo kwa ajili ya kutumia katika kutambua fursa za kifedha na kuchambua mapendekezo ya maombi ya kupata fursa hizo.

251 Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (*FAO*) kwa kushirikiana na mradi wa *Rabobank/ NMB Foundation* lina lengo la kujenga uwezo wa usimamizi wa fedha miongoni mwa wazalishaji na asasi zao, kujenga uhusiano endelevu na watoa huduma za kifedha wa ndani na mawakala wa minyororo wa thamani katika kilimo, na kuboresha mbinu zenye tija. Shirika hilo litaimarisha uhusiano kati ya asasi za wakulima na watoa huduma za kifedha, hali ambayo pia itatoa nafasi ya kuandaliwa kwa mkakati wa masoko wa muda mrefu. Vyama vya wakulima wadogo wa mpunga vitarasimishwa na kuwa Vyama vya Ushirika wa Masoko ya Mazao ya Kilimo (*AMCOS*) ili kufikia uwezo wa viwango vinavyohitajika na kupata uwezo wa kujadiliana bei yenye faida, kuimarisha mahusiano ya kibishara kati ya asasi za wakulima na washiriki wengine katika mnyororo wa thamani wa mchele na kujenga uwezo wa wakulima wadogo katika kusimamia mikopo na kushiriki katika Mfumo wa Stakabadhi ghalani wa kitaifa ambao utawafanya wakopesheke.

**252** **Upatikanaji wa huduma za kifedha za kipindi cha muda mfupi na wa kati** kwa ajili ya kupata pembejeo na uendeshaji wa maghala ambao utasaidia katika uongezaji wa thamani, uboreshaji wa ubora wa nafaka na ukusanyaji mkubwa katika chama/chama cha ushirika wa ujasiriamali cha mkulima ambao ni kigezo muhimu cha mafanikio. Uboreshaji wa ufikivu wa huduma za kifedha vijijini kwa washiriki katika mnyororo wa thamani na wakulima kwa kuwanganisha na taasisi madhubuti za utoaji huduma za kifedha, zikiwemo benki za biashara, lakini pia kuwa na ubia na hatua zilizoasisiwa na mipango mingine katika sekta ya huduma za kifedha vijijini[65]. Katika mwaka wa kwanza, taasisi kadhaa za kifedha zinazoshiriki wa utekelezaji, na taratibu za utoaji wa huduma za kifedha zitabainishwa kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kifedha katika kongani zilizolengwa.

253 Hata hivyo, kutokana na riba kuwa kubwa na ukosefu wa dhamana za mikopo, bado imekuwa ni vigumu kwa vikundi vya wakulima na makampuni binafsi kukopa mikopo ya muda wa kati hadi ya muda mrefu kwa ajili ya uwekezaji katika miundombinu na zana. Hali hii imezuia uwekezaji katika kilimo kwa kiasi kikubwa na hivyo taratibu zinazostahili zinahitajika kuandaliwa. Hata kwa mikopo ya msimu, riba hupungua sehemu kubwa ya mapato halisi ya nyongeza kutokana na uwekezaji (pembejeo) na ufanisi mdogo katika ukuaji wa tija. Kwa muktadha huu, ruzuku lengwa (kama vile riba), mifuko maalum ya wakfu na taratibu zingine kama hizo zinahitaji kujadiliwa na wadau wote wa sekta ili kuwezesha ufikivu endelevu wa huduma za kifedha kwa wadau wa sekta kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo, bila kuingiliana na mfumo wa kifedha.

64 *Angalia pia COWABAMA katika eneo dogo 3.2.*

65 *Programu itashirikiana na mipango mingine ambayo inatoa fedha kwa ajili ya Kilimo ili kuwa na chanzo kinachoaminika cha taarifa katika ngazi zote. Angalia pia shughuli za Rabobank,n.k .*

**254 Maeneo Makuu ya Uwekezaji na shughuli kwa ajili ya kuboresha uwekezaji endelevu katika vijiji/kilimo yameandaliwa kwa kifupi katika Jedwali Na. 38.**

**Jedwali Na. 38: Maeneo ya utekelezaji na Shughuli kwa ajili ya kuboresha uwekezaji katika vijiji/kilimo (rasimu)**

| Maeneo ya Utekelezaji | Shughuli |
|---|---|
| Kuwa na Mkakati Kabambe wa utoaji Huduma za kifedha vijijini na mpango wa utekelezaji | - Kuandaa Rasimu na kuimarisha mkakati kabambe wa kugharamia uwekezaji katika kilimo kwa wadau wote wanaohusika<br>- Kuandaa na kuweka mpango wa utekelezaji kwa ajili uimarishaji wa kutoa na ufikivu wa huduma za kifedha vijijini, ugharamiaji na utaratibu wa utekelezaji wake |
| Kuimarisha uwezo wa kitaasisi na kiufundi wa wazalishaji, wakulima wadogo waliopo na wapya, Asasi na Vyama vya Ushirika vya Wakulima Wafanyabiashara na Wasindikaji | - Kufundisha na kuimarisha uwezo wa kitaasisi na kiufundi wa Asasi za wakulima ili kuimarisha nguvu ya kujadili biashara ya mzalishaji, mfanyabiashara na msindikaji<br>- Kuwezesha uhusiano baina ya Asasi/vyama vya wakulima na vyama vya Ushirika vya Huduma za kifedha -Taasisi za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (*MFIs*)- na/au benki za Biashara<br>- Kuimarisha udhibiti wa sekta yenyewe (ukaguzi) kupitia mtandao wa Asasi kwa ajili ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) vya Vijijini<br>- Kusaidia uenezaji wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani (*WRS*) kwa kupanua katika maeneo mapya na kuongeza mazao mapya<br>- Kuhamasisha uhusiano kati ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) na Vyama vya Ushirika wa Masoko ya Mazao ya Kilimo (*AMCOS*); kutoa mafunzo ya usimamizi wa Asasi za wakulima (*FOs*) / Vyama vya Ushirika wa Masoko ya Mazao ya Kilimo (*AMCOS*) na kwa Wajumbe wa Bodi kuhusu utawala bora na usimamizi . |
| Kuimarisha uwezo wa kitaasisi na kiufundi wa wazalishaji, wakulima wadogo waliopo na wapya, Asasi na Vyama vya Ushirika vya Wakulima Wafanyabiashara na Wasindikaji | - Kusaidia upanuzi wa ufikiaji wa mabenki ya jamii yaliyochaguliwa kama mbadala wa watoa huduma za kifedha vijijini<br>- Kujenga uwezo wa Taasisi zisizo rasmi za huduma za kifedha na Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) ili kuziimarisha ili ziwe vyombo endelevu vinavyojitosheleza, vinavyosaidia Taasisi za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (*MFIs*) zilizochaguliwa<br>- Kuboresha utendaji na uendeshaji wa vyama visivyo rasmi vya ngazi ya chini, Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo(*SACCOS*) na Taasisi zingine za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (*MFIs*)<br>- Kusaidia Tume ya Maendeleo ya Ushirika ya Tanzania ili kuimarisha utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Ushirika na Modenaizesheni |
| Kuongeza upatikanaji na ufikivu wa huduma za kifedha katika sekta ya kilimo za muda mfupi hadi za muda wa kati | - Utoaji wa msaada wa huduma za kifedha vijijini unaolenga kuongeza ufikivu wa wazalishaji wa vijijini na wajasiriamali kwenye huduma za kifedha zitolewazo na mabenki ya biashara, kujaribu mbinu, njia na , huduma mpya katika maeneo ya vijijini kwa manufaa ya kundi lililolengwa, kuboresha mfumo wa kisheria na sera kwa ajili ya huduma ndogo za kifedha za vijijini, na kuhusisha usimamizi wa ujuzi katika programu<br>- Uboreshaji ufikivu wa huduma za kifedha katika misingi endelevu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati wa vijijini (kuongezeka kwa idadi ya wakulima na wajasiriamali wadogo na wa kati (*SMEs*) wanaopata mikopo kutoka taasisi za kifedha) |

| Maeneo ya Utekelezaji | Shughuli |
|---|---|
| Kuwezesha ufikivu wa wakulima kwenye uwekezaji katika kilimo | - Kuboresha Asasi na Vyama vya Wakulima vya utafutaji wa masoko ya pembejeo na mazao<br>- Kuimarisha vyama vya wakulima na masoko ya pembejeo kwa kuwezesha mifumo ya taarifa, ukusanyaji wa mazao na matumizi ya fursa za kupata huduma za kifedha kwa kutumia mali kama dhamana<br>- Kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani (*WRS*) ili kuachana na suala la dhamana<br>- Kueneza na kuimarisha kilimo cha mkataba kadri inavyofaa (mkataba wa makubaliano baina ya asasi za wazalishaji, wafanyabiashara katika kilimo, Wasafirishaji nje na taasisi za kifedha)<br>- Kubuni mipango ambayo itawawezesha wakulima wadogo kupata huduma za mikopo ya kifedha inayopatikana kupitia minyororo ya thamani katika kilimo (kwa kuanza na masomo waliyojifunza katika mipango inayoendelea)<br>- Kuanzisha mifumo ya kisheria na sera ya mikataba ya "kukodisha", huhusan kwa ajili ya kuhamasisha utoaji wa huduma binafsi za matumizi ya zana za kilimo (makubaliano ya kimkataba kati ya waagizaji wa zana, mabenki ya uwekezaji pamoja na watoa huduma binafsi wa zana za kilimo) |

**255** **Utekelezaji.** Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania chini ya Wizara ya Kilimo inalo jukumu la kuandaa mikakati na hatua za kipaumbele kwa kushirikiana na wadau wote wa sekta, ikiwa ni pamoja na Idara za Sera na Mipango za Wizara za Sekta ya Kilimo (ASLMs); Idara zenye dhamana ya uendelezaji wa mazao, mifugo na uvuvi katika Wizara husika; Idara ya Masoko (Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji), Wizara ya Fedha na Mipango; Asasi za wakulima (FOs); Taasisi za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (MFIs) na Mabenki ya Binafsi na Washirika wa maendeleo.

**256** **Muhtasari wa eneo kuu la 3 la Programu:** Gharama za awali za utekelezaji wa mpango kazi unaopendekezwa ni kama unavyoonekana **Jedwali Na. 39.**

**Jedwali Na. 39: Bajeti ya Maendeleo/Makadirio ya uwekezaji katika eneo kuu la 3 (TSh milioni)**

| ENEO KUU LA 3 LA PROGRAMU : BIASHARA NA UONGEZAJI THAMANI KWENYE MAZAO - Makadirio ya Gharama kwa kuzingatia bei za Mwaka 2016 (TSh milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kipengele cha Gharama** | **mwaka 1** | **Mwaka 2** | **Mwaka 3** | **Mwaka 4** | **Mwaka 5** | **Jumla** |
| **3.1.1.1** Kuboresha na kuendeleza miundombinu ya masoko kwa ajili ya kuyafikia masoko ya ndani na nje | 98,346 | 456,728 | 568,733 | 635,561 | 684,371 | 2,443,739 |
| **3.1.2.1** Kuboresha na kuendeleza miundombinu ya masoko ya mifugo na uvuvi kwa ajili ya kuongeza mapato ya ndani na kupanua wigo wa masoko | 7,847 | 9,466 | 156,458 | 171,750 | 368,188 | 713,709 |
| **3.1.2.2** Kuboresha ufikiwaji wa masoko ya kuku bora wa kienyeji | 743 | 2,068 | 2,248 | 369 | 282 | 5,710 |
| **3.1.2.3** Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji (utambulisho) wa mifugo na uvuvi ili kukuza biashara na masoko | 1,834 | 738 | 733 | 643 | 630 | 4,578 |
| **3.1.2.4** Kuhamasisha na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika mnyororo wa thamani wa mazao | 1,239 | 4,073 | 4,376 | 1,442 | 13,999 | 25,129 |
| **3.2.1.**Kuimarisha na kuendeleza viwanda vya usindikaji kwa ajili ya kuongeza thamani kwa mazao yote ya kipaumbele | 10,333 | 14,448 | 15,432 | 16,806 | 18,522 | 75,541 |
| **3.2.1.2** Kuboresha mnyororo wa thamani wa maziwa | 8,886 | 8,536 | 8,014 | 4,213 | 4,571 | 34,220 |
| **3.2.1.3** Kuimarisha mnyororo wa thamani wa ngozi (za wanyama wakubwa na wadogo) | 13,915 | 10,119 | 19,594 | 5,972 | 5,307 | 54,907 |
| **3.2.1.4** Kuimarisha mnyororo wa thamani wa mazao ya bustani | 4,995 | 1,622 | 4,127 | 1,274 | 1,387 | 13,405 |
| **3.2.1.5** Kuendeleza Maghala ya kimkakati yatakayounganishwa na Maghala yanayotumia Mfumo wa Soko la Bidhaa | 26,328 | 21,012 | 22,695 | 24,805 | 27,302 | 122,142 |

| ENEO KUU LA 3 LA PROGRAMU : BIASHARA NA UONGEZAJI THAMANI KWENYE MAZAO - Makadirio ya Gharama kwa kuzingatia bei za Mwaka 2016 (TSh milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kipengele cha Gharama** | **mwaka 1** | **Mwaka 2** | **Mwaka 3** | **Mwaka 4** | **Mwaka 5** | **Jumla** |
| **3.2.1.6** Kuendeleza na Kuimarisha Uongezaji wa thamani ya mazao ya kipaumbele yatokanayo na uvuvi na na ufugaji wa samaki | 5,758 | 6,752 | 7,267 | 7,868 | 8,432 | 36,077 |
| **3.2.1.7** Kuimarisha uongezaji wa thamani ya nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo | 9,633 | 12,739 | 3,507 | 505 | 226 | 26,610 |
| **3.2.1.8** Kuboresha usimamizi katika kuzuia upotevu wa mazao baada ya kuvuna katika mnyororo wa usambazaji chakula ili kuwa na uhakika wa chakula na lishe endelevu | 1,088 | 2,710 | 12,534 | 2,324 | 1,080 | 19,736 |
| **JUMLA YA ENEO KUU LA 3 LA PROGRAMU** | **190,945** | **551,009** | **825,718** | **873,532** | **1,134,297** | **3,575,501** |

## F. Eneo Kuu la 4: Kuimarisha Viwezeshi vya Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini

257 Malengo ya kimkakati, matokeo na viashiria husika vya viwezeshi na uratibu wa programu yameelezwa katika **Jedwali Na. 40**

**Jedwali Na. 40: Eneo kuu la 4 la ASDP II: Malengo Mahususi na Matokeo yanayohusiana na ASDS**

| Lengo | Matokeo | Viashiria vya Matokeo |
|---|---|---|
| **Eneo kuu la 4 la Programu: Kuimarisha Viwezeshi vya Sekta, Uratibu, na Ufuatiliaji na Tathmini** | ***Kuimarishwa kwa Taasisi, Viwezeshi, Uratibu na Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini*** | - Kuwepo kwa Mazingira ya sera na Mfumo wa Udhibiti<br>- Kuwepo na mazingira mazuri ya kufanya biashara (Mabadiliko katika nafasi ya nchi kwa kutumia vigezo vya Benki ya Dunia vya kufanya biashara na kuwezesha biashara katika kilimo)<br>- Usimamizi wa maarifa<br>- Ufanisi katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kusadia sekta ya kilimo<br>- Mifumo jumuishi na yenye ufanisi ya ufuatiliaji na tathmini katika sekta<br>- Uwezeshaji wa Asasi za Wakulima, Wanawake na Vijana<br>- Ufikiwaji wa Huduma za Kifedha kwa ajili ya kilimo |
| | Eneo dogo 4.1 Kuboreka kwa mazingira ya Ufanyaji biashara kupitia Uimarishaji wa Kanuni, Sera na Mifumo ya Kitaasisi | - Sera, Sheria, Kanuni na Mifumo ya Kitaasisi inayohusiana na Sekta ya Kilimo iliyofanyiwa mapitio na kuoanishwa<br>- Kiwango cha Uzingatiaji wa Sera na Kanuni (k.m kasi ya uzingatiaji)<br>- Uwepo wa Mazingira ya Kisera na Mifumo ya uthibiti<br>- Mazingira ya ufanyaji biashara |
| | Eneo doko 4.2 Wakulima, na Asasi na vyama vya Ushirika vya Wakulima vilivyowezeshwa | - Asilimia ya Asasi za wakulima (FOs) na Vyama vya Ushirika vinavyotoa Huduma za Uendelezaji (BDS)<br>- Asilimia ya Asasi za wakulima na Vyama vya Ushirika vilivyotafuta vyenyewe rasilimali zake<br>- Asasi za Wakulima na Wadau wengine katika mnyororo wa thamani zinazoendeshwa na kusimamiwa na Wanachama wenyewe (Utawala Bora) |

| | | |
|---|---|---|
| | Eneo dogo 4.3: Kuimarisha Uratibu wa Sekta | - Uwasilishaji wa taarifa ya robo mwaka zenye ubora unaotakiwa na kwa wakati katika ngazi zote<br>- Kitengo cha Uratibu kwa ajili ya Mipango na ufuatiliaji kuanzishwa na kinafanya kazi<br>- Kiwango cha uzingatiaji miongozo katika ngazi zote |
| | Eneo dogo 4.4: Kuimarishwa kwa Ufuatiliaji na Tathmini na Takwimu za kilimo | - Kutekelezwa kwa Zoezi la Ukusanyaji wa Sampuli ya Takwimu za Kila mwaka za Kilimo *(AASS)*<br>- Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwasilisha takwimu zenye ubora kwa wakati kwa kutumia mifumo mbalimbali ya Ufuatiliaji na Tathmini<br>- Mifumo jumuishi ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Pamoja kuanzishwa na kutumika |
| | Eneo dogo 4.5: Kujenga uwezo wa Kitaasisi, usimamizi wa maarifa, na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano | - Kuimarika kwa usimamizi wa maarifa na mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(TEHAMA)* |
| | Eneo dogo 4.6: Kupanuka kwa ufikiwaji wa huduma za Kifedha kwa ajili ya kilimo | - Utoaji wa riba nafuu katika Benki ya Biashara Tanzania kwa mkulima<br>- Asilimia ya kiwango cha urejeshaji wa mikopo<br>- Asilimia ya ongezeko la matawi ya Taasisi rasmi za huduma za kifedha katika maeneo ya vijijini. |

**Maeneo ya Utekelezaji ya sera /Kitaasisi :** Kusisitiza Sera za kipaumbele kama zilivyoainishwa katika Muungano Mpya wa Uhakika wa Chakula na Lishe zinazohusu: (i) Biashara/masoko; (ii) Sera wezeshi kwa ajili ya ushiriki wa sekta binafsi; (iii) Umiliki wa ardhi; (iv) Ufikiwaji wa huduma za kifedha; na (v) Sera za mbegu.

**Usimamizi wa TEHAMA:** kuoanishwa kwa viwango, taratibu za ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu za kilimo zilizotambuliwa na kuendelezwa katika sekta kupitia matumizi ya nyezo za **TEHAMA, itaimarishwa** ili kuongeza ufanisi katika kutoa maamuzi lakini pia kuwa chanzo na kichocheo cha ukuaji wa sekta katika siku zijazo kupitia ubunifu .

**ENEO KUU LA 4 LA PROGRAMU: KUIMARISHA VIWEZESHI VYA SEKTA , URATIBU , UFUATILIAJI NA TATHMINI** (Ngazi ya Taifa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa)

Eneo dogo 4.1: Muundo wa Sera na Usimamizi
Eneo dogo 4.2: Uwezeshaji na Mpangilio wa Wadau
Eneo dogo 4.3: Uratibu wa Sekta (upangaji na utekelezaji katika ngazi ya Taifa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa
Eneo dogo 4.4: Ufuatiliaji na Tathmini (ikiwa ni pamoja na takwimu za Kilimo)
Eneo dogo 4.5: Kuimarisha uwezo wa Kitaasisi, usimamizi wa maarifa, na TEHAMA katika sekta ya kilimo
Eneo dogo 4.6: Ufikiwaji wa huduma za kifedha vijijini

258 **Eneo kuu la 4 la Programu limegawanyika katika maeneo madogo sita :** Mafanikio ya ASDP II kwa kiasi fulani yanategemea uwezo na Uthabiti wa Taasisi na Washiriki mbalimbali waliopo katika sekta katika kutekeleza shughuli zilizopangwa. Taasisi nyingine kama vile za watunga Sera, wanataaluma wa elimu ya juu, huduma za utafiti, ugani, mafunzo na teknolojia ya habari zinazosaidia sekta ya kilimo zitahitaji kuwa na uwezo wa kupanga upya shughuli zao ili kutekeleza ASDP II. Sababu za kitaasisi ambazo zinazuia maendeleo ya sekta ya kilimo ni kama zilivyoainishwa katika sanduku Na. 6.

**Sanduku Na. 6: Masuala Muhimu Katika Mageuzi ya sera na Kitaasisi na msaada (toka Mpango wa Uwekezaji Katika Kilimo na Uhakika wa Chakula Tanzania)**

- Ufinyu wa bajeti ya Serikali ya maendeleo kwa ajili ya utafiti, huduma za ugani, mahusiano kati ya utafiti na ugani, mipango na majukumu ya udhibiti
- Udhaifu katika uratibu na utekelezaji wa sera na kusababisha kufanyika mara mbili kwa juhudi zinazofanana, kuweka pengo katika kupanga, kutekeleza na kufanya tathmini ya programu
- Udhaifu wa ushirikiano wa kutumia nguvu ya pamoja kati ya Taasisi za kitaaluma na Serikali
- Utengano kati ya Wakulima na Vyombo vya usimamizi wa Vyama vya Ushirika ikilinganishwa na inavyopaswa kuwa
- Uwezo usiotosheleza wa kifedha, rasilimali Watu na wa kiufundi katika kuzalisha, kusimamia na kusambaza taarifa muhimu za kilimo, mifumo dhaifu ya mawasiliano katika ngazi zote na gharama kubwa za kununua pembejeo bora
- Usimamizi dhaifu wa fedha na mali, utunzaji wa kumbukumbu, utoaji taarifa na ufuatiliaji na tathmini
- Uhaba wa Vyuo vya mafunzo ikiwa ni pamoja na Vituo vya Mafunzo ya Wakulima na uhaba wa fedha za kugharamia huduma za mafunzo ya kilimo
- Kasoro zilizoko katika mfumo wa kisheria na udhibiti ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa sheria na kanuni zake
- Kutotosheleza kwa msingi wa takwimu bora na uwezo wa kufanya uchambuzi kwa ajili ya uchambuzi wa sera na utoaji wa maamuzi

## Eneo Dogo 4.1: Muundo wa Sera na Usimamizi

259 Uandaaji wa sera madhubuti na mageuzi ya kitaasisi yaliyo muhimu kwa utekelezaji wa sera ni misingi ya kufikia malengo ya kimkakati ya ASDS. Pia ni mojawapo ya majukumu muhimu ya Serikali. Wakati mfumo wa sera wa Tanzania kwa ajili ya maendeleo vijijini na kilimo ni mpana na thabiti, kufanya mapitio, marekebisho na mchujo katika baadhi ya maeneo kunaweza kuwa na manufaa.

260 Lengo ni kuoanisha, kupanga na kuwianisha sera na mifumo ya udhibiti ambayo inasimamia sekta ya kilimo (kwa Wizara za Sekta ya Kilimo) na sekta husika (mazao, mifugo/uvuvi na maliasili) na kuimarisha uwezo wa kitaasisi kwa ajili ya maendeleo thabiti na usimamizi wa sekta.

**Jedwali Na. 41: Maeneo muhimu ya sera na shughuli zinazohusiana na ukuaji wa sekta ya kilimo (Wizara za Sekta ya Kilimo)**

| Matokeo ya Sera | Shughuli za Kipaumbele (ngazi ya Taifa) |
|---|---|
| **Sera ya Pembejeo za Kilimo** | |
| Kuwezesha sekta binafsi kuendeleza, kufanya kibiashara, na kutumia pembejeo bora ili kuongeza tija na kipato kwa mkulima mdogo | - Uchambuzi na utetezi katika kuhamasisha maeneo ya sera yanayohimiza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora<br>- Kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kutumia viwango vilivyoainishwa na kufanya biashara huru ya mbegu |
| **Sera ya biashara ya Kilimo** | |
| Kupunguza vikwazo vya kibiashara vya ushuru na visivyo vya ushuru ili kuongeza biashara na kuhimiza ukuaji wa uchumi jumuishi (usimamiaji wa uingizaji/uuzaji nje ) | - Kufanya uchambuzi wa uwezo na mahitaji ya mfumo wa uhakika wa chakula, uwezekano wa kufanya biashara ya kikanda ya mazao ya chakula, na athari za kuzuia uuzaji mazao nje ya nchi katika ili kupunguza umaskini na ukuaji wa sekta<br>- Juhudi za utetezi kupitia Bunge na Vyama vya asasi za kiraia ili kujenga uungwaji mkono katika kutafuta njia mbadala<br>- Kukuza masoko ya kilimo ya ushindani na haki<br>- Kufungamanisha sera za biashara za Tanzania na Sera za Kikanda (Jumuia ya Afrika Mashariki/Jumuiya ya Nchi zinazoendelea Kusini mwa Afrika) |
| **Sera Wezeshi kwa ajili ya uwekezaji wa Sekta Binafsi** | |
| **Sera ya Pembejeo za Kilimo** | |

| Matokeo ya Sera | Shughuli za Kipaumbele (ngazi ya Taifa) |
|---|---|
| **Sera ya Pembejeo za Kilimo** | |
| Kupunguza vikwazo vya ushindani, hivyo kuongeza uwekezaji binafsi katika kilimo na kuchochea kasi ya ukuaji wa sekta ya Kilimo | - Kufanya uchambuzi na utetezi ili kutoa njia mbadala ya kukabiliana na vikwazo mahususi vya udhibiti<br>- Kupunguza idadi ya tozo za vyombo vya udhibiti na michakato<br>- Kutekeleza mfumo wa kodi uliorahisishwa zaidi kwenye mazao ya chakula, ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kuondoa kodi<br>- Kukuza uwazi zaidi na mazingira mazuri ya sera yanayofaa kwa kuanzisha soko la bidhaa lenye mafanikio<br>- Kuwepo kwa motisha za sera ili kuhamasisha uongezaji wa thamani kwa lengo la kupunguza uagizaji wa chakula nje ya nchi na kukuza utengenezaji wa ajira<br>- Kufanya uchambuzi wa vivutio vya uwekezaji katika kilimo ili kuhamasisha uwekezaji wa ndani na kutoka nje ya nchi |
| **Sera ya umiliki wa ardhi** | |
| Kuhamamsisha sera ya umiliki ardhi ambayo inaimarisha haki za matumizi ya ardhi, yenye kiwango cha chini kabisa cha uvurugaji wa mfumo wa wafugaji wa kuhamahama na maskini wasiomiliki ardhi, kuchochea uwekezaji wa wakulima wadogo katika shughuli zinazotegemea ardhi na mali zingine ambazo hazihusiani na kilimo zinazoingiza kipato | - Kuandaa/kutekeleza sera na taratibu zilizo wazi kwa ajili ya wawekezaji kupata ardhi kwa haraka kuliko awali na bila kuwepo migogoro<br>- Kuboresh Sheria na Urasimishaji wa haki za ardhi kupitia umilikishaji ardhi<br>- Kupandisha hadhi ya Hati Miliki za Ardhi za Kimila *(CCROs)*<br>- Kupanga upya na kuiongezea majukumu Mamlaka ya Kuendeleza Bonde la Rufiji kwa kuifanya kuwa Benki ya Ardhi kwa ajili ya Ukanda lilipo Bonde hilo ( (katika Mikoa ya Ukanda wa Maendeleo ya Kilimo Kusini mwa Tanzania -SAGCOT tu)<br>- Kupunguza migogoro katika matumizi ya rasilimali ardhi kupitia utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi |
| **Ufikiwaji wa Mitaji na Huduma za Kifedha** | |
| Kuendeleza sera ambayo itawezesha uendelezaji wa huduma za kifedha zitakazochochea uwekezaji wa sekta binafsi, ulimbikizaji wa mali, na ufikiwaji wa pembejeo katika maeneo muhimu ya minyororo ya thamani ya mazao. | - Kuanzisha/kutekeleza mfumo wa kisasa wa usajili wa dhamana pamoja na mfumo husika wa kisheria ili kumlinda mkopeshaji endapo aliyekopa atashindwa kulipa<br>- Kutekeleza utoaji wa mafunzo na ufikiaji ili kuwezesha uenezaji mpana wa matumizi ya mfumo salama wa miamala ya taasisi za huduma za kifedha<br>- Kubuni mipango ya kuwawezesha wakulima wadogo wadogokupata huduma ya mikopo ya Fedha kwa kufuata minyororo ya thamani katika kilimo |
| **Sera ya Sekta ya Kilimo (ikiwa ni pamoja mazao, mifugo/uvuvi na masoko)** | |
| Kusaidia uandaaji wa Sera ya wazi, shirikishi, na yenye uthibitisho ambayo itawezesha kuongezeka uwekezaji wa sekta ya umma na binafsi wenye uthabiti zaidi kwenye kilimo | - Kuimarisha na kudumisha ushirikiano wa Kikanda (shughuli za Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Kilimo Katika Afrika *(CAADP)*<br>- Kuwekeza kwenye kujenga uwezo katika masuala ya takwimu za kilimo<br>- Kuimarisha utulivu, utabilikaji na uwazi wa sera kwa kuweka taratibu na michakato yake katika maboresho ya Sera<br>- Kuoanisha sera zenye kufungamana<br>- Kueneza na kuendeleza Sera zenye kuhamasisha maendeleo jumuishi hususan miongoni mwa Vijana, Wanawake na Masikini sana |
| **Uhakika wa chakula** | - Mapendekezo ya sera: ndani ya uratibu unaovuka mipaka ya Ki-sekta kwa kutumia mfumo wa Mpango wa Uwekezaji Katika Kilimo na Uhakika wa Chakula Katika Tanzania *(TAFSIP)*<br>- Kuimarisha mipango iliyopo ili kuongeza tija katika kilimo kwa kuzingatia upande wa usambazaji katika mnyororo/minyororo ya thamani ya kilimo |

| Matokeo ya Sera | Shughuli za Kipaumbele (ngazi ya Taifa) |
|---|---|
| **Sera ya Pembejeo za Kilimo** | |
| **Uhakika wa chakula** | - Kuzingatia sera mahsusi zinazohusu uhakika wa chakula na shughuli za kaya kwa ajili ya kuboresha maisha na kutengeneza mapato (kuboresha ufikiwaji)<br>- Kuimarisha utayari wa kukabiliana na maafa (ikiwemo kufanya tafiti maalumu) na hatua za kuchukua zinazozingatia kujimudu na ustahimilivu wa Kaya<br>- Kueneza mipango ya usalama wa chakula ( kutoa chakula mashuleni, kupata fedha kwa kufanya kazi za maendeleo ya Kijamii ili kujinunulia chakula) |
| **Lishe** | - Kuwepo kwa Sheria (mfumo wa udhibiti) kuhusu mbadala wa maziwa ya mama, likizo ya uzazi, kuongeza madini joto kwenye chunvi na urutubishaji wa chakula,<br>- Usambazaji na utetezi wa Sera unahitajika ili kufaninisha utekelezaji na kupanua wigo kwa hadhira |

Chanzo: Imekusanywa kutoka "Mjadala wa sera wa G8." Dar es Salaam (February 2015) na ASDP 2 (Rasimu)

### Eneo dogo 4.2: Uwezeshaji wa Mpangilio wa Wadau.

261 **Maelezo mafupi ya uandaaji na utoaji huduma katika kilimo.** Kwa kawaida, Vyama vya Ushirika ndivyo vilivyokuwa ni njia pekee ya kuwaandaa wakulima pamoja ili kupata huduma mbalimbali. Hata hivyo, Vyama vya Ushirika vilijitokeza zaidi kwa ajili ya mazao ya biashara kama vile kahawa, pamba na tumbaku. Kutokana na sababu mbalimbali za kiuchumi na kisiasa, Vyama vingi vya Ushirika vilivunjika. Ili kufufua Vyama vya Ushirika vilivyosajiliwa na Vikundi vya Ushirika, Serikali iliandaa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika (CRMP) na kutunga Sheria ya Ushirika Na. 6 ya 2013 ili kusimamia Wadau wa Vyama vya Ushirika katika shughuli zao za kiuchumi za kutoa huduma za ununuzi na uuzaji wa mazao kama vile mazao ya chakula na ya biashara ya asilia na yasiyo asilia.

262 **Kwa sasa, aina mbalimbali za Asasi zimeanza kujitokeza.** Baadhi ya vikundi hivyo, ni tabaka la Asasi za Wakulima (FO) na wakati vingine ni vya kitaaluma zaidi ambavyo vinajumuisha vyama kama vile Chama cha Wakulima wa Mbogamboga, Matunda, Viungo na Maua Tanzania (TAHA) na Baraza la Kilimo Tanzania (ACT). Hizi ni asasi zisizo za Serikali ambazo hutoa huduma kwa wanachama wake, lakini nyingi bado zinategemea misaada ya kiufundi na kifedha kutoka nje. Asasi kama hizo zinahitaji kusaidiwa ili kukusanya rasilimali za ndani na kuendeleza stadi zao za biashara, ili kuwafanya wawe sekta binafsi iliyo thabiti. Asasi zinazojielekeza zaidi katika bishara, kuwezeshwa ili kusaidia wakulima wadogo kuhama kutoka kwenye mazoea ya kilimo cha kujikimu kwenda kwenye kilimo cha kibiashara. Aidha, asasi hizi hutoa fursa ya kuwaunganisha wakulima na wasambazaji wa pembejeo, wafanyabiashara, watoa huduma za kifedha na wengineo na kwa ajili ya kutengeneza minyororo ya thamani iliyo imara ya mazao mahsusi. Asasi za wakulima zimepambanuliwa katika makundi mbalimbali **(Jedwali Na. 42).**

### Jedwali Na. 42: Vyama vya wakulima kwa vikundi

| Aina ya Asasi za Wakulima (FOa | Mfano | Uwezo na udhaifu |
|---|---|---|
| **Vyama/ Asasi/ Vikundi vya Wazalishaji wa Mazao** | Taasisi na vikundi vya wakulima(COWABAMA) Vyama vya wakulima wa mpunga (idadi ya vyama vya wakulima wa mpunga haijulikani) | Vyama vingi vya wazalishaji havijaunganishwa ipasavyo na wasambazaji wa pembejeo, watoa huduma za kifedha na kibiashara. Aidha, wengi wao wana uwezo usiotosheleza wa usimamizi ambao unakuwa kizuizi cha kupata manufaa.<br>Hata hivyo, vyama hivi vinaweza kuimarishwa ili viweze kujadiliana kuhusu sera na bei bora zaidi, uwezekano wa kuunganishwa vizuri na wanunuzi na watoa huduma wengine katika mnyororo wa thamani. |

| Aina ya Asasi za Wakulima (FOa | Mfano | Uwezo na udhaifu |
|---|---|---|
| **Vyama Kilele** | RUDI anafanya kazi katika wilaya za Mbarali (wanachama 7,000) na Kilombero (wanachama 3,600);<br>Vyama vya wakulima wa miwa Kilombero, Mtibwa na Kagera.<br>Jumuia ya wazalishaji wa maziwa wa Tanzania (TAMPRODA) | Nchini Tanzania hakuna chama cha wazalishaji wa mahindi tofauti na vile ambavyo ni kwa ajili ya bidhaa nyingine, ingawa wakulima wengi katika maeneo ya uzalishaji wa mahindi wako katika vikundi vya wakulima na mitandao ya vyama vya wakulima. Baadhi yao ni wanachama wa MVIWATA, ambacho hakijihusishi na bidhaa maalum. Wazalishaji wa mahindii wanapaswa kujiunga katika vyama ili kuwezesha kuwepo na uhusiano na watendaji wengine katika mnyororo wa thamani (wanunuzi wa mahindi) ili kukusanya mahindi kwa pamoja na kuhifadhi ghalani.<br>Wafugaji/vyama vya ushirika vya wavuvi. |
| **Vyama vya ushirika** (vilivyojumuishwa na vyama vikuu vya ushirika) | Lindi na Mtwara: ufuta huuzwa kupitia chama kikuu cha Ushirika cha Ilulu kilichopo Lindi na chama kikuu cha Ushirika cha Masasi -Mtwara (MMCU) | Vyama hivi bado vina umuhimu katika baadhi ya maeneo, kwa ajili ya mazao asilia ya biashara na kwa mazao mapya. Kwa upande wa ufuta, itakuwa ni vizuri kufanya kazi kupitia vyama vya ushirika vya msingi na vyama vikuu vya ushirika kwa kuimarisha uendeshaji wa biashara zao na masoko. |
| **Vyama vya watumiaji maji na umoja wa wamwagiliaji** | Vyama vya watumiaji wa maji katika wilaya ya Mbarali (kutoka wanachama wachache hadi wanachama 3000 (Madibira) | Vyama hivyo hutofautiana kwa ukubwa na uwezo. Hata hivyo, ni fursa nzuri kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha bustani baada ya mpunga kuvunwa. |
| **Vyama vya wakulima wa kudumu** | MVIWATA (Mtandao wa vikundi vya wakulima Tanzania)<br>HODECT: Baraza la Kuendeleza Kilimo cha Bustani Tanzania[66] | Ni mtandao wa vikundi vya wakulima zaidi ya 5,000 katika mikoa 25. Kwa sasa vinawakilisha kaya 70,000 za kilimo, ingawa idadi halisi haifahamiki. Kwa kawaida vikundi vya wakulima huwa na kaya kati ya 5 na 15 na mitandao ambao huwakilisha makundi 4 – 20 ndani ya kijiji kwa kawaida . |
| **Vyama vikubwa vya wakulima wa kiwango kikubwa (kulingana na bidhaa )** | Chama cha Wakulima wa Tanganyika (TFA), Chama cha Wafanybiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) ama ACT | Idadi ndogo ya wakulima wakubwa inamaanisha kwamba wao hukutana kwa utaratibu usiyo rasmi. Mashamba makubwa na ranchi yana nafasi kubwa katika kuendeleza kilimo cha kisasa, kuongeza uzalishaji kibiashara na kuwa kitovu katika kuendeleza mpango wa wakulima wa nje na kilimo cha mkataba. Wakulima hao watakuwa na matokeo makubwa na kupata faida kama watakuwa na utaratibu rasmi wa kukutana. |

[a] Imekusanywa kutoka vyanzo mbalimbali.

263 ASDP-1 ilichangia katika utekelezaji wa sera na kuboresha ushiriki wa wakulima vijijini ( pamoja na vyama vyao) katika kuandaa na kutekeleza mipango ya mendeleo ya kilimo ya kijiji. Kuna ushahidi wa matokeo chanya ulioonekana katika kuboresha ushiriki wa wakulima (Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo), kujenga uwezo na maarifa ili kuongeza tija na faida. ASDP-1 pia ilihamasisha uanzishwaji wa Jukwaa la Wakulima (FF) katika ngazi ya kata na wilaya, hata hivyo kulikuwa na ufahamu mdogo kuhusu wajibu wao. Kwa ujumla, kuna ukosefu wa mfumo wa kimkakati kwa ajili ya mipango ya uwezeshaji wa wadau na vyama vyao katika minyororo ya thamani katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa. Watoa huduma binafsi wenye ujuzi na uzoefu wanatakiwa katika masuala ya kuanzisha na kuendesha vyama vya wakulima kwa kuvijengea uwezo wa kiufundi wa usimamizi na uongozi kuanzia ngazi ya chini.

66 *http://hodect.org/*

264 Uanzishaji wa vikundi na kutumia mbinu za pamoja ni hatua za lazima kwa ajili ya kuongeza ukuaji wa sekta ya kilimo na kilimo-biashara. Kutambulika kwa uwezo wa vyama vya wakulima, kama sekta binafsi kunahitajika kwa Serikali kufanya maboresho muhimu yafuatayo: (i) Kujenga uwezo wa vyama vya wakulima na kiufundi kupitia ubia wa sekta ya umma na binafsi; (ii) Kuimarisha ujasiriamali na ushindani wa vyama vya wakulima kwa kuvijengea uwezo wa usimamizi na uongozi; (iii) Kuhamasisha ushiriki mpana miongoni mwa wanawake na wakulima wadogo katika vyama vya wakulima; na (iv) Kutoa mfumo wa wazi kwa ajili ya uanzishaji na uendeshaji wa vyama vya wakulima.

265 Lengo la eneo hili dogo ni kusaidia shughuli kwa ajili ya kuwawezesha wakulima na kuimarisha vyama vya wadau katika mnyororo wa thamani, ili viweze kupata huduma, elimu, taarifa, fursa za uwekezaji na masoko kwa ufanisi na udhibiti zaidi. Eneo hilo dogo litaongeza uwezo wa wakulima na kusaidia vyama vyao kujihusisha katika mageuzi ya kilimo biashara. Vikundi vya wakulima/umoja/ushirika vitaimarishwa kuelekea kuwa shirikisho katika mnyororo wa thamani, kwa ajili ya kuongeza faida na manufaa kutoka ndani na nje ili kuongeza faida zao kibiashara. Vikundi vya wakulima vitatumika kama kitovu cha kujifunza, kudhibiti ubora na viwango, lakini pia kuongeza nguvu ya kufanya majadiliano na umiliki.

266 Mafanikio ya wakulima wadogo, mkakati wa kuendeleza masoko huria kwa kiasi kikubwa unategemea na uanzishwaji wa vyama vya ushirika vyenye misingi imara , vyenye uwezo wa kutenda na kufanya maamuzi yanayoboresha maisha ya wanachama wake. Mambo muhimu ya kuwavutia wakulima kujihusisha ndani ya minyororo ya thamani ya ushindani katika kilimo kufikia fursa za nje yanahitaji angalau: (i) Kuwepo kwa mpango wa biashara, sambamba na hali ya ekolojia, wakulima kuwezeshwa kuwa na rasilimali na fursa za soko; (ii) Vyama vya wakulima vyenye utawala bora na uwajibikaji; na (iii) Upatikanaji wa teknolojia mwafaka, habari, uzalishaji na usindikaji, pembejeo na mikopo.

267 Ili kufikia lengo hili kimkakati, ASDP II itawawezesha wakulima na kusaidia kubadilisha muundo wa vyama kwa kutumia uzoefu wa jamii katika kuendeleza shughuli za biashara kwa wakulima wadogo, kuimarisha miundo ya utawala bora ya vyama (yaani, vyama vya kiuchumi, ushirika, makampuni, nk.) na kuweka akiba na mikopo (mfano, SACCOs). Utaratibu wa vyama na mnyororo wa thamani wa bidhaa utatumika kama kitovu katika mkakati wa ugani (eneo dogo 2.2) katika kukabiliana na mahitaji ya wakulima kwa ajili ya teknolojia za uimarishaji, kufikia masoko na taarifa za masoko zinazopatikana kutokana na kuimarishwa kwa huduma za msaada na mifumo ya TEHAMA (eneo dogo 4.2), lakini pia upatikanaji wa pembejeo zenye ubora wa mikakati ya masoko. Muhtsari wa maeneo ya utekelezaji, ni kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na. 43.

**Jedwali Na. 43: Maeneo ya utekelezaji kwa ajili ya kuwawezesha wakulima na kuimarisha vyama vyao**

| Maeneo ya uwekezaji | Shughuli za kipaumbele |
|---|---|
| **Tathmini ya uwezo wa vyama vya wakulima** | |
| | - Tathmini ya awali ya uwezo wa vyama vya wakulima (FO) nchini Tanzania. (ikiwa ni pamoja na mafanikio)<br>- Kuandaa mfumo wa kimkakati kwa ajili ya mipango ya uwezeshaji wa wadau na vyama vyao katika minyororo ya thamani |
| **Uwezeshwaji wa wakulima** | |
| | - Mafunzo ya uongozi wa (menejimenti) kikundi (k.m. msaada kwa ajili ya usajili, utungaji wa sheria ndogo, mafunzo ya uongozi, uandaji wa taarifa ya mwaka, kuitisha mikutano ya vyama)<br>- Mafunzo ya usimamizi wa fedha (k.m. kuweka kumbukumbu za fedha, ukaguzi)<br>- Mafunzo ya mpango biashara (yakiwamo kufikia huduma za mkopo; ona pia eneo dogo 3.4)<br>- Kusaidia katika upatikanaji wa Hati za hati Miliki za Ardhi za Kimila (CCROs) au Hati Miliki ya Ardhi ambayo inaweza kutumika kama dhamana<br>- mashamba darasa kwa mazao maalum<br>- Mafunzo ya FO kuhusu uhifadhi, mauzo na manunuzi kwa pamoja |

| Maeneo ya uwekezaji | Shughuli za kipaumbele |
|---|---|
| **Kuimarisha vyama vya wakulima** | |
| **Muundo wa uongozi wa shirikisho la vikundi vya wakulima na vyama vikuu**<br><br>Kuimarisha vyama katika uwezo wa kiufundi kwa vyama vilivyopo na vipya vya wazalishaji wadogo, wafanyabiashara na ushirika wa wasindikaji | - Kuimarisha/ kusaidia vyama vikuu vya wakulima (vyama vikuu, shirikisho na vyama vya ushirika) na utawala wao<br>- Kuwezesha vyama vinavyoibuka na kuimarisha kiuchumi vyama vya wadau na/au vyama vya ushirika<br>- Kuimarisha mazungumzo na wadau (Wizara, sekta binafsi, wabia wa maendeleo, n.k.)<br>- Kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi ghalani katika maeneo mengine nchini<br>- Kuziwezesha vyama vya ushirika ujuzi wa kiufundi na usimamizi wa usindikaji na masoko<br>- Kuandaa mifumo bora ya uendeshaji kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji<br>- Kuhamasisha uhusiano kati ya SACCOS na Ushirika wa Mazao (AMCOS) |
| Kuimarisha asasi za wadau (TAHA, nk.) | - Majukwaa ya ubunifu ya kikanda ya wadau mbalimbali kwa ajili ya mnyororo wa thamani zilizopewa kipaumbele<br>- Wadau katika myororo wa thamani wa mchele<br>- Wadau wa vyama katika ngazi ya wilaya<br>- Majukwaa kwa ajili ya bidhaa maalum<br>- Kuimarisha mazungumzo na wadau (Wizara) |

**268 Tathmini ya awali ya uwezo wa vyama vya wakulima nchini Tanzania.** Kuhakikisha kiwango cha juu na matokeo ya kudumu ya msaada wa maendeleo ya vyama vya ushirika wa wakulima, tathmini ya kina ya uwezo wa uendeshaji na mahitaji ya kibiashara ya vyama vya wakulima itatekelezwa katika kipindi cha mwaka wa kwanza. Tathmini hii italenga: (i) Rasilimali za ndani na uwezo wa mashirika-kuajiri, usimamizi, ubora wa huduma, uendeshaji wa shamba, (ii) Kuongeza zana za kisasa kwa ajili ya mafunzo na shughuli za shambani; (iii) Ubora wa zana zinazotumika katika tathmini ya mnyororo wa thaman, uchambuzi wa ushindani na msaada wa awali wa maendeleo ya biashara; (iv) Uwezo na mahitaji, ya kuunganishwa na taasisi za fedha, na (v) Mahitaji ya mashirika katika masuala ya msaada wa makao makuu. Kulingana na matokeo, mfumo wa msaada wa kuwezesha wakulima na kuimarisha mashirika utakamilika. Aidha, ramani ya wadau/ wafanyabiashara wa mnyororo wa thamani wa bidhaa juu ya mahitaji ya mafunzo husika ya maendeleo ya itandaliwa.

**269 Uwezeshaji wa wakulima.** Kuimarisha uwezo wa makundi ya wazalishaji na vikundi vya wakulima ni suala muhimu kwa mafanikio ya muda mrefu ya ushiriki wa wakulima wadogo katika minyororo wa thamani wa mazao. Sifa kubwa za eneo hili dogo ni kulenga kujenga uwezo wa wakulima (watendaji wa mnyororo wa thamani) na Mashirika yao (vikundi, vyama vya wafanyakazi, Shirikisho) ili kufanya maamuzi sahihi ya kuboresha biashara na maisha ya wanachama, lakini pia kuongeza uwezo wao wa kukubaliana na watendaji wengine katika minyororo ya thamani. Vikundi vya wakulima vitatumika kama kitovu katika mkakati mpya wa ugani katika kukabiliana na mahitaji ya wakulima ya teknolojia mpya, soko na taarifa nyingine zilizotolewa kwa kutumia mifumo wa TEHAMA, lakini pia mbegu bora na pembejeo, kilimo-biashara na kuongeza thamani na mkakati wa masoko.

270 Mambo matatu yanayo hitajika: (i) Mfumo wa biashara unaotekelezeka unakwenda sambamba na hali ya kilimo kiikolojia, mchanganuo wa rasilimali kwa wakulima na fursa ya masoko; (ii) Ufanisi katika utawala bora na uwajibikaji wa kundi (shirika); na (iii) Upatikanaji wa teknolojia muhimu, taarifa/ habari, uzalishaji na kuandaa pembejeo, na mikopo. Ili kufanikisha hili, ni kuongeza uzalishaji / tija kwa umma kwa kukamilisha mfumo wa ugani katika ngazi ya wilaya, ASDP II itatoa msaada kwa kuweka mikakati ya kuimarisha ushirika na[67] mashirika ya bidhaa, kutumia uzoefu wa ndani katika maendeleo ya wafanyabiashara wadogo, kuanzisha miundo ya utawala bora (kwa mfano, vyama vya ushirika, makampuni) na akiba na uwezeshaji wa mikopo (SACCOS), kama inavyohitajika.

**271 Uimarishaji uwezo wa makundi ya masoko ya wazalishaji na mashirika ya wakulima ngazi ya juu ni muhimu kwa mafanikio ya muda mrefu na umiliki wa wadau katika ukuaji endelevu wa sekta ya kilimo.** Ni muhimu kwa mafanikio ya muda mrefu na umiliki wa wadau ya ukuaji endelevu katika

67 *Angalia pia uzoefu mwingine wa MUVI - IFAD na NGO katika shughuli za uongezaji thamani na uanzishwaji wa vikundi*

sekta ya kilimo. Msaada utatolewa kwa kuongezea mafunzo na vifaa vya ndani, na zana zilizotumika katika kutathmini mnyororo wa thamani wa soko, ushindani wa masoko na msaada wa awali wa maendeleo ya biashara. Vipengele vidogo ni: (i) Kuimarisha vyama vya wakulima ili kushughulikia uhusiano wa mahitaji yanayotokana na washirika wa Kilimo-biashara kwa ajili ya huduma muhimu kama vile usambazaji wa pembejeo, soko la mazao na miundo mbinu ya usindikaji, (ii) Kuimarisha wajibu na uwezo wa mzalishaji wa sasa / ushirikiano wa mashirika ya masoko; na (iii) Kuendeleza mbinu mpya za - TEHAMA ili kurahisisha upatikanaji wa kiufundi, taarifa za masoko na huduma za ushauri wa kifedha. Msaada huu utakuwa wa kijinsia na vijana kwa umoja, utatoa kipaumbele maalum kwa makundi yenye matatizo ya uzalishaji na kupata fursa katika kilimo-biashara.

272 **Kukuza kwa kiwango kikubwa mashirika ya wakulima** (vyama vya wafanyakazi, mashirika ya kilele, vyama vya ushirika, nk). Maendeleo ya taasisi ya wakulima ni muhimu ili kuhakikisha kuwa vyama vya wakulima vinatekeleza majukumu yaliyotajwa katika kubadilisha kutoka kilimo cha kujikimu kwenda kilimo cha kibiashara, lakini pia kuimarisha umiliki na utawala katika shirika. Vikundi vya wakulima / vyama vya ushirika kushiriki katika uzalishaji wa bidhaa (mazao, mifugo na samaki) zinazolengwa katika ngazi ya kijiji itaungwa mkono katika uzalishaji wa ngazi ya juu na masoko ya chama, na kutenda kama chombo cha kiuchumi (vyama vya ushirika au kampuni). Mbali na ushauri wa kiufundi, kuimarishwa uwezo wa kujadiliana/mazungumzo na wadau wengine wa mnyororo wa thamani itahitaji mafunzo na uhamasishaji katika maeneo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na umakini katika ubora wa pembejeo za kilimo, uhifadhi baada ya mavuno, usindikaji, kusafirisha, matumizi ya taarifa za masoko, bei na ujuzi wa masoko. Hii itahusisha kuimarisha uwezo wa vikundi vya wakulima katika ujuzi na maendeleo ya biashara, pamoja na kuwezesha kuundwa kwa vyama vinavyo milikiwa na wakulima katika ngazi ya kijiji, kata na wilaya, ambapo havipo. Aidha, wataendeleza kuunganisha mashirika ya wakulima wadogo ambapo itawezesha kuongeza upatikanaji wa pembejeo, ushauri wa kilimo na masoko. Mpangilio rasmi na wa uwazi kwa mahusiano ya mkataba ya kilimo ni njia muhimu ya kuendeleza ufanisi na ambayo itasaidia kupata bei nzuri na, kwa kipindi kirefu, kupunguza vikwazo vya usambazaji wa bidhaa za kilimo.

**Jedwali Na. 44: Maeneo ya kipaumbele ya ASDP II yaliopendekezwa katika shughuli na uendeshaji wa ushirika**

| Hatua za utekelezaji | Shughuli |
|---|---|
| 1.Kuimarisha mfumo wa udhibiti, taasisi na usimamizi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika wa Tanzania (TCDC) na Mashirika ya jamii | 1.1. Kufanya mafunzo ya wakaguzi 95 wa vyama vya ushirika kila mwaka katika ukaguzi, usimamizi, uhasibu na utunzaji kumbukumbu wa vyama vya ushirika vya jamii |
| | 1.2. Kuwezesha Ofisi ya Msajili, kutekeleza kazi za udhibiti katika ngazi za kitaifa, za kikanda na za wilaya |
| | 1.3. Kuwezesha kufanya mikutano maalum ya jumla ya vyama vya ushirika |
| | 1.4. Kufanya ukaguzi wa mambo na shughuli za Shirikisho la Ushirika Tanzania; 5,500 AMCOS; SACCO 8,000; vyama vya ushirika 45 na muungno wa vyama vya ushirika 4 |
| 2. Kuimarisha harakati za ushirika (ngazi zote) kuchukua jukumu la kukuza na kazi za udhibiti binafsi | 2.1. Kuwezesha utoaji wa elimu ya vyama vya ushirika kwa wanachama wa Bodi ya vyama vya ushirika, usimamizi na wanachama wa kawaida katika jamii za vyama vya ushirika 2,000 kila mwaka. |
| | 2.2. Kuendeleza na kutoa mipango wa utekelezaji kwa vyombo vya habari juu ya maadili ya vyama vya ushirika, shughuli zitakazofanyika na kampeni za kuimarisha SACCO |
| 3. Kujenga uwezo na kuimarisha mashirika ya vyama vya ushirika katika usimamizi wa biashara na mbinu za uongozi | 3.1. Kufanya mafunzo ya wakufunzi (TOT) kwa timu ya wilaya na kuhamasisha ukuaji ndani ya timu ya wizara kuu. |
| | 3.2. Kutoa mafunzo ya kiwango cha juu kwa wafanyakazi wa TCDC juu ya ujuzi wa ujasiriamali, ujuzi wa mazungumzo, mipango ya mradi na usimamizi pamoja na kuandika mipango ya biashara, kuchanganya ujuzi baina ya wafanyakazi |

| Hatua za utekelezaji | Shughuli |
|---|---|
| 4.Kuimarisha na kuendesha mfumo wa usimamizi wa takwimu za ushirika wa vyama vya wakulima (CODAS) | 4.1. Kuimarisha udhibiti wa uwasilishaji wa taarifa/ habari kwa vyama vya ushirika |
| | 4.2. Kuanzisha vituo vya mfumo wa teknolojia ya habari kama zana za kimkakati kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao ya wakulima |

**Chanzo:** Tume ya Ushirika.

### Eneo dogo 4.3: Uratibu wa programu ya ASDP II (Upangaji na Utekelezaji ngazi ya Taifa, Mkoa na Serikali za Mitaa).

273 Changamoto kubwa katika utekelezaji wa ASDP II ni uratibu wa miradi mbalimbali katika sekta ambayo inatekelezwa ndani na nje ya mfumo wa bajeti. Hili linahitaji mfumo mzuri wa uratibu chini ya uongozi imara wa ASLMs na wadau wote wa sekta kuanzia ngazi za Taifa na Halmashauri. Kutokana na hali hiyo kuna haja ya kuimarisha ushirikiano wa mipango / miradi yote ya sekta ya kilimo katika kuzingatia mtazamo mpana chini ya ASDP II. Utaratibu huo ni kwa ajili ya miradi yote ndani au nje ya bajeti. Uratibu wa ASDP II utazingatia uimarishaji wa mawasiliano katika ngazi ya Taifa, Mikoa na Halmashauri (angalia pia eneo dogo la 4.5).

274 ASDP II itaongeza wigo wa uratibu kwa kujumuisha shughuli zinazogharamiwa kupitia mfuko wa pamoja na zile zilizo nje ya mfuko. Mkakati wa sekta una lengo la kuwa na mfumo mpana zaidi wa mipango, bajeti, utekelezaji na ufuatiliaji wa shughuli katika sekta ya kilimo, ikiwa ni pamoja na shughuli za sekta binafsi kwa kufanya yafuatayo: (i) Kuanzisha mfumo wa uratibu wa shughuli zote za kilimo zinazotokana na upangaji wa mipango, mgao wa rasilimali, utekelezaji na ufuatiliaji wa shughuli; (ii) Kuimarisha uratibu wa shughuli katika ngazi ya Taifa na Halmashauri kwa kuimarisha ushiriki wa Tawala za Mikoa kama kiungo kati ya Wizara na Halmashauri; na (iii) Kurekebisha baadhi ya taasisi ili kuboresha uratibu na ufanisi wa utoaji wa huduma kwenye sekta ya kilimo.

275 Muundo imara wa uratibu wa ASDP II utajumuisha: (i) Usambazaji mkubwa wa malengo ya pamoja ya ASDP II kwa wadau wote wa sekta; (ii) Muunganiko wa jitihada za wadau wote wa sekta za kufikia malengo ya ASDP II kulingana na mwongozo bora wa ASLMs; (iii) Mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini wenye takwimu sahihi za kilimo; (iv) Kufanya mapitio ya utekelezaji katika sekta kwa kuwahusisha wadau wote wa sekta, ikiwa ni pamoja sekta ya binafsi kushiriki, (v) Kuwepo na mfumo wa wazi wa majadiliano katika masuala muhimu ya sera na mifumo ya usimamizi, (vi) Kuwepo kwa mitandao taarifa katika masuala yote ya kisekta; na (vii) Kuwepo kwa uwezo mkubwa wa ASLMs katika masuala ya uchambuzi na usimamizi juu ya uratibu wa sekta.

**276 Miundo ya taasisi na majukumu ya uratibu.** Utekelezaji wa uratibu wa sekta kwenye ASDP II utaunganishwa na kuimarishwa kwenye mifumo na miundo iliyopo ya serikali huku ikizingatia uzoefu uliopatikana wakati wa utekelezaji wa ASDP-1 ili kuunga mkono utekelezaji wa mipango iliyopendekezwa. Hii itaruhusu muendelezo wa juhudi za kuimarisha mifumo ya serikali katika ngazi za kitaifa na kijamii kwa ajili ya kuchochea matokeo . Hata hivyo, ASDP II itatilia mkazo vipengele vilivyo nje ya bajeti ya mpango na mfumo wa kutoa taarifa utakuzwa ili kukidhi hivyo vipengele vilivyomo kwenye lengo kubwa la mpango huo.

**277 Uratibu katika ngazi ya Taifa.** Uongozi wa uratibu na kazi zake chini ya ASDP II katika ngazi ya Taifa ni pamoja na kufanyika kwa: (i) Mkutano wa Taifa wa Wadau wa Sekta ya Kilimo (NASSM); (iii) Kamati ya Usimamizi na Maamuzi ya Sekta ya Kilimo (ASC); (iii) Kamati ya Ushauri wa Sekta ya Kilimo (ASCG) (iv) Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi (TCD), (v) Vikundi Kazi (TWGs); na (vi) Kitengo cha Taifa cha Uratibu (NCU). Uratibu wa sekta kwenye ASDP II ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. **45.**

**Jedwali Na. 45: Vyombo vya Uratibu Mifumo na wajumbe wa ASDP II katika ngazi ya Taifa (Muhtasari)**

| Kikao | Mwenyekiti | Wajumbe |
|---|---|---|
| Mkutano wa Taifa wa Wadau wa Sekta ya Kilimo (NASSM) | Waziri Mkuu | Mawaziri wa Sekta ya Kilimo na wale wanaohusiana na sekta (ASLM na Wengine), Washirika wa Maendeleo, na Sekta ya Binafsi, Watendaji Wasio wa Serikali, RS, LGA,Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya (DEDs); DAICOs, DLFOs; Viongozi wa Utafiti; Maafisa wa Mafunzo; Wawakilishi wa vyuo vya Elimu ya Juu; Bodi za bidhaa; Taasisi za Fedha; Vyama vya wakulima na Vyama vya Ushirika Vyama vya Ushirika wa bidhaa, na na SACCOS; wawakilishi wa mashirika mengine ya washirika / wadau katika sekta ya kilimo |
| Kamati ya Usimamizi na Maamuzi ya Sekta ya Kilimo (ASC) | Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu | Makatibu Wakuu wa Wizara za Sekta ya Kilimo na Wale wanaohusiana na Sekta (ASLM na Wengine), Wawakilishi wa Washirika wa Maendeleo na Wawakilishi wa Sekta ya Binafsi |
| Mkutano wa Ushauri wa Sekta ya Kilimo (ASCG) | Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu | Makatibu Wakuu wa Wizara za Sekta ya Kilimo na Wale wanaohusiana na Sekta (ASLM na Wengine), Washirika wote wa maendeleo katika Sekta ya Kilimo  Sekta binafsi, Washirika na NGOs / NSA) (ndani na Kimataifa), Vyama vya wakulima na Ushirika Taasisi za Mafunzo na Utafiti |
| Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi | Mkurugenzi ofisi ya Waziri Mkuu | Wakurugenzi wa Wizara za Sekta ya Kilimo |
| Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II (NCU) | Mratibu wa Taifa wa ASDP II | Wajumbe wa Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP (NCU) |
| Vikundi Kazi | Kiongozi wa Kikundi Kazi | Wenyeviti wa vikundi kazi vya Programu |

278 Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Halmashauri zinasimamiwa na kuongozwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI: Idara ya Uratibu wa sekta inahusika na usimamizi wa halmashauri kwa kushirikiana na Sekretarieti za mikoa. Uratibu kuanzia Ofisi ya Rais-TAMISEMI hadi Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri ulianzishwa na kufanya kazi vizuri chini ya ASDP-1 na ASDP II itaendelea kuimarisha uratibu huo wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

279 Uratibu katika Ofisi ya Rais-TAMISEMI utaanza na Mkutano wa Ushauri wa kila mwaka ambao utaongozwa na Waziri-TAMISEMI. Hii itafuatiwa na: (i) Mkutano wa Ushauri wa Sekta ya Kilimo ukiongozwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-TAMISEMI; (ii) Kamati ya Ufundi ya Viongozi wa Maeneo Makuu ya ASDP *(TCCL-OR-TAMISEMI)* ikiongozwa na Mkurugenzi wa Uratibu wa Sekta, na (iii) Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa. **Jedwali Na. 46** linaonesha kwa kina kutoka ngazi ya kijiji hadi TAMISEMI.

**Jedwali Na. 46: Vyombo vya Uratibu, mifugo na wajumbe wa ASDP II katika ngazi ya TAMISEMI (Muhtasari).**

| Taasisi | Mwenekiti | Wajumbe |
|---|---|---|
| Mkutano wa Ushauri wa Kilimo wa Mikoa na Serikali za Mitaa (ARLGAC). | Waziri TAMISEMI | Makatibu Wakuu wa ASLMS, Wakurugenzi (DPPs) wa Wizara za Sekta ya Kilimo, Washirika wa Maendeleo wa Kilimo wanaosaidia RS na LGA, DED na wataalam wa kilimo ngazi ya Mkoa, Wilaya na Kata, Sekta binafsi, NGOeneo dogoBOs na wadau wengine katika Mikoa na Halmashauri husika |
| Mkutano wa Ushauri wa Sekta ya Kilimo (ASCG) | Katibu Mkuu-TAMISEMI | Wakurugenzi (DPPs) wa Wizara za Sekta ya Kilimo |
| Kamati ya Ufundi ya Viongozi wa Maeneo Makuu ya ASDP (TCCL-OR-TAMISEMI) | Mkurugenzi wa Uratibu wa Sekta- TAMISEMI | Viongozi wa TAMISEMI pamoja naWakurugenzi wengine katika TAMISEMI |
| Kamati ya Ushauri wa Mkoa (RCC) | Mkuuwa Mkoa (RC) | Katibu Tawala wa Mkoa (RAS), Makatibu Tawala wa Wasaidizi, Wakuu wa vitengo (Kama kwa Sheria) |
| Kamati ya Ushauri ya Wilaya | Mkuuwa Wilaya (DC) | Mtendaji wa Wilaya, Wakuu wa Idara |
| Kikao cha Madiwani | Mwenyekiti wa Halmashauri | Wajumbe wa Baraza, Timu ya Menejimenti ya Wilaya( CMT), Mkurugenzi Mtendajiwa Wilaya |
| Halmashauri ya Maendeleo ya Kata | Diwani | Wajumbe wa Halmashauri ya Maendeleo ya Kata |
| Mkutano wa Baraza la Kijiji | Mwenyekiti wa Kijiji | Wajumbe wa Serikali ya Kijijwa Mkutano wa Baraza |
| Mkutano Mkuu wa Kijji | Mwenyekiti wa Kijiji | Wanakijiji wote wenye umri wa zaidi ya miaka 18 na wenye akili timamu |

280 **Makatibu tawala wa Mkoa.** Jukumu la Makatibu tawala wa mkoa ni kuisaidia halmashauri katika maandalizi ya Mipango ya kilimo ya Wilaya (DADPs), usimamizi katika utekelezaji wa DADPs, na kusaidia katika utoaji wa taarifa za robo mwaka na mwaka kwa kufuata Miongozo ya DADPs. Katibu Tawala Msaidizi wa kitengo cha Uchumi na Uzalishaji chini ya RS anawajibika moja kwa moja kusaidia shughuli za maendeleo ndani ya mkoa kwa kusaidiana na Mratibu wa ASDP Mkoa na maofisa wenzake wa sekta ndogo maalum. Maafisa hawa hutoa msaada wa kiufundi na usimamizi kwenye halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa ASDP II. Sekretarieti za mikoa zitafanya kazi kwa karibu na Kikundi Kazi (TWG) na Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II endapo ushauri na msaada utahitajika.

281 **Uratibu katika ngazi ya Halmashauri.** ASDP II itaimarisha mifumo iliyoanzishwa chini ya ASDP-1 kwa ajili ya shughuli za Halmashauri. DADP itaendelea kuwa chombo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kilimo katika ngazi ya Halmashauri. Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya (DED) atasimamia majukumu yote ya utekelezaji wa shughuli na fedha zinazotumika katika ngazi ya Halmashauri. Timu ya Baraza la Usimamizi (CMT), ambayo inaongozwa na Mkurugenzi na kuhudhuriwa na wakuu wote wa idara pamoja na DAICO na DLFO, itapewa taarifa juu ya masuala na hali ya maendeleo ya kilimo chini ya DADP.

282 Mipango ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) na wanakijiji kupitia michakato ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O & OD) ambayo hujumuishwa na kuwa sehemu ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Kijiji (VADPs): mchakato huu huongozwa na Kamati ya Mipango, Afisa Ugani wa kilimo ngazi ya kijiji (VAEO) , Afisa Mtendaji wa Kijiji (VEO) kwa kusaidiwa na Timu ya Wawezeshaji ya Wilaya kulingana na miongozo ya DADP. Mapendekezo kutoka katika kijiji husika yanawasilishwa kwenye kata na kujumuishwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata, ambayo huongozwa na Afisa ugani wa kilimo ngazi ya kata (WAEO) chini ya usimamizi wa Afisa Mtendaji wa Kata (watendaji wa kata), kwa ajili ya

kuwasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (DED). Mapendekezo hayo yatajumuishwa pamoja na DAICO na DFLO ili kupata DADP. Mchakato mzima utakuwa unaongozwa na miongozo ya DADP na maelekezo ya kina ya ASLMs kwa kupitia TAMISEMI, ikiwa ni pamoja na mfungamano wa mpangilio kwenye ASDP II.

283 Njia mojawapo muhimu ya uratibu katika ngazi ya Halmashauri ni kuwepo kwa jukwaa (forum) la kujadili na kuweka kipaumbele cha zao au bidhaa na wadau wa sekta ya kilimo katika ngazi ya Halmashauri (eneo dogo 3.2). Jukwaa hili litaleta pamoja wadau muhimu katika mnyororo wa thamani wa bidhaa za kipaumbele pamoja na kuendeleza, kuendesha na kutekelezaji shughuli za DADPs ikiwa ni pamoja na masuala mbalimbali kama vile kuongeza tija, kuongeza thamani na upatikanaji wa soko. Wadau katika ngazi ya Halmashauri ni pamoja na sekta ya binafsi (wafanyabiashara, wasindikaji, wasafirishaji, taasisi za fedha, nk), NGOs, washirika wa maendeleo na taasisi mbalimbali za umma ambazo zitatoa aina mbalimbali za misaada ya kiufundi. Kwa hivyo ni muhimu sana kwa Halmashauri kuandaa DADPs jumuishi ambayo itajumuisha shughuli za maendeleo ambazo ziko katika mfumo wa bajeti ya Serikali za Mitaa na ile ya nje ya mfumo, na usimamizi wa pamoja wa utekelezaji na ufuatiliaji.

**284 Miradi nje ya bajeti ya Serikali.** Wakati Serikali inaonesha kwamba, washirika wa maendeleo wataendelea kuchangia fedha za maendeleo kupitia msaada wa bajeti, fedha za maeneo yanayolindwa, fedha mahsusi, kupitia miradi na shughuli nje ya bajeti, ni muhimu miradi yote inayofadhiliwa kwa njia yoyote ile kuainishwa na ASDP II. Washirika wa maendeleo wanapaswa kushirikiana katika mfumo wa serikali ili kuhakikisha kuwa wanaendana na malengo ya kitaifa kwa kubadilishana uzoefu. Shughuli za miradi nje ya bajeti ya serikali na mipango ni lazima kuwa chini ya makubaliano kati ya mradi na serikali, kama itakavyoainishwa katika makubaliano na maelewano ambayo yataelezea utaratibu wa utekelezaji ikiwemo kupanga na ufuatiliaji wa shughuli.

**Sanduku Na 7: Miradi ya nje ya bajeti ya Serikali**

**Miradi ya nje ya bajeti katika mfumo wa ASDP II**

Kuna mtizamo kwamba mashirika au taasisi zisizo za kiserikali ni tishio kwa maendeleo ya nchi na hivyo baadhi ya halmashauri kupunguza na kusababisha kukosekana kwa mawasiliano ya kutosha katika kupanga, utekelezaji na kufuatilia kwa pamoja wa miradi ya maendeleo. Mtazamo huu unapaswa kusahihishwa kwa kushirikisha mashirika yasiyo ya kiserikari (NGOs) kwenye matarajio ya maendeleo ya ASDP II na mipango mingine ya kitaifa.

Mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikari (NGOs) katika maendeleo utaimarishwa kwa kuboresha uratibu wa ASDP, na mafunzo yanaweza kupatikana pia uwezo wa wizara katika kupanga kuimarishwa ili kupata maendeleo kwa kupitia ushirikiano mkubwa. Kwa hivyo, miradi ya mashirika yasiyo ya kiserikali inapaswa kutambulika, kusajiliwa na kusambazwa kwa ajili ya ufahamu na kuchangia takwimu ya utendaji kwenye shughulu za ufuatiliaji na tathmini .

Shughuli za washirika wa maendeleo katika kilimo pia zitajumuishwa katika kazi za ufuatiliaji na tathmini kwa niaba ya ASDP II, kama vile ambazo zinaweza kufanywa na miradi ya washirika wa maendeleo kwa manufaa ya tathmini ili kukidhi mahitaji ya mshirika.

## Eneo Dogo 4.4: Ufuatiliaji na Tathmini ikiwa ni pamoja na (Takwimu za Kilimo)

285 Upatikanaji wa takwimu sahihi na kwa wakati yalikuwa ni mapungufu makubwa katika sekta wakati wa utekelezaji wa ASDP-1. Kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Takwimu za Kilimo ( 2014), Sensa ya Taifa ya Kilimo ya Sampuli, Sensa ya mwaka ya kilimo (AASS), na Mfumo wa Kukusanya Takwimu za kilimo (ARDS) ni muhimu kuunganisha na kujumuisha katika muelekeo wa kuwa na chombo cha kusaidia upatikanaji wa takwimu na taarifa za uhakika na kwa wakati kwa ajili ya kufanya maamuzi. ASDS ni matokeo ya kati IR4.5 (Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini na takwimu za kilimo) inalenga maeneo ya kipaumbele katika: (i) Kuimarisha na kuwianisha kazi ya ufuatiliaji na tathmini ili kupata taarifa za awali za kuwezesha kubuni programu na miradi ya maendeleo; na (ii) Kuhuisha ubora wa takwimu, upatikanaji wa takwimu za kilimo kwa wakati na kwa gharama nafuu.

286 Lengo dogo la eneo hili ni kuhakikisha kwamba kuna maboresho ya upatakanaji wa takwimu kwa wakati, ubora na uhakika wa takwimu za mara katika sekta ya kilimo, kutoa takwimu zinazohitajika kufuatilia utekelezaji wa ASDP II , kwa kuanzia na viashiria vilivyopo katika bango kitita, pamoja na takwimu za kijumla.. Katika kipengele hiki, ufadhili utagawanywa katika maeneo mawili muhimu: (i) Ufadhili wa ufuatiliaji na tathmini ya ASDP II; na (ii) Ufadhili wa takwimu za kilimo na juhudi za ufuatiliaji na tathmini ya sekta .

287 Ufuatiliaji na Tathmini ya **ASDP II.** Moja ya mambo ya kujifunza kutoka ASDP-1 ni kwamba ucheleweshaji wa tafiti muhimu ulisababisha upungufu katika taarifa ambao ulifanya ufuatiliaji na tathmini ya matokeo ya awamu ya kwanza kuwa hafifu. Hivyo, ilikuwa rahisi kudai kuwa ASDP-1 haikufikia malengo yake, kwamba hapakuwa na matokeo na kwamba rasilimali zilisambazwa katika miradi mingi midogo midogo. Viashiria vingi muhimu vya ASDP-1 vilitegemea kukamilika kwa wakati Sensa ya Kitaifa ya Kilimo na matokeo yake kusambazwa kwa kasi. Kulikuwa na mkanganyiko katika ufuatiliaji wakati wa ASDP-1 kati ya mradi maalum na ukusanyaji wa takwimu za matokeo ya sekta nzima: kwa sababu ya muunganiko wa wazi na bajeti, miradi ilipewa kipaumbele zaidi kuliko Programu, na kusababisha udhaifu wa ufuatiliaji wa sekta nzima katika ASDP.

**288 ASDP II inatoa na kutekeleza mfumo unaolenga matokeo kwa ajili ya sekta ya kilimo.** Kwa kuwa wahusika mbalimbali watatekeleza shughuli na miradi yao katika ASDP II, ufuatiliaji na tathmini unahitaji uratibu imara na uwezo wa kukusanya, kuchakata, kuchambua na kuwasilisha takwimu. Uwezo wa ufuatiliaji na tathmini kwenye vitengo vya Wizara za sekta ya kilimo, Kikundi kazi cha ufuatiliaji na tathmini na Kitengo cha Taifa cha uratibu kitahitaji kuimarishwa katika ASDP II kupata uratibu imara wa ufuatiliaji na tathmini na timu ndogo za ufuatiliaji na tathmini kupewa kazi za kila siku za uendeshaji na uchakataji wa takwimu katika kila Wizara za sekta ya kilimo. Taarifa juu ya hali ya ukusanyaji wa takwimu na hali kwa ujumla / mafanikio ya sekta zinatakiwa kuwasilishwa katika ngazi ya maaamuzi ya ASDP II , na pia kusambazwa kupitia tovuti au njia nyingine yoyote kwa uwajibikaji wa Programu.

289 Utafiti wa awali utafanyika katika mwaka 2016/2017 na pia utatumia takwimu zilizopo zitakazopatikana kutoka vyanzo mbalimbali. Sensa ya Taifa ya Kilimo itakayofanyika mwaka 2016/2017 (mwaka wa marejeo ni 2015/2016) na kipindi cha miaka 10, kwa kushirikiana na AASS na TWG pia itatoa majumuisho ya viashiria vya awali na vya matokeo na katika ngazi ya mwisho kwa ajili ya programu ya sekta. Kwenye muda wa kati, utafiti wa kati unaweza kufanyika (kama itakavyohitajika) ili kuruhusu marekebisho kufanyika katika mfumo wa matokeo ili kuwa na taarifa sahihi za utekelezaji wa ASDP II.

290 Ili kuruhusu ufuatiliaji wa viashiria muhimu vya mafanikio vilivyotambuliwa katika mfumo wa matokeo, (tazama Kiambatisho Na. II), viashiria vya matokeo ya kati vitatathminiwa kila mwaka ili kutoa mrejesho muhimu kuhusu utekelezaji wa ASDP II na upimaji wa malengo mkakati. Kutokana na kwamba AASS italenga zaidi juu ya takwimu za uzalishaji na tija kwenye mazao, mifugo na uvuvi, njai sahihi ni kujumuisha viashiria mahsusi vya programu katika AASS na takwimu za wilaya; Hata hivyo, siyo viashiria vyote vya matokeo ya kati vitahitajika kutathminiwa kila mwaka. Sampuli hii lazima iwe sawa kwenye ngazi zote za wilaya ili: kuzalisha takwimu sahihi katika kipindi cha muda mfupi (walau miezi 3-4) matumizi ya vifaa vya kielektroniki yatahamasishwa .

291 Mfumo wa matokeo ya jumla ya ufuatiliaji na tathmini wa ASDP II ikiwa ni pamoja na athari na matokeo ya tathmini, matokeo ya ufuatiliaji, taarifa ya robo mwaka ya utekelezaji na taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaratibiwa kupitia mfumo wa OR- TAMISEMI.

**Kielelezo NA. 21: Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa ASDP na utendaji wa sekta**




## Mapendekezo ya maeneo makuu ya utekelezaji.

292 *Uimarishaji wa takwimu za kilimo, uwezo wa kisekta wa kutathmini ufuatiliaji, na uchambuzi*. Kulingana na Mkakati wa dunia wa Kuboresha Kilimo na Takwimu za Vijijini, ulioingizwa nchini Tanzania na Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA), FAO na AfDB, ulilenga kwenye ASSP ambayo iliandaliwa na kikosi kazi cha takwimu za kilimo, eneo hili dogo litahusisha shughuli za kipaumbele zifuatazo:(i) kugharamia sensa ya Taifa ya mazao na mifugo *(NSACA)*, inatarajia utafanyika mwaka 2016/2017 (kwa kurejea mwaka 2015/2016); (ii) ufadhili wa AASS katika kipindi cha utekelezaji wa ASDP II (2015-2025); (iii) kuimarisha mfumo wa kukusanya takwimu za kilimo za mara kwa mara na ufadhili wa idara ya ufuatiliaji na tathmini na TWG; na (iv) kuongeza uwezo wa uchambuzi wa ASLMs kwa ajili ya kupanga na kufanya mapitio ya sera za kisekta , mzunguko wa bajeti ya kila mwaka, na mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya umma *(PERs)*. Uwekezaji huu utakuwa muhimu chini ya ASDP II, ikizingatiwa kwamba hii ni programu kubwa ya umma na kisekta inayofadhiliwa katika sekta, na kwamba hakuna programu nyingine inayoendelea kugharamia katika eneo hili.

293 **Sensa ya Taifa ya Kilimo (NSCA).** Kutokana na kuwa ASDP II itakuwa ni mojawapo kati ya miradi michache mikubwa / programu zitakazogharamia sekta ya kilimo kupitia bajeti ya serikali kwa miaka ijayo, na kwamba ugharamiaji/uwezeshaji kifedha kwa takwimu za kilimo ni mjadala unaoendelea chini ya uangalizi wa Mkakati wa Dunia wa Kuboresha Kilimo na Takwimu Vijijini.washirika kadhaa, ikiwa ni pamoja na serikali, wameonyesha nia ya kushiriki katika ufadhili wa NSCA. Hii inaonekana kama

ni utafiti muhimu na utekelezaji wake wa kawaida utatoa mfumo wa pamoja wa kitaifa kwa miradi yote inayotekelezwa katika sekta ya kilimo ya Tanzania. Inakusudiwa kuwa sensa ya Taifa ya mazao na mifugo ( NSCA) itafanyika kila baada ya miaka 10, na itatoa hadi katika ngazi ya mkoa takwimu katika wigo mpana wa viashiria mbalimbali, kulingana na ukubwa wa sampuli ya kaya 50,000. ASDP II itagharamia sensa ya Taifa ya mazao na mifugo (NSCA) ijayo, ambayo itafanyika katika mwaka 2016/2017.

294 **Sensa ya ya Kilimo ya kila mwaka (AASS).** Mpango mkakati wa Takwimu za Kilimo uliandaliwa na kikosi kazi cha takwimu za kilimo ilitarajiakuwa AASS itatoa takwimu za kila mwaka, za uzalishaji na tija za mazao makuu na aina ya mifugo. Gharama ya kila mwaka ya AASS bado haijaelezwa kikamilifu na wala mbinu za ukusanyaji takwimu hazijabainishwa au dodoso kuandaliwa. Hata hivyo, sensa ya kila mwaka ina lengo la kupata viashiria muhimu vya matokeo kwa ajili ya ufuatiliaji wa sekta. Tija na uzalishaji ni miongoni mwa viashiria hivyo, lakini kuna baadhi ya viashiria muhimu zaidi kama matumizi ya teknolojia bora na upatikanaji wa huduma. Katika ASDP-1 viashiria hivi vilipatikana kutoka kwenye sensa ya Taifa ya kilimo ambayo ilikuwa ikifanyika kila baada ya miaka mitano (5). Katika ASSP, NSCA imebadilika kutoka kipindi cha miaka 5 hadi kipindi cha miaka 10 ya kimataifa.

295 Ndani ya Kikundi kazi cha Takwimu za Kilimo (NBS, ASLMs na msaada wa kiufundi kutoka USDA na FAO), kuna majadiliano yanayoendelea ya kimbinu kuhusu sampuli (inayolenga eneo, orodha au mchanganyiko), maudhui ya dodoso na uwakilishi wa takwimu katika ngazi ya mikoa na wilaya. Kuna wasiwasi kuwa mbinu za sasa za ukusanyaji wa takwimu zinalenga maslahi ya USDA. Ni muhimu kuwa majumuisho ya matokeo kwenye dodoso la AASS yakaingizwa kikamilifu katika tathmini na ufuatiliaji wa ASDP II katika mchakato wa utekelezaji wa sekta ya kilimo.

**296** **Mfumo wa Kukusanya Takwimu za Kilimo (ARDS)** ni mfumo muhimu wa usimamizi na mawasiliano ambao uliboreshwa chini ya ASDP-1. Rasilimali kubwa imewekezwa katika kujenga kanzidata ya kitaifa (awali ilijulikana kama LGMD2, lakini sasa inaitwa (*ARDS web portal )* programu ya wavuti na taarifa zilizogawanywa katika ngazi ya wilaya kufafanua mtiririko wa takwimu, kuandaa mfumo wa takwimu, taratibu kwa ajili ya ukusanyaji wa takwimu katika ngazi ya vijiji na kata na usambazaji wa takwimu kutoka ngazi ya wilaya kwenda ngazi ya kitaifa. Shirika la Kimataifa la Japani (JICA) limetoa msaada wa muda mrefu wa kiufundi na kujenga uwezo wa kueneza ARDS nchi nzima. Mfumo huu hutoa takwimu za matokeo/ mafanikio ya sekta ya kilimo, na hutegemea afisa ugani kutoa taarifa za mwezi, robo mwaka na mwaka, ambazo hujumuishwa katika ngazi ya wilaya na kuingizwa katika kanzidata inayotegemea mtandao, na kufanya zipatikane katika wizara za sekta ya kilimo (ASLMs) kupitia Sekretarieti za Mikoa na OR-TAMISEMI. Mfumo wa kukusanya takwimu za kilimo kwa sasa una dirisha kwa ajili ya watumiaji katika programu ya wavuti ya *"ards.go.tz"* ambapo watumiaji wanaweza kupata taarifa kwa kupata kitambulisho cha mtumiaji kutoka Kikundi kazi cha ufuatiliaji na tathmini. Kuna haja ya kurekebisha wigo wa Mfumo wa kukusanya takwimu za kilimo na vyanzo vingine vya takwimu, kama vile AASS na NSCA, lakini pia taarifa za robo mwaka za utekelezaji na kifedha kuepuka kujirudia na kuboresha ubora wa takwimu, upatikanaji kwa wakati. Pia ni muhimu kuimarisha uratibu kati ya ARDS, mfumo wa utoaji wa taarifa za tahadhari ya chakula pamoja na mifumo mingine ya ukusanyaji takwimu kwa ujumla.

**297** **Kikundi kazi cha Ufuatiliaji na Tathmini** hukusanya ripoti ya mwaka ya utekelezaji wa ASDP ambayo inatoa taarifa juu ya viashiria muhimu vya matokeo na matokeo ya mwanzo na kushiriki katika mapitio ya sekta ya pamoja (JSR) na mapitio ya matumizi ya Umma (PERs) (tazama eneo dogo 4.4), ambayo hufanya tathmini ya kila mwaka ya mafanikio yaliyopatikana chini ya ASDP II.

**298** **Mapitio ya pamoja ya Sekta ya kilimo.** Mapitio ya pamoja ya sekta yatahusisha sehemu muhimu ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini na yatafanyika baada ya kukamilisha Sensa ya mwaka ya kilimo (AASS) zinazofanywa na NBS mara moja kabla ya NASSM. Itakuwa inafanywa na Serikali, washirika wa maendeleo na washauri elekezi kupitia mapitio ya mpango ya wiki kadhaa kwa misingi ya kufanya uchambuzi wa takwimu za kitaifa. Aidha, itahusisha ziara za ufuatiliaji katika mikoa iliyochaguliwa ambapo ASDP II inatekelezwa. Mapitio ya pamoja ya sekta yatakuwa ni jukwaa la uratibu na majadiliano ili kuwezesha kubadilishana mawazo na fursa ili kuchukua hatua sahihi katika usimamizi wa miradi. Mapendekezo ya mapitio ya pamoja ya sekta yatawasilishwa katika Mkutano Mkuu wa Taifa wa Wadau wa Sekta ya Kilimo (NASSM) kwa ajili ya majadiliano na kuchukua hatua sahihi.

Taarifa kutoka mkutano huu itaandaliwa na Timu ya Uratibu wa ASDP II Taifa na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Taifa ya Uendeshaji kwa maamuzi.

299 Vilevile, mapitio ya matumizi ya Umma/Serikali yanatoa fursa zaidi ya kufuatilia maendeleo na mafanikio ya ASDP II katika maslahi mapana ya uchumi wa Taifa. Matokeo ya mapitio ya pamoja ya sekta /mapitio ya matumizi ya umma yatajadiliwa katika mkutano wa ushauri wa sekta ya kilimo (ASCG), na kisha kuwasilishwa kwenye Kamati ya Usimamizi na Maamuzi ya sekta ya kilimo (ASC) kwa hatua zaidi za utekelezaji.

### Eneo Dogo 4.5: Kuimarisha uwezo wa kitaasisi, usimamizi wa maarifa (KM) na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika sekta ya kilimo

300 Sekta ya kilimo inahusisha Wadau wengi na Taasisi nyingi katika ngazi ya Taifa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaotoa huduma mbalimbali zinazohitajika na wakulima na Wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa bidhaa. Hivyo, ni muhimu kuhakikisha uratibu na utoaji wa huduma bora, kuepuka kujirudia kwa juhudi zinazochukuliwa na upotevu wa rasilimali. Malengo ya ASDS ni kuimarisha uwezo wa Taasisi, miongoni mwa mengine, kwa ajili ya (i) Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia utekelezaji wa shughuli za kilimo, ikiwa ni pamoja na Usimamiaji wa Fedha za Umma (PFM); (ii) Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi (PPP) katika uwekezaji kwenye sekta ya kilimo na utoaji wa huduma (ugani); (iii) Rasilimali watu katika wizara za sekta ya kilimo (ASLMs) kuongoza utekelezaji na kuendeleza uvumbuzi; (iv) Mifumo ya uendelezaji wa maarifa ya kwa ajili ya kumbukumbu za Taasisi, kubadilishana masuala ya kujifunza na ufuatiliaji wa muda mrefu wa utendaji wa sekta; na (v) Matumizi ya TEHAMA katika kuboresha ufanisi wa msaada wa kiufundi, utawala na usimamizi wa rasilimali na utekelezaji wa majukumu.

**301** **Mageuzi ya Kilimo** yanahitaji rasilimali watu wenye uwezo kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa teknolojia, kuongeza thamani na kuendeleza masoko na uratibu na usimamizi wa sekta kwa ujumla. Kuna haja ya kufanya mabadiliko makubwa ya kuanzisha kizazi kipya cha wakulima ambao watapatiwa ujuzi muhimu unaohitajika ili kukibadilisha na kukifanya kilimo kiwe cha kisasa. Wakati weledi na utaalamu vitazingatiwa kwa umakini mkubwa, ujuzi na maarifa ya kilimo yatatolewa katika ngazi mbalimbali za mfumo wa elimu. Uwekezaji katika kuongeza uwezo wa rasilimali watu utajaziwa na matumizi mazuri ya TEHAMA kwa ajili ya ufanisi wa usimamizi wa sekta, ikiwa ni pamoja na fedha za bajeti na zilizo nje ya bajeti zinazowekezwa katika sekta ya umma.

**302** **Changamoto ni kuimarisha uwezo wa Taasisi** za umma (ngazi ya Taifa na Mamlaka za Serikali za Mitaa) na binafsi/washirika (vyama/vikundi vya wakulima, sekta binafsi na Wadau wasiokuwa wa kiserikali) kusaidia uimarishaji wa uratibu katika kupanga, kutekeleza, uchambuzi wa sera, utafiti, msaada wa huduma za kitaalam, usindikaji, ugharamiaji na ufuatiliaji na tathmini katika sekta ya kilimo, wakati ikihakikishwa kwamba wanawake na vijana wanashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu muhimu. Sekta ya umma itaweka mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na: kuweka viwango na kanuni sahihi na bora, kuwezesha uwekezaji wa umma, kusaidia majadiliano juu ya masuala ya biashara, kuandaa mifumo ya usalama kwa wadau walengwa, kufafanua upatikanaji na usimamizi endelevu wa maliasili, na kutoa takwimu za kilimo zilizoimarishwa. Sekta binafsi, ikiwa ni pamoja na vyama vya wazalishaji, Asasi za kiraia -(CBOs) Asasi zisizo za Kiserikali -(NGOs) na wafanya biashara, yatashiriki kwenye shughuli na pia kuongeza uwekezaji wenye faida kwenye sekta ya kilimo katika uzalishaji, usindikaji na kibiashara.

**303** **Mawasiliano na Utunzaji wa Maarifa.** Masuala muhimu ya mawasiliano na utunzaji wa maarifa ya sekta ambayo yatashughulikiwa ni pamoja na: (i) Uwezo mdogo wa uzalishaji, ukusanyaji, uchambuzi, na uandaaji wa nyaraka za masomo yenye funzo, kusambaza na kubadilishana taarifa katika ngazi zote; (ii) Uelewa mdogo wa wadau kuhusu ASDP II, Mamlaka, Sera na Majukumu ya Wizara za Sekta ya Kilimo katika kufanikisha malengo ya ASDP II; (iii) Mlolongo mrefu wa mawasiliano kati ya Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa; (iv) Vituo vya Taaluma vya Kilimo na Mifugo vya Kata (WARC) ni vichache, vina vifaa vichache ambavyo havitumiki ipasavyo; (v) Upatikanaji mdogo, uchelewaji na ukosefu wa taarifa za kilimo kuhusu pembejeo , vyombo vinavyotoa mikopo, masoko, taarifa za hali ya hewa na teknolojia zingine, (vi) Udhaifu wa kupeana taarifa kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara za Sekta ya Kilimo kwa hatua za haraka za utekelezaji wa ASDP II; (vii) Uratibu na ushirikiano

dhaifu ndani na baina ya vitengo vya Mawasiliano katika Wizara za Sekta ya Kilimo na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na (viii) Udhaifu na ucheleweshwaji wa mrejesho. Masuala ya uendelezaji wa maarifa yaliingizwa kwa nia ya kujua mambo mazuri yaliyofanyika katika programu, mchakato, na mafanikio kwa ajili ya kushirikishana na wadau nchini na kwingineko.

304 Katika kipindi cha utekelezaji wa ASDP-1 juhudi zilifanywa ili kuimarisha mawasiliano katika ngazi zote kwa kuanzisha kikundi kazi cha Mawasiliano kikiwa na majukumu ya kuratibu mawasiliano na utetezi katika kampeni za ASDP. Kikundi Kazi hiki pia kiliandaa mkakati wa mawasilano na utunzaji wa taarifa kwa lengo la kutumia maarifa kwa ufanisi katika namna ya kufanya kazi ili kufikia mafanikio makubwa. Mkakati huo utaendelea kutekelezwa chini ya ASDP II kwa kuhakikisha kuwa: (i) kuna uratibu wa shughuli za mawasiliano na uendelezaji wa maarifa katika sekta; (ii) Wadau wanapata taarifa sahihi kupitia njia zinazofaa; (iii) Kuna mtiririko mzuri wa taarifa kutoka pande zote mbili za upashanaji taarifa, na (iv) Wakulima wamewezeshwa katika kufanya maamuzi na kushiriki kikamilifu katika uandaaji na utekelezaji wa ASDP II.

305 lengo la mawasiliano na uendelezaji wa maarifa ni kuboresha mtiririko wa upatikanaji taarifa, utunzaji wa maarifa, kushirikishana, na kujifunza na kujenga uhusiano mzuri kati ya watendaji ili kufikia malengo na matokeo ya programu. makusudi mahsusi ya mawasiliano na utunzaji wa maarifa ni: (i) Kuimarisha uratibu wa shughuli za mawasiliano na uendelezaji wa maarifa ndani na baina ya Wizara za Sekta ya Kilimo na kati ya Wizara hizo na Mamlaka za Serikali za Mitaa; (ii) Kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa Wizara za kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa mawasiliano na uendelezaji wa maarifa ; (iii) Kuongeza ufahamu na uelewa wa wadau juu ya ASDP II na miradi/mipango mingine ya maendeleo ya kilimo, na (iv) Kuboresha mtiririko wa taarifa, ufikiwaji, upatikanaji, uendelezaji na ubadilishanaji wa maarifa miongoni mwa wadau. Mikakati iliyopendekezwa pamoja na mingineyo ni: (i) kuzijengea uwezo ASLMs, RS na Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa mawasiliano na uendelezaji wa maarifa kwa; (ii) Kuanzisha uhusiano imara unaofanyakazi kwa ajili ya kupanga, kutekeleza na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za mawasiliano na uendelezaji wa maarifa katika ngazi ya kitaifa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; (iii) Kukuza na kuimarisha ushiriki wa sekta ya umma na ya binafsi katika shughuli za maendeleo ya kilimo, (iv) Kuimarisha utunzaji wa nyaraka za mchakato wa uandaaji, utekelezaji, mafanikio na changamoto za ASDP II kwa ajili ya marejeo ya baadaye; na (v) Kuimarisha uenezaji wa utekelezaji wa ASDP II na mipango mingine ya sekta ya kilimo katika ngazi zote kwa kufanya kazi na vyombo vya habari.

306 Matumizi ya TEHAMA , ikiwa ni pamoja na kompyuta, simu za mkononi nk, huongeza maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kwa kuboresha ufikiaji wa habari, kubadilishana taarifa na huduma ya malipo. Serikali ya Tanzania imeanza kujumuisha matumizi ya TEHAMA katika sera muhimu za maendeleo na mikakati ikiwa ni pamoja na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) na Dira ya Maendeleo ya 2025. Dira ya 2025 inatambua wazi kukuza matumizi ya TEHAMA kama ni chombo muhimu kwa ajili ya mageuzi ya kijamii na kiuchumi ambao utasaidia katika kutoa msukumo wa utekelezaji wa Dira.

**307 Malengo ya kuimarisha uwezo wa kitaasisi.** Eneo hili litasaidia uimarishaji wa taasisi za umma ili kuwawezesha kufanya kazi kama wawezeshaji wa kuendeleza sekta jumuishi ya kilimo. Aidha, washirika wasiokuwa wa kiserikali ambao hawakuhusishwa katika eneo lolote nao watajengewa uwezo ili waweze kuchukua jukumu la kuhamasisha kilimo cha kibiashara cha bidhaa za kipaumbele zilizochaguliwa katika Programu. Msaada wa kujenga uwezo utatolewa katika ngazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mikoa na Taifa. Mwendelezo wa kujenga uwezo utafanyika katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa (katika ngazi mbalimbali) ili kuendeleza pale ambapo ASDP 1 ilifikia.

**308 Katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa,** ASDP II itaendelea kuimarisha michakato ya upangaji Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADP) iliyoanzishwa chini ya ASDP I. Programu itazisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha mbinu za mnyororo wa thamani wa bidhaa ndani ya muunganisho wa mifumo imara ya kilimo na masoko. Ruzuku ya nyongeza ya kujenga uwezo wa kilimo ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa pia itatolewa chini ya ASDP II kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote ili kusaidia kudumisha na kuboresha uwezo na mifumo ya upangaji na utekelezaji wake na uwezo kwa ajili ya upangaji na uratibu wa utekelezaji na ufuatiliaji, taarifa na matumizi yake.

309 Kutokana na mkusanyiko wa uwekezaji ambao unatarajia kutokea chini ya ASDP II, msaada wa kujenga uwezo utatolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa za kipaumbele kuanzia mwaka wa kwanza wa utekelezaji hadi mwaka watano. Wakati Mamlaka za Serikali za Mitaa zote zinatarajiwa kuingia kwenye mkondo kutoka mwaka watano na kuendelea. Mamlaka za Serikali za Mitaa zitazalisha angalau asilimia 20 ya uwezo wa bajeti ya kujenga uwezo kutoka kenye mapato yao. Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo si kipaumbele cha awali zitapokea nyongeza ya msingi ya kujenga uwezo wa juu chini ya ASDP II mpaka zitakapoingia katika mkondo mkubwa wa uwekezaji, kuimarisha uwezo wao wa kupanga na kutekeleza shughuli katika mnyororo wa thamani wa bidhaa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Zaidi ya hayo, Mamlaka za Serikali za Mitaa pia zitaweza kupokea msaada kutoka vyanzo vingine, ikiwa ni pamoja na mapato ya Serikali za Mitaa, ruzuku ya kiujumla ya serikali za mitaa kutoka serikali kuu, na kutoka miradi mingine yenye mahusiano na kilimo inayofadhiliwa nje ya ASDP II.

310 Msaada utatolewa kwa ajili ya: (i) Ruzuku ya kujenga uwezo wa timu za ugani za Wilaya na Kata na wadau wengine kuhusu mchakato wa upangaji kwa mapana na kutambua changamoto/vikwazo muhimu kwa tija na ukuaji wa kipato na fursa za uwekezaji katika minyororo ya thamani wa mazao ya kipaumbele; (ii) Kuimarisha mifumo ya kitaasisi na kujenga uwezo katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ikilenga kuboresha uchambuzi wa mipango na ujuzi wa ufuatiliaji na tathmini; (iii) Kuimarisha wigo wa (DADPs) kama mfumo mpana wa uratibu wa sekta ambao unaunganisha miradi yote na mipango inayotekelezwa katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na (iv) Kuendeleza uwezo wa rasilimali watu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutoa huduma ya kiufundi kwa wataalamu wa kilimo na watoa huduma wengine katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**311 Katika ngazi ya Taifa,** ASDP II inalenga watumishi wa timu ya uratibu wa Programu, vikundi kazi (*TWGs*) na watumishi wengine kutoka Wizara za Sekta ya Kilimo na kutoka Mikoani, ambao wanahitaji mafunzo ya kuimarisha uelewa wao wa kutoa msaada katika shughuli muhimu kwenye masuala mbalimbali, kama vile, kilimo-biashara, mbinu za mnyororo wa thamani, ushirikishwaji katika ugani na upatikanaji wa fedha Vijijini miongoni mwa mengine. Kufuatia kutambuliwa kwa mahitaji na uhitaji wa huduma zilizohusishwa, mpango wa mafunzo utaandaliwa na mafunzo maalumu ya muda mfupi yatatolewa na Taasisi na Vyuo Vikuu vya ndani vitakavyofaa ambavyo vitaandaa na kutoa mafunzo yanayofaa kwa mada hizi, au kukasimu kandarasi kwa wataalamu mahiri wa ndani au wa kimataifa kwa mikataba.

312 Kujenga uwezo wa kuboresha na kukabiliana na mfumo wa upangaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya na utoaji taarifa wa DADP, Watumishi ngazi ya kitaifa na Mkoa watajengewa uwezo wa kuandaa takwimu, kufanya uchambuzi na uandishi wa taarifa. Watumishi wa timu ya uratibu ya ASDP, Vikundi kazi watafaidika, kama ambavyo wangefaidika watumishi kutoka Wizara za Sekta ya Kilimo waliochaguliwa na watumishi kutoka Mikoa ya kipaumbele. Eneo lingine ambalo Programu itagharamia ni kujenga uwezo wa kufanya uchambuzi wa sera ikiwa ni pamoja na kupitia kuboreshwa kwa uwezo wa uchambuzi wa Wizara za Sekta ya Kilimo wa kupanga, kufanya mapitio ya utekelezaji wa sekta na Mapitio ya Matumizi ya Fedha za Serikali. Sambamba na hatua nyingine ya Serikali, msaada utalenga kuboresha uchambuzi wa mnyororo wa thamani na sera, lakini pia kushughulikia sera na masuala ya usimamizi yanayoathiri minyororo ya thamani. Wakurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara za Sekta ya Kilimo wataimarisha kazi zao za kuchambua bidhaa maalum na namna ya kuboresha maeneo mbalimbali ya minyororo ya thamani ya bidhaa/mazao husika kwa kushirikiana na mipango mingine Programu ya Kuboresha Miundombinu ya Masoko kuongeza Thamani na Huduma za Fedha Vijijini (*MIVARF*) na Ukanda wa Maendeleo ya Kilimo Kusini mwa Tanzania (*SAGCOT*) na sekta binafsi.

**313 TEHAMA.** Ugharamiaji wa ASDP II uanzishaji na utumiaji wa TEHAMA utahitaji ushiriki wa wataalam wenye uwezo maalumu wa kitaalam katika kuendeleza mifumo jumuishi na yenye ufanisi ili kuwezesha kubadilishana taarifa (upelekaji na urejeshaji) katika ngazi zote ndani ya Wizara / Taasisi na kwenye Taifa, Mikoa, Wilaya, Mamlaka za Serikali za Mitaa / Kijiji na mtumiaji katika ngazi ya mwisho. Teknolojia kwa ajili ya mifumo ya wazi inaboreka kwa haraka wakati gharama zake zikipungua hatua kwa hatua. Maeneo ya kufanyia kazi katika TEHAMA kwenye sekta ya kilimo ni kama ifuatavyo;

**314** **Kuhusisha zana za TEHAMA na mbinu** za kusaidia shughuli za biashara na mipango ya rasilimali, usimamizi na utendaji katika minyororo ya thamani ya kilimo/mifugo/uvuvi. Katika shughuli hii, ASDP II itasaidia uendelezaji na utekelezaji wa mifumo mpya itakayohusisha matumizi ya TEHAMA katika kutoa huduma kwa wadau katika mnyororo wa thamani ili: (i) Kuwa na upatikanaji bora wa huduma za ushauri wa kitaalam, kuboresha utunzaji wa mashamba na shughuli za kilimo; (ii) Kutoa mrejesho na habari kwa washauri na maofisa wa programu; (iii) Kuanzisha mahusiano ya masoko na wasambazaji wa pembejeo na wanunuzi wa mazao kupitia taarifa zinazopatikana, (iv) Kushiriki katika mradi wa huduma za kimtandao (kwa mfano, kwa ajili ya huduma ya pembejeo au utumiaji wa zana bora za kilimo kama vile huduma za vocha za Pembejeo kwa mtandao, pochi ya fedha katika mtandao, mikopo kwa mtandao, n.k); na (v) Kuboresha michakato ya kufanya biashara ndani ya Serikali kwa kutumia TEHAMA. Mapendekezo ya mbinu na njia za TEHAMA pamoja na mambo mengine itakuwa kama ifuatavyo:

- Kuwezesha wakulima na washauri wao kupata elimu pana ya vitendo na habari ikiwa ni pamoja na, bei na upatikanaji wa pembejeo za kilimo, bei za bidhaa za kilimo, hali ya hewa ya eneo husika shughuli za kilimo na uzalishaji wa mifugo, aina ya mbegu na sifa zake, mbinu za utunzaji wa shamba na zana, kwa kutaja vichache nk;
- Kuwezesha mtiririko rahisi na wa utaratibu wa taarifa kutoka kwa wakulima na / au washauri wao kwenda kwa maafisa wa umma wa programu, kuwezesha ukusanyaji wa takwimu za ngazi ya shamba kwa lengo la ufuatiliaji na tathmini, lakini pia kuruhusu wakulima kutoa maoni ya mara kwa mara na kwa wakati kuhusu utekelezaji wa mipango ya umma;
- Kusaidia wakulima katika kutafuta na kuanzisha uhusiano wa masoko ya pembejeo / mazao na wakulima wengine (ukusanyaji wa bidhaa kwa wingi), wanaoweza kuwa wauzaji na wanunuzi.
- Kusaidia matumizi ya mitambo inayojiendesha katika michakato ya biashara ndani ya Serikali ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za umma kwa kutumia TEHAMA

315 Kwa hiyo ASDP II itasaidia: (i) Uendelezaji na utekelezaji wa mfumo wa TEHAMA na usanifu wa uti wa mgongo wake (takwimu za ujumla za kilimo, huduma za mtandao na ufumbuzi jumuishi na ulioboreshwa); na (ii) Kuwapatia washauri wa kilimo / ugani vifaa vya TEHAMA (*Kompyuta mpakato)* za gharama nafuu kwa ajili ya washauri, simu za mkononi kwa wakulima viongozi) na mbinu ili kuwezesha kufikiwa na taarifa za kitaalam na kiuchumi kupitia mtandao wa kubadilishana taarifa muhimu. Uti wa mgongo wa TEHAMA pamoja na mambo mengine utazingatia yafuatayo: (i) Kuunganisha vituo vya sasa vya Serikali vya takwimu za kilimo kuwa katika kituo kimoja cha umahiri wa hali ya juu, (ii) Utoaji wa miundombinu bora ya TEHAMA na huduma sanifu ya usalama kwa wauzaji wa nje (yaani, makampuni) ya huduma za mtandaoni kama vile vocha za Pembejeo kwa mtandao, pochi ya fedha katika mtandao, (iii) Kuwepo kwa mawasiliano kati ya ufumbuzi jumuishi; na (iv) Ukukusanyaji, uchakataji na uorodheshaji wa takwimu.

316 Wizara imeandaa Sera ya TEHAMA na Mpango Kabambe kwa ajili ya sekta ndogo ya mazao, ambayo sehemu yake iko katika hatua za mwanzo za utekelezaji. Ili kuepuka urudiaji wa juhudi, hii Sera na Mpango Kabambe wa TEHAMA inahitaji kusasishwa (fanya ya kisasa) ili kuingiza sekta ndogo, hasa mifugo na uvuvi, lakini pia masoko yakiongozwa na Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji. Kuwa na Sera na Mpango Kabambe wa sekta wa TEHAMA utasababisha kuwepo na mifumo ya sekta nzima, inayoshughulikia mahitaji ya TEHAMA kwa sekta.

**317** **Mawasiliano katika ngazi zote** yataboreshwa kwa utoaji wa magari, pikipiki, kompyuta na gharama zinazohusiana na uendeshaji na uratibu wa kitaifa, Sekretarieti za Mikoa na timu zilizoko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Zaidi ya hayo, vifaa vya mawasiliano (ikiwa ni pamoja na simu za mikononi au tableti ndogo za gharama nafuu) vitafanyiwa majaribio katika ngazi ya Kata kwa ajili ya kusaidia mahitaji ya usimamizi wa programu, huduma za ugani na masoko, lakini pia kwa ajili ya ukusanyaji, upokeaji na usambazaji wa takwimu kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini. Utaratibu utafanywa na makampuni ya simu za mikononi ili kuruhusu usambazaji wa teknolojia au ujumbe wa maandishi kwa wakulima kuhusiana na masoko, Aidha, ASDP II itakuwa na namba za kupiga bila malipo ili kuwezesha wakulima kuwapigia wataalam wao wa ugani au wataalamu waliobobea katika ngazi za Makao Makuu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wakati TEHAMA inaweza isitumike katika maeneo

yote kutokana na kutounganishwa katika miundombinu, inatarajiwa kwamba mtandao utaendelea kupanuka na kutoa fursa kwa jamii ya wakulima.

318 Mapendekezo ya maeneo ya utekelezaji kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa taasisi, TEHAMA na mawasiliano na utunzaji wa taarifa yameonyeshwa katika **Jedwali Na. 47.**

**Jedwali Na. 47: Mapendekezo ya hatua za kukuza TEHAMA na usimamizi wa mawasiliano na utunzaji wa tarifa**

| Maeneo ya utekelezaji | Shughuli zilizopendekezwa |
|---|---|
| **Kuimarisha Taasisi** | i. Mafunzo kwa Timu ya wewezeshaji/wataalam ya uratibu ya Taifa, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kitaaluma/ uwezeshaji<br>ii. Ruzuku ya kujenga uwezo (ikiwa ni pamoja na asilimia 20 ya ushiriki wa ndani)<br>iii. Kuendelea kusaidia Vituo vya Raslimali za Kilimo vya Kata (WARC) |
| **Maeneo ya Utekelezaji wa Usimamizi wa Mawasiliano na Uendelezaji wa wa Maarifa** | i. Kuandaa taarifa za kitaalam (k.m., taarifa za utafiti) kuwa taarifa rahisi kueleweka ili kuweza kutumika na wadau mbalimbali<br>ii. Kufanya mikutano rasmi na ya kawaida kuhusu Usimamizi Mawasiliano na Uendelezaji wa Maarifa (CKM) kati ya Wizara za Sekta ya Kilimo na Mamlaka za Serikali za Mitaa (kuhusu kujenga ufahamu na kupata maendeleo ya utekelezaji)<br>iii. Kuendesha mafunzo kuhusu Mawasiliano na Uendelezaji wa Maarifa na Teknolojia ya Mawasiliano (IT) katika ngazi tofauti<br>iv. Kuandaa na kusambaza miongozo ya utekelezaji wa mkakati wa Mawasiliano na Uendelezaji wa Maarifa<br>v. Kutoa mafunzo ya kitaaluma na mwongozo wa Uendelezaji wa Maarifa (KM) na mawasiliano kwa wataalam wa Mikoani na Mamlaka za Serikali za Mitaa.<br>vi. Kufanya vikao na vyombo vya habari, warsha na semina juu ya masuala ya sekta ya kilimo<br>vii. Nyenzo za kuhamasisha na kuelimisha / walengwa kuhusu mazao/bidhaa<br>viii. Kuandaa kumbukumbu ya mafunzo yaliyopatikana kutokana ASDP na kutambua miradi bora/mambo mazuri chini ya utaratibu utekelezaji mpana wa Kisekta (SWAp) kwa ajili ya kushirikishana na wadau<br>ix. Kushiriki katika matukio ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na ya Taifa kwa utangazaji wa ASDP / DADPs na mipango mingine ya sekta ya kilimo na usambazaji wa ubunifu mpya<br>x. Mitaala ya wanafunzi |
| **Kusaidia Kuimarisha matumizi yaTEHAMA ili kuboresha ufanisi katika sekta hii** | i. Kusasisha Sera ya TEHAMA ya sekta ndogo ya mazao na Mpango Kabambe wa TEHAMA ulioanzishwa na Wizara ili kuingiza sekta ndogo za mifugo na uvuvi<br>ii. Kubuni na kujenga Mfumo wa Taarifa ya Kilimo wa Taifa ambao utaingiza habari za uzalishaji wa kilimo, utafiti na ugani, usimamizi wa matumizi ya ardhi na taarifa za masoko za uuzaji wa bidhaa za kilimo<br>iii. Kuingiza kenye kompyuta shughuli za ndani za uendeshaji wa biashara za Wizara za Sekya ya Kilimo kama vile miradi ya kilimo na usimamizi wa programu, usimamizi wa fedha, udhibiti wa mali na usimamizi wa hesabu na kuhifadhi na usimamizi wa majalada. Serikali imeweka usimamizi wa rasilimali za kifedha na watu katika ngazi Taifa ambazo hazitoshelezi mahitaji yote ya shughuli ya Wizara za Sekta ya Kilimo katika maeneo hayo, na matumizi ya mfumo wa mawasiliano ya kitaarifa baina ya idara mbalimbali za Serikali (*Enterprise Resource Planning –ERP*) utatumika hapa |

| Maeneo ya utekelezaji | Shughuli zilizopendekezwa |
|---|---|
| Kusaidia Kuimarisha matumizi yaTEHAMA ili kuboresha ufanisi katika sekta hii | iv. Utoaji vifaa, kuboresha ubora wa utoaji wa huduma za ICT na kujenga uwezo wa mafunzo ya kwa Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo, TEHAMA<br>v. Kuunda na kuwezesha vituo vidogo vya takwimu vya Wizara za Sekta ya Kilimo kwa ajili ya usimamizi wa habari wa sekta, kuanzisha na kuimarisha Mitandao ya Mawasiliano ya eneo maalumu (LANs) kwa mawasiliano ya kuaminika ya ndani na nje. Wizara za Sekta ya Kilimo pia zitawezesha uunganishaji wa Kata kwenye mkongo wa Taifa<br>vi. Kuandaa hatua za kuchukua ili kuzuia hatari zinazohusiana na matumizi ya TEHAMA<br>vii. Kuimarisha matumizi ya vyombo vya habari kwa kundi kubwa (yaani, simu za mkononi) kwa kushirikishana habari za kilimo<br>viii. Nambari za bure za kupiga ili kupata huduma za ushauri kwa mtu binafsi<br>ix. Mpango kazi wa majaribio wa kielektroniki na ufuatiliaji (katika ngazi ya Kata)<br>x. Utangazaji wa kuhamasisha sekta (wakulima wenye mafanikio, wawekezaji, redio / runinga, *skype / video*, n.k) |

**Kumbuka:** uwekezaji wote wa ASDP II (vifaa na programu) kwa ajili ya kuhamasisha ushiriki wa sekta ya kilimo katika matumizi ya TEHAMA imejumuishwa kwenye eneo dogo 4.5.

### Eneo dogo 4.6: Ufikiaji wa Huduma za Kifedha Vijijini

319 **Usuli.** Kutotosheleza kwa huduma za kifedha zinazotolewa kwa wakulima wadogo wa kibiashara ni kikwazo kikubwa kwa ukuaji wa Kilimo na inakuwa kizuizi cha kuongezeka kiwango cha uwekezaji na kasi ya kilimo cha kibiashara. Mabenki ya kibiashara yanasita kutoa mikopo kwa sekta ya kilimo na zina ufikiaji mfinyu kwa maeneo ya vijijini. Kuna Taasisi mbalimbali za huduma ndogo za kifedha (*Microfinance Institutions-MFI*s) zinazolenga wakulima, lakini zina uwezo finyu wa kuzifikia kaya nyingi za vijijini kutokana na ukosefu wa wafanyakazi wenye ujuzi, mtandao wa matawi na huduma za fedha. Wajasilimali wadogo na wa kati wanaojihusisha na uongezaji wa thamani pia hukutana na kikwazo cha kupata rasilimali fedha.

320 Kwa sasa, hatua zilizoasisiwa na Serikali za kuhamasisha kuwepo kwa taratibu za upatikanaji wa huduma za kifedha kwa ajili ya kilimo zinahusisha yafuatayo kati ya mengine (i) Mfumo jumuishi wa kifedha wa kitaifa (Kamati ya Uendeshaji iko chini ya uenyekiti wa Benki Kuu ya Tanzania na ina wajumbe kutoka Wizara ya Kilimo, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (*CMSA*), Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (*TIRA*,) Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), Mfuko wa Udhamini wa Sekta ya Fedha (*FSDT*), Chama cha Taasisi za Kutoa Huduma Ndogo ndogo za Fedha (*TAMFI)* na Waendeshaji wa Makampuni ya Simu za Mikononi); (ii) Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOs*), hukopesha akiba na fedha ilizokopa kutoka kwa Mabenki ya Biashara kwa Wakulima wadogo wadogo walio Wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo , lakini pia taratibu kama hizo hufanyika kupitia Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACAS*) na Benki za Jamii Vijijini (*VICOBA*) na Vyama vingine vya aina hizo; (iii) Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo kufikia huduma za Kifedha kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao za kilimo (hususan kwa mazao asilia ya biashara); (iv) Benki ya Taifa ya Ushirika ambayo inalenga kutoa huduma za kifedha kwa Vyama vya Ushirika (Vyama Vikuu vya Ushirika); (v) Dirisha la utoaji mikopo lilopo katika Benki ya Rasilimali Tanzania; (vi) Benki ya Ushirika Kilimanjaro na Benki ya Ushirika ya Wakulima Kagera; (vii) Kutoa mikopo kwa vijana ili kushiriki katika shughuli za kuongeza kipato ikiwa ni pamoja na kilimo (Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo); (viii) Mamlaka za Serikali ya Mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato kutoka vyanzo vyake vya ndani na kuzielekeza katika kukopesha Vijana na Wanawake katika eneo lao la Utawala;(ix) Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (*AGITF*) ambao uko chini ya Wizara ya Kilimo; (x) Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kutoa mikopo kwa watu binafsi na vyama vya ushirika (Wakulima scheme); (xii) Mfumo wa Taifa wa Vocha za Pembejeo za Kilimo (*NAIVS*) na programu nyingine zitakazofuatia; na (xiii) Programu ya Kuboresha Miundombinu ya Masoko kuongeza Thamani na

Huduma za Fedha Vijijini (*MIVARF*) [68] kutoa ruzuku kwa Vikundi vya Umwagiliaji au Vyama vya Ushirika vya Masoko ya Mpunga kwa ajili ya ununuzi wa mashine za ukubwa wa kati za kukoboa mpunga. Serikali inapanga kuanzisha na kuendesha Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili kutenga dirisha maalum kwa ajili ya kutoa mikopo ya uwekezaji katika sekta, wakati Mfuko Kichocheo (angalia mfano wa Ukanda wa Maendeleo ya Kilimo Kusini mwa Tanzania -*SACGOT*) na Mpango wa Dhamana ya Mikopo ni baadhi ya hatua mbalimbali zilizoasisiwa kuelekea Biashara husishi za vijijini.

321 Idadi ya benki za biashara inaongezeka (takriban benki 50 mwaka 2014) na baadhi ya hizo zimepanua wigo wa huduma zao hadi katika sekta ya kilimo na usindikaji wa mazao ya kilimo. Utoaji wa huduma za Kifedha (mazao na mifugo) kutoka Mabenki za Biashara kwa maana ya mkopo jumla katika sekta umekuwa ukiongeza taratibu taratibu na kufikia kiwango sawa na asilimia 10 ya mikopo yote inayotolewa (Takriban Shilingi Trilioni 1). Asasi ya Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (*Private Agriculture Sector Support -PASS*) ambayo ilianzishwa mwaka 2000 kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*) kupitia Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini (*CRDB*) imekuwa ikitoa msaada wa kuandaa mipango biashara na udhamini. Taasisi zilizo rasmi na zisizo rasmi za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (*MFIs*), utoaji wa huduma za kifedha kwa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) pia zinasaidia uchumi wa kilimo wa wakulima wadogo wadogo katika maeneo ya vijijini. Hatua zilizoasisiwa za kuwepo mfumo jumuishi wa huduma za kifedha wa kitaifa kupitia Wizara ya Fedha na Mipango zinakusudia kuwa na mpango wa utekelezaji unaolenga asilimia 50 ya watu wazima kupata huduma rasmi za kifedha ifikapo mwaka 2016.

322 Kwa ujumla, hatua mbalimbali zinazoasisiwa na Umma, zinazohusiana na Miradi na Taasisi za kifedha zipo katika ngazi ya Taifa na ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuhamasisha ufikiwaji wa huduma za kifedha za sekta ya Umma, lakini hakuna mkakati ulio wazi (na mpango wa kueleweka na kabambe wa utekelezaji ) unaohamasisha uwepo wa mifumo ya utoaji huduma za kifedha Vijijini ili kuongeza uwekezaji wa Wadau katika sekta ya kilimo kupitia Ubia endelevu wa Umma na Sekta Binafsi (*PPP*). Kuboresha huduma za kifedha katika sekta ni suala muhimu la sera ili kuwezesha uwekezaji wa sekta binafsi.

**323 Kwa upande wa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (*ASDS*),** hatua za umma zinazohitajika zilizopendekezwa, na Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDS*) ni pamoja na: (i) Kuhamasisha huduma za benki za kijamii zilizopo na kuanzisha nyingine mpya katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; (ii) Kubuni vifurushi vya mikopo ya kilimo vinavyowafaa wakulima wadogo wadogo; (iii) Kutoa msaada wa kuanzisha taasisi imara za kifedha ngazi ya chini kama vile Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) na Benki za Jamii Vijijini (*VICOBA*) ikiwa ni chanzo cha awali cha kutoa huduma za kifedha kwa wakulima wadogo wa kibiashara; (iv) Sasisha Sera ya Taifa ya Huduma ndogo za Fedha kwa kushirikiana na Wizara zingine ili zizingatie mabadiliko ya sasa ya kiteknolojia kama vile matumizi ya huduma za kibenki kwa kutumia simu za mikononi, mifuko ya malipo ya Uzeeni na Bima, ambayo ni muhimu kwa kaya za vijijini zinazoingia katika kilimo cha kibiashara; (v) Kuimarisha majukumu ya usimamizi/udhibiti ya Idara ya Ushirika katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji wa Taasisi za Huduma ndogo za kifedha; (vi) Kuharakisha juhudi za kupanua huduma za kifedha katika kilimo kupitia dirisha la kilimo lililopo Benki ya Uwekezaji Tanzania (*TIB*), Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (*AGITF*), kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa ajili ya uwekezaji wa muda mrefu na wakati kwenye uzalishaji na usindikaji katika kilimo; na (vii) Kuhamasisha utoaji wa mikopo kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo kutoka benki za biashara.

324 Katika ASDP II, maeneo ya kipaumbele ya kufanyia kazi kwa ajili ya kupanua ufikivu wa huduma za kifedha vijijini kwa ajili ya wazalishaji wadogo na wana-mageuzi/wasafirishaji nje ya nchi (Wajasiriamali Wadogo na wa Kati -SME/ Wenye Viwanda Vidogo na vya Kati- SMI), ni pamoja na:.

i. **Kuandaa mkakati kabambe wa huduma za kifedha wa vijijini pamoja na** mpango wa utekelezaji kwa ajili ya kuhamasiha uwekezaji wa kibiashara na faida katika uendelezaji wa minyororo ya thamani ya mazao ya kilimo kwa Wadau wote wanaoshiriki.

68 *MIRVAF inalenga uendelevu wa utoaji wa huduma za kifedha kwa ajili ya (i) taasisi zisizo rasmi za kifedha vijijini, SACCOS na taasisi zingine ndogo za kifedha (ii) Wajasiriamali wadogo na wakubwa vijijini*

ii. Kuimarisha Vyama vya Ushirika na vyama vingine vya kiuchumi pamoja na Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*)/ Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACAS*) vinavyohusiana na hivyo (udhibiti wa kijamii kama dhamana) kwa ajili ya kutoa huduma endelevu za kifedha (ndogo) (na zinazomilikiwa na wadau) katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

iii. Kuongeza upatikanaji na ufikivu wa huduma za kifedha katika sekta ya kilimo za muda mfupi hadi za muda wa kati kupitia utaratibu wa Ubia kati ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*), kwa kushirikisha kati ya wengine, Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Mabenki ya Binafsi yanayowekeza katika sekta za maeneo ya vijijini , n.k.

**iv. Kuwezesha wakulima katika uwekezaji wa kilimo** kwa kufanya yafuatayo kati ya mengine: (a) Kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani (*WRS*) ili kuepuka suala la dhamana; (b) Kuimarisha kilimo cha mkataba (makubaliano ya kimkataba kati ya vyama vya wazalishaji, *wafanyabiashara za kilimo*, wasafirishaji nje ya nchi mabenki/na Watoa huduma za kifedha; (c) Kuandaa mfumo wa sera wa kisheria kwa ajili mikataba ya 'kukodisha', huhusan kwa ajili ya kuhamasisha utoaji wa huduma binafsi za matumizi ya zana za kilimo (makubaliano ya kimkataba kati ya waagizaji wa zana, mabenki ya uwekezaji pamoja na watoa huduma binafsi wa zana za kilimo).

**325 Mkakati Kabambe wa Huduma za kifedha Vijijini na Mpango wa Utekelezaji. Kuna fungamano dogo miongoni mwa hatua kadha zilizoasisiwa na sekta ya umma na binafsi** katika kuhamasisha kuwepo kwa utaratibu wa kutoa huduma za kifedha Vijijini, hivyo kusababisha kuwepo kwa haja ya kuandaa, kuimarisha na kutekeleza mkakati unaohusisha wadau mbalimbali ili kukuza uwekezaji katika kilimo. Mikakati kwa ajili ya kuboresha viungo vya huduma za kifedha vijijini inaweza kujumuisha yafuatayo kati ya mengine (i) Kuhamasisha na kuimarisha udhibiti wa sekta yenyewe kupitia mitandao ya Asasi za Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) za Vijijini; (ii) Kuwezesha uunganishwaji wa Asasi za Wakulima (vyama) na Vyama vya Ushirika vya huduma za kifedha, Taasisi za mikopo midogo na/au Mabenki ya Biashara; (iii) Kuongeza uwezo wa wazalishaji wa kujadiliana, wafanyabiashara, vyama vya wasindikaji, vyama na vyama vya ushirika kwa kuwapatia taarifa za zilizoboreshwa za hali ya masoko, ukusanyaji wa pamoja wa mazao na kutumia orodha ya fursa za huduma za kifedha; (iv) Kuimarisha Sekta ya Umma katika majukumu yake ya usimamizi wa sekta ya fedha.

**326 Huduma za kifedha ngazi za chini**[69], kwa lengo la kuzijengea uwezo Taasisi zisizo rasmi za huduma za kifedha na Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) kwa kuziimarisha ili ziwe vyombo endelevu vinavyojitosheleza, kuzisaidia Taasisi za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (*MFIs*) zilizochaguliwa ili ziweze kupanua wigo wa ufikiaji wa Jamii za Vijijini na kusaidia benki za kijamii zilizochaguliwa kama mbadala wa Watoa huduma za kifedha Vijijini. Kipengele kidogo husika pia kinalenga kusaidia Maendeleo ya Ushirika Tanzania kuimarisha utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika. Maeneo ya utekelezaji ni pamoja na kuimarisha utendaji wa kifedha na kiuendeshaji wa Vyama visivyo rasmi ngazi ya chini, Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) na Taasisi zingine za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (*MFIs*) (vyama visivyo rasmi kugeuzwa kuwa Taasisi za Utoaji Huduma ndogo za Fedha katika misingi uendelevu), lakini pia kuimarisha uhusiano wa kiutekelezaji kati ya Taasisi za Utoaji Huduma ndogo za Fedha na Taasisi rasmi za kifedha/mikopo.

**327 Mfumo wa Stakabadhi Ghalani (WRS)**[70] kutumia mazao yaliyoko ghalani kama dhamana ya kuweza kupata mkopo unaowezekana kutoka Taasisi za kifedha zinazoshiriki (*PFIs*).Taasisi za kifedha huweka vigezo kwa waendesha ghala wanaostahili kupata mikopo kwa kuzingatia orodha ya vigezo vya kupimia na vigezo vya rejea ambavyo ni pamoja na: (i) Utawala na muundo wa Uanachama; (ii) Kuwepo kwa Sheria ndogo ndogo, nyaraka za maelekezo na dondoo za mikutano; (iii) Tamko la kifedha ambalo hujumuisha tamko la mapato, matumizi, faida/hasara katika biashara na mizania ya mali na madeni (iv) Mali; (v) Historia ya mikopo; na (vi) Makubaliano ya kimkataba na wanunuzi wa mazao. ASDP II itasadia Taasisi za kifedha zinazoshiriki katika usimamizi wa dhamana ya mazao yaliyohifadhiwa

*69 Angalia pia MIRVAF (IFAD).*
*70 Angalia pia (COWABAMA).*

ghalani, kufanya uchambuzi wa mnyororo wa thamani, usimamizi wa vitisho katika kilimo; na utafiti na uchunguzi wa masoko ili kupunguza vitisho vitokanavyo na kudiriki kufanya shughuli hizo. Kwa ajili ya kuimarisha ufikiwaji wa Taasisi za huduma za kifedha vijijini katika kupata takwimu za fursa za kutoa huduma za kifedha, uchambuzi wa kina wa kifedha utafanyika kwa ajili ya kufahamu mapato halisi kama asilimia ya mapato ghafi, uwezo wa kutumia raslimali kutengeza mapato zaidi kuliko matumizi, na uwezo wa kurejesha mkopo n.k., kwa Wadau wote katika minyororo ya thamani wanaopata msaada na kuandaa nyaraka za maelekezo/kiada na miongozo ya mafunzo kwa ajili ya kutumia njia zilizotumika katika kutambua fursa za kifedha na kuchambua mapendekezo ya maombi ya kupata fursa hizo.

328 Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (*FAO*) kwa kushirikiana mradi wa *Rabobank/NMB Foundation* lina lengo la kujenga uwezo wa usimamizi wa fedha miongoni mwa wazalishaji na Asasi zao, kujenga uhusiano endelevu na watoa huduma za kifedha wa ndani na mawakala wa minyororo wa thamani katika kilimo, na kuboresha mbinu zenye tija. Shirika hilo litaimarisha uhusiano kati ya Asasi za wakulima (*FOs*) na watoa huduma za kifedha, hali ambayo pia itatoa nafasi ya kuandaliwa kwa mkakati wa masoko wa muda mrefu. Vyama vya wakulima wadogo wa mpunga vitarasimishwa na kuwa Vyama vya Ushirika wa Masoko ya Mazao ya Kilimo (*AMCOS*) ili kufikia uwezo wa viwango vinavyohitajika na kupata uwezo wa kujadiliana bei yenye faida, kuimarisha mahusiano ya kibishara kati Asasi za wakulima (*FOs*) na Washiriki wengine katika mnyororo wa thamani wa mchele na kujenga uwezo wa wakulima wadogo wadogo katika kusimamia mikopo na kushiriki katika Mfumo wa Stakabadhi ghalani wa Kitaifa ambao utawawezesha wakopesheke.

329 **Upatikanaji wa Huduma za kifedha za kipindi cha muda mfupi na wa kati** kwa ajili ya kupata pembejeo na uendeshaji wa maghala ambao utasaidia katika uongezaji wa thamani, uboreshaji wa ubora wa nafaka na ukusanyaji mkubwa katika chama/chama cha ushirika wa ujasiriamali cha Mkulima ambao ni kigezo muhimu cha mafanikio. Uboreshaji wa ufikiwaji wa huduma za kifedha Vijijini kwa Washiriki katika mnyororo wa thamani na wakulima kwa kuwanganisha na Taasisi madhubuti za utoaji huduma za kifedha, yakiwemo mabenki ya biashara, lakini pia kuwa na ubia na hatua zilizoasisiwa kwa mipango mingine katika sekta ya huduma za kifedha vijijini[71]. Katika mwaka wa kwanza, Taasisi kadhaa za kifedha zinazoshiriki wa utekelezaji, na tarakibu ya utoaji huduma za kifedha zitabainishwa kwa lengo la kuyakinisha upatikanaji wa huduma za kifedha katika kongani zilizolengwa.

330 Hata hivyo, kutokana na riba kubwa na ukosefu wa dhamana za mikopo, bado imekuwa ni vigumu kwa vikundi vya wakulima na makampuni binafsi kukopa mikopo ya muda wa kati hadi ya muda mrefu kwa ajili ya uwekezaji katika miundombinu / zana. Hii huzuia uwekezaji katika kilimo kwa kiasi kikubwa na hivyo taratibu zinazostahili zinahitajika kuandaliwa. Hata kwa mikopo ya msimu, riba hupunguza sehemu kubwa ya mapato halisi ya nyongeza kutokana na uwekezaji (pembejeo) kutokana na ufanisi mdogo katika ukuaji wa tija. Kwa muktadha huu, ruzuku lengwa (kama vile riba), mifuko maalum ya wakfu na taratibu zingine kama hizo zinahitaji kujadiliwa na wadau wote wa sekta ili kuwezesha ufikiaji endelevu wa huduma za kifedha kwa wadau wa sekta kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo, bila kushindana na mfumo wa kifedha.

**331** **Maeneo** makuu ya utekelezaji na shughuli kwa ajili ya kuboresha uwekezaji endelevu katika vijiji/ kilimo yameandaliwa kwa kifupi katika Jedwali Na. 48.

**Jedwali Na. 48: Shughuli na Maeneo ya Utekelezaji na Kuboresha Uwekezaji Vijiji/Kilimo**

| Maeneo ya utekelezaji | shughuli |
|---|---|
| Kuwa na Mkakati Kabambe wa utoaji huduma za kifedha vijijini na mpango wa utekelezaji | - Kuandaa rasimu na kuimarisha Mkakati kabambe wa kugharamia uwekezaji katika kilimo kwa wadau wote wanaohusika<br>- Kuandaa na kuweka mpango wa utekelezaji kwa ajili uimarishaji wa kutoa na ufikivu wa huduma za kifedha vijijini, ugharamiaji na utaratibu wa utekelezaji wake |

71 *Programu itashirikiana na mipango mingine ya utoaji fedha ili kujenga msingi wa upataji taarifa ambazo zitasaidia katika kuingiza masuala ya fedha katika ngazi tofauti angalia pia shughuli zingine zinazohusiana na Rabobank.*

| Maeneo ya utekelezaji | shughuli |
|---|---|
| Kuimarisha uwezo wa Kitaasisi na Kiufundi wa Wazalishaji wadogo wadogo waliopo na wapya, Asasi na Vyama vya Ushirika vya Wakulima Wafanyabiashara na Wasindikaji, | - Kufundisha na kuimarisha uwezo wa Kitaasisi na Kiufundi wa wa Asasi za Wakulima ili kuimarisha nguvu ya kujadili biashara ya Mzalishaji, Mfanyabiashara na Msindikaji<br>- Kuwezesha uhusiano baina ya Asassi/vyama vya Wakulima na Vyama vya Ushirika vya Huduma za kifedha -Taasisi za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (MFIs)- na/au Mabenki ya Biashara<br>- Kuimarisha udhibiti wa sekta yenyewe (ukaguzi) kupitia mtandao wa Asasi kwa ajili ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) vya Vijijini<br>- Kusaidia uenezaji wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani (WRS) kwa kupanua katika maeneo mapya na kuongeza mazao mapya<br>- Kuhamasisha uhusiano kati ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) na Vyama vya Ushirika wa Masoko ya Mazao ya Kilimo (AMCOS); kutoa mafunzo ya usimamizi wa Asasi za wakulima (FOs) / Vyama vya Ushirika wa Masoko ya Mazao ya Kilimo (AMCOS) na kwa Wajumbe wa Bodi kuhusu utawala bora na usimamizi .<br>- Kusaidia upanuzi wa ufikiaji wa mabenki ya jamii yaliyochaguliwa kama mbadala wa watoa huduma za kifedha vijijini<br>- Kujenga uwezo wa Taasisi zisizo rasmi za huduma za kifedha na Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) ili kuziimarisha ziwe vyombo endelevu vinavyojitosheleza, vinavyosaidia Taasisi za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (MFIs) zilizochaguliwa<br>- Kuboresha utendaji kifedha na uendeshaji wa vyama visivyo rasmi vya ngazi ya chini, Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) na Taasisi zingine za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (MFIs)<br>- Kusaidia Tume ya Maendeleo ya Ushirika ya Tanzania ili kujimarisha |
| Kuongeza upatikanaji na ufikiaji wa huduma za kifedha katika sekta ya kilimo za muda mfupi hadi za muda wa kati | Utoaji wa Msaada wa huduma za kifedha vijijini unaolenga kuongeza ufikivu wa wazalishaji wa vijijini na wajasiriamali kwenye huduma za kifedha zitolewazo na Mabenki ya Biashara, kujaribu mbinu, njia na, huduma mpya katika maeneo ya vijijini kwa manufaa ya kundi lililolengwa, kuboresha mfumo wa Kisheria na Kisera kwa ajili ya huduma ndogo za kifedha za vijijini, na kuhusisha usimamizi wa ujuzi katika programu<br>- Uboreshaji ufikivu wa huduma za kifedha katika misingi endelevu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati wa vijijini (kuongezeka kwa idadi ya wakulima na wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati (SMEs) wanaopata mikopo kutoka taasisi za kifedha) |
| Kuwezesha ufikivu wa wakulima kwenye uwekezaji katika kilimo | - Kuboresha Asasi na Vyama vya Wakulima vya utafutaji wa masoko ya pembejeo na mazao kwa mifumo ya habari, ukusanyaji wa mazao na matumizi ya fursa za kupata huduma za kifedha kwa kutumia mali kama dhamana (*inventory financing*)<br>- Kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani (WRS) ili kuachana na suala la dhamana<br>- Kueneza na kuimarisha kilimo cha mkataba kadri inavyofaa (mkataba wa makubaliano baina ya Asasi za wazalishaji, wafanyabiashara katika kilimo, Wasafirishaji nje na Taasisi za kifedha)<br>- Kubuni mipango ambayo itawawezesha Wazalishaji wadogo wadogo kupata huduma za Mikopo ya kifedha inayopatikana kupitia minyororo ya thamani katika kilimo (kwa kuanza na mafunzo waliyojifunza katika mipango inayoendelea)<br>- Kuanzisha mifumo ya Kisheria na sera ya mikataba ya 'kukodisha', huhusan kwa ajili ya kuhamasisha utoaji wa huduma binafsi za matumizi ya zana za kilimo (makubaliano ya kimkataba kati ya waagizaji wa zana, mabenki ya uwekezaji pamoja na watoa huduma binafsi wa zana za kilimo) |

**332 Utekelezaji.** Tume ya Maendeleo ya Ushirika ya Tanzania chini ya Wizara ya Kilimo inapaswa kuchukua jukumu la kuongoza katika kuandaa mikakati na hatua za kipaumbele kwa kushirikiana kwa karibu na wadau wote wa sekta, ikiwa ni pamoja na Idara za Sera na Mipango za Wizara za Sekta ya Kilimo (ASLMs); Idara zenye dhamana ya uendelezaji wa mazao, mifugo na uvuvi katika Wizara husika; Idara ya Masoko (Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji), Wizara ya Fedha na Mipango; Asasi za wakulima (FOs); Taasisi za Utoaji Huduma ndogo za Fedha (MFIs) na benki binafsi na Washirika wa Maendeleo.

**Muhtasari wa uwekezaji kwa Eneo Kuu la 4.**

**Jedwali Na. 49: bajeti ya maendeleo/makadirio ya uwekezaji kwa miaka mitano kwenye Eneo Kuu la 4 (TSh milioni)**

| ENEO KUU LA 4: KUIMARISHA UWEZESHAJI WA SEKTA –MAKADIRIO YA GHARAMA KWA KUTUMIA BEI ZA MWAKA 2016 ( (Shilingi za Kitanzania) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli zinazogharamiwa** | **mwaka 1** | **mwaka 2** | **mwaka 3** | **mwaka 4** | **mwaka 5** | **Jumla** |
| 4.1.1.1 Kupitia na kuhuisha sera zinazohusiana na sekta ya kilimo na mfumo wa usimamizi wa mazingira bora ya biashara | 310 | 967 | 352 | 387 | 426 | 2442 |
| 4.1.1.2 Kuimarisha Ufuatiliaji, Udhibiti na uchunguzi ili kukabiliana na Uvuvi haramu, (IUU) | 6,019 | 2,023 | 1,647 | 1,685 | 1,847 | 13221 |
| 4.1.1.4 Kuimarisha na kudhibiti ajira za watoto katika Kilimo | 1,585 | 1,050 | 1,094 | 808 | 684 | 5221 |
| 4.1.1.5 Kuhamasisha kazi zenye staha, afya kazini na usalama katika sekta ya kilimo | 587 | 933 | 427 | - | - | 1947 |
| 4.2.1.1 Kuimarisha Ushirika, Asasi za wakulima na vyama vya wahusika wengine katika mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo | 4,014 | 3,742 | 2,299 | 2,116 | 1,195 | 13366 |
| 4.2.2. Kuboresha unufaikaji wa wanawake na vijana katika mnyororo wa thamani wa bidhaa za kilimo mifugo na uvuvi (WAYA) | 3,025 | 3,238 | 2,779 | 852 | 930 | 10824 |
| 4.3.1.1 1 Kuimarisha mifumo ya kitaasisi katika sekta ya kilimo kwa kuboresha uratibu na mawasiliano ngazi zote | 6,872 | 6,673 | 4,280 | 2,115 | 2,197 | 22137 |
| 4.4.1.1 Kujenga uwezo na kuunganisha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za sekta ya kilimo na mifumo ya usimamizi wa takwimu (m.f ARDS, NSCA, AASS) ili kupata matokeo mazuri yanayotokana na usimamizi katika ngazi zote. | 4,425 | 6,998 | 2,879 | 2,591 | 2,196 | 19089 |
| 4.4.2.1 Kuimarisha na kuunganisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya sekta ya kilimo kwa ufanisi na uthabiti wa uwajibikaji katika ngazi zote. | 11,333 | 3,209 | 1,597 | 1,294 | 1,123 | 18556 |
| 4.5.1.1 Kuboresha uwezo katika ngazi ya Taifa, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (idadi na ubora) kwa ngazi zote | 3,429 | 6,350 | 3,781 | 2,501 | 1,142 | 17203 |
| 4.5.2.1 Kuanzisha usimamizi jumuishi wa uendelezaji wa maarifa na mfumo wa TEHAMA katika ngazi zote. | 3,047 | 2,377 | 336 | 213 | 400 | 6373 |

| ENEO KUU LA 4: KUIMARISHA UWEZESHAJI WA SEKTA –MAKADIRIO YA GHARAMA KWA KUTUMIA BEI ZA MWAKA 2016 ( (Shilingi za Kitanzania) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli zinazogharamiwa** | **mwaka 1** | **mwaka 2** | **mwaka 3** | **mwaka 4** | **mwaka 5** | **Jumla** |
| 4.6.1.1 Upatikanaji wa fedha za kugharamia kilimo kwa ajili ya kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi | 1,481 | 1,833 | 1,600 | 1,514 | 639 | 7067 |
| **Jumla ya ENEO KUU LA 4** | **46,127** | **39,393** | **23,071** | **16,076** | **12,779** | **137,446** |

## V. GHARAMA, UGHARAMIAJI NA USIMAMIZI WA FEDHA ZA PROGRAMU

### A. Gharama za Programu kwa ujumla

333 Kwa kuzingatia misingi ya bajeti na maendeleo kwa kila eneo kuu la ASDP II, gharama za uwekezaji zimekadiliwa (Jedwali Na.50). Takwimu katika Jedwali Na.50 linaonesha kuwa gharama za ASDP II zinakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 13, 819 (Dola za Kimarekani milioni 5,979) ambapo makisio ya gharama za uwekezaji kwa mwaka ni wastani wa Shilingi bilioni 2,284 (Dola za Kimarekani,milioni 988) hadi bilioni 3,238 (Dola za Kimarekani milioni 1,400) katika kipindi cha miaka 5. Hata hivyo, gharama za ruzuku ya NFRA na ruzuku ya pembejeo hazikujumuishwa.

334 Eneo Kuu 1: Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Maji na Ardhi inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 2,024 (Dola za Kimarekani milioni 941) ambapo kiasi kikubwa cha bajeti hii kimetengwa kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Eneo la 1 limetengewa asilimia 15 ya gharama zote za Programu. Gharama za Eneo la 2: Kuongeza Tija katika kilimo inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 8,081 (Dola za Kimarekani milioni 3,758) au asilimia 58 ya gharama zote za Programu . Eneo la 3: Biashara na Uongezaji Thamani kwenye mazao (ikiwemo uwekezaji ili kuhamasisha uendelezaji wa kipaumbele katika mnyororo wa thamani) inakadiriwa kugharimu Shilingi bilioni 1,483 (Dola za Kimarekani milioni 1,663) au asilimia 26 ya gharama zote za Programu. Aidha, gharama ya Eneo la 4: Kuweka mazingira wezeshi ya kisera, sheria na taratibu ili kuvutia mazingira ya kibiashara, uratibu ,ufuatiliaji na tathmmini inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 137 (Dola za Kimarekani milioni 67), au asilimia moja (1%) ya gharama zote za Programu. MaJedwali Na. 50 na 51 yanaonyesha makisio ya gharama ya fedha za uwekezaji na asilimia.

**Jedwali Na. 50: Mahitaji ya Bajeti ya ASDP II kwa kila eneo kuu na Asilimia kwa miaka mitano ya kwanza**

| Eneo | | Makisio ya bajeti | % |
|---|---|---|---|
| **Eneo Kuu 1** | Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Maji na Ardhi | **2,024,646,012,085** | **15%** |
| **Eneo Kuu 2** | Kuongeza tija na faida katika kilimo,mifugo na uvuvi | **8,081,495,303,009** | **58%** |
| **Eneo Kuu 3** | Biashara na Uongezaji Thamani kwenye mazao | **3,575,493,642,854** | **26%** |
| **Eneo Kuu 4** | Kuweka mazingira weeshi ya kisera, sheria na taratibu ili kuvutia mazingira ya kibiashara, uratibu ,ufuatiliaji na tathmmini | **137,442,668,522** | **1%** |

**Jedwali Na. 51: Bajeti ya Maendeleo ya ASDP II kwa Ujumla**

| MAKADIRIO YA BAJETI YA ASDP II kwa kutumia Bei ya mwaka 2016 (Shilingi za Kitanzania Milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli** | **Mwaka 1** | **Mwaka 2** | **Mwaka 3** | **Mwaka 4** | **Mwaka 5** | **Jumla** |
| **Eneo Kuu 1:** Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Maji na Ardhi | | | | | | |
| 1.1.1.1 Mpango jumuishi wa matumizi na usimamizi wa ardhi kwa ajili ya utatuzi wa migogoro ,uzalishaji endelevu katika sekta ya kilimo na maendeleo ya viwanda (bidhaaa zote/ kanda zote) | 29,759 | 31,014 | 34,532 | 0 | 0 | 95,305 |
| 1.1.1.2 Kuimarisha uzalishaji wa malisho na uhifadhi kwa ajili ya uzalishaji endelevu na tija ya mifugo | 14,132 | 14,517 | 13,715 | 13,501 | 16,284 | 72,149 |
| 1.1.1. 3 Kuongeza upatikanaji wa ardhi ya kilimo kwa ajili ya kuwawezesha vijana | 4,464 | 4,150 | 5,753 | 4,534 | 6,321 | 25,222 |
| 1.1.1.4 Kuboresha uratibu na usimamizi wa mfumo wa ufuatiliaji wa mbwawa ya maji *(watershed)* kwa ajili ya matumizi endelevu ya rasilimali. (Bidhaa zote). | - | 1,366 | 928 | 839 | 916 | 4,049 |
| 1.2.1.1 Kukarabati na kujenga miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji na tija | 16,370 | 184,589 | 172,338 | 175,278 | 189,619 | 738,194 |
| 1.2.1.2 Uendelezaji wa mifumo midogo ya umwagiliaji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na tija. | 5,873 | 50,129 | 57,162 | 59,915 | 65,430 | 238,509 |
| 1.2.2.1 Kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji. | 1,823 | 1,652 | 2,250 | 1,787 | 2,592 | 10,104 |
| 1.2.3.1 Kuendeleza miundombinu ya maji kwa ajili ya kuongeza tija na uzalishaji wa mifugo | 2,856 | 66,582 | 77,456 | 76,103 | 85,464 | 308,461 |
| 1.2.3.2 Kuhamasisha na kujenga vituo jumuishi vya kisasa vya maji kwa ajili ya mazao, mifugo na uvuvi | 42,069 | 79,875 | 111,447 | 158,157 | 88,773 | 480,321 |

| MAKADIRIO YA BAJETI YA ASDP II kwa kutumia Bei ya mwaka 2016 (Shilingi za Kitanzania Milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli** | **Mwaka 1** | **Mwaka 2** | **Mwaka 3** | **Mwaka 4** | **Mwaka 5** | **Jumla** |
| 1.3.1.1 Kuendeleza na kuhamasisha teknolojia za kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi na hifadhi ya mazingira.. | 1,905 | 13,984 | 8,745 | 6,345 | 10,445 | 41,424 |
| 1.3.1. Kuhamasisha matumizi ya mfumo wa ikolojia katika usimamizi wa uvuvi na ufugaji wa samaki | 1,090 | 1,045 | 1,730 | 795 | 1,329 | 5,989 |
| 1.3.1.3 Kuimarisha mfumo madhubuti wa kutoa tahadhari mapema katika sekta ya kilimo na maandalizi ya tahadhari | 1,960 | 1,052 | 1,009 | 396 | 501 | 4,918 |
| **Jumla ndogo** | **122,301** | **449,955** | **487,065** | **497,648** | **467,674** | **2,024,643** |
| **Eneo Kuu 2:** Kuongeza tija na faida katika kilimo,mifugo na uvuvi | | | | | | |
| 2.1.1.1 Kuimarisha na kuhamasisha upatikanaji wa huduma za ugani katika sekta ya kilimo (bidhaa zote) | 1,311,913 | 772,652 | 849,529 | 838,081 | 921,148 | 4,693,323 |
| 2.1.1.2 Kuimarisha na kuhamasisha mafunzo yanayolenga ujuzi unaohitajika katika kilimo, mifugo na uvuvi (bidhaa zote) | 4,373 | 9,720 | 9,349 | 8,506 | 9,222 | 41,170 |
| 2.2.1.1 Kuboresha upatikanaji na ufikiwaji wa pembejeo bora kwa bei nafuu ili kuongeza tija na faida (mazao zote) | 149,389 | 136,695 | 150,284 | 164,670 | 181,057 | 782,095 |
| 2.2.1.2 Kuboresha ufikiwaji na upatikanaji wa pembejeo bora za kuku | 4,176 | 2,652 | 2,800 | 2,962 | 3,141 | 15,731 |
| 2.2.1.3 Kuendeleza uvuvi wa jodari kwa kununua meli ili kuongeza uzalishaji | 1,664 | 93,408 | 768 | 1,099 | 987 | 97,926 |
| 2.2.1.4 Kuimarisha na kuanzisha maeneo ya kutia nanga kwa ajili kuongeza faida katika uvuvi | 1,146 | 4,533 | 5,008 | 4,246 | 4,639 | 19,572 |

| MAKADIRIO YA BAJETI YA ASDP II kwa kutumia Bei ya mwaka 2016 (Shilingi za Kitanzania Milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli** | **Mwaka 1** | **Mwaka 2** | **Mwaka 3** | **Mwaka 4** | **Mwaka 5** | **Jumla** |
| 2.2.1.5 Kujenga bandari ya uvuvi ili kuongeza faida katika uvuaji wa samaki | 4,115 | 5,176 | 7,350 | 4,460 | 2,090 | 23,191 |
| 2.2.1.6 Kuboresha uvuvi mdogo ili kuongeza uzalishaji wa samaki na tija | 55,090 | 50,853 | 48,517 | 6,658 | 4,388 | 165,506 |
| 2.2.1.7 Kuimarisha vitengo vya usimamizi wa fukwe (BMUs) kwa ajili ya usimamizi endelevu, kulinda na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi | 2,537 | 2,134 | 2,199 | 2,147 | 2,319 | 11,336 |
| 2.2.1.8 Uboreshaji wa huduma za afya ya mimea | 13,322 | 11,191 | 7,608 | 1,389 | 478 | 33,988 |
| 2.2.1.9 Uzalishaji wa chanjo na madawa | 44,570 | 36,191 | 39,700 | 3,705 | 4,380 | 128,546 |
| 2.2.1.10a Uboreshaji wa huduma za afya ya mifugo | 262,550 | 295,128 | 332,216 | 371,559 | 420,078 | 1,681,531 |
| 2.2.1.10b Uboreshaji wa huduma za afya za samaki | 1,518 | 1,238 | 1,241 | 1,340 | 1,395 | 6,732 |
| 2.3.1.1 Kuimarisha uwezo wa utafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi kwa ajili ya kuendeleza teknolojia, kama chombo muhimu cha viwanda na kusambaza matokeo ya utafiti (sekta zote ndogo) | 7,559 | 29,197 | 29,504 | 8,708 | 9,516 | 84,484 |
| 2.3.2.1 Kuendeleza na kusambaza teknolojia unganifu kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na tija (bidhaa zote) | 12,409 | 16,384 | 11,616 | 11,110 | 11,371 | 62,890 |

| MAKADIRIO YA BAJETI YA ASDP II kwa kutumia Bei za mwaka 2016 (TSh. Milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Eneo la gharama** | **mwaka 1** | **mwaka 2** | **mwaka 3** | **mwaka 4** | **mwaka 5** | **Jumla** |
| 2.3.2.2 Kuendeleza na Kuimarisha uwezo wa vinasaba vya mifugo kupitia teknolojia ya kisasa ya uzalishaji | 4,833 | 3,895 | 2,683 | 2,738 | 3,011 | 17,160 |

| MAKADIRIO YA BAJETI YA ASDP II kwa kutumia Bei za mwaka 2016 (TSh. Milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Eneo la gharama** | **mwaka 1** | **mwaka 2** | **mwaka 3** | **mwaka 4** | **mwaka 5** | **Jumla** |
| 2.4.1.1 Kuimarisha na kuendeleza matumizi ya zana za kisasa za kilimo kuboresha mnyororo wa thamani | 9,250 | 5,753 | 5,699 | 5,707 | 5,717 | 32,126 |
| 2.5.1.1 Kuboresha upatikanaji, ubora, ufikiwaji na matumizi ya vyakula vyenye virutubisho muhimu (bidhaa zote) | 14,153 | 11,722 | 12,960 | 14,297 | 10,394 | 63,526 |
| 2.5.1.2 Kuongeza na kuhamasisha uzalishaji wa mtama na ulezi kwa ajili ya matumizi ya chakula | 20,538 | 22,167 | 23,955 | 25,921 | 28,084 | 120,665 |
| **Jumla ndogo** | **1,925,105** | **1,510,689** | **1,542,986** | **1,479,303** | **1,623,415** | **8,081,498** |
| Eneo kuu la 3: Biashara na Uongezaji Thamani kwenye Mazao | | | | | | |
| 3.1.1.1 Kuboresha na kuendeleza miundombinu ya masoko ili kuyafikia masoko ya ndani na nje | 98,346 | 456,728 | 568,733 | 635,561 | 684,371 | 2,443,739 |
| 3.1.2.1 Kuboresha na kuendeleza miundombinu ya masoko ya mifugo na samaki ili kuongeza mapato ya ndani na kupanua masoko | 7,847 | 9,466 | 156,458 | 171,750 | 368,188 | 713,709 |
| 3.1.2.2Kuboresha upatikanaji wa masoko ya kuku wa kienyeji na kisasa | 743 | 2,068 | 2,248 | 369 | 282 | 5,710 |
| 3.1.2.3 Kuimarisha mfumo wa kufuatilika wa mifugo na uvuvi (utambulisho) ili kuhamasisha biashara na uuzaji | 1,834 | 738 | 733 | 643 | 630 | 4,578 |
| 3.1.2.4 Kuhamasisha na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika mnyororo wa thamani wa bidhaa | 1,239 | 4,073 | 4,376 | 1,442 | 13,999 | 25,129 |
| 3.2.1.1 Kuimarisha na kuendeleza viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuziongezea thamani bidhaa zote za kipaumbele | 10,333 | 14,448 | 15,432 | 16,806 | 18,522 | 75,541 |
| 3.2.1.2 Kuboresha mnyororo wa thamani wa maziwa | 8,886 | 8,536 | 8,014 | 4,213 | 4,571 | 34,220 |

| MAKADIRIO YA BAJETI YA ASDP II kwa kutumia Bei za mwaka 2016 (TSh. Milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Eneo la gharama** | **mwaka 1** | **mwaka 2** | **mwaka 3** | **mwaka 4** | **mwaka 5** | **Jumla** |
| 3.2.1.3 Kuimarisha mnyororo wa thamani wa ngozi za mifugo wa dogo na wakubwa | 13,915 | 10,119 | 19,594 | 5,972 | 5,307 | 54,907 |

| MAKADIRIO YA BAJETI YA ASDP II kwa kutumia Bei ya mwaka 2016 (Shilingi za Kitanzania Milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli** | **Mwaka 1** | **Mwaka 2** | **Mwaka 3** | **Mwaka 4** | **Mwaka 5** | **Jumla** |
| 3.2.1.4 Kuimarisha mnyororo wa thamani kwa bidhaa za kilimo cha bustani | 4,995 | 1,622 | 4,127 | 1,274 | 1,387 | 13,405 |
| 3.2.1.5 Kuendeleza na kujenga maghala ya kimkakati yatakayo unganishwa na soko la bidhaa | 26,328 | 21,012 | 22,695 | 24,805 | 27,302 | 122,142 |
| 3.2.1.6 Kuendeleza na kuimarisha uongezaji wa thamani katika bidhaa za kipaumbele zitokanazo na uvuvi na ufugaji wa samaki | 5,758 | 6,752 | 7,267 | 7,868 | 8,432 | 36,077 |
| 3.2.1.7 Kuongeza thamani katika nyama ya ngo'mbe, mbuzi na kondoo | 9,633 | 12,739 | 3,507 | 505 | 226 | 26,610 |
| 3.2.1.8 Kuimarisha usimamizi wa mazao ya chakula katika mnyororo mzima wa usambazaji ili kuwa na upatikanaji/ usalama wa chakula na lishe endelevu | 1,088 | 2,710 | 12,534 | 2,324 | 1,080 | 19,736 |
| **Jumla ndogo** | **190,945** | **551,009** | **825,718** | **873,532** | **1,134,297** | **3,575,501** |
| Eneo kuu la 4: Kuweka mazingira wezeshi ya sera, sheria na taratibu ili kuvutia mazingira ya kibiashara, uratibu, ufuatiliaji na tathmini | | | | | | |
| 4.1.1.1 Kupitia na kuoanisha sera zinazohusiana na kilimo pamoja na mifumo ya usimamizi ili kuboresha mazingira ya biashara | 310 | 967 | 352 | 387 | 426 | 2,442 |
| 4.1.1.2 Kuimarisha ufuatiliaji, usimamizi na uchunguzi (MCS) ili kukabiliana na uvuvi haramu, usiotolewa taarifa na usiofuata taratibu (IUU uvuvi) | 6,019 | 2,023 | 1,647 | 1,685 | 1,847 | 13,221 |
| 4.1.1.4 Kuimarisha na kudhibiti ajira za watoto katika Kilimo | 1,585 | 1,050 | 1,094 | 808 | 684 | 5,221 |

| MAKADIRIO YA BAJETI YA ASDP II kwa kutumia Bei ya mwaka 2016 (Shilingi za Kitanzania Milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli** | **Mwaka 1** | **Mwaka 2** | **Mwaka 3** | **Mwaka 4** | **Mwaka 5** | **Jumla** |
| 4.1.1.5 Kuhamasisha upatikanaji wa kazi zenye staha, usalama na afya makazini katika sekta ya kilimo | 587 | 933 | 427 | - | - | 1,947 |
| 4.2.1.1 Kuimarisha vyama vya ushirika, mashirika ya wakulima na vyama vya wadau wengine katika mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo | 4,014 | 3,742 | 2,299 | 2,116 | 1,195 | 13,366 |
| 4.2.2.1 Kuendeleza unufaikaji wa wanawake na vijana katika mnyororo wa thamani wa bidhaa za kilimo (WAYA) | 3,025 | 3,238 | 2,779 | 852 | 930 | 10,824 |

| MAKADIRIO YA BAJETI YA ASDP II kwa kutumia Bei ya mwaka 2016 (Shilingi za Kitanzania. Milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli** | **mwaka 1** | **mwaka 2** | **mwaka 3** | **mwaka 4** | **mwaka 5** | **Jumla** |
| 4.3.1. Kuimarisha mifumo ya kitaasisi ya sekta ya kilimo kwa ajili ya kuboresha uratibu na mawasiliano ya wima na mshazari *(vertical and horizontal)* | 6,872 | 6,673 | 4,280 | 2,115 | 2,197 | 22,137 |
| 4.4.1.1 Kujenga uwezo na kuwa na mifumo jumuishi ya ukusanyaji na usimamizi wa takwimu ( kwa mfano ARDS, NSCA, AASS) ili kuboresha matokeo ya usimamizi katika ngazi zote | 4,425 | 6,998 | 2,879 | 2,591 | 2,196 | 19,089 |
| 4.4.2.1 Kuimarisha na kuunganisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini katika sekta ya kilimo ili kuongeza ufanisi na tija ya uwajibikaji katika ngazi zote. | 11,333 | 3,209 | 1,597 | 1,294 | 1,123 | 18,556 |
| 4.5.1.1 Kuboresha uwezo katika ngazi ya Kitaifa, RS na Halmashauri (idadi na ubora) | 3,429 | 6,350 | 3,781 | 2,501 | 1,142 | 17,203 |
| 4.5.2.1 Kuandaa mfumo jumuishi wa usimamiaji /utumiaji wa maarifa na TEHAMA katika ngazi zote | 3,047 | 2,377 | 336 | 213 | 400 | 6,373 |

| MAKADIRIO YA BAJETI YA ASDP II kwa kutumia Bei ya mwaka 2016 (Shilingi za Kitanzania. Milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli** | **mwaka 1** | **mwaka 2** | **mwaka 3** | **mwaka 4** | **mwaka 5** | **Jumla** |
| 4.6.1.1 Upatikanaji wa fedha za kilimo kwa ajili ya mnyororo wa thamani wa bidhaa ulioboreshwa | 1,481 | 1,833 | 1,600 | 1,514 | 639 | 7,067 |
| **Jumla ndogo** | ***46,127*** | ***39,393*** | ***23,071*** | ***16,076*** | ***12,779*** | ***137,446*** |
| **Jumla kuu katika Shilingi za Kitanzania. (milioni)** | 2,284,478 | 2,551,046 | 2,878,840 | 2,866,561 | 3,238,165 | 13,819,090 |
| **Jumla kuu katika Dola za Kimarekani (milioni)** | **988.4** | **1,103.70** | **1,245.50** | **1,240.20** | **1,400.90** | **5,979** |

## B. Mpango wa Ugharamiaji

335 Kwa upande wa ugharamiaji wa bajeti ya ASDP II, vyanzo vikuu vya fedha vitakuwa ni pamoja na bajeti ya Serikali, washirika wa maendeleo na wadau wengine kama vile sekta binafsi, taasisi zisizo za kiserikali na wakulima, wafugaji na wavuvi. Kwa kila eneo dogo la Programu, kiwango cha uwiano cha bajeti ambacho mfadhili husika atatoa kimetumika katika kuandaa rasimu ya mpango wa ugharamiaji wa ASDP II. Kiasi cha fedha cha bajeti ya maendeleo na vyanzo mbalimbali vya fedha ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 52.

**Jedwali Na. 52: Makadirio ya bajeti kwa ajili ya ASDP II kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha**

| MAKADIRIO YA MICHANGO KWA AJILI YA ASDP II – Kiasi kutoka vyanzo mbalimbali kwa asilimia (%) | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Eneo la Gharama** | **Serikali** | **Washirika wa Maendeleo** | **Washirika wa Maendeleo** | **Sekta binafsi/ Wakulima** | **Jumla (%)** | **Kiasi cha uwekezaji** | |
| | **A** | | | | | | |
| | | **Fedha zilizo ndani ya bajeti** | **Fedha zilizo nje ya Bajeti** | | | **Kitaifa** | **h/ shauri** |
| Eneo la 1: Usimamizi endelevu wa matumizi ya maji na ardhi | 15 | 60 | 16 | 10 | 100 | 27 | 73 |
| Eneo la 2: Kuongeza Tija na Faida katika kilimo,mifugo na uvuvi | 51 | 29 | 15 | 5 | 100 | 31 | 69 |
| Eneo la 3: Kuboresha Biashara, Kuongeza Thamani kwenye mazao | 33 | 40 | 22 | 5 | 100 | 31 | 69 |
| Eneo la 4: Kuweka mazingira wezeshi ya sera, sheria na taratibu ili kuvutia mazingira ya kibiashara, uratibu ,ufuatiliaji na tathmini | 51 | 23 | 25 | 1 | 100 | 52 | 48 |

[a] Serikali ni katika ngazi ya Kitaifa na Halmashauri (LGA)

336 Kutokana na dhana ya hapo juu, misingi na bajeti yote ya maendeleo ya ASDP II na wachangiaji kwa muhtasari inaonekana katika Jedwali Na.53. Uchambuzi unaonesha kuwa Serikali pamoja na washirika wa maendeleo itatoa kiasi cha asilimia 41 ya fedha za Programu, wakati sekta binafsi na wadau wengine watachangia asilimia 59.

**Jedwali Na. 53: Ufafanuzi wa mpango wa kuchangia fedha kwa ajili ya ASDP-II (Muhtasari wa gharama zote katika Shilingi za Kitanzania. Milioni)**

| Eneo la gharama | Serikali | Washirika wa maendeleo | | Wanufaikaji | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ndani ya bajeti | Nje ya bajeti | Sekta binafsi/ Wakulima | |
| **Eneo la 1: Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Maji na Ardhi** | ***302,067*** | ***1,205,008*** | ***316,732*** | ***200,835*** | ***2,024,643*** |
| **Eneo la 2: Kuongeza Tija na Faida katika Kilimo, Mifugo na Uvuvi** | 4,096,501 | 2,368,697 | 1,212,225 | 404,075 | 8,081,498 |
| **Eneo la 3: Biashara na Kuongeza Thamani ya mazao** | ***1,197,203*** | ***1,419,823*** | ***779,701*** | ***178,774*** | ***3,575,501*** |
| **Eneo la 4: Kuweka Mazingira wezeshi ya sera, Sheria na Taratibu ili kuvutia mazingira ya kibiashara, uratibu ,ufuatiliaji na tathmini** | 70,028 | 32,278 | 33,775 | 1,364 | 137,446 |
| Jumla ya gharama katika Shilingi za Kitanzania milioni **(matumizi ya dharura yamejumishwa)** | ***5,665,800*** | ***5,025,806*** | ***2,342,434*** | ***785,048*** | ***13,819,088*** |
| Jumla ya gharama katika Dola za Kimarekani (milioni) **(matumizi ya dharura yamejumishwa)** | 2,451 | 2,174 | 1,013 | 340 | 5,979 |
| % | 41% | 36% | 17% | 6% | ***100%*** |

## C. Utaratibu wa ugharamiaji wa Programu

337 Chini ya ASDP-I uchangiaji wa fedha za Programu ulifanyika kupitia Mfuko wa Pamoja. Taasisi zilizowajibika katika utekelezaji wa Programu ngazi ya kitaifa zilikuwa ni Wizara ya Kilimo na Chakula (MAFC), Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi (MLFD) na Wizara ya Biashara na Viwanda (MIT). Utekelezaji katika ngazi za Mikoa na Halmashauri uliratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI. Aidha, uratibu wa shughuli za Mfuko wa Pamoja ulikuwa unafanyika kupitia Kamati ya Uendeshaji wa Mfuko, ambayo wajumbe wake walikuwa ni Makatibu Wakuu wa Wizara za Sekta ya Kilimo, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Fedha na wawakilishi wa washirika wa maendeleo waliokuwa wanachangia katika Mfuko.

338 Mfumo wa Mfuko wa Pamoja ni tofauti na ule uliozoeleka wa kuanzisha akaunti ya mradi ambayo fedha zake zinazowekwa husimamiwa na kitengo cha utekelezaji wa mradi Utaratibu wa uchangiaji wa fedha za ASDP-1ulikuwa umehuishwa kikamilifu katika miundo ya kifedha iliyopo serikalini, ambayo ni pamoja na kupanga, kuandaa bajeti, kufanya mahesabu, kutoa taarifa na huduma za ukaguzi.

339 Kamati ya simamizi na maamuzi ya ASDP II (ASC) itapitia mipango kazi na bajeti ya ASDP itakayowasilishwa na Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi (TCD) kwa ajili ya kuridhia na kuidhinisha matumizi. Kamati ya Uendeshaji pia itapitisha mipango na bajeti ya ASDP II. Upelekaji wa fedha kwenda mkoani kwa ajili ya shughuli za Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri utafanyika kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa (RAS), na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya (DED). Fedha kutoka Mfuko wa Pamoja ambao utakuwa na akaunti yake Benki Kuu ya Tanzania kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina ambao utatumika kutuma fedha kwenda Wizara za Sekta ya Kilimo (ASLMs), Secretariati za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Wahasibu Wakuu wa Wizara zinazohusika wana wajibu wa kuhakikisha kuwa fedha zinazotumwa zinasimamiwa ipasavyo ili kutekeleza shughuli za Programu kama inavyotakiwa kulingana na viwango vya kimataifa na makubaliano yaliyofikiwa kati ya Serikali na washirika wa maendeleo.

340 Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi (TCD) ina jukumu la: (i) kuwezesha michango ya Serikali na washirika wa maendeleo kwa ajili ya shughuli za ASDPII zilizoidhinishwa kabla ya mwaka husika wa bajeti kupitishwa; (ii) kuidhinisha uhamishaji wa rasilimali na matumizi ya fedha za Mfuko kulingana na taarifa zilizohakikiwa za kiufundi na kifedha za Wizara za Sekta ya Kilimo; (iii) Kutoa maagizo

ya kisera kuhusu upelekaji na matumizi ya fedha za Mfuko wa Pamoja ; na (iv) kuzitambua Serikali za Mitaa ambazo zinastahili kupata ruzuku ya maendeleo na kukubaliana na mabadiliko ya kanuni ya mgao wa Halmashauri. Aidha, TCD ina wajibu wa kufanya maamuzi juu ya masuala ya kifedha yanayozihusu Halmashauri.

341 Katika ngazi ya Serikali za mitaa, fedha za ASDP II zitagharamia utekelezaji wa shughuli zilizopitishwa na kamati ya ASC. Fedha za shughuli maalum kama vile za kujenga uwezo, huduma za ugani na Umwagiliaji za Wilaya zilizoidhinishwa na ASC kupitia mapendekezo ya Wakurugenzi. Fedha hizo za ruzuku zinaingizwa katika utaratibu wa mipango ya fedha inayotumiwa na LGDG na zinatumika kutekeleza mpango wa kilimo wa wilaya (DADP). Mtiririko wa fedha katika ASDP II umeonyeshwa katika **Kielelezo Na. 22.**

**Kielelezo Na. 22: Mfumo wa utoaji Fedha kwa ajili ya ASDP II**




342 Aidha, pamoja na kuwa na Mfuko wa Pamoja wa ASDP II, miradi ya sekta ya kilimo inaweza kufadhiliwa moja kwa moja kupitia fedha za miradi hiyo zinazopitia katika mfumo wa bajeti ya Serikali. Kadhalika, miradi inaweza kufadhiliwa moja kwa moja na washirika wa maendeleo kwa fedha iliyo nje ya bajeti ya Serikali. Hata hivyo, ufadhili wa fedha nje ya bajeti ya serikali hauonyeshwi katika akaunti ya matumizi ya Serikali kwa ajili ya sekta ya kilimo.

343 Kuhusu ugharamiaji wa shughuli za ASDP II, Serikali inapenda kuendelea na utaratibu wa kuchangia kwenye Mfuko wa Pamoja ulioanzishwa chini ya ASDP-1. Huu ni utaratibu jumuishi na wenye manufaa katika utekelezaji wa Programu kabambe ya kuendeleza sekta ya kilimo, kama vile ASDP II. Utaratibu huo pia unazuia mfumo wa kugawanya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi tofauti inayofadhiliwa na aina mbalimbali ya washirika wa maendeleo. Pia hupunguza gharama za uendeshaji.

344 Mtiririko wa fedha na utaratibu wa utoaji wa fedha kwa miradi ya pamoja (JPs) / sekta ya umma na binafsi (PPPs) na kati ya sekta ya umma na binafsi wanakubaliana wakati wa utiaji saini wa mkataba na Makubaliano ya Maelewano (MOU) kati ya pande zinazohusika katika mradi huo. Ni muhimu kwamba fedha zote (bajeti ya Serikali, fedha za Mfuko wa Pamoja na zile za kupeleka fedha moja kwa

moja katika mradi) ambazo zinasaidia utekelezaji wa ASDP II zijumuishwe wakati wa mchakato wa kupanga na kutekeleza bajeti.

345 Utekelezaji wa ASDP-1 ulionesha kuwa utaratibu wa Mfuko wa Pamoja ulikuwa na ufanisi katika utekelezaji wa mfumo wa kutoa ruzuku kwa Serikali za Mitaa (Ruzuku ya huduma za ugani za kilimo, ruzuku ya kujenga uwezo na ruzuku ya uwekezaji) ambazo ziliwezesha utoaji wa huduma za sekta ya umma na uwekezaji katika halmashauri kwa kutumia utaratibu wa kanuni. Kwa sababu hiyo, Serikali inapendelea kuendelea na utaratibu wa kutumia Mfuko wa Pamoja ili kuhakikisha kuwa utoaji wa huduma bora (ugani na utafiti) na utekelezaji wa mfumo wa kongani chini ya ASDP II ambao unalenga kuendeleza utekelezaji wa mnyororo wa thamani wa bidhaa za kipaumbele katika ngazi ya kanda.

346 Katika hali ambayo itajitokeza kuwa sera za nchi wanakotoka washirika wa maendeleo haziruhusu kuchangia katika Mfuko wa Pamoja, Serikali itawaruhusu kutumia fedha moja kwa moja kwenye miradi husika ndani ya utaratibu wa mfuko wa pamoja na washirika wake.

347 Kuunganisha kwa bajeti iliyo ndani (bajeti ya msaada, Mfuko wa Pamoja na bajeti inayopelekwa moja kwa moja kwenye programu na miradi) maeneo muhimu kama vile ya Uratibu na Usimamizi wa Programu, Mipango na Bajeti; Ufuatiliaji na Tathmini na kuimarisha uwezo katika ngazi ya Kitaifa na Serikali za mitaa yatahitaji kugharamiwa kwa kuchangia asilimia 5 za gharama kutoka katika kila (ndani- na nje ya bajeti ) programu na mradi ambayo iko katika sekta.

348 Kwa muktadha huo, washirika wa maendeleo (waliomo ndani au nje ya bajeti ya serikali) wanapaswa kuchangia asilimia tano (5%) ya gharama za mradi wanayoitekeleza hapa nchini kwa ajili ya kugharamia uratibu wa Programu. Fedha zitakazochangiwa zitakuwa zinapitia katika akaunti ya pamoja itakayo kuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ( utaratibu). Akaunti hiyo itasimamiwa na kuratibiwa na Kitengo cha Taifa cha Uratibu (NCU) ambacho kina majukumu ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za ASDP II ili kuhakikisha zinafanyika kwa mujibu wa ratiba na kutoa taarifa ambazo zitasambazwa kwa wadau. NCU ambayo itatumika kama ASDP II Sekretarieti ni timu huru itakayotumia mfumo mmoja wa usimamizi wa fedha kwa ajili ya uhasibu, utoaji wa taarifa na ukaguzi. Watumishi ambao watakuwa katika NCU ni wale watakaoajiriwa kulingana na uwezo na sifa stahiki. Kitengo kitakuwa na mchanganyiko mzuri wa kiufundi na kitaalamu ikiwa ni pamoja na wataalam maalum wa mazao, mifugo na uvuvi ambao watasimamia maeneo makuu manne ya utekelezaji wa ASDP II. Kwa kupitia NCU ambayo itakuwa inajitegemea, kunatoa wigo muhimu wa kuboresha uwajibikaji na usimamizi wa mifumo ya fedha kupitia mafunzo na kujenga uwezo wa kukabiliana na mapungufu mengi ya sasa ambayo ni pamoja na kupanga mipango, bajeti, uhasibu, kuripoti na ukaguzi. Katika usimamizi wa kila siku wa ASDP II, NCU itakuwa inaripoti kwa Katibu Mkuu ofisi ya waziri mkuu. Hata hivyo, kwa ajili ya kupanga mipango, bajeti, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini, NCU itaripoti kwa TCD katika kipindi cha kila robo mwaka.

349 Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo inapaswa kuanzisha Mfuko wa Pamoja wa ASDP II. Mbali na Mfuko wa Pamoja, akaunti ya pamoja itaanzishwa kuruhusu washirika wa maendeleo (wote kwenye bajeti na nje ya bajeti) kuchangia gharama za ASDP II za usimamizi, uratibu, ufuatiliaji, tathmini na ukaguzi. Taratibu hizi zitaiwezesha Serikali kufahamu uwekezaji wote wa umma, binafsi na washirika wa maendeleo unaofanyika katika sekta. Aidha, hiyo inatoa hali ya uwazi na uwajibikaji na kuwawezesha wadau wote katika sekta kuelewa sababu na mantiki ya kuchangia kupitia utaratibu wa Mfuko wa Pamoja.

350 Mtiririko wa fedha kwa ajili ya ASDP II utakuwa kama unavyoonekana katika **Kielelezo Na. 22.** Kwa upande wa taratibu nyingine za kiufadhili, Serikali na washirika wa maendeleo/au washirika wengine, watakubaliana kuhusu mtiririko wa fedha kutoka akaunti teule kwenda kwa wakala wa utekelezaji.

# VI. MUUNDO WA TAASISI NA MGAWANYO WA MAJUKUMU KWA AJILI YA UTEKELEZAJI

## A. Utekelezaji wa ASDP II katika Ngazi ya Taifa

351 Utekelezaji wa ASDP II utafanyika kwa kuzingatia miundo iliyopo ya Kitaasisi ya Serikali katika Wizara za Sekta ya Kilimo ambayo itakuwa inaimarishwa kupitia mafunzo na kujenga uwezo wa watumishi. Wizara za sekta ya kilimo zinajumuisha Wizara za Kilimo; Mifugo na Uvuvi; Viwanda Biashara na Uwekezaji; Maji na Umwagiliaji; Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR-TAMISEMI. Utekelezaji utakavyokuwa unaonyeshwa kwa muhtasari katika **Jedwali Na. 54** na maelezo zaidi ya utaratibu utakaotumika ikiwa ni pamoja na wajibu na majukumu yametolewa katika **Kiambatisho Na. III.**

**Jedwali Na. 54 : Muhtasari wa Mfumo wa Kisekta wa Uratibu wa ASDP II Ngazi ya Taifa , Wajumbe na Utaratibu wa Vikao**

| Aina ya Kikao | Mwenyekiti | Wajumbe | Utaratibu wa Vikao |
|---|---|---|---|
| Mkutano wa Taifa wa Wadau wa Sekta ya Kilimo | Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Mawaziri wa Wizara za Sekta ya Kilimo na Wizara zenye shughuli zinazochangia Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Washirika wa Maendeleo, na Sekta ya Binafsi, Wadau wasio wa Kiserikali, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa; | Mara moja kwa mwaka |
| Kamati ya Usimamizi na Maamuzi (ASC) | Waziri - Ofisi ya Waziri Mkuu | Makatibu Wakuu Wizara za Sekta ya Kilimo na Wizara zenye shughuli zinazochangia Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Wawakilishi wa Wabia wa Maendeleo, na Sekta ya Binafsi, | Kila robo mwaka |
| Mkutano wa Mashauriano wa Sekta ya Kilimo (ASCG) | Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu | Wadau wote wa Sekta ya Kilimo (Serikali, Wabia wote wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Asasi zisizo za Kiserikali/Wadau wasio wa Kiserikali wa Kitaifa na Kimataifa (NGOs/ NSAs), Taasisi za Mafunzo na Utafiti n.k. | Kila robo mwaka |
| Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi wa Wizara za Sekta ya Kilimo | Katibu Mkuu au, Mkurugenzi Ofisi ya Waziri mkuu | Wakurugenzi wa Wizara za Sekta ya Kilimo, | Kila robo mwaka |
| Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II | Mratibu wa Taifa wa ASDP II | Wajumbe wa Timu ya Uratibu katika Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II cha Taifa | Kila mwezi |
| Kamati ya Ufundi ya Viongozi wa Maeneo makuu ya Programu- OR-TAMISEMI | Mkurugenzi wa Uratibu wa Sekta – Ofisi ya Rais -TAMISEMI | Viongozi wa Maeneo makuu ya Programu- OR-TAMISEMI pamoja na Wakurugenzi wengine wa OR-TAMISEMI | Kila robo mwaka |

## B. Ngazi ya Mkoa

352 Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaratibiwa na Ofisi ya Rais -TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara nyingine za Sekta ya Kilimo kupitia Sekretarieti za Mikoa. Idara ya Uratibu wa Sekta-OR-TAMISEMI

kwa kushirikiana na Sekretariati ya Mkoa ina wajibu wa kuzisimamia na kuzisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mfumo uliopo wa uratibu wa Ofisi ya Rais -TAMISEMI kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya chini kupitia Sekretarieti za Mikoa ulifanya kazi vizuri wakati wa ASDP-1 na ASDP II itaendelea kuuimarisha mfumo huo na majukumu hayo ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Wakati wa ASDP- I, majukumu ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -TAMISEMI hayakuwa bayana katika utekelezaji wa Programu hiyo, lakini katika *ASDP II* atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano wa mwaka wa Mashauriano na Wadau wa Kilimo wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (*ARLGAC*), utakaohusisha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Huo utakuwa ni mkutano wa wawakilishi wote na Wadau wanaotekeleza shughuli za sekta ya kilimo katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wadau hao wanajumuisha Serikali, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo, Asasi Zisizo za Kiserikali/ Asasi za Kijamii (*NGOs/ CBOs*).

353 Kwa upande wa usimamizi wa ASDP II, uratibu kati ya Sekretarieti za Mikoa, Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi wa Wizara za Sekta ya Kilimo (*TCD*) utafanyika kupitia Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II. Vilevile Vikundi Kazi vya Kitaaluma vitadumishwa wakati wote ili kufanikisha mtiririko mzuri wa taarifa kuhusu hali ya utekelezaji wa shughuli na utendaji wake chini ya ASDP II. Muundo huu kwa kina umetolewa katika **Kiambatisho Na III.**

## C. Ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

354 Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakuwa na wajibu wa kupanga, kubuni na kutekeleza maeneo makuu ya programu chini ya usimamizi wa Sekretarieti za Mikoa ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. LGA zitahakikisha kuwa Sheria na Kanuni zinazingatiwa wakati wa utekelezaji na matengenezo na kuwajibika katika utoaji wa huduma za ugani na usimamizi wa raslimali ikiwa ni pamoja na kupanga matumizi bora ya ardhi kwa kushirikiana na wawekezaji wa sekta binafsi. Ni muhimu kwa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) kujumuishwa katika Mipango ya Maendeleo na bajeti ya Wilaya (*DDP*). Mamlaka za Serikali za Mitaa pia zitaunda vikundi kazi vya kitaaluma ambavyo vitakuwa na Wataalam wa fani mchanganyiko (mfano: fani za kilimo, biashara, ardhi, mipango na bajeti, ushirika, na maendeleo ya jamii, mazingira / hifadhi); wawakilishi wa Sekta binafsi katika wilaya, asasi zisizo za Kiserikali/ Asasi za Kijamii ambao wanatekeleza shughuli zao katika eneo husika.

## D. Uratibu wa Programu

355 Ngazi za vyombo vya uratibu na majukumu ya *ASDP II* katika ngazi ya Kitaifa zinaelezewa kwa kifupi hapa chini na kwa maelezo ya kina zaidi katika **Kiambatisho Na.III.**

356 Mkutano wa Taifa wa Wadau wa Sekta ya Kilimo (*NASSM*) utafanyika mara moja kwa mwaka baada ya kufanya Mapitio ya Pamoja ya Sekta / Mapitio ya Matumizi ya Fedha za Umma (*JSR / PER*) ambayo hushirikisha Serikali, Washirika wa Maendeleo, Wadau wasio wa Kiserikali, na Sekta Binafsi ili kufuatilia maendeleo ya sekta. Taarifa itawasilishwa na kukubaliwa na Kamati ya Usimamizi na Maamuzi ya Sekta ya Kilimo kisha kujadiliwa katika Mkutano wa Taifa wa Wadau wa Sekta ya Kilimo (*NASSM*).

**357 Kamati ya Usimamizi na Maamuzi** *(ASC)* kitakuwa chombo muhimu cha usimamizi na uidhinishaji wa utekelezaji na uratibu wa *ASDP-II*. Chombo hicho kitakuwa kinaidhinisha mpango kazi wa mwaka , bajeti, kusimamia hali ya utekelezaji na matumizi ya fedha, kufuatilia matokeo ya ukaguzi na kujadili juu ya masuala muhimu kuhusiana na utendaji na uratibu wa sekta ili kutoa mwongozo kwa Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi wa Wizara za Sekta ya Kilimo (*TCD*) na Vikundi kazi vya Kitaaluma *(TWGs)*. Pia itasimamia ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa *ASDP II.*

**358 Mkutano wa Mashauriano wa Sekta ya Kilimo** (*ASCG*). Mkutano huu utakuwa ni jukwaa la kushauriana na kutoa ushauri kupitia majadiliano kati ya Serikali (Wizara za Sekta ya Kilimo), Washirika wote wa Maendeleo wenye nia (kama inavyoelezwa katika Mkakati wa Pamoja wa Utoaji Misaada kwa Tanzania - JAST), Sekta Binafsi na Wadau Wasio wa Kiserikali (Asasi Zisizo za Kiserikali, Asasi za Kijamii (*CBOs*), na Asasi za Sekta Binafsi (*PSOs*)) katika Sekta ya Kilimo. Mkutano huu utakuwa unaratibu majadiliano katika ngazi mbili: majadiliano ya mara kwa mara kuhusu Sera za Sekta na Kanuni;

Mipango ya kila mwaka, Bajeti ya kila mwaka ya Sekta ya Kilimo ; taarifa za mwaka za Mapitio ya Pamoja ya Sekta / Mapitio ya Matumizi ya Umma (*ASR / PER*). *ASCG* ni jukwaa la ushauri, wakati Kamati ya Usimamizi na Maamuzi ya Sekta ya Kilimo ni chombo cha kufanya maamuzi.

359 **Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi wa Wizara za Sekta ya Kilimo** (*TCD*). Kamati hii itatoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati ya Usimamizi na Maamuzi ya Sekta ya Kilimo kuhusu masuala ya kitaalam yanayohusiana na maeneo makuu ya programu na maeneo yake madogo ya vipaumbele vya uwekezaji na uendelezaji wa miradi. Kamati hii itakuwa inasaidiwa na Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa *ASDP II* (*NCU*) na Vikundi kazi vya Kitaalam vya kila eneo kuu la programu (*TWGs*).

360 **Vikundi Kazi vya Kitaaluma (TWGs):** Wajumbe wa Vikundi Kazi vya Kitaaluma watatokana na wataalam wenye fani stahiki (yaani, Idara / Taasisi) kutoka katika kila Wizara ya Sekta ya Kilimo na watakaribisha ushiriki wa wataalamu bingwa wa fani hizo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Vikundi Kazi vya Kitaaluma vitakuwa vinatoa mwongozo wa Programu kuhusu masuala ya kitaalam na / au usimamizi na pia kuishauri Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi wa Wizara za Sekta ya Kilimo (*TCD*) na kufuatilia utekelezaji wa hatua zilizopendekezwa kuchukuliwa kama ilivyoainishwa katika mipango kazi ya kila mwaka.

361 **Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II:** Kitaongozwa na Mratibu wa Taifa wa Programu na kitakuwa na Maafisa wa kujitegemea walioteuliwa kutoka katika soko la ajira pamoja na Wizara za Sekta ya Kilimo / Taasisi za Serikali na kitakuwa na majukumu ya kusimamia, kufuatilia na kuandaa mikutano ya vyombo vingine katika muundo wa uratibu wa ASDP II pamoja na kuelekeza utekelezaji wa majukumu hayo. Timu hii itakuwa inatekeleza majukumu hayo wote na kuwajibika kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo kwa masuala ya usimamizi na utawala na pia kuwajibika kwa Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi wa Wizara za Sekta ya Kilimo kuhusu masuala ya utekelezaji wa programu. Timu hiyo itajishughulisha na utekelezaji wa ASDP II pekee kwa kipindi chote cha programu.

362 **Mkutano wa Mashauriano wa Sekta ya Kilimo** (*ASCG*): Mkutano huu si sehemu ya ngazi za uratibu wa ASDP II, bali ni mkutano muhimu wa mashauriano wa Wadau wa Sekta ya Kilimo . Mkutano huu utakuwa jukwaa la majadiliano kati ya Serikali (Wizara ya Sekta ya Kilimo), Washirika wa Maendeleo na Wadau wa Sekta ya Kilimo wasiokuwa wa Kiserikali na kuratibu majadiliano ya mara kwa mara kuhusu sera za sekta na bajeti, taarifa za mwaka za Mapitio ya Pamoja ya Sekta / Mapitio ya Matumizi ya Fedha za Umma (*ASR / PER*). Itakuwa inataarifu kuhusu masuala ya kisera na kufanya mapitio ya masuala ya kibajeti, kuwezesha majadiliano ya sekta kuhusu Mkakati wa Pamoja wa Utoaji Misaada kwa Tanzania -JAST na na Mfuko wa Misaada ya Bajeti wa Pamoja (*GBS*).

**Jedwali Na. 55: Muhtasari wa ASDP II katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekretarieti ya Mkoa, vyombo vya Uratibu vya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wajumbe na Taratibu za Mikutano**

| Aina ya Kikao | Mwenyekiti | Wajumbe | Utaratibu wa Vikao |
|---|---|---|---|
| Mkutano wa mwaka wa Mashauriano wa Wadau wa Kilimo wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (*ARLGAC*), | Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI | Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM), Maafisa Kilimo, Umwagiliaji na ushirika wa MSM, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo, Asasi zisizo za Kiserikali / Asasi za Kijamii na Wadau wengine katika Mikoa na MSM husika | Mara moja kwa mwaka |
| Mkutano wa Mashauriano wa Sekta ya Kilimo (ASCG) | Katibu Mkuu-OR- TAMISEMI | Wakurugenzi (DPPs) wa Wizara za Sekta ya Kilimo | Kila nusu mwaka |

| Aina ya Kikao | Mwenyekiti | Wajumbe | Utaratibu wa Vikao |
|---|---|---|---|
| Kamati ya Ufundi ya Viongozi wa Maeneo makuu ya Programu- OR-TAMISEMI | Mkurugenzi wa Uratibu wa Sekta- OR- TAMISEMI | Wataalam Viongozi wa Maeneo makuu ya Programu - wa OR-TAMISEMI na Wakurugenzi wengine katika OR-TAMISEMI | Kila robo mwaka |
| Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) | Mkuu wa Mkoa (RC) | Katibu Tawala wa Mkoa (RAS), Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mkoa, Wakuu wa vitengo (kwa mujibu wa Sheria) | Kila robo mwaka |
| Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) | Mkuu wa Wilaya (DC) | Wakurugenzi Watendaji wa MSM, Wakuu wa Idara katika MSM (Kwa mujibu w Sheria) | Kila robo mwaka |
| Baraza la Madiwani | Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani | Wajumbe wa Baraza, Timu ya Wataalam ya Usimamizi ya Halmashauri (CMT), Wakurugenzi Watendaji wa MSM, | Kila robo mwaka |
| Kamati ya Maendeleo ya Kata | Diwani wa Kata | Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kata | Kila robo mwaka |
| Mkutano wa Serikali ya Kijiji | Mwenyekiti wa Kijiji | Wajumbe wa Mkutano wa Serikali ya Kijiji | Kila mwezi |
| Mkutano Mkuu wa Kijiji | Mwenyekiti wa Kijiji | Wanakijiji wote wenye umri kuanzia miaka 18 na mwenye akili timamu | Kila robo mwaka |

## E. Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa na Ufuatiliaji

363 Ufuatiliaji na tathmini ni eneo muhimu kwa ajili ya ufanisi katika usimamizi wa programu. Hivyo, unatakiwa kufafanuliwa na kuandaliwa katika hali ya kueleweka vema kuanzia mwanzo wa utekelezaji wa program ili kuwafahamisha wadau wote wa sekta juu ya matarajio katika viashiria vya utendaji. ASDP II itatumia TEHAMA katika kuongeza ufanisi wa utoaji na uchambuzi wa taarifa kutoka katika maeneo ya utekelezaji. Hii itahusisha matumizi ya *tableti*, simu janja na tarakishi (kompyuta) ili kuongeza uwezo wa Maafisa katika ngazi ya Kijiji/Kata, Halmashauri na Mikoa wa kuandaa na kusimamia ubora wa takwimu.

364 Ubunifu wa mfumo wa tathmini na ufuatiliaji unahitaji mbinu za kitaaluma ili kufanikisha kusudi lake. Umakini kwenye usahihi kwa pande zote za mawasiliano utaimarishwa wakati wa kutoa mrejesho kutokana na uchambuzi, ambapo pia husaidia kuongeza ufahamu wao juu ya utendaji wao wenyewe na kudumisha nia ya kujiendeleza. Kubadilishana maoni kunatokana na majadiliano juu ya takwimu na uchambuzi wa takwimu pia husaidia kuimarisha uratibu na kuboresha uwazi wa mifumo ya usimamizi, matarajio na utendaji.

365 Katika muktadha huu, Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II cha Taifa kitatumia mfumo wa ufuatiliaji na tathmini na taratibu zilizowekwa kuanzia mwanzo wa utekelezaji ili kuleta ufanisi katika kutekeleza program hii. Mfumo lazima ueleze njia za kupashana taarifa, wahusika katika utekelezaji wake, muda wa utekelezaji, mbinu ya uchambuzi kwa kuzingatia malengo ya mchakato husika na utaratibu wa kukabiliana na mazingira kadri yatakavyojitokeza. Ushirikiano na Wataalamu kutoka Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) utaleta matokeo bora ya pamoja na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu.

366 Mtaalamu wa ufuatiliaji na tathmini ataajiriwa kufanya kazi sehemu ya Kitengo cha Uratibu wa ASDP II cha Taifa. Mtaalam huyo atasimamia mchakato na kuhakikisha umuhimu na ufanisi wake: taarifa za kila robo zitalingana na mwongozo uliowekwa. Majibu yanapaswa kuwa rasmi, mafupi, yenye takwimu, na kadri itakavyowezekana, yanaweza kurahisishwa kwa majibu ya ndiyo / hapana. Kama kuna haja ya kutoa maelezo basi yanapaswa kuwekewa muundo, yasiwe na utata na kujielekeza katika maelezo mafupi. Takwimu zinazotolewa lazima zitaarifu Kitengo cha Uratibu wa *ASDP II* cha Taifa na Makundi yote katika ngazi za kitaasisi za uratibu wa *ASDP II* kuhusu mwenendo wa utekelezaji kuelekea malengo ya Taifa kama ilivyoelezwa katika malengo ya *ASDP II,* pamoja na mwenendo wa utekelezaji wa maeneo makuu ya programu, maeneo madogo programu, maeneo ya vipaumbele vya uwekezaji na miradi, ufanisi wa utekelezaji na manufaa ya uzalishaji, usalama wa chakula, mabadiliko ya tabianchi, na uwezo au uwezekano kulingana na lengo la miradi. Kipimo cha jumla na tathmini ya matokeo kitafanyika kupitia mfumo wa matokeo.

367 Madhumuni ya kukusanya taarifa lazima yajulikane kwa wale wanaohitaji na wale wanaotoa ili kuboresha umuhimu wa zoezi hilo na kuwajulisha haja ya kuwajibika ipasavyo. Hitimisho kutokana na uchambuzi lazima litoe taarifa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Wizara za Sekta ya Kilimo, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kata na Vijiji. Kama sehemu ya mchakato wa bajeti ya kila mwaka, inapaswa kuboresha utendaji wa utekelezaji wa programu, kuchochea uhitaji na kusababisha kuingiza dhana ya kuunganishwa Kitaifa na ina madhumuni ya pamoja.

368 Kwa mujibu wa Makubaliano/Maelewano, taarifa kuhusu shughuli na mafanikio yake pia zitakusanywa kutoka katika miradi ya Asasi Zisizo za Kiserikali au miradi ya Washirika wa Maendeleo wasiopitisha fedha zao katika bajeti ya Serikali ili kuzingatiwa kwenye utekelezaji mpana wa Kisekta pamoja na viashiria vya matokeo vinavyolenga malengo ya Kitaifa. Takwimu zitakazokusanywa katika ngazi ya Kijiji zitawasilishwa kwa nakala ngumu (fomu za karatasi) mpaka pale itakapowezekana kutumia TEHAMA kukusanya na kuwasilisha takwimu kwa njia ya kielectroniki. Taarifa za kijiji zitawasilishwa katika Kata na kutoka Kata kwenda ngazi ya Halmashauri.

369 Katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, matokeo yatalinganishwa, kuunganishwa na kupangiliwa kidigitali katika muundo uliosanifiwa kwa ajili ya usambazaji kwa njia ya kielekitroniki kwenda kwenye Mikoa. Mikoa "itasafisha" taarifa kwa kuhakiki ili kuhakikisha kuwa taarifa hazibadiliki badiliki na kuziunganisha katika muundo uliosanifiwa ili kuandaa taarifa ya Mamlaka za Serikali za Mitaa iliyounganishwa pamoja kwa ajili ya kuiwasilisha Ofisi ya Rais -TAMISEMI, na nakala kutumwa katika Kitengo cha Uratibu wa *ASDP II* cha Taifa , ambako kutafanyika uunganishaji na uchambuzi zaidi ili kupata taarifa ya Kitaifa kwa kila robo mwaka na za mwaka mzima.

370 Uchaguzi wa viashiria ni lazima uzingatiwe kwa uangalifu kwa kujielekeza katika kutoa taarifa muhimu kwa watoa maamuzi ili kuepuka kuwabebesha mzigo mkubwa watoa taarifa na kuwatengenezea hali ya kuelemewa na kazi na hivyo kukusanya taarifa zisizo na umuhimu. Viashiria sahihi vya mfumo wa ufuatiliaji na matokeo lazima vitaarifu kuhusu maendeleo ya utekelezaji kuelekea malengo ya miradi/programu na kuzingatia taarifa juu ya ufanisi, uthabiti, umuhimu na matokeo fikiwa ili pia yaweze kutafsiriwa katika uwiano wa gharama/faida. Takwimu zinapaswa pia kutaarifu programu namna masuala mtambuka yalivyozingatiwa na malengo ikiwa ni pamoja na masuala ya jinsia na mazingira.

## F. Masuala ya Usalama, Usimamizi wa Kijamii na Kimazingira

371 Kwa kuwa "maendeleo" bila ya kuzingatia mazingira au maendeleo ya kijamii yanaweza kurudishwa nyuma katika kipindi cha muda mrefu, ni muhimu kuzingatia kwa kina masuala hayo na kuyajumuisha katika mchakato wa uchaguzi wa mradi.

372 Uzingatiaji wa mazingira unaweza kuhusisha wigo mpana wa matokeo ikiwa ni pamoja na mmomonyoko wa udongo, uharibifu wa misitu, uchafuzi wa hewa, uchafuzi wa vyanzo vya maji, mafuriko, uharibifu wa sifa za udongo, kelele, kufifia kwa mandhari ya nchi, msongamano wa magari, madhara ya kiafya

kutokana kemikali za kilimo au ajali, milipuko wa wadudu au visumbufu vya mimea na wanyama ikiwa ni pamoja na malaria, kichocho, ndigana - kwa mifugo/Malale – kwa binadamu n.k. Ulinzi wa kijamii ni pamoja na usawa wa kijinsia, mazingira ya kazi, uharibufu wa familia, unyonyaji wa wafanyakazi na watoto walioajiriwa, kukatiza masomo shuleni, usalama wa kibinafsi, lishe, msongo wa mawazo, kujiweka katika mazingira ya ajali na madhara ya kiafya, ugomvi wa kiraia kutokana na tofauti ya utajiri, uhamiaji n.k.

373 Masuala ya ulinzi yanajumishwa katika mchakato ambao una hatua mbili. Kwanza, kwa kuweka vigezo vya uteuzi wa miradi kwa kuzingatia misingi ya kimazingira na kijamii. Pili, kwa miradi ambayo inaweza kuwa na athari, kwa kupitia Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (*ESIA*) ambayo inafanywa na wataalam bingwa katika fani hiyo kabla ya kuanza utekelezaji.

374 Wataalamu bingwa katika tathmini za athari ya mazingira wanaweza kusajiriwa na kupelekwa kufanya tathmini kama inavyotakiwa kwa mkataba au, kama kuna uhitaji wa kutosha, chini ya ajira ya muda mrefu katika Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa *ASDP II*. Gharama ya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii pale inapobidi, ijumuishwe katika gharama ya utekelezaji wa mradi .

**375 Mfumo wa usimamizi.** Sheria Mama ya Kitaifa ya Mazingira nchini Tanzania ni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, ambayo inasisitizia haja ya kufanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza utekelezaji au kufadhili mradi. Kanuni zinazofaa kutumika kuongoza usimamizi wa mazingira na kijamii chini ya ASDP II, ni za Tathmini ya Athari za Mazingira na Kanuni za Ukaguzi wa Mazingira za mwaka 2005. Kanuni hizo, zinaelekeza mahitaji na taratibu za kuchukua, kupitia, kuidhinisha na ukaguzi wa Tathmini ya Athari za Mazingira kwa aina tofauti za miradi na viwango vyao vya tathmini inayohitajika. Jukumu la jumla la kuongoza usimamizi wa mazingira na kijamii katika ngazi ya kitaifa liko chini ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) lililoko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Wizara ya Kilimo ina Kitengo kamili cha Usimamizi wa Mazingira ambacho kinaratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala ya mazingira na kijamii katika sekta ya kilimo, ikiwa ni pamoja na ASDP II. Katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, usimamizi wa mazingira na kijamii utaratibiwa na Afisa Mazingira wa Wilaya (*DEMO*)

376 Kwa mujibu wa Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii Mfumo wa Kisera wa fidia kwa wanaohamishwa kutoka maeneo yao na Kanuni za Ukaguzi, uwekezaji katika sekta ya kilimo unaangukia katika miradi ya Kundi 'A' ambayo ina uwezekano wa kuwa na athari za mazingira. Kwa hiyo, Tathmini za Athari za Mazingira ni lazima kwa ajili ya miradi ya kilimo ambayo inajumuisha kufanya tafiti za kina ili kubainisha ukubwa na umuhimu wa athari zinazotarajiwa na utambuzi wa hatua zinazofaa za kupunguza. Msaada wa ASDP II katika kuongeza uzalishaji na biashara kwa mazao yaliyochaguliwa katika Kanda mbalimbali za kiikolojia za kilimo unaweza kuleta athari chanya na hasi za kimazingira, ikiwa ni pamoja na: (i) kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia na matumizi ya pembejeo; (ii) uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji; na (iii) kuboresha ufanisi wa masoko kwa kukusanya mazao pamoja (kama vile matumizi ya maghala) na kuongeza thamani ili kuongeza mapato.

377 Athari chanya za kijamii na kiuchumi ambazo zitatokana na utekelezaji wa ASDP II ni pamoja na: (i) ongezeko la tija katika uzalishaji na mapato kwa Jamii za Vijijini katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizochaguliwa kwa kuzingatia utengenezaji wa fursa nyingi na bora za ujasiriamali; (ii) kupunguza Kaya zenye uwezekano wa kuathirika; na (iii) kuboreshwa kwa viwango vya maisha na kuongezeka kwa fursa za ajira Vijijini. Haya yote yatasababisha kuboreka kwa uhakika wa chakula na hali ya lishe katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazoshiriki, na kuboresha hali za maisha, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma bora za kijamii na kiuchumi. Kadhalika, Programu itaongeza uwezo wa kujumuisha masuala ya mazingira na kijamii na kiuchumi katika shughuli za maendeleo na kuboresha ufahamu wa wadau kuhusu masuala ya kimazingira na ki-jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizochaguliwa

378 Athari hasi zinaweza kuhusishwa na utekelezaji wa shughuli katika mnyororo wa thamani wa bidhaa na uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji na miradi midogo ya kuongeza thamani. Athari hizo zinaweza kujumuisha: (i) Uchafuzi wa vyanzo vya maji kutokana na kumwagika kwa kemikali za kilimo au maji taka kutoka kwenye viwanda vya usindikaji; (ii) Mmomonyoko wa udongo na upungufu wa virutubisho katika udongo na masuala mengine yanayotokana na matumizi yasiyofaa ya pembejeo

za kilimo; (iii) kelele na uchafuzi wa hewa; (iv) kuenea kwa magonjwa (kama vile VVU / UKIMWI), hasa wakati wa ujenzi wa miradi; na (v) migogoro ya matumizi ya ardhi, miongoni mwa mengine. Ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji na upanuzi inaonekana kuwa tatizo zaidi kwa sababu inaweza kusababisha uharibifu wa maeneo ya vidaka maji ya mito na mfumo wa kiikolojia wa viumbe vinavyoishi karibu na kingo za vyanzo vya maji / bioanuai, kuongeza chumvi chumvi katika udongo, kupoteza misitu na mimea mbalimbali, kupungua kwa hali ya kawaida ya utiririkaji wa maji ya mito na manufaa yake katika mazingira uharibifu wa maeneo ambayo ni mepesi kuathirika kiikolojia katika maeneo ya ardhi oevu, kuongezeka kwa magonjwa yanayoenezwa na maji, na uchafuzi wa maji kutokana na matumizi yasiyofaa ya kemikali za kilimo. Zaidi ya hayo, uingiliaji wa haki za mali za watu wengine na haki za kupata mali, idadi ya watu wanaohamia maeneo mengine kutafuta ajira au fursa nyingine za kiuchumi, kuongezeka kwa migogoro ya matumizi ya maji katika skimu baina ya watumiaji walioko mkondo wa juu wa maji na waliko mkondo wa chini wa maji pia inatakiwa kushughulikiwa. Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira na Kijamii (SESA) kwa ajili ya Mpango Kabambe wa Umwagiliaji wa Taifa (*NIMP*) na Sera ya Taifa Umwagiliaji ya mwaka 2011 inatoa maelezo ya kina na mapendekezo ya kupunguza athari zinazoweza kutokea kutokana na utekelezaji wa shughuli za umwagiliaji nchini.

379 **Uwezo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii;** Kwa miaka mingi, uboreshaji wa uwezo wa kusimamia masuala ya mazingira na kijamii umefanywa kupitia utekelezaji na mafunzo yaliyofadhiliwa na benki mbalimbali katika sekta ya kilimo, kama vile ASDP-1, PADEP na AFSP. Hata hivyo, uwezo wa kitaasisi na kiufundi katika usimamizi wa mazingira na kijamii katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na ngazi za chini za Serikali za Mitaa bado unahitaji kuboreshwa. Upungufu huu utashughulikiwa kwa kina wakati wa utekelezaji wa program katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

380 Wakati wa ASDP-1, Tathmini ya kimkakati ya Mazingira na Kijamii (*SESA*) ilifanyika. Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira na Kijamii inajumuisha Sera ya Umwagiliaji ya Taifa na Mpango wa Kabambe wa Umwagiliaji wa Taifa, na hutoa mwongozo maalum kwa uwekezaji katika Kilimo cha umwagiliaji. Tathmini ya kimkakati ya Mazingira na Kijamii inatambua uwezekano wa athari za mazingira na kijamii kutokana na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji / Mpango Kabambe wa Umwagiliaji wa Taifa na unaainisha mwongozo wa kimkakati kuhusu kupunguza na kufikisha kiwango cha chini kabisa cha athari hizo wakati wa kutekeleza miradi /program katika sekta. Ukaguzi wa mazingira na kijamii kwa ASDP-1, ambao unaendelea, utatoa ufahamu zaidi na somo juu ya uwezo katika Taasisi kuu zinazotekeleza masuala yanayohusiana na usimamizi wa kimazingira na kijamii.

## VII. FAIDA NA UCHAMBUZI WA KIUCHUMI NA KIFEDHA

### A. Muhtasari Kuhusiana na Faida

381 Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta, mageuzi katika kilimo na kasi ya maendeleo vijijini vitaleta mchango mkubwa kwenye matarajio ya kitaifa ya maendeleo ya Tanzania. Faida za msingi za programu zitakuwa: (i) ongezeko endelevu la tija na uzalishaji wa chakula na mazao yasiyo ya chakula ili kuboresha kipato vijijini, kuimarisha uhakika wa chakula ngazi ya Kaya za vijijini na Taifa, na kutoa malighafi kwa ajili ya sekta ya Viwanda vya kuchakata mazao na utengenezaji wa bidhaa za kilimo; (ii) kupunguza kuenea kwa tatizo la lishe duni na utapiamlo katika jamii za vijijini na kinga dhidi ya majanga ya kiasili; (iii) kuharakisha sekta za kuzalisha kibiashara ili kuongeza mapato ya fedha kutokana na shughuli za mashambani na zisizo za mashambani, hususan kwa Wakulima wadogo (wanaofikia takriban 97.5% ya Kaya za Vijijini); (iv) kulinda na kuimarisha uwezo wa muda mrefu wa uzalishaji wa rasilimali za msingi za Tanzania kwa kuzingatia mbinu bora endelevu za usimamizi wa ardhi na maji; (v) kuimarisha uwezo wa taasisi kuhamasisha upatikanaji na kusisimamia rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya kilimo. Kwa kuzingatia kiwango cha uwekezaji kilichopangwa ndani ya kipindi cha miaka 5 na upeo wa shughuli zitakazofadhiliwa, wigo wa faida utaongezeka[72]. Faida hizi zote zitachangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya kitaifa kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025.

72 *Mfumo wa Matokeo katika kiambatisho na II unaonesha uhusiano kati ya shughuli mbalimbali na matokeo yake ya kimkakati.*

382 Faida nyingine nyingi zinazotegemewa zitapatikana kadri sekta inavyoendelea kukua ni pamoja na: (i) kupunguza upotevu wa mazao baada na kabla ya kuvuna ; (ii) kuongeza mapato ya nje; (iii) uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kilimo yenye thamani kubwa; (iv) kuboresha ufikiwaji wa huduma za kifedha kwa wakulima wadogo na wajasiriamali vijijini (v) kupunguza gharama za miamala na kuongeza ufanisi katika minyororo ya thamani kabla na baada ya kutoka mashambani (vi) kuongezeka ushiriki wa wakulima katika vyama vya ushirika na aina nyingine za asasi za wakulima; (vii) kuboresha ufikiwaji wa masoko kupitia uendelezaji wa miundombinu; (viii) kuongezeka kwa ajira vijijini (ix) kuongezeka kwa tija na kupunguza athari za ukame kutokana na upanuzi wa wigo wa kilimo cha umwagiliaji; (x) kudumisha bioanuai za kilimo; na (xi) kuboresha mfumo wa usimamizi wa kukabiliana na majanga kwa kutafiti matumizi ya zana bunifu za usimamizi wa athari hizo. Mageuzi ya kilimo pia yatahakikisha (xii) kupunguza uwiano usio sawa wa masuala ya kijinsia ; (xiii) kupunguza ajira za watoto katika sekta ya kilimo kwa kukuza kazi zenye staha kwa mujibu wa miongozo wa Shirika la Wafanyakazi Duniani; na kupunguza mchango wa kilimo katika mabadiliko ya tabianchi kwa kuhamasisha kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi. ASDP 1 ilisisitiza kueneza teknolojia za uzalishaji ili zitumiwe na wakulima. Uendelezaji wa stadi za kibiashara na uimarishaji wa mitandao, uunganishaji wa wakulima na masoko ulikuwa bado una mapungufu. Kwa hiyo, uandaaji wa ASDP II umelenga katika kuendeleza mtandao wa minyororo ya thamani yenye kufanya kazi na inayoongozwa na hali ya masoko, kwa kushirikisha wadau muhimu (wakulima, wauzaji na wasindikaji) ambao wanafahamu mahusiano yaliyopoa baina yao, ikiwa ni pamoja na uwekezaji, kufanya jitihada za makusudi za kuwaboresha, na kujipanga wao wenyewe kwa namna ambayo wanaweza kufaidika na ushiriki katika mnyororo wa thamani wa mazao. ASDP II ina lenga kupunguza utengano baina ya wadau, kuhamasisha na kuimarisha utendaji wa pamoja na kujenga mitandao miongoni mwa washirika wa mnyororo wa thamani ili kuongeza nia ya kuwekeza katika teknolojia mpya, miundombinu, uzalishaji na usindikaji ili kupata kipato kikubwa zaidi.

383 **Upunguzaji wa Gharama kwa Njia ya Kuongeza Uwezo wa Kuzalisha Zaidi** *(Economy of scale):* katika uzalishaji, upunguzaji wa gharama kwa njia ya kuongeza uwezo wa kuzalisha zaidi ni kikwazo. Uzalishaji na tija miongoni mwa wazalishaji wadogo ni kidogo ikilinganishwa na fursa za masoko ya ndani na nje ya nchi. Kiwango cha uzalishaji ni kidogo sana kiasi kwamba wanunuzi wakubwa wa mazao wanakosa umakini katika kujenga ubia. Kwa hiyo, msisitizo umewekwa katika kuimarisha ushirika na asasi za wakulima na katika uhamasishaji wa uzalishaji chini ya programu ili kuwawezesha kukusanya bidhaa kwa pamoja na kuongeza tija kufikia kiwango ambacho kitaonesha maana halisi ya kiuchumi katika kushiriki kwenye mnyororo wa thamani.

384 **Kuimarisha Ushindani.** Shughuli zinazolenga kukabiliana na changamoto za soko, kuboresha tija, masoko na ushindani zitatoa faida kubwa kwa washiriki wote katika mnyororo wa thamani. Hivyo, mambo muhimu yafuatayo yanayoathiri ushindani yatashughulikiwa kupitia utekelezaji wa programu: (i) Vikwazo vya kiteknolojia katika mifumo ya uzalishaji na baada ya uzalishaji na miundombinu duni itashughulikiwa katika eneo kuu la 2 la programu; (ii) Ufikiwaji wa masoko unashughulikiwa na eneo kuu la 3 la programu, (iii) Misaada ya kifedha na taarifa kuhusu mikopo, na ukosefu wa vyama vya wakulima, vyama vya wazalishaji, imara, vyama vya biashara, na mifumo ya uratibu miongoni mwa wadau vitashughulikiwa na eneo kuu la 4 la programu. Zaidi ya hayo, shughuli za programu zitaleta manufaa ya moja kwa moja kama vile: (i) Kuongezeka kwa ufanisi wa kazi shambani kutokana na maboresho katika hatua ya uzalishaji na uendelezaji wa masoko, usafiri na usafirishaji, na taasisi za masoko; (ii) Kuongezeka kwa shughuli za uongezaji wa thamani katika ngazi za shambani / au baada ya kutoka shambani kwa ujumuishi mpana kati ya wazalishaji, wafanyabiashara na wasindikaji katika minyororo thamani (iii) Kuongezeka kwa ufikiwaji wa masoko. Pia, mradi wa uimarishaji vyama vya ushirika, asasi za wakulima pamoja na vyama vingine vya washiriki katika mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo vitatoa faida zaidi ya zisizo za moja kwa moja katika hali ya: (i) Asasi za wakulima ambazo zinaweza kujihusisha na masoko kwa faida; (ii) Shughuli zaidi zinazotegemea masoko na shughuli za kilimo za kibiashara pamoja na viungo imara vya wazalishaji; na (iii) Mpango uliopangiliwa vizuri wa kuboresha mnyororo wa thamani katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mkoa na Taifa.

385 **Utaratibu wa Utekelezaji Unaolenga Matokeo.** Utaratibu wa utekelezaji wa Programu, kwa kuzingatia vipaumbele vya minyororo ya thamani ambavyo vinazingatia Kanda za Kiikolojia za Kilimo (*AEZs*), pamoja na kuzingatia uwekezaji kulingana na mahitaji halisi, programu hii itawezesha kuchangia katika

kuleta matokeo makubwa. Programu itajikita katika minyororo ya thamani ya mazao yenye fursa kubwa katika kanda za kiikolojia za kilimo; Kwa kutumia mbinu hii, programu itajikita katika utekelezaji wa uwekezaji na uzalishaji wa mazao ambayo yataleta matokeo makubwa, yenye faida, katika Kilimo, ukuaji wa faida ya mkulima, fursa za kibiashara na uendelezaji wa viwanda..

386 **Mfumo jumuishi wa wadau wengi katika utoaji wa huduma,** ambapo watoa huduma binafsi, Umma, na wa Asasi Zisizo za Kiserikali watashiriki katika kuandaa washiriki wa mnyororo wa thamani , kuimarisha uhusiano wa kitaasisi na utoaji huduma za ushauri wa kiufundi na kibiashara utakuwa na athari chanya endelevu. Ujenzi wa miundombinu ya masoko ya vijijini utategemea mahitaji na utagharamiwa kwa pamoja na wanufaika, kwa kutumia uwezo wa ushawishi uliopo wa utafutaji wa rasilimali, ikijumuisha raslimali za kutoka sekta binafsi.

387 **Kukabiliana na Ukame na Mabadiliko ya (Tabianchi).** Programu hii ina miradi mikubwa ya maendeleo ya umwagiliaji chini ya eneo kuu la kwanza (1) la programu . Hii ni kwa ajili ya kukabiliana na athari zinazoinyemelea sekta ya kilimo na uchumi wa Tanzania kwa ujumla kutokana na kilimo cha kutegemea mvua kisichokuwa na uhakika, ambacho ni sehemu kubwa ya aina ya kilimo kinachotumika. Kilimo kinaathiriwa na ukame wa mara kwa mara, ambao unasababisha njaa na una athari hasi kubwa kwenye Pato la Taifa (*GDP*). Mabadiliko ya tabianchi pia yanatarajiwa kupunguza mvua na kuongeza tofauti za upatikanaji wa mvua katika maeneo ambayo ni kame na ambayo yanapata mvua chache kwa mwaka hapa Tanzania. Zaidi ya uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji, shughuli za kipaumbele pia zitahamasisha teknolojia na mbinu za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi (*CSA*). Programu inahakikisha inajumuisha usimamizi wa udongo na maji, kilimo hifadhi na kilimo mseto ili kukabiliana na changamoto hizi na kuwezesha kuboresha uendelevu wa tija na uhimilivu wa sekta katika hali ya kutegemea kilimo cha mvua.

388 **Faida zitatokana pia na maeneo kadhaa yaliyo mtambuka kitaaluma ya ASDP II** ikiwa ni pamoja na: (i) kuimarisha uwezo wa kitaasisi na rasilimali watu katika ngazi zote; (ii) uwiano mzuri zaidi wa ushiriki wa wanawake na wanaume (wazee na vijana) katika maendeleo na shughuli za kuongeza kipato pamoja na kuweza kushiriki michakato ya kutoa maamuzi; (iii) kutambua mahitaji maalum ya familia za vijijini zilizoathirika na VVU / UKIMWI na /au lishe duni na juhudi za kuboresha lishe katika kaya ili kukabiliana na kuenea kwa ugonjwa, na (iv) kuboresha uwezo wa sekta ya kilimo katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza mchango wa Tanzania Kimataifa katika uzalishaji wa hewa ukaa. Athari chanya za kiuchumi zitakuwa kwa miradi yote inayotarajiwa kuwekezwa kwa kupitia mchakato wa upembuzi yakinifu wa kitaalam na kifedha, ili kujihakikishia kwamba ile miradi yenye uwezekano wa kurejesha mapato makubwa kifedha na kiuchumi ndiyo inapewa kipaumbele kikubwa, na kwamba miradi yote itakayowekezwa ianzie kiwango cha chini cha urejeshaji mapato kinachokubalika.

## B. Uchambuzi wa Kiuchumi na Kifedha

### Utangulizi

389 Uchambuzi wa kiuchumi na kifedha ulifanyika ili kutathmini uwezekano wa uwekezaji unaotarajiwa kutekelezwa katika ASDP II. Manufaa makubwa ya kiuchumi kutokanana shughuli hizo yanatarajiwa kuwa yafuatayo: (i) kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kutokana na ongezeko la tija, kuongeza uwiano wa eneo ghafi lililopandwa kwa eneo halisi linalolimwa, uzalishaji wa mazao tofauti tofauti yenye thamani kubwa, (ii) kuimarisha uzalishaji wa mifugo na uvuvi; (iii) mapato makubwa kutokana uzalishaji katika kilimo; (iv) Ongezeko la mapato kutokana na kilimo-biashara na uongezaji mkubwa wa thamani; na (v) Mapato makubwa ya mauzo ya nje.

390 Inakadiriwa kuwa wakulima katika hekta 2,000,000 za mashamba ambayo hayamwagiliwi maji watafaidika kutokana na msaada wa huduma bora za kilimo, uendelezaji wa vyama vya wakulima, na ufikiwaji bora wa masoko na taasisi za kifedha za vijijini. Zaidi ya hayo, uwekezaji katika usimamizi wa ardhi na vyanzo vya maji utasaidia kuhakikisha kwamba kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kunakuwa endelevu katika maeneo ambayo yanaathirika kwa mmomonyoko wa udongo na kupungua kwa rutuba ya udongo. Pia, inakadiriwa kuwa miundombinu ya umwagiliaji iliyoboreshwa itanufaisha jumla ya eneo la kilimo cha umwagiliaji kiasi cha hekta 165,000, ikijumuisha hekta 65,000 za skimu

mpya pamoja na skimu za kupanua kilimo cha umwagiliaji na hekta 100,000 za skimu za umwagiliaji zilizopo ambazo zitakarabatiwa chini ya ASDP II.

391 Katika eneo linalolimwa kwa kutumia umwagiliaji, uwiano wa eneo lililolimwa kwa eneo lililopandwa unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia 135% wakati katika eneo lisilolimwa kwa kumwagiliwa inatarajiwa kuwa uwiano huo utaongezeka hadi kufikia 100%. Hali kadhalika, inatarajiwa kuwa wastani wa mavuno ya mpunga yataongezeka kutoka tani 1.75 - 3.0 / ha. Ongezeko kama hilo kwa mazao mengine ni: tani 1.35 -2.20/ ha (mahindi), tani 1.0 -1.4 / ha (mbegu za mafuta / mikunde) na tani 15.0 -25.0 / ha (mazao ya bustani).

392 Uendelezaji wa miradi ya maji kwa ajili ya mifugo pamoja na utoaji wa huduma za msaada zinatarajiwa kusababisha ongezeko la tija katika ufugaji na kipato cha wafugaji . Kimsingi ongezeko katika tija ya uzalishaji mifugo litatokana na kukubalika kwa uendelezaji wa nyanda za malisho bora, uimarishaji wa lishe na afya bora ya mifugo. Miradi ya kuendeleza uvuvi inayotarajiwa inalenga katika kuongeza ufugaji wa samaki kupitia kuongeza mabwawa ya ufugaji wa samaki pamoja na huduma bora za msaada.

393 ASDP II pia inajumuisha shughuli za kupanua wigo wa wakulima kufikia masoko ya vijijini. kuboresha mifumo ya masoko na msaada wa serikali kwa wakulima katika kilimo biashara. Shughuli hizi zinatarajiwa kutoa faida kubwa kiuchumi, kama vile kuimarisha minyororo ya thamani ya mazao, kuongeza ongezeko la thamani, na kuboresha kipato na fursa za ajira kwenye kilimo biashara.Hata hivyo, faida za kiuchumi za hatua hizi hazijabainishwa katika uchambuzi wa kiuchumi na kifedha.

## Uchambuzi wa Kifedha

### Bajeti za Mazao

394 Uchambuzi wa fedha ulifanyika kutathmini mafanikio yanayotarajiwa kutokana na shughuli za ASDP II katika pato la shamba. Bajeti nne ziliandaliwa ili kuwakilisha mazao makuu yanayolimwa Tanzania, ambayo ni mahindi, mchele (mpunga), mbegu za mafuta/ mikunde na mboga mboga. Bajeti za mazao zimeandaliwa kwa kuzingatia hali ya sasa, siku zijazo bila kuwa na mradi huo, na siku zijazo kukiwa na mradi.

395 Pato halisi la la mazao kama asilimia ya pato ghafi limewekwa kwa muhtasari katika **Jedwali Na. 56** ni dhahiri kwamba, wakati wa siku zijazo katika hali ya kuwa na mradi, kuna mafanikio makubwa ya mapato halisi kwa mazao yote. Hii inaakisi ongezeko la tija linalotambulika linalotengeneza ongezeko la pato zaidi la gharama za uzalishaji zilizoongezeka. Pia ni dhahiri kwamba pato halisi kutokana na mbogamboga ni kubwa kuliko pato halisi la mazao mengine. Hata hivyo, pato kubwa litokanalo na mazao ya bustani linapunguzwa na athari zitokanazo na mabadiliko makubwa sana ya bei katika msimu. kwenye kilimo cha mazao ya ma inapunguzwa na hatari zinazohusiana simu mkubwa wa kushuka na kupanda kwa bei.

**Jedwali Na. 56: Faida Ghafi ya mazao wakati wasasa,wakati ujao bila mradi na wakati ujao kukiwa na mradi**

| | Pato Halisi Kama Asilimia ya Pato Ghafi (TSh kwa hekta) | | |
|---|---|---|---|
| | Wakati wa Sasa | Wakati ujao bila mradi | Wakati Ujao kukiwa na mradi |
| Mahindi | 67,088 | 119,831 | 216,550 |
| Mchele (Mpunga) | 322,500 | 423,844 | 709,375 |
| Mbegu za mafuta/jamii ya mikunde | 512,625 | 613,250 | 807,500 |
| Mboga mboga | 2,267,000 | 2,583,875 | 2,927,250 |

**Chanzo:** makadirio ya bajeti ya mazao

396 Inakusudiwa kwamba wakati ujao kukiwa na mradi, viwango vya tija vitakuwa vimefikiwa kikamilifu ndani ya miaka mitano ya kukamilisha uimarisha wa huduma za msaada katika kilimo, utekelezaji wa maboresho ya usimamizi wa ardhi na vyanzo vya maji, pamoja na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji iliyotajwa katika programu.

397 Katika uchambuzi wa kifedha, bajeti pia iliandaliwa kwa ajili ya miradi miwili ya ufugaji, yaani uzalishaji wa maziwa na unenepeshaji wa ng'ombe wa nyama (**Jedwali Na. 57**). Wakati ujao katika hali ya kuwa na mradi, kuboreshwa kwa mapato halisi kunaashiria kuwepo kwa viwango vya juu vya tija.

**Jedwali Na. 57: Faida ghafi ya Mifugo Wakati wa Sasa, Wakati Ujao Bila Mradi na Wakati Ujao Kukiwa na Mradi**

| Biashara ya mifugo | Pato Halisi Kama Asilimia ya Pato Ghafi (TSh kwa kichwa) | |
|---|---|---|
| | Wakati wa Sasa na Wakati Ujao bila mradi | Wakati Ujao kukiwa na mradi |
| Uzalishaji wa maziwa | 176,975 | 311,975 |
| Unenepeshaji wa mifugo | 77,900 | 102,900 |

Chanzo: Makadirio ya bajeti ya mifugo

## Mpangilio wa Upandaji Mazao

398 Katika eneo la umwagiliaji lililopo, inatarajiwa kuwa eneo la mazao ya mpunga, mbegu za mafuta / jamii ya mikunde na mboga litaongezeka katika msimu wamvua na kiangazi. Katika eneo lilopendekezwa kwa kilimo cha umwagiliaji, kutakuwa na mabadiliko makubwa ya mpangilio wa upandaji mazao kwa ongezeko kubwa la eneo la zao la mpunga katika msimu wa mvua na baadaye katika mazao ya mahindi, mpunga, mbegu za mafuta / mikunde na mboga. Ujazo wa upandaji mazao, yaani uwiano wa eneo ghafi lililopandwa kwa eneo halisi linalolimwa unatarajiwa kuongezeka kutoka 125% hadi 135%, ambapo katika eneo linalopendekezwa kulimwa kwa umwagiliaji ujazo wa upandaji mazao, yaani uwiano wa eneo ghafi lililopandwa kwa eneo halisi linalolimwa unatarajiwa kuongezeka kutoka 90% hadi 135%. Kwa maeneo yasiyolimwa kwa kilimo cha umwagiliaji, ujazo wa upandaji mazao, yaani uwiano wa eneo ghafi lililopandwa kwa eneo halisi linalolimwa, unakadiriwa kufikia 100% kukiwa na miradi. Kwa ujumla, ujazo wa upandaji mazao, yaani uwiano wa eneo ghafi lililopandwa kwa eneo halisi linalolimwa katika maeneo ya ASDP II unatarajiwa kuongezeka kutoka 92% hadi 103%.

## Uchambuzi wa Bajeti ya Shamba

399 Bajeti ya shamba iliandaliwa kwa eneo la shamba lenye ukubwa wa wastani wa hekta 2.0 na muhtasari wa pato halisi la shamba kwa ajili ya maeneo tofauti tofauti ya ASDP II umetolewa katika Jedwali Na. 58. Ukilinganisha hali ya wakati wa sasa na wakati ujao kukiwa na mradi, mapato halisi ya shamba katika eneo lililopo la umwagiliaji mapato yanatarajiwa kuongezeka kutoka shilingi 900,568 hadi shilingi 2,665,228 (kabla ya kutoa gharama za uendeshaji na matunzo za umwagiliaji) wakati, katika maeneo yasiyo ya umwagiliaji, pato halisi la shamba linakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi 367,385 hadi shilingi 1,158,275. Kwa ujumla, mapato halisi ya shamba yanatarajiwa kuongezeka kutoka shilingi 436,699 hadi shilingi 1,655,569 kwa mwaka.

400 Iwapo gharama za uendeshaji na matunzo za umwagiliaji zitajumuishwa, pato halisi la shamba katika maeneo ya umwagiliaji litashuka na kufikia shilingi 2,229,994 kwa mwaka. Hata hivyo, kwa kuwa gharama za uendeshaji na matunzo za umwagiliaji zinafikia 16% tu ya pato halisi la shamba, wakulima wataweza kukidhi gharama za uendeshaji na matunzo za umwagiliaji za kila mwaka.

**Jedwali Na. 58: Kipato Halisi cha Shamba cha Wakati wa Sasa, Wakati Ujao Bila Mradi na Wakati Ujao Kukiwa na Mradi**

| Hali ya Umwagiliaji | Pato Halisi la Mkulima/Shamba (TSh kwa Mwaka) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Wakati Ujao Kukiwa na Mradi | |
| | Wakati wa Sasa | Wakati Ujao Bila Mradi | Ukiondoa Gharama za Uendeshaji na Matunzo za Umwagiliaji | Ukijumuisha Gharama za Uendeshaji na Matunzo za Umwagiliaji |
| Eneo la umwagiliaji lililokarabatiwa | 900,568 | 1,138,498 | 2,665,228 | 2,229,994 |
| Eneo jipya la umwagiliaji | 367,385 | 496,902 | 2,665,228 | 2,229,994 |
| Eneo lisilo la umwagiliaji | 367,385 | 496,902 | 1,158,275 | |
| Kwa ujumla | 436,699 | 580,309 | 1,655,569 | |

Chanzo : makadirio ya bajeti ya shamba

### Uchambuzi wa Kiuchumi

### Upangaji Bei za Kiuchumi

401 Bei za kiuchumi za bidhaa za biashara ya Kimataifa zimepatikana kutoka katika makadirio ya bei za bidhaa ya Benki ya Dunia kwa mwaka 2015. Gharama za usafirishaji wa ndani, utayarishaji, uhifadhi na usindikaji zilizingatia viwango vya sasa vilivyopo Tanzania. Hata hivyo, bei hizi za kifedha zilibadilishwa kuwa bei za kiuchumi kwa kutumia Kiwango Sanifu Kilichowekwa cha Kubadilisha Fedha cha 0.95. Gharama za nguvu kazi zilizingatia viwango vya mishahara vya vijijini. Hata hivyo, kutokana na kiwango cha juu cha upungufu wa ajira, kiwango cha mshahara cha 0.65 kilitumika kuamua thamani ya kiuchumi ya nguvu kazi.

402 Uchambuzi wa kiuchumi ulifanyika mwaka 2015 kwa kuzingatia kipindi cha zaidi ya miaka 50 kwa bei zisizobadilika kutokana na mfumuko wa bei na punguzo la kiwango cha 12% lilitumika. Shilingi ya Kitanzania ilitumika na kiwango cha kubadilisha fedha cha shilingi za Kitanzania 2,150 kwa Dola 1.0 za Kimarekani (Juni, 2015) kilitumika. Ilitarajiwa kuwa progarmu ingetekelezwa katika kipindi cha miaka 10.

## C. Faida za Kiuchumi

403 Katika makadirio ya faida za kilimo, kiwango cha mapato halisi kiuchumi cha mazao kwa hekta kama asilimia ya mapato ghafi kilikokotolewa kwa kuthaminishwa na kiasi cha nyenzo za kuzalishia na kiasi kilichozalishwa kwa kuzingatia bei za kiuchumi za kila kimoja. Kisha kiwango cha mapato halisi kiuchumi ya mazao kwa hekta kama asilimia ya mapato ghafi kilizidishwa kwa maeneo ya mazao ili kukadiria faida halisi ya mazao kwa wakati wa sasa, wakati ujao kukiwa na mradi na wakati ujao bila mradi. Hali kadhalika, faida halisi za mifugo zilikadiriwa katika hali zote tatu za mradi (kulingana na idadi ya mifugo na kiwango cha mapato halisi kiuchumi ya mazao kwa hekta kama asilimia ya mapato ghafi).

404 Kutokana na ongezeko hilo katika uzalishaji wa mazao na ufugaji, faida halisi ya kilimo kwa wakulima katika eneo la mradi ilikuwa inakadiriwa kuongezeka kwa kiasi cha shilingi milioni 626,572 kwa mwaka (kutoka shilingi milioni 245,152 hadi shilingi milioni 859,700 kwa mwaka kwenye ukamilifu wa mradi). Imekusudiwa kwamba faida za kilimo katika wakati ujao kukiwa na mradi zingefikiwa kwa ukamilifu katika kipindi cha miaka miwili baada ya kukamilika kwa utekelezaji wa programu. Faida zinazotokana na uzalishaji wa mazao zinakadiriwa kufikia 81% ya faida za jumla za kilimo.

### D. Gharama za Uendeshaji

405 Gharama za muda mrefu za uendeshaji na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji kwa mwaka pia zilijumuishwa katika uchambuzi wa kiuchumi. Gharama hizi za kifedha, baadaye zilibadilishwa na kuwa katika thamani ya kiuchumi, na katika gharama za kiuchumi za uendeshaji na matunzo za mwaka. Hali kadhalika, gharama za kila mwaka za utoaji huduma stahiki zilijumuishwa katika uchambuzi ili kuhakikisha kuwa uzalishaji katika kilimo unaendelea kukua baada ya kumalizika kwa utekelezaji wa ASDP II.

### E. Uchambuzi wa kiuchumi na Matokeo ya Mradi katika Mazingira ya Uwekezaji

406 Matokeo ya uchambuzi wa kiuchumi yanaonyesha kuwa punguzo la riba (ya ASDP II) ambayo ni tofauti kati ya limbikizo la mapato yaliyothaminishwa kwa kiwango cha punguzo kwa wakati wa sasa katika kipindi chote cha Programu na gharama ya mtaji uliowekezwa kuwa sawa na sifuri ni kiasi cha 14.8%. Matokeo haya yanaonyesha kuwa uwekezaji wa mradi uliopendekezwa ni sahihi kwenye nyanja ya kiuchumi. Uchambuzi wa uathiriwaji wa matokeo ya mradi katika mazingira ya uwekezaji pia ulifanyika ili kupima uwezekano wa kiuchumi wa hatua zilizopendekezwa katika mabadiliko mbalimbali kwenye gharama na faida. Uchambuzi huu umeonyesha kwamba ASDP II inaathirika kwa kiwango cha kawaida kutokana na mabadiliko katika faida na gharama na kutokuwa na tija kiuchumi kwa kuogezeka kwa mtaji na gharama za kawaida kwa asilimia 21. Vilevile, kupungua kwa asilimia 18 ykwenye ongezeko la faida za mradi kutasababisha kiwango cha riba punguzo inayowezesha tofauti kati ya limbikizo la mapato yaliyothaminishwa kwa kiwango cha punguzo kwa wakati wa sasa katika kipindi chote cha Programu na gharama ya mtaji uliowekezwa kuwa sawa na sifuri kushuka chini ya asilimia 12.

407 Matokeo ya uchambuzi wa uathiriwaji wa matokeo ya mradi katika mazingira ya uwekezaji yameonyeshwa katika **Jedwali Na. 59,** yanayoonyesha kuwa kupungua kwa mtaji na gharama za kawaida kwa asilimia 20 kulisababisha kiwango cha punguzo la riba inayowezesha tofauti kati ya limbikizo la mapato yaliyothaminishwa kwa kiwango cha punguzo kwa wakati wa sasa katika kipindi chote cha Programu na gharama ya mtaji uliowekezwa kuwa sawa na sifuri, kuwa ni asilimia 18.8, wakati ongezeko la gharama kwa asilimia 20 lilishusha kiwango cha punguzo riba inayowezesha tofauti kati ya limbikizo la mapato yaliyothaminishwa kwa kiwango cha punguzo kwa wakati wa sasa katika kipindi chote cha Programu na gharama ya mtaji uliowekezwa kuwa sawa na sifuri, hadi kufikia asilimia 12.1. Kadhalika, asilimia 20 ya kuongezeka kwa nyongeza ya faida kulizalisha asilimia 18.0 ya kiwango cha punguzo la riba inayowezesha tofauti kati ya limbikizo la mapato yaliyothaminishwa kwa kiwango cha punguzo kwa wakati wa sasa katika kipindi chote cha Programu na gharama ya mtaji uliowekezwa kuwa sawa na sifuri, kuwa asilimia 18.0 na asilimia 20 za kupungua kwa faida kulipunguza kiwango cha punguzo la riba inayowezesha tofauti kati ya limbikizo la mapato yaliyothaminishwa kwa kiwango cha punguzo kwa wakati wa sasa katika kipindi chote cha Programu na gharama ya mtaji uliowekezwa kuwa sawa na sifuri, hadi kufikia asilimia 11.6. Zaidi ya hayo, mabadiliko yaliyotarajiwa katika uwiano wa eneo ghafi lililopandwa na eneo halisi linalolimwa yalifanyiwa tathmini na uchambuzi ulionesha kwamba, iwapo katika wakati ujao kukiwa na mradi, asilimia 100 ya uwiano wa eneo ghafi lililopandwa kwa eneo halisi linalolimwa utakadiriw, (ikilinganishwa na kiwango cha awali cha asilimia 103), kiwango cha riba punguzo inayowezesha tofauti kati ya limbikizo la mapato yaliyothaminishwa kwa kiwango cha punguzo kwa wakati wa sasa katika kipindi chote cha Programu na gharama ya mtaji uliowekezwa kitashuka hadi asilimia 10.7, wakati uwiano wa eneo ghafi lililopandwa na eneo halisi linalolimwa kwa asilimia 95 kitapunguza kiwango cha punguzo la riba inayowezesha tofauti kati ya limbikizo la mapato yaliyothaminishwa kwa kiwango cha punguzo kwa wakati wa sasa katika kipindi chote cha Programu na gharama ya mtaji uliowekezwa hadi asilimia 7.7.

408 Kwa kuzingatia tija ya zao, uchambuzi umeonyesha kwamba, kama tija ya mahindi na mchele tu inaongezeka kwa asilimia 50 (ikilinganishwa na viwango vya asilimia 57 na asilimia 67), kiwango cha punguzo la riba inayowezesha tofauti kati ya limbikizo la mapato yaliyothaminishwa kwa kiwango cha punguzo kwa wakati wa sasa katika kipindi chote cha Programu na gharama ya mtaji uliowekezwa inashuka hadi asilimia 10.7, na ASDP II inakuwa haina faida kiuchumi. Hivyo basi inapaswa kusisitiziwa kwamba matumizi ya mbinu bora za kilimo na ongezeko linalotarajiwa kwenye mavuno ya

zao (kudumisha uwezekano wa mradi kiuchumi) yanaweza kufikiwa iwapo tu huduma sahihi za kilimo, ikiwa ni pamoja na huduma za ugani / mafunzo na usambazaji wa pembejeo pamoja na kuboresha ufikiwaji wa masoko na huduma za kifedha vijijini, zitafikishwa kwa wakulima kwa njia fanisi na fasaha.

**Jedwali Na. 59: Uwezekano Kiuchumi na Uchambuzi Uathiriwaji waMatokeo ya Mradi Katika Mazingira yaUwekezaji**

| Hali | EIRR (%) | NPV (TSh millioni) |
|---|---|---|
| Hali ya Msingi | 14.8% | 370,009 |
| Mtaji na gharama za kawaida -20% | 18.8% | 722,428 |
| Mtaji na gharama za kawaida +20% | 12.1% | 17,589 |
| Manufaa yanayoongezeka +20% | 18.0% | 796,430 |
| manufaa yanayoongezeka -20% | 11.6% | -56,413 |
| Gharama - 20% na manufaa ya kilimo ya ziada +20% | 22.6% | 1,148,850 |
| Gharama + 20% na manufaa ya kilimo ya ziada -20% | 9.3% | -408,832 |
| Uwiano wa eneo ghafi lililopandwa kwa eneo halisi linalolimwa kwa100% kukiwa na Mradi | 14.3% | 299,966 |
| Uwiano wa eneo ghafi lililopandwa kwa eneo halisi linalolimwa kwa 95% kukiwa na mradi | 11.8% | -21,536 |
| Ongezeko la 50% katika tija ya mazao | 10.7% | -531,096 |
| Ongezeko la 40% katika tija ya mazao | 7.7% | -165,650 |

## F. Uendelevu wa Programu

409 Uendelevu wa muda mrefu wa programu utatokana na namna ambavyo unatoa matokeo, yaani, kuboresha utoaji wa huduma za kilimo na kilimo-biashara kwa ajili ya ukuaji endelevu wa tija na matokeo yake katika uongezaji wa uzalishaji wa mashambani, mapato na uhimilivu, hususan katika mifumo ya uzalishaji wa mazao na mifugo kwa kutegemea mvua. Kuboresha mwitikio wa huduma muhimu katika kukidhi mahitaji ya wakulima, pamoja na kuwezesha uwekezaji katika kilimo-biashara, miundombinu, huduma za kitaaluma na mazingira ya sera yanapaswa kuboresha matokeo kiujumla. Katika muda wa kati, uwezeshaji wa wakulima wadogo na uunganishaji wa Asasi za wakulima utawapa sauti na uwezo mkubwa wa kutoa huduma za kiufundi na kiuchumi kwa wanachama.

410 ASDP II ina lengo la kufikia ongezeko endelevu katika uzalishaji wa kilimo na biashara kwa wakulima wadogo wengi (angalau asilimia 20). Hili litafikiwa kwa kueneza teknolojia zinazofaa, zenye gharama nafuu na zenye faida kwa wakulima wadogo, na zinazoweza kudumu kwa muda mrefu. Aidha, ASDP II itatumia kanuni endelevu za kilimo shadidi kwa kuwawezesha wakulima kuendeleza mifumo ya uzalishaji wa mazao tofauti kwa wingi, huku mazingira wezeshi yakijengwa kwa ajili ya kuongeza biashara vijijini, ambapo wakulima wanaweza kufikia masoko ya biashara za pembejeo na mazao, kupelekea tija na faida bora ya kilimo kwa ajili ya biashara.

411 ASDP II inashughulikia wigo wa maendeleo na ustawi endelevu wa kijamii kwa kuhakikisha kuwa mahitaji ya chakula na lishe kwa kila kaya yanajitosheleza na watu wa vijijini wanalindwa dhidi ya athari za majanga ya asili na upungufu mkubwa wa chakula, ambazo zinaweza kupunguza mali za kaya na kurudisha nyuma mafanikio yaliyopatikana kwa kutumia nguvu nyingi. Kwa umuhimu wake , programu inashughulikia ueneaji mkubwa wa lishe duni na utapiamlo, ambavyo huzuia tija na kutishia uendelevu wa maendeleo ya binadamu katika kaya na jamii za vijijini. Ili Tanzania ifikie matarajio yake ya maendeleo kuna haja ya kuwa na ongezeko kubwa la kiwango cha uwekezaji katika kilimo na uhakika wa chakula. ASDP inalenga kutoa nyongeza ya raslimali kwa ajili ya kuboresha matokeo katika maeneo yote ya programu ili kufikia lengo la programu.

412 Kwa muhtasari, ASDP II imeweka mwongozo katika juhudi zinazoendelea za kuongeza ushindani na faida katika sekta na inaelekeza majukumu ya Serikali na washirika wa maendeleo kufadhili ili kutatua changamoto za mageuzi ya sekta ya kilimo ndani ya mbinu iliyoratibiwa.

# VIII. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA ASDP II NA ATHARI ZAKE

## A. Upimaji wa Utekelezaji na Wadau

413 Utekelezaji wa ASDP II utafuata miundo/mifumo ya serikali ya manunuzi, usimamizi wa fedha na hifadhi ya mazingira na jamii. Mpango uliopendekezwa utahitaji maboresho katika utoaji wa taarifa kwenye matokeo na athari. Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utajumuishwa na mfumo wa kufuatilia matokeo ya mpango. Aidha, uratibu wa sekta uliopo chini ya ASDP II utahitajika kuendana na mfumo mzima wa ASDP II katika ngazi ya taifa na serikali za Mitaa kwa ajili ya ufanisi wa utekelezaji na ufasaha wa uwasilishaji wa matokeo.

**414 Kwa kuzingatia ASDP-1.** ASDP-II imeandaliwa kwa kutumia uzoefu, mafanikio, uwezo na mifumo iliyoendelezwa katika kipindi cha ASDP-1, kwa kufuata kipaumbele cha uwekezaji wa serikali ili kupata matokeo ya haraka. Wakati lengo, mbinu na wigo wa ASDP II unatofautiana sana na ule wa ASDP-1, mifumo na miundo ya uwasilishaji kwa kiasi kikubwa itabaki sawa, itaimarishwa ili kujenga uwezo wa kupata matokeo yaliyotarajiwa ya utekelezaji wa Programu. Muundo wa Programu umejumuishwa kwa ajili ya uimarishaji wa taasisi ya mawakala wa utekelezaji wa shughuli za kujenga uwezo kwa wakulima na maeneo mengine muhimu ya kiufundi pamoja na ufuatiliaji na uratibu wa matokeo.

**415 Tathmini ya wadau wa programu.** Utekelezaji wa programu utajumuisha wadau, washirika na wanufaikaji mbalimbali wa ngazi tofauti. Hii ikiwa ni pamoja na taasisi za kiserikali (ngazi ya Taifa. mkoa, wilaya na mitaa), sekta binafsi, wafanyabiashara wa pembejeo na mazao, PSPs, viwanda/ wasindikaji wa kilimo, FOs, NGO, taasisi za fedha na nyingine. Uwezo wa wadau unatofautiana kwa kila ngazi ya utekelezaji ushiriki wa sekta binafsi kwenye kilimo unabaki kuwa mdogo na upungufu wa mfumo wa uratibu wa wadaukatika ngazi ya mtaa. Mfumo wa sasa wa uratibu wa sekta nzima utaboresha uhusiano miongoni mwa wahusika wengi wanaounga mkono sekta ya kilimo.Pia kuna jitihada za kuanzisha jukwaa la mnyororo wa thamani hasa kwenye wilaya ili kuimarisha uhusiano wa wadau.

416 Uwezo wa watu na kitaasisi ulioendelezwa wakati wa awamu ya kwanza ya ASDP utatumika katika utekelezaji wa mapendekezo. ASLMs zitaimarishwa ili kuongeza ujuzi wake wa kufanya uchambuzi, usimamizi na uratibu wa matokeo. Masuala ya kifedha, ufuatiliaji na tathmini na ustadi mwigine muhimu wa kiufundi, kama vile uchambuzi wa mnyororo wa thamani wa bidhaaa, utaimarishwa kwa ajili ya ufanisi na uendelevu. ASDP II itahitaji kutilia mkazo katika uimarishwaji wa utoaji wa taarifa za uhakika zinazohusu matokeo kwa wakati unaohitajika. Uratibu wa sekta chini ya Programu katika ngazi ya taifa na mitaa unahitaji kuhakikiwa na kufanywa kwa ufanisi zaidi ili kuzidisha utoaji na uwasilishaji wa taarifa.

**417 Washirika wa maendeleo.** Washirika wengi wa maendeleo walionyesha nia ya kusaidia juhudi za Serikali za kuendeleza sekta ya kilimo kwa njia ya mtazamo mpana wa sekta kama vile ASDP II kuanzia 2015 / 2016-2024 / 2025. Hata hivyo, baadhi ya michango hii tayari imetengwa au kuandaliwa kama miradi ya inayojitegemea, kama vile michango ya JICA (hasa uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji ), IFAD (mradi wa sukari wa wakulima wadogo Bagamoyo)[73] na IDA na *Bill na Melinda Gates Foundation (BMGF*). Kwa hiyo, fedha ambazo siyo za mfuko wa pamoja zinatarajia kutoka kwa washirika wa maendeleo na kutoka katika bajeti ya Serikali ya Tanzania. Kwa hiyo, fedha ambazo siyo za kwenye mfuko wa pamoja zinatarajiwa kutoka kwa washirika wa maendeleo na katika bajeti ya Serikali ya Tanzania[74]. Mikataba ya maelewano inayoainisha kanuni kwa ajili ya kusimamia Mfuko wa Pamoja itawekwa saini na kila mshirika wa maendeleo anayechangia katika Mfuko wa Pamoja.

---

*73 Mradi unaoendelea kuandaliwa na IFAD kwa ajili ya mkono wa wakulima wadogo wa miwa Bagamoyo ni jaribio la kuhusisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) kutokana na uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa mradi wa kilimo cha mafuta ya mawese nchini Uganda na sukari nchini Swaziland*

*74 Michango ya washirika wa maendeleo na NGO zitatolewa nje ya bajeti ya serikali kama vile fedha za USAID kupitia makubaliano na Mfuko wa Barabara kuendeleza miundombinu ya barabara za vijijini katika maeneo ya SAGCOT.*

## B. Athari

418 Athari zinazohusiana na programuni:

i. Sera za sekta na mazingira ya kiuchumi hazikuwa nzuri kwa ajili ya kuendeleza kilimo-biashara. Hali hii inaweza kusababisha ushiriki duni wa washirika wa kilimo-biashara katika shughuli za programu, hususan katika majukumu yaliyokusudiwa katika mnyororo wa thamani na kibiashara wa wakulima wadogo. Ili kupunguza athari hii, programu imependekeza kuanzisha ruzuku za kilimo ili kutoa nafasi kwa majukwaa ya mnyororo wa thamani wa bidhaa wa wilaya,wadau na wakulima wa biashara kushiriki katika shughuli za programu. Ruzuku hizi zitatumika katika kuongeza kasi ya ufadhili wa uwekezaji kwenye kilimo-biashara utakaofanywa na vyama vya wakulima. Majukwaa ya mnyororo wa thamani wa bidhaa ya wilaya yatatumika kama kichocheo cha ushirikiano katika ngazi za chini. Wakati wa utekeleza , majukwaa ya wadau wa mnyororo wa thamani wa bidhaa wa kiwilaya ni muhimu katika kufikia mafanikio ya programu, hata hivyo jukwaa la mnyororo wa thamani wa bidhaa lina asili ya ugumu katika suala la ufuatiliaji na kutoa motisha. Zaidi ya hayo, mabadiliko katika mazingira ya sera yanahitajika, hasa kuhusiana na mauzo ya nje na kodi za ndani kwa bidhaa za kilimo, kuchukua hatua za makusudi kama vile kusamehe ushuru na kuzuia kuuza nje, nk, kwa ajili ya uboreshaji endelevu.

*Upungufu wa sera za kutoa motisha kwa ajili ya ushiriki wa wadau binafsi wa Kilimo-biashara katika shughuli za programu, hususani jukumu lao lililokusudiwa katika maendeleo ya mnyororo wa thamani litadhoofisha ufanikishaji wa malengo ya mpango wa biashara. Mazungumzo ya kuboresha mazingira ya uwekezaji wa sekta binafsi yataendelea, na serikali ina nia ya kuimarisha uwekezaji binafsi katika kilimo kupitia mipango mbalimbali kama Kilimo Kwanza na SACGOT.*

ii. Programu itatekelezwa chini ya muundo changamani wa taasisi, sekta mbalimbali, Mfuko wa Pamoja, sambamba na miradi kadhaa ambayo iko nje ya bajeti ya Serikali (ndani - na nje ya bajeti). Hii inaweza kusababisha mgongano wa ajenda na maslahi, na hivyo kudhoofisha uwezo wa ndani wa kusimamia na kuratibu shughuli za programu. Ili kupunguza athari hii: (a) shughuli za programu zimeanishwa katika mfumo jumuishi wa Serikali; (b) kuimarisha uratibu na kuoanisha miradi na programu za sekta katika mfumo wa uratibu wa sekta nzima, pamoja na mbinu za msaada katika ngazi mbalimbali; (c) programu itasaidia Serikali za Mitaa (chini ya Eneo kuu la 4) kuendeleza mfumo wa uratibu wa sekta kwakina kwa kuunganisha shughuli za miradi yote kwenye sekta katika ngazi za chini kwenye DADPs; (d) Mikataba ya maelewano itawekwa saini na kila mfadhili wa mfuko wa pamoja wa ASDP na serikali na kukubaliana juu ya kanuni ya uendeshaji na usimamizi kwa ujumla; na (e) mipangilio ya kitaasisi na taratibu za uratibu wa utekelezaji katika ASDP-1 itaimarishwa.

*iii.* *Upunguaji wa kiwango cha utekelezaji wa bajeti,* ucheleweshaji na utoaji usiokamilika wa fedha za maendeleo zikiwemo fedha za kigeni inaweza ikapelekea matatizo katika mtiririko wa fedha kwa wanufaika wa programu na hivyo kuzuia ufikiwaji wa madhumuni ya programu.Ili kukabiliana na changamoto hii, serikali imebadilisha mzunguko wake wa bajeti, kuanza mapema (mwezi wa nne) ili kuongeza mtiririko wa fedha kwa wakati na kuboresha utekelezaji wa bajeti. Hata hivyo, kalenda ya kifedha ya washirika wa maendeleo mara nyingi haiendani na kalenda ya serikali hivyo utolewaji wa fedha za wafadhili haziendani na na muda wa utekelezaji wa bajeti. Hivyo, majadiliano ya mara kwa mara ya masuala haya kupitia PRSC ni muhimu.

*iv.* *Ufuatiliaji wa matokeo bado umebakia kuwa changamoto* kwenye sekta kutokana na uwezo hafifu wa uchambuzi na usimamizi wa ukusanyaji wa takwimu. Ili kukabiliana na hilo, taasisi zitaimarishwa kwa kujengewa uwezo ili kuboresha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa kuchambua na kusambaza matokeo. Mipango pia inatakiwa ipangwe katika mfumo wa kawaida wa serikali wa ufuatiliaji na tathmini ambao utaimarisha usimamizi, uwazi na uwajibikaji kwa matokeo.

v. Mtazamo wa usimamizi wa athari za kilimo unaweza kujumuishwa rasmi katika ASDP II kwa kuwa inatambulika kwamba athari za uzalishaji na bei ni vigezo vya uhaba wa chakula na kupata hasara ya fedha kwa washiriki katika minyororo mikuu ya thamani ya bidhaa. Kuanzisha mfumo wa

kukabiliana na athari kutachangia katika uwekezaji endelevu kwenye uzalishaji. Maeneo muhimu ya kujumuishwa kwa ajili ya usimamizi wa athari yanatakiwa kutambuliwa katika kila kanda ya ikolojia ya kilimo na mfumo wa uzalishaji. Mazao mseto, kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima wadogo, kilimo hai, usimamizi jumuishi wa udongo na maji, pamoja na na kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi tayari vimeanishwa chini ya utafiti na huduma za ushauri, maghala yaliyounganishwa na soko la bidhaa. Yote haya yatachangia katika ustahimilivu na ustawi wa mfumo wa uzalishaji wa kilimo.

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO Na. I: Mpangilio wa Utekelezaji wa Maeneo Makuu ya ASDP II, Mpango wa Utekelezaji, Mtiririko

### SEHEMU YA NNE MPANGILIO WA MIRADI (Mazingira wezeshi, uratibu, ufuatiliaji na tathmini)

**Lengo la eneo:** Uimarishaji wa mazingira wezeshi ya sekta,uratibu na ufuatiliaji na tathmini
**Matokeo:** Uimarishaji wa taasisi, uwezeshaji, uratibu na ufuatiliaji na tathmini
**Viashiria muhimu vya utekelezaji katika eneo:**

- Mapitio na uhuishwaji wa sera za kilimo, sheria, kanuni na taratibu za kitaasisi,
- Uboreshaji viashiria vya ufanyaji biashara kwa vigezo vya "Benki ya Dunia" ili kuwezesha Kilimo-biashara
- Ongezeko la tija katika sekta, thamani / bei, faida na uwezo wa ukuaji kwa kutokana na kuongeza maarifa ya usimamizi na matumizi ya TEHEMA
- Mfumo jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini katika Sekta

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO YA KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mwaka 1 | mwaka 2 | mwaka 3 | mwaka 4 | mwaka 5 | |
| 4.1 Sera na Sheria | i) Mapitio na uhuishwaji sera, sheria, na taratibu za taasisi zinazohusiana na sekta ya kilimo | **4.1.1** Sera na Mfumo wa Udhibiti na Maboresho ya Mazingira ya Biashara | **4.1.1.1** Mapitio na uhuishwaji sera zinazohusiana na sekta ya kilimo na mfumo wa udhibiti wa mazingira bora ya biashara | | | | | | Wezeshi kwenye maeneo mengine, mazingira ya sera yanaruhusu maboresho |
| | | | **4.1.1.2** Kuimarisha Ufuatiliaji, Udhibiti na Usimamizi wa uvuvi haramu (IUU Uvuvi) | | | | | | Mradi unaoendelea |
| | ii) Kiwango (%) cha kuzingatia sera na Udhibiti (k.m., "viwango vya kufuata") | | **4.1.1.3** Kuendeleza Mwongozo wa Uvuvi Tanzania Bara | | | | | | Ni njia ya mwogozo ya sekta ndogo za uvuvi |
| | | | **4.1.1.4** Kuimarisha na udhibiti wa ajira ya watoto katika Kilimo | | | | | | Inategemeana na marekebisho na kuoanishwa kwa sera na kanuni husika |
| | | | **4.1.1.5** Kuimarisha usalama kazini na kuhamasisha ajira zenye staha katika sekta ya kilimo | | | | | | Inategemeana na marekebisho na kuoanishwa kwa sera na kanuni husika |
| | | | | | | | | | |

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mwaka 1 | mwaka 2 | mwaka 3 | mwaka 4 | mwaka 5 | |
| 4.2 Kuwezesha wadau na vikundi | Uboreshaji wa usimamizi wa maarifa na mifumo ya TEHAMA | **4.2.1** Kuimarisha uwezo wa shirika na wa kiufundi wa wazalishaji wadogo waliopo na wapya, biashara na usindikaji, Mashirika ya wakulima na vyama vya ushirika | **4.2.1.1** Kuimarisha Ushirika, vyama vya wakulima na vyama vingine wahusika katika mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo | | | | | | Ni muhimu kwa ajili ya utekelezajii wa programu |
| | Kamati ya Utendaji na mikutano ya ushauri iliofanyika na maazimio yaliyotekelezwa kwa ngazi za kitaifa na za mitaa. | | | | | | | | |
| | • Ufanisi wa biashara wa serikali katika kutoa huduma kwa wateja na (k.m. majibu ya haraka kwa matatizo na utoaji wa suluhisho) | | | | | | | | |
| | Taarifa za gharama nafuu kwa wakati, zenye uhusiano, sahihi na za kirafiki zinapatikana kwa wadau kwa wakati na mahali zinapohitajika | | | | | | | | |
| | DADPs zinazofikia vigezo vya tathmini | **4.2.2** Kukuza na kuimarisha ushirikiano wa kijinsia katika sekta ya kilimo | **4.2.2.1** Kuboresha faida kwa wanawake na vijana kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa za kilimo (WAYA) | | | | | | Inatekelezwa katika maeneo yote ya utekelezaji (1,2,3) |
| | | | | | | | | | |
| 4.3 uratibu wa sekta wa ASDP II (kupanga na utekelezaji katika ngazi kitaifa,mkoa na tawala za serikali za mitaa) | Uwekezaji wa kilimo kuratibiwa chini ya ASDP II (ndani/nje ya bajeti) Utekelezaji wa bajeti iliyobuniwa | **4.3.1** Kuboresha na kuimarisha uratibu wa wima (kutoka TAMISEMI hadi kwa RSs na LGA) na uratibu kati ya ASLMs | **4.3.1.1** Kuimarisha mifumo ya taasisi ya sekta ya kilimo kwa uratibu na mawasiliano (wima na mlalo) bora | | | | | | Ni muhimu kwa ajili ya utekelezajii wa programu |
| | Ubora na uwasilishwaji kwa wakati wa ripoti za kila wakati katika ngazi zote | | | | | | | | |
| | Kuanzisha Kitengo cha uratibu wa kupanga na ufuatiliaji | | | | | | | | |

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mwaka 1 | mwaka 2 | mwaka 3 | mwaka 4 | mwaka 5 | |
| | • Kiwango cha kufuata Mwongozo katika ngazi zote | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| 4.4 Ufuatiliaji na Tathmini (ikiwa ni pamoja na takwimu za Kilimo) | AASS iliyotekelezwa | **4.4.1** Uwezo na mifumo bora ya ukusanyaji na usimamizi wa takwimu za kilimo | **4.4.1.1** Kuboresha uwezo na ushirikiano wa mifumo ya ukusanyaji na usimamizi wa takwimu za kilimo (m.f G ARDS, NSCA, AASS) kwa usimamizi bora wa matokeo katika ngazi zote. | | | | | | Ni muhimu kwa ajili ya utekelezajii wa programu |
| | RS na LGA kutoa takwimu bora kupitia mifumo tofauti ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa wakati | **4.4.2** Kuendeleza mfumo wa Ufatiliaji na Tathmini wa sekta ya Kilimo | **4.4.2.1** Kuimarisha na kuunganisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya sekta ya kilimo kwa ufanisi na ufasaha | | | | | | Ni muhimu kwa ajili ya utekelezajii wa programu |
| | Mifumo ya pamoja ya Ufatiliaji na Tathmini imeanzishwa na inafanya kazi | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| 4.5 Kujenga uwezo wa kitaasisi,na usimamizi wa TEHAMA | | **4.5.1** Uboreshaji wa Uwezo katika ngazi zote | **4.5.1.1** Kuboresha uwezo wa kitaifa, RS na tawala za mitaa (idadi na ubora) kwa ngazi zote | | | | | | Ni muhimu kwa ajili ya utekelezajii wa programu |
| | | **4.5.2** Uboreshaji wa TEHAMA kwa Huduma na mifumo ya taarifa za Kilimo | **4.5.2.1** Kuendeleza usimamizi kamili wa maarifa na mfumo wa TEHAMA katika ngazi zote | | | | | | Ni muhimu kwa ajili ya uratibu wa programu |
| 4.6. Upatikanaji wa fedha vijijini | | **4.6.1** Kutoa huduma za ufadhili | **4.6.1.1** Upatikanaji wa fedha za kilimo kwa ajili ya mnyororo wa thamani wa bidhaa | | | | | | Ni muhimu kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya kilimo |

## ENEO KUU LA TATU MPANGALIO WA MIRADI (Biashara na Uongezaji Thamani kwenye mazao)

**Lengo la eneo:** Kuboresha na kupanua masoko ya vijijini na kukuza thamani kwa kutumia ushindani wa sekta binafsi na ufanisi wa vikundi vya wakulima
**Matokeo:** Kuimarisha ushindani katika mnyororo wa thamani wa bidhaa
**Viashiria muhimu vya utekelezaji:**

- Asilimia ya ongezeko la thamani na kiasi cha fedha za mauzo ya nje
- Asilimia ya ongezeko la thamani la fedha kutokana na uwekezaji wa nje (FDI) na mtiririko wa pesa binafsi kwa sekta ya kilmo
- Asilimia ya ongezeko la ajira mpya na kupanua uwekezaji katika kilimo biashara
- Asilimia ya kupunguza kiasi na thamani ya kifedha ya kuagiza chakula nje
- Asilimia ya ongezeko la faida ya mazao na bidhaa kwa mkulima na kiwango cha shirika
- Asilimia ya ongezeko la sehemu ya soko ya bidhaa katika ngazi zote za soko
- Asilimia ya ongezeko la bidhaa zinazozingatia viwango vya kitaifa na kimataifa
- Asilimia ya ongezeko la miundombinu sanifu ya masoko ndani ya mnyororo wa thamani
- Asilimia ya ongezeko la ushiriki wa makundi maalum (Wanawake, Vijana, na Wafugaji) kwenye biashara na uongezaji kwenye mazao thamani katika kufanya maamuzi na kunufaika na programu katika mnyororo wa thamani

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mwaka 1 | mwaka 2 | mwaka 3 | mwaka 4 | mwaka 5 | |
| 3.1 Masoko | Mabadiliko ya % katika uwekezaji wa miundombinu ya masoko | **3.1.1** Kuendeleza upatikanaji wa masoko kwa bidhaa zote za kipaumbele | **3.1.1.1** Kuboresha na kuendeleza miundombinu ya masoko kwa ajili ya kupata masoko ya ndani na ya nje | | | | | | vifaa vya kuhifadhia ni muhimu kubwa kwa ajili ya kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna, ubora na wingi wa mazao |
| | % wakulima/ FO/ Idadi ya wafanyabiashara wanaotumia miundombinu bora ya soko katika maeneo ya vijijini | **3.1.2** Kuendeleza upatikanaji wa soko kwa ajili ya uvuvi na bidhaa za mifugo | **3.1.2.1** Kuboresha na Kuendeleza miundombinu ya masoko ya mifugo na Samaki kwa ajili ya mapato ya ndani | | | | | | vifaa vya kuhifadhia ni muhimu kubwa kwa ajili ya kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna, ubora na wingi wa mazao |
| | | | **3.1.2.2** Kuboresha eneo na upatikanaji/ufikiaji wa soko la kuku | | | | | | Mradi wa kufanikiwa haraka utakaoleta matokeo kwa jamii nyingi za vijijini |

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mwaka 1 | mwaka 2 | mwaka 3 | mwaka 4 | mwaka 5 | |
| | | | **3.1.2.3** Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji(utambulisho) wa mifugo & uvuvi wa kukuza biashara na uuzaji | | | | | | Kuhakikisha ubora / usalama; kuwezesha kufika katika soko |
| | | | **3.1.2.4** Kukuza na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika mnyororo wa thamani wa bidhaa | | | | | | Kichocheo muhimu katika sekta |
| | | | **3.1.2.5** Kuboresha upatikanaji wa soko la nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo | | | | | | Inategemeana na kuboreshwa kwa miundombinu ya mifugo |
| | | | | | | | | | |

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mwaka 1 | mwaka 2 | mwaka 3 | mwaka 4 | mwaka 5 | |
| 3.2 Maendeleo ya kilimo - biashara Kuongeza thamani na usindikaji wa mazao | Ongezeko la thamani ya mazao na bidhaa | 3.2.1 Maendeleo ya usindikaji na kuongeza thamani ya mazao, mifugo na bidhaa za uvuvi | **3.2.1.1** Kuimarisha na kuendeleza viwanda vya usindikaji wa mazao kwa kuongeza thamani ya bidhaa zote kipaumbele | | | | | | Mauzo ya nje; Ajenda ya Viwanda |
| | % Kupungua kwa upotevu wa mazao baada ya mavuno | | **3.2.1.2** Kuboresha mnyororo wa thamani wa maziwa | | | | | | Upungufu wa miundombinu ya msingi |
| | | | **3.2.1.3** Kuimarisha mnyororo wa thamani wa kwato na ngozi | | | | | | Uhaba wa vifaa vya msingi; Havifanyi kazi |
| | | | **3.2.1.4** Kuimarisha mnyororo wa thamani wa bidhaa za kilimo cha bustani | | | | | | Mipango inayoendelea kuna matumaini makubwa ya baadaye kwa Tanzania |
| | | | **3.2.1.5** Kujenga maghala ya kimkakati yatakayo huianishwa na soko la bidhaa za maghalani | | | | | | Kuongeza upatikanaji wa soko na kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna |

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mwaka 1 | mwaka 2 | mwaka 3 | mwaka 4 | mwaka 5 | |
| | | | **3.2.1.6** Kuendeleza na kuhamasisha kuongeza thamani katika bidhaa za samaki na ufugaji wa samaki | | | | | | Kuna uhakika wa upatikanaji wa soko kwa ajili ya nyama na samaki |
| | | | **3.2.1.7** Kuongeza thamani katika nyama, mbuzi | | | | | | Malighafi inapatikana kwa urahisi |
| | | | **3.2.1.8** Kuimarisha usimamizi wa kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna katika mnyororo wa usambazaji ili kuwa na uendelevu katika chakula na lishe | | | | | | |

**ENEO KUU LA 2 MPANGILIO WA MIRADI (kuchochea tija na faida ya kilmo)**

**Lengo:** Kuongeza kiwango cha ukuaji wa tija katika ukuaji kwenye kilimo-biashara kwa ajili ya masoko ya bidhaa za kipaumbele

**Matokeo:** Ongezeko la tija na faida

**Viashiria muhimu vya utekelezaji:**

- Ongezeko la tija (MT / ha , lita / ng'ombe / utoaji wa maziwa, mayai / kuku / siku, uzito / ng'ombe katika hatua ya soko, kg / samaki) katika minyororo ya thamani ya mazao ya kipaumbele
- Ongezeko la faida ghafi (TSh / ha, TSh / maziwa ng'ombe, TSh / LU, nk ) kwa ajili ya minyororo ya thamani
- Ongezeko la Faida kuu (TSh / bidhaa au biashara) ya bidhaa za kipaumbele
- Ongezeko la ufanisi wa kazi (TSh / mkulima / msimu) na faida kwa wakulima
- Kupungua kwa utapiamlo (%) (udumavu na uzito mdogo)

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | |
| 2.1 Mafunzo ya ugani na huduma za mawasiliano | 1 Asilimia ya wakulima wanaotumia teknolojia ya kuongeza tija | **2.1.1** Kuimarisha huduma za ugani, mafunzo na uendelezaji / huduma za taarifa (mazao, mifugo na uvuvi) | **2.1.1.1** Kuimarisha na kukuza huduma za ugani wa kilimo (bidhaa zote) | | | | | | Ili kufanya kilimo kiwe cha biashara kuna haja ya kusambaza matokeo ya utafiti kwa wakulima wadogo kama vile kupitia ushiriki wa sekta binafsi |
| | 2. 2.Asilimia wakulima waliridhishwa [2] na huduma za ugani | | **2.1.1.2** Kuimarisha mafunzo ya ustadi wa kilimo na ukuzaji (bidhaa zote) | | | | | | Kuzingatia wakulima wadogo |
| | 3.Asilimia ya teknolojia zilizosambazwa na zilizopitishwa | | | | | | | | |
| | 4. Asilimia ya wafanyakazi wa ugani wanaotoa huduma bora za ugani | | | | | | | | |
| | 5. Kupungua kwa matukio ya wadudu na magonjwa (mzunguko na hasara) ya umuhimu wa kiuchumi | | | | | | | | |
| | 6. Ongezeko la wastani wa mapato ya kaya kwa wakulima ambao wanatumia teknolojia | | | | | | | | |

| KIPENGELE KIDOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | |
| 2.2 Upatikanaji wa pembejeo za kilimo na huduma za afya ya mazao, mifugo na samaki | 1.Asilimia ya wakulima wanaotumia pembejeo bora za kilimo | **2.2.1** Upatikanaji wa pembejeo bora na huduma za afya ya mazao, mifugo na uvuvi | **2.2.1.1** Kuboresha uwepo na upatikanaji wa pembejeo za kilimo zenye ubora na za bei nafuu kwa ajili ya kuongeza tija na faida (bidhaa zote) | | | | | | Kuongezeka kwa tija na faida |
| | Asilimia ya wakulima wanaonufaika na ruzuku ya pembejeo | | **2.2.1.2** Kuboresha upatikanaji na uwepo wa pembejeo za kuku zenye ubora | | | | | | Ukosefu wa pembejeo na gharama kubwa |
| | | | **2.2.1.3** Kuendeleza uvuvi wa samaki aina ya Jodari kwa ajili ya kuongeza tija | | | | | | Kutangaza biashara ya uvuvi wa kina cha bahari kupitia ushiriki wa sekta binafsi |
| | | | **2.2.1.4** Kuimarisha na kuanzisha bandari za uvuvi kwa aili ya faida bora ya uvuvi | | | | | | Inayoendelea |
| | | | **2.2.1.5** Maendeleo ya bandari ya uvuvi wa baharini kwa ajili ya kuongezeka kwa faida | | | | | | Utafiti wa uwezekano unafanyika |
| | | | **2.2.1.6** Kuboresha Uvuvi (kwa wavuvi wadogo) ili kuboresha uzalishaji wa samaki na tija | | | | | | Inahitajika kuongeza tija kwa wavuvi wadogo kwa kutumia vifaa vya kuchanganya samaki (FADs) |
| | | | **2.2.1.7** Kuimarisha vitengo vya Usimamizi wa fukwe (BMUs) kwa usimamizi endelevu, usalama na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi | | | | | | inayoendelea |

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | |
| | | | **2.2.1.8** Uboreshaji wa huduma za afya ya mimea | | | | | | Milipuko ya magonjwa na wadudu ni masuala ambayo yanaweza kuathiri ukuaji na uzalishaji. Kuzalisha teknolojia kwa njia ya utafiti na matumizi ya njia nzuri za kilimo yatapunguza kiwango cha tishio / hatari. |
| | | | **2.2.1.9** Uzalishaji wa chanjo na madawa | | | | | | Gharama kubwa ya kuagiza kutoka nje |
| | | | **2.2.1.10** Uboreshaji wa huduma za afya ya samaki na mifugo | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| 2.3 Utafiti wa Kilimo kwa Maendeleo (AR4D) | 1.Asilimia ya teknolojia mpya iliyotolewa na kusambazwa na vituo vya utafiti | **2.3.1** Kuimarisha AR4D (mazao, mifugo na uvuvi) | **2.3.1.1** Kuimarisha uwezo wa utafiti wa kilimo kwa maendeleo ya teknolojia, uhusiano wa viwanda na uhamishaji matokeo (sekta ndogo ndogo zote) | | | | | | Utafiti ni muhimu katika kuzalisha teknolojia ya kuongeza tija na ubunifu kutokana na mahitaji ya kizazi kipya cha teknolojia na kuboresha uhusiano wa utafiti-wafugaji kwa ajili ya kuendesha biashara na usambazaji wa teknolojia. |
| | 2. Uboreshaji wa uwezo [1] wa vituo vya utafiti ili kuzalisha teknolojia | **2.3.2** utafiti na maendeleo | **2.3.2.1** Maendeleo ya teknolojia jumuishi na usambazaji kwa ajili ya tija na uzalishaji ulioongezeka (bidhaa zote) | | | | | | Teknolojia iko wazi kwa ajili ya uzalishaji ulioongezeka |

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAENEO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | |
| | 3.Asilimia ya bajeti iliyotengwa (matumizi ya kawaida na maendeleo) kwa Utafiti na Maendeleo | | **2.3.2.2** Kukuza na kuimarisha uwezekano wa mazao ya ufugaji kupitia teknolojia ya uzalishaji wa kisasa | | | | | | Inayoendelea |
| | | | | | | | | | |
| 2.4 Upatikanaji wa Huduma za utumiaji wa mashine | 1.Asilimia ya kaya zinazopata huduma za mashine / kuasa katika minyororo ya thamani ya bidhaa | **2.4.1** Kuimarisha na kukuza uchumi wa kilimo (mazao, mifugo na uvuvi) | **2.4.1.1** Kuimarisha na kukuza uchumi wa kilimo kwa ajili ya kuboresha mnyororo wa thamani | | | | | | Matuimiz ya zana/ mashine katika mnyororo wa thamani |
| | 2.Asilimia ya kaya zinazopata huduma za usindikaji katika mnyororo wa thamani wa bidhaa za kipaumbele | | | | | | | | |
| | 3.Asilimia ya upotevu iliyopungua ya bidhaa katika mnyororo wa thamani | | | | | | | | |

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | |
| **2.5 Usalama wa chakula na lishe** | 1. Ongezeko la asilimia ya kaya juu ya mstari wa umasikini wa chakula | **2.5.1** Usalama wa chakula na lishe bora | **2.5.1.1** Kuboresha upatikanaji, ubora na matumizi ya vyanzo vya vyakula vyenye virutubisho muhimu (bidhaa zote) | | | | | | |
| | 2. Kuongezeka kwa uwiano wa chakula cha kutosha kitaifa | | **2.5.1.2** Kuongezeka kwa uzalishaji na kukuza mtama kwa chakula na matumizi ya ndani | | | | | | Kuongezeka kwa mahitaji ya lishe na viwanda vya lishe |
| | 3. Kupunguza vikwazo vya utapiamlo (sugu na kati) | | | | | | | | |
| | 4. Asilimia ya kupungua kwa upungufu wa virutubisho vidogo kwa watoto na wanawake wajawazito | | | | | | | | |
| | 5. Asilimia ya kaya zinazopata chakula chenye lishe na cha aina tofauti | | | | | | | | |
| | 6. Asilimia ya kaya zinazofanya mifumo ya kilimo tofauti kwa ajili ya chakula bora na kupunguza uwezekano wa uhaba wa chakula. | | | | | | | | |
| | 7.Asilimia ya kaya zinazopata mifugo na protini za samaki. | | | | | | | | |

## ENEO KUU LA 1 MPANGILIO WA MIRADI (usimamizi endelevu wa matumizi ya ardhi na maji)

**Lengo:** Kuboresha usimamizi endelevu wa matumizi ya Ardhi na Maji (Umwagiliaji, Maji kwa ajili ya Mifugo, Ardhi iliyopandwa mazao, malisho, Mabwawa / visima, usimamizi wa rutuba ya udongo)
**Matokeo:**Ukuaji endelevu wa matumizi ya maji na ardhi, na kuboresha usimanizi wa Mazao, Mifugo na Uvuvi
**Viashiria muhimu vya utekelezaji :**

- Asilimia ya ongezeko la skimu za kilimo endelevu cha umwagiliaji
- Asilimia ya ongezeko la wafugaji wenye vyanzo vya kudumu vya maji (vya asili au kujengwa)
- Asilimia ya vifaa vya kisasa vya umwagiliaji na kuwepo kwa usimamizi wa utaalamu
- Kuboresha malisho endelevu na maji kwa ajili ya mifugo
- Kuongezeka eneo (ha) la ufugaji wa samaki
- Kuongeza idadi ya wafugaji wa samaki baharini
- Asilimia ya ongezeko la wadau wanaotumia teknolojia za kilimo cha kuhimili mabadiliko ya tabianchi

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | |
| **1.1 Mpango wa matumizi ya ardhi na usimamizi endelevu wa vyanzo vya maji na udongo** | Ongezeko la asilimia za wilaya zenye mipango ya matumizi ya ardhi | **1.1.1** Mpango wa matumizi ya ardhi na usimamizi wa mabwawa | **1.1.1.1** Mpango jumuishi wa matumizi ya ardhi na usimamizi kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo endelevu na maendeleo ya viwanda (bidhaa zote/kanda zote) | | | | | | Mipango ya matumizi ya ardhi ni msingi wa utekelezaji mzuri wa miradi |
| | Ongezeko la asilimia ya vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi | | **1.1.1.2** Uimarishaji katika uzalishaji wa malisho na uhifadhi kwa ajili ya uzalishaji endelevu wa mifugo | | | | | | Kupunguza migogoro kupitia upatikanaji wa malisho |
| | Ongezeko la asilimia ya mabwawa yenye mipango jumuishi ya usimamizi | | **1.1.1.3** Kuchochea upatikanaji wa ardhi ya kilimo kwa ajili ya uwezeshaji wa vijna | | | | | | Uboreshaji wa mazingira wezeshi |
| | Ongozeko la eneo(ha) la uzalishaji bora wa kilimo | | **1.1.1.4** Kuboresha uratibu wa mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa mabwawa kwa matumizi endelevu ya rasilimali | | | | | | Kuhakikiha upatikanaji wa maji kwa ajili ya shughuli za kilimo |
| | Ongezeko la asilimia kwenye kiasi cha maji kwaajili ya uzalishaji wa kilimo | | | | | | | | |

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | |
| 1.2 Matumizi jumuishi ya maji na ardhi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji mazao na mifugo | Kuongezeka kwa eneo (ha) la kilimo cha umwagilijai | **1.2.1** Maendeleo ya miundombinu ya umwagiliaji | **1.2.1.1** Ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili kuongeza uzalishaji na tija | | | | | | Inajumuisha miradi inayoendelea |
| | Uwiano wa eneo lililopandwa na lisilopandwa kwa mazao ya umwagiliaji | | **1.2.1.2** Ukuzaji wa mfumo wa umwagiliaji kwa ajili ya uzalishaji na tija bora ya mazao mazao | | | | | | Ongezeko la uhitaji wa hizi teknolojia kwa ajili ya uhifadhi wa maji |
| | Vituo vya maji vya ziada vya kudumu kwa ajili ya mifugo | **1.2.2** Usimamizi na Uendeshaji wa umwagiliaji | **1.2.2.1** Kuimarisha Usimamizi na Uendeshaji wa umwagiliaji | | | | | | Kuhakikisha uhimilivu wa miundombinu ya umwagiliaji |
| | Ongezeko la eneo (ha) kwa ajili ya ufugaji wa samaki | **1.2.3** Kuendeleza vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo na uvuvi | **1.2.3.1** Kuendeleza miundombinu kwa ajili a uzalishaji wa mifugo na samaki | | | | | | Kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo na kupunguza migogoro |
| | Kuongezeka kwa idadi ya wafugaji wa samaki wa baharini | | **1.2.3.2** Kuendeleza na kujenga vituo vya kisasa vya maji kwa ajili ya mazao, mifugo na uvuvi | | | | | | Kujumuisha miradi inayoendelea |

| ENEO DOGO | VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI | MAENEO KIPAUMBELE YA UWEKEZAJI | MIRADI ILIYOPENDEKEZWA | Mtiririko | | | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 | |
| 1.3 Kujumuisha uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili | Ongezeko la asilimia ya wazalishaji (mazao, mifugo na uvuvi) wanaotumia teknolojia za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi | **1.3.1** Kuendeleza kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi | **1.3.1.1** Kukuza na kuendeleza matumizi ya teknolojia za kuhimili mabadiliko ya tabianchi | | | | | | 1. Kuunganisha CSA na CA kwa ajili ya usimamizi wa rutuba ya udongo<br>2. Kuwepo kwa mfumo wa kutoa tahadhari mapema |
| | Uwiano wa LGA ambazo zimeingiza CSA katika DADPs zao | | **1.3.1.2** Kuendeleza mifumo ya ikolojia kwa ajili ya uvuvi na kilimo | | | | | | Kuongeza mgawanyo wa makazi ya samaki |
| | Uwiano wa ASLM ambazo mipango yao inajumuisha CSA | | **1.3.1.3** Kuimarisha mfumo mpana wa kutoa taarifa ya tahadhari mapema na maandalizi ya kukabiliana na dharura | | | | | | |
| | Kupungua kwa asilimia za kaya ambazo zipo chini ya hatari ya mafuriko au ukame | | | | | | | | |

Mambo yaliyozingatiwa katika mtiririko wa miradi: Mpango wa matumizi ya ardhi umewekwa kwanza kwa kuwa ni msingi wa uwekezaji, inafuatiwa na ukarabati wa miradi ya umwagiliaji inayoendelea na kujenga skimu mpya. Eneo la tatu ni la kueneza matumizi ya teknolojia zinazohimili mabadiliko tabianchi na hifadhi kwa nia ya kuhuisha matumizi ya teknolojia za kilimo hifadhi (CA) kwenye hatua za awali za kuandaa mipango.

# KIAMBATISHO Na. II: Mfumo wa ufuatiliaji wa matokeo ya ASDP II

Angalizo: Mfumo huu wa matokeo kwa sasa unataja bidhaa chache muhimu kama mfano kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa. Uteuzi wa Mnyororo wa thamani wa bidhaa utakuwa unabadilishwa inapohitajika mara baada ya mfumo kuimarika . Mfumo ni wa miaka mitano ya Programu. Mfumo umefanyiwa tathmini na kubainika kuwa ulikuwa na mapungufu ya takwimu ambazo malengo yanatakiwa kuandaliwa.

**Malengo ya Programu (PDO) au Shabaha: kubadilisha sekta ya kilimo (mazao, mifugo na uvuvi) kuelekea tija ya juu, ushindani, na kibiashara na kuboresha kipato, maisha, na usalama wa chakula na lishe kwa wakulima wadogo.**

**Viashiria muhimu vya utekelezaji wa lengo kuu:**

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji wa takwimu na utoaji taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 1 | Kiwango cha ukuaji | Sekta ya kilimo | Kuendeleza ustahimilivu wa ukuaji wa Pato la Taifa kwa mwaka angalau kwa 6%, kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka 2025. . | 2.1 | Mabadiliko ya asilimia ya Pato la Taifa la sekta hiyo | (GDP ya sasa- GDP ya awali/ GDP ya awali)*100 | Kwa mwaka | ASLMs /NBS |
| | | Mazao | 6% | 1.4 | Mabadiliko ya asilimia ya Pato la Taifa la sekta ndogo ya mazao | (GDP ya sasa- GDP ya awali/ GDP ya awali)*100 | Kwa mwaka | ASLMs/NBS |
| | | Mifugo | 6% | 2.6 | Mabadiliko ya asilimia ya Pato la Taifa la sekta ndogo ya mifugo | (GDP ya sasa- GDP ya awali/ GDP ya awali)*100 | Kwa mwaka | ASLMs/NBS |
| | | Uvuvi | 6% | 4.2 | Mabadiliko ya asilimia ya Pato la Taifa la sekta ndogo ya uvuvi | (GDP ya sasa- GDP ya awali/ GDP ya awali)*100 | Kwa mwaka | ASLMs/NBS |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji wa takwimu na utoaji taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 2 | Tija | Mahindi | Kuongezeka mara mbili (100%) kwa kiwango cha sasa cha mazao ya kilimo, kuanzia mwaka 2016 mpaka mwaka 2025 | 1.72 | Uzalishaji kwa eneo | Uzalishaji kwa ujumla katika tani kugawa kwa eneo katika Ha | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | Mpunga | Ongezeko la 100% katika MT/ha | 3.06 | Uzalishaji kwa eneo | Uzalishaji kwa ujumla katika tani kugawa kwa eneo katika Ha | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | Alizeti | Ongezeo la 100% katika MT/ha | | Uzalishaji kwa eneo | Jumla ya uzalishaji katika tani kugawa kwa eneo katika Ha | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | Maziwa | ongezeko la 50% lita/ng'ombe /siku | 2.25 | Uzalishaji kwa mnyama kwa siku (ng'ombe asili) | Lt/ng'ombe/siku/ | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | Nyama | Kuongezeka kwa 100% katika kg/ mnyama | 145 | Uzalishaji wa nyama kwa mnyama | Kg/mnyama | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | Mbuzi | Kuongezeka kwa 100% katika kg/ mnyama | 37 | Uzalishaji wa nyama kwa mnyama | Kg/mnyama | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | Kondoo | Kuongezeka kwa 100% katika kg/ mnyama | 40 | Uzalishaji wa nyama kwa mnyama | Kg/mnyama | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | Kuku | Kuongezeka kwa 100% katika kg/ndege | 1.5 | Uzalishaji wa nyama kwa ndege | Kg/ndege | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | Samaki wa baharini | Kuongezeka kwa uvuvi wa samaki hadi tani 1,000,000 ifikapo mwaka 2025 | 362,000 | Kiasi katika MT cha uvuvi kwa mwaka | uvuvi kwa mwaka | Kwa mwaka | ASLMs- wavuvi |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji wa takwimu na utoaji taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 3 | Jumla ya uzalishaji wa kila mwaka | mahindi | Uzalishaji wa mahindi kuongezeka (100% kuongezeka) (MT) | 6,100,000 | Jumla ya uzalishaji katika MT | Jumla ya uzalishaji kwenye eneo | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | mpunga | Uzalishaji wa mpunga kuongezeka (100% kuongezeka) (MT) | 3,400,000 | Jumla ya uzalishaji katika MT | Jumla ya uzalishaji kwenye eneo | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | maziwa | (28% kuongezeka) uzalishaji wa maziwa (lita) | 2,087,000 | Jumla ya uzalishaji katika lita kwa mwaka (ng'ombe wa asili) | Jumla ya lita zote za maziwa zinazozalishwa | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | nyama | Uzalishaji wa nyama kuongezeka (100% kuongezeka) (MT) | 319,112 | Jumla ya uzalishaji wa nyama katika MT | Jumla ya nyama zote zinzozalishwa katika MT | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | Mbuzi/ kondoo | (50% kuongezeka) uzalishaji wa nyama ya mbuzi/kondoo(MT) | 124,74 | jumla ya mbuzi / kondoo uzalishaji wa nyama ya mbuzi/ kondoo katika MT | Jumla ya mbuzi/kondoo wanaozalishwa katika MT | Kwa mwaka | ARDS/AASS |
| | | Kuku | (50% kuongezeka) uzalishaji wa nyama ya kuku (MT) | 104,292 | Jumla ya uzalishaji wa nyama ya kuku katika MT | Jumla ya kuku wanaozalishwa katika MT | Kwa mwaka | ARDS/AASS |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji wa takwimu na utoaji taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 4 | Ukuaji wa asilimia ya mauzo ya kilimo (Thamani kwa dola) | mahindi | Ziada ya kusafirisha nje kwa 100% kufikia mwaka 2025 | 1,056,559 | | Mavuno kutoa mahitaji (hasa kwa ajili ya nafaka) | Kwa mwaka | TRA/ASLMs |
| | | mchele | Kusafirisha nje mara tatu zaidi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Mabadiliko ya asilimia ya mauzo ya nje | Pato la Taifa (GDP) la sasa -Pato la taifa la msingi/Pato la Taifa la msingi * 100 | Kwa mwaka | TRA |
| | | Pamba | Kusafirisha nje mara tatu zaidi ifikapo mwaka 2025 | 23.4 | Mabadiliko ya asilimia ya mauzo ya nje | Pato la Taifa (GDP)la sasa -Pato la taifa la msingi/Pato la Taifa la msingi * 100 | Kwa mwaka | TRA |
| | | Kilimo cha bustani (viazi mviringo) | Kusafirisha nje mara tatu zaidi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Mabadiliko ya asilimia ya mauzo ya nje | Pato la Taifa (GDP)la sasa -Pato la taifa la msingi/Pato la Taifa la msingi * 100 | Kwa mwaka | TRA |
| | | nyama | Kusafirisha nje mara tatu zaidi kufikia mwaka 2025 | GAP | Mabadiliko ya asilimia ya mauzo ya nje | Pato la Taifa la sasa-Pato la taifa la msingi/Pato la Taifa la msingi * 100 | Kwa mwaka | TRA |
| | | Samaki wa baharini | Kusafirisha nje mara tatu zaidi kufikia mwaka 2025 | GAP | Mabadiliko ya asilimia ya mauzo ya nje | Pato la Taifa la sasa-Pato la taifa la msingi/Pato la Taifa la msingi * 100 | Kwa mwaka | TRA |
| 5 | Kiasi kilichoingizwa kutoka nje | mchele | Kupungua kwa uingizaji wa mchele hadi 50% ifikapo mwaka 2025 | 1,277,296 | Kiasi cha mchele kilizoagizwa kwa tani | Uagizaji wa sasa kutoa msingi wa uagizaji | Kwa mwaka | TRA |
| | | mahindi | Kupungua kwa uingizaji wa mahindi hadi 50% ifikapo mwaka 2025 | GAP | Kiasi cha mahindi kilizoagizwa kwa tani | Uagizaji wa sasa kuto msingi wa uagizaji | Kwa mwaka | TRA |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji wa takwimu na uwasilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 6 | Kupunguza kiwango cha pengo kati ya bei ya jumla na bei ya shambani | mahindi | Kushiriki katika kupunguza umasikini kwa kupunguza pengo kati ya bei ya jumla na bei ya shambani, kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2025 | GAP | Tofauti kati ya bei ya jumla na bei ya shambani | (Bei ya jumla kutoa bei ya shambani) kugawanywa na bei ya shambani * 100 | Kwa mwaka | MITI |
| | | mchele | Kiwango kinapungua kwa 50% | GAP | Tofauti kati ya bei ya jumla na bei ya shambani | ((Bei ya jumla toa bei ya shambani) kugawanywa na bei ya shambani * 100 | Kwa mwaka | MITI |
| | | maziwa | Kiwango kinapungua kwa 50% | GAP | Tofauti kati ya bei ya jumla na bei ya shambani | (Bei ya jumla toa bei ya shambani) kugawanywa na bei ya shambani * 100 | Kwa mwaka | MITI |
| | | Nyama | Kiwango kinapungua kwa 50% | GAP | Tofauti kati ya bei ya jumla na bei ya shambani | (Bei ya jumla toa bei ya shambani) kugawanywa na bei ya shambani * 100 | Kwa mwaka | MITI |
| 7 | Asilimia ya idadi ya watu vijijini chini ya mstari wa umaskini | Mstari wa umaskini wa Taifa | Kupunguza kiwango cha umaskini kwa asilimia 50%, katika mstari wa umaskini wa kitaifa, kutoka mwaka wa 2016 ifikapo mwaka 2025. | 28.2 | Kiwango cha idadi ya watu vijijini chini ya mstari wa umaskini wa kitaifa | (Uwiano mkuu wa umasikini katika uwiano wa kitaifa wa umaskini wa 2016 katika taifa la 2025) / umaskini mkuu uwiano kwa kitaifa 2016 * 100 | Kwa mwaka | HBS-NBS |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji wa takwimu na uwasilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 8 | Chakula cha Taifa cha kujitegemea | Nafaka na kilicho sawa na nafaka | Kuongeza utoshelevu wa chakula (SSR) kati ya 100% hadi 120% au zaidi | 124 | Uwiano wa jumla ya uzalishaji wa ndani wa chakula umefananishwa na mahitaji ya chakula cha ndani. | Jumla ya uzalishaji wa chakula kutoa mahitaji ya jumla ya chakula juu ya mahitaji ya jumla ya chakula | Kwa mwaka | ASLMs(usalama wa chakula) |
| 9 | Sehemu ya Kaya zinazopata mchanganyiko hafifu wa vyakula | Kipimo cha wigo wa mchanganyiko wa chakula cha Kaya | Kupunguza nusu ya Jamii wasiopata wigo mpana wa mchanganyiko wa vyakula vyenye lishe bora kwa mwaka kuanzia 2016 hadi 2025 | Vijijini: (21.4%)<br><br>Mijini: (8.6%) | Kaya zisizopata wigo mpana wa mchanganyiko wa vyakula vyenye lishe bora | Idadi ya Kaya zisizopata wigo mpana wa mchanganyiko wa vyakula vyenye lishe bora kugawa kwa Idadi ya Kaya zote | Kwa mwaka | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, jinsia, Wazee na Watoto (Taasisi ya Chakula na Lishe ya Tanzania - TFNC)/ Wizara ya Kilimo |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji wa takwimu na uwasilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 10 | Kupatikana kwa wenye utapiamlo (mkali na wa mpito) katika Tanzania | Udumavu | Kupunguza asilimia ya watoto wanaodumaa hadi kufikia 10%, ifikapo mwaka 2025. | 34 | Kuenea kwa walio na udumavu (% ya Watoto walio chini ya miaka 5) | | Kwa mwaka | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, jinsia, Wazee na Watoto (Taasisi ya Chakula na Lishe ya Tanzania - TFNC)/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Uzito mdogo | Kupunguza asilimia ya watoto wenye uzito mdogo hadi 5% au pungufu zaidi ifikapo mwaka 2025. | 14 | Kuenea kwa walio na uzito mdogo (% ya Watoto walio chini ya miaka 5) | | Kwa mwaka | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, jinsia, Wazee na Watoto (Taasisi ya Chakula na Lishe ya Tanzania - TFNC)/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Ukondefu | Kupunguza asilimia ya watu wenye ukondefu hadi 5% au pungufu zaidi ifikapo mwaka 2025 | 5 | Kuenea kwa walio na ukondefu (% ya Watoto walio chini ya miaka 5) | | Kwa mwaka | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, jinsia, Wazee na Watoto (Taasisi ya Chakula na Lishe ya Tanzania - TFNC)/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| 11 | Sehemu ya Watu wanaopata lishe duni | | Kupunguza asilimia ya watu wanaopata lishe duni hadi kufikia 5% au pungufu zaidi ifikapo mwaka 2025. | 5.5 | Sehemu ya Watu waliopata lishe duni (% ya watu katika nchi) | | Kwa mwaka | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, jinsia, Wazee na Watoto (Taasisi ya Chakula na Lishe ya Tanzania - TFNC)/ Wizara za Sekta ya Kilimo |

## ENEO LA KWANZA

### Usimamizi endelevu wa matumizi ya maji na na ardhi

**Lengo Kuu la Eneo la Programu: Uboreshaji na Usimamizi Endelevu Husishi wa Matumizi ya Raslimali Maji na Ardhi** ***(kama vile maji kwa ajili ya umwagiliaji, maji kwa ajili ya mifugo, mabwawa /visimba kwa ajili ya ufugaji samaki, ardhi kwa ajili ya kilimo, malisho ya mifugo, rutuba ya udongo n.k)***

### Viashiria Vikuu vya Utekelezaji

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| **Mpango wa Matumizi ya Ardhi na Usimamizi wa vyanzo vya Maji** | | | | | | | | |
| 1 | Sehemu ya Vijiji vyenye ardhi iliyopimwa. | | Kuhakikisha kwamba 100% ya ardhi za Vijiji zimepimwa ifikapo 2025. | GAP | % ya vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya mazao, mifugo, uvuvi, maeneo ya hifadhi na vyanzo vya maji | Jumla ya idadi vyenye mipango ya matunmizi bora ya ardhi gawa kwa idadi ya jumla ya vijiji vilivyosajiliwa sehemu ya Vijiji vyenye ardhi iliyopimwa. | Kwa mwaka | Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi – Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi |
| 2 | Sehemu ya Kaya za wakulima (kwa jinsia) zenye kumiliki ardhi | Hati miliki ya ardhi za kimila | Kuhakikisha kwamba 100% ya wakulima na Wajasiriamali katika kilimo wenye nia ya kujishughulisha na kilimo wanapata fursa ya kutumia ardhi wanayohitaji ifikapo 2025. | GAP | Idadi ya hati miliki za kimila zilizotolewa kwa wanaomiliki ardhi | Jumla ya idadi ya hati miliki za kimila zilizotolewa kwa kaya kugawanya kwa jumla ya idadi ya kaya zote | Kwa mwaka | Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi – Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi |
| | | Hati miliki za ardhi | Kuhakikisha kwamba 100% ya wakulima na Wajasiriamali katika kilimo wenye nia ya kujishughulisha na kilimo wanapata fursa ya kutumia ardhi wanayohitaji ifikapo 2025. | GAP | Idadi ya hati miliki za kimila zilizotolewa kwa wanaomiliki ardhi | Jumla ya idadi ya hati zilizotolewa kwa kaya kugawanya kwa jumla ya idadi ya kaya zote | Kwa mwaka | Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi – Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| **Matumizi ya Maji kwa ajili ya Kilimo cha Mazao, Mifugo na Uvuvi/ufugaji samaki** | | | | | | | | |
| 4 | Idadi ya skimu za kilimo zinazotumia kilimo cha umwagiliaji | Mpunga | Skimu za umwagiliaji 549 (yaani 276 zilizokarabitiwa na 273 mpya ) zinaendeshwa kwa uendelevu ifikapo mwaka 2025 | GAP | Idadi ya Skimu za Kilimo zinazotumia kilimo cha Umwagiliaji kwa uendelevu (zina umoja wa wamwagiliaji waliosajiriwa, wanakusanya ushuru kutoka kwa wanaumoja, wana akaunti ya benki na mpango wa matunzo ya skimu yao | Jumla ya skimu zote zilizoendelezwa | Kwa mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS)/Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/Wizara ya Maji na Umwagiliaji/Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. |
| 5 | Idadi miundombinu ya skimu za umwagiliaji iliyoendelezwa kikamilifu | | Miundombinu ya Skimu za umwagiliaji 549 kuendelezwa kikamilifu ifikapo mwaka 2025 | GAP | Idadi ya jumla ya miundombinu ya umwagiliaji iliyoendelezwa kikakilifu | Jumla ya skimu zote zilizoendelezwa | Kila robo mwaka/ Kwa mwaka | Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/Wizara ya Maji na Umwagiliaji/Tume ya Taifa ya Umwagiliaji |
| 6 | Eneo linalomwagiliwa | Hekta | Kuongeza eneo linalomwagiliwa hadi kufikia hekta 1,000,000 ifikapo mwaka 2025 | 468,338 | Eneo la umwagiliaji lililoendelezwa (Hekta) | Jumla ya Eneo linalomwagiliwa | Kwa mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS)/Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/Wizara ya Maji na Umwagiliaji/Tume ya Taifa ya Umwagiliaji/ Wizara za Sekta ya Kilimo |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| **Matumizi ya Maji kwa ajili ya Kilimo cha Mazao, Mifugo na Uvuvi/ufugaji samaki** | | | | | | | | |
| 7 | Kamati Hai za Umoja wa Wamwagiliaji | Idadi ya Kamati Hai za Umoja wa wamwagiliaji | Kamati 549 za wamwagiliaji maji kuwa hai ifikapo mwaka 2025 | GAP | Idadi ya jumla ya Kamati za wamwagiliaji maji | Jumla ya Kamati za Umoja wa Wamwagiliaji maji | Kila mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS)/ Wizara ya Maji na Umwagiliaji/Tume ya Taifa ya Umwagiliaji |
| 8 | Idadi ya Vituo vya kunyweshea maji mifugo | Malambo na visima virefu | Ongezeko la 100% la vituo vya kunyweshea maji mifugo ambavyo viko ndani ya umbali wa 3 km ifikapo mwaka 2025 | 1443 | Idadi ya malambo na visima virefu vya maji kwa ajili ya mifugo | Jumla ya malambo na visima virefu kwa ajili ya maji ya mifugo | Kila mwaka | Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS)/ |
| 9 | Eneo la mita za mraba kwa ajili ya ufugaji samaki | Perege na Kambale | Kuongeza maradufu eneo la ufugaji wa samaki ifikapo mwaka 2025 | 4,540,400 | Eneo la ardhi linalotumika kwa ajili ya ufugaji wa samaki | Jumla ya Mita za Mraba za Eneo la ardhi linalotumika kwa ajili ya ufugaji wa samaki | Kila mwaka | Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| **Kuingiza dhana za uhimili dhidi ya mabadiliko ya tabianchi na kukabiliana na majanga ya kiasili katika utekelezaji** | | | | | | | | |
| 10 | Asilimia ya Kaya za Wakulima, Wafugaji na wavuvi ambazo zinahimili mabadiliko ya tabianchi na misukosuko inayohusiana na hali ya hewa. | Kilimo, Mifugo | Kuhakikisha kuwa 30% ya Kaya zinahimili mabadiliko ya tabianchi na misukosuko inayohusiana na hali ya hewa ifikapo mwaka 2025. | GAP | Idadi ya Wakulima, Wafugaji na wavuvi wanaotumia kilimo cha umwagiliaji au uvunaji wa maji, mbegu zinazokomaa mapema au ufugaji wa ndani | Jumla ya Wakulima, ambao wanahimili mabadiliko ya tabianchi | Kila mwaka | Wizara za Sekta ya Kilimo -Mazingira Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS)/ Wizara ya Maji na Umwagiliaji |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| **Matumizi ya Maji kwa ajili ya Kilimo cha Mazao, Mifugo na Uvuvi/ufugaji samaki** | | | | | | | | |
| 11 | Sehemu ya ardhi ya kilimo inayotumika kwa mbinu na usimamizi endelevu | Kilimo | Kuhakikisha angalau asilimia 30 ya ardhi ya kilimo inatumika kwa mbinu na usimamizi endelevu | 5.40% | ardhi ya kilimo inayotumika kwa kilimo kwa kuzingatiwa mbinu na usimamizi endelevu | Inakokotolewa kama: ardhi ya kilimo inayotumika kwa kilimo kwa kuzingatiwa mbinu na usimamizi endelevu kugawa kwa jumla ya ardhi yote ya kilimo | Kwa mwaka | Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| 12 | Sehemu ya Halmashauri zilizoingiza shughuli za Kilimo zinazozingatia Mabadiliko ya Tabianchi katika Mipango yao ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) | Sekta ya Kilimo | Shughuli za Kilimo zinazozingatia Mabadiliko ya Tabianchi kuingizwa katika Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) ya Halmashauri zote ifikapo mwaka 2025. | GAP | DADPs zenye bajeti ya uwekezaji au uhamasishaji wa matumizi ya teknolojia za kuvuna maji, umwagiliaji wa matone na matumizi ya mbegu zinazokomaa mapema | Jumla ya Halmashauri zilizoingiza shughuli za kilimo zinazozingatia Mabadiliko ya Tabianchi katika Mipango yao ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) | Kwa mwaka | Wizara za Sekta ya Kilimo / Wizara za Sekta ya Kilimo - Idara za Sera na Mipango (Tathmini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya -DADPs ) |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| **Matumizi ya Maji kwa ajili ya Kilimo cha Mazao, Mifugo na Uvuvi/ufugaji samaki** | | | | | | | | |
| 13 | Kuwepo kwa vifungu vya bajeti ya Serikali kwa ajili ya shughuli za kujenga uhimili | | Kuweka vifungu vya kudumu vya Serikali kwa ajili ya shughuli za kujenga uhimilivu hususan katika mipango ya utayari dhidi ya majanga ya asili, Mfumo hai wa kutoa tahadhari ya mapema wa kutambua na kukabiliana na majanga, Mitandao ya usalama wa Jamiii na Bima kwa ajili ya madhara yatokanayo na hali ya hewa kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2025. | GAP | Kuwepo kwa vifungu vya bajeti ya Serikali kwa ajili ya Sera na Mkakati , EIRB1; Kuwepo kwa vifungu vya bajeti ya Serikali kwa ajili ya Mfumo wa kutoa tahadhari mapema ya kutambua na kukabiliana na majanga, Mitandao ya usalama wa Jamiii na Bima kwa ajili ya madhara, EIRB2; Bajeti kwa ajili ya Utafiti na Umwagiliaji, EIRB3; Kuwepo kwa vifungu vya bajeti ya Serikali kwa ajili yashughuli za kujenga uhimilivu wa majanga (%),EIRB = wastani (EIRBi) i=1 hadi 3 | | Kwa mwaka | Wizara za Sekta ya Kilimo |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Takwimu Msingi (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 14 | Idadi ya kaya za Wakulima, Wafugaji na Wavuvi | Wakulima | Kuwa na idadi inayokubalika kwa kuzingatia uharibifu wa mazingira | GAP | Idadi ya Wafugaji/ Wavuvi | | Kwa mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS)/Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS) |
| | | Wafugaji | Kuwa na idadi inayokubalika kulingana na uwezo wa upatikanaji wa malisho | GAP | Idadi ya Wafugaji/ Wavuvi | | Kwa mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS)/Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS) |
| | | Wavuvi | Kuwa na idadi inayokubalika kwa kuzingatia uharibifu wa mazingira | 25,259 | Maji baridi (perege na kambale) na maji chumvi (mwani), Kamba na Mwatiko (milk fish) | | Kwa mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS)/Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS) |

## ENEO LA PILI
## Jina la Eneo: Kuchochea tija na faida katika uzalishaji wa kilimo

**Lengo Kuu la Eneo la Programu: Kuongeza tija na faida kupitia kilimo biashara na kilimo kinachozingatia mahitaji ya masoko (kilimo, mifugo na uvuvi)**

### Viashiria Vikuu vya Utekelezaji wa Lengo la Mpango

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| **Uzalishaji na Tija** | | | | | | | | |
| 1 | Kasi ya ukuaji kwa Tija ya mazao ya kipaumbele | Mahindi, Mpunga, Alizeti, Maziwa, Nyama ya ngombe, Nyama ya mbuzi, nyama ya kondoo, samaki wa maji chumvi (rejea lengo Kuu la Mpango 2) | | | | | | |
| | | Muhogo | Ongezeko kwa 100% la tani/ha | 5.95 | Uzalishaji kwa eneo | Jumla ya Tani zilizozalishwa kwa hekta moja | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Mikunde (maharage) | Ongezeko kwa 100% la tani/ha | 1.11 | Uzalishaji kwa eneo | Jumla ya Tani zilizozalishwa kwa hekta moja | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Mtama/Uwele | Ongezeko kwa 100% la tani/ha | 1 | Uzalishaji kwa eneo | Jumla ya Tani zilizozalishwa kwa hekta moja | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Kilimo cha mbogamboga-matunda-viungo-(viazi mviringo) | Ongezeko kwa 100% la tani/ha | 13 | Uzalishaji kwa eneo | Jumla ya Tani zilizozalishwa kwa hekta moja | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| | | Pamba | Ongezeko kwa 100% la tani/ha | 1 | Uzalishaji kwa eneo | Jumla ya Tani zilizozalishwa kwa hekta moja | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Bodi ya Pamba |
| | | Kahawa | Ongezeko kwa 100% la tani/ha | 25 | Uzalishaji kwa eneo | Jumla ya Tani zilizozalishwa kwa hekta moja | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Bodi ya kahawa |
| | | Miwa | Ongezeko kwa 100% la tani/ha | 40 | Uzalishaji kwa eneo | Jumla ya Tani zilizozalishwa kwa hekta moja | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Bodi ya sukari |
| | | Chai | Ongezeko kwa 100% la tani/ha | 9 | Uzalishaji kwa eneo | Jumla ya Tani zilizozalishwa kwa hekta moja | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Bodi ya Chai |
| | | Korosho | Ongezeko kwa 100% la tani/ha | 3 | Uzalishaji kwa eneo | Jumla ya Tani zilizozalishwa kwa hekta moja | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Bodi ya Korosho |
| | | Perege/Kambale | Ongezeko kwa 100% la Kg/m2 | 1.11 | Uzalishaji kwa eneo | Jumla ya Kilo zilizozalishwa kwa mita moja ya mraba | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Mwani/Magugu | Ongezeko kwa mara mbili ya uzalishaji | - | Uzalishaji kwa eneo | Jumla ya Kilo zilizozalishwa kwa mita moja ya mraba | Kwa mwaka | Wizara ya Mifugo na Uvuvi |
| 2 | Jumla ya uzalishaji kwa mwaka | Mahindi, Mpunga, Alizeti, Maziwa, Nyama ya ngombe, Nyama ya mbuzi, nyama ya kondooo, samaki wa maji chumvi (rejea lengo Kuu la Mpango 3) | | | | | | |
| | | Muhogo | Ongezeko maradufu la tani za uzalishaji wa muhogo | 6614.4 | Jumla ya Tani zilizozalishwa | Jumla ya uzalishaji kwa eneo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| | | mikunde (maharage) | Ongezeko maradufu la tani za uzalishaji wa mikunde (maharage) | 1306.5 | Jumla ya Tani zilizozalishwa | Jumla ya uzalishaji kwa eneo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | mtama/uwele | Ongezeko maradufu la tani za uzalishaji wa mtama/uwele | 729.5 | Jumla ya Tani zilizozalishwa | Jumla ya uzalishaji kwa eneo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Kilimo cha mbogamboga-matunda-viungo-(viazi mviringo/ulaya) | Ongezeko maradufu la tani za uzalishaji wa viazi mviringo | 1342.2 | Jumla ya Tani zilizozalishwa | Jumla ya uzalishaji kwa eneo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Pamba | Ongezeko maradufu la tani za uzalishaji wa pamba | 149.5 | Jumla ya Tani zilizozalishwa | Jumla ya uzalishaji kwa eneo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/Bodi ya Pamba |
| | | Kahawa | Ongezeko maradufu la tani za uzalishaji wa kahawa | 60.9 | Jumla ya Tani zilizozalishwa | Jumla ya uzalishaji kwa eneo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/Bodi ya Kahawa |
| | | Miwa | Ongezeko maradufu la tani za uzalishaji wa sukari | 2839.2 | Jumla ya Tani zilizozalishwa | Jumla ya uzalishaji kwa eneo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)//Bodi ya Sukari |
| | | Chai | Ongezeko maradufu la tani za uzalishaji wa chai | 32.6 | Jumla ya Tani zilizozalishwa | Jumla ya uzalishaji kwa eneo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)//Bodi ya Chai |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 2 | Jumla ya uzalishaji kwa mwaka | Korosho | Ongezeko maradufu la tani za uzalishaji wa korosho | 155.4 | Jumla ya Tani zilizozalishwa | Jumla ya uzalishaji kwa eneo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)//Bodi ya Korosho |
| | | Perege/kambale | Ongezeko la 100% la kilo za uzalishaji perege/ kambale | GAP | Jumla ya Kilo zilizozalishwa | Jumla ya uzalishaji kwa eneo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| 3 | Tija ya Raslimali watu na ardhi | Tija ya raslimali Watu | Kuongeza mara mbili Tija ya raslimali watu (ongezeko la 100% kutoka kiwango cha sasa cha tija ya raslimali watu) ifikapo mwaka 2025 | GAP | Jumla ya Raslimali Watu inayojihusisha katika kilimo | Pato ghafi litokanalo na kilimo kugawanya kwa Raslimali watu kwenye Kilimo | Kwa mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (/ Wizara za Sekta ya Kilimo /Wizara ya Maji na Umwagiliaji |
| | | Tija ya matumizi ya ardhi | Kuongeza tija ya ardhi maradufu (ongezeko la 100% kutoka kiwango cha sasa cha tija ya matumizi ya ardhi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Jumla ya eneo linalotumia kwa kilimo | Pato ghafi litokanalo na kilimo kugawa kwa eneo linalolimwa | Kwa mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS)/ Wizara za Sekta ya Kilimo / Wizara ya Maji na Umwagiliaji |
| **Huduma za Ugani** | | | | | | | | |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 4 | | Mbolea za Viwandani | Angalau nusu ya wakulima wanatumia mbolea za viwandani (N+P+K) | GAP | Kiwango cha wakulima kukubali kutumia mbolea za viwandani | Idadi ya Wakulima wanaotumia mbolea za viwandani kugawa kwa Idadi jumla ya wakulima | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Mbegu Bora | Angalau nusu ya wakulima wanatumia mbegu bora | GAP | Kiwango cha wakulima kukubali kutumia mbegu bora | Idadi ya Wakulima wanaotumia mbegu bpora kugawa kwa Idadi jumla ya wakulima | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Madawa ya kilimo (mazao yote) | Angalau nusu ya wakulima wanatumia madawa ya kilimo | GAP | Kiwango cha wakulima kukubali kutumia madawa ya kilimo | Idadi ya Wakulima wanaotumia madawa ya kilimo kugawa kwa Idadi jumla ya wakulima | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | zana bora za kilimo | Angalau nusu ya wakulima wadogo kutumia teknolojia za zana bora za kilimo | GAP | Kiwango cha wakulima kukubali kutumia zana bora za kilimo | Idadi ya Wakulima wanaotumia zana bora za kilimo kugawa kwa Idadi jumla ya wakulima | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Udhibiti husishi wa visumbufu vya mazao | Ongezeko la mara mbili la wakulima wadogo wanaotumia teknolojia ya udhibiti husishi wa visumbufu vya mazao | GAP | Kiwango cha wakulima kukubali kutumia udhibiti husishi wa visumbufu vya mazao | Idadi ya Wakulima wanaotumia udhibiti husishi wa visumbufu vya mazao kugawa kwa Idadi ya jumla ya wakulima | Kwa mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| | | Kilimo Shadidi cha Mpunga | Ongezeko la mara mbili la wakulima wadogo wanaotumia teknolojia ya kilimo shadidi cha mpunga | GAP | Kiwango cha wakulima kukubali kutumia Kilimo Shadidi cha Mpunga | Idadi ya Wakulima wanaotumia Kilimo Shadidi cha Mpunga kugawa kwa Idadi jumla ya wakulima | Kwa mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS)/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Uvunaji wa maji | Angalau nusu ya wakulima wadogo wanatumia teknolojia za uvunaji wa maji | GAP | Kiwango cha wakulima kukubali kutumia teknolojia za Uvunaji wa maji | Idadi ya Wakulima wanaotumia teknolojia za Uvunaji wa maji kugawa kwa Idadi jumla ya wakulima | Kwa mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Umwagiliaji wa njia ya matone au kinyunyizo mrashi | Angalau nusu ya wakulima wadogo kutumia teknolojia umwagiliaji wa njia ya matone au kinyunyizo mrashi | GAP | Kiwango cha wakulima kukubali kutumia teknolojia za Umwagiliaji ya njia ya matone au kinyunyizo mrashi | Idadi ya Wakulima wanaotumia teknolojia za Umwagiliaji wa njia ya matone au kinyunyizo mrashi kugawa kwa idadi ya jumla ya wakulima | Kwa mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Kukausha kwa njia ya nguvu ya jua (samaki) | Ongezeko la mara mbili (ongezeko la 100%) | 3600 | Kiwango cha wavuvi kukubali kutumia teknoljia ya kukausha kwa njia ya nguvu ya jua (samaki) | Idadi ya Wakulima wanaotumia teknolojia ya Kukausha kwa njia ya nguvu ya jua (samaki) kugawa kwa Idadi ya jumla ya wavuvi | Kwa mwaka | Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 5 | Idadi ya Maafisa Ugani | Kilimo | Ongezeko maradufu la Mafisa Ugani wa Sekta ya Umma | 11,000 | Mafisa Ugani wote wa kilimo wa Sekta ya Umma | Jumla ya Mafisa Ugani wote wa kilimo wa Sekta ya Umma | Kwa mwaka | Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Mifugo | Ongezeko maradufu la Mafisa Ugani wa Sekta ya Umma | 8,725 | Mafisa Ugani wote wa Mifugo wa Sekta ya Umma | Jumla ya Mafisa Ugani wote wa Mifugo wa Sekta ya Umma | Kwa mwaka | Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Uvuvi | Ongezeko maradufu la Mafisa Ugani wa Sekta ya Umma | 750 | Mafisa Ugani wote wa Uvuvi wa Sekta ya Umma | Jumla ya Mafisa Ugani wote wa Uvuvi wa Sekta ya Umma | Kwa mwaka | Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Sekta Binafsi | Waliopo wanaojihusisha na kilimo kupitia ubia na Serikali | GAP | Maafisa Ugani wote waliopo katika Sekta binafsi | Jumla ya Maafisa Ugani wote waliopo katika Sekta binafsi | Kwa mwaka | Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS)/ Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) |
| 6 | Vituo vya Raslimali za Kilimo vya Kata | Idadi ya Vituo vya Raslimali za Kilimo vya Kata | Kuwepo kwa angalau kituo kimoja cha Raslimali za Kilimo vya Kata kwa kila Kata ifikapo mwaka 2025 | 319 | Idadi ya Vituo vya Raslimali za Kilimo vya Kata vilivyopo | Kujumlisha Vituo vya Raslimali za Kilimo vya Kata | Kwa mwaka | Mfumo wa ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Vituo vya Raslimali za Kilimo vya Kata (WARCs) vinavyofanya kazi | Kufanya kazi kwa Vituo vyote vya Raslimali za Kilimo vya Kata ifikapo mwaka 2025 | 208 (pengo) | Vituo vya Raslimali za Kilimo vya Kata vilivyoendelezwa na vinavyofanya kazi | Kujumlisha Vituo vya Raslimali za Kilimo vya Kata | Kwa mwaka | Wizara za Sekta ya Kilimo ASLMs |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 7 | Idadi ya wakulima na Maafisa Ugani waliopatiwa mafunzo | Wakulima waliopata mafunzo | Wakulima wote wapatiwe mafunzo ifikapo mwaka 2025 | 0 | Wakulima wote waliopata mafunzo kupitia Mashamba darasa na mbinu zingine kama vile semina, warsha, ziara za mafunzo, mafunzo ya eneo la makazi n.k. | Kujumlisha idadi ya Wakulima waliopata mafunzo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Maafisa Ugani waliopatiwa mafunzo | Asilimia 50 ya Maafisa Ugani wapatiwe mafunzo ya kozi zinazostahili kwa malengo ifikapo mwaka 2025 | GAP | Kuwepo kwa Maafisa Ugani waliopata mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu | Kujumlisha idadi ya Maafisa Ugani waliopata mafunzo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| **Kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora na pembejeo za kilimo, mifugo, uvuvi na huduma za afya.** | | | | | | | | |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 8 | Upatikanaji wa Pembejeo kwa Wakulima | Matumizi ya mbolea za viwandani (kg. za viini lishe kwa hekta moja ya eneo la kilimo) | Angalau kilo 50 kwa hekta ifikapo mwaka 2025. | 19 | Jumla ya kilo za mbolea za viwandani zinazotumika kwa eneo lililolimwa (N+P, N+P+K) | Kujumlisha Kiasi cha mbolea za viwandani kilichotumika kugawa kwa eneo lililolimwa (Kg za viini lishe zilizotumika kwa hekta) | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Tani za mbegu bora (nafaka, mikunde n.k. isipokuwa miche na pingili za kupanda ) (mahitaji kwa mwaka ni tani 120,000 za mbegu bora) | Kuongeza maradufu kiwango cha matumizi ya mbegu bora cha sasa ifikapo mwaka 2025 | 28,000 | Jumla ya tani za mbegu bora zilizotumika katika eneo lililolimwa | kujumlisha tani za mbegu bora zilizotumika katika eneo lililolimwa | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Tani za madawa ya kilimo | Kuongeza matumizi ya madawa ya kilimo hadi 100% ifikapo mwaka 2025 | GAP | Jumla ya kiasi cha madawa ya kilimo kilichotumika | kujumlisha kiasi cha madawa ya kilimo kilichotumika katika mazao, mifugo | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Vifaranga vya samaki | Kuongeza kiasi cha vifaranga vya samaki | GAP | Jumla ya vifaranga vya samaki vilivyozalishwa na kukuzwa | kujumlisha vifaranga vya samaki vilivyozalishwa na kukuzwa | | |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| | | Mbari za mifugo (Uhimilishaji)-(mahitaji kwa mwaka 1,000,000) | Ongezeko la Uhimilishaji kwa 100% ifikapo mwaka 2025 | 100,000 | Uhimilishaji wa mifugo kwa ajili ya kuboresha mbari za mifugo | | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| **Utafiti na Maendeleo katikaKilimo** | | | | | | | | |
| 9 | Teknolojia zilizosambazwa | | Angalau asilimia 70 ya teknolojia za kilimo zilizoendelezwa zisambazwe ifikapo mwaka 2025 | GAP | Idadi ya Teknolojia zilizosambazwa | kujumlisha teknolojia zilizosambazwa | Kwa mwaka | Utafiti/Idara ya Maendeleo ya Utafiti/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| 10 | Jumla ya Matumizi katika Utafiti na maendeleo ya kilimo kama sehemu ya pato ghafi la Taifa la Kilimo ( | Matumizi katika Utafiti na maendeleo ya kilimo (kilimo, mifugo, uvuvi) | Kuongeza kiwango cha uwekezaji katika utafiti na maendeleo ya kilimo kufikia angalau 1% ya pato ghafi la Taifa litokanalo ifikapo mwaka 2025. | 0.28 | Asilimia ya Matumizi katika Utafiti na maendeleo ya kilimo kama sehemu ya pato ghafi la Taifa litokanalo na Kilimo | Matumizi katika Utafiti na maendeleo ya kilimo kama sehemu ya pato ghafi la Taifa litokanalo na Kilimo kugawa kwa pato ghafi la Taifa litokanalo na Kilimo kisha kuzidisha kwa 100 | Kwa mwaka | Wizara ya Kilimo/Wizara ya Mifugo na Uvuvi/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| **Kuimarisha upatikanaji na Kuendeleza Huduma za matumizi ya zana bora** | | | | | | | | |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 11 | Sehemu ya Matumizi ya mashine na mitambo katika shughuli za kilimo | Matumizi ya zana bora | Takriban asilimia 50 ya ardhi ya kilimo inalimwa kwa matrekta/ matrekta ya mkono au na wanyamakazi ifikapo mwaka 2025 | 14% (matrekta/ matrekta ya mkono (powertillers)<br><br>24% wanyama kazi | Kulima ardhi yote ya kilimo kwa kutumia matrekta/ matrekta ya mkono au wanyamakazi | ardhi ya kilimo inayolimwa kwa matrekta/ matrekta ya mkono au kwa wanyamakazi kugawa kwa jumla ya eneo la ardhi linalolimwa kisha kuzidisha kwa 100 | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| 12 | Idadi ya zana bora za kilimo (matrekta n.k); Vituo vya huduma za kukodishia zana bora za kilimo | Vituo vya huduma za kukodishia zana bora za kilimo | Uanzishwaji wa vituo angalau viwili vya huduma za kukodishia zana bora za (matrekta, matrekta ya mkono na wanyama kazi) katika kila Halmashauri ifikapo mwaka 2025 | 5 = (1 Rukwa, 1 Masasi, 1 Songea, 1 Arusha na 1 Singida) | Uanzishwaji wa vituo vya huduma za kukodishia zana bora za kilimo | Kujumlisha vituo vya huduma za kukodishia zana bora za kilimo vilivyoanzishwa | Kwa mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| **Usalama wa chakula na lishe** | | | | | | | | |
| 13 | Uwezo wa Nchi kujitosheleza kwa chakula | Uwezo wa kujitosheleza kwa chakula rejea Lengo la Programu 10 | | | | | | |
| 14 | Kupatikana kwa watu wenye utapiamlo (mkali na wa mpito) katika Tanzania | Kupatikana kwa watu wenye utapiamlo rejea Lengo la Programu 12 | | | | | | |
| 15 | Sehemu ya watu yenye kupata lishe duni | Sehemu ya watu yenye kupata lishe duni rejea Lengo la Programu 13 | | | | | | |
| 16 | Sehemu ya kaya zenye kupata wigo hafifu wa mchanganyiko wa viini lishe | Sehemu ya watu yenye kupata wigo mpana wa mchanganyiko wa viini lishe rejea Lengo la Programu 11 | | | | | | |

## ENEO LA TATU
## Biashara na Uongezaji Thamani kwenye mazao

**Lengo Kuu la Eneo la Programu:** *Kuboresha na kuongeza masoko, pamoja na kuongeza thamani ya mazao kwa kuhamasisha ushindani wa Sekta Binafsi na vyama/ vikundi imara vya wakulima*

### Viashiria muhimu vya utendaji:

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanz (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| **Bidhaa Zenye Ushindani na Uongezaji wa Thamani** | | | | | | | | |
| 1 | Kiasi na Thamani ya Bidhaa za Kilimo za nchi yetu zinazouzwa nje ya Nchi | **Mahindi; Mchele; Pamba; mazao ya bustani, nyama ya ngombe ; samaki wa maji chumvi (rejea Lengo la Programu 5)** | | | | | | |
| | | Alizeti | Kuongezeka mara mbili kwa kiasi cha mauzo ya alizeti nje ya nchi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Badiliko katika asilimia la kiasi cha alizeti kinachouzwa nje ya nchi | (Pato Ghafi kutoa Pato Ghafi Msingi) kugawa kwa Pato Ghafi Msingi na kuzidisha kwa 100 | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Maziwa | Kuongezeka mara tatu kwa kiasi cha mauzo ya maziwa nje ya nchi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Badiliko katika asilimia la kiasi cha maziwa kinachouzwa nje ya nchi | (Pato Ghafi kutoa Pato Ghafi Msingi) kugawa kwa Pato Ghafi Msingi na kuzidisha kwa 100 | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Kahawa | Kuongezeka mara mbili kwa kiasi cha mauzo ya kahawa nje ya nchi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Badiliko katika asilimia la kiasi cha kahawa kinachouzwa nje ya nchi | (Pato Ghafi kutoa Pato Ghafi Msingi) kugawa kwa Pato Ghafi Msingina kuzidisha kwa 100 | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanz (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| | | Sukari | Kuongezeka mara tatu kwa kiasi cha mauzo ya sukari nje ya nchi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Badiliko katika asilimia la kiasi cha sukari kinachouzwa nje ya nchi | (Pato Ghafi kutoa Pato Ghafi Msingi) kugawa kwa Pato Ghafi Msingi na kuzidisha kwa 100 | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Chai | Kuongezeka mara mbili kwa kiasi cha mauzo ya chai nje ya nchi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Badiliko katika asilimia la kiasi cha chai kinachouzwa nje ya nchi | (Pato Ghafi kutoa Pato Ghafi Msingi) kugawa kwa Pato Ghafi Msingi na kuzidisha kwa 100 | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Korosho | Kuongezeka mara mbili kwa kiasi cha mauzo ya korosho nje ya nchi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Badiliko katika asilimia la kiasi cha korosho kinachouzwa nje ya nchi | (Pato Ghafi kutoa Pato Ghafi Msingi) kugawa kwa Pato Ghafi Msingi kuzidisha kwa 100 | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Nyama ya mbuzi | Kuongezeka mara mbili kwa kiasi cha mauzo ya nyama ya mbuzi nje ya nchi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Badiliko katika asilimia la kiasi cha nyama ya mbuzi kinachouzwa nje ya nchi | (Pato Ghafi kutoa Pato Ghafi Msingi) kugawa kwa Pato Ghafi Msingi kuzidisha kwa 100 | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Nyama ya kondoo | Kuongezeka mara mbili kwa kiasi cha mauzo ya nyama ya kondoo nje ya nchi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Badiliko katika asilimia la kiasi cha nyama ya kondoo kinachouzwa nje ya nchi | (Pato Ghafi kutoa Pato Ghafi Msingi) kugawa kwa Pato Ghafi Msingi kuzidisha kwa 100 | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Korosho | Kuongezeka mara mbili kwa kiasi cha mauzo ya korosho nje ya nchi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Badiliko katika asilimia la kiasi cha korosho kinachouzwa nje ya nchi | (Pato Ghafi kutoa Pato Ghafi Msingi) kugawa kwa Pato Ghafi Msingi kuzidisha kwa 100 | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanz (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 2 | Kiasi na Thamani ya Manunuzi ya Bidhaa za Kilimo zinazoingizwa kutoka nje ya Nchi (import) | Mahindi; Mchele (rejea PDO 6) | | | | | | |
| | | Samaki wa maji chumvi | Kuongeza kilo za uzalishaji wa samaki wa maji chumvi mara mbili (ongezeko la Asilimia 100) | GAP | Jumla ya kilo zilizozalishwa | Kujumlisha uzalishaji katika eneo | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Mbegu za mafuta ya kula | Kuongeza tani za uzalishaji wa Mbegu za mafuta ya kula mara mbili (ongezeko la Asilimia 100) | GAP | Jumla ya tani zilizozalishwa | Kujumlisha uzalishaji katika eneo | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Maziwa | Kuongeza lita za uzalishaji wa Maziwa mara mbili (ongezeko la Asilimia 100) | GAP | Jumla ya lita zilizozaliswa | Kujumlisha uzalishaji katika eneo | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Kahawa | Kuongeza tani za uzalishaji wa kahawa mara mbili (ongezeko la Asilimia 100) | GAP | Jumla ya tani zilizozalishwa | Kujumlisha uzalishaji katika eneo | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Sukari | Kuongeza Tani za uzalishaji wa sukari mara mbili (ongezeko la Asilimia 100) | GAP | Jumla ya tani zilizozalishwa | Kujumlisha uzalishaji katika eneo | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Nyama ya ng'ombe | Kuongeza tani za uzalishaji wa Nyama ya ng'ombe mara mbili (ongezeko la Asilimia 100) | GAP | Jumla ya tani zilizozalishwa | Kujumlisha uzalishaji katika eneo | Kwa mwaka | Mamlaka ya Mapato Tanzania/ Wizara za Sekta ya Kilimo |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanz (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 3 | Kasi ya upungufu wa pengo kati ya Bei jumla ya sokoni na Bei ya mkulima shambani kwa mazao yote ya kipaumbele | **Mahindi , Mpunga, Maziwa rejea PDO 7** | | | | | | |
| | | Muhogo | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei ya jumla) na Bei ya mkulima shambani | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | maharage | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei ya jumla) na Bei ya mkulima shambani (farm-gate price) | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Mtama/uwele | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei ya jumla) na Bei ya mkulima shambani | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Mbogamboga na matunda (viazi ) | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei ya jumla) na Bei ya mkulima shambani | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |
| | | Alizeti | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei ya jumla) na Bei ya mkulima shambani | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Kilimo (ARDS)/ Sampuli ya Sensa ya Mwaka ya Kilimo (AASS) |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanz (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| | | Pamba | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei ya jumla) na Bei ya mkulima shambani | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | ARDS/ AASS |
| | | Kahawa | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei za jumla) na Bei ya mkulima shambani | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | ARDS/ AASS |
| | | Miwa | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei za jumla) na Bei ya mkulima shambani | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | ARDS/ AASS |
| | | Chai | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei za jumla) na Bei ya mkulima shambani | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | ARDS/ AASS |
| | | Korosho | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei za jumla) na Bei ya mkulima shambani | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | ARDS/ AASS |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanz (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| | | Nyama ya ng'ombe | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei za jumla) na Bei ya mkulima shambani) | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | ARDS/ AASS |
| | | Mbuzi | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei za jumla) na Bei ya mkulima shambani | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | ARDS/ AASS |
| | | Kondoo | Uwiano kupungua kwa Asilimia 50 | GAP | Tofauti kati ya Bei ya sokoni (bei za jumla) mkulima shambani | [(Bei ya sokoni kutoa Bei ya mkulima shambani) kugawa kwa Bei ya mkulima shambani] kuzidisha kwa 100 | Kila nusu mwaka | ARDS/ AASS |
| 4 | Uwiano wa thamani ya fedha ya malighafi za kilimo zinazosafirishwa nje na kusindikwa | kwato/ngozi | Angalau Asilimia 100 ya kwato na ngozi zinasindikwa kwa ajili ya kuuza nje ifikapo mwaka 2025 | GAP | Thamani ya fedha ya malighafi za kilimo zinazosafirishwa nje na kusindikwa | Jumla ya mauzo ya nje ya mazao yaliosindikwa kugawa kwa jumla ya mauzo ya nje | Kila nusu mwaka | AASS/ ARDS |
| | | Korosho | Angalau Asilimia 100 ya korosho inasindikwa kwa ajili ya kuuza nje ifikapo mwaka 2025 | GAP | Thamani ya fedha ya malighafi za kilimo zinazosafirishwa nje na kusindikwa | Jumla ya mauzi ya nje ya mazao yaliyosindikwa kugawa kwa jumla ya mauzo ya nje | Kila nusu mwaka | AASS/ ARDS |
| | | Nyama ya ng'ombe | Angalau Asilimia 100 ya nyama ya ng'ombe inasindikwa kwa ajili ya kuuza nje kufikia mwaka 2025 | GAP | Thamani ya fedha ya malighafi za kilimo zinazosafirishwa nje na kusindikwa | Jumla ya mauzo ya nje ya mazao yaliyosindikwa /jumla ya mauzo ya nje | Kila nusu mwaka | AASS/ ARDS |
| **Upatikanaji wa masoko na miundombinu vijijini** | | | | | | | | |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanz (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 5 | Idadi ya miundombinu ya msoko inayotumika na uwekezaji mpya | Muundo wa soko | Asilimia 100 ya miundombinu ya masoko inafanya kazi ifikapo mwaka 2025 | GAP | Miundombinu yote ya masoko ya kilimo | Jumla ya miundombinu ya masoko yana yotumika | Kila nusu mwaka | MoA/ MLF/ MITI/ ASLM |
| | | Ghala / | Asilimia 100 ya maghala yaliyoanzishwa na kutumika | GAP | Miundombinu yote ya maghala ya kilimo | Jumla ya miundombinu ya maghala yanayo tumika | Kila nusu mwaka | MoA/ MLF/ MITI/ ASLM |
| | | Ghala | Asilimia 100 ya maghala imejengwa na kutumika | GAP | Miundombinu zote za Maghala ya kilimo | Idadi ya maghala yanayo tumika | Kila nusu mwaka | MoA/ MLF/ MITI/ ASLM |
| 6 | Kiwango cha bidhaa kinachouzwa kupitia Mpango wa stakabadhi ghalani | Mahindi, mchele, korosho | Asilimia 100 ya mazao ya kilimo yanauzwa kupitia mfumo wa Stakabadhi za Ghala | GAP | Kiasi cha mahindi, mchele, korosho kinachouzwa kupitia mfumo wa Stakabadhi za Ghala | Bidhaa zote zinazouzwa kupitia mfumo wa Stakabadhi za Ghala | Kila nusu mwaka | MoA/ MITI/ ASLM |
| 7 | Upunguaji kiwango cha upotevu wa mazao baada ya mavuno kwa (angalau) bidhaa 11 za kipaumbele za Taifa | Nafaka | Kupungua kwa nusu (imepungua kwa Asilimia 50) viwango vya sasa vya upotevu wa mazao baada ya mavuno (PHL), Kufikia mwaka 2025 kuanzia mwaka 2016. | 30-40 | upotevu kwa tani | Uzalishaji (tani) wa bidhaa 1, Pd1; kutoa (hasara katika uvunaji, LH; hasara katika kuhifadhi, LS; hasara katika usafiri, LT; hasara katika usindikaji, LP; hasara katika upakiaji, LPz; &hasara katika mauzo, LS); Upotevu =Pd1-(LH-LS-LT-LP- LPz-LS) kwa tani | Kwa mwaka | AASS/ MoA |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanz (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| | | Mazao ya jamii ya mizizi | Imepungua kwa Asilimia 50 | 45 | Upotevu kwa tani | | Kwa mwaka | AASS/ MoA |
| | | Mbegu za mafuta | Imepungua kwa Asilimia 50 | 40-50 | Upotevu kwa tani | | Kwa mwaka | AASS/ MoA |
| | | Kilimo cha maua na mbogamboga | Imepungua kwa Asilimia 50 | Zaidi ya 50 | Upotevu kwa tani | | Kwa mwaka | AASS/ MoA |
| | | Samaki na bidhaa za uvuvi | Imepungua kwa Asilimia 50 | 70 | Upotevu kwa tani | | Kwa mwaka | AASS/ MLF |

## ENEO LA NNE
## Uwezeshaji wa Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini

**lengo: Uimarishaji wa wawezeshaji wa sekta, uratibu na ufuatiliaji na tathmini**

### Viashiria muhimu vya utendaji:

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| **Mazingira ya biashara** | | | | | | | | |
| 1 | Mazingira ya sera na kanuni | Mazao, mifugo na uvuvi | marejeo/sasisha/ kuwianisha / utekelezaji wa sera, vifungu vya sheria, kanuni na sheria | mazao (2013), mifugo(2006), uvuvi(2015), soko (2008) | Mazingira ya sera za kilimo | kupitia, sasisha, na kuwianisha kama ilivyohitajika | Kwa mwaka | ASLMs/MOF |
| 2 | Muundo wa kitaasisi | Wadau wa kilimo | kupitia, sasisha na kuwianisha muundo wa kitaasisi | ASDP-I Muundo wa kitaasisi | ASDP-II muundo wa kiutekelezaji | kupitia, sasisha, na kuwianisha muundo uliopo | Kwa mwaka | Wizara za Sekta ya Kilimo/Wizara ya Fedha na mipango |
| Uratibu wa sekta (wima na mlalo) | | | | | | | | |
| 3 | Uwasilishaji wa taarifa za kilimo kwa wakati katika ngazi zote | Mazao,mifugo na uvuvi | Asilimia 100 ya uwasilishaji kwa Serikali za Mitaa zote | 90 | Taarifa za robo mwaka na za mwaka | Kawaida na isiyokuwa ya kawaida | Kila robo/ mwaka/ kipindi maalum | AASS/ARDS/ ASLMs |
| 4 | Kiwango cha uzingatiaji wa mwongozo wa kilimo | Mwongozo wa upangaji na utekelezaji | Asilimia 100 ya uzingatiaji | GAP | Kiwango cha kufuatilia utekelezaji wa miongozo ya kilimo | Maandiko ya uchambuzi wa DADPs | Kwa mwaka | Wizara ya tathmini ya DADPs |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 5 | Ugawaji wa bajeti na utoaji wa fedha katika Sekta ya kilimo | Bajeti ya Kawaida | Asilimia 100 ya utoaji wa fedha za bajeti iliyotengwa | 80.57 (mazao), (mifugo), (uvuvi), (masoko), TAMISEMI | Taarifa za fedha zilizoidhinishwa, zilizotolewa na zilizotumika | Taarifa za fedha kuhusu fedha zilizotolewa | Kwa mwaka | Wizara ya Fedha na Mipango/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| | | Bajeti ya Maendeleo | 100% utoaji wa fedha za bajeti iliyotengwa | 3.91 (mazao), (mifugo), (uvuvi), (masoko), TAMISEMI | Taarifa za fedha zilizoidhinishwa, zilizotolewa | Kumbukumbu ya taarifa za fedha zilizotolewa | Kwa mwaka | Wizara ya Fedha na Mipango/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| 6 | Matumizi ya umma ya kilimo ikiwa kama asilimia ya Pato la Taifa la kilimo | Sekta ya kilimo | Kuongeza bajeti ya sekta ya Kilimo angalau kufikia asilimia 10 ya bajeti yote ya Serikali ifikapo mwaka 2025 | 5.30% | Matumizi ya Wizara za Sekta ya Kilimo kwenye matumizi ya jumla ya umma | Matumizi ya Kilimo ya Umma kugawanya kwa matumizi ya jumla ya umma | Kwa mwaka | Wizara ya Fedha na Mipango/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| 7 | Matumizi ya Kilimo ya Umma kama % ya Pato la Taifa la kilimo | | Kudumisha matumizi ya kilimo ya umma kwa asilimia 19% ya Pato la Taifa la kilimo kufikia 2025 | 5.20% | Matumizi ya Wizara za Sekta ya Kilimo kama sehemu ya Pato la Taifa la kilimo | Matumizi ya Kilimo ya Umma kugawanya kwa Pato la Kilimo | Kwa mwaka | Wizara ya Fedha na Mipango/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| 8 | Misaada ya Bajeti ya Maendeleo (ODA) iliyotolewa kwa ajili ya kilimo kama asilimia ya ahadi zilizotolewa | Sekta ya Kilimo | Upatikanaji kwa asilimia 100 ya misaada ya bajeti ya Maendeleo rasmi (ODA) kila mwaka kuanzia 2016 hadi 2025 | Mazao, mifugo, uvuvi na masoko | Ahadi za washirika wa maendeleo katika ASLMs | Msaada wa bajeti kwa sekta ya kilimo (umma, binafsi, PPP, DPs, shirika la kimataifa, NGOs, mashirika ya kiraia, Asasi zisizo za kiserikali, nk) | Kwa mwaka | Wizara ya Fedha na Mipango/ Wizara za Sekta ya Kilimo |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 9 | Uwiano kati ya uwekezaji wa sekta binafsi na uwekezaji wa Serikali katika kilimo | | Kuhakikisha serikali inashawishi uwekezaji binafsi wa ndani angalau mara tatu ifikapo mwaka 2025. | GAP | Uwekezaji wa sekta binafsi kwenye uwekezaji wa umma katika kilimo | Uwekezaji wa sekta binafsi gawanya kwa uwekezaji wa sekta ya umma | Kila mwaka | Wizara ya Fedha na Mipango/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| 10 | Uwiano kati ya uwekezaji binafsi wa kigeni wa moja kwa moja (FDI) na uwekezaji wa serikali katika kilimo | | Kuhakikisha Serikali inashawishi kuongeza uwekezaji wa kigeni angalau mara tatu ifikapo mwaka 2025 | GAP | Uwekezaji binafsi wa kigeni wa moja kwa moja kwenye uwekezaji wa serikali katika kilimo | Uwekezaji binafsi wa kigeni wa moja kwa moja kugawanya kwa uwekezaji wa serikali katika kilimo | Kwa mwaka | Wizara ya Fedha na Mipango/ Wizara za Sekta ya Kilimo |
| **Ufuatiliaji & tathmini na takwimu za Kilimo** | | | | | | | | |
| 11 | Utafiti wa Sampuli ya Kilimo Kila mwaka (AASS) kutekelezwa | Sekta ya kilimo | AASS kutekelezwa kila mwaka na matokeo kutolewa ndani ya miezi mitatu | Ilifanyika Februari 2015 | Utafiti ulifanywa kila mwaka | Utafiti | Kila mwaka | AASS/ARDS |
| **Uwezeshaji wa Wadau na Shirika** | | | | | | | | |
| 12 | Uwezeshaji wa vyama vya wakulima, wanawake na vijana | Vijana | Angalau asilimia 30 ya vijana wanapewa hati miliki za ardhi ya Kilimo ifikapo 2025. | GAP | Asilimia ya vijana wanaojishughulisha na Kilimo na wenye hati miliki za ardhi | Jumla ya idadi ya vijana wanaojishughulisha na Kilimo wana hati miliki ya ardhi | Kwa mwaka | TIC/ASLMS/ MoW/ MLHSH |
| | | Wanawake wa vijijini | Angalau asilimia 20 ya wanawake wa vijijini wanapata na rasilimali za uzalishaji kufikia 2025. | GAP | Uwezeshaji wa wanawake wa vijijini ambao wana uwezo wa kufanya uzalishaji kwenye lilimo k.m. ardhi, mikopo, pembejeo (mbolea na mbegu), nk. | Jumla ya idadi ya wanawake waliopewa rasilimali za uzalishaji kwenye kilimo | Kwa mwaka | ASLM/BOT |

| Kiashiria | | Makundi ya Kiashiria | Lengo kwa kila kundi katika Kiashiria | Thamani ya kuanzia (2016) | Ukusanyaji takwimu na Utoaji Taarifa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ufafanuzi | Njia iliyotumika | Vipindi vya utoaji taarifa | Chanzo cha Takwimu |
| 13 | Uwiano kati ya wakulima ambao ni wanachama vyama vya wakulima na wa vyama vya ushirika | SACCOS kwa jinsia | Kuongeza mara mbili ya wanachama wa SACCOS kufikia 2025 | GAP | Uwiano wa wakulima ambao ni wanachama wa SACCOS | Idadi ya wakulima ambao ni wanachama katika vyama a vya ushirika linagawanyika na jumla ya idadi ya wakulima | Kwa mwaka | AASS/ARDS |
| | | Vyama vya wakulima na vyama vya ushirika | Kuongeza maradufu wanachama wa SACCOS ifikapo mwaka 2025 | GAP | Uwiano wa wakulima ambao ni wanachama wa SACCOs | Idadi ya wakulima ambao ni wanachama katika wa SACCOs gawanywa kwa jumla ya idadi ya wakulima | Kila mwaka | Wizara za Sekta ya Kilimo |
| **Upatikanaji wa Fedha za Vijijini** | | | | | | | | |
| 14 | Idadi ya wanawake na wanaume wanaojishughuisha na kilimo ambao wanapata huduma za kifedha | Iliyo rasmi | Kuongeza maradufu (100%) wakulima wanaopata mikopo kwa ajili ya kilimo | GAP | Jumla ya wakulima wanaofikiwa na huduma za kifedha (mikopo) kwa jinsia | Idadi ya wakulima wanaopata mikopo kwa jinsia kugawanya kwa jumla ya idadi ya wakulima | Kila mwaka | Benki Kuu ya Tanzania |
| 15 | Uwiano wa matawi ya taasisi rasmi za fedha katika maeneo ya vijijini | Taasisi rasmi | Angalau zaidi ya nusu ya matawi yanaanzishwa katika maeneo ya vijijini | GAP | Jumla ya idadi ya matawi ya taasisi rasmi za kifedha kwenye maeneo ya vijijini | Matawi ya Benki katika maeneo ya vijijini kugawanya kwa idadi ya matawi ya benki nchini Tanzania | Kila mwaka | Benki Kuu ya Tanzania |
| 16 | Kiasi na thamani ya mkopo kutoka sekta ya fedha kwa ajili ya sekta ya kilimo | Kwa ajili ya sekta ndogo | Angalau asilimia 50 ya thamani ya mikopo ya sekta ya fedha zitatengwa kwa ajili ya kilimo ifikapo 2025 | GAP | Uwiano wa mikopo iliyotengwa kwenye sekta ya kilimo na taasisi za fedha | Kiasi na thamani ya mikopo iliyotolewa kwa ajili ya kilimo gawanya kwa jumla ya kiasi cha mikopo iliyotolewa | Kila mwaka | Benki Kuu ya Tanzania |
| 17 | Viwango vya urejeshaji wa mikopo (%) kwa mabenki | Kwa ajili ya sekta ndogo | Angalau viwango vya urejeshaji wa mkopo kuwa zaidi ya 80% ifikapo 2025 | GAP | Uwiano wa mikopo iliyorejeshwa kwenye taasisi za fedha | Idadi ya mikopo iliyorejeshwa gawanya kwa idadi ya jumla ya mikopo iliyotolewa | | Benki Kuu ya Tanzania |

# KIAMBATISHO Na. III: MFUMO WA URATIBU WA ASDP II

## Kielelezo Na. A23: Mfumo wa Uratibu wa ASDP II



***Uratibu katika ngazi ya kati na kitaifa***

**419** Muundo wa uratibu wa ASDP II ngazi ya Taifa:

i. Mkutano waTaifa wa Wadau wa Sekta ya Kilimo (NASSM)

ii. Kamati ya Usimamizi na Maamuzi ya Sekta ya Kilimo (ASC)

iii. Mkutano wa Ushauri wa Sekta ya Kilimo (ASCG)

iv. Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi (TCD)

v. Vikundi Kazi vya Kitaalam (TWGs)

vi. Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II (NCU)

**420** **Mkutano wa Taifa wa Wadau wa Sekta ya Kilimo (NASSM)** ni tukio la juu zaidi la uratibu katika utawala wa programu na utawasaidia kuunganisha na katika kuongoza sekta nzima. Mkutano utafanyika mara moja kwa mwaka na utafanyika kwa siku moja au mbili kama hitimisho la kazi ya mapitio ya sekta (JSR / PER), ambayo itawasilishwa kwenye NASSM. Mkutano huo utafanyika chini ya uenyekiti wa Waziri Mkuu ili kupima mafanikio ya ASDP II na mchango wake katika maendeleo ya kitaifa na kupunguza umasikini. Madhumuni ya NASSM yatakuwa:

- Kutoa fursa kwa wawakilishi wote wa wadau ili kubadilishana maoni yao na kupata ufahamu juu ya mafanikio ya programu
- Kutathmini mapitio yaliyotolewa na JSR / PER kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kilimo ndani ya programu ili kufikia malengo yaliyopangwa, matokeo na matokeo
- Kutoa ushauri kwa taasisi mbalimbali za serikali, washirika wa maendeleo, asasi zisizo za kiserikali, na wadau wa sekta binafsi kuhusu fursa za kuleta mageuzi makubwa kwenye sekta ya kilimo na kuongeza kasi ya kufikia malengo ya ASDP II na matokeo yaliyokusudiwa.
- Kutathmini na kujadili masuala ya mageuzi ya kilimo na matokeo mchango wa programu katika sekta hiyo

**421** **NASSM** itahudhuriwa na:

- Mawaziri wote, Makatibu Wakuu wa ASLMs na Wakurugenzi wa Sera na Mipango kutoka ASLMs, Viongozi wa maeneo ya programu; na viongozi wengine wa serikali toka sekta zinazohusiana na kilimo
- Washirika wa maendeleo -wajumbe wa Kikundi cha Kilimo, Washirika wa Maendeleo wa Sekta Binafsi (PSD) na washirika wa maendeleo wengine wa wanaojihusisha na kilimo.
- Secretariati za Mikoa-maafisa waliochaguliwa
- Serikali za Mitaa, DAICOs, DLFO, DLOs, DCO, kutoka kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizochaguliwa
- Maafisa waliochaguliwa kutoka kwenye taasisi za utafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi (ASLMs)
- Wakuu wa idara kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine na taasisi nyingine za kitaaluma / taasisi za mafunzo zinazohusika katika utafiti na mafunzo ya kilimo.
- Bodi za mazao/bidhaa
- Wawakilishi wa sekta binafsi
- Mashirika yasiyo ya kiserikali / NGOs / wawakilishi wa CBO
- Taasisi za kifedha zinazohusika na shughuli za kilimo na uwekezaji
- Mashirika na vyama vya ushirika-wawakilishi wa vyama vya ushirika, na vyama vya kilimo na SACCOS,
- Wawakilishi wa mashirika mengine.

422 Kabla mkutano wowote wa NASSM haujaitishwa kutafanyika mapitio ya pamoja ya sekta (JSR / PER) ambayo yataelezea kwa kina kazi ziliofanywa na serikali, washirika wa maendeleo, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, na sekta binafsi kwa ajili ya kufuatilia maendeleo ya sekta kwa mwaka. Mapitio yatafanywa na, serikali, washirika wa ya maendeleo na wataalamu elekezi kwa kupitia utekelezaji wa Programu kwa kuchambua takwimu za utekelezaji na kutoa taarifa ya kina za ASDP II. Kazi hiyo inahusisha kutembelea mikoa itachaguliwa ambayo inatekeleza ASDP II sawa na kama ambavyo ilikuwa inafanyika wakati wa utekelezaji wa ASDP 1. JSR/PER zitakuwa ni shughuli ambazo zitawezesha kufanyika kwa majadiliano na uratibu wa sekta. Taarifa ya JSR / PER itawasilishwa kwanza kwenye mkutano wa ASCG, na baadaye kwenye kamati ya uendeshaji ya sekta ya kilimo kabla ya kuwasilishwa kwenye NASSM. Mapendekezo ya JSR /PER yatawasilishwa kwenye NASSM kwa ajili ya majadiliano na utekelezaji wa pamoja. Muda wa kufanya kazi ya mapitio ya sekta unatakiwa kuzingatia muda wa vikao vya ASCG, ASC, NASSM, muda (mzunguko) wa bajeti ya serikali na matukio mengine yanayohusiana.

423 **Kamati ya Usimamizi na Maamuzi ya sekta ya kilimo (ASC).** Hiki ni chombo kikuu na muhimu cha usimamizi na utoaji wa maamuzi. Ni chombo cha utekelezaji wa ASDP II na uratibu. Kazi za msingi zitakuwa ni kupitisha mpango kazi wa mwaka na bajeti, kusimamia utekelezaji wa bajeti , kufuatilia matokeo ya ukaguzi na kujadili juu ya masuala muhimu kuhusiana na utekelezaji wa sekta na uratibu. Mapendekezo yatasaidia kuelekeza TDC na TWG juu ya kazi zitakazofuata. Mkutano huu utafanyika kila baada ya miezi mitatu na utakuwa chini ya uenyekiti wa Waziri ofisi ya Waziri Mkuu. Wajumbe ni Makatibu Wakuu wa ASLMs na wa kutoka wizara za mashirikiano, wajumbe wa TDC, wawakilishi wa washirika wa maendeleo, vikundi vya wakulima, sekta binafsi, wawakilishi wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, na wawakilishi wa sekta binafsi. Kikao hicho kitawezeshwa na Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Kilimo (MoA) na NCU.

424 ASC ni chombo kikuu cha usimamizi wa ASDP II. Malengo makuu ni :

i. Kufikia malengo ya sekta na matokeo kwa njia ya mazungumzo na mashauriano ya kuanzisha sera thabiti ya sekta ya kilimo , mikakati na programu za kuzingatia Mpango ya muda mrefu ya Maendeleo, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na mifumo ya maendeleo wa taifa

ii. Kuhakikisha mipango, bajeti na mgawo wa bajeti, utekelezaji na matumizi ni kwa mujibu wa vipaumbele vya sera ya sekta ya kilimo, programu na mikakati

iii. Kuboresha usimamizi wa fedha za umma na uwajibikaji katika ASLMs

iv. Kutekeleza sekta ya kilimo kwa kuzingatia utaratibu wa JAST

v. Kutekeleza sekta ya kilimo kwa kuzingatia ahadi ya GBS kama ilivyoainishwa katika makubaliano ya PAF na Mfumo wa mkataba wa ushirikiano

vi. Kuheshimiana na kuimarisha uwajibikaji

425 **Mkutano wa Mashauriano wa sekta ya kilimo (ASCG).** ASCG itakuwa sehemu ya mashauriano ambapo wadau wote katika sekta watakuwa tayari kukutana kila robo mwaka kujadili masuala na utekelezaji wa ASDP II. Mkutano huu ni muhimu sana kwa sababu ASC itafanyakazi kama bodi na itahudhuriwa na wawakilishi tu. ASCG iko wazi kwa wadau wote mwenyekiti ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, itakuwa na nafasi ya kukutana na kujadili na wadau muhimu katika sekta. Hizi ni pamoja na ASLMs, Washirika wa Maendeleo, sekta binafsi, NGO, BOs, Asasi za wakulima / Vyama vya ushirika, taasisi za utafiti na mafunzo, watekelezaji na wadau wengine wa ASDP II.

426 **Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi (TCD).**TCD itadumishwa na kuchukua baadhi ya kazi za makatibu wakuu (ICC) kama ilivyokuwa kwenye ASDP I. Itakuwa Kamati ya masuala ya kiufundiya kilimo kuhusiana na maendeleo ya maeneo makuu ya ASDP II, maeneo madogo, maeneo ya uwekezaji na miradi na kuwa chini ya uenyekiti wa Katibu Mkuu, Mkurugenzi ofisi ya Waziri Mkuu Wizara ya Kilimo na kusaidiwa na Kitengo cha Taifa cha Uratibu (NCU). TCD ni kamati ya serikali tu na itajumuisha kila Mkurugenzi wa Sera na Mipango (DPPs) / Wakurugenzi ya ASLMs na Viongozi wa maeneo makuu ya ASDP II.

427 **TCD** watakutana kila baada ya miezi mitatu na inaweza kuwa wito wa mikutano wa dharula kama kunahitaji. TCD itakagua ripoti za robo mwaka na kuchangia ripoti ya kila mwaka. Wao watatoa uangalizi wa utekelezaji na ufuatiliaji wa utendaji wa ASDP II kuhakikisha mafanikio ya malengo.Kazi za TCD ni pamoja na:

- Kufanya mapitio ya maendeleo ya kila hatua ya ASDP II kuhakikisha matakwa ya sera, mikakati ya jumla na sekta na kufuata ratiba kwa njia ya muhtasari na taarifa za fedha maendeleo na kuchukua hatua muhimu za marekebisho
- Kutoa ushauri kwa Kamati ya ASC mara kwa mara juu ya maendeleo na mahitaji kwa ajili ya utekelezaji wa ASDP II
- Kusimamia maendeleo na utekelezaji wa maamuzi ya sera za msingi ya ASDS na ASDP II
- Kusimamia maandalizi ya ASDP II Jumuishi na Mpango wa Bajeti kwa mwaka
- Kupitia na kupendekeza mapendekezo ya bajeti kwa kamati ya uendeshaji kwa ajili ya idhini na kuwasilisha hazina
- Kupendekeza kwa Kamati ya Usimamizi na Maamuzi ya Sekta ya Kilimo juu ya uhamisho wa fedha kutoka Akaunti kwa ajili ya utekelezaji kwenye maeneo husika
- Kufafanua masharti ya kukidhi kuhusu programu mpya na miradi chini ya ASDP II
- Kufanya mapitio ya ripoti kutoka miradi inayotekelezwa nje ya mfumo wa bajeti ya serikali

428 **Vikundi kazi vya ASDP II (TWGs)** vitaandaliwa kazi kwenye vikundi kulingana na uzoefu uliopatikana chini ya ASDP-1. Kwa ASDP II kimaudhui vikundi kazi vitatokana na Maeneo Makuu ya ASDP II, maeneo madogo na maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji. Wajumbe wa vikundi kazi watatokana na wataalam ndani ya maeneo husika (yaani, idara/taasisi) katika kila ASLMs au taasisi husika, sekta binafsi, washirika wa maendeleo na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali / NGOs. Ingawa makundi yanaweza kuungana au kusambazwa au kupanuka ili kukidhi mahitaji ya masuala kwa kipindi hicho upande, misingi ya uwanachama itabakia. Kuboresha uratibu miongoni mwa wadau chini ya ASDP II, hasa katika sekta binafsi, TWGs lazima zipanuliwe na kukaribisha ushiriki wa washirika wa maendeleo wataalam, pamoja na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na sekta binafsi kushiriki katika eneo la ufadhili. TWGs itatoa mwongozo wa mpango juu ya masuala ya kiufundi na / au usimamizi na ushauri TCD. Watakuwa wakikutana kwa muda na dharura ili kusimamia shughuli za jumla ya chini ya TWG na kutatua masuala ya kiufundi. Watakutana angalau kila mwezi na kushirikisha wajumbe ambao ni pamoja na washirika wa maendeleo na sekta binafsi lakini unaweza kufanyika baada ya miezi mitatu. Kikundi kazi cha Watalaamu kitafanya rejea za taarifa za robo mwaka kuanzia ngazi za serikali za mitaa na vyanzo vingine (ikiwa ni pamoja miradi iliyo nje ya bajeti), na kuwajulisha mikutano ya TCD na Kamati ya Uongozi wa maendeleo ya miradi mbalimbali katika ngazi ya kiufundi. Kazi nyingine muhimu ya TWGs itakuwa ya kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mapendekezo ya JSR iliyopita ili kuhakikisha kuwa yanajumuishwa katika mipango yao ya kazi ya kila mwaka. TWGs watatakiwa kuhakikisha kuwa kazi zote zilizotolewa na TCD zinatekelezwa.

429 mpangilio wa TWGs utakuwa katika ngazi tatu

**Kikundi kazi cha eneo kuu la proramu:** hiki ni kikundi kazi kuhusu masuala ya maeneo makuu ya manne ya program.Wajumbe wake ni wenyeviti wa maeneo makuu ya programu. Mwenyekiti / Mwakilishi kutoka kikundi cha Ufuatiliaji na Tathmini na Mwenyekiti / Mwakilishi kutoka kikundi cha Mipango na Bajeti (PB). NCU itakuwa inaratibu vikundi hivi.

Kulingana na hali na mahitaji, maeneo ya programu yanaweza kugawanywa katika maeneo madogo ili kuongeza ufanisi.TDC itaidhinisha uundaji wa vikudi hivi. Vikundi vyote vitaratibiwa na NCU.

430 Wajumbe wa TWG watakuwa kama wawezeshaji wa kazi za kiufundi na / au usimamizi katika shughuli zitokanazo na maombi kutoka Serikali za Mitaa. Kila TWG itachangia utaalamu wa kiufundi na ushauri kulingana na majukumu ya kikundi na katika kukabiliana na mahitaji. Shughuli za msingi na wajibu wa TWGs itakuwa ni pamoja na:

- Kuandaa taarifa ya utekelezaji na kuwasilisha TCD
- Kutoa utaalamu kwenye maandalizi ya mpango kazi na utekelezaji wa ASDP II na kuwasilisha kwenye TCD
- Kutoa ufumbuzi kwa vikwazo vya utekelezaji
- Kufanya uchambuzi kwa masuala ya kiufundi ya matokeo
- Kutoa ufumbuzi kwa masuala yaliyowasilishwa.

431 TWGs pia itatoa timu ya uwezeshaji wa taifa ambayo itatoa Wajumbe (mmoja au Zaidi) wa TWGs ambao watakuwa wanatumwa kwa misingi ya dharula ili kusaidia katika utekelezaji au kutatua matatizo katika ngazi ya mradi

**432 Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa Sekta ya Kilimo (NCU)** kitakuwa kinangozwa na Mratibu wa Taifa wa ASDP II na ni chombo ambacho kitakuwa kinawajibika moja kwa moja kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo. Kiutaratibu utekelezaji wa kazi za kila siku za programu ni pamoja na kufuatilia utekelezaji na kuitisha mikutano yote ya ASDP II. Timu itaripoti kwa TDC kwa masuala ya kiutendaji na itaundwa na wataalamu wafuatao.

- Wajumbe wenye ujuzi wa usimamizi wa mpango ambao wataongozwa na Mratibu wa Taifa wa ASDP II, mwenye ujuzi na uzoefu katika fani za kilimo
- Wataalam katika: biashara na uzalishaji; masoko na mnyororo wa thamani (Kwa ajili ya mazao, mifugo, na uvuvi);
- Wachambuzi wa sera na historia ya kilimo/uchumi na uzoefu mpana wa Kilimo-biashara
- Mtaalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini
- Mtaalamu wa usimamizi wa mawasiliano na maarifa
- Mtaalamu wa mipango, fedha na bajeti
- Mtaalamu wa uhasibu na manunuzi

Muundo wa NCU utaandaliwa ili kukidhi baadhi ya marekebisho katika ASLMs na serikali.

433 Wao pia watapewa uwezekano wa kuwa na wataalamu elekezi ambao watakuwa wanashauri kulingana na mahitaji yanavyojitokeza.

434 Ili kuhakikisha uwajibikaji, NCU itapewa Hadidu za rejea na mikataba ya kazi kwa kuzingatia taratibu za uratibu wa sekta na usimamizi wa programu ya ASDP II kwa kutumia viashiria vya programu kwa muda wote wa utekelezaji. Wajumbe wa timu watapewa vyombo vya usafiri , ofisi na vifaa vya mawasiliano ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Itakuwa na wajibu wa:

- Kutoa kichocheo na kusaidia jukumu la kusukuma ajenda ya mageuzi ya kilimo
- Kusaidia na kutumika kama sekretarieti kwa TCD, ASC, ASCG, na NASSM na kuhudhuria mikutano yote
- Kuimarisha mawasiliano na mwingiliano wa karibu na vikundi kazi (TWGs) katika kutekeleza shughuli zao muhimu
- Kuimarisha mtandao wa kubadilishana taarifa kati ya wadau wote juu ya shughuli zao (ikiwa ni pamoja na miradi ya ndani ya bajeti na nje ya bajeti); na kutambua wadau wote muhimu
- Kuratibu maandalizi ya Mpango Kazi na Bajeti Jumuishi ya ASDP II ya mwaka kwa ushirikiano wa karibu na TWGs, washirika wa maendeleo ili kujumuisha shughuli za nje ya bajeti,
- Kuratibu,kuhuisha, kuoanisha utekelezaji wa miradi ya sekta ya kilimo na utekelezaji ndani ya mfumo wa ASDP II
- Kusimamia, kufuatilia, kutathmini, kuoanisha na kuratibu utekelezaji wa shughuli zote za ASDP II
- Kukusanya, kuchambua, kuratibu na kutoa taarifa ya utekelezaji wa programu
- Kuandaa kila baada ya miezi mitatu, nusu mwaka na kila mwaka taarifa ya utekelezaji wa ASDP II

na kuwasilisha kwenye TDC, ASC na vikao vingine vya taifa.

- Kutoa msaada wa kiufundi juu ya ufuatiliaji na tathmini jumuishi ya programu
- Kutoa msaada wa uchambuzi na kutatua matatizo kwenye maeneo makuu ya programu
- Kutoa miongozo na mawasiliano kuhusu utekelezaji wa ASDP II
- Kuweka na kushiriki njia bora na mambo ya kujifunza ya kilimo kwa kutumia uzoefu wa njia ya Mtazamo Mpana wa sekta
- Kusaidia kuratibu ASDP II katika ukaguzi wa fedha na kuwasilisha kwenye TDC na ASC
- Kuandaa taarifa za ukaguzi wa kifedha na utekelezaji wa ASDP II
- Kujumuisha wadau wote wa sekta katika shughuli za ASDP II
- Kuandaa utaratibu endelevu wa ushirikiano na uratibu kwa wadau wote katika ASDP II
- Kuendelea kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maendeleo ya kila siku ya ASDP II
- Kutambua hatua sahihi za kuchukua kutimiza malengo ya ASDP II na serikali na
- Kutoa huduma ya secretariat kwa vikao vyote vya ASDP II

435 **Mkutano wa Mashauriano wa Sekta ya Kilimo (ASCG).** Hili ni jukwaa muhimu la mashauriano, hata hivyo si sehemu ya maamuzi ya ASDP II. ASCG itatoa mashauriano na ushauri katika serikali (ASLMs), washirika wote wa maendeleo, sekta binafsi na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (CSO na PSO) katika sekta ya kilimo. ASCG itaratibu mazungumzo katika ngazi mbili: mazungumzo kuhusu sera ya sekta na kanuni; mipango ya kila mwaka, bajeti ya kila mwaka ya sekta ya kilimo / umma, ukaguzi na ripoti ya matumizi (ASR / PER)

436 Kazi za ASCG ni za ushauri zaidi katika sekta na hivyo kuna haja ya kupata taarifa kuhusu: (1) sera (Mpango wa Muda mrefu wa Maendeleo (LTDP), Mpango wa Maendeleo wa Miaka Tano, sera za sekta ya kilimo,GBS, Bajeti ya serikali katika kilimo); na (2) masuala ya bajeti na matumizi ya umma. Mkutano ya ASCG utabaki kuwa moja ya miundo ya msingi kwa ajili ya mchakato ya kitaifa na kutoa ushauri kwa ASC juu ya

(i) Mpango wa Mtazamo wa Maendeleo wa Muda Mrefu na mchakato wa Mpango wa Miaka Tano wa Maendeleo

(ii) Bajeti ya Taifa na mchakato wa mapitio ya matumizi ya fedha za umma(PER)

437 ASCG itawezesha majadiliano ya sekta juu ya masuala ya JAST na GBS, ambayo ni ya kujumuishwa kwenye mchakato wa LTDP na 5YDP na bajeti ya taifa / PER. Itakuwa inatumika kama jukwaa la:

i. Majadiliano ya kisera
ii. Kubadilishana taarifa
iii. Kutoa ushauri na majadiliano juu ya bajeti na vipaumbele
iv. Mashauriano juu ya vipaumbele vya sekta, mikakati na utekelezaji wa programu ikiwa ni pamoja na mahusiano na sekta nyingine kama vile mali asili
v. Uchambuzi wa pamoja na tathmini ya masuala ya sekta ya kilimo / utekelezaji na uzinduzi wa masuala muhimu ya sekta
vi. Kutoa ushauri wa masuala ya kimkakati, bajeti na masuala mengine

438 Jedwali Na. A1 linatoa muhtasari wa eneo la uratibu wa sekta ya ASDP II.

**Jedwali Na. A1: Muhtasari wa uratibu wa ASDP II, utaratibu, wajumbe na kazi**

| Aina ya Mkutano/chombo | Wajumbe | Majukumu |
|---|---|---|
| i) **Mkutano Wa taifa wa Wadau wa Sekta ya Kilimo (NASSM).** Ukiongozwa na Waziri Mkuu | Mawaziri wa Wizara za Sekta ya Kilimo na Wizara zingine zinazohusiana na kilimo, Washirika wa Maendeleo, na Sekta binafsi, taasisi zisizo za kiserikali, RS, Serikali za Mitaa, Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya (DEDs); DAICOs, DLFOs; viongozi wa utafiti; maafisa wa mafunzo; wawakilishi wa mafunzo; bodi za mazao; taasisi za fedha; Vyama vya wakulima / vyama vya ushirika na, vyama vya bidhaa, na vyama vya kilimo / SACCOS; wawakilishi wa mashirika mengine ya wadau, Wakurugenzi wa Mipango na sera wa Wizara za Sekta ya Kilimo DPP wa wizara ya kilimo-Sekretarieti<br>NCU: Waandishi | Ajenda itaamuliwa na wadau: Masuala ya kujadiliwa ni pamoja na: kutoa ushauri na miongozo ya sera kwenye ajenda ya mageuzi ya kilimo; kutoa ushauri na mwongozo wa utekelezaji wa ASDP II; kuwezesha na kutoa msaada inapohitajika, kuwaalika washirika wengine muhimu katika sekta hiyo. |
| Kamati ya Usimamizi na Maamuzi ya Sekta ya kilimo (ASC) ikiongozwa na: Waziri ofisi ya Waziri Mkuu | Makatibu Wakuu wa Wizara za Sekta ya Kilimo na wa Wizara zinazohusiana (ASLM na Wengine); Mwenyekitiwa AWG,wajumbe 2 wa sekta binafsi (wenyeviti), wajumbe 2 wawakilishi wa sekta binafsi, wajumbe 3 wawakilishi wa NGOs, NSAs; DPPs wa ASLMs (mazao, mifugo na uvuvi); NCU – Secretariati | Kupitia na kuidhinisha mipango ya ASDP II, bajeti, ripoti za ufuatiliaji na tathmini,<br>Kuidhinisha Hadidu za Rejea za mapitio ya sekta na matumizi ya fedha za umma (JSR / ASR / PER) na Ufuatiliaji na Tathmini,<br>Kuwezesha na kuidhinisha uanzishwaji wa mifumo ya uwezeshaji wa kifedha wa ASDP II,<br>Kujadili masuala ya ushirikiano wa pamoja na kubalishana taarifa,<br>Kufanya mapitio na kuidhinisha ripoti za fedha na ukaguzi za ASDP II,<br>Kuidhinisha mabadiliko katika sera na kanuni za kuwasilishwa Bungeni,<br>Kupendekeza kalenda ya mkutano wa Taifa wa Wadau wa Kilimo (NASSM) na ajenda zake<br>Kuidhinisha masuala ya uendeshaji wa NCU |
| Mkutano wa Mashauriano wa Sekta ya Kilimo (ASCG)<br>mwenyekiti: Waziri ofisi ya Waziri Mkuu, | Wajumbe wote katika Sekta ya Kilimo (GoT, Sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo / Washirika<br>na NGOs / NSA) (ndani na Kimataifa)<br>Taasisi za Mafunzo na Utafiti<br>DPP- wizara ya kilimo -Secretariati<br>NCU- waandishi | Kutoa ushauri juu ya sera za sekta, mpango, bajeti, ukaguzi wa matumizi ya fedha za umma katika kilimo,<br>Kuratibu mazungumzo ya wadau mara kwa mara juu ya sera za sekta,<br>Kutoa msaada (fedha, vifaa na vingine) kwa sekta hiyo,<br>Kushiriki katika mikutano ya kila mwaka ya mipango na bajeti jumuishi,<br>Majadiliano na sauti juu ya maoni ya washiriki wa maendeleo, Sekta binafsi, NGOs / NSAeneo dogoBOs. |

| Aina ya Mkutano/chombo | Wajumbe | Majukumu |
|---|---|---|
| Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi (TCD) mwenyekiti: **Katibu Mkuu / Mkurugenzi ofisi ya Waziri Mkuu** | Wakurugenzi wa maeneo makuu ya programu toka ASLMS, viongozi/wenyeviti wa maeneo ya programu, TAMISEMI Uratibu wa ASDP II Mkuu waTume ya Taifa ya Umwagiliaji. Mkuu waTume ya Maendeleo ya Ushirika Mkuu bodi ya stakabadhi mazao ghalani, NBS, Wizara ya Fedha na Mipango ,Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Taasis ya Lishe, Wizara ya Elimu, Wawakilishi wa taasisi za utafiti/mafunzo ya kilimo<br>Mratibu Kitengo cha uratibu cha Taifa (NCU) **-Secretariat** | Kupitia, kuchambuana kuunganisha mipango,bajeti, ripoti za Ufuatiliaji na Tathmini kwa maeneo makuu ya ASDP II,<br>Kupendekeza kwenye ASC juu ya miongozo ,taratibu za usimamizi na utekelezaji wa ASDP II,<br>Kupendekeza kwenye ASC ToR za JSR / ASR / PER na Ufuatiliaji na Tathmini,<br>Kuandaa na kupitia nyaraka za kuwasilisha ASCG na ASC<br>Kupitia na kupendekeza mabadiliko sera na kanuni katika sekta na kuwasilisha kwenye ASC,<br>Kutoa ushauri na uratibu kwa vikundi kazi vya ASDP II,<br>Kupendekeza kwa ASC juu masuala ya uendeshaji usimamizi na uratibu wa NCU. |
| **Vikundi kazi vya programu (TWGs)**wenyeviti/viongozi wa maeneo ya programu | viongozi wa maeneo makuu na madogo ya programu , Wataalamu wa kiufundi waliochaguliwa kutoka ASLMs mbalimbali, Sekta binafsi, Wataalamu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Watendaji wasio wa kiserikali na wawakilishi wa timu ya nchi ya CAADP kwa masuala mtambuka. | Kuandaa na kuchambua mipango na bajeti za ASDP II na kuwasilisha kwa wakuu wa maeneo ya program, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa ASDP II.<br>Kutoa ushauri juu ya matatizo ya utekelezaji na kutoa mwongozo kwa TCD,<br>Kuwasilisha masuala mtambuka na kuyajadili. |
| **Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa programu (NCU)** | Mratibu wa taifa wa programu<br>Wataalamu katika: tija na biashara; masoko na mnyororo wa thamani;(kwa mazao,mifugo na uvuvi); Ufuatiliaji na Tathmini; mchambuzi wa sera za kilimo; | Kuwa kichocheo na kusukuma ajenda ya mageuziya kilimo;<br>Kuandaa Mipango kazi jumuishi na bajeti chini ya ASDP II kwa kazi zote ndani na nje ya bajeti;<br>Kusimamia, kufuatilia, kutathmini, kuunganisha na kuratibu utekelezaji wa ASDP II;<br>Kuandaa ripoti za utekelezaji wa robo mwaka kwa ajili ya kuwasilisha mbele ya TDC, ASC na vikao vingine vya kitaifa;<br>Kutoa msaada wa kiufundi juu ya ufuatiliaji wa pamoja, na kutathmini mpango ya kuwasilisha mbele ya Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi (TCD)<br>Kutoa usaidizi wa uchambuzi vikwazo,maandalizi ya miongozo na vifaa vya mawasiliano ya ASDP II;<br>Kuratibu kazi za ufuatiliaji na tathmini; kuanzisha na kubadilishana mbinu bora za mafunzo yaliyopatikana chini ya SWAp ya Kilimo;<br>Kuwezesha na kuratibu ukaguzi wa fedha za ASDP II na kuwasilisha kwenye TDC<br>Kutoa huduma ya sekretarieti kwenye vikao vya ASDP II |

***Uratibu katika ngazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa***

439. Miundo ya ASDP-1 katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa iutaimarishwa na kuendelea kutumika chini ya ASDP II. Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADP) itaendelea kuwa chombo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kilimo katika ngazi za Mamlaka ya serikali za mitaa. Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya (DED) atasimamia shughuli zote na matumizi ya fedha katika ngazi hii. Timu ya Baraza la Usimamizi (CMT), ambayo inaongozwa na Mkurugenzi na kuhudhuriwa na wakuu wote wa idara, akiwemo DAICO na DLFO watajadili juu ya masuala ya maendeleo ya kilimo chini ya DADP. Muundo wa kina wa mfumo wa uratibu wa kijiji hadi ngazi ya kitaifa na vyombo mbalimbali umeonyeshwa katika Kiambatisho III.

440. Mipango ya DADPs inaibuliwa kutoka kwenye jamii vijijini kupitia mchakato wa *O&OD* na kujumuishwa katika Mipango ya Maendeleo ya kilimo ya Kijiji.Mchakato unaongozwa na Afisa ugani (VAEO), Afisa Mtendaji wa Kijiji (VEO) na kuungwa mkono na Timu ya uwezeshaji ya Wilaya ambayo huwezesha maandalizi ya mpango kulingana na Miongozo ya DADPs. Mapendekezo kutoka vijijini huwasilishwa kwenye kata ambapo huunganishwa na Maafisa kilimo wa Kata (WAEO) chini ya usimamizi wa Afisa Mtendaji wa Kata (watendaji wa kata) na kuongozwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata na kuwasilishwa kwa DED ambapo mipango hii inajumuishwa katika ngazi ya wilaya na kuwa DADPs. Lengo la DADP ni kuongeza tija katika kilimo ili kufikia malengo ya uwekezaji ya ASDP II ambayo ni kuleta mageuzi ya kilimo kwa kuendeleza mazao ya kipaumbele ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuzingatia mnyororo wa thamani kwenye kanda za kiikolojia. Shughuli hizi zinasimamiwa na waratibu wa kanda za kilimo, Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II na vikundi kazi husika (TWGs).

441. Kama njia ya msingi ya uratibu katika ngazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, mnyororo wa thamani wa bidhaa ngazi ya wilaya (DVC) kati ya wadau wa sekta katika hii itaunganisha na wadau wakuu katika mazao husika ya kipaumbele katika mnyororo wa thamani wa bidhaa pamoja kuendeleza na kuendesha utekelezaji wa shughuli za DADP ambazo ni pamoja na masuala mbalimbali kama vile kuongeza uzalishaji, kuongeza thamani na upatikanaji wa soko. Wadau katika ngazi hii ni pamoja na sekta binafsi (wafanyabiashara, wasindikaji, wasafirishaji, taasisi za fedha, nk), NGOs, washirika wa maendeleo na taasisi mbalimbali za umma ambao wanaweza kushirikiana kutoa aina mbalimbali za misaada ya kiufundi.

442. Kwa hivyo ni muhimu kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuunda DADPs jumuishi ambayo inajumuisha shughuli zote za maendeleo zinazotekelezwa kwa kupitia bajeti ya ndani na nje ya bajeti ya serikali katika miradi ya ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwa ajili hiyo, ni lazima kuwepo na utaratibu imara ili kuhakikisha kwamba mchango wa kila mmoja unakuwepo na kuwa na taarifa sahihi juu ya hatua zote za utekelezaji wa mpango.

***Uratibu ngazi ya taifa katika mamlaka ya serikali za mitaa – TAMISEMI***

443. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinasimamiwa na kuongozwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Idara ya Uratibu wa Sekta ina wajibu wa kusimamia na kuratibu utekelezaji ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa (RSs). Mfumo wa uratibu chini ya ASDP-1 ulifanya kazi vizuri na ASDP II itaendelea kuimarisha mfumo huo. Katika ngazi ya Mkoa, kutakuwa na Kamati ya Mkoa ya Ushauri ya (RCC) chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa (RC). Kamati inatoa ushauri katika wilaya, kufuatilia na kusimamia shughuli wilayani ikiwa ni pamoja na DADPs.

444. Kila RS inaongozwa na Katibu Tawala wa Mkoa (RAS). Nafasi ya RAS ni kusaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa DADPs, kutoa mafunzo na usimamizi na msaada katika utekelezaji wa DADPs. RAS pia atasaidia katika utoaji wa taarifa za robo mwaka na kila mwaka kwa kufuata Miongozo ya DADPs.

445. Msaidizi wa Katibu Tawala sehemu ya Uchumi na sehemu ya Uzalishaji katika RS watawajibika moja kwa moja kusaidia shughuli za maendeleo ndani ya mkoa na kusaidiwa kazi na waratibu wa ASDP Mkoa na maafisa wenzake kwenye eneo hilo. Maafisa hao huzunguka kwenye wilaya na kutoa msaada wa kiufundi, na usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Waratibu wa ASDP II pia wana wajibu wa kufuatilia na kutathmini shughuli za kilimo za wilaya zinazotekelezwa chini ya ASDP II. RS itafanya kazi kwa karibu na TWGs husika pamoja na NCU ili kuhakikisha utekelezaji sahihi wa programu na kutoa taarifa zote za utekelezaji wa ASDP II kwa wadau wote.

# KIAMBATISHO Na. IV: Mahitaji ya Bajeti ya Programu na Miradi

| Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya Pili (ASDP II) Bajeti2017/2018 - 2021/2022 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ENEO KUU LA PROGRAMU | ENEO DOGO LA PROGRAMU | MAENEO YA UWEKEZAJI YA KIPAUMBELE | MIRADI | MWAKA WA 1 | MWAKA WA 2 | MWAKA WA 3 | MWAKA WA 4 | MWAKA WA 5 | Bajeti za Miradi (Miaka 5) |
| | | | | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | |
| **Bajeti ya Eneo kuu la 4:(Uwezeshi wa Sekta, Uratibu,Ufuatiliaji na Tathmini)** | | | | | | | | | |
| **Uwezeshi wa Sekta, Urati-bu,Ufuatiliaji na Tathmini** | **4.1 muundo wa sera na kanuni** | 4.1.1 Sera na Mfumo wa Udhibiti na Maendeleo ya Mazingira ya Bi-ashara | 4.1.1.1 Tathmini na kuoanisha sera zinazo-husiana na sekta ya kilimo na mfumo wa udhibiti wa mazingira bora ya biashara | 310,300,000 | 967,330,000 | 352,038,000 | 387,241,800 | 425,965,980 | 2,442,875,780 |
| | | | 4.1.1.2 Kuimarisha Ufuatiliaji, udhibiti na Uhimilivu (MCS) kwa Uvuvi usio halali, Uvuvi usiorejeshwa na usio na sheria (IUU Uvuvi) | 6,019,012,325 | 2,022,862,500 | 1,646,501,250 | 1,684,491,375 | 1,846,466,513 | 13,219,333,963 |
| | | | 4.1.1.4 Kuimarisha na kudhibiti ajira ya watoto katika Kilimo | 1,584,790,000 | 1,050,194,000 | 1,094,008,400 | 808,132,240 | 684,175,260 | 5,221,299,900 |
| | | | 4.1.1.5 Kuhamasisha kazi zenye staha na salam katika sekta ya kilimo | 587,350,000 | 932,655,000 | 426,593,000 | - | - | 1,946,598,000 |
| | **Jumla-Eneo Dogo** | | | **8,501,452,325** | **4,973,041,500** | **3,519,140,650** | **2,879,865,415** | **2,956,607,753** | **22,830,107,643** |

| Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) Bajeti 2017/2018 - 2021/2022 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ENEO KUU LA PROGRAMU | ENEO DOGO LA PROGRAMU | MAENEO YA UWEKEZAJI YA KIPAUMBELE | MIRADI | MWAKA WA 1 | MWAKA WA 2 | MWAKA WA 3 | MWAKA WA 4 | MWAKA WA 5 | Bajeti za Miradi (Miaka 5) |
| | | | | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | |
| | **4.2 Kuwezesha wadau na taasisi** | 4.2.1 Kuimarisha uwezo wa taasisi na wa kiufundi wa wazalishaji wadogo waliopo na wapya, biashara na vikundi vya wakulima wa usindikaji na vyama vya ushirika | 4.2.1.1 Kuimarisha Ushirika, vyama vya wakulima na vyama vingine vinavyohusika kwenye mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo | 4,013,830,000 | 3,741,656,000 | 2,298,944,600 | 2,116,074,810 | 1,194,736,731 | 13,365,242,141 |
| | | 4.2.2 Kukuza na kuimarisha ushirikiano wa kijinsia katika sekta ya kilimo | 4.2.2.1 Kuboresha faida kwa wanawake na vijana kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa za kilimo (WAYA) | 3,024,921,667 | 3,238,193,500 | 2,779,148,100 | 852,268,200 | 930,673,180 | 10,825,204,647 |
| | **Jumla -Eneo Dogo** | | | **7,038,751,667** | **6,979,849,500** | **5,078,092,700** | **2,968,343,010** | **2,125,409,911** | **24,190,446,788** |
| | **4.3 Uratibu wa sekta wa ASDP II (kupanga na kutekelezangazi ya kitaifa, mkoa na Mamlaka ya Serikali za mitaa)** | 4.3.1 Kuboresha na kuimarisha uratibu (kutoka PO-RALG , RSs na LGA) na ura-tibu kati ya ASLMs | 4.3.1.1 Kuimarisha mifumo ya taasisi ya sekta ya kilimo kwa uratibu na mawasiliano bora | 6,872,144,000 | 6,672,824,000 | 4,280,182,000 | 2,114,683,800 | 2,196,777,780 | 22,136,611,580 |
| | **Jumla- Eneo Dogo** | | | | | | | | **22,136,611,580** |

**Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya Pili (ASDP II) Bajeti 2017/2018 - 2021/2022**

| ENEO KUU LA PROGRAMU | ENEO DOGO LA PROGRAMU | MAENEO YA UWEKEZAJI YA KIPAUMBELE | MIRADI | MWAKA WA 1 | MWAKA WA 2 | MWAKA WA 3 | MWAKA WA 4 | MWAKA WA 5 | Bajeti za Miradi (Miaka 5) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | |
| | 4.4 Ufuatiliaji na Tathmini (ikiwa ni pamoja na takwimu za Kilimo) | 4.4.1 Uwezo na mifumo ya ukusanyaji na usimamizi bora wa takwimu za kilimo | 4.4.1.1 Kuboresha uwezo na ushirikiano wa mifumo ya ukusanyaji na usimamizi wa takwimu za kilimo (m.f G ARDS, NSCA, AASS) kwa kuimarisha usimamizi wa matokeo katika ngazi zote. | 4,425,342,000 | 6,997,451,125 | 2,879,056,270 | 2,591,046,637 | 2,195,567,312 | 19,088,463,344 |
| | | 4.4.2 Kuendeleza mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini katika sekta ya kilimo | 4.4.2.1 Kuimarisha na kuunganisha mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini ya sekta ya kilimo kwa ufanisi na ufasaha. | 11,332,900,000 | 3,208,586,000 | 1,596,941,100 | 1,293,583,000 | 1,122,429,763 | 18,554,439,863 |
| | **Jumla – Eneo Dogo** | | | **15,758,242,000** | **10,206,037,125** | **4,475,997,370** | **3,884,629,637** | **3,317,997,074** | **37,642,903,206** |
| | 4.5 Maendeleo ya uwezo wa kitaasisi, na usimamizi wa maarifa na TEHAMA | 4.5.1 Uboreshaji wa Uwezo katika ngazi zote | 4.5.1.1 Kuboresha uwezo wa kitaifa, RS na Mamlaka ya Serikali za mitaa (idadi na ubora) katika ngazi zote | 3,429,157,500 | 6,349,550,000 | 3,781,150,000 | 2,501,350,000 | 1,142,220,000 | 17,203,427,500 |
| | | 4.5.2 Uboreshaji wa TEHAMA kwa Huduma na mifumo ya taarifa za Kilimo | 4.5.2.1 Kuendeleza usimamizi kamili wa maarifa na mfumo wa TEHAMA katika ngazi zote | 3,047,300,000 | 2,376,405,000 | 336,377,000 | 212,645,350 | 400,139,770 | 6,372,867,120 |
| | 4.6. Upatikanaji wa fedha vijijini | 4.6.1 Kutoa huduma za ufadhili | 4.6.1.1 Upatikanaji wa fedha za kilimo Kwa ajili ya mnyororo wa thamani wa bidhaa | 1,481,305,000 | 1,833,055,000 | 1,599,616,600 | 1,513,723,796 | 638,604,290 | 7,066,304,686 |
| | **Jumla- Eneo Dogo** | | | **7,957,762,500** | **10,559,010,000** | **5,717,143,600** | **4,227,719,146** | **2,180,964,060** | **30,642,599,306** |

| Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) Bajeti 2017/2018 - 2021/2022 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ENEO KUU LA PROGRAMU | ENEO DOGO LA PROGRA-MU | MAENEO YA UWEKEZAJI YA KIPAUM-BELE | MIRADI | MWAKA WA 1 | MWAKA WA 2 | MWAKA WA 3 | MWAKA WA 4 | MWAKA WA 5 | Bajeti za Miradi (Miaka 5) |
| | | | | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | |
| **JUMLA-ENEO KUU** | | | | **39,256,208,492** | **32,717,938,125** | **18,790,374,320** | **13,960,557,208** | **10,580,978,798** | **137,442,668,522** |
| **Bajeti ya Eneo kuu la 3 (Biashara na Uongezaji Thamani kwenye Mazao)** | | | | | | | | | |
| 3.Biashara na kuongeza thamani | 3.1 Masoko | 3.1.1 Kuendeleza upatikanaji wa soko kwa bidhaa zote za kipaum-bele. | 3.1.1.1 Kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya masoko kwa kupata masoko ya ndani na ya nje | 98,345,805,000 | 456,727,977,000 | 568,733,077,800 | 635,560,647,800 | 684,371,127,488 | 2,443,738,635,088 |
| | | 3.1.2 kuendeleza upatikanaji wa soko kwa ajili ya uvuvi na bidhaa za mifugo | 3.1.2.1 Kuboresha na kuendeleza miundombinu ya soko la mifugo samaki kwa ajilli ya mapato ya ndani yaliyoongezeka na soko lililopa-nuka | 7,847,305,000 | 9,464,598,000 | 156,458,314,800 | 171,750,092,140 | 368,188,102,190 | 713,708,412,130 |
| | | | 3.1.2.2 Kuboresha eneo na kubore-shwa upatikanaji/ ufikiaji wa soko la kuku | 742,875,000 | 2,067,455,500 | 2,247,754,750 | 369,351,650 | 282,526,169 | 5,709,963,069 |
| | | | 3.1.2.3 Kuimar-isha mfumo wa ufuatiliaji (kitam-bulisho)cha mifugo uvuvi kwa ajili ya kukuza biashara na uuzaji | 1,833,825,000 | 737,989,000 | 732,995,000 | 643,247,150 | 629,633,366 | 4,577,689,516 |

| ENEO KUU LA PROGRAMU | ENEO DOGO LA PROGRA-MU | MAENEO YA UWEKEZAJI YA KIPAUM-BELE | MIRADI | MWAKA WA 1 | MWAKA WA 2 | MWAKA WA 3 | MWAKA WA 4 | MWAKA WA 5 | Bajeti za Miradi (Miaka 5) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | |
| | | | 3.1.2.4 Kukuza na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika mnyororo wa tha-mani wa bidhaa | 1,238,470,000 | 4,073,370,000 | 4,376,132,500 | 1,442,114,675 | 13,998,798,538 | 25,128,885,713 |
| | **Jumla -Eneo Dogo** | | | **110,008,280,000** | **473,071,389,500** | **732,548,274,850** | **809,765,453,415** | **1,067,470,187,751** | **3,192,863,585,516** |
| | 3.2 Maendeleo ya bishara za kilimo kuongeza thamani na usindikaji wa mazao | 3.2.1 Maendeleo ya usindikaji na kuongeza thamani ya Mazao, mifugo na bidhaa za uvuvi | 3.2.1.1 Kuimarisha na kuendeleza viwanda vya usindikaji wa mazao kwa kuongeza thamani ya bidhaa zote za kipaumbele | 10,332,690,000 | 14,447,726,000 | 15,432,309,800 | 16,806,037,745 | 18,521,995,935 | 75,540,759,480 |

| Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) Bajeti 2017/2018 - 2021/2022 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ENEO KUU LA PROGRAMU | ENEO DOGO LA PROGRAMU | MAENEO YA UWEKEZAJI YA KIPAUMBELE | MIRADI | MWAKA WA 1 | MWAKA WA 2 | MWAKA WA 3 | MWAKA WA 4 | MWAKA WA 5 | Bajeti za Miradi (Miaka 5) |
| | | | | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | |
| | | | 3.2.1.2 Kuboresha mnyororo wa thamani wa maziwa | 8,885,940,000 | 8,536,245,500 | 8,013,592,850 | 4,212,492,265 | 4,570,786,337 | 34,219,056,952 |
| | | | 3.2.1.3 Kuimarisha mnyororo wa thamani wa kwato na ngozi | 13,914,590,000 | 10,119,086,500 | 19,593,434,900 | 5,971,608,190 | 5,306,513,481 | 54,905,233,071 |
| | | | 3.2.1.4 Kuimarisha mnyororo wa thamani wa bidhaa za kilimo cha mazao ya bustani | 4,994,890,000 | 1,621,794,000 | 4,126,542,200 | 1,273,611,645 | 1,386,890,047 | 13,403,727,892 |
| | | | 3.2.1.5 Kuendeleza Mkakati wa vifaa vya ghala ili kuunganishwa na Ghala la Soko la Bidhaa | 26,327,700,000 | 21,011,437,000 | 22,694,470,650 | 24,804,587,300 | 27,302,251,665 | 122,140,446,615 |
| | | | 3.2.1.6 Kuendeleza na kuhamasisha ongezeko la thamani kwa bidhaa za kipaumbele za uvuvi na ufugaji | 5,757,355,000 | 6,752,314,000 | 7,266,361,600 | 7,867,464,680 | 8,431,888,328 | 36,075,383,608 |
| | | | 3.2.1.7 Kuboresha Ongezeko la thamani ya nyama, kwato, pembe | 9,632,790,000 | 12,738,732,000 | 3,507,122,200 | 504,939,770 | 225,448,930 | 26,609,032,900 |
| | | | 3.2.1.8 Kuimarisha usimamiziwa mazao baada ya mavuno pamoja na mnyororo wa kusambaza chakula kwa ajili ya usalama endelevu wa chakula na lishe | 1,088,340,000 | 2,710,417,500 | 12,533,992,850 | 2,323,718,420 | 1,079,948,052 | 19,736,416,822 |
| | **Jumla- Eneo Dogo** | | | **80,934,295,000** | **77,937,752,500** | **93,167,827,050** | **63,764,460,015** | **66,825,722,774** | **382,630,057,339** |
| | **JUMLA ENEO KUU** | | | **190,942,575,000** | **551,009,142,000** | **825,716,101,900** | **873,529,913,430** | **1,134,295,910,524** | **3,575,493,642,854** |
| **Bajeti ya Eneo Kuu la 2 (Kuongeza Tija na Faida Katika Kilimo)** | | | | | | | | | |

| Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) Bajeti 2017/2018 - 2021/2022 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ENEO KUU LA PROGRAMU | ENEO DOGO LA PROGRAMU | MAENEO YA UWEKEZAJI YA KIPAUMBELE | MIRADI | Y1 | Y2 | Y3 | Y4 | Y5 | Bajeti za Miradi (Miaka 5) |
| | | | | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | |
| 2. Kuongeza Tija na Faida katika Kilimo | 2.1 Mafunzo ya ugani na huduma za mawasiliano | 2.1.1 Kuimarisha ugani wa kilimo, mafunzo na uendelezaji / huduma za taarifa (mazao, mifugo na uvuvi) | 2.1.1.1 Kuimarisha na kukuza huduma za ugani wa kilimo (bidhaa zote) | 1,311,912,630,000 | 772,651,750,500 | 849,529,380,050 | 838,081,042,930 | 921,147,859,276 | 4,693,322,662,756 |
| | | | 2.1.1.2 Kuimarisha mafunzo ya ustadi wa kilimo na ukuzaji (bidhaa zote) | 4,372,604,150 | 9,719,504,500 | 9,349,112,950 | 8,505,972,245 | 9,221,909,470 | 41,169,103,315 |
| | Jumla - Eneo Dogo | | | 1,316,285,234,150 | 782,371,255,000 | 858,878,493,000 | 846,587,015,175 | 930,369,768,745 | 4,734,491,766,070 |
| | 2.2 Upatikanaji wa pembejeo za kilimo na huduma za afya | 2.2.1 Upatikanaji Bora wa pembejeo na huduma za afya ya Mazao, Mifugo na uvuvi | 2.2.1.1 Kuboresha uwepo na upatikanaji wa pembejeo za ubora na za bei nafuu za kilimo kwa kuongeze-ka kwa tija na faida (bidhaa zote) | 149,389,300,000 | 136,694,880,000 | 150,284,368,000 | 164,670,257,650 | 181,057,283,415 | 782,096,089,065 |
| | | | 2.2.1.2 Kuboresha upatikanaji na uwepo wa pembejeo bora za kuku | 4,176,191,250 | 2,652,218,625 | 2,799,882,488 | 2,962,312,736 | 3,140,986,010 | 15,731,591,109 |
| | | | 2.2.1.3 Maendeleo ya uvuvi wa Tuna kwa ajili ya kuongezeka kwa tija | 1,664,250,000 | 93,407,668,200 | 768,004,545 | 1,098,600,080 | 987,463,628 | 97,925,986,452 |
| | | | 2.2.1.4 Kuimarisha na kuanzisha maeneo ya kutia nanga kwa ajili ya faida ya uvuvi | 1,146,337,500 | 4,533,411,750 | 5,008,172,925 | 4,245,593,993 | 4,638,653,392 | 19,572,169,559 |
| | | | 2.2.1.5 Maendeleo ya bandari ya uvuvi wa baharini ili kuongeza faida | 4,114,772,384 | 5,175,475,000 | 7,350,242,000 | 4,460,007,000 | 2,090,273,670 | 23,190,770,054 |

| Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) Bajeti 2017/2018 - 2021/2022 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ENEO KUU LA PROGRAMU | ENEO DOGO LA PROGRAMU | MAENEO YA UWEKEZAJI YA KIPAUMBELE | MIRADI | MWAKA WA 1 | MWAKA WA 2 | MWAKA WA 3 | MWAKA WA 4 | MWAKA WA 5 | Bajeti za Miradi (Miaka 5) |
| | | | | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | |
| | | | 2.2.1.6 Wavuvi wadogo ili kuboresha Uzalishaji wa Samaki na tija | 55,089,477,353 | 50,853,035,000 | 48,517,288,500 | 6,657,553,200 | 4,388,210,355 | 165,505,564,408 |
| | | | 2.2.1.7 Kuimarisha vitengo vya Usimamizi wa fukwe (BMUs) kwa usimamizi endelevu, usalama na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi | 2,537,220,000 | 2,134,277,250 | 2,199,129,975 | 2,146,830,473 | 2,319,001,645 | 11,336,459,342 |
| | | | 2.2.1.8 Uboreshaji wa huduma za afya ya mimea | 13,322,105,000 | 11,190,853,500 | 7,608,436,004 | 1,388,679,306 | 477,989,282 | 33,988,063,092 |
| | | | 2.2.1.9 Uzalishaji wa chanjo na madawa | 44,569,605,614 | 36,191,315,000 | 39,699,992,500 | 3,705,147,750 | 4,379,467,025 | 128,545,527,889 |
| | | | 2.2.1.10a Uboreshaji wa huduma za afya ya mifugo | 262,550,032,281 | 295,128,209,145 | 332,216,208,381 | 371,558,679,638 | 420,078,299,939 | 1,681,531,429,384 |
| | | | 2.2.1.10b Uboreshaji wa huduma za afya ya mifugo ya kwenye maji | 1,517,656,875 | 1,238,258,438 | 1,240,903,519 | 1,339,594,371 | 1,395,264,758 | 6,731,677,960 |
| | **Jumla ndogo** | | | **540,076,948,257** | **639,199,601,907** | **597,692,628,836** | **564,233,256,195** | **624,952,893,118** | **2,966,155,328,313** |
| | 2.3 Utafiti wa Kilimo kwa Maendeleo (AR4D) | 2.3.1 Kuimarisha AR4D (mazao, mifugo na uvuvi) | 2.3.1.1 Kuimarisha uwezo wa utafiti wa kilimo kwa maendeleo ya teknolojia, uhusiano wa viwanda na usambazaji wa matokeo (sekta ndogo ndogo) | 7,558,670,000 | 29,196,530,000 | 29,503,788,600 | 8,707,708,130 | 9,516,387,793 | 84,483,084,523 |
| | | 2.3.2 utafiti na maendeleo | 2.3.2.1 Maendeleo na usambaji wa teknolojia jumuishi kwa ajili ya kuboresha tija na uzalishaji (bidhaa zote) | 12,408,638,000 | 16,383,957,425 | 11,615,699,430 | 11,110,318,211 | 11,371,090,422 | 62,889,703,487 |

| ENEO KUU LA PROGRAMU | ENEO DOGO LA PROGRAMU | MAENEO YA UWEKEZAJI YA KIPAUMBELE | MIRADI | MWAKA WA 1 | MWAKA WA 2 | MWAKA WA 3 | MWAKA WA 4 | MWAKA WA 5 | Bajeti za Miradi (Miaka 5) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | |
| | | | 2.3.2.2 Kukuza na kuimarisha ufugaji kupitia teknolojia ya uzalishaji wa kisasa | 4,832,950,500 | 3,894,671,550 | 2,682,470,175 | 2,737,590,818 | 3,011,349,899 | 17,159,032,942 |
| | **Jumla - Eneo Dogo** | | | **24,800,258,500** | **49,475,158,975** | **43,801,958,205** | **22,555,617,158** | **23,898,828,114** | **164,531,820,952** |
| | 2.4 Upatikanaji wa Huduma za utumiaji wa mashine | 2.4.1 Kuimarisha na kukuza uchu-mi wa kilimo (mazao, mifugo na uvuvi) | 2.4.1.1 Kuimarisha na kukuza uchumi wa kilimo kwa ajili ya kuboresha mn-yororo wa thamani | 9,249,492,000 | 5,753,278,650 | 5,698,585,515 | 5,707,520,942 | 5,717,349,911 | 32,126,227,017 |
| | **Jumla - Eneo Dogo** | | | | | | | | **32,126,227,017** |
| | 2.5 usalama wa chakula na lishe | 2.5.1 usalama bora wa chakula na lishe | 2.5.1.1 Kuboresha upatikanaji, ubora na matumizi ya vyanzo vya vyakula vyenye ya virutubisho muhimu (bidhaa zote) | 14,152,477,500 | 11,721,816,750 | 12,960,295,425 | 14,297,133,428 | 10,393,795,970 | 63,525,519,073 |
| | | | 2.5.1.2 Kuongezeka kwa uzalishaji na kukuza uwele na mtama kwa ajili ya matumizi ya chakula majumbani | 20,537,475,000 | 22,167,043,500 | 23,954,717,850 | 25,921,159,635 | 28,084,245,599 | 120,664,641,584 |
| | **Jumla – Eneo dogo** | | | **34,689,952,500** | **33,888,860,250** | **36,915,013,275** | **40,218,293,063** | **38,478,041,569** | **184,190,160,656** |
| **JUMLA- ENEO KUU** | | | | **1,915,852,393,407** | **1,504,934,876,132** | **1,537,288,093,316** | **1,473,594,181,591** | **1,617,699,531,545** | **8,081,495,303,009** |
| | | | | | | | | | |
| **Bajeti ya Eneo kuu la 1 (Matumizi Endelevu ya Maji na Ardhi)** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) Bajeti 2017/2018 - 2021/2022** | | | | | | | | | |

| ENEO KUU LA PROGRAMU | ENEO DOGO LA PROGRAMU | MAENEO YA UWEKEZAJI YA KIPAUMBELE | MIRADI | MWAKA WA 1 | MWAKA WA 2 | MWAKA WA 3 | MWAKA WA 4 | MWAKA WA 5 | Bajeti za Miradi (Miaka 5) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | |
| 1 Matumizi Endelevu ya Maji na Ardhi | 1.1 Mpango wa matumizi ya ardhi na usimamizi wa mabwawa endelevu ya maji na udongo | 1.1.1 mpango wa matumizi ya ardhi na usimamizi wa mabwawa | 1.1.1.1 Mpango jumuishi wa matumizi ya ardhi na usimamizi kwa ajili ya uzalishaji endelevu wa kilimo na maendeleo ya viwanda (bidhaaa zote/kanda zote) | 29,758,830,000 | 31,014,157,500 | 34,532,074,500 | | | 95,305,062,000 |
| | | | 1.1.1.2 Uimarishaji wa uzalishaji wa malisho na uhifadhi kwa ajili ya uzalishaji endelevu wa mifugo | 14,132,350,000 | 14,517,360,000 | 13,715,440,000 | 13,501,214,000 | 16,283,985,400 | 72,150,349,400 |
| | | | 1.1.1.3 Kuchochea upatikanaji wa ardhi ya kilimo kwa ajili ya vijana | 4,464,055,000 | 4,149,595,000 | 5,753,069,750 | 4,533,911,000 | 6,321,240,750 | 25,221,871,500 |
| | | | 1.1.1.4 kuboresha uratibu wa mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa mabwawa kwa matumizi endelevu ya rasilimali (bidhaa zote) | - | 1,366,429,750 | 927,979,000 | 838,670,020 | 916,057,022 | 4,049,135,792 |
| | **Jumla - Eneo Dogo** | | | **48,355,235,000** | **51,047,542,250** | **54,928,563,250** | **18,873,795,020** | **23,521,283,172** | **196,726,418,692** |
| | 1.2 Matumizi jumuishi ya maji kwa kilimo cha umwagiliaji na maendeleo ya Mifugo na Uvuvi | 1.2.1 Mendeleo ya miundombinu ya umwagiliaji | 1.2.1.1 Ukarabati na kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya uzalishaji na tija | 16,369,940,000 | 184,589,225,292 | 172,338,444,067 | 175,277,962,887 | 189,618,773,923 | 738,194,346,168 |
| | | | 1.2.1.2 Ukuzaji wa Mfumo wa umwagiliaji mdogo kwa ajili ya uzalishaji na mavuno bora ya mazao | 5,873,183,333 | 50,128,619,250 | 57,162,204,550 | 59,915,108,463 | 65,430,495,378 | 238,509,610,973 |
| **Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) Bajeti 2017/2018 - 2021/2022** | | | | | | | | | |

| ENEO KUU LA PROGRAMU | ENEO DOGO LA PROGRAMU | MAENEO YA UWEKEZAJI YA KIPAUMBELE | MIRADI | MWAKA WA 1 | MWAKA WA 2 | MWAKA WA 3 | MWAKA WA 4 | MWAKA WA 5 | Bajeti za Miradi (Miaka 5) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | |
| | | 1.2.2 Usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji | 1.2.2.1 1 Kuimarisha Usimamizi na Uendeshaji wa skimu za umwagiliaji. | 1,822,835,000 | 1,651,922,500 | 2,249,454,750 | 1,786,470,225 | 2,592,437,428 | 10,103,119,903 |
| | | 1.2.3 Kuendeleza vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo na Uvuvi | 1.2.3.1 Kuendeleza miundombinu ya maji kwa ajiliya uzalishaji wa mifugo | 2,855,560,000 | 66,582,431,000 | 77,456,128,600 | 76,102,476,900 | 85,464,005,000 | 308,460,601,500 |
| | | | 1.2.3.2 Kukuza na Kujenga vituo vya kisasa vya Maji kwa ajili ya mazao, Mifugo na Uvuvi | 42,068,700,000 | 79,875,420,000 | 111,447,304,000 | 158,157,213,500 | 88,772,625,300 | 480,321,262,800 |
| | **Jumla – Eneo Dogo** | | | **68,990,218,333** | **382,827,618,042** | **420,653,535,967** | **471,239,231,974** | **431,878,337,028** | **1,775,588,941,344** |
| | 1.3 Kuimarisha udhibiti wa mabadiliko ya Hali ya Hewa na majanga ya asili | 1.3.1 Kukuza matumizi ya teknolojia ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi | 1.3.1.1 Kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi | 1,905,425,000 | 13,984,275,833 | 8,745,740,917 | 6,345,077,933 | 10,444,742,727 | 41,425,262,410 |
| | | | 1.3.1.2 Kukuza Mbinu za mifumo ya kiikolojia katika usimamizi wa uvuvi na ufugaji wa samaki | 1,089,637,500 | 1,044,926,000 | 1,729,778,250 | 794,675,575 | 1,329,264,100 | 5,988,281,425 |
| | 1.3 Udhibiti jumuishi wa mabadiliko ya Tabianchi /kukabiliana na Maafa ya Asili | 1.3.1 Kukuza matumizi ya teknologia ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi | 1.3.1.3 kuimarisha mfumo Mpana wa tahadhari za mapema na kukabiliana na dharura ya kilimo | 1,959,756,667 | 1,051,870,333 | 1,008,738,867 | 395,675,420 | 501,066,927 | 4,917,108,214 |
| | **Jumla Eneo Dogo** | | | **4,954,819,167** | **16,081,072,167** | **11,484,258,033** | **7,535,428,928** | **12,275,073,754** | **52,330,652,049** |
| **JUMLA ENEO KUU** | | | | **122,300,272,500** | **449,956,232,458** | **487,066,357,250** | **497,648,455,923** | **467,674,693,954** | **2,024,646,012,085** |
| **JUMLA KUU** | | | | **2,268,351,449,399** | **2,538,618,188,716** | **2,868,860,926,786** | **2,858,733,108,151** | **3,230,251,114,821** | **13,819,077,626,470** |

# KIAMBATISHO V: Ufuatiliaji, Tathmini na Takwimu

### Historia

446. Chini ya ASDP-1 (2006-2013), Wizara za sekta ya kilimo zilianzisha Timu mbalimbali za wataalamu ambapo mwaka 2007 iliundwa Timu ya Wataalam ya kufanya ufuatiliaji na tathmini. Timu hiyo ilihusisha wataalam kutoka katika Idara za Sera na Mipango za Wizara za sekta ya kilimo pamoja na msaada wa kitaalam kutoka Shirika la Maendeleo la Japan (JICA). Jukumu kuu la Timu hii ilikuwa ni kufuatilia, kutoa ushauri wa kitaalam, kutoa mwongozo wa jumla wa utekelezaji wa Programu kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa ASDP, kukusanya takwimu za sekta na kufanya maboresho ya mfumo wa ukusanyaji wa takwimu/taarifa na kukuza uwezo wa Wizara za kisekta wa kufuatilia na kutathmini katika ngazi za mikoa  na wilaya.

447. Timu ya Wataalam ya Ufuatiliaji na Tathmini iliandaa mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini mwaka 2008. Mfumo huo uliainisha maeneo ambayo ASDP ingeleta matokeo makubwa kwa ujumla kulingana na maeneo ya kimkakati (miundombinu, huduma za kilimo, mifumo ya masoko, muundo wa kitaasisi, pamoja na masuala mtambuka) pamoja na matokeo ya utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyopendekezwa. Orodha ya awali ilihusisha viashiria 100 ambavyo baadaye vilipunguzwa hadi kufikia viashiria vikuu 20-25 kama vinavyoonekana katika Kiambatisho Na. II. Hata hivyo, orodha hii ilikuwa inafanyiwa marekebisho ya mara kwa mara ili kuweza kuzingatia masuala ya msingi kama vile uwezeshaji, maboresho ya huduma na utafiti. Viashiria vikuu katika ASDP II vimeandaliwa kwa kuzingatia sehemu na maeneo muhimu ya uwekezaji. Orodha kamili ya viashiria ni kama vinavyooneka katika Mfumo wa Matokeo.

448. Ilikupata matokeo mazuri ya mipango na matumizi ya fedha, tathmini na ufuatiliaji, kutakuwa na timu mbili za wataalamu kutoka katika sekta mtambuka (Timu ya Wataalamu kwa ajili ya kufanya tathmini na utuatiliaji na Timu ya Mipango na Bajeti) kwa ajili ya kusaidia na kuwezesha kazi za kupanga, kuandaa bajeti na kufanya tathmini na ufuatiliaji.

449. Mojawapo ya majukumu ya Timu ya Kufanya Tahmini na Ufuatiliaji ni kuandaa taarifa ya utekelezaji wa ASDP kwa mwaka na kuainisha mchango wake katika sekta. Taarifa ya utekelezaji ya mwaka inatoa taarifa za wakati zilizo katika orodha ya viashiria katika ngazi tatu: kwa kuzingatia matokeo ya baadae, matokeo katika ngazi ya juu na matokeo katika ngazi ya chini, kulinganisha malengo na takwimu halisi kila inavyowezekana na kuainisha chanzo cha mapungufu. Ukusanyaji wa takwimu ulifanyika kwa kutumia njia za kawaida: (i) Kwa takwimu za ndani, dodoso lilitumika ili kupata takwimu za ndani ya nchi ambazo zilikuwa zinawasilishwa kwa njia ya kupiga simu au barua pepe. na (ii) Kwa takwimu za kitaifa, Timu ya tathmini na ufuatiliaji iliwasiliana na wahusika kwa njia ya simu au kutembelea ofisi husika moja kwa moja. Bila kuwasilishwa katika Kamati ya Mfuko wa Pamoja wa ASDP, taarifa zilikuwa zinatumiwa kwa uchache na mfumo wa tathmini na ufuatiliaji wa ASDP. Taarifa za katikati ya mwaka za ufutiliaji na tathmini za ASDP 1 zinaonesha kuwa japokuwa kulikuwa na maendeleo katika maeneo yaliyochaguliwa kumekuwa na mkanganganyiko katika matokeo yake. Mfano, katika ngazi ya matokeo ya baadaye, viashiria vinahusisha ukuaji wa kilimo, umaskini katika maeneo ya vijijini pamoja na thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi na maendeleo yake yamekuwa ya chini tofauti na jinsi ilivyotegemewa. Katika ngazi ya matokeo, viashiria muhimu kama vile matumizi ya teknolojia zilizoboreshwa (mbegu, mbolea, umwagiliaji na matumizi ya zana za kisasa) hayajaonesha matokeo yaliyotarajiwa. Hata hivyo, picha ya jumla inaonesha kuwa matokeo halisi ni mazuri katika nyanja ya utoaji wa huduma ikiwemo ujenzi wa miundombinu na kujenga uwezo.

450. Tathmini ya hitimisho la utekelezaji wa ASDP iliyofanyika Juni, 2011 ilionesha kuwa matokeo na athari chanya katika ASDP I hayakuweza kufikiwa kikamilifu katika maeneo yote kama ilivyotarajiwa wakati wa kuandaa. Taarifa inasisitiza umuhimu wa kufanya tafiti mara kwa mara kwa umakini na kwa haraka ili kupata matokeo makubwa.

451. Chini ya Programu ya ASDP II Timu ya Wataalam ya Ufuatiliaji na Tathmin itaendelea kutekeleza majukumu yake ya awali hata hivyo, katika kila ngazi ya utekelezaji (kuanzia ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa) baadhi ya vipengele vya tathmini na ufuatiliaji vitatekelezwa. Kila ngazi itatakiwa kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapitio ya pamoja ya utekelezaji wa mradi kwa kila

sekta yatafanyika kila mwaka kwa kushirikisha wadau wote. Ili kuleta ubora na ufanisi, kila ngazi katika muundo wa Serikali itatekeleza majukumu ya kufanya tathmini na ufuatiliaji. Kwa mfano, Afisa Mtendaji wa kata atasimamia na kutoa tathmin ya Afisa Mtendaji wa kijiji. Utaratibu madhubuti wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utawekwa kuanzia katika ngazi ya Taifa (imenukuliwa kutoka katika mapendekezo ya ASDP II - 2013/2014).

452. Timu ya Wataalam ya Mipango na Utekelezaji katika ASDP I imelenga kusaidia Wilaya katika kuandaa Mpango wa Wilaya wa kuendeleza sekta ya kilimo (DADP) pamoja na kutekeleza na kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za ASDP kupitia DADP. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) itahakikisha kuwa Wilaya zote zinafuata mwongozo na kutimiza matakwa ya misaada ya maendeleo inayotolewa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Ruzuku ya maendeleo -LGDG). Tathmini ya utekelezaji wa LGDG iliyofanywa chini ya usimamizi wa iliyokuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inahusisha matokeo maalum ya tathmini ya DADP na matokeo ya jumla na hatua za utekelezaji. Ripoti tofauti ya tathmini ya ubora wa DADP imeandaliwa kwa ajili ya kilimo na inaweza kutumika kutangaza viashiria. Tathmini hii ilifanywa na Timu ya wataalamu ya mipango na utekelezaji pamoja na waratibu wa ASDP wa mikoa.

453. Wakati wa utekelezaji wa Awamu ya Pili ya ASDP, kutakuwa na Timu ya Wataalam inayohusika na mipango na fedha. Timu hii itakuwa na jukumu la kuratibu mipango na fedha katika ngazi za Serikali kuu, Sekretariati ya mkoa pamoja na Mamlaka ya Serikali ya Mitaa. Vipengele vyote muhimu vya mapato na matumizi ya fedha vitaandaliwa katika ngazi ya Serikali kuu na kuwasilishwa kwa Timu ya Wataalam inayohusika na mipango na fedha kwa ajili ya kukaguliwa pamoja na kuunganishwa. Timu ya wataalam itahakikisha kunakuwa na usawa na vipengele vyote muhimu vya mipango na fedha vinaendana na malengo makuu ya ASDP. Mapendekezo ya Mipango na Fedha yatawasilishwa kwa TDC na kuridhiwa na ASC. Timu ya wataalam inayohusika na Mipango na Fedha itaweza kusimamia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango na fedha katika ngazi zote za utekelezaji wa madhumuni na malengo ya ASDP II.

454. Kutokana na utekelezaji wa ASDP-I kuendana na mahitaji, ilisaidia katika kukuza utendaji kutoka chini kwenda juu ambapo vikundi vya wakulima, vyama vya ushirika, na vyama vya watumiaji viliandaa miradi kwa kufuata miongozo na kanuni na kuomba fedha kutoka katika mifuko ya ruzuku iliyopo katika ngazi za wilaya. Maafisa wa Wilaya hufanya ufuatiliaji wa miradi (kukarabati majosho, mfumo mdogo wa umwagiliaji, nk) kila baada ya robo ya mwaka.Taarifa hii ilikusanywa na iliyokuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kusambazwa kwa Timu za Wataalam za Wizara za Sekta ya Kilimo, Wakurugenzi na kuwasilishwa katika Kamati ya Utendaji ya Mfuko wa Ufadhili wa ASDP kwa ajili ya mapitio na kuridhiwa na kupata kibali (kukataliwa au kufanyiwa marekebisho iwapo itahitajika).

455. Wilaya zote zinatakiwa kutoa taarifa ya robo mwaka ya utekelezaji halisi na matumizi ya fedha za ASDP II. Timu ya Wataalam wa Mipango na Fedha itaandaa majedwali mbalimbali ya mfano. Majedwali hayo yatatoa taarifa kwa kila mradi ikilenga kutoa taarifa za utekelezaji halisi, matokeo na taarifa ya fedha pamoja na kutoa taarifa ya jumla ya wanufaika. Majaribio yatafanyika ili kupata taarifa ya matokeo katika kila mradi kulingana na viashiria vikuu vya utekelezaji. Tathmini ya pamoja hufanywa kila mwaka ili kuangalia mafanikio yaliyofikiwa na inaleta pamoja wadau wa sekta ya kilimo,washirika wa maendeleo, watendaji wasio wa Serikali, Sekta binafsi ili kushiriki na kujadili utendaji na utekelezaji, vipaumbele na masuala yanayoendana. Timu ya pamoja ya tathmini huonesha maeneo muhimu ambapo maendeleo yamefanyika na kutoa mapendekezo kuhusu masuala mbalimbali yanayoathiri utekelezaji wa ASDP. Kielelezo Na. A24 kinatoa maelezo ya muhtasari wa mfumo wa tathmini na ufuatiliaji ulioanzishwa chini ya ASDP I pamoja na ule wa sekta ya kilimo Tanzania.

456. Chini ya Mpango huu, maendeleo ya kila sekta yatasimamiwa kupitia Mfumo wa Takwimu za Kilimo (angalia sehemu ya Ufuatiliaji na Tathmini) na/au kupitia ripoti maalum. Matokeo ya kila sekta yatasimamiwa mahsusi kupitia NSCA, AASS na/au Utafiti wa kitaifa wa kufuatilia kaya, mwongozo wa kilimo (angalia sehemu ya takwimu). NSCA ilianzishwa kwa lengo la kutoa taarifa ya viashiria muhimu vilivyoainishwa katika orodha ya viashiria vya utekelezaji vya ASDP II.

457. Ufanisi wa kila mradi utapimwa kupitia DADP kwa miradi iliyopo katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali

za Mitaa kwa kutoa taarifa halisi za utekelezaji na matumizi ya fedha kwa kila robo ya mwaka. Kwa zile zinazohusisha ngazi ya Taifa zitatolewa na NCU na zile za Tawala za Mikoa na Mratibu wa ASDP wa mkoa. Chini ya ASDP-I, mfumo ulikuwa unatoa taarifa za miradi iliyotekelezwa na kufadhiliwa. Mpango wa uratibu ulioboreshwa chini ya ASDP II unaitaka miradi yote inayotekelezwa katika Sekta iunganishwe katika taarifa jumuishi ya utekelezaji ingawa mipango ambayo si ya kifedha ina utaratibu wake wa utendaji na utoaji wa taarifa. Njia ya kupata taarifa za mipango isiyo ya kifedha ni: taarifa za robo mwaka kwa mradi unaotekelezwa na kila Taasisi zisizo za Kiserikali (NGOs) ambazo zintakiwa ziwasilishwe kuendana na matakwa yaliyoainishwa katika mikataba ya makubaliano ya kila NGO, taarifa hizo zinahusu chanzo na matumizi ya fedha. Taarifa hizo zinaweza kutolewa iwapo wahusika wataridhia kuzitoa ili kulinganisha na miradi inayotekelezwa kupitia mipango ya Serikali. NSCA inalenga kuangalia taarifa nyingi katika viashiria vya kimatokeo vilivyoainishwa katika utekelezaji wa shughuli za ASDP II. Utendaji wa kila mradi utatekelezwa kupitia DADP kwa Serikali za Mitaa kwa miradi inayofanana na taarifa ya utekelezaji wa miradi husika itatolewa kwa pamoja kila robo ya mwaka. Na zile zinazoshughulikiwa katika ngazi ya kitaifa zitatekelezwa na NCU na zile zilizpo katika RS zitatekelezwa na mratibu wa Mkoa wa ASDP II. ASDP-1 imetekeleza miradi kwa kutumia chanzo kimoja tu cha bajeti. Aidha, ASDP II imeboresha usimamizi wa ndani wa SWAP ambapo inahitaji miradi yote ifanyike katika sekta, imejumlishwa katika taarifa za utekelezaji za pamoja. Hata hivyo, kwa miradi isiyo na bajeti iwe na usimamizi wake peke yake na utaratibu wake wa kutoa taarifa na kufanya kazi nje ya bajeti ujumuishwe: taarifa ya kila robo mwaka kwa kila miradi ya mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) kulingana na mahitaji yaliyoorodheshwa kwenye mikataba kwa kila miradi ya mashirika ya misaada, lakini unaondoa taarifa za vyanzo na maombi ya fedha au kulingana na mradi iliypo ndani ya mipango ya Serikali

**Jedwali Na. 60: Mzunguko wa Ufuatiliaji katika Ngazi za Utekelezaji wa ASDP II**

| Ngazi ya ufuatiliaji | Ndani | Nje |
|---|---|---|
| Kijiji | Kwa mwezi | Robo mwaka |
| Kata | Kwa mwezi | Robo mwaka |
| Tarafa | Robo mwaka | Robo mwaka |
| Wilaya | Robo mwaka | Robo mwaka |
| Mkoa | Robo mwaka | Robo mwaka |
| Kitaifa ( NCU) | Robo mwaka | Robo mwaka |
| Mapitio ya pamoja ya sekta | Kwa mwaka | Kwa mwaka |

**Jedwali Na. 61: Mzunguko wa Ufuatiliaji katika Ngazi za Utekelezaji wa ASDP II**

| Ngazi ya tathmini | Ndani | Nje |
|---|---|---|
| Kijiji | Kwa mwaka | Miaka 1.5 |
| Kata | Kwa mwaka | Miaka 1.5 |
| Tarafa | Kwa mwaka | Miaka 1.5 |
| Wilaya | Miaka 1.5 | Miaka 2 |
| Mkoa | Miaka 1.5 | Miaka 2 |
| Tathmini ya pamoja ya kitaifa | Miaka 2.5 | Miaka 2.5 |

**Kielelezo Na. A24: mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa ASDP kwa utendaji wa sekta na mradi (Imetoholewa kwa ajili ya ASDP II)**




458. Moja ya mafunzo kutokana na ASDP-1 ilikuwa ni pamoja na kuchelewa kufanya tafiti muhimu, kama NSCA, ambayo ingesaidia kupata viashiria vingi vya matokeo, hali ambayo imesababisha upungufu katika taarifa zinazoweza kufuatiliwa vizuri na kutathmini matokeo ya awamu ya kwanza ya utekelezaji wa ASDP. Hivyo , ilikuwa 'rahisi' kudhani kuwa ASDP-1 haikufikia matokeo yake, kwamba hapakuwa na 'mshindo' na kuwa rasilimali zilikuwa zinasambazwa. Vilevile, tafiti iliyopangwa kufanywa wa utoaji wa huduma za kila mwaka ambayo matokeo kama vile kupitishwa ya kupokelewa kwa teknolojia bora haukutekelezwa, na hii imeonekana kuwa pengo kubwa. Hii inasisitiza haja ya kuhakikisha kwamba tafiti za kitaifa zinakuwa na rasilimali za kutosha ili kutoa uchambuzi muhimu na matokeo kwa wakati, ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa kila mwaka ambao hutoa tathmini muhimu ya utendaji wa kila mwaka. Pia inaelezea ukweli kwamba kuna ulazima wa kutenganisha matumizi ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kama chombo cha kufuatilia mchakato wa mageuzi, kama vile kupima faida za kawaida kwenye uzalishaji na teknolojia zilizopitishwa.

## Ufuatiliaji na Tathmini

459. Ufuatiliaji. Ili kufuatilia ASDP na utendaji wa sekta ya kilimo, mifumo miwili ya ukusanyaji wa takwimu iliandaliwa chini ya ASDP-1: (a) Mfumo wa Kukusanya Takwimu za Kilimo (ARDS) kwa ajili ya ufuatiliaji wa utendaji wa sekta hiyo, na (b) DADP kwa ajili taarifa za utekelezaji na matumizi ya fedha za Mfuko wa Pamoja za kila robo mwaka.

460. ARDS imeandaliwa kwa ajili ya kutoa takwimu za kilimo za wilaya na mkoa kwa ASLMs kwa kila robo mwaka. Viongozi wa vijijini na / au maafisa ugani wa kilimo wanatakiwa kuwasilisha taarifa ya kila mwezi, kila robo mwaka na kila mwaka kwa maafisa wa kilimo na mifugo wa wilaya ambao wanatathmini ripoti katika ngazi ya wilaya. Taarifa za Wilaya zinawasilishwa katika Sekretriat ya Mkoa ambako zinapitiwa upya na kuidhinishwa na maafisa wa kilimo wa mkoa, kabla ya kuwasilishwa kwenye Wizara za Sekta ya Kilimo. Uzingatiaji wa utaratibu wa utoaji wa taarifa utafuatiliwa na mtaalaam wa ufuatiliji wa CMT.

461 Kwa kupitia msaada wa JICA, Mfumo wa Kukusanya Takwimu za Kilimo (ARDS) umeunganishwa na mtandao kwa kutumia programu inayoitwa ufuatiliaji katika ngazi ya Serikali za Mitaa (LGMD 2) ambayo inaruhusu takwimu kuingizwa kielektroniki katika ngazi ya wilaya na kufuata mchakato wa uidhinishaji uliopo. Lengo ni kuwa na mfumo mmoja jumuishi wa utoaji wa taarifa zilizopo katika ngazi ya wilaya. Hata hivyo, takwimu katika ngazi ya kijiji na ya kata bado hukusanywa kwa kutumia karatasi.

**Kielelezo Na. A25: Mfumo wa Kukusanya Takwimu za Kilimo**




462. Ingawa ARDS inapaswa kutoa taarifa za sekta ya kilimo kutoka katika ngazi ya kijiji hadi wilaya na ASLM kupitia mikoa kila robo mwaka, mfumo huu haujafanya kazi vizuri. Hata hivyo, kuanzishwa kwa LGMD2 kunatarajia kuboresha hali hiyo, kama fomu za ripoti, na mtiririko umehuishwa kupitia mtandao.

463. Kupitia msaada wa JICA, miongozo kwa ajili ya VAEO na WAEO imeadaliwa kuhusu utaratibu wa kukusanya takwimu zinazohitajika. Hata hivyo, kutokana na mfumo wa ARDS kuwa changamani , ni kweli kwamba ripoti za kila mwezi, robo mwaka na kila mwaka viashiria vinatofautiana. Viashiria vya kila mwezi ni pamoja na hali ya hewa, bei ya mazao, magonjwa ya mazao na viuatilifu vilivyotumika, idadi ya mifugo iliyochinjwa, ukaguzi wa nyama na maziwa, afya ya mifugo (chanjo na tiba) na huduma

za mifugo (uhimilishaji). Kwa upande wa robo mwaka viashiria ni pamoja na idadi ya vikundi vya wakulima / wanachama, idadi ya wakulima waliopata mafunzo, eneo la umwagiliaji, eneo la kilimo lililolimwa mazao, uzalishaji na tija ya mazao. Viashiria vya mwaka ni pamoja na takwimu za idadi ya watu, matukio ya kilimo cha mkataba, eneo linalomwagiliwa, idadi ya vyama vya wamwagiliaji, orodha ya mashine na zana za kilimo, idadi ya Mashamba Darasa, matumizi ya mbolea, madawa, mbegu, idadi ya mifugo, miundombinu ya mifugo, taarifa kuhusu malisho na misitu. Majukumu ya ufuatiliaji katika ngazi za chini ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 62.**

**Jedwali Na. 62: Majukumu ya ufuatiliaji katika ngazi ya halmashauri**

| Taarifa ya kila mwezi ya VAEO / WAEO | VAEO / WAEO Taarifa ya Robo waka | Taarifa ya Mwaka ya VAEO / WAEO |
|---|---|---|
| 1. Utangulizi (hali ya hewa, muhtasari wa shughuli)<br>2. Mazao: Eneo lililopandwa, Uzalishaji, Tija na Bei<br>3. Huduma za Afya ya mimea<br>4. Mifugo iliyochinjwa<br>5. Ukaguzi wa Nyama<br>6. Bidhaa za Mifugo<br>7. Afya ya Mifugo<br>8. Mafanikio na Changamoto<br>9. Wageni | 1. Hali ya chakula ya Kijiji<br>2. Vikundi vya wakulima/ SACCOs<br>3. Huduma za ugani<br>4. Vipimo vya udhibiti wa kibaolojia<br>5. Umwagiliaji (eneo lililopandwa, uzalishaji, nk.)<br>6. Mmomonyoko wa udongo<br>7. Eneo lililolimwa na mbinu zilizotumika | 1. Utangulizi (Idadi ya watu na idadi ya kaya)<br>2. Umwagiliaji (chanzo cha maji, eneo, wanachama wa IO, nk)<br>3. Kilimo cha mkataba<br>4. Zana za kilimo, mifugo na uvuvi<br>5. Huduma za ugani (FFS)<br>6. Matumizi ya pembejeo<br>7. Idadi ya mifugo<br>8. Miundombinu ya mifugo<br>9. Eneo la kuchungia/ malisho ya mifugo<br>10. Malisho ya mifugo<br>11. Eneo linalofikiwa na runinga, redio na mawasiliano ya simu |

464. Kama inavyoonekana, baadhi ya viashiria hivi (mfano tija na kupokelewa kwa teknolojia) havipaswi kuchukuliwa na mfumo wa kawaida wa ukusanyaji wa takwimu, kutokana na kwamba mfumo ni wa wazi na unaweza kushawishi wadau mbalimbali kuingilia matokeo yanayopatikana kutokana na juhudi mbalimbali za ukusanyaji wa takwimu. ARDS hutegemea VAEO / WAEO kutoa taarifa, lakini nafasi nyingi zipo wazi, na mara nyingi VAEO / WAEO wanakumbana na changamoto za usafiri, na hivyo kutegemea mwenyekiti wa kijiji kutoa taarifa.

465. Kwa mtazamo wa mwingiliano kati ya uwezo wa ARDS na baadhi ya tafiti za kitaifa za kilimo, kuhusu utendaji wa sekta ya kilimo (kwa kuanzia na takwimu za uzalishaji na tija), mapendekezo yalitolewa kwamba ARDS inalenga katika kupunguza idadi ya viashiria ambavyo vinaweza kukusanywa vizuri kupitia mfumo wa utawala, juu ya misingi ya "wanahitaji kujua", na sio "ni vizuri kujua". Pamoja na kuwepo kwa makubaliano kuwa ARDS lazima izingatie upunguzaji wa idadi ya viashiria ambavyo vinaweza kuchukuliwa kwa urahisi katika ngazi za chini, suala hili halikushughulikiwa ipasavyo wakati wa mapitio ya ARDS yaliyofanyika mwishoni mwa mwaka 2012, kabla ya ARDS kuenezwa. Hata hivyo, orodha ya viashiria iliachwa bila kuguswa.

466. Utekelezaji wa ARDS ulikamilika mwezi Machi mwaka 2014 katika mikoa yote 25. Hata hivyo, utegemezi wa kutumia karatasi katika ngazi ya kijiji na kata ni wa gharama kubwa na usiokuwa na uhakika. Mbinu zaidi za kisasa, kama vile matumizi ya kompyuta zinapendekezwa chini ya ASDP II ili kusaidia mfumo utumike kama ulivyokusudiwa. ARDS sasa umekuwa mfumo rasmi wa ukusanyaji takwimu kwa ajili ya sekta ya kilimo kutokana na TAMISEMI kuziruhusu kwa maandishi kwa kutumia barua kwa mratibu/Mkuu wa Wilaya, pamoja na maelekezo kwamba taarifa za ARDS zilizokusanywa za kila robo mwaka ziwasilishwe kwa njia ya kielektroniki

467. Taarifa za DADP za kila robo mwaka kuhusu utekelezaji pamoja na matumizi ya fedha zimekuwa zikiandaliwa kwa kusaidiwa na Kikundi cha Wataalamu wa mpango na utekelezaji cha ASDP. Miongozo ya DADP kwa ajili ya kuandaa na utekelezaji iliandaliwa mwezi Juni 2006, kwa kupitia msaada wa mradi wa kujenga uwezo unaofadhiliwa na JICA. Lengo la miongozo hiyo ni kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa kipengele cha Kusaidia Utekelezaji katika Serikali za Mitaa ili kutekeleza DADP.

Kikundi cha Wataalamu pia huandaa taarifa ya uchambuzi ya mwaka ya ambayo hufanyiwa uchambuzi iwapo DADP kwa miaka mitatu ijayo imezingatia mwongozo na taarifa ya utekelezaji wa DADP kwa kutumia fedha ambazo hazikutumika katika mwaka husika.

468. Taarifa iliandaliwa na TAMISEMI ambayo ilijumuisha miradi yote ambayo ilikuwa inatekelezwa katika kila wilaya pamoja na ile ambayo ilikuwa inafadhiliwa na ASDP. Miradi hii ni sehemu ya DADP, ambayo ni ya miaka mitatu. Watumishi wa Wilaya hufanya mawasiliano na walengwa wa mradi au afisa ugani ambaye anatoa taarifa kuhusu utekelezaji wa mradi (maeneo ya utekelezaji, viashiria vya matokeo, kulinganisha malengo na utekelezaji halisi). Taarifa za matumizi ya fedha hupatikana katika ngazi ya wilaya, kwa kuwa kila "Mradi"una akaunti benki.

469. Miradi hiyo ilikuwa ni pamoja na miradi midogo ya umwagiliaji, ukarabati wa majosho, FFSs, nk. Taarifa hiyo inafuatilia utekelezaji wa miradi 70 aina tofauti na hutoa idadi ya walengwa kwa kila mradi. Aidha, taarifa ilikuwa inafuatilia fedha ambazo zimebaki na zile ambazo hazikutumika kabisa kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa mradi maalum. Tarifa hizo huunganishwa pamoja na kuandaliwa muhtsari ambao unaruhusu kufuatilia aina ya hatua zilizochukuliwa, unaweza kuongeza idadi ya wanufaika pamoja na msaada wa kifedha kwa kila hatua.

470. Pamoja na kwamba jitihada zimefanywa, DADPs ina maono madogo ya kimkakati kwa ajili ya maendeleo ya kilimo katika ngazi ya wilaya na haitoi taswira ya kina ya shughuli za sekta ya kilimo zinazotekelezwa katika ngazi ya wilaya. Hiyo inatokana na kwamba Serikali za Mitaa zimeichukulia DADPs kama chombo cha kuombea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa DADP. Hata hivyo, kumekuwa na majaribio ya kuandaa mpango mpana zaidi, ikiwa ni pamoja na taarifa kutoka kwa serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali zinazohusu rasilimali nyingine.

471. Mfumo huu kwa kawaida unalenga katika kupata matokeo kupitia njia mbalimbali, hata hivyo, kwa sababu ya mtazamo itakuwa ni muhimu kunasa matokeo ya taarifa za kiujumla katika ngazi ya mradi na uwezo wa kuonyesha matokeo kwamba ASDP imeyafikia. Kutokana na hili, taarifa tofauti imeandaliwa ili kutoa taarifa juu ya shughuli za mradi / katika ngazi ya matokeo.

472. Taarifa ya matokeo inalenga katika kuongeza uzalishaji na tija ya mazao na mifugo na pia kuongeza thamani ya mazao na mifugo, na upatikanaji wa huduma za kifedha, yote haya katika ngazi ya mradi, mtu binafsi au kuingilia kati, hata hivyo, bado haijawahi kutekelezwa

473. Hi ni mojawapo ya mbinu ambayo italeta maana. Matatizo yanayofanana kuna uwezekano wa wadau kushawishi matokeo yaliyopatikana kutokana na juhudi za ukusanyaji wa takwimu. Taarifa za matokeo kwa kawaida hupatikana kwa kufanya tafiti au mapitio, na si kwa njia ya mifumo ya utoaji taarifa maalum. Kulikuwa na mkanganyiko wakati wa ufuatiliaji wa ASDP kati ya mradi mahsusi na sekta nzima kuhusu ukusanyaji wa takwimu za viashria vya matokeo. Kutokana na uhusiano wa bajeti, taarifa za matokeo ya mradi mahsusi zilipewa kipaumbele kuliko viashiria vya matokeo ya sekta nzima, na hivyo kusababisha uendelezaji hafifu wa ufuatiliaji wa ASDP na sekta nzima kwa ujumla. Hata hivyo, inatambulika kwamba mfumo wa Ufuatiliaji na tathmini wa ASDP II ni lazima uwe na uhusiano mkubwa na bajeti na mahitaji ya mgao wa fedha kwa ajili ya ufuatiliaji.

### Takwimu

474. Serikali ya Tanzania inatumia tafiti mbalimbali na sensa kupata taarifa kwa ajili ya kufanya maamuzi kuhusu sera ya usalama wa chakula na kwa ajili ya kupanga mipango. Taasisi muhimu ni Ofisi ya Taifa ya Takwimu(NBS, www.nbs.go.tz)

475. Mpango Mkakati wa Takwimu Tanzania (TSMP) uliandaliwa kati ya kipindi cha 2010-2014, ili kuhakikisha kunakuwa na uratibu bora, kuongeza uelewa wa takwimu na kuzalisha takwimu nzuri. Mpango huo hutoa mfumo wa kitaifa kwa ajili ya kuendeleza mfumo wa takwimu nchini. Uratibu ni pamoja na makundi kazi ya sekta .Hii inajumuisha takwimu za sehemu ya kilimo, ambayo inashughulikia tu Sensa ya Taifa ya Kilimo. Bajeti ya Mpango Mkakati wa Takwimu - Tanzania (TSMP) ni Dola za Kimarekani milioni 64 ambazo zitatumika katika kipindi cha zaidi ya miaka 5 na inachangiwa na wafadhili mbalimbali kupitia Mfuko wa Pamoja (Benki ya Dunia, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Kanada (CIDA).

476. Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo zinatekeleza mradi unaosimamiwa na FAO kuhusu takwimu. Katika muktadha huu, Kikundi kazi cha wataalamu ambacho kinajumuisha wataalamu wa kitaifa kutoka taasisi mbalimbali kimeundwa ili kupitia na kuoanisha takwimu zilizopo. Vyanzo vikuu vya takwimu za kilimo na muda wa mara kwa mara wa kufuatilia ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 63:

**Jedwali Na. 63: Tafiti na sensa muhimu kwa ajili ya takwimu za kilimo[155]**

| Jina | Sifa/tabia | Mara ya mwisho kufanyika | Mzunguko unayotarajiwa |
|---|---|---|---|
| Sensa ya Taifa ya Kilimo | Inachukua vigezo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na idadi ya kaya zinazohusika katika Kilimo, vyanzo vya mapato, eneo ambalo lilipandwa mazao, uzalishaji na tija ya mazao na ufugaji, masoko na uhifadhi, umwagiliaji na matumizi ya pembejeo, upatikanaji wa huduma za ugani na mikopo, hesabu ya mali , matumizi ya chakula. Sampuli ya ukubwa wa kaya 50,000, hutoa takwimu katika ngazi ya wilaya. | 2002/2003<br>2007/2008 | Miaka 5 |
| Utafiti wa Kufuatilia Kaya | Ni tafiti ambayo inahusisha viwango vya maisha na inafadhiliwa na Benki ya Dunia katika nchi nyingi duniani. Tafiti hiyo inatathmini viwango vya maisha pamoja na athari za sera zinazohusu kaya. Ina moduli kwenye kilimo na inalenga katika umaskini. Ukubwa wa mfano wa kaya 3,200, inaruhusu tu makadirio ya taifa ya Tanzania ya vijijini. Inaweka daraja kati ya Utafiti wa Bajeti ya Kaya | 2008/2009<br>2010/2011 | Kila miaka 2 |
| Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi | Takwimu kutoka Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi hutumika kufuatilia maendeleo kutokana na sera za serikali za kupunguza umaskini. Inatoa chanzo rasmi cha uamuzi wa umaskini nchini Tanzania | 2001/2002<br>2007/2008<br>2011/2012? | Miaka 5 |
| Sensa ya Taifa ya Idadi ya Watu na Makazi | Hutoa takwimu za idadi ya watu, na hujumuisha baadhi ya taarifa kuhusu kilimo. Matokeo yanapatikana tu. Idadi ya wakazi wa Tanzania ni milioni 45 | 2002/2003<br>2012/2013 | Miaka 10 |

Tafiti za hapo juu zinatoa matokeo yafuatayo ya kimkakati kwa ajili ya kuimarisha uandaaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakaotumika katika ASDP II:

477. Kutokana na uhaba wa fedha, tafiti za kitaifa zimekuwa zikitoa matokeo yanayokinzana na siyo ya mara kwa mara. NSCA 2007/2008 iliyofanyika kitaifa na kikanda matokeo yake yalipatikana mwezi Julai 2012 na toleo la 2012/2013 liliahirishwa hadi 2015/2016. Matokeo ya NPS 2, ambayo yalifanyika mwaka 2011 yalitolewa mwezi Septemba 2012.

478. Ujumbe wa takwimu za Kilimo kutoka USDA ulieleza kuwa: *"licha ya umuhimu wa kilimo katika uchumi, takwimu za kilimo hazijajumuishwa katika takwimu za msingi, au kufadhiliwa chini ya TSMP. Shughuli za ukusanyaji wa takwimu zinategemea sana ufadhili wa washirika wa maendeleo. Bila ya kutenga fedha za kutosha katika bajeti ya Serikali kwa ajili ya ukusanyaji wa takwimu muhimu za kilimo , uendelevu hautaweza kupatikana"*. Vikwazo vingine vinavyohusu mfumo wa takwimu wa Tanzania ni pamoja na kiwango cha usahihi wa takwimu hakijulikani, utofauti kati ya vyanzo mbalimbali vya takwimu, uhaba wa takwimu za mwendelezo, ukosefu wa uratibu wa kutosha na kuoanisha mbinu za ukusanyaji wa takwimu na, uhaba wa watumishi na ukosefu wa kiufundi pamoja na utegemezi wa fedha za wafadhili.

479. Kutokana na hali hiyo ya hapo juu, USDA imekuwa ikishirikiana na FAO, Benki ya Dunia na nchi nyingine, Ofisi ya Taifa ya Takwimu pamoja na Wizara ya kilimo kuendeleza Mkakati wa Kuboresha Kilimo na Takwimu Vijijini. Mkakati huo wa Kimataifa ambao unalenga katika kukabiliana na kupungua kwa ubora na wingi wa takwimu duniani kote ni mpango wa Tume ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa. Mkakati unatoa msingi wa kina ili kuhakikisha uendelevu wa takwimu za kilimo zilizopo na zile zinazojitokeza. AfDB inaziwezesha Sekretariat za Mikoa katika mpango huu.

480. Misheni mbili zilizofanywa kwa pamoja kati ya FAO, USDA na AfDB kupitia mpango huu zilifika nchini mwezi Januari 2012 na Machi 2013. Matokeo ya safari zake ilikuwa ni kuandaa mapendekezo ya kuboresha takwimu za kilimo nchini Tanzania, kama ambavyo imefafanuliwa katika Mkakati wa Kimataifa. Vipengele vya mapendekezo ni pamoja na: (i) kuwa na takwimu ambazo zinaboreshwa mara kwa mara katika ASSP; (ii) kuimarisha ARDS; (Iii) kuandaa sampuli na kubuni sampuli sahihi kwa ajili ya kuzalisha takwimu za kilimo; (iv) kubuni na kutekeleza sampuli ya utafiti wa kilimo ya kila mwaka; na (v) kujenga uwezo kwa ajili ya takwimu za kilimo.

481. ASSP ambayo ilitayarishwa na NBS kwa kushirikiana na ASLM, pamoja na msaada wa kiufundi kutoka FAO, imefafanua mpango sahihi kwa kutimiza mahitaji ya takwimu za kilimo kwa kutumia rasilimali za serikali, ikizingatia mzunguko na muda wa utoaji, kuzingatia kiwango cha usahihi unaohitajika na watumiaji wa takwimu. Aidha, inabainisha mbinu sahihi ya ukusanyaji wa takwimu kwa kila kipengele cha mfumo, kisha kuweka kipaumbele cha shughuli na kutambua rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji. Mpango huo unatakiwa kuunganishwa na Mkakati wa Kimataifa na ni lazima kuingizwa katika TSMP na kutengewa fedha na Serikali kwa ajili ya utekelezaji.

482. AASS inalenga katika kutoa takwimu za mazao na mifugo kwa uhakika na kwa wakati na kwa kila mwaka. Mapendekezo kutoka ujumbe wa pamoja na kuzingatia makadirio ya kitaifa na kimkoa kwa mazao 8-10 na aina 3-5 ya mifugo. USDA itatoa msaada wa kiufundi kwa NBS na ASLM katika suala hili, na kukuza sampuli hii, kwa kutumia picha za satelaiti ili kutambua maeneo, kiwango cha wingi wa mimea katika eneo, ndiyo ukubwa wa maeneo, na kisha kufuatilia kwa ajili ya mahojiano ya nyumbani. Dhamira ni kutumia vifaa vya GPS na vya kieletroniki ya kubeba mkononi katika ukusanyaji wa takwimu ili kuongeza kasi ya ukusanyaji wa takwimu za eneo na kuhakikisha usahihi wa takwimu. Majaribio ya utafiti yalianza kutekelezwa mwaka 2013, na ya pili mwaka 2014. Taarifa ya mwisho ilitegemea kutolewa 2015 au 2016 ( kutegemeana na kufanyika kwa Sensa ya Taifa ya Kilimo)

483. Wasiwasi ni kuwepo kwa dodoso fupi; Hata hivyo, ni muhimu kupata viashiria vilivyopitishwa vya matumizi ya uboreshaji wa teknolojia na upatikanaji wa huduma za kimkakati (kwa mfano, fedha vijijini nk), ambayo ilikusanywa chini ya Mfumo wa ufuatiliaji na tathimni ASDP-1. Hivi pia vitakuwa viashiria muhimu vya matokeo katika Mfumo wa Matokeo wa ASDP II. Kadhalika, wasiwasi mwingine ni kama eneo la sampuli hii ni mbinu bora kwa ajili ya Afrika kutokana na mazingira ya kilimo na sifa ya mashamba yake kuwa madogo madogo, mchanganyiko wa kilimo na kilimo cha kuhamahama na maeneo makubwa ya mifugo. Hii pia inaondokana na kuwa na orodha ya sampuli hii, pamoja na maeneo ya kuhesabia, ambayo NBS inayaelewa vizuri. Aidha, gharama ya mbinu hii inaonekana kuwa ya juu, kutokana na sampuli ambayo inatarajiwa kuzungumziwa. Mambo haya yanahitaji majadiliano na NBS, ASLM, FAO na USDA

484. Kuandaa ASSP, Kikundi Kazi cha Takwimu za Kilimo kinachoundwa na timu ya wataalam wa takwimu za kilimo kimeanzishwa chini ya uratibu wa Kikundi Kazi cha Kilimo cha TSMP. Mratibu kutoka NBS ameteuliwa na wajumbe wengine ni pamoja na watakwimu kutoka ASLM ambao watatolewa kwa mkataba rasmi kwa ajili ya kufanya kazi na shughuli za kipaumbele. FAO imeajiri mshauri wa kitaifa kufanya kazi kama afisa mkazi wa kufuatilia masuala yote ya mpango huu na kusaidia Kikundi Kazi , pamoja na mshauri wa kimataifa ili kutoa msaada hasa katika maandalizi ya ASSP. Kikundi Kazi cha Kilimo cha TSMP kitasimamia kazi ya Kamati.

485. Kabla ya uwekezaji haujafanywa wa kuboresha takwimu za kilimo, wafadhili walitaka kufahamu kama Serikali inaona takwimu za kilimo ni kipaumbele kwa kujumuisha hayo kati ya viashiria vya msingi vya kiuchumi na kuweka masharti muhimu katika bajeti ya Serikali. Sehemu hii ilikuwa wazi wakati wa ujio wa pili, ambapo maafisa mbalimbali kutoka NBS, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu walithibitisha kuwa Serikali ya Tanzania imedhamiria kikamilifu kuboresha takwimu za kilimo na iko tayari kutoa msaada unaohitajika. Pande zote mbili zilisisitiza kuwa NBS inapaswa kuongoza mchakato, kwa mujibu wa mamlaka yake katika Sheria ya Takwimu, na kwa wafanyakazi wa kitaifa kuwa mstari wa mbele. Msaada wa ziada lazima ulenge kuendeleza katika mifumo iliyopo na taratibu.

## Msaada wa Usimamizi na Tathmini ya ASDP II chini ya ASDP II

486. Lengo la sehemu hii ndogo ni kuhakikisha kwamba takwimu zina ubora unaostahili, zinatolewa kwa wakati na kwamba kutoa takwimu zinazohitajika katika kufuatilia utekelezaji wa ASDP II, kuanzia na viashiria vilivyopo katika mfumo wa matokeo. Kiambatisho Na.II kinaonesha mfumo na aina ya viashiria kama vile mapato ya wakulima, mazao, thamani ya mazao / mauzo ya nje, eneo chini ya teknolojia bora, eneo la umwagiliaji, nk. Katika sehemu hii ndogo, kimaudhui msaada umegawanywa katika maeneo mawili: (i) Ufuatiliaji na Tathmini wa kujitolea wa ASDP II na Sekta ya kilimo na ; na (ii) Msaada kwa takwimu za kilimo na sekta nyingine zinazohusiana na shuguli za ufuatiliaji na tathmini. Mtaalamu wa ufuatiliaji na tathmini wa NCU atasimamia ufuatiliaji na tathmni kwa kushirikiana na NBS kuandaa moduli ya ufuatiliaji katika tafiti.

487. Msingi na utafiti wa mwisho. Kutokana na uhakika kuhusu idadi ya marudio, upeo na ufadhili wa tafiti za kilimo, kama vile NSCA, kutekelezwa kupitia NBS, utafiti wa awali na maalum utatekelezwa kuendana na msimu wa 2014/2015 kwa kutoa takwimu za msingi kuhusu vigezo vilivyotambuliwa katika mfumo wa matokeo. Hiyo itazingatia wilaya za kipaumbele zilizochaguliwa katika ASDP II.

488. Jumla ya sampuli zenye ukubwa wa takriban kaya 5,000 zinatarajiwa kutoka katika wilaya 30. Hii inapaswa kuwa kubwa ya kutosha ili kuruhusu taarifa zilizogawanywa kwa wilaya. Sampuli hii na dodoso itaandaliwa kwa kushirikiana na NBS na kuzingatia Mpango Mkakati wa Takwimu za Kilimo, ambao utafanyiwa mapitio ili kutumika kwa ajili ya mwaka 2007/2008 NSCA na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012/2013 na 2012/13 ili kuboresha ufafanuzi na uteuzi wa maeneo ya kukusanyia takwimu pamoja na wadadisi. Matumizi ya sampuli hii ya kawaida yataruhusu kulinganisha kati ya matokeo ya awali ya ASDP II na matokeo ya NSCA.

489. Sampuli hii pia inahusisha kwa pamoja kaya zisizonufaika na zile zinazonufaika na msaada kutoka ASDP II, ama katika wilaya hiyo hiyo, au katika wilaya ya jirani. Sampuli hii kubwa itaruhusu kukamilisha tathmini kwa kulinganisha na mabadiliko kati ya kaya zinazonufaika kutokana ASDP II, na zile ambazo hazinufaiki moja kwa moja na mabadiliko haya. Utafiti wa mwisho kwa ASDP II utaoanishwa na NSCA na AASS uliofanywa katika mwaka wa mwisho wa mradi huo, na kutumia sampuli hii, na, kwa kiasi iwezekanavyo, kutembelea kaya hizo, kwa njia ya utafiti.

490. Inatarajiwa kuwa utekelezaji wa utafiti huo utafanywa na ama Chuo Kikuu kinachoheshimika au kampuni binafsi kwa kupitia zabuni ya ushindani. Hata hivyo, uzoefu wa ASLMs na makampuni ambayo yameingia nayo mikataba yamekuwa hayafanyi kazi ya kuridhisha, hivyo inapendekezwa kuwa kazi hiyo ifanywe na NBS, lakini kwa usimamizi kutoka taasisi huru ya kitaaluma. Wadadisi wa muda mfupi wataajiriwa kwa tafiti hizi mbili kusimamiwa na ofisi za mikoa za NBS. Matumizi ya vifaa vya kielektroniki vya kubeba mkononi vitatumika ili kuongeza kasi ya kuingiza na kusafisha takwimu, na kusambaza matokeo kwa kasi. Dodoso litaandaliwa kwa ushirikiano wa karibu na kikundi kazi cha takwimu za kilimo pamoja na ufuatiliaji na tathmini cha ASDP.

481. Tafiti za matokeo ya kati. Tafiti hizo zitafanyika ili kuruhusu ufuatialiji wa viashiria muhimu vya utekelezaji ambavyo vimetambuliwa katika mfumo wa matokeo, viashiria vya kati vya matokeo vitafanyiwa tathmini ya kila mwaka ili kutoa mrejesho kuhusu utekelezaji wa ASDP II. Takwimu hizo zitatokana na AASS ambayo itaongezwa kwa lengo la kukusanya takwimu za mazao na tija ya mifugo. Gharama za kazi hii zinakadiriwa kuwa jumla ya Shilingi bilioni 2.4. Kutakuwa na mapitio ya mfumo wa matokeo (kama sehemu ya ASDP II) ili kurekebisha utekelezaji halisi wa ufuatiliaji na tathmini wa ASDP II.

## Msaada kwa takwimu za kilimo na juhudi za ufuatiliaji na tathmini ya sekta

492. Kulingana na Mkakati wa kitaifa wa Kuboresha Takwimu za Kilimo na za Vijijini, ambao unatekelezwa na USDA, FAO na AfDB, na kwa kuzingatia ASSP ambayo inaendelezwa, kikundi kazi cha takwimu za kilimo, sehemu hii ndogo kitakuwa na shughuli zifuatazo:

(i) Ugharamiaji wa pamoja kwa ajili ya Sensa ya Taifa ya Kilimo (NSCA-2015/2025);

(ii) Uwezeshaji wa kifedha kwa ajili AASS katika kipindi cha 2015–2024;

(iii) Kuimarisha ARDS; na

(iv) Kusaidia kikundi kazi cha ufuatiliaji na tathmini.

492. Sensa ya Taifa ya Kilimo *(NSCA)*. Kutokana na kwamba ASDP II itakuwa moja ya miradi michache mikubwa ya kutoa fedha katika kilimo kupitia sekta ya umma kwa miaka ijayo, na kwa kuwa fedha kwa ajili ya takwimu za kilimo ni mjadala unaoendelea chini ya uangalizi wa Mkakati wa Kimataifa wa Kuboresha Takwimu za Kilimo za Vijijini, washirika kadhaa, ikiwa ni pamoja na serikali, wameonyesha nia yao ya kutoa fedha kwa ajili ya NSCA. NSCA inachukuliwa kama utafiti muhimu kwa ajili ya sekta na utekelezaji wake wa kawaida usingeweza katika kutoa mfumo wa pamoja wa kitaifa kwa miradi yote inayofanya kazi katika sekta hiyo nchini Tanzania.

493. NSCA inatarajiwa kuwa itafanyika kila baada ya miaka 10, na itatoa takwimu katika ngazi ya wilaya na aina mbalimbali ya viashiria, kulingana na ukubwa wa sampuli ya kaya 50,000. NSCA nyingine ili ilifanyika mwaka 2016 (kwa ajili ya msimu wa kilimo 2015/2016). Kutokana na gharama yake kuwa kubwa, karibu shilingi bilioni 10, ilipendekezwa kuwa ASDP II ichangie kwa karibu asilimia 50 ya gharama hii, wakati asilimia iliyobaki ilifadhiliwa na Mpango Mkakati wa Takwimu za Tanzania *(TSMP)*.

494. Sensa ya Kilimo ya Kila Mwaka (AASS). ASSP ambayo inaandaliwa na kikundi kazi cha takwimu za kilimo inakadiriwa kuwa katika ngazi ya mkoa kila mwaka takwimu za uzalishaji wa mazao makuu na aina ya mifugo. Gharama za kila mwaka na dodoso la mwisho la AASS zilikamilika na kujumuishwa mwisho wa mpango wa majaribio (2014).

495. Kuna majadiliano yanayoendelea kuhusu mbinu zitakazotumika kama kutakuwa na eneo la sampuli au orodha ya sampuli ya eneo, au mchanganyiko wa zote mbili. Majadiliano haya yanafanyika katika mfumo wa kikundi kazi cha takwimu za kilimo, kati ya NBS, ASLM, na msaada maalumu wa kiufundi katika takwimu kutoka USDA na FAO. Kundi hili ni pamoja na watakwimu kutoka MAFC na MLFD, chini ya uenyekiti wa NBS, na pia litakuwa na jukumu la kufanya maandalizi. Kulingana na gharama za majaribio, ambayo yamefanyika nchini mwaka 2013 na 2014, AASS ilikadiriwa kugharimu kiasi cha TSh. bilioni 1.6 TSh. kila mwaka

496. Kutokana na kwamba *TSMP* hakuna uwezekano wa kutoa fedha kwa ajili ya utafiti huu kila mwaka, na kwa kuwa utafiti huu wa kila mwaka utaifanya sekta kuwa na makadirio ya kuaminika ya uzalishaji na tija, angalau katika ngazi ya mkoa (majadiliano yanaendelea kuangalia fursa za kuimarisha takwimu kutegemea ngazi ya wilaya), *ASDP II* inapaswa kutoa fedha kwa ajili ya utafiti huu wa kila mwaka. Hata hivyo, kuna wasiwasi kuhusu mbinu ya sasa ya takwimu kuwa ililetwa na USDA na hivyo kuna haja ya kujadiliwa na Kikundi kazi cha wataalamu cha ufuatiliaji na tathmini wa ASDP na ASCG.

497. Mfumo wa Kukusanya Takwimu za Kilimo. Mojawapo ya mifumo muhimu ya usimamizi wa taarifa ambayo imeendelezwa kupitia *ASDP-1* ni *ARDS*. Rasilimali nyingi zimewekezwa katika kujenga Tovuti kwa taarifa ambazo zimegawanyika katika ngazi ya wilaya, kuandaa mfumo wa ukusanyaji takwimu, taratibu za kukusanya takwimu katika ngazi ya kijiji na kata na uwasilishaji wa takwimu kutoka ngazi ya wilaya hadi ya ngazi ya Kitaifa. JICA imetoa msaada kwa muda mrefu na kujenga uwezo wa kiufundi wa *ARDS* kitaifa ambao utafikia mwisho wake ifikapo 2015[75]. Mfumo huu hutoa takwimu juu ya utendaji wa sekta ya kilimo, na hutegemea wagani kutoa taarifa za kila mwezi, robo mwaka na mwaka, ambazo zimeandaliwa katika ngazi ya wilaya na kuingizwa katika mtandao, na kupatikana kwenye *ASLM* kupitia Sekretarieti na *TAMISEMI*.

498. Mapitio ya hivi karibuni yamebainisha kuwepo kwa viashiria ambavyo vinaweza kukusanywa kikamilifu katika baadhi ya vijiji na kata[76]. Hata hivyo, maoni haya hayajaweka bayana kama hakutakuwa na mwingiliano kati ARDS na vyanzo vingine vya takwimu, kama vile AASS na NSCA, kama ilivyopendekezwa na ujumbe wa pamoja wa *USDA* / *FAO* / *AfDB* uliokuja nchini mwaka 2012.

499. Mpango Mkakati wa Takwimu za Kilimo (ASSP) unatarajiwa kwamba ARDS italenga taarifa za uhakika

*75 Mfumo wa kukusanya Takwimu za kilimo (ARDS), mpango wa Usambazaji, ACDP M&E TWG,2010*

*76 Tathmini ya mfumo wa kukusanya Takwimu za kilimo.*

zinazotolewa na maafisa ugani lakini kwa kutambua umuhimu wa kuwa na mifumo ya usimamizi wa taarifa kwajili ya sekta. ASDP II itakuwa na fedha kwa ajili ya kufanya mapitio ya ARDS katika mwaka wa kwanza (1), ili kuisaidia Kikundi kazi cha wataalamu cha ufuatiliaji na tathmini katika kuhakikisha kwamba ni vizuri kujumuisha mifumo mingine ya ukusanyaji wa takwimu na kwamba taarifa inatolewa kwa mapana zaidi na sahihi. Mbali na utafiti huu, ASDP II itatoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ARDS, wakati serikali za mitaa zinatakiwa kuweka katika bajeti zao za matumizi ya kawaida.

500. Gharama kwa ajili ya utaratibu wa utekelezaji wa ARDS imekuwa inakadiriwa kuwa takriban TSh. milioni 6 / wilaya / mwaka kwa kuzingatia dhana ya kwamba kila Serikali ya Mitaa ina wastani wa kata 15. Hivi karibuni, hata hivyo, Halmashauri nyingi ziliongeza idadi ya kata na hivyo kuwa na kata zaidi ya 20 kwa kila wilaya. Kupitia dhana ya kata 20 kwa Halmashauri, inatarajiwa kuwa gharama za Halmashauri kwa mwaka zitakuwa ni Shilingi milioni 8. Hivyo jumla ya gharama kwa mwaka ni Shilingi bilioni 1.20 au Shilingi bilioni 6.00 katika kipindi cha miaka 5 (mtiririko USD 0.74 milioni / mwaka na USD3.7 milioni kwa ajili ya kipindi chote). Bajeti hii ni pamoja na posho ya kusafiri kwa afisa wa ufuatiliaji na tathmini wa wilaya (siku 4 kwa mwezi), pamoja na mafuta na matengenezo ya baiskeli kwa WAEO na VAEO katika mtiririko huo, vifaa kwa ajili ya watumishi hao wawili, gharama ya usambazaji wa taarifa (nauli), na gharama za uchapishaji na kurudufu dodoso pamoja na karatasi zinazotumika.

501. Kikundi Kazi cha Ufuatiliaji na Tathmini. Kikundi kazi cha ufuatiliaji na tathmini huandaa Taarifa ya Utekelezaji wa ASDP kwa Mwaka, ambayo inatoa taarifa kuhusu kila kiashiria muhimu cha utekelezaji[77], na kushiriki katika mapitio ya pamoja ya sekta ambayo hufanya tathmini ya kila mwaka ya mafanikio yaliyopatikana chini ya ASDP, na pia matokeo katika ripoti[78]. ASDP II itawezesha kikundi kazi cha ufuatiliaji na tathmini kwa kutenga kwenye bajeti kiasi cha Shilingi milioni 100 kwa mwaka.

## Mfumo Unaopendekezwa wa uratibu wa ufuatiliaji na Tathminini chini ya ASDP II

502. Kutokana na mazingira ya ASDP II ambapo wahusika mbalimbali watatekeleza shughuli zao husika na miradi, ufuatiliaji na tathmini ya ASDP II inahitaji uwezo imara wa uratibu na uandaaji wa takwimu (ukusanyaji, uandaji, uchambuzi na utoaji wa taarifa)

503. Pamoja na kwamba utaratibu wa taasisi ya ASDP-1, yaani, Kikundi kazi cha utawala cha utafiti na tathmini na Kikundi kazi cha wataalamu cha mipango na bajeti, vinaweza kubaki katika ASDP II, vipengele viwili vya ziada ni lazima viongezwe ili kuimarisha uwezo wa utendaji kazi : (i) Mamlaka za juu zisimamie vikundi kazi vyote vya kitaalamu pamoja; na (ii) Kundi dogo (maafisa wawili au tatu) kutoka kwenye vitengo vya ufuatiliaji na tathmini, takwimu na kitengo cha teknolojia ya habari katika kila ASLM ambao watakuwa na wajibu wa kila siku wa kushughulia masuala ya takwimu. Hiyo ya kwanza itahakikisha ufanisi katika uratibu wa ukusanyaji takwimu, wakati hiyo ya pili itawezesha ASLMs kutoa taarifa sahihi kutokana na aina mbalimbali za takwimu.

504. Uratibu katika ngazi ya Taifa ya uendeshaji, wigo wa uratibu utapunuka katika ASDP II kwa kuijumuisha NBS sambamba na wawakilishi kutoka katika miradi/programu. Ili kuongeza ufanisi wa ufuatiliaji na tathmini chini ya ASDP II, vikao vya uratibu vya mara kwa mara (angalau kila robo mwaka au kila mwezi) vinahitajika, ambavyo vitakuwa vinawezeshwa na mtaalamu wa ufuatiliaji na tathmini wa CMT ambaye atakuwa anaitisha mikutano. Mikutano hiyo ni muhimu ikahudhuriwa na wajumbe wa kutoka vitengo vya takwimu na tekinolojia ya habari katika ASLMs, na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kama vile vyama vya wakulima, na MUVITA miongoni mwa wengine ambao watadai kupewa taarifa za utekelezaji. Taarifa kuhusu ukusanyaji wa takwimu na hali ya jumla ya sekta ziwasilishwe kwenye mkutano wa uratibu wa kufuatilia shughuli za ufuatiliaji na tathmini chini ya ASDP II. Taarifa hizo pamoja na takwimu za ufuatiliaji na tathmini zisambazwe katika maeneo mengi ikiwa ni pamoja na njia ya tovuti au njia nyingine yoyote ya uwajibikaji.

77 *Taarifa za mwaka za Utekelezaji wa ASDP 2009/2010, Machi 2011; Novemba 2011;Rasimu kwa ajili mwaka 2011/2012 inaendelea kuandaliwa, Aprili 2013.*

78 *Taarifa ya Mapitio ya Saba ya Pamoja 5 Mei, 2012 hadi 18 Juni 2012.*

505. Ili kuziba pengo la taarifa juu ya uwekezaji katika kilimo na kuboresha uratibu, mwaka 2013 taasisi ya *Bill na Melinda Gate Foundation (BMGF)* iliingia mkataba na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Shule ya Biashara (UDBS) kukusanya kwa kina taarifa za uwekezaji katika sekta ya kilimo kupitia mradi wa TAN-AIM Awamu ya 1 na II (2013-2017). Mradi huo ulilenga katika kuboresha mtiririko wa taarifa zote za uwekezaji katika kilimo na kuziba pengo la uelewa wa uwekezaji katika sekta na uhusiano kati ya wadau husika. Mradi unatarajiwa: (i) kuziba pengo la upatikanaji wa taarifa na kuboresha upashanaji wa taarifa, (ii) kujenga uhusiano na ushirikiano ili kuepuka mwingiliano miongoni mwa wadau; (iii) kuboresha uratibu na ushirikiano kati ya washirika na wadau katika sekta, (iv) kuongeza ufanisi katika utumiaji wa rasilimali (vi) kujenga uwezo wa watumishi kwa ajili ya uendelevu wa mradi. Mradi umetoa taarifa ambazo zinaonesha nani yuko wapi na anafanya nini na nani katika mnyororo mzima wa thamani wa kilimo. Mradi unatarajia kukusanya takwimu za uwekezaji kutoka Serikali ya Tanzania, washirika wa maendeleo, Sekta Binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali / AZISE. Mradi pia umeweza kuendeleza TAN-AIM kwenye mtandao (TMT) na ikiwa na taarifa za uwekezaji kutoka Kundi la Washirika wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo (AWG) na Maendeleo ya Sekta Binafsi (PSD), Serikali ya Tanzania (GoT) na vikundi kazi vya Biashara kupitia utekelezaji wa ASDP I. Sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali / NSA hawakutoa taarifa. Aidha, taarifa za uwekezaji katika kilimo hazikuweza kukusanywa katika ngazi za halmashauri (LGAs) kutokana na ukosefu wa usimamazi wa kumbukumbu na ukosefu wa mfumo wa pamoja wa kupata taarifa hizi kutoka katika ngazi ya kijiji hadi wilaya, ambayo huathiri ubora na usahihi wa takwimu. Ili kuboresha uratibu, ufuatiliaji, na kuendeleza ushirikiano miongoni mwa wadau, TANAIM inapaswa kuboreshwa mara kwa mara ili kuwa na taarifa sahihi. Kielelezo Na. 25 chini kinaonesha msaada wa Washirika wa Maendeleo katika minyororo mbalimbali ya thamani ya bidhaa.

**Kielelezo A26: Michango ya Washirika wa Maendeleo kwa kuzingatia eneo na Mnyororo wa Thamani katika Sekta Ndogo ya Mazao .**



**Kielelzo A27: Michango ya Washirika wa Maendeleo kwa kuzingatia eneo na Mnyororo wa Thamani katika Sekta Ndogo za Mifugo na Uvuvi**



**Jedwali Na. 64: Matokeo na Viashiria vya ASDP-1**

| | Viashiria | Idadi ya marudio | Jukumu | | | Mtoa Taarifa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wilaya | Mkoa | Taifa | |
| Mshindo (IM) | 1. Ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) kwa Mwaka [MKUKUTA] | Mwaka | | | √ | NBS |
| | 2 Uwiano wa watu vijijini na mahitaji yao ya msingi – [MKUKUTA] | Katika kipindi maalum | | √ | √ | NBS (HBS) |
| | 3. Thamani ya mazao yanayouzwa nje | Mwaka | | | √ | TRA |
| Matokeo ya viashiria (OC) | 1. Uwiano wa utoshelevu wa chakula [MKUKUTA] | Mwaka | | √ | √ | MAFC |
| | 2. Uzalishaji na Tija ya Mazao na Mifugo | Katika kipindi maalum | √ | √ | √ | NBS (NSCA) |
| | 3. Uwiano wa wakulima wanaotumia teknolojia za kisasa | Katika kipindi maalum | √ | √ | √ | NBS (NSCA) |
| | 4. Mtiririko wa fedha toka sekta binafsi kwa ajili ya Kilimo na Ufugaji | Mwaka | | √ | √ | TIC |
| | 5. Uwiano wa wakulima wanaotumia zana za kisasa | Katika kipindi maalum | √ | √ | √ | NBS (NSCA) |
| | 6. Uwiano wa bidhaa zilizosindikwa za kilimo na zile zilizo safirishwa nje ya nchi | Mwaka | | | √ | TRA |
| | 7. Uwiano wa wakulima walioingia mkataba na ambao wanajitegemea [MKUKUTA] | Mwaka | √ | √ | √ | LGAs |
| | 8. Uwiano wa Halmashauri zilizopata ruzuku ya nyongeza | Mwaka | | | √ | PMO-RALG |
| | 9. Uwiano wa Halmashauri zilizopata nyongeza ya ruzuku/ ya ziada | Mwaka | | | √ | PMO-RALG |
| Matokeo (OP) | 1. Idadi ya miundombinu ya uzalishaji | Mwaka | √ | √ | √ | LGAs |
| | 2. Idadi ya miundombinu ya masoko na mashine | Mwaka | √ | √ | √ | LGAs |
| | 3. Idadi ya maafisa ugani waliopata mafunzo ya teknolojia ya kisasa | Mwaka | √ | √ | √ | LGAs |
| | 4. Thamani ya mikopo iliyotolewa na SACCOs kwa ajili ya kilimo | Mwaka | √ | √ | √ | LGAs |
| | 5. Idadi ya sheria na kanuni zilizopo za masoko | Mwaka | | | √ | MITM, MAFC, MLDF |
| | 6. Idadi ya masoko ambayo bei za jumla na rejareja zinakusanywa | Mwaka | | | √ | MITM |
| | 7.Idadi ya vikao vya Kisekta vilivyokaa ngazi ya Kitaifa | Mwaka | | | √ | ASDP Secretariat |
| | 8.Uwiano wa taarifa za robo mwaka zilizowasilishwa kwa wakati | Mwaka | √ | √ | √ | Regions, ASLMs |
| | 9. Uwiano wa idadi ya wanawake katika kamati za Fedha na Mipango | Mwaka | √ | √ | √ | LGAs |

Angalizo: Viashiria vyenye [MKUKUTA] ni kutoka *Poverty Monitoring Master Plan.*

# KIMBATISHO Na. VI: Uchambuzi wa kiuchumi na kifedha

## 1. Utangulizi

506. Uchambuzi wa kiuchumi na kifedha ulifanyika ili kutathmini uwezekano wa uwekezaji uliopendekezwa kwa ajili ya ASDP II. Maeneo makuu ya mradi ni pamoja na: (i) Ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya umwagiliaji; (ii) Upanuzi wa usimamizi wa maji na kilimo hifadhi, (iii) Kuendeleza miradi ya maji kwa ajili ya mifugo na uvuvi, (iii) Upanuzi na uboreshaji wa huduma za utafiti wa kilimo, ugani na mafunzo, (iv) Kuboresha upatikanaji wa pembejeo za kilimo na mashine (ikiwa ni pamoja na ruzuku ya pembejeo); (v) Kuendeleza vyama vya wakulima na kuboresha upatikanaji wa masoko na fedha vijijini (vi) Kuendeleza kilimo-biashara na kuimarisha mnyororo wa thamani, na (vii) Kuimarisha sera /mfumo wa usimamizi na uwezo wa taasisi; (viii) Kuboresha usalama wa chakula na lishe (ikiwa ni pamoja na ruzuku ya NFRA ); na (ix) Uratibu wa sekta na ufuatiliaji na tathmini.

507. Faida kuu za kiuchumi zinazotarajiwa kupatikana ni: (i) Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kutokana na ongezeko katika tija kwa eneo, (ii) Kuimarisha uzalishaji wa mifugo na samaki (iii) Kuongezeka kwa mapato kutokana na uzalishaji wa kilimo, (iv) Ongezeko la mapato kutokana na kilimo-biashara na kuongeza thamani, na (v) Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na kuuzaji nje ya nchi.

### Uzalishaji wa mazao

508. Uwekezaji katika ardhi na usimamizi wa maji, pamoja na kilimo hifadhi, utasaidia katika kuhakikisha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ni endelevu katika maeneo ambayo yanakabiriwa na mmomonyoko wa udongo na kupungua kwa rutuba ya udongo. Zaidi ya hayo, inakadiriwa kuwa miundombinu ya umwagiliaji yenye hekta 461,326 itaendelezwa, na hekta 100,000 za miradi iliyopo ya umwagiliaji kwamba itakarabatiwa kupitia ASDP II.

509. Kufuatia utoaji wa huduma za kilimo, kuboresha matumizi ya ardhi na usimamizi wa maji, pamoja na upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji, wingi wa mazao kwa eneo utaongezeka kutoka 92% hadi takribani 103% katika hekta 2,165,000 zinazolimwa. Kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji, wingi wa mazao unatarajiwa kuongezeka kwa 135%, na kwa kilimo kisichokuwa cha umwagiliaji wingi wa mazao utaongezeka kutoka 90% hadi 100%.

510. Kwa upande wa uboreshaji wa tija katika uzalishaji, inatarajiwa kuwa wastani wa tija kwa zao la mpunga utaongezeka kutoka tani 1.75 / ha hadi tani 3.0 / ha. Aidha, kwa zao la mahindi, mbegu za mafuta / jamii ya mikunde na mboga, ongezeko litakuwa ni tani 1.35-2.20 / ha (mahindi), tani 1.0-1.4 / ha (mbegu za mafuta / kunde), na kutoka tani 15.0-20.0 / ha (mboga).

511. Kwa ujumla ongezeko hili la uzalishaji wa mazao katika maeneo ya ASDP II litaendelea kuongezeka kwa mapato halisi kwa wakulima wadogo. Aidha, kutakuwa na ongezeko la mapato na ajira kutokana na upanuzi wa usindikaji, usafirishaji na uuzaji wa mazao na bidhaa zitokanazo na mazao, mifugo na uvuvi.

512. Kuendeleza miradi ya maji kwa ajili ya mifugo na utoaji wa huduma za msaada inatarajia kusababisha kuongezeka kwa tija. Hivi sasa, mifugo ni chanzo cha aina mbalimbali za bidhaa ikiwa ni pamoja na maziwa, nyama, mbolea na pia mapato ya fedha, lakini tija ni ya chini sana. Katika siku za baadaye kutokana na kuwepo kwa mradi, tija ya mifugo itaongezeka kutokana na usimamizi wa malisho bora na kanuni bora za mifugo na ufugaji hasa katika maeneo ya lishe na afya ya mifugo. Hali hiyo itaboresha tija katika uzalishaji wa maziwa na kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa nyama kutokana na kuongezeka kwa uzito. Mapendekezo ya maeneo kwa upande wa uvuvi yana lengo la kuongeza uzalishaji wa samaki kwa njia ya upanuzi wa mabwawa ya samaki pamoja na upatikanaji wa huduma bora. Hii itaboresha hali ya maisha ya jamii za vijijini wanaoshiriki katika uzalishaji na uuzaji wa samaki.

### Msaaada kwa vyama vya wakulima, masoko na kilimo-biashara

513. ASDP II imekusudia kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupanua upatikanaji wa masoko ya vijijini, kuboresha mifumo ya masoko na kutoa msaada kwa ajili ya Kilimo-biashara. Hatua hizi zina uwezekano wa kutoa faida kubwa kiuchumi, kama vile kuimarisha minyororo ya thamani, kuongeza thamani na kuboresha mapato na fursa za ajira kwenye kilimo kwa wanaojihusisha na usafirishaji, uhifadhi, usindikaji na uuzaji wa mazao ya kilimo. Hata hivyo, faida ya kiuchumi kwa maeneo hayo hazikufanyiwa uchambuzi wa kiuchumi.

514. Aidha, kutokana na tofauti kubwa za bei za kilimo za kila mwaka na za msimu uwezekano wa kuongezeka kwa bei ya shambani (kutokana na upatikanaji bora wa masoko na kuboresha ufanisi wa mifumo ya masoko) haikuzingatiwa katika uchambuzi wa kifedha.

## 2. Uchambuzi wa kifedha

### Bajeti za mazao

515. Uchambuzi wa kifedha ulifanyika kutathmini athari za utekelezaji wa ASDP II kuhusu mapato anayopata mkulima akiwa shambani. Bajeti nne zimeandaliwa ambazo zinawakilisha mazao makuu yanayolimwa nchini Tanzania, ambayo ni mahindi, mpunga, mbegu za mafuta / jamii ya mikunde na mboga. Bajeti hizo zimeandaliwa kwa kuzingatia hali ya sasa, ya baadaye ya kutokuwepo na kuwepo kwa mradi. .

516. Kwa upande wa hali ya baadaye ya kuwepo kwa mradi, mshauri mwelekezi alikadiria matarajio ya tija na matumizi ya pembejeo, pamoja na mahitaji ya zana na nguvukazi kwa ajili ya shughuli za shambani. Ongezeko katika uzalishaji wa mazao litatokana na uendelezaji wa miunndombinu ya umwagiliaji pamoja na matumizi ya kanuni bora za uzalishaji wa mazao katika maeneo ya kilimo cha umwagiliaji na yale ambayo hayamwagiliwi. Aidha, kuongezeka kwa upatikanaji wa pembejeo za mazao pamoja na matumizi ya zana kwa kiasi kikubwa kutaongeza uzalishaji wa mazao katika maeneo ya ASDP II.

517. Wastani wa tija ya mazao uliofanyiwa uchambuzi wa hali ya sasa ilivyo, itakavyokuwa baadaye kutokana na kuwepo au kutokuwepo kwa mradi inaonekana kwa muhtasari katika Jedwali Na. A2. Viwango vya ukuaji wa tija kwenye mazao katika hali ya baadaye ya kuwepo kwa mradi inatarajiwa kuwa itafikiwa ndani ya kipindi cha miaka miwili kutokana na kuimarishwa kwa huduma za kilimo, kuboresha matumizi ya ardhi na usimamizi wa maji, pamoja na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ambao utafanyika kupitia programu. Ili kuhakikisha kwamba maboresho haya ya muda mrefu yanakuwa endelevu, huduma za kilimo pia zimejumuishwa katika gharama za muda mrefu za matumizi ya kawaida.

**Jedwali Na. A2: Tija ya mazao katika hali ya sasa, baadaye kukiwa na mradi na bila ya mradi**

| | Wastani wa mavuno ya mazao (tani kwa hekta) | | |
|---|---|---|---|
| | Sasa | Baadaye bila mradi | Baadaye na mradi |
| Mahindi | 1.35 | 1.50 | 2.20 |
| Mpunga | 1.75 | 1.95 | 3.00 |
| Mbegu za mafuta/jamii ya mikunde | 1.00 | 1.10 | 1.40 |
| Mboga | 15.00 | 16.50 | 20.00 |

Chanzo: Taarifa ya Sekta ya Mazao (2012) na Makisio.

518. Katika hali ya baadaye ya kutokuwepo kwa mradi, tija inatarajia kuongezeka kutokana na kuzingatia kanuni bora za kilimo. Hivyo, inatazamiwa kutakuwa na ongezeko la tija la asilimia moja kwa mwaka. Wastani wa tija katika uzalishaji wa mazao katika hali ya kutokuwepo kwa mradi (inaonekana katika Jedwali Na.A2) unaakisi kiwango cha tija cha miaka 10 baadaye.

519. Uchambuzi wa kifedha kwa hali ya sasa, na baadaye bila na kuwepo kwa mradi ulifanyika kwa kuzingatia tija katika uzalishaji, pembejeo za mazao, bei ya kuuzia, viwango vya mishahara, pamoja na nguvukazi, matumizi ya wanyamakazi na zana. Aidha, uchambuzi wa faida halisi ya kifedha ulifanywa kwa kila zao lililochaguliwa kwa kuondoa gharama za uzalishaji na mapato ya mazao. Katika hali zote mbili za baadaye za kuwa na mradi na bila mradi, inaaminika kuwa bei ya mazao shambani (kwa misingi ya mara kwa mara) haitabadilika thamani yake ya sasa. Faida ghafi kwa muhtsari imeoneshwa katika Jedwali Na. A3.

**Jedwali Na. A3: Faida ya Ghafi ya mazao katika hali ya sasa, baadaye kukiwa na mradi na bila mradi**

| | Faida ya Ghafi (TSh kwa hekta) | | |
|---|---|---|---|
| | Sasa | Baadaye bila mradi | Baadaye kukiwa na mradi |
| Mahindi | 67,088 | 119,831 | 216,550 |
| Mchele | 322,500 | 423,844 | 709,375 |
| Mbegu za mafuta/jamii ya mikunde | 512,625 | 613,250 | 807,500 |
| Mboga za majani | 2,267,000 | 2,583,875 | 2,927,250 |

Chanzo: Makisio ya Bajeti za mazao

520. Kutokana na Jedwali Na. A3 ni dhahiri kuwa katika siku za baadaye za kuwepo kwa mradi, faida ghafi inaonekana kupatikana katika mazao yote. Hii inaonesha kuwa tija kubwa katika uzalishaji inasaidia kuongeza mapato pamoja na kuwepo kwa gharama za ziada za uzalishaji. Kadhalika, ni dhahiri kwamba faida halisi kwa hekta katika kilimo cha mboga ni kubwa zaidi kuliko mahindi, mpungana mbegu za mafuta/jamii ya mikunde. Hata hivyo, faida kutokana na mazao ya bustani inatokana na mabadiliko ya bei kwa msimu.

## Mpangilio wa mazao

521. Mpangilio wa mazao wa sasa ulifanywa kwa: (i) Kuangalia maeneo ya umwagiliaji yaliyopo, (ii) Maeneo yanayopendekezwa ya umwagiliaji na (iii) Maeneo yasiyomwagiliwa kupitia programu. Mpangilio wa mazao hayo hautabadilika kwa kiasi kikubwa katika hali ya baadaye ya kutokuwepo kwa mradi kwani idadi ya wingi wa mazao hautawezekana bila ya kuwepo kwa miundombinu bora ya umwagiliaji.

522. Katika eneo la umwagiliaji lililopo, inatarajia kuwa maeneo ya mpunga, mbegu za mafuta/ jamii ya mikunde na mbogamboga yataongezeka katika misimu yote ya mvua na kiangazi kutokana na kuwepo kwa shughuli za ASDP II. Aidha, katika maeneo yanayopendekezwa ya umwagiliaji, kutakuwa na mabadiliko makubwa katika muundo (kutokana mvua ya kutosha kwa ajili ya umwagiliaji) na upanuzi mkubwa katika maeneo ya zao la mpunga katika msimu wa mvua na kuanzishwa kwa kilimo cha mahindi, mpunga, mbegu za mafuta / jamii ya mikunde na mbogamboga katika msimu wa kiangazi. Mpangilio wa mazao uliotumika katika uchambuzi wa kifedha na kiuchumi ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. A4**

523. Katika eneo la umwagiliaji lililopo, kiwango cha wingi wa mimea kinatarajiwa kuongezeka kutoka 125% hadi 135%, wakati, katika maeneo yanayopendekezwa ya umwagiliaji, wingi wa mazao utaongezeka kutoka 90% hadi 135%. Kwa maeneo yasiyo ya umwagiliaji, wingi wa mazao katika hali ya kuwepo kwa mradi inakadiriwa kuwa 100%. Kwa ujumla, kiwango cha wingi wa mazao katika maeneo ya ASDP II kinatarajia kuongezeka kutoka 92% hadi 103%. Ukosefu wa upatikanaji wa maji ya uhakika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kutachangia katika kupunguza ongezeko la wingi wa mazao wakati wa kiangazi.

**Jedwali Na. A4: Mpangilio wa mazao na wingi wa mimea**

| Aina ya shughuli | Sasa na baadaye bila mradi: Mpangilio wa mazao (% ya eneo lililolimwa) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | maeneo ya umwagiliaji yaliyo karabatiwa | maeneo mapya ya umwagiliaji | maeneo yasiyo ya umwagiliaji | Kwa ujumla |
| **Msimu wa masika** | | | | |
| Mahindi | 45 | 63 | 63 | 62 |
| Mchele | 40 | 5 | 5 | 7 |
| Mbegu za mafuta/jamii ya mikunde | 5 | 20 | 20 | 19 |
| Mbogamboga | 5 | 2 | 2 | 2 |
| **Jumla ndogo** | 95 | 90 | 90 | 90 |
| **Msimu wa Kiangazi** | | | | |
| Mahindi | 15 | 0 | 0 | 1 |
| Mchele | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mbegu za mafuta/jamii ya mikunde | 10 | 0 | 0 | 0 |
| Mboga mboga | 5 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla ndogo** | 30 | 0 | 0 | 1 |
| Kiwango cha wingi wa mimea | 125 | 90 | 90 | 92 |

| Aina ya shughuli | Hali ya Baadaye kukiwa na mradi: Mpangilio wa mazao (% ya eneo lililolimwa) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | maeneo ya umwagiliaji yaliyo karabatiwa | maeneo mapya ya umwagiliaji | maeneo yasiyo ya umwagiliaji | Kwa ujumla |
| **Msimu wa masika** | | | | |
| Mahindi | 30 | 30 | 67 | 64 |
| Mchele | 50 | 50 | 5 | 8 |
| Mbegu za mafuta/jamii ya mikunde | 10 | 10 | 25 | 24 |
| Mboga mboga | 10 | 10 | 3 | 4 |
| **Jumla ndogo** | 100 | 100 | 100 | 100 |
| **Msimu wa Kiangazi** | | | | |
| Mahindi | 10 | 10 | 0 | 1 |
| Mchele | 5 | 5 | 0 | 0 |
| Mbegu za mafuta/jamii ya mikunde | 10 | 10 | 0 | 1 |
| Mboga mboga | 10 | 10 | 0 | 1 |
| **Jumla ndogo** | 35 | 35 | 0 | 3 |
| Kiwango cha wingi wa mimea | 135 | 135 | 100 | 103 |

Chanzo: Taarifa ya Taifa ya Mazao (2012) na Makisio ya Mwelekezi

### Mifugo

524. Kwa upande wa sehemu ya mifugo ASDP II inatarajia kuboresha tija ya uzalishaji katika aina mbalimbali za shughuli za ufugaji kama vile ng'ombe wa maziwa na kunenepesha ng'ombe wa nyama. Ongezeko katika tija ya uzalishaji wa mifugo litatokana na uzingatiaji wa kanuni bora za ufugaji na upatikanaji wa malisho bora.

525. Katika uchambuzi wa kifedha, bajeti imeandaliwa kwa ajili ya shughuli mbili za ufugaji, yaani uzalishaji wa maziwa na unenepeshaji wa ng'ombe wa nyama. Gharama na mapato yatokanayo na mifugo yalithaminishwa kwa kuzingatia bei ya shambani ya mwaka 2015 ili kukokotoa faida ghafi kwa kila aina moja ya shughuli (**Jedwali Na. A5**). Katika hali ya baadaye ya kuwepo kwa mradi, maboresho katika mapato ya faida halisi yanaakisi tija ya juu katika uzalishaji.

**Jedwali Na. A5: Faida ya Jumla katika hali ya sasa, baadaye kukiwa na mradi na bila ya mradi**

| Aina ya shughli | Faida ya Jumla (TSh kwa kichwa) | |
|---|---|---|
| | Sasa na baadaye bila mradi | Baadaye na mradi |
| Uzalishaji wa maziwa | 176,975 | 311,975 |
| Unenepeshaji wa ng'ombe wa nyama | 77,900 | 102,900 |

Chanzo; makadirio ya bajeti ya mifugo

### Uchambuzi wa bajeti ya shamba

526. Uchambuzi wa bajeti ya shamba ulifanyika kuamua matokeo ya utekelezaji wa mradi kwenye kipato cha shamba. Bajeti za shamba ziliandaliwa kwa ajili ya mashamba ya ukubwa wa wastani wa hekta 2.0. Kwa kuzingatia mpangilio wa mazao ambao umeoneshwa katika **Jedwali Na. A4**, maeneo ya mazao yalikokotolewa na kisha kutumika katika maeneo husika ya faida ghafi ili kupata faida halisi ya hali ya sasa, ya baadaye ya kuwepo na kutokuwepo kwa mradi. Faida halisi kutokana na shughuli za mifugo zilijumlishwa ili kupata faida ghafi kwa ujumla. Kutokana na kutolewa kwa gharama zisizobadilika, (kwa mfano kodi ya ardhi, zana, vifaa / mashamba), mapato halisi yalipatikana. Muhtasari wa mapato halisi katika maeneo mbalimbali ya ASDP II yameoneshwa katika **Jedwali Na. A6**

527. Kutoka katika **Jedwali Na. A6** ni dhahiri kwamba kuna uwezekano wa kuwa na ongezeko kubwa sana la kipato anachopata mkulima akiwa shambani. Kulinganisha hali ya sasa na ya baadaye kukiwa na mradi, mapato katika maeneo ya umwagiliaji yaliyopo yanatarajiwa kuongezeka kutoka Shilingi 900,568 hadi Shilingi 2,665,228 (kabla ya kuweka gharama za uendeshaji na matengenezo kwa ajili ya umwagiliaji ), wakati huo huo katika maeneo yasiyo ya umwagiliaji, mapato yanakadiriwa kuongezeka kutoka TSh 367,385 hadi Tsh 1,158,275. Kwa ujumla mapato halisi yanatarajiwa kuongezeka kutoka Shilingi 436,699 hadi Shilingi 1,655,569 kwa mwaka.

528. Gharama za uendeshaji na matengenezo za kilimo cha umwagiliaji zikijumuishwa, mapato halisi katika kilimo cha cha umwagiliaji yanapungua na kuwa Shilingi 2,229,994 kwa mwaka katika maeneo ya umwagiliaji. Hata hivyo, kama gharama za umwagiliaji zinachangia 16% ya mapato halisi, hivyo wakulima watakuwa na uwezo wa kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo kwa mwaka.

**Jedwali Na. A6: Mapato halisi katika hali ya sasa, baadaye bila ya na kuwepo kwa mradi**

| Hali ya umwagiliaji | Mapato halisi (TSh kwa mwaka) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Baadaye na mtaji | |
| | Sasa | Baadaye bila mradi | Bila ya gharama za uendeshaji na matengenezo | Jumuisha gharama za uendeshaji na matengenezo |
| Maeneo ya umwagiliaji yaliyo karabatiwa | 900,568 | 1,138,498 | 2,665,228 | 2,229,994 |
| Maeneo mapya ya umwagiliaji | 367,385 | 496,902 | 2,665,228 | 2,229,994 |

| Hali ya umwagiliaji | Mapato halisi (TSh kwa mwaka) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Sasa | Baadaye bila mradi | Baadaye na mtaji | |
| | | | Bila ya gharama za uendeshaji na matengenezo | Jumuisha gharama za uendeshaji na matengenezo |
| Maeneo yasiyo ya umwagiliaji | 367,385 | 496,902 | 1,158,275 | |
| Kiujumla | 436,699 | 580,309 | 1,655,569 | |

Chanzo: makadirio ya bajeti ya shamba

## 3. Uchambuzi wa kiuchumi

### Bei za kiuchumi

529. Bei za kiuchumi kwa ajili ya bidhaa zinazofanyiwa biashara kimataifa (kama vile mchele, mahindi, maharagwe ya soya na mbolea) zilipatikana kutokea kwenye makadirio ya Benki ya Dunia ya bei ya bidhaa kwa mwaka 2015. Bei hizo za kimataifa zilirekebishwa kidogo kwa kuzingatia gharama za mizigo ya bahari, bima za mpakani, pamoja na usafirishaji, utunzaji wa ndani na, ikiwa inafaa, gharama za usindikaji, ili kupata bei za uchumi za mashambani.

530. Gharama za usafiri, utunzaji, uhifadhi na usindikaji za ndani zilizingatia viwango vya sasa vilivyopo nchini Tanzania. Hata hivyo, bei za kifedha zilibadilishwa kwenda bei za kiuchumi kwa kutumia kiwango cha kubadilishia (SCF) cha 0.95. SCF huonesha kiwango kivuli cha fedha katika Tanzania ambayo ni tofauti na kiwango rasmi cha fedha kutokana na kuvurugika kwa soko la fedha za kigeni. Bei ya uchumi kwa ajili ya bidhaa nyingine za kilimo zisizofanyiwa biashara za kimataifa, kama vile mboga na majani makavu, zilichukuliwa kutoka bei za kifedha za mwaka 2015 zilizopo ndani ya eneo la mradi.

531. Gharama za kazi zilizingatia viwango vya mishahara ya vijijini ambayo ilitofautiana kulingana na aina ya shughuli za mashambani lakini ilikuwa ni wastani wa Shilingi 5,000 kwa siku. Hata hivyo, kutokana na kiwango cha juu cha kutokutumika kikamilifu katika ajira ndani ya eneo la mradi, kiwango kivuli cha mshahara cha 0.65 kilitumika kuthaminisha thamani ya ajira kiuchumi.

532. Uchambuzi wa kiuchumi ulifanyika kwa kutumia takwimu za kipindi cha miaka 50 kwa kuzingatia bei za mwaka 2015 kiwango kivuli cha 12%. Shilingi ya Tanzania ilitumika katika kubadilisha kwenda Dola ambapo kiwango cha ubadilishaji kilikuwa Shilingi 2,150 kwa Dola 1.0 (Juni 2015) . Mradi huo ulitarajia kutekelezwa katika muda wa miaka 10

### Manufaa ya kiuchumi

533. Katika kufanya makadirio ya faida ya kilimo, pato la jumla la kiuchumi kwa hekta lilikokotolewa kwa kuthaminisha kwa kutumia bei za kiuchumi. Mapato ya jumla kwa kuzingatia hali ya sasa na ya baadaye ya kuwepo na kutokuwepo kwa mradi kwa muhtasari ni kama yanavyoonekana katika **Jedwali Na. A7.** Mapato ya jumla kiuchumi yalizidishwa na maeneo ya mazao husika ili kupata makisio ya faida halisi kwa hali ya sasa, ya baadaye ya kuwepo na kutokuwepo kwa mradi. Tofauti ya faida halisi ilikokotolewa ili kupata matokeo ya kiuchumi kutokana na mabadiliko ya mpangilio wa mazao na kuongezeka kwa tija.

**Jedwali Na. A7: Mapato ya jumla kwa upande wa mifugo katika hali ya sasa, baadaye kukiwa na mradi na bila mradi**

| Aina ya shughuli | Mapato ya jumla ya kiuchumi (TSh kwa hekta) | | |
|---|---|---|---|
| | Sasa | Baadaye bila mradi | Baadaye na mradi |
| Mahindi | -80,084 | -37,321 | 42,813 |
| Mchele | 98,649 | 185,461 | 359,371 |

| Aina ya shughuli | Mapato ya jumla ya kiuchumi (TSh kwa hekta) | | |
|---|---|---|---|
| | Sasa | Baadaye bila mradi | Baadaye na mradi |
| Mbegu za mafuta/jamii ya mikunde | 416,142 | 511,441 | 697,594 |
| Mboga mboga | 1,589,450 | 1,860,013 | 2,115,150 |

Chanzo: Makadirio ya bajeti ya mazao

534. Aidha, faida ya jumla ya mifugo inakadiriwa katika hali ya sasa, ya baadaye ya kuwepo na kutokuwepo kwa mradi (kulingana na idadi ya mifugo husika na faida ya jumla ya kiuchumi kwa mazao). Faida hizo kisha ziliongezwa kwenye faida halisi ya mazao. Muhtasari wa faida ya jumla kwa mifugo ni kama yalivyooneshwa katika **Jedwali Na. A8**

**Jedwali Na. A8: Faida ya jumla kwa mifugo sasa, baadaye kukiwa na mradi na bila mradi**

| Aina ya shughuli | Mapato ya jumla ya kiuchumi (TSh kwa kichwa) | |
|---|---|---|
| | Sasa na baadaye bila mradi | Baadaye na mradi |
| Uzalishaji wa maziwa | 104,225 | 237,975 |
| Unenepeshaji wa ng'ombe wa nyama | 56,500 | 86,500 |

Chanzo: Makadirio ya bajeti ya mazao

535. Kutokana na ongezeko hilo katika uzalishaji wa mazao na mifugo, faida halisi ya kilimo kwa wakulima katika eneo la mradi ilikuwa inakadiriwa kuongezeka kwa Shilingi milioni 626,572 kwa mwaka (kutoka Shilingi milioni 245,152 na Shilingi milioni 859,700 kwa mwaka baada ya kuendelezwa kikamilifu). Aidha, ilitarajiwa kuwa manufaa ya kilimo yatokanayo na kuwepo kwa mradi yatafikiwa ndani ya kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji wa Programu. Faida kutokana na uzalishaji wa mazao inakadiriwa kuchangia 81% ya faida ya jumla ya Kilimo.

## Gharama za uwekezaji na kawaida

536. Makadirio ya bajeti ya maendeleo kwa ajili ya uwekezaji unaohitajika ili kutekeleza maeneo makuu ya ASDP II, yaani, Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Maji, Kuongeza Tija na Faida, Biashara na Kuongeza Thamani, na Mazingira wezeshi, Uratibu na Ufuatiliaji na Tathmini yaliandaliwa kutokana na makadirio yaliyotolewa na timu ya ushauri. Gharama hizo zimewekwa katika maeneo hayo makuu kwa kuzingatia kipindi cha utekelezaji cha miaka 10.

537. Kimsingi gharama za uwekezaji zimekadiriwa kuwa Shilingi milioni 6,230,100 (Dola milioni 2,898) na kama zitaongezwa gharama za dharura, gharama za programu zitaongezeka na kufikia Shilingi milioni 7,882,948 (Dola milioni 3666). Ghrama za dharura zilikadilikuwa kuwa ni 10% ya gharama zote za uwekezaji.

538. Ili kupata gharama za kiuchumi, kodi na ushuru wa serikali pamoja na ruzuku (kwa mfano, ruzuku ya pembejeo za kilimo na NFRA) ziliondolewa kwanza kutoka kwenye gharama za kifedha kutokana na kuwa ni malipo yanayohamishwa na hivyo si gharama ya rasilimali halisi . Kiwango cha kubadilishia cha 0.95 kilitumika kwa gharama za kifedha za nyenzo za ndani, mashine / vifaa na wafanyakazi wenye ujuzi. Gharama za wafanyakazi wasio na ujuzi zilipunguzwa kwa kutumia kiwango kivuli cha 0.65. Hata hivyo, gharama za kifedha za bidhaa na huduma za kigeni hazikubadilika. Aidha, vigezo vya kiuchumi vya ubadilishaji ili kutambua gharama ya uwekezaji kiuchumi ambayo ilikuwa inakadiriwa kuwa Shilingi milioni 2,778,544 (Dola milioni 1,292). Fedha na gharama za mtaji kiuchumi za maeneo makuu ya ASDP II kwa muhtasari ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. A9**.

**Jedwali Na. A9: Fedha na gharama za uwekezaji kiuchumi**

| Maeneo makuu ya Programu | Gharama za kifedha (TSh million) | Gharama za kiuchumi (TSh million) |
|---|---|---|
| Eneo kuu la 1: Usimamizi Endelevu wa maji na Matumizi ya Ardhi | 1,450,593 | 1,233,004 |
| Eneo kuu la 2: Kuongeza Tija na Faida | 1,517,960 | 607,184 |
| Eneo kuu la 3: Biashara na Uongezaji Thamani Kwenye Mazao | 1,483,429 | 1,260,915 |
| Eneo kuu la 4: Kuimarisha viwezeshi vya sekta | 1,778,118 | 711,247 |
| Gharama za msingi | 6,230,100 | 3,812,350 |
| Dharura | 1,652,848 | 1,011,418 |
| **Jumla ya gharama za mtaji** | **7,882,948** | **4,823,768** |

539. Gharama za uendeshaji na matengenezo za muda mrefu za miundombinu ya umwagiliaji pia zilijumuishwa katika uchambuzi wa kiuchumi, na hizi gharama za matumizi ya kawaida zinatakiwa zitengweikiwa faida ya baadaye ya uwekezaji inatakiwa kuwa endelevu. Gharama za uendeshaji na matengenezo ya miundombinu kwa mwaka zilikadiriwa kuwa Shilingi milioni 38915 (Dola milioni 21.8). Gharama hizi za kifedha zilithaminishwa na kuwa za kiuchumi ambapo gharama za uendeshaji na matengenezo kwa mwaka zinakadiriwa kuwa Shilingi milioni 34,614 (Dola milioni 16.1).

540. Kadhalika, ilichukuliwa kwamba huduma za kilimo zitakuwa zikihitajika kila mwaka kwa kipindi cha miaka 50. Hivyo, gharama zakila mwaka zahuduma za kilimozilijumuishwa katika uchambuzi ili kuhakikisha kuwa uzalishaji wa kilimo unaendelea kukua baada ya kumalizika kwa utekelezaji wa ASDP II. Kwa ujumla, gharama za matumizi ya kawaida za kiuchumi baada ya kumalizika kwa programuzimefikia kiasi cha Shilingi 67,740 milioni kwa mwaka (Dola milioni 31.5 kwa mwaka).

### Uwezekano kiuchumi na Uchambuzi wa kina

541. Faida inayoongezeka kwa ajili ya programu katika kipindi cha miaka 50 (kwa kuzingatia bei za mwaka 2015) ilipatikana baada ya kutoa gharama za matumizi ya maendeleo na ya kawaida kutoka katika uchambuzi wa kiuchumi. Faida inayoongezeka ilitumika kukadiria kiwango cha faida kiuchumi (EIRR) na thamani halisi ya sasa *(NPV)* ilikokotolewa kwa kutumia kiwango pungufu cha 12%. Matokeo ya uchambuzi wa kiuchumi yanaonyesha kuwa *EIRR* ya ASDP II ni **14.8%** na *NPV* ya Shilingi 370,009 milioni (Dola milioni 172). Matokeo haya yanaonesha kuwa mapendekezo ya uwekezaji katika mradi yamethibitishwa uhalali wake kwenye uwanja wa kiuchumi.

542. Aidha, uchambuzi wa kina ulifanyika ili kupima uwezekano wa kiuchumi wa hatua zilizopendekezwa za mabadiliko mbalimbali katika mikondo ya gharama na faida. Uchambuzi huo ulionesha kwamba ASDP II inaweza kuhimili mabadiliko katika faida na gharama na inakuwa isiyo na faida kiuchumi kama kutakuwa na ongezeko la 21% katika gharama za uwekezaji na matumizi ya kawaida. Vilevile, kupungua kwa 18% kwa faida inayoongezeka ya mradi itasababisha EIRR kushuka chini ya 12%.

543. Matokeo ya uchambuzi wa kina katika **Jedwali Na. A10** yanaonesha kuwa kupungua kwa gharama za uwekezaji na gharama za kawaida kwa 20% kulisababisha kuwa na *EIRR* ya 18.8%, wakati ongezeko la gharama kwa 20% litapunguza *EIRR* kwa 12.1%. Aidha, kuongezeka kwa faida inayoongezeka kwa 20% kunazalisha *EIRR* ya 18.0% na upungufu wa faida wa 20% na hivyo kupunguza *EIRR* kwa 11.6%. Vilevile, uchambuzi uliangalia uwezekano wa mchanganyiko wa 20% ya ongezeko la faida na kupungua kwa gharama za mradi kwa 20%. Katika hali hiyo, *EIRR* itaongezeka hadi 22.6%. Kinyume chake ni kwamba kama upungufu wa faida wa 20% utaunganishwa na kuongezeka kwa gharama kwa 20%, *EIRR* itashuka hadi 9.3%.

544. Vilevile, mabadiliko katika idadi ya wingi wa mimea unaotarajiwa ulifanyiwa tathmini na uchambuzi ulionesha kuwa kama hali ya baadaye ya mradi ikiwa wingi wa mimea kwa 100% inadhaniwa (kwa kulinganisha na 103% katika suala la msingi), *EIRR* itashuka hadi 14.3%, wakati wingi wa mimea ikiwa ni 95 % tu itapunguza zaidi *EIRR* hadi 11.8%.

545. Kwa upande wa uzalishaji wa mazao, uchambuzi ulionesha kuwa kama mavuno ya mahindi na mpunga yataongezeka kwa 50% tu (kwa kulinganisha na 57% na 67% katika suala la msingi), EIRR itapungua hadi 10.7% na ASDP II inakuwa haina faida kiuchumi. Zaidi ya hayo, kama tija ya mazao kwa jumla ni 40% baada ya kumalizika kwa utekelezaji wa programu, *EIRR* inapungua hadi 7.7%. Hivyo, kuna uwezekano wa kiuchumi wa ASDP II katika kufikia mavuno ya kiwango kinachotarajiwa. Aidha, inatakiwa isisitizwe kwamba matumizi ya kanuni bora za kilimo na uongezekaji wa tija unaotarajiwa (kudumisha uwezekano wa kiuchumi) utafanikiwa kama huduma zinazofaa za kilimo zikijumuisha ugani/mafunzo na usambazaji wa pembejeo na pamoja na upatikanaji wa masoko na huduma za fedha vijijini zitapatikana kwa urahisi na ufanisi.

**Jedwali Na. A10: Uchambuzi wa Kina na Uwezekano wa Kiuchumi**

| Hali | EIRR (%) | NPV (TSh milioni) |
|---|---|---|
| Kwa kuanzia | 14.8% | 370,009 |
| Gharama za uwekezaji na gharama za kawaida -20% | 18.8% | 722,428 |
| Gharama za uwekezaji na gharama za kawaida +20% | 12.1% | 17,589 |
| Faida inayoongezeka +20% | 18.0% | 796,430 |
| Faida inayoongezeka −20% | 11.6% | −56,413 |
| Gharama -20% na Faida za kilimo inayoongezeka +20% | 22.6% | 1,148,850 |
| Gharama + 20% na Faida za kilimo inayoongezeka−20% | 9.3% | −408,832 |
| | | |
| Idadi ya wingi wa mimea wakati wa uwepo wa mradi kwa 100% | 14.3% | 299,966 |
| Idadi ya wingi wa mimea wakati wa uwepo wa mradi kwa 95% | 11.8% | −21,536 |
| 50% kuongezeka tija katika mazao | 10.7% | −531,096 |
| 40% kuongezeka tija katika mazao | 7.7% | −165,650 |

## KIAMBATISHO NA. VII: Uchambuzi wa vihatarishi na mikakati/hatua za kukabiliana navyo

| | | |
|---|---|---|
| **Wadau wa programu**<br>Kukosekana kwa sera zinazochochea ushiriki wa washirika wa kilimo-biashara katika shughuli za programu, hasa majukumu yao yanayotarajiwa katika uendelezaji wa mnyororo wa thamani inaweza ikadhoofisha kasi ya ufikiaji wa malengo ya programu. | Wastani | Majadiliano kuhusu kuboresha mazingira kwa ajili ya uwekezaji wa sekta binafsi yanaendelea, na Serikali imejiandaa kuimarisha uwekezaji binafsi katika kilimo kupitia mipango kama vile Kilimo Kwanza na Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania wa Nyanda za Juu (SAGCOT). Majukwaa ya Wadau ya Wilaya ya Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa chini ya programu yataboresha ushirikiano na mashauriano miongoni mwa wadau wa mnyororo wa thamani. |
| **Mazingira ya hatari ya uendeshaji** | | |
| Ukuaji wa uchumi wa nchi nchini Tanzania unakabiliwa na mshtuko wa kutoka nje na ndani ya nchi ambao unaweza kutokana na vikwazo vya miundo ya ndani. Kuna athari ya kuendelea na mshtuko mkubwa kutokana na kushuka kwa uchumi duniani,kuongezeka kwa bei za mafuta na chakula katika masoko ya kimataifa.<br><br>Vihatarishi vingine ni pamoja na ukame. Mishtuko hiyo ya nje inatokana na nchi kutegemea misaada ya wafadhili na hivyo kuifanya nchi iwe katika hali ambayo inashindwa kukabiliana na mabadiliko hayo. Mfumo wa fedha unazidi kuathiriwa kutokana na maamuzi ya kimkakati yanayotolewa na Serikali, ikiwa ni pamoja na kuongeza matumizi ya fedha zisizokubaliana kwa miradi ya uwekezaji, ugawaji usio na usawa wa rasilimali kati ya miundombinu na sekta za kijamii, na shinikizo la ndani la mishahara. Kiwango cha madeni ya umma kimeongezeka kwa kiasi kikubwa katika miaka ya hivi karibuni, kimefikia takriban 40% ya Pato la Taifa.<br>Uwezo mdogo katika mfumo wa Serikali na wafanyakazi wake wa kutekeleza na kusimamia ajenda ya maboresho pia ni kihatarishi kingine. Hii inajumuisha, hasa zaidi katika PFM, ikiwa ni pamoja na upangaji wa bajeti na utekelezaji. Vikwazo PFM kwenye serikali za mitaa ni wasiwasi hasa, kama Serikali za mitaa zinafuatilia sera ya ugatuaji wa madaraka. | | PRSC inatoa fursa za jukwaa ambalo Benki inaweza kushiriki katika majadiliano na Serikali kuhusu hali ya uchumi ili kujenga ujasiri dhidi ya mshtuko wa nje na wa ndani, kudumisha uendelevu wa fedha na kuimarisha programu ya maboresho<br><br>Mfululizo huu wa PRSC, kwa njia yake unazingatia PIM na PFM ikiwa ni pamoja na usimamizi wa madeni, moja kwa moja huchangia katika kupunguza vihatarishi vinavyohusiana na matumizi ya mikopo isiyo ya kawaida, taasisi za fedha, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa madeni<br><br>Mchakato wa majadiliano chini ya PRSC, kama vile PER, hushughulikia matatizo ya uwezo. Kazi inayofaa ya ujuzi chini ya PRSC ni kujenga uwezo wa uchanganuzi ambao pia utaongeza ushiriki wa Serikali na wadau wengine wa kitaifa, kama vile CSO na jumuiya ya kitaaluma ili kuongeza uwezo wa uchambuzi na kubadilishana ujuzi nchini, ambayo ni muhimu katika kuimarisha uwajibikaji wa ndani. |
| **Sekta ya kilimo na sekta mbalimbali**<br>Programu hii itatekelezwa chini ya mfumo wa taasisi mbalimbali, mazingira mbalimbali ya wafadhili, pamoja na utekelezaji wa miradi mingi. Hali hiyo, inaweza kusababisha ajenda na maslahi yanayokinzana, pamoja na uwezo wa kusimamia na kuratibu kwa ufanisi shughuli kadhaa chini ya miradi tofauti. | Wastani | Programu inatoa mfumo wa utekelezaji uliokubalika na Serikali, kwa kutumia mifumo imara ya Serikali. Mfumo wa uratibu wa sekta nzima utasaidia kuimarisha utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta ya kilimo. Mikataba ya maelewano itasainishwa kati ya washirika wa maendeleo wote wanaotekeleza ASDP II (na sekta) kukubaliana juu ya kanuni za uendeshaji na kusimamia misaada kwa sekta hiyo, kwa mujibu wa mfumo wa jumla wa uratibu wa sekta. . |

| | | |
|---|---|---|
| Vihatarishi kwa watekelezaji, Udhaifu katika usimamizi wa kifedha, manunuzi, tathmini na ufuatiliaji na usimamizi wa miradi hasa katika serikali za mitaa inaweza kudhoofisha uwajibikaji na kufuatilia matokeo ya programu. | Juu | Programu imefungamana na (inajumuisha) mpango wa Serikali ambao unasisitizia usimamizi wa matokeo na uwajibikaji. Kitengo cha Kilimo kitaanzishwa katika Wizara ya Kilimo ili kuongeza uwajibikaji na ufuatiliaji wa matokeo katika sekta hiyo. Aidha, kuna jitihada zinazoendelea za serikali za kuimarisha uwezo wa FM na manunuzi kwa kuajiri wafanyakazi na kutoa mafunzo. Programu iliyopendekezwa inajumuisha pia misaada kwa ajili ya kuimarisha taasisi na kujenga uwezo kwa wasimamizi wa programu. Jitihada za kuboresha takwimu za kilimo na mfumo wa tathmini na ufuatiliaji na kuanzishwa kwa Mfumo wa taarifa za masoko (MIS) chini ya programu kutaongeza mtiririko wa taarifa na uwajibikaji. Mkakati wa mawasiliano ulioandaliwa chini ya awamu ya kwanza utaimarisha usimamizi wa taarifa katika ngazi mbalimbali, uamuzi, na uwajibikaji na kuimarisha tathmini na ufuatiliaji na ubora wa taarifa. |
| **Utawala.** Mifumo duni ya bajeti na uwajibikaji hasa katika ngazi za mitaa inaweza kudhoofisha udhibiti wa ndani na fedha haziwezi kutumika kwa ufanisi na kiuchumi kwa madhumuni yaliyotarajiwa. Taratibu/kanuni na mfumo wa kodi katika ngazi ya Halmashauri zinaweza kuchangia katika kupunguza faida ya programu.<br>. | Wastani | Kila ASLM ina kitengo cha ukaguzi wa ndani na kamati ya ukaguzi. Kitengo cha uratibu wa programu kitatoa uangalizi wa ugawaji na matumizi ya rasilimali za programu ili kuhakikisha kwamba fedha zinatumiwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Uajiri wa wafanyakazi wa uhasibu wenye ujuzi, wahasibu wa ndani, na wafanyakazi wa manunuzi katika ngazi ya kitaifa umefanywa, na jitihada za kuimarisha uwezo wa Serikali za Mitaa katika uhasibu, ukaguzi wa ndani na ununuzi zinaendelea. |
| **Vihatarishi vya utawala,** udanganyifu na rushwa hasa kwa shughuli za manunuzi, kutokana na kutokuwepo kwa uwazi na uwezo mdogo wa kufuatilia na kutoa ripoti ya udanganyifu na rushwa, hasa katika ngazi ya Serikali za mitaa. | Wastani | Wakaguzi wa ndani wamepewa mafunzo kuhusu ukaguzi unaolingana na thamani ya fedha. Mbinu nyingine za uangalizi zitajumuisha ukaguzi wa utendaji wa mara kwa mara na ukaguzi wa kawaida wa matumizi ya fedha za umma. Utaratibu wa uwajibikaji wa jamii utaimarisha uwazi ubora na usahihi wa matokeo. |
| **Vihatarishi vya programu** | | |
| Uandaaji. Watekelezaji katika ngazi ya Taifa na Serikali za mitaa hawana uwezo wa kutosha kwa ajili ya kuendeleza mnyororo wa thamani na aina ya kilimo cha kibiashara kinachopendekezwa. Hii itaathiri ufikiaji wa malengo ya programu. Uwezo mdogo wa watoa huduma binafsi na udhaifu wa vyama vya wakulima wadogo unaweza kuzuia kuwafanya wakulima wadogo wawe wa kibiashara, uhamisho wa teknolojia na upataji wa faida kutokana na uwekezaji katika mnyororo wa thamani. | Juu | Kuna jitihada zinazoendelea za kuendeleza uchambuzi katika mnyororo wa thamani / mbinu katika ASLM na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Programu kwa ujumla itaunga mkono za juhudi za kuwajengea uwezo wa watoa huduma za biashara. Aidha, usaidizi wa ziada utatolewa ili kuimarisha vyama vya wakulima na kuwezesha uhusiano na watoa huduma binafsi / Kilimo-biashara. |

| | | |
|---|---|---|
| **Jamii na mazingira**<br>Kuna athari ya kushindwa kuzingatia matakwa ya sera za mazingira na kijamii kuhusiana na utekelezaji wa shughuli za programu, kama vile uwekezaji kwenye kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya mbolea na madawa ya kilimo. | Wastani | Serikali imeanzisha kitengo cha mazingira katika ngazi ya Kitaifa na Maafisa wa Mazingira wa Wilaya katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao wanafundishwa masuala ya kutunza mazingira. Maendeleo yaliyofanywa hadi sasa katika ushirikiano wa kutunza mazingira na jamii yataimarishwa zaidi katika utekelezaji wa programu ili kukidhi mahitaji ya Programu. Mpangilio wa ESMF / RPF, IPMP na INMP utarekebishwa ili kutoa mwongozo wa kuzuia hatari za ulinzi.<br>Mamlaka ya Serikali za Mitaa imechagua Maafisa wa Usimamizi wa Mazingira wa Wilaya (DEMOs) ambao wanawajibika katika uratibu na usimamizi wa uwekezaji ili kuhakikisha ushirikiano wa masuala ya uhifadhi. DEMO wamepewa mafunzo juu ya utekelezaji wa kanuni za ESMF / RPF, na Tathmini ya Mazingira na Jamii (ESIAs) na maandalizi ya Mpango wa Mazingira na Jamii (ESMPs) na / au Mipango ya Utekelezaji wa Makazi (RAPs). |
| **Programu na wafadhili**<br>Programu hii itafadhiliwa sambamba na wafadhili wengine wanaounga mkono mpango wa Serikali na miradi inayofadhiliwa na wafadhili wengine wasiokuwa wa ASDP II na sekta binafsi. Hali hiyo italeta ushindani wa uratibu na hivyo kudhoofisha utekelezaji wa malengo ya programu | Juu | Programu hii itasaidia Mpango wa Serikali uliokubaliwa. Makubaliano ya Maelewano yatasainiwa na wafadhili wote wa ASDP II ili kukubaliana juu ya kanuni za kifedha husika kwa ajili ya kuboresha uratibu miongoni mwa wafadhili. Mpango wa Serikali pia unahusisha msaada kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuboresha mipango ya sekta; kuwa na mfumo wa pamoja wa kufuatilia matokeo , ikiwa ni pamoja na malengo ya sekta na viashiria vya matokeo. Uratibu huu utatekelezwa chini ya SWAp 'iliyopanuliwa'. |
| Ufuatiliaji endelevu wa utekelezaji. Athari ya muda mrefu na uendelevu wa shughuli za programu ni uwezo mdogo na ushiriki mdogo wa watoa huduma binafsi katika maendeleo ya mnyororo wa thamani, ujuzi mdogo wa ufuatiliaji na tathmini na umiliki wa jamii kwenye uwekezaji wa programu | Wastani | Programu hiyo itazingatia makundi makubwa ya wilaya na kuimarisha uwekezaji wa sekta binafsi katika ngazi ya chini. ASDP II itatoa msaada wa kujenga uwezo kuhusu ufuatiliaji wa matokeo. |

# KIAMBATISHO NA.VIII: Ramani na Vielelezo muhimu

## Kielelezo Na. A28: Kanda za Ikolojia za Kilimo

**Kanda za ikolojia za kilimo Kitaifa**




Ramani imeandaliwa na Taasisi ya tafiti za Kilimo
Chanzo cha takwimu De Pauw 1984

| Aez_code | Altitude(masl) | Rainfall(mm/year) | Physiography |
|---|---|---|---|
| C1 | <200 | 1000-1200 | Coastal uplands |
| C2 | <500 | 800-1000 | Coastal lowlands |
| C3 | <500 | 800-1000 | Coastal uplands and rolling to steep hills |
| C4 | <200 | 1200-1400 | Flat, riverine floodplains and deltas |
| C5 | <200 | 1000-1200 | Flat to gently undulating plains |
| C6 | <100 | 1600-2000 | Nearly level to undulating and rolling plains |
| C7 | <100 | 1400-1600 | Nearly level to undulating and rolling plains |
| E1 | 500-1200 | 400-500 | Gently undulating to rolling plains |
| E10 | 400-600 | 1400-1600 | Flat alluvial plains with complex sedimentation pattern |
| E11 | 500-1000 | 1000-1200 | Complex depression |
| E12 | 1000-2000 | 800-1000 | Dissected, rolling to hilly mountain |
| E14 | 1000-2000 | 1000-1200 | Very strongly dissected mountain block |
| E15 | 800-1700 | 1000-1200 | Flat, undulating to rolling plains and plateaux |
| E2 | 500-1200 | 800-1000 | Gently undulating to rolling plains and plateaux |
| E3 | 200-750 | 800-1000 | Flat to rolling plains |
| E4 | 200-500 | 800-1000 | Flat to rolling plains |
| E5 | 200-500 | 800-1000 | Level to rolling plains |
| E6 | 150-500 | 1000-12000 | Undulating to rolling plains |
| E7 | 800-1500 | 800-1000 | Flat to rolling palns, locally hilly at medium altitude |
| E8 | Wide range | 500-600 | Flat alluvial plains affected by salinity |
| E9 | 400-500 | 800-1000 | Flat, alluvial plains with homogenous sedimentation pattern |
| H1 | 1500-2000 | 600-1600 | Flat to undulating and rolling plains and plateaux |
| H2 | 1500-2100 | 1400-1600 | Undulating to rolling plains |
| H3 | 1500-2300 | 1000-1200 | Strongly dissected hills and mountains |
| H4 | 500 | > 2000 | Flat to very gently undulating lacustrine plains |
| H5 | 1200-2400 | 1000-1200 | Undulating to rolling volcanic plains and plateaux |
| H6 | 2300-2700 | 1000-1200 | Undulating to hilly plateau |
| H7 | 1500-2300 | 800-1000 | Mainly mountaineous, undulating to hilly plateau crests |
| Lake | | | |
| N1 | 1500-2500 | 600-700 | Undulating plains |
| N10 | 1500-1800 | 1400-1600 | Undulating to rolling plateaux and plains |
| N2 | 2000-2500 | 800-1000 | Rolling to hilly plateau with calderas and volcanic cones |
| N3 | 900-1100 | 400-500 | Flat lacustrine plains |
| N4 | 900-1600 | 500-600 | Volcanic mountains with gentle to steep slopes |
| N5 | 1300-1700 | 1000-1200 | Flat to rolling plains |
| N6 | 1300-1700 | 200-400 | Flat to rolling plains |
| N7 | 1300-1800 | 600-700 | Level to rolling plains |
| N8 | 1300-2300 | 800-1000 | Level to undulating or rolling plains |
| N9 | 1100-1800 | 700-800 | Gently undulating plains with some rocky hill-footslope associations |
| Lake | | | |
| P1 | 1100-1300 | 600-700 | Undulatingpalins |
| P10 | 1100-1400 | 500-600 | Gently undulating plains |
| P11 | 900 | 500-600 | Flat plains |
| P12 | 900-1200 | 600-700 | Flat, seasonally inundated plains with permanent or semi-permanent swamps |
| P13 | 900-1200 | 800-1000 | Flat, seasonally inundated lowland plains |
| P2 | 1100-1300 | 200-400 | Gently undulating plains |
| P3 | 1100-1300 | 800-1000 | Gently undulating plains |
| P4 | 1200-1300 | 800-1000 | Flat to gently undulating plains with scattered hill-footslope associations |
| P5 | 1100-1300 | 600-1000 | Gently undulating plains |
| P6 | 800-1800 | 800-1000 | Undulating plains and plateaux |
| P7 | 1000-1100 | 600-700 | Flat to very gently undulating plains |
| P8 | 1000-1200 | 600-800 | Flat to gently undulating plains |
| P9 | 1000-1400 | 500-600 | Gently undulating plains |
| R | | | Rocky terrain |
| R1 | 800-1000 | 1000-1200 | Flat plains covered by riverine or lacustrine alluvium, saline or sodic and vari |
| R2 | Variable | 1000-1200 | Flat to very gently undulating plains covered by lacustrine alluvium |
| R3 | 900-1400 | 600-1000 | Flat plains covered by riverine alluvium and regularly flooded |
| R4 | 1000 | 1200-1400 | Complex terrain |
| S1 | 200-500 | 800-1000 | Gently undulating to rolling plateaux |
| S2 | 200-1000 | 1000-1200 | Gently undulating to rolling plateaux |
| U | 1400-2300 | 1000-1200 | Complex of flat to gently undulating plains |
| W1 | 1300-1800 | 1000-1500 | Dissected hilly plateaux |
| W2 | 1500-1700 | 1000-1500 | Strongly dissected hills |
| W3 | 1200-1600 | 800-1000 | Undulating to rolling upland plains |
| W4 | 1400-1500 | 1000-1500 | Undulating to rolling plains |

**Jedwali Na. A11: Kanda za Ikolojia za Kilimo (AEZ), bidhaa na Wilaya za kipaumbele (kwa majaribio)**

| AEZ | | Bidhaa kipaumbele | | Mikoa | Wilaya |
|---|---|---|---|---|---|
| | | mazao | mifugo/ uvuvi | | |
| 1 | **Maeneo kame (mvua ya mara moja 400–900 mm)** | alizeti/ mahindi/ mtama/ uwele, mchele, viazi, mhogo, kilimo cha mazao ya bustani, | nyama ya ng'ombe, maziwa, mbuzi, | Mara (E) | Musoma TC, Musoma DC, Serengeti, Bunda, Tarime, Rorya |
| 2 | **Mashariki ya Pwani** | mahindi ,mchele, korosho, mhogo, maharagwe, miwa, Mazao ya mafuta, kilimo cha maua, mwani. | mbuzi, (mvua ya mara moja) ndege, samaki | Dodoma (E) | Nyanda za Umasaini (Masai Steppe), Tarangire, Mkomazi, Pangani na Dodoma Mashariki |
| | | | | Simiyu | Bariadi DC, Maswa, Meatu, Itilima, Busega |
| | | | | Manyara (E) | Kiteto, Simanjiro |
| | | | | Lindi | Lindi DC, Lindi MC, Liwale, Ruangwa, Kilwa, Nachingwea. |
| | Maeneo ya mbuga na chepechepe | Mchele na miwa | maziwa (Mvua za mara mbili), nyama ya ng'ombe, kuku, mbuzi, ngozi/ kwato, samaki, | Mtwara | Mtwara T.C, Mtwara DC,Masasi, Nanyumbu, Tandahimba,Newala |
| | | | | Tanga | Handeni, Kilindi, Korogwe DC, Lushoto, Muheza, Mkinga, Pangani, Tanga, Korogwe |
| | | | | Pwani | Kibaha TC, Kibaha DC, Bagamoyo,Mafia, Mkuranga, Kisarawe, Rufiji |
| | | | | Dar-es-Salaam | Ilala, Kinondoni, Temeke |
| | | | | Pwani | Rufiji |
| | | | | (Mbeya) | Mbarali |
| | | | | (Morogoro) | Kilombero |
| 3 | **Nyanda za juu kaskazini (Mvua mara mbili)** | Maharage, mchele, jamii ya mikunde/ maharage, mboga za majani, ndizi | nyama ya ng'ombe, mbuzi, maziwa | Arusha (S) | Arusha DC, Meru, Arusha MC, Karatu, Monduli, Longido, Ngorongoro |
| 4 | **Tambarare (Mvua mara moja)** | **Mahindi na jamii ya mikunde** | | Kilimanjaro (N) | Moshi D. C., Hai, Siha, Moshi M. C, Mwanga, Rombo, Same |
| | | | | Manyara (E) | Babati TC, Babati D.C Hanang, Mbulu |
| | | | | W: Tabora, Rukwa/ Katavi | Tabora MC, Igunga, Nzega, Sikonge, Tabora(Uyui, Urambo Mpanda DC, Mpanda TC, Mlele |

| AEZ | | Bidhaa kipaumbele | | Mikoa | Wilaya |
|---|---|---|---|---|---|
| | | mazao | mifugo/ uvuvi | | |
| | | | | Mbeya (N) | Chunya (partie N) |
| | | | | Ruvuma + Morogoro (S) | Songea T. C, Songea D.C, Namtumbo, Mbinga, Tunduru, Ulanga (Mo) |
| | | | | Mwanza | Mwanza CC, Magu, Geita, Ukerewe, Misungwi, Sengerema, Kwimba |
| | | | | Geita | Geita DC, Chato, Bukombe, Nyang'wale, Mbogwe |
| **5** | **Kati (Mvua mara moja)** | **Mbegu za mafuta** mahindi/ mtama/ uwele, mchele, kilimo cha mazao ya bustani, miwa | nyama ya ng'ombe, mbuzi, ndege, maziwa, | Dodoma (W) | Kondoa, Dodoma MC, Mpwapwa, Kongwa, Bahi, Chamwino |
| | | | | Singida | Singida DC, Singida MC, Manyoni, Iramba, Ikungi, Mkalama |
| | | | | Shinyanga | Shinyanga M C, Shinyanga D.C, Kishapu ,Kahama |
| | | | | Morogoro | Morogoro MC, Morogoro DC, Mvomero |
| **6** | **Nyanda za juu kusini** | mahindi, Mchele, viazi, kilimo cha Mazao ya bustani, Chai / Kahawa, miwa | nyama ya ng'ombe, mbuzi, ndege, maziwa. | S-Mbeya | Mbeya MC, Mbeya D. C, Mbarali, Kyela, Rungwe, Mbozi, Ileje, Chunya (S) |
| | | | | S-Iringa | Iringa DC, Kilolo DC, Iringa (S), Mufindi, |
| | | | | Njombe | Makete, Ludewa, Njombe TC, Njombe DC. Makambako, |
| | | | | Morogoro NW | Kilombero, Kilosa |
| **7** | **Nyanda za juu kusini magharibi** | Maharage, kilimo cha mazao ya bustani, pembe, viazi, ngano, mchele, **mbegu za mafuta** | ndege, nyama ya ng'ombe,maziwa, mbuzi, samaki | Rukwa | Sumbawanga D.C, Sumbawanga TC, Nkasi, Mpanda DC, Mpanda TC |
| **8** | **Nyanda za juu magharibi** | Pamba, miwa, Mchele, Mahindi, mhogo, mbegu/ mazao ya mafuta /, ndizi, kahawa | ndege, nyama ya ng'ombe, mbuzi, samaki | Kigoma | Kasulu, Kibondo, Kigoma DC, Kigoma TC |
| | | | | Kagera (bimodal) | Biharamulo, Bukoba D. C, Misenyi, Bukoba T. C, Karagwe, Muleba, Ngara |

Chanzo: ASDP II BF (2013)—ARD; Mpango wa Kilimo wa Kuhimilili Mabadiliko ya Tabianchi Tanzania (2015) na de Pawn (1984)

### Jedwali Na. A12: Uzalishaji wa Kilimo —mazao ya kilimo

| | | | | | | Tani '000 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka/ Mazao | 2003/ 2004 | 2004/ 2005 | 2005/ 2006 | 2006/ 2007 | 2007/ 2008 | 2008/ 2009 | 2009/ 2010 | 2010/ 2011 | 2011/ 2012 | 2012/ 2013 | 2013/ 2014 |
| Mahindi | 3,157 | 3,219 | 3,423 | 3,302 | 3,556 | 3,326 | 4,475 | 4,341 | 5,104 | 5,288 | 6,734 |
| Mtama | 757 | 714 | 712 | 971 | 861 | 709 | 789 | 807 | 839 | 782 | 883 |
| Uwele | 201 | 221 | 228 | 194 | 203 | 220 | 372 | 312 | 214 | 292 | 363 |
| Mchele | 688 | 759 | 805 | 872 | 875 | 868 | 1,700 | 1,461 | 1,170 | 1,342 | 1,681 |
| Ngano | 67 | 102 | 110 | 83 | 92 | 95 | 62 | 113 | 109 | 102 | 167 |
| Jamii ya mikunde | 879 | 886 | 1,050 | 1,156 | 1,126 | 1,116 | 1,254 | 1,632 | 1,827 | 1,871 | 1,697 |
| Muhogo | 1,480 | 1,846 | 2,053 | 1,733 | 1,797 | 1,972 | 1,464 | 1,549 | 1,821 | 1,878 | 1,664 |
| Ndizi | 734 | 991 | 1,169 | 1,028 | 982 | 1,073 | 975 | 1,048 | 842 | 1,317 | 1,064 |
| Viazi | 874 | 931 | 1,396 | 1,322 | 1,379 | 1,392 | 1,231 | 1,710 | 1,418 | 1,808 | 1,761 |

### Jedwali Na. A13: Uzalishaji wa Kilimo —mazao ya biashara (katika vipimo vya tani)

| Mwaka/ Mazao | 2004/ 2005 | 2005/ 2006 | 2006/ 2007 | 2007/ 2008 | 2008/ 2009 | 2009/ 2010 | 2010/ 2011 | 2011/ 2012 | 2012/ 2013 | 2013/ 2014 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Chai | 32,000 | 30,000 | 34,446 | 32,698 | 34,165 | 33,160 | 35,000 | 33,000 | 33,700 | 33,000 |
| Miwa | 229,620 | 263,317 | 192,535 | 265,434 | 276,605 | 279,850 | 317,000 | 260,055 | 286,380 | 293,011 |
| Tumbaku | 51,970 | 56,500 | 65,299 | 55,567 | 58,702 | 60,900 | 78,000 | 126,624 | 74,240 | 100,000 |
| Pamba | 344,210 | 376,591 | 130,565 | 200,662 | 368,229 | 267,004 | 260,000 | 225,938 | 351,151 | 246,767 |
| Pareto | 1,000 | 2,800 | 1,500 | 2,800 | 3,280 | 3,320 | 5,000 | 5,700 | 6,100 | 7,000 |
| Katani | 26,800 | 27,794 | 30,934 | 33,039 | 33,208 | 26,363 | 35,000 | 33,406 | 23,344 | 41,104 |
| Kahawa | 54,000 | 34,334 | 48,869 | 43,000 | 62,345 | 40,000 | 60,575 | 33,219 | 71,200 | 48,599 |
| Korosho | 81,600 | 77,158 | 92,232 | 99,107 | 79,068 | 74,169 | 121,070 | 160,00 | 121,704 | 127,939 |
| | | | | | | | | | | |
| Matunda | | | | | 557,400 | 3,297,910 | 3,751,170 | 3,938,730 | 4,096,280 | 4,416,690 |
| Mbogamboga | | | | | 602,000 | 766,570 | 858,740 | 901,680 | 937,750 | 1,005,305 |
| Maua | | | | | | 8,670 | 9,100 | 9,850 | 10,200 | 10,790 |
| Viungo | | | | | 6,865 | | 7,150 | 7,370 | 8,125 | 8,377 |

## Kielelezo Na. A29: Kanda na Vituo vya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Kanda za Kati, Mashariki, Ziwa, Kaskazini, Kusini na Magharibi )

**Ramani Na: 2: Kanda na Vituo vya Utafiti wa Kilimo Tanzania**




## Kielelezo Na. A30: Kanda za Ikolojia za Kilimo Tanzania



**Kielelezo Na. A31: Mifumo ya Uzalishaji ya Kilimo Tanzania**




**Kielelezo Na. A32: Ramani- Wilaya ambazo hazina na uhakika wa usalama wa chakula (2006-13)**



**Kielelezo Na. A33: Ramani– Mtawanyiko wa Ng'ombe Tanzania 2008**



# KIAMBATISHO Na. IX: Vigezo vya chagua wa wilaya za kipaumbele

**Vigezo vya kuteua wilaya lengwa (ndani ya kanda za ikolojia za kilimo -AEZ)**

a. Kanda za Ikolojia ya Kilimo (tazama Jedwali Na. lenye mnyororo wa thamani wa awali)
b. Asilimia ya sasa inayouzwa katika mnyororo wa thamani wa bidhaa unaolengwa
c. Asilimia katika mfumo wao wa kilimo (% ya mapato)
d. Usalama wa chakula na lishe
e. Uwezo wa uwekezaji katika kipindi cha miaka mitano iliyopita
f. Msaada wa mashirika yasiyo ya kiserikali hasa katika maendeleo ya mnyororo wa thamani
g. Vyama vya wakulima vilivyoimarika

**Mbinu.** Kwa madhumuni ya kuelekeza msukumo katika huduma zinazohitajika katika uzalishaji, kongani za uzalishaji (zitawekwa katika makundi matatu au sita katika kila wilaya) zitaanzishwa kwa bidhaa za kimkakati zilizochaguliwa katika kila kanda ya ikolojia ya kilimo (saba). Mbinu ya kutumia kongani huongeza utoaji wa huduma muhimu, kusaidia katika uendelezaji wa kiuchumi, kuendeleza miundombinu inayohitajika, kuwezesha uzalishaji kwa wingi wa mazao, kuwezesha usindikaji na kupunguza gharama za kufanya biashara. Kongani ya bidhaa itakuwa ni eneo thabiti linalojumuisha wilaya tatu hadi sita, ambapo tayari kuna uwezekano uliothibitika wa bidhaa hiyo maalum, ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa watendaji wa mnyororo wa thamani (mfano, wazalishaji, wafanyabiashara, wasindikaji na watoa huduma), MSIP na miundombinu ya msingi ya masoko. Mradi utalenga mahindi, mpunga, mbegu za mafuta na bidhaa nyingine za kimkakati ambazo zitakuwa mbadala wa kuagiza au kusafirisha nje katika masoko ya kikanda.

Kwa kupitia mbinu ya mnyororo wa thamani, programu hiyo itasaidia upatikanaji wa matumizi ya teknolojia zinazoongeza tija katika uzalishaji (mbegu bora, mbolea, utumiaji wa mashine na maji kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo) pamoja na miundombinu na huduma za kilimo biashara kwa ajili ya uuzaji na kuongeza thamani. Uwezo wa wa sekta binafsi, ikiwa ni pamoja na vyama vya wakulima na vyama vya ushirika, utaimarishwa ili kuwezesha wadau kupata pembejeo, masoko na usindikaji. Matumizi ya pembejeo bora ni kikamilisho kwenye utafiti na huduma za ushauri na ni majibu ya gharama nafuu kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na mapato ya kilimo, lakini pia ni njia nzuri ya wa kuzuia uwezekano wa athari za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa ardhi. Upatikanaji wa uhakika wa aina na mbegu zilizochaguliwa, usimamizi husishi wa rutuba ya udongo na maandalizi ya ardhi kwa wakati pia kutasaidia wakulima kuelekea kwenye kilimo endelevu na kukabiliana na athari za hali ya hewa. Utumiaj wa zana na teknolojia sahihi kwa ajili ya shughuli za uzalishaji na zile za baada ya kuvuna si tu kutaongeza tija kwa wafanyakazi vijijini lakini pia kuvutia wajasiriamali vijana katika sekta.

**Wigo na Mwelekeo wa Programu.** Programu italenga katika bidhaa moja / au mbili za kipaumbele (mazao na mifugo) kwa kila kanda ya ikolojia ya kilimo. Katika kila kanda, wilaya zenye uwezekano (tatu hadi sita) zitatambuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu kulingana na vigezo ambavyo wamekubaliana.

### Vigezo vya uchaguzi vinaivyopendekezwa

1. Uwezo wa uzalishaji wa kilimo wa bidhaa lengwa (ardhi ya kilimo / kame / nusu jangwa /, vipindi vya mvua, n.k)
2. Upatikanaji wa miundombinu ya uzalishaji na masoko (barabara, reli, umeme, nk)
3. Historia ya nyuma ya wilaya kuhusu michango ya wanufaika / kuhusika kwao (wanufaikaji) katika mipango ya maendeleo
4. Kuwepo kwa sekta binafsi itakayoshiriki katika mnyororo wa thamani ya bidhaa za kipaumbele
5. Kiwango cha uzalishaji cha mazao yanayolengwa / idadi na aina ya mifugo
6. Mipango mingine inayoendelea kutekelezwa (programu) katika maeneo ili kuepuka kurudia

**Kielelezo Na. A34: Ramani ya Wilaya za kipaumbele zinazolengwa katika ASDP II**




## KIAMBATISHO Na. IX: Uendeshaji wa AEZ na mbinu za kongani

1. ASDP II inalenga katika Kanda za Ikolojia ya Kilimo na kutumia mbinu za kongani. Bidhaa / kongani inajumuisha wilaya tatu hadi sita na zenye mnyororo wa thamani wa bidhaa wenye fursa ya juu zaidi, pamoja na kuwepo kwa wadau wa mnyororo wa thamani (mfano, wazalishaji, wafanyabiashara, wasindikaji na watoa huduma).
2. Timu mbalimbali (DCP/MSIP) zitaundwa ili kuwezesha uendeshaji wa makundi chini ya usimamizi na uratibu wa Mkoa **kupitia sehemu ya sekta za Uchumi na Uzalishaji.**
3. Kama kongani moja inajumuisha wilaya kutoka mkoa zaidi ya mmoja, basi mikoa husika itachagua mkoa kiongozi wa kusimamia na kuratibu shughuli za kongani.
4. Kazi ya timu ya wilaya ya mnyororo wa thamani (DCP) itakuwa ni kuwezesha mazungumzo kati ya watendaji wakuu wa bidhaa (Wazalishaji, Wafanyabiashara, Wasindikaji, Watoa Huduma wa Umma na Binafsi - PSP) kuandaa kwa pamoja mkakati, mpango kazi na ufuatiliaji na tathmini ili kuboresha utendaji wa minyororo unaolengwa wa thamani ya bidhaa.
5. Aidha, DCP itakuwa muhimu katika suala la kuanzisha rasmi au hata taratibu za dharura za kuhimiza muunganiko katika mnyororo wa thamani kati ya wadau binafsi na wa umma na kuendesha uvumbuzi / mabadiliko kuelekea kwenye viwango vya juu vya uzalishaji kibiashara katika kipaumbele kinacholengwa cha mnyororo wa thamani (au kikundi kinachofanana cha minyororo ya thamani).

## KIAMBATISHO NA. X: Mabadilko ya Tabianchi na Utekelezaji wa Mpango wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (ACRP)

Wizara ya Kilimo inachukua hatua mbalimbali kuhusu mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania. Kwa mujibu wa Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa (2013), ambao unazitaka sekta zote nyeti kwa masuala ya hali ya hewa kuanda mipango kazi kwa ajili ya utekelezaji wa maeneo ya kimkakati ya mkakati huo, Wizara ya Kilimo imeandaa Mpango wa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (*ACRP*) ili kutambua na kukabiliana na athari zaidi zinazosababishwa na kutofautiana kwa hali ya hewa na mabadiliko ya hali ya hewa kwa sekta ndogo ya mazao. ACRP itatumika kama mfano wa kuimarisha mabadiliko ya hali ya hewa ndani ya sera za sasa za kilimo, mipango, na njia bora, pamoja na kutambua maeneo mapya ya uwekezaji yanayoweza kuhitajika. Utakuwa ni mfumo wa kuongoza kwa njia kamili zaidi na thabiti ya kukabiliana na moja ya vihatarishi vikubwa katika uzalishaji wa sasa wa mazao na uwekezaji wa baadaye.

**Kwa nini mabadiliko ya hali ya hewa ni changamoto kwa kilimo cha mazao?** Kilimo ni sekta muhimu Katika uchumi wa Tanzania, na inachangia asilimia 25 ya Pato la Taifa, 24% ya mauzo ya nje, hutegemewa na asilimia 75-80 ya Watanzania ambao wengi wao ni maskini. Ni sekta ya kipekee sana licha ya kuwa na rasilimali za ardhi na maji za kutoshana hali ya hewa nzuri katika maeneo mengi kwa miaka mingi, bado inakabiliwa na tija ndogo na umaskini unaoendelea. Pamoja na kuwepo kwa aina nyingi ya mazao ya chakula, lakini kaya nyingi zinazohusika katika sekta huzalisha aina chache ya mazao ya chakula kwa ajili ya kujikimu licha ya kuwa na rasilimali hizi kaya zinakuwa na changamoto ya usalama wa chakula na mshtuko wa kiuchumi. Japokuwa uchumi wa Tanzania na sekta ya kilimo umepata mafanikio ya kiuchumi, hata hivyo mchango wake haujapunguza umaskini kutokana na wananchi walio wengi vijijini bado wanategemea matumizi ya teknolojia duni na mvua ambazo hazitabiriki kwa ajili ya maisha yao na upatikanaji wa uhakika wa chakula.

Sababu hizo zinaathiri mabadiliko ya hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi ambayo yana athiri sekta ya kilimo, pamoja na uwezo wa kukabiliana na hali ya sasa ya mabadiliko. Mwelekeo wa kimkakati wa sekta ya kilimo ni kuboresha kilimo kuwa cha kisasa kwa kukuza mashamba makubwa ya kibiashara, upanuzi wa kilimo cha umwagiliaji, kuimarisha minyororo ya thamani, na kuboresha uhusiano na wakulima wadogo. Upunguzaji wa umaskini vijijini, ukuaji wa uchumi, na utoshelevu wa chakula unaotarajiwa, lakini hii itaongeza shinikizo kwenye matumizi ya maliasili ambazo tayari zinakabiliwa na kiwango cha juu cha uharibifu kutokana na kilimo, pamoja na ushindani wa matumizi.

Hali ya hewa ya Tanzania ina utofauti mkubwa na ni changamani, na mwenendo wa hali ya hewa unaonesha kuwa joto linapanda na mvua haitabiriki. Taarifa za hivi karibuni zinaonesha kwamba wastani wa joto la mwaka litaongezeka kwa 1ºC ifikapo 2050, na mabadiliko katika mifumo ya mvua inaweza kusababisha mabadiliko makubwa katika maeneo ya kanda za ikolojia za kilimo, kuongezeka kwa mashaka katika mwanzo wa msimu wa mvua, na kuongeza ukame na mafuriko. Masuala mengine kama vile kujitokeza kwa wadudu na magonjwa na kuhamia katika maeneo mapya ya kijografia tayari imekisiwa kama athari za moja kwa moja za mabadiliko ya hali ya hewa. Athari zinazohusiana na hali ya hewa tayari zinaigharimu sekta ya kilimo takriban Dola milioni 200 kwa mwaka (Benki ya Dunia, 2013), na bila ya kukabiliana kwa haraka gharama hizi zinaweza kuongezeka kutokana na kuongezeka kwa utofauti wa wa hali ya hewa.

Kilimo nchini Tanzania kitaendelea kutegemea mvua katika siku zijazo. Kwa Kuangalia mbele, mvua zinapopungua kwa asilimia 10 imekua ikihusiana na kushuka kwa asilimia 2 ya Pato la Taifa, na kupanda kwa joto kwa 2 ° C kunaweza kupunguza mavuno ya mahindi kwa 13% na mpunga kwa zaidi ya asilimia 7. ambazo zinawezekana kutokea Tanzania katika zaidi ya karne ijayo. Athari za hali ya hewa zitazidisha ushindani wa rasilimali maji, mmomonyoko wa udongo na afya, na uharibifu wa ardhi: uhaba wa maji na mtiririko mdogo na ubora wa maji na , ubora wa maji tayari umeonekana katika maeneo muhimu ya uwekezaji wa kilimo kutokana na ufanisi mdogo wa matumizi ya maji na ushindani kutoka kwa watumaji wengine, na baadhi ya mifano ya hali ya hewa huonyesha kuwa mvua inatarajia kupungua, lakini maeneo haya yamepangwa kwa ajili ya uwekezaji katika mazao makubwa yanayotumia maji kama mpunga na miwa pamoja na upanuzi wa kilimo cha umwagiliaji.

Kama suala mtambuka la kisekta na matokeo makubwa ya kiuchumi, kijamii na mazingira, mipango ya

mabadiliko ya hali ya hewa haiwezi kutokea bila kuwekewa mkazo. Wakati huo huo, mchakato thabiti lazima utambue mabadiliko ya mara kwa mara, kutokana na upeo wa muda mrefu na mapungufu ya hali ya hewa na mazao na kutabiri athari za kupanda kwa joto pamoja na mabadiliko ya mvua katika mazao. Njia mojawapo ya kukabiliana na mapungufu haya ni kutumia mbinu shirikishi za kukabiliana na athari , kama ilivyofanyika kwa ACRP. Mchakato wa ACRP umehusisha wataalam kutoka mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa, mipango ya matumizi ya ardhi, zana, hali ya hewa, sayansi ya udongo, usimamizi wa rasilimali za maji, usimamizi wa wadudu, maendeleo ya jamii na uhamasishaji kushirikiana ili kuandaa mpango kazi na uwekezaji unaoendana na muktadha wa Tanzania kuanzia ngazi ya sera hadi shambani.

**Ni jinsi gani mabadiliko ya tabianchi yanaweza kubadili kilimo cha Tanzania?** Athari tatu zimejitokeza katika mchakato wa kutengeneza mpango, ambayo ni muhimu ili kuongeza ustadi wa kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa katika kipindi kifupi kijacho ikizingatiwa pia hali ya mabadiliko ya muda mrefu

1. **Kwanza, mabadiliko ya hali ya hewa yataongeza mahitaji ya rasilimali za maji kutokana na usimamizi mbaya, uharibifu na matumizi ya ushindani.** Umwagiliaji peke yake hautaweza kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa, na unaweza kuleta athari zisizo za moja kwa moja ikiwa rasilimali za maji haziwezi kusimamiwa ipasavyo. Hatua za kukabiliana ili kuboresha maji, udongo na usimamizi wa ardhi zinahitajika kwa haraka ili kujenga ujasiri wa kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa yajayo kwa wakulima wadogo na mashamba makubwa ya kibiashara.

2. **Pili, uzalishaji wa mazao muhimu ya nafaka unaweza kupungua kutokana na kupanda kwa joto na kupungua kwa upatikanaji wa maji, ambayo yatakuwa na athari kwa uwekezaji wa kibiashara, wakulima wadogo, na usalama wa chakula.** Hatua za kukabiliana ni lazima zizingatie kuongeza uzalishaji wa mazao ya nafaka, hasa kujenga uwezo wa wakulima wadogo ili waongeze uzalishaji kwa kutumia "mbinu bora za usimamizi", na kutafiti athari za kupanda kwa joto na mabadiliko ya kipindi cha mvua kwenye mazao muhimu.

3. **Tatu, wakulima wadogo ni miongoni mwa waathirika wa mabadiliko ya hali ya hewa , pamoja na athari kubwa juu ya maisha na usalama wa chakula.** Hatua za kukabiliana zinatakiwa kuzingatia jinsi ya kupunguza athari za hali ya hewa kwa wakulima wadogo, kukuza mbinu za kilimo ambazo zitaongeza uzalishaji na kulinda rasilimali za asili, na kwa makusudi kulenga maeneo yaliyoathirika.

Ujumbe huu, unaakisi michango ya wadau, sayansi ya sasa ya hali ya hewa na uchambuzi wa athari za kilimo nchini Tanzania, ambazo zilikuwa katika kuandaa maeneo ya kipaumbele ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

**Jinsi gani Kilimo kinaweza kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa?** Ili kupunguza athari, hatua za kipaumbele na uwekezaji zimeandaliwa, kuweka msingi wa kuzihimili katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Hizi zilitambuliwa kama maeneo yenye uwezo wa juu wa athari kwa ajili ya kukabiliana nazo. Wadau wa kilimo walipendekeza hatua za kuchagua za kukabiliana na hali ambayo itasaidia kuunganisha masuala ya ustahimilivu katika maamuzi ya sera za kilimo, kusaidia mchakato wa mipango, na uwekezaji.

1. **Hatua ya 1: Kuboresha upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo na usimamizi wa ardhi.** Uwekezaji wa kipaumbele ni pamoja na ufanisi wa matumizi ya maji na uhifadhi wa maji, maboresho katika usimamizi wa vyanzo vya maji katika mipango ya kilimo, na kupitishwa kwa usimamizi wa ardhi na maji endelevu ili kupunguza uharibifu.

2. **Hatua ya 2: Kuharakisha uendelezaji wa kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi.** Uwekezaji wa kipaumbele ni pamoja na kujenga msingi wa mbinu za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na kutoa motisha ili kufidia gharama za matumizi kupokelewa, kuhamasisha matumizi yake katika ngazi ya Wilaya, na kujenga uwezo na uelewa kuhusu mbinu hizo.

3. **Hatua ya 3: Kuwalinda wenye mahitaji maalum dhidi ya athari za hali ya hewa.** Uwekezaji wa kipaumbele ni pamoja na hatua za kujiandaa na kukabiliana na dharura na atharii zinazohusiana na hali ya hewa -na udhibiti bora wa wadudu na magonjwa zijumuishwe katika hatua hizi, kujenga ujasiri kwa kuhamasisha kufanya shughuli nyingine mbalimbali na kufanya majaribio usimamizi wa athari kama vile kutoa fedha .

4. **Hatua ya 4: Kuimarisha ujuzi na mifumo ili kukabiliana na athari za hali ya hewa.** Uwekezaji wa kipaumbele ni pamoja na kujaza mapengo muhimu ya utafiti, kufanya tathmini ya kina ya mabadiliko ya hali ya hewa na kuathirika kwa kilimo, kuandaa mifumo ya usimamizi wa taarifa na kampeni za mawasiliano, hasa taarifa sahihi na kwa wakati za hali ya hewa, na kuingiza masuala ya kijinsia katika shughuli za mabaodiliko ya hali ya hewa kwa ajili ya kilimo.

**Jedwali Na. A14: Maeneo ya kipaumbele ya utekelezaji wa uwekezaji: ACRP (Iliyopigiwa mstari ni maeneo muhimu ya kipaumbele)**

| Hatua na uwekezaji kipaumbele | Maeneo ya utekelezaji/ hatua | Uwekezaji/hatua muhimu | S/C |
|---|---|---|---|
| **1. Kuboresha ardhi ya kilimo na usimamizi wa maji** (Ustawi wa Ardhi na Usimamizi wa Maji) | *Ufanisi wa matumizi ya maji (ufanisi wa umwagiliaji, SRI nk)* | 1. Mwongozo kwa ajili ya kujumuisha mabadiliko ya hali ya hewa katika upanuzi / ukarabati na usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji.<br>2. Kupitia sera ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya maji na kuingilia mabadiliko ya hali ya hewa<br>3. Kukusanya takwimu za maji, kuvuna, teknolojia ya kuhifadhi na ufanisi wa matumizi<br>4. Tathmini ya karibu ya kuunganisha upatikanaji wa maji na mabadiliko ya hali ya hewa katika mipango ya umwagiliaji<br>5. Kuhamasisha matumizi endelevu ya maji ya chini ya ardhi kwa ajili ya umwagiliaji<br>6. Kusaidia uvunaji wa asili na wa kisasa wa maji ya mvua<br>7. Kuhamasisha uhifadhi wa maji vijijini/mashambani<br>8. Kuhamasisha matumizi ya teknolojia zenye ufanisi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji<br>9. Kuunga mkono mbinu sanifu za uzalishaji wa mchele | Sc 1.3 |
| | *Uvunaji wa maji ya mvua & usimamizi husishi wa maji na udongo* | 10. Kuandaa mbinu za kuratibu ardhi ya kilimo / maji<br>11. Mpango wa usimamizi wa uhifadhi na mipango ya umwagiliaji<br>12. Kulinda vyanzo vya maji kwa kwa ajili ya kilimo<br>13. Kuandaa miongozo,mitaala na mafunzo ya kujenga uwezo kwa ajili ya WUA<br>14. Kuongeza uhifadhi wa udongo na maji katika eneo linalomwagiliwa na eneo kavu | |
| | *Usimamizi wa ardhi & vyanzo vya maji* | 15. Kuandaa miongozo juu ya usimamizi endelevu wa udongo na maji.<br>16. Kujenga uwezo wa kupanga, kutekeleza na kufuatilia Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Maji<br>17. Mipango ya usimamizi wa ardhi ya kijiji ili kuwezesha matumizi endelevu ya ardhi<br>18. Mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Wilaya na kufuatilia kilimo cha kujikimu/ kibiashara<br>19. Kuongeza ufahamu wa usimamizi endelevu wa ardhi ya kilimo na maji,<br>20. Kukuza teknolojia zinazofaa za kilimo cha misitu<br>21. Kukuza mifumo endelevu ya kilimo, IK na mipango katika ikolojia za kilimo zinazofanana | |
| **2. Kuharakisha uendelezaji wa kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi (CSA).** kuongeza uzalishaji, kulinda mazingira kujenga na kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa | *mbinu za kilimo Kilimo, hifadhi, usimamizi wa maji na udongo; rutuba ya udongo, kilimo cha misitu* | 1. Kujenga msingi wa ushahidi wa kukuza *CSA*<br>2. Kuandaa machapisho ya miongozo na sera kuhusu teknolojia na mbinu za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi<br>3. Kuanzisha takwimu za awali kwa ajili ya sekta ya kilimo kuhusu uchafuzi<br>4. Kujenga uwezo wa wilaya ili kujumuisha CSA katika kupanga<br>5. Kukuza CSA katika mchakato wa kupanga DADP<br>6. Kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa vipengele vya CSA,<br>7. Kuandaa motisha kwa ajili ya kufidia gharama za CSA kwa wakulima wadogo<br>8. Kuongeza uelewa na kufundisha matumizi ya CSA<br>9. Kuonyesha matumizi mazuri ya CSA katika shamba | |

| Hatua na uwekezaji kipaumbele | Maeneo ya utekelezaji/ hatua | Uwekezaji/hatua muhimu | S/C |
|---|---|---|---|
| **3. Kulinda wenye mahitaji maalum dhidi ya majanga yanayohusiana na hali ya hewa** | *Athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwa ajili ya tija ya Kilimo na usalama wa chakula (Jinsi ya ku-kabiliana na mikakati )* | 1. Kutekeleza mpango wa TAFSIP kuhusu usimamizi wa maafa<br>2. Jumuisha masuala ya wadudu / magonjwa katika mifumo ya ufuatiliaji na utoaji wa tahadhari za mapema<br>3. Mawasiliano ya hali ya hewa na maelezo ya tahadhari za mapema kwa wakulima<br>4. Kujifunza kutokana na miradi ya mtandao wa EWS, DRM, na usalama wa kijamii na kuieneza<br>5. Fanya utafiti juu ya kujenga ujasiri kupitia ongezeko la thamani baada ya mavuno<br>6. Kuandaa progamu ya kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani kwa ajili ya bidhaa za kilimo<br>7. Kuandaa programu ya kukabiliana na vihatarishi kwa ajili ya wakulima wadogo | |
| **4. Kuimarisha ujuzi na mifumo kwa ajili ya kulenga shughuli za hali ya hewa** | *kutoa ujumbe muhimu kwa walengwa* | 1. Kuandaa na kutekeleza mpango wa CC na utafiti wa kilimo<br>2. Kuandaa mfumo wa kukabiliana na hali ya hewa katika maeneo hatarishi<br>3. Kufanya tathmini kamili kuhusu masuala ya jinsia na CC katika kilimo<br>4. Kuandaa/kufanyisha kazi mfumo wa taarifa za masoko (MIS) na programu ya tovuti kwa ajili CC katika kilimo<br>5. Kuanzisha ushirikiano wa wadau na mitandao ya mawasiliano<br>6. Kuandaa mfumo wa uratibu wa jinsia na Kilimo katika Wizara ya Kilimo<br>7. Kuongeza ufahamu na kusambaza taarifa za hali ya hewa inayolengwa (TEHAMA) | |

Fungamanisha Wizara nyingine za ASMLs (Mifugo, uvuvi, mazingira, ardhi) katika mkakati na mpango kazi .

Ili kujenga ujasiri katika sekta ya kilimo tayari mengi yamefanyika. ACRP imetambua mipango na uwekezaji mwingi ambao unazingatia moja kwa moja mabadiliko ya hali ya hewa. Uwekezaji wa ACRP unalenga kurekebisha katika shughuli zilizopo ili kusambaza mafanikio yaliyopatikana na kwa kiasi kikubwa kujumuisha masuala ya mabadiliko ya hali ya hewa katika kila ngazi ya shughuli za Wizara ya Kilimo.

**Jedwali Na. A15: Vipengele vya kushughulikia na Mipango Mkakati**

| Vipengele vya kushughulikia | Hatua za kimakakti |
|---|---|
| Kupitisha mpango mkakati | Mazao yanayostahimili katika AEZ tofauti; kutathmini faida ya kulinganisha mazao ya asilia ya biashara ya kuuza nje; kuhamasisha mifumo sahihi ya umwagiliaji; mazao yanayokomaa mapema; kuongeza mifumo ya kilimo na miundombinu; KI, IPM, bima ya mazao; utabiri wa hali ya hewa; kupunguza hasara ya mazao na kuongeza thamani; kuboresha usimamizi wa udongo |
| Shughuli za kimkakati za kupunguza | Kuanzisha Kilimo cha misitu, usimamizi wa taka za kilimo, upandaji mdogo na matumizi ya mbolea yenye ufanisi; kuhamasisha matumizi ya kanuni bora za kilimo na kilimo cha uhifadhi |
| Vipengele vya kimkakati vya rasilimali za maji kwa ajili ya kilimo | Kulinda / kuhifadhi mifumo ya maji, kugundua maji chini ya ardhi, kusindika maji na kutumia tena, kuvuna maji ya mvua |

**Maazimio: Mikakati Endelevu kwa ajili ya Kilimo shadidi**

ASDP II, inahamasisha kuendeleza mifumo ya kilimo, ambayo kwa pamoja inaongeza uzalishaji kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi. Mikakati mikuu ni pamoja na :

1. **Kuimarisha taasisi (na uongozi)** kutekeleza ACRP kupitia ASDP II inayohusisha wadau wa sekta ya umma (ASLM), binafsi na washirika katika ngazi za kitaifa na za mitaa
2. **Wizara ya Kilimo itahitaji kuongeza fedha za ziada kwa kujenga uwezo wa kukabiliana** ambapo uwekezaji wa Dola za Kimarekani milioni 25 kwa mwaka utahitajika ikilinganishwa na hasara za sasa zinazokadiriwa kuwa Dola za Kimarekani milioni 200.
3. **Ufuatiliaji na tathmini madhubuti utakuwa muhimu ili kuonyesha matokeo (mifumo imara).**

## KIAMBATISHO NA.XI: Kimkakati mbadala ya Kuhamasisha Uwekezaji katika Pembejeo Bora za Kilimo

Pamoja na kuwa na zaidi ya kipindi cha miaka kumi ya utoaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima wadogo, viwango vya matumizi ya mbegu bora, mbolea za kemikali na pembejeo zinazohusiana na kilimo kwa kiasi bado ni kidogo, huhusan kwa mbolea. Kaya nyingi za kilimo zinaendelea kutumia aina ya mbegu za asili na kutumia jembe la mkono isipokuwa kwa zao la mahindi. Zaidi ya hayo, baadhi ya pembejeo za mifugo (chanjo) hutolewa bila malipo kama huduma ya umma.

Mpango wa Taifa wa kutoa Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo (NAIVS), umeonyesha kwamba wakulima wanatamani sana kutumia teknolojia bora na wanaweza kupata faida kubwa ya tija ya uzalishaji: wakati wanaboresha viwango vya matumizi ya mbegu na mbolea za kemikali, mpango huo pia umechangia katika kuimarisha minyororo ya mawakala wa pembejeo. Ushahidi unaonyesha kwamba wakulima wengine wanahitimu kwa ufanisi kutoka kuwa wapokeaji wa pembejeo za ruzuku hadi kuwa wakulima wanaojitegemea katika kununua pembejeo kibiashara (theluthi mbili za mbegu na theluthi moja ya wanufaika wa mbolea). Hata hivyo, pamoja na kulenga hasa wazalishaji ambao wanajiweza, bado wakulima wanalalamika kuwa mbegu na mbolea za kemikali ni ghali sana, kulingana na upatikanaji (malipo ya awali), lakini pia kulingana na faida (ufanisi wa matumizi).

Yanayotakiwa ili kutekeleza teknolojia mpya / ilioboreshwa ni pamoja na: (i) Mazao- mbegu, mbolea, madawa ya kilimo, maandalizi ya shamba/ huduma za zana za kupandia; (ii) Mifugo-mbegu za malisho, chakula cha mifugo, chanjo, madawa ya mifugo, matengenezo ya mashine za malisho, ukusanyaji wa nyasi kavu na (iii) Uvuvi-vifaranga vya samaki, chakula, dawa, zana bora /nyavu, nk. Malengo ya kutoa msaada umma yanahitaji kufafanuliwa ili kutambua njia bora za kutoa msaada huo (bidhaa za umma) kwa kulenga malengo mahsusi ya matumizi ya pembejeo, ujuzi na upatikanaji kwa wakulima:

| Malengo maalum | Shughuli ya kipaumbele | Wadau |
|---|---|---|
| 1.Maarifa ya teknolojia mpya kwa ajili ya tija bora | -Utafiti wa ziada (AE4D)<br>-Ugani(umma na sekta binafsi) | Utafiti / ugani (umma na faragha) + Mafunzo na ICT |
| 2. Upatikanaji: kujenga minyororo ya usambazaji wa pembejeo kibiashara na huduma | -Kujenga mtandao wa mawakala wa pembejeo | Kuunganisha kati ya mawakala, wazalishaji / waagizaji na mabenki |
| 3.Mkulima kupata teknolojia inayojulikana / pembejeo na huduma | -Kupatikana kwa mikopo<br>-Kutafuta mtaji<br>-Kuzalisha mbegu? | Mkataba wa kilimo<br>Benki; vyama vya ushirika /SACCOS<br>Kuendeleza |
| 4. Matumizi endelevu (faida) ya pembejeo bora: | -Kuendeleza kiufundi (AR4D)<br>-Kuendeleza masoko<br>-Athari ya usimamizi (uhakika?) | Kuboresha uwezo wa kuzalisha k kwa ufanisi kwa ili kupata faida kutokana na kilimo shadidi |

Kwa ujumla, wakulima wanakumbana na na muunganiko wa vikwazo vya kiufundi, kifedha na masoko, na matumizi yanaweza kuchukuliwa kama mchakato wa hatua mbili wa kujifunza kwanza kuhusu teknolojia mpya na ya pili kutumia teknolojia hizi katika mfumo mzuri wa uzalishaji wa kibiashara. NAIVS ilianzishwa ili kuhamasisha matumizi ya teknolojia mpya za mbegu na mbolea za kemikali kwa mazao ya mahindi na mpunga kwa wakulima wadogo milioni 2.5 ambao hawajawahi kutumia, lakini wanaweza kulipa asilimia 50 ya gharama za mbegu na mbolea. Hii ilihusisha mkakati ambao wakulima wangehitimu katika kipindi cha miaka mitatu, kwa kuzingatia kwamba wakulima watakuwa na ujuzi lakini pia wana uwezo wa kuendelea kununua wenyewe (uwezo wa kupunguza athari na kulimbikiza mitaji kutokana na ongezeko la tija katika uzalishaji). Chaguo kwa msaada wa baadaye pamoja na malengo mahususi/ vipaumbele ni:

***Hatua ya 1. Kuchochea uigizaji wa haraka aina mpya ya mbegu mpya kwa ajili ya usalama wa chakula (na lishe)*** – Usambazaji unaolengwa wa OPV au / na pakiti za mwanzo. Kaya milioni 3.5 hazijanufaika na NAIVS, (na hata baadhi ya zile zilizosaidiwa), wanajitahidi kuzalisha nafaka za kutosha na vyakula vingine

ili kufikia usalama wa chakula na kupata au kukidhi mahitaji ya chakula nyumbani. Uzalishaji wowote wa ziada unaotokana na teknolojia bora hutoa matarajio makubwa ya usalama wa chakula na lishe lakini pia baadhi ya masoko (kupunguza misaada ya chakula wakati ambapo uzalishaji unapopungua). Njia ya dhahiri zaidi ya kusaidia kaya hizi ni kutoa na kuhakikisha upatikanaji wa haraka wa mbegu bora aina ya OPV: mbegu bora ni chanzo cha kupata tija kubwa. Mbegu zilizotolewa zinatakiwa zizalishwe kwa kiwango kikubwa na kusambazwa kwa ajili ya kujaribiwa na wakulima, na kuzalishwa na kutumiwa ili kuzalisha tija kwa miaka mingi. Ikiwa zitakataliwa, maoni ya wakulima yanaweza kusaidia watafiti katika kuboresha mpango wa kuzalisha mbegu bora ili kutatua masuala yaliyogunduliwa na wakulima.

Wizara ya Kilimo inapaswa: (i) Kukamilisha orodha ya aina mpya za mbegu kwa ajili ya mazao yote ya chakula, na (ii) Kuandaa mpango wa kuongeza na kusambaza kwa haraka kwa lengo la kuwahakikisha kuwa wakulima wote nchini wanapata aina za mbegu kulingana na mahitaji ya kanda za zao za ikolojia ya kilimo na fursa ya kufikia mafanikio endelevu katika uzalishaji; (iii) Juhudi za ufuatiliaji zilizounganishwa na jitihada za mpango wa kuongeza uzalishaji wa mbegu za kitaifa ili kuwahakikishia watafiti wa mbegu wanaunganisha mahitaji na upendeleo wa wakulima; na (iv) Kuongeza utoaji mafunzo kwa wakulima kuhusu uteuzi wa mbegu na kuhifadhi.

Aina mpya ya mbegu ambazo siyo chotara zinaweza kutolewa bure (pakiti ndogo za nyota) ili kuharakisha kujaribiwa na kukubalika na wakulima: gharama za kufanyia majaribio kwa mkulima (sehemu) mara nyingi ni za juu zaidi kuliko mapato yanayoweza kupatikana. Shughuli zinaweza kuwa zinabadilika ili kuwa na aina mpya ya mbegu kila mwaka, kuanzia na seti muhimu za aina ya nafaka na kuendelea na aina nyingine zilizopo za mbegu ya jamii ya mkunde, muhogo, viazi vitamu na ndizi.

***Hatua ya 2. Kuongeza kasi ya kupitishwa kwa teknolojia pana na mpya kuelekea mifumo mikubwa ya uzalishaji.*** Wakulima wanajifunza kwa kuona (uthibitisho, nk) lakini kwa ujumla huwa wanaamini katika kufanya. Ruzuku, inafidia gharama zote na athari(ikiwa ni pamoja na hali ya hewa, uendelevu) ambazo kila mkulima anayejaribu teknolojia mpya anakabiliana nazo. Miaka mitatu ya ruzuku katika NAIVS iliwasaidia wakulima kuelewa kiwango cha faida ya uwekezaji, na kuruhusu kujenga mtaji mdogo wa kuwekeza wenyewe: faida ya kiuchumi kwa uwekezaji wa serikali katika ruzuku ilikuwa juu sana. Aidha, msaada wa kila mmoja ulihamasisha uwekezaji binafsi wa kibiashara katika kujenga minyororo ya usambazaji na utoaji wa mbegu na mbolea kupitia idadi kubwa ya wauzaji wa jumla na rejareja wa kijijini.

*Mantiki hiyo inaweza kutumika katika teknolojia nyingi za kilimo, kama vile maandalizi ya shamba / upandaji kwa kutumia zana, matumizi ya mbolea, udhibiti wa magugu, kuvuna maji, IPM nk. Ruzuku inafidia athari za uwekezaji na kuwashawishi wakulima kuhusu faida za uwekezaji. Njia hii inajaribu kutatua vikwazo vya maarifa na vya upatikanaji wa matumizi ya teknolojia / pembejeo bora kwa wakulima: matumizi ya vocha za kielektroniki yatasaidia katika kuboresha, kupunguza thamani ya vocha na kuimarisha mpango bora wa utawala na ufuatiliaji na tathmini.*

***Hatua ya 3. Kusimamia kupitishwa kwa teknolojia bora na msaada wa mkopo na soko.*** Wakulima wanashawishika na thamani ya teknolojia mpya, lakini wanapata ugumu wa kupata fedha zinazohitajika kwa ajili ya uwekezaji. Mawazo ya wakulima ya gharama za juu za pembejeo pia huonyesha uwiano mkubwa wa pembejeo kwa bei za bidhaa. Hatua za msaada zinazowezekana ni:
**a) Kupunguza riba ya mkopo:** utoaji wa ruzuku katika mikopo ya kibiashara na baadaye kuhamasisha na dhamna ya mkopo, inaweza kuthibitisha kuwa halali kwa muda mfupi mpaka uwekezaji mkubwa muhimu unafikiwa wa kuhakikisha ushindani unaoendelea au kama msaada wa mapato kwa kaya maskini za vijijini (lakini mikopo kwa ajili ya kutokuwa na uhakika wa chakula, wazalishaji wanapaswa kuepuka).

**b) Dhamana ya mkopo** ili kupunguza vihatarishi ambavyo benki inaviona katika utoaji wa mikopo kwa ajili ya kilimo, mikakati ya kawaida ambayo inatumika ni kama vile: (i) Kilimo cha mkataba (hasa kwa mazao ya biashara kama vile tumbaku, pamba, kahawa au chai); (ii) Mikopo ya kikundi na uwajibikaji wa pamoja (kiwango kikubwa cha kuuza bidhaa zinahitajika ili kuruhusu mifumo ya kudumu ); na (iii) Mpango wa dhamana ya mikopo.
Usambazaji wa pembejeo na huduma kwa kutumia vyama kilele vya wakulima, sekta binafsi, nk, ili kupunguza gharama za kufanya biashara ya pembejeo

## KIAMBATISHO Na. XII: ASDP II Uratibu Usimamizi na mawasiliano ya ASDP II kuanzia ngazi ya Kijij hadi Taifa:170

| NGAZI | Usimamizi | Jukumu na uhusiano | Chombo cha kufanya maamuzi | Wajumbe | Jukumu na wajibu |
|---|---|---|---|---|---|
| Kijiji | Afisa Ugani wa Kilimo wa Kijiji (VAEO) | Kudhibiti, kutekeleza na kutayarisha taarifa ya kijiji, mipango, bajeti na kufuatilia shughuli za kilimo katika kijiji | Kamati ya mradi wa kijiji [wanachama 10] | Hakuna | hakuna |
| Kata | Maafisa wa Ugani wa Kilimo wa Kata (WAEO) | Kusimamia, kutekeleza, kupanga, kuandaa bajeti na kuunganisha taarifa za kijiji, kufuatilia shughuli za kilimo katika kata | Hakuna | Hakuna | Hakuna |
| Kata | Afisa Mtendaji wa Kata (WEO) | Kuandaa ripoti za vijiji, kusimamia, kumshirikisha DAS katika miradi ya maendeleo | Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) | • Mwenyekiti: Diwani aliyechaguliwa<br>• Afisa Mtendaji wa Kata<br>• Maafisa wa Ugani<br>• Wapandaji wa Kijiji<br>• Maafisa wa Kijiji | • Kuchambua mipango ya maendeleo ya kijiji, ripoti za maendeleo.<br>• Kukusanya na kuwasilisha mipango ya maendeleo ya vijiji , taarifa za utekelezaji na sheria ndogo katika Halmashauri ya Wilaya<br>• Kufuatilia maendeleo ya programu katika kata |
| Tarafa | Afisa Tarafa | Kusimamia, kuandaa taarifa za kata na kufuatilia shughuli za kilimo | Hakuna | Hakuna | Hakuna |

Siyo Kata zote zina WAEO katika sekta ndogo za Mazao, Mifugo Uvuvi, DAICO Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Wilaya
DPLO-Afisa Mipango wa Wilaya
DCO-Afisa Ushirika wa Wilaya
DTO-Afisa Biashara wa Wilaya
DLFO-Afisa Mifugo na Uvuvi wa Wilaya

| Ngazi | Usimamizi | Jukumu na uhusiano | Chombo cha kufanya maamuzi | Wajumbe | Jukumu na wajibu |
|---|---|---|---|---|---|
| Wilaya | Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Wilaya (DAICO), Ofisi za Mifugo na Uvuvi wilaya (DLFO) | Kukusanya na kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (DADP) na Bajeti;<br>Ripoti ya Ufuatiliaji na Tathmini, jukumu la ushauri juu ya masuala yanayohusiana na Kilimo | Timu ya Uwezeshaji Wilaya<br>Vikundi Kazi vya Kilimo vya Wilaya | ☞ Mwenyekiti: DAICO / DLFO<br>☞ DLO (Ardhi)<br>☞ DTO (Biashara)<br>☞ DPLO<br>☞ Mwakilishi wa Sekta Binafsi ya Kilimo<br>☞ DCOs<br>Wajumbe wa NGOs za Wilaya katika Kilimo<br>(+ Wajumbe wengine wa kikundi cha mazingira na uhifadhi)(CSA) | • Kukusanya, kuchambua, kuunganisha na kuratibu mipango na bajeti,<br>• Kuanzisha, kuhamasisha na kusaidia kupanga mipango ya kijiji na kata, kufuatilia utekelezaji na kutoa ushauri kwa Wilaya<br>• Kusaidia kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi na usajili,<br>• Kusimamia shughuli za kilimo katika mamlaka za serikali za mitaa |
| Wilaya | Mwakilishi wa ASDP II / DADP | -Ripoti kwa DAICO/ DLFO<br>-Kuunganisha shughuli za ASDP II | Hakuna | Hakuna | Hakuna |
| Wilaya | Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa / Mji / Wilaya | Kusimamia shughuli za maendeleo na kuandaa ripoti kwa ajili ya vikao vya Mabaraza ya Wilaya / Manispaa / Miji | Timu ya Usimamizi wa Baraza (CMT)<br><br>Kamati ya Ushauri ya Wilaya (Sheria ya Utawala wa Mkoa No.19 ya 1997) | • Mwenyekiti: Mkuu wa Wilaya<br>• DED<br>• Wakuu wa Idara za Wilaya | • Kuchunguza, kukusanya ripoti na kutoa ushauri kwa Halmashauri ya Wilaya |
| | | | Kikao cha Madiwani (DC) | • Mwenyekiti: Mwenyekiti wa Halmashauri<br>• Wajumbe kama Sheria ya 1982 inavyoelekeza. | • Kupitisha mipango ya maendeleo, bajeti, ripoti za utendaji na sheria. Ajenda kuhusisha pia masuala ya mali asili za wilaya |
| Mkoa | Katibu Tawala Msaidizi - Sekta ya Uchumi na Uzalishaji. | Kutoa ushauri wa kifundi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuandaa taarifa kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwasilisha kwa afisa wa mipango wa Mkoa ambaye ataziwasilisha kwa RAS | Hakuna | Hakuna | Hakuna |

| Ngazi | Usimamizi | Jukumu na uhusiano | Chombo cha kufanya maamuzi | Wajumbe | Jukumu na wajibu |
|---|---|---|---|---|---|
| Mkoa | Afisa Mipango wa Mkoa | Kuandaa mipango yote ya Wilaya na Bajeti na kuwasilisha katika Mkutano wa Ushauri wa Mkoa | Mkutano wa Ushauri wa Mkoa | • **Mwenyekiti: Mkuu wa Mkoa (RC)**<br>• AASs (wajumbe 8)<br>• Wakuu wa vitengo<br>• Idadi ya Wajumbe kama Sheria Na. 19 ya 1997 inavyoelekeza | Kufanya mapitio ya mipango na bajeti zote za Mkoa |

| Ngazi | Usimamizi | Jukumu na uhusiano | Chombo cha kufanya maamuzi | Wajumbe | Jukumu na wajibu |
|---|---|---|---|---|---|
| Mkoa | Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) | Katibu wa Kamati ya Ushauri wa Mkoa (RCC), kutoa miongozo ya sera na kusimamia shughuli za maendeleo za mkoa | Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) | • **Mwenyekiti: Katibu Tawala wa Mkoa (RAS)**<br>• Wajumbe ni kama ilivyo katika maboresho ya Utawala wa Mkoa (Juni 2011) | • Kushauri wilaya.<br>• Ufuatiliaji wa ajenda za shughuli za wilaya kuhusisha pia masuala ya mali asili za mkoa |
| OR-TAMISEMI | OR-TAMISEMI – Uratibu wa Sekta ya Kilimo | Kupanga, Kukusanya, Kuchambua, Kuratibu, kufuatiliaji na kutahmini ya mipango na bajeti za mkoa na wizara na kuwasilisha taarifa Ofisi za wakurugenzi wa sera na mipango wa wizara za kisekta (ASLMs) | Kikao cha Ushauri cha wa Kilimo wa Mkoa na Wilaya (ARLGAC) | • Mwenyekiti- Waziri - OR - TAMISEMI)<br>• RC, RAS, DED, ASLMs, DAICO, Sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo wanaofanya kazi katika mamlaka za Serikali za Mitaa, NGOeneo dogoBOs na wadau wengine muhimu katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. | • Kuushauri OR-TAMISEMI, Mikoa, na Mamlaka ya Serikali za Mitaa<br>• Mashauriano kati ya wadau wanaofanya kazi katika mikoa na Mamlaka ya Serikali za mitaa |
| Kitengo cha Uratibu | -Mratibu Mkuu<br>-Uratibu wa Maeneo Makuu ya<br>-ASDP II | Kukusanya, Kuchambua, Kuratibu, Kufuatilia na Kutathmini Utekelezaji wa ASDP II | Mkutano wa Kikundi Kazi (TWG) | • **Mwenyekiti: Mwenyekiti wa TWG** aliyechaguliwa na Mkuu wa Uratibu wa maeneo makuu ya utekelezaji<br>• Wataalamu wa Kiufundi waliochaguliwa na Mratibu Mkuu<br>• kushiriki katika Vikundi Kazi<br>• Wajumbe wengine wa kukaribishwa kwa ajili ya masuala mtambuka na ya dharura | • Kujadili, Kupanga , Kukusanya, Kuchambua, Kuratibu, Kufuatilia na Kutathmini Utekelezaji wa ASDP II |
| | | Kuandaa na Kupitia mipango na bajeti ya maneno makuu ya ASDP II na kuwasilisha kwa Wakala mkuu - Utaratibu wa maeneo makuu ya ASDP II | | | • Kuandaa na Kupitia mipango na bajeti ya ASDP II na kuwasilisha kwa Mratibu mkuu wa uratibu wa maeneno makuu ya ASDP II<br>• Kushauri TDC juu ya masuala yanayohusiana na utekelezaji wa ASDP II |

| Ngazi | Usimamizi | Jukumu na uhusiano | Chombo cha kufanya maamuzi | Wajumbe | Jukumu na wajibu |
|---|---|---|---|---|---|
| Kitengo cha Uratibu | Mratibu wa ASDP II | Kupanga, Kukusanya, Kuchambua ,Kuratibu, Kufuatilia na kutathmini mipango na bajeti za ASDP II<br>na kuwasilisha kwa Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II (NCU) | Kamati ya Ufundi ya maeneo makuu ya ASDP II | • **Mwenyekiti: Mratibu Mkuu**<br>• Mwenyekiti wa Kikundi Kazi (TWG)<br>• Mwenyekiti / Mwakilishi kutoka M & E TWG<br>• Mwenyekiti / Mwakilishi wa Kikundi Kazi cha Mipango na Bajeti<br>• Mwakilishi kutoka NCU | • Kupitia upya mipangilio ya vipengele vyenye, bajeti; kupitia na kuchambua ripoti;<br>• Kuratibu, kufuatilia na kutathmini<br>• Mipango na bajeti ya ASDP II na kuwasilisha Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II (NCU) |

| Ngazi | Usimamizi | Jukumu na uhusiano | Chombo cha kufanya maamuzi | Wajumbe | Jukumu na wajibu |
|---|---|---|---|---|---|
| Taifa | Mkurugenzi Ofisi ya Waziri Mkuu | Kupanga, kusimamia, kufuatilia na kutathmini, kuunganisha na kuratibu ASDP II.<br>NCU inakusanya mipango yote / Mipango ya Miradi na Bajeti chini ya ASDP II na kuandaa mipango na bajeti ya kazi ya kila mwaka iliyoimarishwa; Kuandaa , kuchambua, kuratibu, kutoa msaada wa vifaa vya programu; kufuatilia pamoja na kutathmini mpango na kuwasilisha katika Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi (TCD) | Kamati ya Ufundi ya Wakurugenzi (TCD) | • Mwenyekiti: Mkurugenzi (Ofisi ya Waziri Mkuu)<br>• Wakurugenzi wa ASLMS<br>• OR-TAMISEMI Uratibu wa ASDP II<br>• Mkurugenzi Mkuu wa NIC<br>• Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushirika,<br>• Mkurugenzi wa Bodi ya Stakabadhi za Ghala<br>• Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)<br>• Wizara ya Fedha na Mipango<br>• Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi<br>• Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania<br>• Wizara ya Nishati<br>• Wizara ya Uchukuzi<br>• Wizara ya Elimu<br>• Mwakilishi wa Taasisi za Utafiti wa Kilimo / Mafunzo<br>• Sekretarieti ya Kitengo cha Taifa cha Uratibu wa ASDP II (NCU) | • Kupitia, kuchambua na kuonganisha Mipango ya ASDP II na bajeti iliyowasilishwa na Waratibu viongozi wa Maeneo makuu ya utekelezajia , ripoti za ufuatiliaji na tathmini<br>• Kupendekeza miongozo ya utawala na usimamizi kwa ASC na taratibu za utekelezaji wa ASDP II<br>• Kupendekeza kwa ASC hadidu za Rejea za kufanya mapitio ya pamoja ya sekta / Matumizi ya Umma (JSR / ASR / PER) Ufuatiliaji na Tathmini<br>• Kuandaa na kuwasilisha machapisho kwa ajili ya ASCG na ASC<br>• Tathmini na kupendekeza mabadiliko ya sera katika ASC<br>• Kushauri na kuratibu vikundi kazi vya ASDP II<br>• Kuishauri NCU kuhusu utawala, usimamizi, uratibu na masuala ya uendeshaji |

| Ngazi | Usimamizi | Jukumu na uhusiano | Chombo cha kufanya maamuzi | Wajumbe | Jukumu na wajibu |
|---|---|---|---|---|---|
| Taifa | Katibu Mkuu - Ofisi ya Waziri Mkuu | Kupanga, kusimamia, kufuatilia, kutathmini, kuunganisha na kuratibu shughuli za ASDP II na kukutanisha TCD | Mkutano wa Ushauri wa Sekta ya Kilimo (ASCG) | • **Mwenyekiti: Katibu Mkuu Ofisi Waziri Mkuu**<br>• Wadau wote katika Sekta ya Kilimo (Serikali, Sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo / Washirika na NGOs / NSA) (ndani na Kimataifa)<br>• Taasisi za Utafiti na Mafunzo<br>• DPP –Kilimo Sekretarieti<br>• NCU- Mwandishi wa kumbukumbu<br>• Makatibu Wakuu | • Kutoa ushauri juu ya masuala ya sekta<br>• Kutoa msaada (fedha, vifaa na vingine) kwa sekta hiyo<br>• Kushiriki katika Mipango ya Pamoja na Mikutano ya Bajeti<br>• Kushauri juu ya sera za sekta,bajeti, kufanya mapitio ya matumizi ya umma katika kilimo |
| Taifa | Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu | Usimamizi, Maamuzi na uidhinishaji wa utekelezaji wa ASDP II | Kamati ya Usimamizi na Maamuzi (ASC) | • **Mwenyekiti: Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Utaratibu)**<br>• Makatibu Wakuu wa ASLM<br>• Wawakilishi wa Washirika wa Maendeleo (AWG- Wenyeviti ) (Wajumbe 2)<br>• Wawakilishi wa Sekta Binafsi<br>• (wajumbe 3)<br>• Wawakilishi wa NGOs / NSAs (Wajumbea 3)<br>• DPPs -ASLMs (Mazao na<br>• Mifugo<br>• NCU- Sekretarieti | • Kupitia na kuidhinisha mipango, bajeti, taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya ASDP II<br>• Kuidhinisha hadidu za rejea kwa ajili ya mapitio ya pamoja ya JSR / ASR / PER na Ufuatiliaji na Tathmini<br>• Kuwezesha na kuidhinisha uanzishwaji wa mifumo ya fedha za ASDP II;<br>• Kujadili masuala ya pamoja na ushirikiano wa taarifa;<br>• Kupitia na kuidhinisha ripoti za fedha na ukaguzi wa ASDP II,<br>• Kuthibitisha mabadiliko katika sera na kanuni kwa ajili ya kuwasilisha katika bunge<br>• Kupendekeza kalenda na ajenda za Mkutano wa Taifa wa Wadau wa Sekta ya Kilimo |

| Ngazi | Usimamizi | Jukumu na uhusiano | Chombo cha kufanya maamuzi | Wajumbe | Jukumu na wajibu |
|---|---|---|---|---|---|
| Taifa | Ofisi ya WAziri Mkuu | Kuangalia utendaji wa sekta kwa kutoa maelekezo na ushauri juu ya mabadiliko ya sekta ya kilimo na pia uendeshaji wa ASDP II | • Mkutano wa Taifa wa Wadau wa Sekta ya Kilimo (NASSM) | • **Mwenyekiti: Waziri Mkuu (WM)**<br>• Mawaziri wa Wizara za kisekta, na Makatibu Wakuu<br>• Washirika wote wa Maendeleo wanaohusika na kushiriki katika kilimo<br>• Sekta Binafsi zote zinazosaidia na kushiriki katika kilimo<br>• Asasi zisizo za kiserikali zinazohusiana na kilimo<br>• Wakurugenzi wote Sera na Mipango wa Wizara za kisekta<br>• NCU- Mwandishi wa Kumbukumbu | • Kutoa ushauri wa sera na miongozo ya ajenda ya mabadiliko ya kilimo<br>• Kutoa ushauri na miongozo ya utekelezaji wa ASDP II<br>• Kuwezesha na kutoa msaada wakati inahitajika. |

**Angalizo** kwa Kamati ya Kiufundi ya Wakurugenzi[79]



79 *Wakurugenzi wanaohusiana na maeneo mahsusi makuu ya utekelezaji wa ASDP II watashiriki katika vikao*

## KIAMBATISHO NA. XIII: Kanuni za Uwekezaji katika Kilimo (FAO, August 2014)

Kanuni Na.1: Mchango wa zao katika usalama wa chakula na lishe
Kanuni Na.2: Mchango wa zao katika ukuaji wa uchumi jumuishi na kupunguza umaskini
Kanuni Na.3: Kuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia na kuwezesha wanawake
Kanuni Na.4: Kushirikisha na kuwawezesha vijana katika upatikanaji wa mali za uzalishaji, huduma, elimu na ubunifu
Kanuni Na.5: Kuheshimu haki za umiliki ardhi , uvuvi na misitu na upatikanaji wa maji
Kanuni Na.6: Hifadhi na kuendelea kusimamia maliasili, kuongeza ustahimilivu na kupunguza athari za maafa
Kanuni Na.7: Kuheshimu urithi wa kitamaduni na ujuzi wa asili toa usaidizi katika uvumbuzi
Kanuni Na.8: Kuhamasisha kilimo salama na mifumo ya chakula
Kanuni Na.9: Kuingiza miundo ya utawala inayojumuisha uwazi, michakato na taratibu za kushughulikia malalamiko
Kanuni Na.10: Tathmini na shughulikia athari na kuhamasisha uwajibikaji

## KIAMBATISHO NA.XIV: Nyaraka Muhimu za Rejea

1-1 ASDS 2001
02-1 ASDP II Programme Document
02-2 ASDP-1 M&E_Framework_Revised_March 2011
03 TAFSIP Final version 2012
04 CAADP COMPACT Final 07 072010
05-1 National Agricultural Policy 2013
05-2 Livestock-Policy 2006
05-3 Agricultural Marketing Policy 2008
06-1 ASDP-1 Irrigation impact assessment
06-2 ASDP-1 Extension impact assessment
06-3 ASDP-1 Local Infrastructure impact assessment_ July 2014
06-4 ASDP-1 Final Report (Agricultural Support Service) TEAGASC Review Group13-02-11
06-5 Final Environmental and Social Audit Report 2014 December
06-6 ASDP EVALUATION Final Report June 2011
06-7 ICR ASDP Draft Final July 2014
07-1 Agricultural BRN – Executive Summary
07-2 Agricultural BRN 2013 (6 June) Agric Lab (detailed report)
07-3 Agricultural BRN- PDB - Stakeholder engagement meeting
08-0 ASR-PER-2014_TZ-Mainland Annex1
08-1 ASR-PER 2011-12 Final Submitted
08-2 ASR-PER 2010-11 Final Report Edited and Submitted March 2011(2)
09-0 RBA Agriculture 2014 Background Note
09-1 RBA Agriculture 2013 Background Note -Near Final Draft (2)2013-11-05
09-2 RBA Agriculture 2012 Agriculture RBA 2012_9 Jan2012
10-1 Tanzania Development Vision 2025
10-2 MKUKUTA_II_01
10-3 LTPP_2012-03-19_PRINT
10-4 5-Year Plan Draft (June 2011)

11-1 MAFAP Preliminary_Analysis_of_Public_Expenditures_in_Tanzania_Jan 2013
12-0 PHC-2012 National Socio-Economic Profile_ 26 APRIL2014
12-1 PHC-2012 Census General Report - 29 March 2013_Combined_Final for Printing
13-1 NSCA v2 Final Crops National Report 11 June2012
14-1 DGP-Macroeconomic data
15 ASDP Basket Fund 2 preparation 2013June

- PD Draft 25 Jun-2013 Draft final - Maintext
- PD Draft 25 Jun-2013 Draft final –Annexes

16 ASDP Basket Fund 2 preparation 2013 August revised

- ASDP II-BF version5.2
- Comments ASWG- 31-07 2013 response to comments
- Agricultural Sector for Industrial Development
- Master 4 Annex ASDPII-BF-BRN

17 TZ Mainland ASDP II workshop report 2013 September
18 Bank of Tanzania report

- MER Monthly Economic Review October 2014[1]
- QEB Quarterly Economic Bulletin June 2014[1]

19 National Sample Census of Agriculture. 2007–2008 (from National Bureau of Statistics)

- 13-1 NSCA Final Crops National Report 11 JUNE 2012
- Table 2.1.4 Types of Ag HH by types and size1
- Table 2.1.8 Types of Ag HH by types and size2
- Table 5.8 Crop production (short & long rainy season) by regions
- Table 5.11 Crop production by household
- Table 5.14 Crop production (yield int/ha)

20 PER_NAIVS_ National Ag. Input Voucher System (NAIVS)

- Tanzania_Final_Report-March_2014Feb
- 21 Tanzania_NAIVS Agricultural PER 2013_4

22 2011-12 HBS Main Report (Household Budget Survey)
23-1 General Report on Donor Funded Projects 2011-12
23-2 General Report on Donor Funded Projects 2010-11
24-1 Donor Mapping List (AWG)
24-2 Donor Mapping List (TAN-AIM)